

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

# TAFSIR IBN KATHIR

**Juzuu ya Tano**

**Hud mpaka An-Nahl**

Kimetafsiriwa na:  
**Kamati ya Wataalamu**

**IBN HAZM MEDIA CENTER**

Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم  
للإمام ابن كثير

# TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

**Msimamizi Mkuu wa Mradi:**  
Yassir Salim Awadh Masoud

**Kimetafsiriwa na:**  
Kamati ya Wataalamu

**Kimehaririwa na:**  
Wanazuoni wa Kiislamu

**Usanifu Kurasa:**  
Ally Said Abdallah  
Ibn Hazm Media Center  
P.O. Box 22197,  
Dar es Salaam  
Tanzania.

**Kimechapwa:**  
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

**Haki Zote Zimehifadhiwa.**

## Yaliyomo:

<b>Tafsiri ya Suratu Hud.....</b>	<b>1</b>
Surat Hud ni katika sura ambazo zilizomtoa mvi Mtume ﷺ.....	1
Qur'an na kulingania kwake Kumuabudu Allah ﷻ Peke Yake.....	2
Allah ﷻ ni Mjuzi wa Kila Jambo.....	6
Allah ﷻ Ndie Anayedhamini Rizki za Viumbe Wote.....	7
Allah ﷻ Ameziumba Mbingu na Ardhi kwa Siku Sita.....	9
Mjadala wa Washirikina katika Kufufuliwa baada ya Kufa.....	12
Maana ya Neno <i>Ummah</i> .....	13
Kugeuka kwa Mwanaadamu Msimamo wake katika Hali ya Furaha.....	16
Kudhikika kwa Mtume ﷺ Kutokana na Maneno ya Washirikina.....	19
Kubainisha Muujiza wa Qurani.....	20
Mwenye Kutaka Dunia Yeye Hana Fungu Akhera.....	21
Na Yule ambaye Anaamini Katika Qurani Yupo Katika Ukweli.....	23
Ushahidi wa Kila Hadithi na Maelezo Yake Umehakikiwa.....	27
Wenye Kumzulia Allah ﷻ, Wanawazuia Watu na Njia Yake.....	29
Malipo ya Watu wa Imani.....	34
Mfano wa Waumini na Makafiri.....	35
Kisa cha Nuhu عليه السلام na Mjadala Wake Pamoja na Watu Wake.....	36
Majibu ya Nuhu عليه السلام.....	39
Watu wa Nuhu عليه السلام Kudai Waletewe Adhabu na Majibu.....	44
Kutoka Nje ya Mada kwa Ajili ya Ubainifu wa Ukweli wa Mtume ﷺ.....	45
Wahyi kwa Nuhu عليه السلام Kuhusu Hatima ya Watu Wake.....	46
Mwanzo wa Tufani, na Nuhu عليه السلام Kuchukua katika Jahazi.....	49
Kupanda katika Jahazi na Kusafiri katika Mawimbi Makubwa.....	52
Kisa cha Kuzamishwa Mtoto wa Nuhu عليه السلام Aliyekuwa Kafiri.....	54
Mwisho wa Tufani.....	55
Kurejea Kwenye Kisa cha Mtoto wa Nuhu عليه السلام na Kutaja Yaliyojiri.....	57
Kuamrisha Kushuka katika Jahazi kwa Amani na Baraka.....	58
Kuhadithia Visa vya Ghaibu, ni Dalili Juu ya Wahyi wa Allah ﷻ.....	60
Kisa cha Hud عليه السلام na Jamaa Zake 'Aad.....	63
Mjadala kati ya 'Aad na Hud عليه السلام.....	64
Kuangamizwa kwa Aadi na Kuokolewa Walioamini Miongoni Mwao.....	67
Kisa cha Saleh عليه السلام na Thamud.....	69
Mjadala kati ya Saleh عليه السلام na Thamud.....	70
Ujio wa Malaika kwa Ibrahim عليه السلام na Kumpa Bishara ya Kuzaliwa.....	74
Mjadala wa Ibrahim عليه السلام Kuhusu Watu wa Lut عليه السلام.....	80
Ujio wa Malaika kwa Lut عليه السلام, Dhiki Iliyompata na Yaliyojiri.....	81

Kushindwa kwa Lut عليه السلام na Kutamani Awe na Nguvu.....	85
Kugeuzwa juu chini Kitongoji cha Watu wa Lut عليه السلام.....	87
Kisa cha Mji wa Madyana na Wito wa Shu'aib عليه السلام.....	89
Majibu ya Watu wa Shuaib عليه السلام.....	92
Majibu ya Shuaib عليه السلام kwa Watu Wake.....	94
Majibu ya Watu ya Shuaib عليه السلام.....	98
Majibu ya Shu'aibu عليه السلام kwa Jamaa Zake.....	98
Vitisho vya Shua'ib عليه السلام kwa Watu Wake.....	100
Kisa cha Mussa عليه السلام na Firauni.....	102
Kuonyeka Kutokana na Miji Iliyoangamizwa.....	106
Kuangamizwa kwa Miji ni Dalili ya Kusimama Kiyama.....	109
Hali ya Waovu na Hatima Yao.....	111
Hali ya Watu Wema na Hatima Yao.....	113
Kumshirikisha Allah تعالى ni Upotevu Usio na Shaka Ndani Yake.....	117
Amri ya Kusimama Thabiti Katika Njia Iliyonyooka.....	119
Amri ya Kusimamisha Sala.....	120
Mema Yanafuta Maovu.....	121
Hapana Budi Liwepo Kundi Linalokataza Machafu.....	125
Allah تعالى Hakuifanya Imani Ikubalike na Watu Wote wa Ardhi.....	127
Hitimisho.....	130
<b>Tafsiri ya Suratu Yusuf</b> .....	133
Sifa za Qur'ani.....	134
Ndoto ya Yusuf عليه السلام.....	136
Amri ya Ya'aqub عليه السلام kwa Yusuf عليه السلام Kuificha Ndoto .....	137
Tafsiri ya Ndoto ya Yusuf عليه السلام.....	138
Kuna Ishara Ndani ya Kisa cha Yusuf عليه السلام.....	141
Ndugu Zake Yusuf عليه السلام Waomba Ruhusa kwa Baba Yao.....	143
Ya'aqub عليه السلام Anawajibu Ombi Lao.....	144
Yusuf عليه السلام Anatupwa ndani ya Kisima.....	145
Hila za Ndugu Zake Yusuf عليه السلام kwa Baba Yao.....	147
Yusuf عليه السلام Anaokolewa Kutoka Kisimani na Anauzwa kama Mtumwa.....	149
Yusuf عليه السلام Akiwa Misri.....	152
Mapenzi ya Mke wa Mtawala wa Misri kwa Yusuf عليه السلام .....	155
Habari Zinawafikia Wanawake wa Mji .....	163
Yusuf عليه السلام Anafungwa Bila Uthibitishaji wa Haki.....	168
Wafungwa Wawili Wanamuomba Yusuf عليه السلام Kuwafasiria Ndoto Zao.....	169
Wito wa Yusuf عليه السلام kwa Wafungwa Wawili Wampwekeshe Allah تعالى .....	170
Kufasiri Ndoto.....	174
Yusuf عليه السلام Anamuomba Mkamuaji Mvinyo wa Mfalme.....	175

Ndoto ya Mfalme wa Misri.....	178
Mfalme Anachunguza Yaliyojiri baina ya Mkewe Azizi, Wanawake.....	181
Yusuf عليه السلام Amapewa Cheo cha Hadhi ya Juu na Mfalme wa Misri.....	185
Utawala wa Yusuf عليه السلام katika Misri.....	187
Nduguze Yusuf عليه السلام Wanasafiri Wanakwenda Misri.....	189
Nduguze Yusuf عليه السلام Wanaomba Idhini kwa Baba Yao.....	191
Nduguze Yusuf عليه السلام Wanakuta Fedha Zao Zimerejeshwa.....	194
Yaakub عليه السلام Anawaamrisha Watoto Wake Waingie Misri.....	196
Yusuf عليه السلام Anamliwaza Bin Yamin.....	197
Yusuf عليه السلام Anaweka Bakuli lake la Dhahabu Kwenye Mzigo.....	198
Ndugu wa Yusuf عليه السلام Walimtuhumu kwa Wizi.....	203
Ndugu wa Yusuf عليه السلام Watoa Pendekezo la Kutiwa Hatiani.....	204
Ndugu Zake Yusuf عليه السلام Kushauriana Kwao kisiri.....	206
Yaakub عليه السلام Anapata Habari za Kuhuzunisha.....	208
Yaakub عليه السلام Anawaamuru Wanaye Wapeleleze.....	213
Nduguze Yusuf عليه السلام Wanasimama Mbele Yake.....	213
Yusuf عليه السلام Anajitambulisha kwa Nduguze na Kuwasamehe.....	214
Ya'kub عليه السلام Anapata Harufu ya Yusuf عليه السلام kwenye Kanzu.....	217
Yahudha Analeta Kanzu ya Yusuf عليه السلام na Habari Njema.....	219
Nduguze Yusuf Wanasikitika na Kujuta .....	219
Yusuf عليه السلام Anawakaribisha Wazazi Wake, Ndoto Yake Inatimia.....	222
Yusuf عليه السلام Anamuomba Allah تعالى Amfische Hali ya Kuwa Muislamu.....	225
Kisa hiki ni Wahyi wa Allah تعالى.....	226
Watu Wanapuuzwa Kutafakari Ishara Zilizo Mbele Yao.....	229
Njia ya Mtume ﷺ.....	233
Mitume Wote ni Wanadamu Wanaume.....	234
Mitume Walikuwa Wanadamu si Malaika.....	235
Kujifunza Kutokana na Matukio Yaliyotangulia.....	236
Mitume wa Allah تعالى Walinusuriwa katika Nyakati za Dhiki Sana.....	237
Zingatia kwa Wenye Akili.....	241
<b>Tafsiri ya Suratu Ar-ra'ad.....</b>	243
Qur'ani ni Maneno ya Allah تعالى.....	243
Kuweka Wazi Ukamilifu wa Allah تعالى.....	245
Kulingana Sawa.....	246
Kudhalilishwa kwa Jua na Mwezi na Kwenda Kwao.....	246
Ishara za Allah تعالى katika Ardhi.....	249
Kukanusha Uhai baada ya Kufa ni Jambo la Ajabu.....	252
Makafiri Wanataka Adhabu Iwapate Haraka.....	254
Washirikina Wataka Waletewe Muujiza na Majibu Yao.....	257

Mjuzi wa Mambo Yaliyojificha ni Allah <b>تعالى</b> Pekee.....	258
Elimu ya Allah <b>تعالى</b> Imekizunguka kila Chenye Kuonekana.....	262
Malaika Wenye Kulinda.....	264
Mawingu, Umeme, Radi na Sauti ya Radi ni katika Uwezo wa Allah <b>تعالى</b> .....	266
Kuomba Wakati wa Radi.....	268
Kuonesha Mfano wa Kushindwa kwa Miungu ya Washirikina.....	272
Kuthibitisha Tawhidi ya Allah <b>تعالى</b> .....	273
Mifano Miwili ya Kubaki Haki na Kutoweka Batili.....	278
Qur'an na Sunna Imesheheni Mifano Mingi ya Maji na Moto.....	280
Malipo ya Wema na Waovu.....	283
Halingani Muumini na Kafiri.....	285
Sifa za Watu Wema Zitakazowaingiza Peponi.....	287
Sifa za Watu Waovu Zitakazowafanya Wapate Adhabu.....	291
Ukunjufu wa Riziki na Ufinyo Wake Vimo Mikononi mwa Allah <b>تعالى</b> .....	293
Washirikina Kutaka Miujiza na Majibu Juu Yao.....	295
Utulivu wa Moyo wa Muumini kwa Sababu ya Kumtaja Allah <b>تعالى</b> .....	296
Kuweka Wazi Maana ya Neno "Tubaa".....	297
Makusudio ya Kupelekwa kwa Mtume <b>ﷺ</b> ni Kusoma.....	299
Ubora wa Qur'an na Kuikanusha kwake Makafiri.....	302
Kuliwazwa kwa Mitume wa Allah <b>تعالى</b> .....	306
Hapana Ushirika kati ya Allah <b>تعالى</b> na Waungu wa Washirikina.....	308
Kuiweka Wazi Adhabu ya Makafiri na Malipo ya Watu Wema.....	311
Watu Wakweli Katika Waliopewa Kitabu Wanafurahia.....	316
Mitume Walikuwa Wanadamu.....	319
Mtume Yeyote Hawezi Kuleta Miujiza Isipokuwa kwa Amri ya Allah <b>تعالى</b> .....	320
Mambo Yanayofutwa na Kuondoshwa Katika Kadari ya Allah <b>تعالى</b> .....	321
Ni Juu ya Mtume Kufikisha na ni Juu ya Allah <b>تعالى</b> Kuhesabu.....	323
Vituko vya Makafiri na Karipio Juu ya Hilo.....	325
Anatosha Mwenyezi Mungu na Wale Ambao Iko Mbele Zao Elimu.....	326
<b>Tafsiri ya Suratu Ibrahim عليه السلام</b> .....	329
Taarifa Juu ya Qur'an Tukufu na Makusudio Yake.....	330
Kila Mtume Amepelekwa kwa Lugha ya Watu Wake.....	332
Kisa cha Musa عليه السلام na Watu Wake.....	334
Ukadhibishaji wa Umma za Mwanzo kwa Mitume.....	340
Majadiliano Kati ya Mtume <b>ﷺ</b> na Makafiri.....	343
Makafiri Hawaikubali Utume wa Mitume kwa Sababu ni Wanadamu.....	344
Mataifa Yasiyomuamini Allah <b>تعالى</b> Kuwatishia Kuwatoa Mitume Yao.....	346
Mfano wa Matendo ya Makafiri.....	355
Ushahidi wa Uhai baada ya Mauti.....	357

Wasioamini na Wakubwa Wao na Wafuasi Wao Watabishana.....	360
Iblisi Atawakana Wafuasi Wake Siku ya Kiama.....	363
Mfano wa Tamko la Uislamu na Tamko la Ukafiri.....	369
Allah تعالی Huwaweka Waumini Katika Uimara Duniani na Akhera.....	372
Hatima ya Mwenye Kubadilisha Neema ya Allah تعالی kwa Kufuru.....	382
Amri ya Kusali na Kutoa Sadaka.....	384
Ubainifu wa Neema Nyingi za Allah تعالی.....	386
Maombi ya Ibrahim عليه السلام Wakati Alipomuweka Ismail عليه السلام.....	389
Allah تعالی Kuwapa Muda Makafiri Hakutokani na Kughafilika.....	395
Hapana Kuongezewa Muda baada ya Ujio wa Adhabu.....	398
Allah تعالی Havunji Ahadi .....	402
Hali za Waovu Siku ya Kiama.....	406
<b>Tafsiri ya Surat u Hijr.....</b>	<b>411</b>
Wasioamini Huenda Kuna Siku Watatamani kuwa Waislamu.....	411
Kila Mji Una Muda Wake Maalumu.....	413
Kumsingizia Mtume Kwamba ni Mwendawazimu.....	414
Washirikina wa Kila Umma Waliwakejeli Mitume Wao.....	416
Makafiri Sugu, Hawatoamini Hata kwa Miujiza na Maajabu.....	417
Uweza wa Allah تعالی na Miujiza Yake Mbinguni na Ardhini.....	419
Mtoaji Pekee wa Kila Kitu ni Allah تعالی.....	422
Manufaa ya Upepo.....	422
Maji Matamu ni Neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu .....	423
Nguvu na Uweza wa Allah تعالی wa Kuanza Uumbaji na Kuurudia.....	424
Asili Aliyombiwa Mwanadamu na Jini.....	426
Kuumbwa kwa Adamu عليه السلام na Kuamrisha kwa Malaika Kumsujudia.....	428
Ibilisi Anaondoshewa Hadhi ya Utukufu, na Anafukuzwa, .....	429
Tishio la Ibilisi la Kujigamba Kupoteza Watu na Allah تعالی.....	430
Milango ya Jahanam ni Saba.....	433
Ubainifu wa Watu wa Peponi na Hali Zao.....	434
Wageni wa Ibrahim عليه السلام na Kumbashiria Kupata Mtoto.....	439
Sababu ya Kuja kwa Malaika.....	440
Ujio wa Malaika kwa Lut عليه السلام.....	441
Kuamrisha Lut عليه السلام Kutoka Pamoja na Familia Yake Usiku.....	442
Wakazi wa Mji Wanawaendea Malaika Wakidhanja ni Wanaume.....	443
Kuangamizwa kwa Watu wa Lut عليه السلام.....	446
Mji wa Sodoma Upo Njiani .....	447
Kuangamizwa Watu wa Msitu, Watu wa Shu'aib عليه السلام.....	448
Kuangamizwa kwa Watu wa Al-Hijri, Nao ni Thamud.....	449
Imeumbwa Dunia kwa Madhumuni Maalumu Kisha Kitasimama Kiama.....	451

Ukumbusho wa Neema za Qur'an na Amri ya Kuzingatia Ujumbe Wake.....	453
Mtume ﷺ ni Mhofishaji .....	457
Tafsiri ya Tamko <i>Al-Muqtasimin</i> .....	458
Amri ya Kudhihirisha Ukweli kwa Uwazi.....	461
Amri ya Kuwapuza Washirikina.....	461
Uhamasishaji Katika Kuyavumilia Matatizo.....	464
<b>Tafsiri ya <i>Suratu An-Nahl</i></b> .....	467
Onyo la Kukaribia Kiyama.....	467
Allah تعالی Anamtuma Amtakae na Ujumbe wa Tawhidi.....	469
Allah تعالی Ndiye Ambae Ameumba Mbingu, Ardhi na Mwanadamu.....	471
Wanyama ni Miongoni mwa Alivyoviumba Allah تعالی .....	473
Ufafanuzi wa Njia za Tafauti za Dini.....	477
Rehema za Mvua na Faida Zake na Mvua ni katika Alama Zake.....	480
Ishara Zilizoto Ndani ya Kuudhalilisha Usiku na Mchana.....	482
Ishara za Uweza wa Allah تعالی Ndani ya Bahari, Milima, Mito.....	484
Ibada ni Haki ya Allah تعالی.....	486
Miungu ya Washirikina Imeumbwa Haiumbi.....	487
Hakuna wa Kuabudiwa Isipokuwa Allah تعالی Tu.....	488
Kuangamizwa Makafiri na Kuongezwa Ukali wa Adhabu.....	490
Majadiliano ya Walichokifanya Waliotangulia na Walichofanyiwa.....	492
Hali za Makafiri Wakati wa Kufa Kwao na Baada Yake.....	495
Kauli ya Wachamungu Kuhusu Wahyi, Malipo Yao na Hali Zao.....	498
Maana ya Makafiri Kuchelewa Kuamini Ili Wangojee Adhabu.....	501
Hoja ya Washirikina Juu ya Ushirikina Wao .....	503
Kufufuliwa Baada ya Kufa ni Kweli, na Ndani Yake Kuna Hekima.....	509
Malipo ya Muhajirina.....	511
Hakupelekwa Mtume Yeyote Isipokuwa ni Miongoni mwa Wanadamu.....	513
Ni Kwanini Waovu Wanajiaminisha.....	516
Kusujudu kwa Kila Kitu ni kwa Ajili ya Allah تعالی.....	520
Ni Allah تعالی Peke Yake Anayestahiki Kuabudiwa.....	523
Miongoni mwa Tabia za Washirikina ni Kuweka Nadhiri.....	525
Washirikina Wanakataa Kunasibishwa na Mabinti.....	527
Allah تعالی Hana Haraka ya Kuadhibu Waliokaidi.....	530
Washirikina Wanamnasibishia Allah تعالی Wanavyovichukia.....	530
Kutafuta Faraja kwa Waliopita Kabla Yetu.....	533
Sababu ya Kuteremshwa Qur'an.....	533
Mafundisho na Neema katika Wanyama na Matunda.....	534
Katika Nyuki na Asali Yake Kuna Neema na Mafundisho.....	537
Katika Vipindi vya Umri wa Mwanadamu Kuna Mazingatio.....	540



Katika Mambo ya Maisha ya Wanadamu Kuna Ishara na Neema.....	542
Miongoni mwa Neema na Ishara ni Kuruzukiwa Wake.....	544
Kupingwa Ibada ya Yoyote Asiyekuwa Allah تعالی .....	545
Mfano wa Muumini na Kafiri au Ushirikina na Mungu wa Kweli.....	547
Ghaibu ni ya Allah تعالی Pekee, na Ndiye Mwenye Elimu ya Kiyama.....	550
Miongoni mwa Neema za Allah تعالی Alizowapa Wanaadamu.....	550
Katika Kuwadhilisha Ndege Angani Kuna Alama.....	552
Nyumba, Samani na Nguo ni Miongoni mwa Neema za Allah تعالی.....	553
Kivuli, Milima, Kanzu za Nguo na Chuma Pia ni katika Neema za Allah تعالی.....	554
Hakuna Wajibu kwa Mtume Isipokuwa Kufikisha Ujumbe.....	555
Hali ya Washirikina Siku ya Kukusanywa Siku ya Hesabu.....	558
Miungu ya Washirikina Itawakataa.....	560
Kila Kitu Siku ya Kiyama Kitajisalimisha kwa Allah تعالی.....	561
Wale Miongoni mwa Waharibifu Waliyowaharibu Wengine.....	562
Kila Nabii Atatoa Ushahidi kwa Umma Wake Siku ya Kufufuliwa.....	563
Qur'an ni Ufafanuzi wa Kila Kitu.....	564
Amri ya Kufanya Uadilifu na Kufanya Hisani.....	565
Amri ya Kudumisha Mahusiano ya Kindugu .....	566
Tukio la Ushuhuda la Uthman Ibn Madhuun رضي الله عنه.....	567
Amri ya Kutekeleza Ahadi.....	570
Allah تعالی kama Angalitaka Watu Wote Angewafanya Umma Mmoja.....	574
Katazo la Kuapa kwa Lengo la Hadaa.....	575
Msiwunje Yamini kwa Sababu ya Manufaa ya Dunia.....	575
Matendo Mema na Malipo Yake.....	576
Amri ya Kuanza Kujilinda na Shetani Kabla ya Kusoma Qur'an.....	578
Tuhuma za Washirikina kwa Mtume ﷺ kuwa ni Mzushi.....	580
Washirikina Wainasibisha Qur'an kuwa ni Mafundisho ya Mwanadamu.....	581
Ghadhabu za Allah تعالی Juu ya Aliyeritadi.....	585
Sababu ya Kuteremka kwa Aya.....	586
Atasamehewa Mwenye Kulazimishwa Kama Atafanya Mema.....	588
Huu ni Mfano wa Mji wa Makkah.....	591
Baadhi ya Mazuri Waliyoharamishiwa Mayahudi.....	594
Mayahudi Kuharamisha Vilivyo Vizuri.....	596
Rafiki wa Allah تعالی .....	599
Jumamosi Iliwekwa kwa Mayahudi.....	601
Amri ya Kulingania kwa Hekima na Mawaidha Mazuri.....	603
Amri ya Kufanya Usawa Katika Kisasi.....	605

## Tafsiri ya Suratu Hud

### Sura ya 11

#### Iliteremshwa Makkah

سُورَةُ هُودٍ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّحْمَنِ كَتَبْتُ أَحْكَمْتَ ءَايَتُهُ ثُمَّ فَصَلْتَ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ  
 خَبِيرٍ ﴿١﴾ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ إِنِّي لَكُمْ مِنْهُ نَذِيرٌ وَنَشِيرٌ  
 ﴿٢﴾ وَإِنْ أَسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُمْ مَتَاعًا  
 حَسَنًا إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِي فَضْلٍ فَضْلَهُ وَإِنْ  
 تَوَلَّوْا فَلِيَّ أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيرٍ ﴿٣﴾ إِلَىٰ اللَّهِ  
 مَرْجِعُكُمْ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤﴾

Suratu Hud ni katika sura ambazo zilizomtoa mvi Mtume ﷺ.

Abuu Issa Tirmidhi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: Abubakar رضي الله عنه alisema, 'Ewe Mjumbe wa Allah, kwa hakika umekuwa na mvi', akamjibu:

«سَيَسْتَنِي هُوْدٌ وَالْوَاقِعَةُ وَالْمُرْسَلَاتُ وَعَمَّ يَتَسَاءَلُونَ وَإِذَا السَّمَاسُ كُوْرَتْ»  
 "Imenitoa mvi, Hud, Al-Waqiah, Al-Mursalat, Amma

Yatasaa aluun, na Idhash-Shamsu Kuwwirat"

Na katika mapokezi mengine,

«هُودٌ وَأَخَوَاتُهَا»

"Hud, na ndugu zake."<sup>1</sup>

الرَّحْمَنِ كَتَبْتُ أَحْكَمْتَ ءَايَتُهُ ثُمَّ فَصَلْتَ مِنْ لَدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ ﴿١﴾ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ إِنِّي لَكُمْ مِنْهُ نَذِيرٌ وَنَشِيرٌ ﴿٢﴾ وَإِنْ أَسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُمْ مَتَاعًا حَسَنًا إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِي فَضْلٍ فَضْلَهُ وَإِنْ تَوَلَّوْا فَلِيَّ أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيرٍ ﴿٣﴾ إِلَىٰ اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤﴾

<sup>1</sup> Tuhfatul Ahwadhy 9/184.

**1. Alif Lam Ra. Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimewekwa wazi, kisha zikapambanuliwa, kilichotoka kwa Mwenye Hikima na Mwenye Khabari,**

**2. Ili msimuabudu isipokuwa Allah, Mwenyezi Mungu. Hakika mimi kwenu ni muonyaji na mbashiri nitokae Kwake.**

**3. Na ili mumuombe msamaha Mola wenu Mlezi, kisha mtubie Kwake. Ataku starehesheni starehe nzuri mpaka muda maalumu. Na Atampa kila mwenye fadhila, fadhila yake. Na ikiwa mtakengeuka basi mimi nakukhofieni adhabu ya hiyo Siku Kubwa.**

**4. Marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu tu. Naye ni Muweza wa kila kitu.**

### **Qur'an na kulingania kwake Kumuabudu Allah تعالی Peke Yake**

Maelezo kuhusu herufi za kuendeleza (*Alhijai*) yametangulia mwanzoni mwa Suratul Baqarah - kwa kiwango ambacho kimetoshela na hamna haja kuyarudia maelezo hayo hapa. Na ni kwa Allah تعالی tu kuomba kuwezesha.

Ama Kauli Yake Allah تعالی,

أَحْكَمْتَ آيَاتِهِ ثُمَّ فَضَّلْتَ

**"Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimewekwa wazi." (11:1)**

Maana: Hizo zimetengenezwa vyema katika matamshi yake, zimepambanuliwa katika maana zake, kwa hiyo Qur'ani imekamiliwa kwa muundo na maana. Haya ndiyo maana ya maneno ambayo yamepokewa kutoka kwa Mujahid na Qatadah<sup>1</sup> na ameyachagua Ibn Jarir رحمه الله تعالی, na maana ya Kauli Yake:

مِن لَّدُنْ حَكِيمٍ حَبِيرٍ ﴿١﴾

**"...kilichotoka kwa Mwenye Hikima na Mwenye Khabari." (11:1),**

Maana yake: Kutoka kwa Allah تعالی, Mwingi wa Hekima, katika Maneno Yake na Hukumu Zake, Mtambuzi wa mwisho wa mambo.

<sup>1</sup> Tabari 15 /227.

أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ

**“...Ili msimuabudu isipokuwa Allah tu.” (11:2)**

Maana: Imeshuka Qur’ani hii ambayo imetengenezwa vyema iliyopambanuliwa kwa ajili ya kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, Hana mshirika.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢١﴾

**“Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimpa wahyi kuwa asiabudiwe yeyote isipokuwa Allah.” (21:25)**

Na Amesema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**“Na Hakika Tulituma katika kila umma Mtume, kuwa muabuduni Mwenyezi Mungu na jiepusheni na matwaguti.” (16:36)**

Na Kauli Yake Allah تعالى,

إِنِّي لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيرٌ وَنَشِيرٌ ﴿٢٢﴾

**“Hakika mimi kwenu kutoka Kwake ni Muonyaji na Mbashiriaji.”**

Hii ina maana: Kwa hakika Mimi kwenu ni Mkhofishaji wa adhabu iwapo mtampinga, na Mbashiriaji wa khabari njema juu ya thawabu iwapo mtamtii.

Kama ilivyokuja katika Hadithi sahihi kwamba Mtume ﷺ alipanda juu ya Mlima wa Swafa akaita koo za jamaa zake wa karibu wa Maquraishi, kisha wanaowafuata wao kwa ukaribu, wakakusanyika akasema:

«يَا مَعْشَرَ قُرَيْشٍ! أَرَأَيْتُمْ لَوْ أَخْبَرْتُمْ أَنَّ خَيْلًا نَّصَبَحُكُمْ أَلَسْتُمْ مُصَدِّقِي؟»

**“Enyi jamaa katika Maquraishi hivi mnaonaje lau nitawaeleza kwamba kuna farasi ambao watawajieni wakati wa asubuhi. Ana maana ya jeshi - hivi hamtanisadikisha?”**

Wakasema: ‘Hatujakujaribu katika uongo’, Akawaambia:

«فَإِنِّي نَذِيرٌ لَّكُمْ بَيْنَ يَدَيِ عَذَابٍ شَدِيدٍ»

*“Hakika mimi ni Mkhofishaji kwenu juu ya adhabu kali.”<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake:

وَأَنْ أَسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُمْ مَتَاعًا حَسَنًا إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِي فَضْلٍ فَضْلَهُ<sup>ط</sup>

***“Na kwamba mtakeni msamaha Bwana wenu kisha rejeeni Kwake Atawastarehesha kuwastarehesha kwema na Atampa kila mwenye wema, wema wake.”***

Maana yake: Ninawaamrisha kutaka msamaha kutokana na madhambi ambayo yametangulia na kuleta toba kutokana nayo, na kuelekea kwa Allah تعالى, Mshindi, Mwenye Kutukuka, katika mnayoyaelekea na mwendelee juu ya hilo,

يُمَتِّعْكُمْ مَتَاعًا حَسَنًا

***“Atawastarehesha kuwastarehesha kwema...”***

Kwa maana: Hapa duniani.

إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِي فَضْلٍ فَضْلَهُ<sup>ط</sup>

***“Mpaka muda ambao umewekwa na Atampa kila mwenye wema, wema wake.”***

Maana yake: Katika nyumba ya akhera. Haya ameyasema Qatadah,<sup>2</sup> kama ilivyo katika Kauli Yake Allah تعالى:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهٗ حَيٰوةً طَيِّبَةً<sup>ط</sup>

***“Mwenye kufanya wema akiwa mwanamume au mwanamke nae ni muumini Tutamhuisha maisha mazuri.” (16:97)***

<sup>1</sup> Dalaailun Nubuwwah 2/181.

<sup>2</sup> Tabari 15/231.

وَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيرٍ ﴿٣﴾

***“Na ikiwa mtakengeuka basi mimi nakukhofieni adhabu ya hiyo Siku Kubwa.” (11:3)***

Hili ni karipio kali kwa mwenye kuzipinga amri za Allah ﷻ na akawakadhibisha Mitume Wake, kwa hakika adhabu itampata siku ya Kiyama, hapana budi.

إِلَى اللَّهِ مَرْجِعُكُمْ ط

***“Ni kwa Mwenyezi Mungu tu marejeo yenu.”***

Kwa maana: Marejeo yenu ni siku ya Kiyama:

وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤﴾

***“Na Yeye juu ya kila jambo ni Muweza sana.”***

Maana yake: Yeye ni Muweza wa Alitakalo miongoni mwa Kuwafanyia Hisani vipenzi vyake, na Kuadhibu adui zake, na Kuwarejesha viumbe siku ya Kiyama, na hii ni nafasi ya kuogopesha, kama ambavyo ile ya mwanzo ni nafasi ya kubembeleza.

\* \* \*

أَلَا إِنَّهُمْ يَنْتُونَ صُدُورَهُمْ لَيَسْتَخْفُوا  
 مِنْهُ ؕ أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ  
 يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ؕ إِنَّهُ  
 عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٥﴾ \* وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا  
 عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ؕ كُلٌّ فِي  
 كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦﴾ وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ  
 فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ لِيَبْلُوكُمْ  
 أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ؕ وَلَئِنْ قُلْتُمْ إِنَّكُمْ مَبْعُوثُونَ مِنْ  
 بَعْدِ الْمَوْتِ لَيَقُولَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ  
 مُبِينٌ ﴿٧﴾ وَلَئِنْ أَخَّرْنَا عَنْهُمْ الْعَذَابَ إِلَى أُمَّةٍ مَعْدُودَةٍ  
 لَيَقُولُنَّ مَا نَحْبِسُهُ ؕ أَلَا يَوْمَ يَأْتِيهِمْ لَيْسَ مَصْرُوفًا  
 عَنْهُمْ وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِمِيسِرٍ يَعْتَزُّونَ ﴿٨﴾

أَلَا إِنَّهُمْ يَنْتُونَ صُدُورَهُمْ لَيَسْتَخْفُوا  
 مِنْهُ ؕ أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ  
 يَعْلَمُ مَا يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ؕ إِنَّهُ  
 عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٥﴾

**5. "Hebu angalia! Ati wana-  
 funika vilivyomo vifuani  
 mwao ili wamfiche  
 Mwenyezi Mungu! Jueni  
 kuwa wanapojigubika nguo  
 zao Yeye Anajua wana-  
 yoyaficha na wanayo-  
 yatangaza. Hakika Yeye ni  
 Mjuzi wa yaliyomo vifuani."**

## Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa Kila Jambo

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما: Walikuwa wanachukia kuelekea mbinguni  
 kwa tupu zao, na wakati wa kujamiana kwao, Allah تعالى Akaiteremsha aya hii.  
 Bukhari amepokea kutoka kwa Ibn Jurajji kutoka kwa Muhammad Bin Abbaad  
 Bin Ja'afar. Kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema:

(أَلَا إِنَّهُمْ تَنْتُونِي صُدُورُهُمْ)

"Hebu sikieni, hakika wao wanavipinda vifua vyao...",

Nikasema: Ewe Abal Abbas nini maana ya; "wanavipinda vifua vyao?" Akasema:  
 Mtu alikuwa anamuingilia mke wake huku anaona haya au anakidhi haja huku  
 anaona haya ikashuka aya hii:

أَلَا إِنَّهُمْ يَنْتُونِ صُدُورَهُمْ

**“Hebu angalia! Ati wanafunika vilivyomo vifuani mwao.”<sup>1</sup>**

Na katika tamko jingine, amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما: Hao ni watu waliokuwa wanaona haya kukidhi haja na hali ya kuwa wameelekea mbinguni au kuwaingilia wake zao wakielekea mbinguni, ikashuka ayah hii kwa sababu yao,<sup>2</sup> na Imamu Bukhari amenukuu kutoka kwa ibn Abbas رضي الله عنهما,

يَسْتَغْشُونَ

**“Wanafunika”**

Maana yake: Wanafunika vichwa vyao.<sup>3</sup>

﴿ وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦﴾

**“Na hakuna kiumbe yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.”**

### **Mwenyezi Mungu Ndie Anayedhamini Riziki za Viumbe Wote.**

Allah تعالى Ameeleza kwamba Yeye Amedhamini riziki za aina zote za viumbe wenye kwenda juu ya ardhi wadogo na wakubwa wao, wa baharini na nchi kavu, na kwamba Yeye Anajua matulizano yao na makao yao. Maana: Anajua ni wapi unakomelea mwendo wao katika ardhi na ni wapi wanashukia miongoni mwa viota vyao, navyo ndiyo makao yao. Ali bin Abi Twalha na wengine wamesema, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا

**“Naye Anajua makao yake...”** Maana yake: Mahali wanapoishi.

<sup>1</sup> Fat’hul-Baary 8/200.

<sup>2</sup> Fat’hul-Baary 8/200.

<sup>3</sup> Fat’hul-Baary 8/200.



وَمُسْتَوْدَعَهَا<sup>٤</sup>

**“Na mapitio yake.”** Mahali watakapokufa<sup>1</sup> na kwamba yote hayo yameandikwa yote hayo yamo katika “kitabu” mbele ya Allah تعالیٰ “chenye kubainisha” kuhusu yote hayo, kama ilivyo katika Kauli Yake,

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَيْرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَّمٌ أَمْثَالُكُمْ<sup>٤</sup> مَا قَرَّطْنَا فِي الْكِتَابِ

مِنْ شَيْءٍ<sup>٤</sup> ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يُحْشَرُونَ ﴿٦٨﴾

**“Hapana kiumbe yoyote katika ardhi au ndege anaruka kwa mbawa zake isipokuwa ni uma mfano wenu hatukuacha katika kitabu chochote kisha kwa Mola wao watarejeshwa.”** (6:38) na

\* وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ<sup>٤</sup> وَمَا تَسْقُطُ مِنْ

وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦٩﴾

**“Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye Anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha.”** (6:59)

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى السَّمَاءِ

لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا<sup>٥</sup> وَلَئِنْ قُلْتُمْ إِنَّكُمْ مَبْعُوثُونَ مِنْ بَعْدِ الْمَوْتِ لَيَقُولَنَّ

الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُبِينٌ ﴿٧٠﴾ وَلَئِنْ أَخْرْنَا عَنْهُمُ الْعَذَابَ إِلَىٰ أُمَّةٍ مَعْدُودَةٍ

لَيَقُولُنَّ مَا مَحْسَبُهُمْ<sup>٥</sup> إِلَّا يَوْمَ يَأْتِيهِمْ لَيْسَ مَصْرُوفًا عَنْهُمْ وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ

يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٧١﴾

**7. Na Yeye Ndiye Aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Na Kiti Chake cha Enzi kilikuwa juu ya maji, ili Akufanyieni mtihani ajulikane ni nani miongoni mwenu mzuri zaidi wa vitendo. Na wewe ukisema: Nyinyi hakika mtafufuliwa baada ya kufa; wale walio kufuru husema: Hayakuwa haya ila ni uchawi uliyo wazi.**

<sup>1</sup> Tabari 15/241.

**8. Na Tukiwacheleweshea adhabu mpaka muda uliokwisha hisabiwa wao husema: Nini kinachoizuia hiyo adhabu? Jueni! Siku itakapowajia basi haitoondolewa hiyo kwao. Na yatawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia mzaha.**

**Allah تعالیٰ Ameziumba Mbingu na Ardhi kwa Siku Sita:**

Allah تعالیٰ, Anaeleza kuhusu Uweza Wake juu ya kila kitu, na kwamba Yeye Ameziumba mbingu na ardhi katika siku sita, na kwamba Arshi Yake ilikuwa juu ya maji kabla ya hapo, kama alivyopokea Imamu Ahmad kutoka kwa Imrani Bin Huswayni ambaye amesema, Mtume ﷺ amesema:

«اقْبَلُوا الْبُشْرَىٰ يَا بَنِي تَمِيمٍ!»

“Kubalini habari njema enyi Bani Tamim!”

Wakasema: ‘Kwa hakika umetupa habari njema na tumetii’ akasema.

«اقْبَلُوا الْبُشْرَىٰ يَا أَهْلَ الْيَمَنِ»

“Kubalini habari njema enyi watu wa Yemeni.”

Wakasema: ‘Tumeikubali basi tueleze kuhusu mwanzo wa jambo hili ulikuwa vipi?’ Akasema:

«كَانَ اللَّهُ قَبْلَ كُلِّ شَيْءٍ، وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ، وَكَتَبَ فِي اللَّوْحِ الْمَحْفُوظِ ذِكْرَ كُلِّ شَيْءٍ»

“Mwenyezi Mungu Alikuwa kabla ya kila kitu na Arshi Yake ilikuwa juu ya maji, na Aliandika katika Lauhil Mahfuudhi utajo wa kila kitu”,

Akasema: akanijia mwenye kuja akasema: ‘Ewe Imran, ngamia wako amefunguka kamba yake.’ Akasema, ‘Nikatoka kufuata athari yake kwa hiyo sielewi ni jambo gani ambalo lilikuwa baada yangu.’<sup>1</sup>

Na hadithi hii imetolewa katika sahihi mbili Bukhary na Muslim kwa matamshi mengi.<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Ahmad 4/431.

<sup>2</sup> Fat’hul al-Bari 6/330, na Muslimu 4/2041.

Katika Sahihi Muslimu toka kwa Abdillahi Bin Amri Ibnil-'Aas رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ قَدَّرَ مَقَادِيرَ الْخَلَائِقِ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِخَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ  
وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ»

*"Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amekadiria vipimo vya viumbe kabla ya Kuumba mbingu na ardhi, kwa muda wa miaka khamsini elfu na Arshi yake ilikuwa juu ya maji."*<sup>1</sup>

Na Bukhari amepokea katika tafsiri ya ayah hii Kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه kwamba, Mtume ﷺ amesema:

«قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: أَنْتَقِ أَنْتَقِ عَلَيْكَ»

*"Amesema Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda na Ametukuka: Toa nitakupa."*

Na amesema:

«يَدُ اللَّهِ مَلَأَى لَا يَغِيضُهَا نَفَقَةً، سَحَاءَ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ»

*"Mkono wa Mwenyezi Mungu Umejaa Kutoa hakuupunguzi kitu, unamimina usiku na mchana."*

Na amesema:

«أَفْرَأَيْتُمْ مَا أَنْتَقَ مِنْذُ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فَإِنَّهُ لَمْ يَغِيضْ مَا فِي يَمِينِهِ، وَكَانَ  
عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ، وَيَبِيدُهُ الْمِيمِرَانُ يَخْفِضُ وَيَرْفَعُ»

*"Jee mmeyaona yale ambayo Ameyatoa tokea Alipoumba mbingu na ardhi, kwa hakika hayakupungua yaliyo katika Mkono Wake wa Kuume na ilikuwa Arshi Yake ipo juu ya Maji, na Mkononi Mwake kuna mizani inashuka na inapanda."*<sup>2</sup>

Na Kauli Yake Allah تعالى:

لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا<sup>3</sup>

*"...ili akufanyieni mtihani ajulikane ni nani miongoni mwenu mzuri zaidi wa vitendo."*

<sup>1</sup> Muslim 4/2044.

<sup>2</sup> Fat'hul al-Bari 8/202.

Maana yake: Ameumba mbingu na ardhi kwa manufaa ya waja Wake, ambao Amewaumba ili wamuabudu na wasimshirikishe na Yeye kitu chochote, na Hakuviumba vyote hivyo kwa mchezo, ni kama Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطْلًا ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ  
كَفَرُوا مِنَ النَّارِ ﴿٣٨﴾

**“Na Hatukuumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa batili hiyo ni dhana ya wale ambao wamekufuru basi ole wao ambao wamekufuru na moto.” (38:27)**

Na Amesema Allah تعالى:

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٩﴾ فَتَعَلَىٰ اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۚ  
لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿٤٠﴾

**“Na mnadhani kuwa Sisi Tumekuumbeni kwa upuuzi, na kuwa nyinyi Kwetu hamtarejeshwa. Basi Ametukuka mola wa haki...hapana mola asiye kuwa Yeye Mola wa Arshi tukufu”. (23:115-116)**

Na Amesema Allah تعالى:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥١﴾

**“Sikuwaumba majini na watu ispokuwa waniabudu.” (51:56),**

Isome aya hiyo na Kauli Yake:

لِيَبْلُوكُمْ

**“...ili akufanyieni mtihani...”** Maana yake: Awatie katika majaribio

أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ

**“...ajulikane ni nani miongoni mwenu mzuri zaidi wa vitendo.”**

Na hakusema ‘mwingi’ wenu wa matendo bali ‘mzuri wenu sana wa matendo’ na wala matendo hayawi mazuri mpaka yawe yametakasika kwa ajili ya Allah تعالى, na ni lazima matendo hayo yawiane na maelekezo ya Mtume ﷺ. Wakati wowote matendo yatakapokosa moja ya masharti mawili haya yataporomoka na kubatilika.

## Mjadala wa Washirikina katika Kufufuliwa Baada ya Kufa na Kuharakishwa Kwao Adhabu:

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَيْسَ قُلْتُمْ إِنَّا كُنَّا مَبْعُوثُونَ مِنْ بَعْدِ الْمَوْتِ

**“Na wewe ukisema: Nyinyi hakika mtafufuliwa baada ya kufa.”**

Allah تعالى Anasema: Lakini ukiwapa khabari ee Muhammad, hao washirikina kuwa Allah تعالى Atawafufua baada ya kutaka kwao kama Alivyowaanza, pamoja na kuwa wao wanajua kuwa Allah تعالى Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَيْن سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

**“Kama ukiwauliza wao ni nani aliewaumba wao watasema ni Mwenyezi Mungu...” (43:87)**

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَلَيْن سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

**“Na kama ukiwauliza ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na Akalidhalilisha jua na mwezi watasema ni Mwenyezi Mungu.” (29:61)**

Wao pamoja na haya wanakanusha kufufuliwa na kurejeshwa kwa Allah تعالى Siku ya Kiyama, kurejeshwa ambako kukilinganishwa na Uwezo wa Allah تعالى ni jambo jepesi sana kuliko kuanza Kuumbwa, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

**“Na Yeye ni Ambaye Anaanzisha viumbe kisha Huvirejesha nayo ni sahali zaidi kwake.” (30:27)**

Kasema Allah تعالى:

مَا خَلَقْنَاكُمْ وَلَا نَبْعَثُكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ

**“Hakukuwa kuumbwa kwenu wala kurudishwa kwenu isipokuwa ni kama nafsi moja.” (31:28)**

Na Kauli Yake,

إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧﴾

***“Hakuwa huyu isipokuwa ni mchawi wa wazi.”***

Maana yake: Wanasema kwa ukafiri na upingaji hatukusadiki juu ya kutokea ufufuo, na halikumbuki hilo isipokuwa yule ambaye umemcheza shere, kwa hiyo huyo anakufuata kwa ambayo unayasema. Na Kauli Yake:

وَلَيْنَ أَخْرَجْنَا عَنْهُمْ الْعَذَابَ إِلَىٰ أُمَّةٍ مَّعْدُودَةٍ

***“Na lakini ukichelewesha miongoni mwao adhabu mpaka kwenye umati uliohesabiwa...”***

Allah تعالیٰ Anasema: Lakini tunawacheleweshea adhabu hao washirikina mpaka siku maalumu na muda uliowekewa mpaka na tukawaahidi hadi muda maalumu “Watasema” kwa kuikadhibisha na kuiharakisha

مَا تَحْسِبُهُ

***“Lipi linaizuia...”***

Maana yake: Linaloichelewesha adhabu kwetu, kwa hakika tabia zao zimezoea kukadhibisha na kutia shaka kwa hiyo hakukubakia kwao kimbilio kuepukana na adhabu hiyo wala ujanja.

### **Maana ya Neno Ummah**

Tamko la neno ‘Ummah’ linatumiwa sana katika Qur’an na Sunna. Kwa maana mbalimbali hukusudiwa tamko hilo, mfano limetumika kwa maana ya muda.

Kama Kauli Yake Allah تعالیٰ katika aya hii

إِلَىٰ أُمَّةٍ مَّعْدُودَةٍ

***“Mpaka muda uliowekwa...”***

Na Kauli Yake katika Surat Yusuf,

وَقَالَ الَّذِي نَجَّا مِنْهُمَا وَادَّكَرَ بَعْدَ أُمَّةٍ

***“Na alisema yule ambaye ameokoka na akakumbuka baada ya muda.” (12:45)***

Na hutumiwa tamko hilo kwa maana ya 'kiongozi mwenye kufuatwa' kama ilivyo katika Kauli Yake Allah تعالى:

﴿١٦﴾ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

***"Hakika Ibrahiim amekuwa ni umma mwenye kumcha Mungu Mwenye kumpwekesha na si katika washirikina." (16:120)***

Na hutumiwa tamko hilo katika maana ya 'mila na dini', kama Kusema Kwake Allah تعالى Akitoa khabari kuhusu washirikina kwamba wao wamesema:

﴿٢٣﴾ إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّقْتَدُونَ

***"Kwa hakika sisi tumewakuta baba zetu juu ya dini na sisi juu ya nyayo zao ni wenye kufuata." (43:23).***

Na hutumiwa tamko hili katika maana ya 'kundi la watu' kama Kusema Kwake Allah تعالى:

﴿٢٣﴾ وَلَمَّا وَرَدَ مَاءَ مَدْيَنَ وَجَدَ عَلَيْهِ أُمَّةً مِّنَ النَّاسِ يَسْقُونَ

***"Na alipoyakuta maji ya Madiana, alikuta juu yake Umma wa watu wakinyweshwa." (28:23)***

Na Kauli Yake Allah تعالى:

﴿٣٦﴾ وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

***"Na hakika Tulituma Mtume katika kila umma, kuwa muabuduni Mwenyezi Mungu na jiepusheni na matwaghuti." (16:36)***

Na Akasema Allah تعالى,

﴿٤٧﴾ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَسُولٌ فَإِذَا جَاءَ رَسُولُهُمْ قُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

***"Na kila umma una mtume, na anapokuja Mtume wao huhukumiwa baina yao kwa uadilifu na wao hawadhulumiwi." (10:47)***

Na makusudio ya tamko Ummah hapa ni watu ambao hupelekwa juu yao Mjumbe sawa sawa watu hao walikuwa waumini au Makafiri, kama lilivyokuja hilo katika Sahihi ya Muslim:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يَسْمَعُ بِي أَحَدٌ مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ يَهُودِيٍّ وَلَا نَصْرَانِيٍّ ثُمَّ لَا يُؤْمِنُ  
بِي إِلَّا دَخَلَ النَّارَ»

*“Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu imo Mikononi Mwake hatanisikia mimi mtu yoyote katika Ummah huu Mayahudi wala Manaswara kisha asiniamini isipokuwa ataingia motoni.”<sup>1</sup>*

Ama Ummah unapotii na kufuata, wanakuwa ni wale wenye kuwasadikisha Mitume, kama Alivyosema Allah تعالى:

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

**“Mmekuwa bora ya umma uliotolewa kwa watu.” (3:110)**

Na katika Sahihi Mtume ﷺ amesema:

«فَأَقُولُ: أُمَّتِي أُمَّتِي»

*“Na ninasema: Umma wangu umma wangu.”<sup>2</sup>*

Na neno Ummah linatumiwa katika maana ya 'kikundi na taifa' kama Kusema Kwake Allah تعالى:

وَمِنْ قَوْمِ مُوسَىٰ أُمَّةٍ يَهْدُونَ بِالْحَقِّ وَبِهِ يَعْدِلُونَ ﴿٧٥﴾

**“Na miongoni mwa watu wa Musa kuna umma unaofuata haki na kwayo wanafanya uadilifu.” (7:159)**

Na kama Kauli Yake,

مِنَ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ

**“Na miongoni mwa watu wa Kitabu kuna umma uliosimama...” (3:13)**

\* \* \*

<sup>1</sup> Muslim 1/134.

<sup>2</sup> Muslim 1/184.



وَلَئِن أَدَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنَّا رَحْمَةً ثُمَّ نَزَعْنَاهَا مِنْهُ إِنَّهُ لَيَكُفِّرُ  
 كُفُورًا ﴿٩﴾ وَلَئِن أَدَقْنَاهُ نِعْمَاءَ بَعْدَ ضَرَاءٍ مَّسْتَهُ لَيَقُولُنَّ  
 ذَهَبَ الْبَرَائِثُ عَنِّي إِنَّهُ لَفَرِحَ فَخُورًا ﴿١٠﴾ إِلَّا الَّذِينَ  
 صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَئِكَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ  
 كَبِيرٌ ﴿١١﴾ فَلَعَلَّكَ تَارِكٌ بَعْضَ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ  
 وَضَائِقٌ بِهِ صَدْرُكَ أَنْ يَقُولُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ كِتَابٌ أَوْ جَاءَ  
 مَعَهُ مَلَكٌ إِنَّمَا أَنْتَ نَذِيرٌ ﴿١٢﴾ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ  
 ﴿١٣﴾ أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِّثْلِهِ  
 مُفْتَرِيَاتٍ وَادْعُوا مَنِ اسْتَدْعَيْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ  
 صَادِقِينَ ﴿١٤﴾ فَإِلَّمْ يَسْتَجِيبُوا لَكُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّمَا أُنزِلَ  
 بِعِلْمِ اللَّهِ وَأَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَهَلْ أَنتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٥﴾  
 مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوفِيَ إِلَيْهِمْ أَعْمَالَهُمْ  
 فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ﴿١٦﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ  
 فِي الْآخِرَةِ إِلَّا النَّارُ ۗ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا فِيهَا وَبِطِلَ مَا  
 كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

وَلَئِن أَدَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنَّا رَحْمَةً ثُمَّ  
 نَزَعْنَاهَا مِنْهُ إِنَّهُ لَيَكُفِّرُ كُفُورًا ﴿٩﴾  
 وَلَئِن أَدَقْنَاهُ نِعْمَاءَ بَعْدَ ضَرَاءٍ مَّسْتَهُ  
 لَيَقُولُنَّ ذَهَبَ الْبَرَائِثُ عَنِّي إِنَّهُ  
 لَفَرِحَ فَخُورًا ﴿١٠﴾ إِلَّا الَّذِينَ  
 صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَئِكَ لَهُمْ  
 مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١١﴾

**9. Na Tukimwonjesha mtu  
 rehema inayotoka Kwetu,  
 kisha Tukamwondolea,  
 hukata tamaa akakufuru.**

**10. Na Tukimwonjesha  
 neema baada ya madhara  
 yaliyompata husema:  
 Taabu zimekwishani-  
 ondokea. Hakika yeye  
 hujitapa na kutafakhari.**

**11. Ila wale waliosubiri  
 wakatenda mema. Hao  
 watapata msamaha na  
 ujira mkubwa.**

**Kugeuka kwa Mwanaadamu Msimamo wake katika Hali ya Furaha na Shida**

Allah تعالى Anaeleza kuhusu mwanadamu na yale ambayo anayo miongoni mwa sifa mbaya, isipokuwa wale ambao Allah تعالى Amewarhemu katika waja wake waumini, kwa hakika mwanadamu pindi yampatapo matatizo baada ya neema, hukata tamaa na kuvunjika moyo katika kupata kheri, kwa mnasaba wa yanayomsibu, na hukufuru na kukanusha hali iliyopita kana kwamba

hajaona kheri yoyote, na hatarajii baada ya hapo faraja yoyote. Na hali yake huwa kama hivi anapopata neema baada ya mateso,

ذَهَبَ السَّيِّئَاتُ عَنِّي

**“Taabu zimekwishaniondokea”.**

Maana yake: Anasema haitanipata baada ya hapa dhulma wala ubaya wowote.

إِنَّهُ لَفَرِحٌ فَخُورٌ ﴿١٠﴾

**“Hakika yeye hujitapa na kutafakhari.”**

Maana yake: ni mwenye furaha sana kwa kile kilicho mkononi mwake huku akiwa ni mwenye kujivuna mwenye kujifakarisha sana kwa wengine.

Allah تعالى Amesema:

إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا

**“...Ila wale waliosubiri...”**

Maana yake: Juu ya matatizo na mambo yenye kukera.

وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

**“...wakatenda mema...”**

Maana yake: Katika raha na afya,

أُولَئِكَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ

**“...Hao watapata msamaha...”**

Maana yake: Kutokana na yale yanayowapata miongoni mwa madhara.

وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١١﴾

**“...Na ujira mkubwa”**

Kwa yale ambayo wameyatanguliza katika wakati wa raha kama ilivyokuja katika hadithi:

وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يُصِيبُ الْمُؤْمِنِينَ هَمٌّ وَلَا غَمٌّ وَلَا نَصَبٌ وَلَا وَصَبٌ وَلَا حَزَنٌ، حَتَّى السَّوْكَةُ يُشَاكَهَا إِلَّا كَفَرَ اللَّهُ عَنْهُ بِهَا مِنْ خَطَايَاهُ،

*“Naapa kwa Mwenyezi Mungu Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake hayampati Muumini majonzi (wasiwasi) (Hammun), wala Simanzi (Sikitiko) (Ghammun), wala balaa (Nasabun), wala ugonjwa (Wasabun), wala huzuni (Hazanun) hata mwiba ambao unamchoma, isipokuwa Mwenyezi Mungu Husamehe kwa hayo yote, makosa yake.”<sup>1</sup>*

Na katika Sahihi Mtume ﷺ Amesema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يَقْضِي اللَّهُ لِلْمُؤْمِنِ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، إِنْ أَصَابَتْهُ سَرَاءٌ فَشَكَرَ كَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ فَصَبَرَ كَانَ خَيْرًا لَهُ، وَلَيْسَ ذَلِكَ لِأَحَدٍ غَيْرِ الْمُؤْمِنِ»

*“Naapa kwa ambae nafsi yangu imo Mikononi Mwake Mwenyezi Mungu Hahukumu hukumu yoyote kwa ajili ya muumini isipokuwa huwa ni kheri kwake, iwapo itampata yeye furaha akashukuru inakuwa ni kheri kwake, na iwapo itampata yeye dhara akasubiri inakuwa ni kheri kwake; na hilo si kwa yeyoyte isipokuwa kwa muumini.”<sup>2</sup>*

Na kwa sababu hiyo Allah ﷻ Amesema:

وَالْعَصْرِ ﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَّصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَّصَوْا بِالصَّبْرِ ﴿٣﴾

***“Naapa kwa Zama! Hakika wanadamu wote wamo katika khasara, Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausia kutenda haki, na wakausia kusubiri.” (103:1-3)***

Allah ﷻ Amesema:

﴿١﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴿٢﴾

***“Hakika mwanadamu ameumbwa kwa babaiko.” (70:19),***

<sup>1</sup> Ahmad 4/3.

<sup>2</sup> Muslim 4/2295.

فَلَعَلَّكَ تَارِكٌ بَعْضَ مَا يُوحَىٰ ۖ وَإِلَيْكَ وَصَّيْتُ بِهِمْ صَدْرَكَ أَن يَقُولُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ كِتَابٌ أَوْ جَاءَ مَعَهُ مَلَكٌ ۚ إِنَّمَا أَنْتَ نَذِيرٌ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ ﴿١٢﴾ أَمْ يَقُولُونَ أَفَنزَلْنَاهُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِّثْلِهِ مُفْتَرِيْنَ ۖ وَادْعُوا مَنِ اسْتَضَعْتُمْ مِّن دُونِ اللَّهِ إِن كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿١٣﴾ فَلَا تَسْتَجِيبُوا لَكُمْ فَاعْلَمُوا أَنَّمَا أُنزِلَ بِعِلْمِ اللَّهِ وَأَن لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ فَهَلْ أَنْتُمْ مُّسْلِمُونَ ﴿١٤﴾

**12. Basi labda utaacha baadhi ya yale yaliyofunuliwa kwako, na kifua kitaona dhiki kwa hayo, kwa sababu wanasema: Mbona hakuteremshiwa khazina, au wakaja naye Malaika? Wewe ni mwonyaji tu, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa kila kitu.**

**13. Au wanasema: Ameizua? Sema: Basi leteni Sura kumi zilizozuliwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli.**

**14. Na wasipokuitikieni, basi jueni ya kwamba (Qur'ani hii) imeteremshwa kwa ujuzi wa Mwenyezi Mungu, na kwamba hapana mungu ila Yeye. Basi je! Nyinyi ni Waislamu?"**

**Kudhikika kwa Mtume ﷺ Kutokana na Maneno ya Washirikina na Kufarajiwa Kwake**

Allah تعالى Anasema Akimliwaza kwa Kumfariji Mjumbe wake ﷺ kutokana na ukaidi wa washirikina waliokuwa wakimfanyia, miongoni mwa waliokuwa wanayasema kuhusu Mtume ﷺ. Kama Allah تعالى Alivyoeliza kuhusu wao katika Kauli Yake:

وَقَالُوا مَالِ هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ لَوْلَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُونُ مَعَهُ نَذِيرًا ﴿١٥﴾ أَوْ يُلْقَىٰ إِلَيْهِ كِتَابٌ أَوْ تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا وَقَالَ الظَّالِمُونَ إِن تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿١٦﴾

**"Na wakasema: Ana nini Mtume huyu? Anakula chakula, na anatembea masokoni! Mbona hakuteremshiwa Malaika akawa**

***mwonyaji pamoja naye? Au akaangushiwa khazina juu yake, au akawa na bustani ale katika hiyo? Wakasema madhaalimu: Nyinyi hamumfuati ila mtu aliyerogwa.” (25:7-8)***

Kwa hiyo Allah تعالى Akamuamuru Mjumbe wake ﷺ na akamuongoza ili kifua chake kisidhikike kwa sababu ya wanayosema wao, wala lisimzuie hilo na lisimvunje moyo katika kuwalingania wao kwa Allah تعالى, Mwenye Kushinda na Kutukuka, nyakati za usiku na ncha za mchana.

Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَلَقَدْ نَعَلْنَا أَنكَ يَضْبِقُ صَدْرَكَ بِمَا يَقُولُونَ ﴿٧٧﴾

***“Na Sisi kwa hakika Tunajua kuwa wewe kifua chako kinaingia dhiki kwa wayasemayo.” (15:97)***

فَلَعَلَّكَ تَارِكٌ بَعْضَ مَا يُوحَىٰ ۖ وَإِلَيْكَ وَصَّيْقُ بِمِءٍ صَدْرَكَ أَنْ يَقُولُوا

***“Basi labda utaacha baadhi ya yale yaliyofunuliwa kwako, na kifua kitaona dhiki kwa hayo, kwa sababu wanasema...”***

Maana yake: Kwa sababu ya kusema kwao hivyo, kwa hakika hapana jambo jingine wewe ni mkhofishaji, na wewe una kigezo kwa ndugu zako miongoni mwa Mitume waliyokuwa kabla yako, kwa hakika wao walikadhibishwa na waliudhiwa wakasubiri mpaka ikawajia nusura ya Allah تعالى Mwenye Kushinda na Kutukuka.

### **Kubainisha Muujiza wa Qurani**

Kisha Allah تعالى Ameweka wazi Muujiza wa Qurani, na kwamba mtu yoyote hawezi kuleta mfano wake, wala sura kumi au moja mfano wake, kwa sababu maneno ya Bwana Mwenye Kutukuka hayafanani na maneno ya viumbe, kama ambavyo Sifa Zake hazifanani na sifa za maneno ya kubuni, na Dhati Yake haifanani na kitu chochote, Ametukuka na Kutakasika Ambaye hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, na hapana Bwana asiyekuwa Yeye. Kisha Allah تعالى Akasema:

فَالْمَرَّيْسَتَجِيبُوا لَكُمْ

***“...Na wasipokuitikieni...”***

Wasipofanya hayo mliyowaeleza basi eleweni kwamba wao ni wenye kushindwa na hilo, na kuwa maneno hayo yameteremshwa kutoka kwa Allah تعالی yamekusanya Elimu, Maamrishi na Makatazo Yake.

Kisha Allah تعالی Akasema:

وَأَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَهَلْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٥﴾

**“Na kwamba hapana mungu ila Yeye. Basi je! Nyinyi ni Waislamu?”**

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيْهِمْ أَعْمَلَهُمْ فِيهَا وَهُمْ فِيهَا لَا يُبْخَسُونَ ﴿١٦﴾  
 أُولَئِكَ الَّذِينَ لَيْسَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ إِلَّا النَّارُ وَحَبِطَ مَا صَنَعُوا فِيهَا وَبِطِلَ مَا كَانُوا  
 يَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

**15. Wanaotaka maisha ya dunia na pumbao lake Tutawalipa humo vitendo vyao kamili, na wao humo hawatopunjwa.**

**16. Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika waliyoyafanya, na yatapotea bure waliyokuwa wakiyatenda.**

### Mwenye Kutaka Dunia Yeye Hana Fungu Akhera

Al-Awafi amesema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika kutoa maelezo ya ayah hii. Hakika watu wa ria wanaofanya matendo kwa madhumuni ya kuwaonesha watu, watalipwa matendo yao mema hapa duniani, na hilo ni kwamba wao hawatadhulumiwa kitu hata chenye kulingana na kokwa ya tende. Anasema: Mwenye kufanya tendo jema kwa kuitaka dunia, mithili ya swaumu, Sala na kisimamo cha usiku, hafanyi hayo isipokuwa kwa kutafuta dunia, Allah تعالی Anasema: ‘Nitamlipa ambacho amekitaka hapa duniani, miongoni mwa malipo, na yatabatilika matendo yake ambayo alikuwa anayatenda kwa kutaka dunia na yeye akhera ni katika wenye kupata hasara.’<sup>1</sup>

Kama hivi imepokewa kutoka kwa Mujahid, Dhahhak na watu wengine.<sup>2</sup> Na Anas Bin Maliki na Hassan wamesema: Ilishuka aya hii kwa Mayahudi na

<sup>1</sup> Tabari 15/263.

<sup>2</sup> Tabari 15/264, 265.

Manaswara.<sup>1</sup> Mujahid na wengine wamesema: Ilishuka kwa watu wa ria<sup>2</sup> wenye kuwaonesha watu matendo yao. Qatadah amesema: Yule ambaye dunia imekuwa ndiyo hamu na matakwa yake Atamlipa yeye kwa matendo yao mema hapa duniani, kisha atakwenda akhera hali ya kuwa hana jema lolote ambalo atapewa malipo kwa hilo. Ama Muumini, atalipwa kwa matendo yake mema duniani na pia atalipwa kwa matendo hayo huko akhera.<sup>3</sup> Allah تعالى Amesema:

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصْلَاهَا  
 مَذْمُومًا مَدْحُورًا ﴿١٧﴾ وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ  
 سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا ﴿١٨﴾ كُلًّا نُمِدُّ هُنُوًا وَهَنُورًا ۖ وَهَنُورًا ۖ وَهَنُورًا ۖ وَهَنُورًا ۖ وَمَا كَانَ عَطَاءُ  
 رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿١٩﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۗ وَلَٰلِآخِرَةِ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ  
 تَفْضِيلًا ﴿٢٠﴾

***“Anaye taka yapitayo upesi upesi, Tutafanya haraka kumletea hapahapa Tunayo yataka kwa Tumtakaye. Kisha Tumemuekea Jahannamu; ataingia humo hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa na kufurushwa. Na anayeitaka Akhera, na akazifanyia juhudi a’ mali zake, naye ni Muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa. Wote hao Tunawakunjulia - hawa na hao - katika neema za Mola wako Mlezi. Wala neema za Mola wako Mlezi hazizuiliki. Angalia vipi Tulivyo wafadhili baadhi yao kuliko wenginewe. Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na fadhila kubwa zaidi.” (17:18-21)***

مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي حَرْثِهِ ۗ وَمَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ  
 مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ ﴿٢١﴾

***“Mwenye kutaka mavuno ya Akhera Tutamzidishia katika mavuno yake, na mwenye kutaka mavuno ya duniani Tutampa katika hayo, lakini katika Akhera hana fungu.” (42:20)***

<sup>1</sup> Tabari 15/265.

<sup>2</sup> Tabari 15/266.

<sup>3</sup> Tabari 15/264.

أَفَمَن كَانَ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّهِ وَيَتْلُوهُ شَاهِدٌ مِّنهُ وَمِن قَبْلِهِ  
 كَتَبَ مُوسَىٰ إِمَامًا وَرَحْمَةً ۗ أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَمَن  
 يَكْفُرْ بِهِ مِّن الْأَحْزَابِ فَالْأَنَارُ مَوْعِدُهُ ۗ فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ  
 مِّنْهُ ۗ إِنَّهُ الْحَقُّ مِن رَّبِّكَ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا  
 يُؤْمِنُونَ ﴿١٧﴾ وَمَن أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۗ  
 أُولَٰئِكَ يُعْرَضُونَ عَلَىٰ رَبِّهِمْ وَيَقُولُ الْأَشْهَادُ هَٰؤُلَاءِ  
 الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ أَلَا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ  
 ﴿١٨﴾ الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا  
 وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿١٩﴾ أُولَٰئِكَ لَمْ يَكُونُوا  
 مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانَ لَهُم مِّن دُونِ اللَّهِ مِن  
 أَوْلِيَاءَ ۗ يَضْعَفُ لَهُمُ الْعَذَابُ ۗ مَا كَانُوا يَسْتَطِيعُونَ السَّمْعَ  
 وَمَا كَانُوا يُبْصِرُونَ ﴿٢٠﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ حَسِبْنَا أَنفُسَهُمْ  
 وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢١﴾ لَا جَرَمَ لَهُمْ فِي  
 الْآخِرَةِ هُمْ الْأَخْسَرُونَ ﴿٢٢﴾

أَفَمَن كَانَ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّهِ وَيَتْلُوهُ  
 شَاهِدٌ مِّنهُ وَمِن قَبْلِهِ كَتَبَ مُوسَىٰ  
 إِمَامًا وَرَحْمَةً ۗ أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ  
 وَمَن يَكْفُرْ بِهِ مِّن الْأَحْزَابِ فَالْأَنَارُ  
 مَوْعِدُهُ ۗ فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّنْهُ ۗ إِنَّهُ  
 الْحَقُّ مِن رَّبِّكَ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ  
 لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٧﴾

17. "Basi je, mtu aliye na dalili  
 wazi itokayo kwa Mola  
 wake Mlezi, inayofuatwa na  
 shahidi anayetoka kwake,  
 na kabla yake kilikuwa  
 Kitabu cha Musa kilicho-  
 kuwa mwongozi na rehema  
 - hao wanamuamini, na  
 anayemkataa katika  
 makundi, basi Moto ndio  
 pahala pa miadi yao. Basi  
 usiwe na shaka juu ya hayo.

**Hii ni Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi; lakini watu wengi hawaamini."**

**Na Yule Ambaye Anaamini Katika Qurani Yupo Katika Ukweli Uliyo Sahihi  
 Kutoka kwa Mola Wake**

Allah تعالی Anaeleza kuhusu hali ya waumini ambao wao wako juu ya umbile halisi, Allah تعالی ambalo Amewaumba waja wake miongoni mwa kumkiri Yeye, kwamba hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye.

Kama Allah تعالی Alivyosema:



فَأَقْرَهُ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ اللَّهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا

**“Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu...” (30:30)**

Na katika Sahihi mbili (Bukhary na Muslim), kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema,

«كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ عَلَى الْفِطْرَةِ فَأَبَوَاهُ يُهَوِّدَانِهِ أَوْ يُنَصِّرَانِهِ أَوْ يُمَجْسِبَانِهِ كَمَا نُوَلِّدُ الْبَيْهَمَةَ بِبَيْمَةٍ جَمْعَاءَ هَلْ تُجْسُونَ فِيهَا مِنْ جَذَعَاءَ؟»

*“Kila mtoto anazaliwa katika umbile halisi Aliloumbiwa na Allah, kwa hiyo wazazi wake wanamfanya awe Myahudi au Mnasara au Mmajusi. Kama anavyozaliwa mnyama hali ya kuwa amekamilika viungo vyake. Je mnahisi mapungufu yoyote katika viungo vyake?! (Kwa maana katika umbile lake la asili)”<sup>1</sup>*

Na imekuja katika Sahihi ya Muslim kutoka kwa Iyadhi Bin Himaar رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ amesema: Allah تعالى Anasema:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حُنَفَاءَ فَجَاءَتْهُمْ الشَّيَاطِينُ فَاجْتَنَّتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ وَحَرَمَتْ عَلَيْهِمْ مَا أَحَلَّلْتُ لَهُمْ، وَأَمَرْتُهُمْ أَنْ يُشْرِكُوا بِي مَا لَمْ أَنْزِلْ بِهِ سُلْطَانًا»

*“Hakika Mimi Nimewaumba waja wangu wakiwa ni wasafi, mashetani wakawajia na kuwatoa katika dini yao na kuwaharamishia Niliyowahalalishia na wakawaamrisha wanishirikishe Mimi kwa ambayo Sijayateremshia ushahidi.”<sup>2</sup>*

Kwa hiyo Muumini ni mwenye kubaki juu ya umbile hilo halisi. Kauli Yake Allah تعالى:

وَيَتْلُوهُ شَاهِدٌ مِّنْهُ

**“Inayofuatwa na shahidi anayetoka kwake.”**

Maana yake: Akamjia shahidi kutoka kwa Allah تعالى, na shahidi mwenyewe ni yale aliyoyafunua kwa njia ya wahyi kwa Mtume ﷺ, miongoni mwa sheria

<sup>1</sup> Fat'hul al-Bari 3/290, na Muslim 4/2047.

<sup>2</sup> Muslim 4/2197.

zilizo safi zilizo hitimishwa zilizo tukufu zinazokamilishwa kwa sheria ya Muhammad ﷺ rehma za Allah تعالى na amani ziwe juu yake, na juu yao wote. Na hilo ni kwa sababu ya kuwa Muumini mbele yake kuna maumbile yanayoshuhudia sheria kwa jumla, na ufafanuzi unachukuliwa kutokana na sheria na maumbile yanaisadikisha sheria na yanaiamini. Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

أَفَمَنْ كَانَ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّهِمْ وَيَتْلُوهُ شَاهِدٌ مِّنْهُ

***“Basi je, mtu aliye na dalili wazi itokayo kwa Mola wake Mlezi, inayofuatwa na shahidi anayetoka Kwake...”***

Nayo ni Qur’ani, ameifikisha Jibril عليه السلام kwa Mtume Muhammad ﷺ, naye ameifikisha kwa Ummah wake.

Kisha Allah تعالى Amesema:

وَمِن قَبْلِهِمْ كَتَبْنَا مُوسَىٰ

***“...Na kabla yake kilikuwa Kitabu cha Musa...”***

Maana yake: Na kabla ya Qur’ani kuna kitabu cha Musa عليه السلام nacho ni Taurati,

إِمَامًا وَرَحْمَةً

***“Hali ya kuwa ni kiongozi na rehma...”***

Maana yake: Amekiteremsha Allah تعالى kwa Ummah huo, hali ya kuwa ni kiongozi kwao na ni kigezo ambacho wanakifuata na ni rehma kutoka kwa Allah تعالى kwao, kwa hiyo mwenye kuiamini Taurati ukweli wa kuiamini, Imani hiyo itampeleka kwenye kuiamini Qur’ani, na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِمْ

***“Hao wanamuamini...”***

Kisha Allah تعالى Amesema, hali ya Kumkemea yule ambaye ameikadhibisha Qur’ani au chochote kutoka humo,

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِمْ مِنَ الْأَحْزَابِ فَآلِنَا لَهُ مَوَٰعِدُهُمْ

***“Na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao...”***

Kwa maana: Mwenye kuikadhibisha Qur'ani miongoni mwa baki ya watu wa ardhini, washirikina wao na makafiri wao, na watu wa kitabu miongoni mwa mataifa mbalimbali ya wanadamu, kwa kutofautiana rangi zao na jinsi zao na maumbile yao, katika wale ambao Qur'an imewafikia.

Kama Allah تعالى Alivyosema:

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

**“Nikukumbusheni kwayo na aliefikiwa” (6:19)**

Na Allah تعالى Amesema:

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

**“Sema enyi watu mimi ni mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote...”(7:158)**

Allah تعالى Akasema:

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنْ الْأَحْزَابِ فَأَلْنَا مَوْعِدَهُ

**“Na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao...”**

Na imekuja katika Sahihi ya Muslim kutoka kwa Abu Musa al-'Ashari رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَا يَسْمَعُ بِي أَحَدٌ مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ يَهُودِيٍّ! [أَوْ] نَصْرَانِيٍّ ثُمَّ لَا يُؤْمِنُ بِي إِلَّا دَخَلَ النَّارَ»

**“Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake hatanisikia mimi mtu yeyote katika Ummah huu, Myahudi wala Mnaswara. Kisha asiniamini isipokuwa ataingia motoni”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Muslim 1/135.

## Ushahidi wa Kila Hadithi na Maelezo Yake Umehakikiwa Ndani ya Qur'ani

Amesema Abuu Ayyuub Sakhtiyaaniy kutoka kwa Saeed bin Jubayr رضي الله عنه, amesema: Nilikuwa sisikii hadithi yoyote kutoka kwa Mtume ﷺ isipokuwa ninakuta ushahidi wake au alisema kusadikishwa kwake katika Qur'ani, ikanifikia kwamba Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَسْمَعُ بِي أَحَدٌ مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ يَهُودِيٍّ وَلَا نَصْرَانِيٍّ ثُمَّ لَا يُؤْمِنُ بِي إِلَّا دَخَلَ النَّارَ»

*"Hatanisikia mimi mtu yeyote katika Ummah huu Myahudi wala Mnaswara kisha asiniamini, isipokuwa ataingia motoni."*

Nikawa ninasema uko wapi uthibitisho wake katika kitabu cha Allah تعالى. Amesema: Na ni mara chache sana ambapo nimesikia kutoka kwa Mtume ﷺ isipokuwa ninapata kwa maneno hayo uthibitisho wake katika Qur'ani, mpaka nikaikuta aya hii:

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَالنَّارُ مَوْعِدُهُ.

***"...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao".***

Amesema, katika mila zote. Na Kauli ya Allah تعالى:

فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّنْهُ إِنَّهُ الْحَقُّ مِن رَّبِّكَ

***"...Basi usiwe na shaka juu ya hayo. Hii ni Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi..."***

Na hali ya kuwa: Qur'ani ni haki kutoka kwa Allah تعالى haina shaka ndani yake, kama Allah تعالى Alivyosema:

الْمُر ۞ تَنْزِيلُ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ۞

***"Alif laam miim, uteremsho wa kitabu hakina shaka ndani yake kutoka kwa mola wa walimwengu." (32:1-2)***

Na Allah تعالى Akasema:

الْم ﴿١٧﴾ ذَٰلِكَ الْكِتَابُ لَا رَيْبَ فِيهِ

**“Alif laam miim, hicho kitabu hakina shaka ndani yake.”**

Na kama Kauli Yake:

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٨﴾

**“...Lakini watu wengi hawaamini”**

Na kama Kauli Yake:

وَمَا أَكْثَرَ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٩﴾

**“...Na hawawi wengi wa watu japo utafanya pupa hawaamini.” (12:103)**

Allah تعالی Amesema:

وَإِنْ تُطِيعْ أَكْثَرُ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

**“Ukiwatii wengi walioko katika ardhi watakupoteza katika njia.” (6:116).**

Allah تعالی Amesema:

وَلَقَدْ صَدَقَ عَلَيْهِمْ إِبْلِيسُ ظَنَّهُ فَاتَّبَعُوهُ إِلَّا فَرِيقًا مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٠﴾

**“Na hakika Ibilisi amewasadikisha dhana yake wakamfuata isipokuwa kundi miongoni mwa waumini.” (34:20)**

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ۗ أُولَٰئِكَ يُعْرَضُونَ عَلَىٰ رَبِّهِمْ وَيَقُولُ

الْأَشْهَادُ هَٰؤُلَاءِ الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ أَلَا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿٢١﴾ الَّذِينَ

يَصُدُّونَ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٢٢﴾ أُولَٰئِكَ لَمْ يَكُونُوا

مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانَ لَهُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن أَوْلِيَاءَ ۗ يُضَعِفُ لَهُمْ الْعَذَابَ ۗ مَا

كَانُوا يَسْتَطِيعُونَ السَّمْعَ وَمَا كَانُوا يُبْصِرُونَ ﴿٢٣﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ وَضَلَّ

عَنَّهُمْ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٢٤﴾ لَا جَرَمَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمْ الْآخِسِرُونَ ﴿٢٥﴾

**18. Na nani aliyedhaalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia Mwenyezi Mungu uwongo? Hao watahudhurishwa mbele ya Mola wao Mlezi, na mashahidi watasema: Hawa ndio waliomtungia uwongo Mola wao Mlezi. Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate waliodhulumu,**

**19. Ambao wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanaitakia ipotoke, na wanaikataa Akhera.**

**20. Hao hawawezi kushinda katika ardhi, wala hawana walenzi isipokuwa Mwenyezi Mungu. Watazidishiwa adhabu. Hawakuwa wakiweza kusikia wala hawakuwa wakiona.**

**21. Hao ndio waliozikhasiri nafsi zao, na yakawapotea waliyokuwa wakiyazua.**

**22. Bila ya shaka hakika wao ndio wenye kukhasiri huko Akhera.**

**Wenye Kumzulia Allah تعالی, Wanawazuia Watu na Njia Yake, Hao Ndiyo Wenye Kupata Hasara Sana.**

Allah تعالی Anabainisha hali ya wale ambao wanamzulia na kufedheheka kwao katika nyumba ya Akhera mbele za viumbe miongoni mwa Malaika, Mitume na Manabii, bali watu na majini.

Kama alivyopokea Imamu Ahmad kutoka kwa Swafwan bin Muhrizi amesema: 'Nilikuwa nimeushika mkono wa Ibni Omar رضي الله عنهما, ghafla alimtokea mtu akasema: 'Vipi ulimsikia Mtume ﷺ akisema kuhusu kunong'ona Siku ya Kiyama?', Akasema: 'Nilimsikia akisema:

«إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يُدْنِي الْمُؤْمِنَ فَيَضَعُ عَلَيْهِ كَفَّهُ، وَيَسْتُرُهُ مِنَ النَّاسِ، وَيَقْرُرُهُ بِدُنُوبِهِ وَيَقُولُ لَهُ: أَتَعْرِفُ ذَنْبَ كَذَا؟ أَتَعْرِفُ ذَنْبَ كَذَا؟ أَتَعْرِفُ ذَنْبَ كَذَا؟ حَتَّى إِذَا قَرَّرَهُ بِدُنُوبِهِ وَرَأَى فِي نَفْسِهِ أَنَّهُ قَدْ هَلَكَ قَالَ: فَإِنِّي قَدْ سَتَرْتُهَا عَلَيْكَ فِي الدُّنْيَا وَإِنِّي أَغْفِرُهَا لَكَ الْيَوْمَ»

*"Hakika Mwenyezi Mungu Aliyeshinda na Utukufu Atamsogeza muumini, Ataiweka juu yake Hifadhi Yake na Atamsitiri na watu na Atamtaka athibitisha madhambi yake na Atamuambia: 'Je unajua*

*dhambi kadha? Je unaijua dhambi kadha? Je unaijua dhambi kadha mpaka atakapomfanya ayakubali madhambi yake na akaona katika nafsi yake kwamba yeye ameangamia, Atasema, 'Hakika Mimi Ndiye Niliyeyasitiri juu yako duniani na hakika Mimi Nitakusamehe madhambi hayo leo."*

Kisha atapewa kitabu cha matendo yake mema. Ama kuhusu makafiri na wanafiki, mashahidi watasema:

هُتُولَاءِ الَّذِينَ كَذَبُوا عَلَىٰ رَبِّهِمْ ۗ أَلَا لَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٧﴾

***"Hawa ndio waliomtungia uwongo Mola wao Mlezi. Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate waliodhulumu."***<sup>1</sup>

Bukhari na Muslim wameinukuu hadithi hii katika Sahihi mbili.<sup>2</sup>

Na Kauli Yake,

الَّذِينَ يَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا

***"Ambao wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanaitakia ipotoke."***

Maana yake: wanawarudisha watu kutokuifuata haki na kufuata njia ya uongofu ambayo inafikisha kwa Allah تعالى Mwenye Kushinda, Mwenye Kutukuka, na wanawaepusha na Pepo.

وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا

***"Wanaitakia ipotoke..."***

Maana yake: Na wanataka njia yao iwe ni kombo si yenye kunyooka.

Na Kauli Yake,

وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٢٢﴾

***"Na wanaikataa Akhera."***

Maana yake: Wanaikanusha wanakadhibisha kutuka kwake na kuwepo kwake

<sup>1</sup> Ahmad: 2/74.

<sup>2</sup> Fat'hul al-Bari: 8/204, na Muslim: 4/2120.

أُولَئِكَ لَمْ يَكُونُوا مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كَانَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ

**“Hao hawawezi kushinda katika ardhi, wala hawana walenzi isipo kuwa Mwenyezi Mungu.”**

Maana yake: Watakuwa chini ya Nguvu Zake, Uwezo Wake, Mashiko Yake na Utawala Wake, na Yeye Anaweza Kuwaadhibu katika nyumba ya dunia kabla ya akhera.

إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِیَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ ﴿٤٢﴾

**“Hakika hapana jambo jengine anawachelewesha mpaka siku ambayo yatakodoka ndani yake macho.” (14:42)**

Katika Sahihi mbili (Bukhary na Muslim), Mtume amesema ﷺ,

«إِنَّ اللَّهَ لَيُنْبِئِي لِلظَّالِمِ حَتَّى إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يُفْلِتْهُ»

**“Hakika Mwenyezi Mungu Humpa muda dhalimu mpaka Atakapomkamata Hamuachii.”<sup>1</sup>**

Na kwa sababu hiyo Allah تعالی Amesema:

يُضَعَفُ لَهُمُ الْعَذَابُ

**“Watazidishiwa adhabu...”**

Kwa maana: Wataongezewa adhabu kwa sababu Allah تعالی Amewapa masikio, macho na nyoyo, kwa hiyo basi haukuwasaidia uoni wao wala kufahamu kitu, bali walikuwa viziwi katika kusikia haki, vipofu katika kuifuata, kama Alivyoeleza Allah تعالی kuhusu wao wakati wa kuingia kwao motoni.

Katika Kauli Yake:

وَقَالُوا لَوْ كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا فِي أَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١٠﴾

**“Na watasema: Lau kuwa tungelisikia, au tungelikuwa na akili, tusingelikuwa katika watu wa Motoni!” (67:10)**

<sup>1</sup> Fat'hul al-Bari 8/205, na Muslim 4/1997.



Akasema tena,

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَاهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ

**“Na ambao wamekufuru na wakazuia na njia ya Mwenyezi Mungu Tunawazidishia adhabu juu ya adhabu...” (16:88)**

Kwa ajili hii wataadhibiwa juu ya kila jambo ambalo waliliacha na juu ya kila katazo ambalo walilifanya.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

أُولَئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ وَصَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢١﴾

**“Hao ndio waliozikhasiri nafsi zao, na yakawapotea waliyokuwa wakiyazua.” (11:21)**

Maana yake: Wamezitia katika hasara nafsi zao, kwa sababu hiyo, wako katika moto mkali sana, wanaadhibiwa humo na haisitishwi kwao adhabu yake, hata kwa kiasi cha kufumba jicho na kufumbua.

Kama Allah تعالى Alivyosema:

كُلَّمَا حَبَتِ زِدْنَاهُمْ سَعِيرًا ﴿٩٧﴾

**“Kila unapofia Tunauzidishia mwako.” (17:97)**

Na Kauli Yake,

وَصَلَّ عَنْهُمْ

**“...na yakawapotea...”** Maana yake: Yamewaondoka.

مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٠٦﴾

**“...waliyokuwa wakiyazua.”**

Kinyume cha Allah تعالى miongoni mwa washirika na Masanamu hayakuwatosholeza jambo lolote bali yamewadhuru kuwadhuru kukubwa sana.

Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كُفْرِينَ ﴿٦﴾

**“Na pindi watu wakifufuliwa watakuwa ni maadui zao na kwa ibada zao watazikataa.” (46:6)**

Ni kama Kauli Yake,

إِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتُّبِعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا وَرَأَوُا الْعَذَابَ وَتَقَطَّعَتْ بِهِمُ الْأَسْبَابُ ﴿١٦٦﴾

**“Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata, na hali ya kuwa wamekwisha iona adhabu; na yatakatika mafungamano yao.” (2:166)**

Na zisizokuwa hizo miongoni mwa aya mbalimbali zenye kufahamisha juu ya kupata kwao hasara na kuangamia kwao.

Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

لَا جَرَمَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمْ الْأَخْسَرُونَ ﴿١١٢﴾

**“Hapana shaka kuwa wao katika akhera ni walio na khasara zaidi.” (11:22)**

Katika Aya hii Allah تعالى Anaeleza kuhusu mwisho wao, kwamba wamepata hasara zaidi kuliko watu wengine katika mauzo yao katika nyumba ya akhera, kwa sababu wameacha daraja za juu peponi, na wakachagua vidato vya chini katika moto, na wamebadilisha neema za Peponi wakachukua moto mkali sana, na wameacha kunywa mvinyo uliofunikwa na kuchukua upepo wa moto, maji ya kuchemka na kivuli cha moshi mweusi. Na wameacha wanawake wa Peponi (*Hurul-Ain*) wenye macho yenye kupendeza – wakachagua chakula ambacho ni maji machafu yanayotiririka kutoka katika viwiliwili vya watu wa motoni, na wameacha makasri ya juu kwa kuchagua moto mkali, wameacha kuwa karibu na Allah تعالى na kumuona Kwake, wakachukua machukivu ya Allah تعالى na Mateso Yake, kwa hiyo ni hakika kwamba wao huko Akhera wao ndiyo wenye kupata hasara zaidi.

\* \* \*

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَأَخْبَتُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ  
 أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٣﴾ \* مَثَلُ  
 الْفَرِيقَيْنِ كَالْأَعْمَىٰ وَالْأَصْمَىٰ وَالْبَصِيرِ وَالسَّمِيعِ ۗ هَلْ  
 يَسْتَوِيَانِ مَثَلًا ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٢٤﴾ ۖ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ  
 قَوْمِهِ إِنِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢٥﴾ ۖ أَنْ لَا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۖ  
 إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمِ إِلْيَاسَ ﴿٢٦﴾ فَقَالَ الْمَلَأُ  
 الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ مَا تَرَنَّاكَ إِلَّا بَشْرًا مِثْلَنَا وَمَا  
 تَرَنَّاكَ أَتَّبَعَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَادُوا بِادِّئِ الرَّأْيِ وَمَا  
 نَرَىٰ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ بَلْ نَظُنُّكُمْ كَاذِبِينَ ﴿٢٧﴾  
 قَالَ يَبْقَوْمِ اأَرَأَيْتُمْ إِن كُنتُ عَلَىٰ بَيْنَةٍ مِّن رَّبِّي وَءَاتَنِي رَحْمَةً  
 مِّن عِندِهِ فَعَمَّيْتُ عَلَيْكُمُ نَارًا مِّن مَّوَاهِجِهَا وَأُشْرُهَا كَرِهُونَ  
 ﴿٢٨﴾ وَيَبْقَوْمِ لَآ أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مَالًا ۖ إِن أُجِرَىٰ إِلَّا عَلَىٰ  
 اللَّهِ ۗ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۖ إِنَّهُمْ مُلْقُوا رَبِّهِمْ وَلِيكِنِّي  
 أَرْتِكُمُ قَوْمًا يَّجْهَلُونَ ﴿٢٩﴾ وَيَبْقَوْمِ مَنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ  
 إِن طَرَدْتُهُمْ ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٣٠﴾

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ  
 وَأَخْبَتُوا إِلَىٰ رَبِّهِمْ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ  
 الْجَنَّةِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ \*  
 مَثَلُ الْفَرِيقَيْنِ كَالْأَعْمَىٰ وَالْأَصْمَىٰ  
 وَالْبَصِيرِ وَالسَّمِيعِ ۗ هَلْ يَسْتَوِيَانِ  
 مَثَلًا ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٢٣﴾

**23. Hakika wale walio-  
 amini, na wakatenda  
 mema, na wakanyenyekea  
 kwa Mola wao Mlezi, hao  
 ndio watu wa Peponi, na  
 humo watadumu.**

**24. Mfano wa makundi  
 mawili ni kama kipofu  
 kiziwi, na mwenye kuona  
 na anasikia. Je, wawili  
 hawa wanakuwa sawa kwa  
 kufananishwa? Basi, je,  
 hamfikiri?**

## Malipo ya Watu wa Imani

Allah تعالیٰ Alipotaja hali ya watu waovu Amefuatisha kwa Kutaja hali ya watu wema, nao ni wale ambao wameamini na wakatenda matendo mema na zikaamini nyoyo zao, na viungo vyao vikatenda matendo mema, kwa maneno na matendo katika kuleta utii na kuacha matendo maovu. Na kwa sababu hiyo wamerithi Pepo zenye kukusanya vyumba vya juu na vitanda vilivyopangwa, matunda yaliyo karibu na matandiko yaliyonyanyuka, wanawake

wazuri walio bora, matunda mbalimbali, vyakula vyenye kutamaniwa, vinywaji vyenye ladha na kumtazama Muumba wa ardhi na mbingu, na wao katika neema hizo ni wenye kukaa milele, hawatakufa, hawatakuwa wazee, hawatakuwa wagonjwa, hawatalala, hawatajisaidia (haja kubwa na ndogo), hawatatema mate na hawatatoa kamasi. Hakitakuwa kile kitakachowatoka isipokuwa ni jasho la miski.

### Mfano wa Waumini na Makafiri

Kisha Allah تعالی Akapiga Mfano wa makafiri na waumini, Amesema,

﴿ مَثَلُ الْفَرِيقَيْنِ ﴾

*“Mfano wa makundi mawili...”*

Maana yake: Wale ambao Amewasifu huko mwanzo kwa uovu, na waumini kwa wema, hao.

﴿ كَالْأَعْمَىٰ وَالْأَصْمَىٰ ﴾

*“Ni kama kipofu na kiziwi.”*

Na hawa ni kama mwenye kuona na mwenye kusikia. Kwa hiyo kafiri ni kipofu wa njia ya haki duniani na akhera haongoki kwenye kheri na wala haijui, ni kiziwi wa kuzisikia hoja. Kwa hiyo hayasikii yenye kumnufaisha,

﴿ وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَّأَسْمَعَهُمْ ۗ ﴾

*“...Na lau Angejuwa Mwenyezi Mungu kwao kheri Angewafanya wasikie...” (8:23)*

Ama Muumini ni mjanja, mwerevu, ana ufahamu, anaiona haki, ana pambanua kati ya haki na batili. Kwa hiyo anafuata kheri na anaacha shari, anasikiliza sana hoja, anateganisha kati yake na shubuha na utatanishi, haifungamanishi na batili. Je analingana huyu na huyu?

﴿ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴾

*“Hivi hamkumbuki.”*

Hivi hamzingatii mkaweza kutofautisha kati ya hawa na wale? Kama Alivyosema katika aya nyengine.

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۗ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

**"Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu."** (59:20)

Kisha Allah تعالى Akasema tena:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ ۖ إِنِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢١﴾ أَنْ لَا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۗ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمِ الْبُرْجِ ﴿٢٢﴾ فَقَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَوْمِهِ مَا تَرْتَلِكُ إِلَّا بَشْرًا مِّثْلَنَا وَمَا تَرْتَلِكُ إِلَّا الَّذِينَ ۖ هُمْ أَرَادُوا بَادِيَ الرُّؤْيِ وَمَا تَرَىٰ لَكُمْ عَلَيْنَا مِن فَضْلٍ ۖ بَلْ نُنظِّمُ كَذِبِينَ ﴿٢٣﴾

**25. Na Sisi Tulimtuma Nuhu kwa watu wake, akawaambia: Hakika mimi ni mwonyaji kwenu ninayebainisha.**

**26. Ya kwamba msimuabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu tu. Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Chungu.**

**27. Na wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake: Hatukuoni wewe ila ni mtu tu kama sisi, wala hatukuoni wamekufuata ila wale waliokuwa kwetu watu duni, wasiokuwa na akili. Wala hatukuoneni kuwa mna ubora wowote kutushinda sisi. Bali tuna hakika nyinyi ni waongo.**

**Kisa cha Nuhu عليه السلام na Mjadala Wake Pamoja na Watu Wake**

Allah تعالى anaeleza kuhusu Mtume Nuhu عليه السلام, Mtume wa kwanza ambaye Allah تعالى Alimpeleka kwa watu wa ardhi miongoni mwa washirikina wenye kuabudu Masanamu, na kwamba yeye aliwaambia watu wake,

إِنِّي لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢١﴾

**"Hakika mimi ni mwonyaji kwenu ninayebainisha."**

Maana yake: Muwazi wa kukukhofisheni, adhabu ya Allah تعالى iwapo mtaabudu asiye kuwa Allah تعالى, na kwa sababu hiyo amesema Nuhu عليه السلام:

أَنْ لَا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ

**“Ya kwamba msimuabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu tu.”**

Na Kauli Yake:

إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمِ أَلِيمٍ ﴿٢٣﴾

**“Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku Chungu.”**

Maana yake: Iwapo mtaendelea juu ya yale ambayo nyinyi mko juu yake Atawaadhibuni Allah تعالى adhabu yenye kuumiza yenye kutia uchungu iliyo ngumu, katika nyumba ya Akhera.

فَقَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ

**“...Na wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake...”**

Na Malau, ni mabwana na wakuu katika makafiri miongoni mwao.

مَا نَرَاكَ إِلَّا بَشَرًا مِثْلَنَا

**“Hatukuoni wewe ila ni mtu tu kama sisi.”**

Maana yake: Hukuwa malaika isipokuwa wewe ni mtu, vipi umeletewa wahyi kinyume chetu? Kisha:

وَمَا نَرَاكَ اتَّبَعَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَادُوا

**“Wala hatukuoni wamekufuata ila wale waliokuwa kwetu watu duni.”**

Kama vile wauzaji, wafumaji na mifano ya hao, na wala hawakukufuata watukufu wala viongozi miongoni mwetu. Kisha hawa ambao wamekufuata, hakukuwa kufuata kwao kunatokana na busara walizokuwa nazo au maarifa ya kupima mambo, bali wamekufuata kwa kuwalingania kwako tu, hivyo wakakuitikia na wakakufuata, kwa sababu hiyo wakasema:

وَمَا نَرَاكَ اتَّبَعَكَ إِلَّا الَّذِينَ هُمْ أَرَادُوا بِرَأْيِ

**“Wala hatukuoni wamekufuata ila wale waliokuwa kwetu watu duni, wasiokuwa na akili.”**

Maana yake: Katika mwanzoni mwa maoni:

وَمَا نَرَىٰ لَكُمْ عَلَيْنَا مِن فَضْلٍ

**“Wala hatukuoneni kuwa mna ubora wowote.”**

Wanasema: hatukuona kwenu juu yetu ubora wowote katika maumbile, tabia, kipato, wala hali yoyote wakati mlipoingia katika dini yenu hii.

بَلْ نُنظِّئُكُمْ كَذِبِينَ ﴿٣٠﴾

**“Bali tuna hakika nyinyi ni waongo.”**

Maana yake: Katika lile ambalo mnadai kuwa mnalo, miongoni mwa ubora, wema, ibada na mafanikio ya Akhera, wakati mtakapokuwa mmefika huko. Huu ndiyo upingaji wa makafiri juu ya Nuhu عليه السلام na wafuasi wake, na hiyo ni dalili ya ujinga wao na uchache wa elimu na akili zao. Kwa hakika dosari haipo katika haki au kufuatwa na wanyonge, kwa kuwa haki hiyo yenyewe iko sahihi, ni sawasawa wameifuata watukufu au wanyonge, bali ni ukweli ambao hauna shaka ndani yake, kuwa wafuasi wa haki wao ndiyo watukufu, japokuwa ni wanyonge na mafukara, na wale wanaoukataa ukweli, hao ndio wanyonge japokuwa ni matajiri. Kisha hali halisi ni kwamba mara nyingi wanaofuata haki ni wanyonge wa watu, na mara nyingi watukufu na wakubwa ndio wanaoipindisha haki, kama Allah تعالى Alivyosema:

وَكَذَلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِّن نَّذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ

أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِم مُّقْتَدُونَ ﴿٣١﴾

**“Na kadhaalika hatukumtuma mwonyaji kwenye mji wowote ila watu wake waliodeka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao.” (43:23)**

Na wakati Hiraqil Mfalme wa Roma alipomuuliza, Abuu Sufiyani Swakhri bin Harb kuhusu sifa za Mtume ﷺ alimuuliza: ‘Je waliomfuata ni watukufu wa watu au wanyonge wao?’ Akasema, ‘bali wanyonge wao.’ Hiraqli akasema: ‘Hao ndiyo wafuasi wa Mitume.’<sup>1</sup> na kauli yao

<sup>1</sup> Fat’hul al-Bari 1/42.

## بَادِيَ الرَّأْيِ

**“Wasiokuwa na akili.”**

Siyo kasoro au aibu kwani haki inapokuwa wazi maoni na fikra yanakuwa hayana nafasi yoyote, bali hapana budi kufuata haki, na hali hii inakuwa kwa kila mwenye weledi na werevu - bali ni kwamba hapa hafikiri isipokuwa mpumbavu au mwenye kulemewa. Na Mitume Rehema za Allah تعالى na amani Yake ziwe juu yao, wote wamekuja na jambo lililo wazi na dhahiri,

Na Kauli Yake:

وَمَا نَرَىٰ لَكُمْ عَلَيْنَا مِن فَضْلٍ

**“Wala hatukuoneni kuwa mna ubora wowote kutushinda sisi...”**

Wao hawaoni hilo, kwa sababu wao ni vipofu wa kuona haki hawasikii wala hawaoni, bali wao wako ndani ya shaka yao, wanazingazinga na katika kiza cha ujinga wanatangatanga. Hao ndiyo wazushi, waongo, wachache na ni wanyonge, na wao katika akhera ndiyo wenye kukhasirika zaidi.

قَالَ يَنْقَوْمِ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيْنَيْهِ مِّن رَّبِّي وَأَتَانِي رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِهِ فَعَمِمَتْ عَلَيْكُمْ  
أَنْ تُلْزِمُوهَا وَأَنْتُمْ هَا كَرِهُونَ ﴿٢٧﴾

**28. Akasema: Enyi watu wangu! Hebu fikirini! Ikiwa mimi ninayo hoja wazi iliyotoka kwa Mola wangu Mlezi, na Amenipa rehema kutoka Kwake, nayo ikakufichikieni; je, tukulazimisheni kuikubali hali nyinyi mnaichukia?**

**Majibu ya Nuhu** عليه السلام

Allah تعالى Anasema Akielezea yale ambayo Nuhu عليه السلام, aliwajibu watu wake, katika hayo:

أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيْنَيْهِ مِّن رَّبِّي

**“Hebu fikirini! Ikiwa mimi ninayo hoja wazi iliyo toka kwa Mola wangu Mlezi.”**

Maana yake: Juu ya yakini, jambo lililo wazi na utume wa kweli, na hiyo ndiyo rehema kubwa kutoka kwa Allah تعالى, kwake na kwao,



فَعُمِّيَتْ عَلَيْكُمْ

**“Nayo ikakufichikieni.”**

Maana yake: Imefichika juu yenu, kwa hiyo hamkuongoka kuifuata, na wala hamkujua thamani yake, bali mmefanya haraka kuikanusha na kuipinga,

أَنْتُمْ كُفُّوا عَنْهَا

**“Je, Tukulazimisheni kuikubali.”**

Maana yake: Tuwafanyie nguvu kuikubali, na hali ya kuwa nyinyi mnaichukia?

وَيَقَوْمٍ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مَا لَمْ يَكُنْ مِنْكُمْ إِلَّا عَلَى اللَّهِ ۗ وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ إِنَّهُمْ مُلْتَقَوْنَ رَبِّهِمْ وَلَكِنِّي أَرَىٰ ذُكُورًا مُّجْهَلُونَ ۗ ﴿٢٩﴾ وَيَقَوْمٍ مِّنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ ۗ إِنَّ طَرْدُهُمْ ءَأَفْلا تَذَكَّرُونَ ﴿٣٠﴾

**29. Na enyi watu wangu! Mimi sikuombeni mali kwa ajili ya haya. Mimi sina ujira ila kwa Mwenyezi Mungu; na mimi sitawafukuza walioamini. Hakika wao watakutana na Mola wao Mlezi, lakini mimi nakuoneni mnafanya ujinga.”**

**30. Na enyi watu wangu! Ni nani atakayenisaidia kwa Mwenyezi Mungu nikiwafukuza hawa? Basi je, hamfikiri?**

Anawaambia watu wake: Siwaombi juu ya kukunasihini, ujira wowote wala mali, ambayo nitaichukua kutoka kwenu, hakika ninachokitaka ni malipo kutoka kwa Allah Mwenye Kushinda na Kutukuka

وَمَا أَنَا بِطَارِدِ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ

**“Na mimi sitawafukuza walioamini.”**

Kana kwamba wao walitaka kwake kuwafukuza waumini, kwa ajili ya kujikweza, na nafasi ya yeye kukaa nao. Kama watu mfano wao walivyomuomba Mtume wa Mwisho ﷺ alifukuze kundi la wanyonge, na akae pamoja nao katika baraza maaalumu.

Allah تعالی Akateremsha:

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ

**“Wala usiwafukuze wanao muomba Mola Mlezi wao asubuhi na jioni...” (6:52)**

Na Allah تعالی Amesema:

وَكَذَلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لِيَقُولُوا أَهْتُوا لِمَنْ آتَى اللَّهُ عَلَيْهِم مِّن بَيْنِنَا أَلَيْسَ اللَّهُ

بِأَعْلَمَ بِالشَّاكِرِينَ ﴿٥٣﴾

**“Na hivi ndivyo Tunavyowajaribu wao kwa wao, ili waseme: Ni hao ndio Mwenyezi Mungu Amewafadhilisha miongoni mwetu? Kwani Mwenyezi Mungu Hawajui wanaoshukuru?” (6:53)**

\* \* \*

وَلَا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ إِنِّي مَلَكٌ وَلَا أَقُولُ إِنِّي مَلَكٌ وَلَا أَقُولُ لِلَّذِينَ تَزْدَرِي أَعْيُنُكُمْ لَنْ يُؤْتِيَهُمُ اللَّهُ خَيْرًا ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا فِي أَنْفُسِهِمْ ۗ وَإِنِّي إِذَا لَمَنْ الظَّالِمِينَ ﴿٣١﴾ قَالُوا يَنْبُوحُ قَدْ جَدَلْتَنَا فَأَكْزَرْتَ جِدَالَنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٣٢﴾ قَالَ إِنَّمَا يَأْتِيكُمْ بِهِ اللَّهُ إِن شَاءَ وَمَا أَنشُرُ بِمُعْجِزِينَ ﴿٣٣﴾ وَلَا يَنْفَعُكُمْ نُصْحِي إِنْ أَرَدْتُ أَنْ أُنصَحَ لَكُمْ إِنْ كَانَ اللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يُغْوِيَكُمْ ۗ هُوَ رَبُّكُمْ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٣٤﴾ أَمْ يَقُولُونَ أَفْتَرَنَاهُ ۗ قُلْ إِنْ أَفْتَرَيْتُهُ ۗ فَعَلَىٰ إِجْرَامِي وَأَنَا بَرِيءٌ ۗ مِمَّا تُخْرَمُونَ ﴿٣٥﴾ وَأَوْحَىٰ إِلَىٰ نُوحٍ أَنَّهُ لَنْ يُؤْمِنَ مِن قَوْمِكَ إِلَّا مَن قَدْ ءَامَنَ فَلَا تَبْتَئِسْ بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾ وَأَصْنَعِ الْفُلَكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحَيْنَا وَلَا تَخْطُبِنِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا ۗ إِنَّهُمْ مُّغْرَقُونَ ﴿٣٧﴾ وَيَصْنَعِ الْفُلَكَ وَكُلَّمَا مَرَّ عَلَيْهِ مَلَأَ مِنْ قَوْمِهِ سَخِرُوا مِنْهُ ۗ قَالَ إِنْ تَسَخَرُوا مِنِّي مِنَّا فَإِنَّا نَسْخَرُ مِنْكُمْ كَمَا تَسْخَرُونَ ﴿٣٨﴾ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ۗ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٣٩﴾ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أُمَّرْنَا وَقَارَ التَّنُورُ ۗ قُلْنَا احْمِلْ فِيهَا مِن كُلِّ زَوْجَيْنِ آتَيْنِ وَأَهْلِكَ إِلَّا مَن سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ وَمَنْ ءَامَنَ ۗ وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ ۗ إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٤٠﴾

وَلَا أَقُولُ لَكُمْ عِندِي خَزَائِنُ اللَّهِ وَلَا أَعْلَمُ الْغَيْبَ وَلَا أَقُولُ إِنِّي مَلَكٌ وَلَا أَقُولُ لِلَّذِينَ تَزْدَرِي أَعْيُنُكُمْ لَنْ يُؤْتِيَهُمُ اللَّهُ خَيْرًا ۗ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا فِي أَنْفُسِهِمْ ۗ وَإِنِّي إِذَا لَمَنْ الظَّالِمِينَ ﴿٣١﴾

**31. Wala sikwambiini kuwa nina khazina za Mwenyezi Mungu; wala kuwa mimi najua mambo ya ghaibu; wala sisemi: Mimi ni Malaika. Wala siwasemi wale ambao yanawadharau macho yenu kuwa Mwenyezi Mungu hatawapa kheri Mwenyezi Mungu Anajua yaliomo katika nafsi zao. Hapo bila ya shaka ningekuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.**

Nuhu عليه السلام Anawaeleza kwamba yeye ni Mtume ﷺ analingania kwenye kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, hana mshirika, kwa idhini ya Allah تعالى Kwake katika hilo, na hawaombi juu ya hilo malipo yoyote, bali yeye analingania anayekutana naye miongoni

mwa watukufu na wanyonge, basi atakayemuitikia atakuwa ameokoka. Na anawaeleza kwamba yeye hana uwezo wa kufanya alitakalo katika hazina za Allah تعالى na hajui ghaibu iliyojificha, isipokuwa yale ambayo Allah تعالى Amemuonesha, na yeye si Malaika, bali yeye ni mtu aliyetumwa, mwenye kupewa nguvu kwa miujiza, na sisemi kuhusu hawa ambao mnaowadharau na mnao wanyongesha kwamba wao hawana malipo yoyote mbele ya Allah تعالى, juu ya matendo yao,

اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا فِي أَنْفُسِهِمْ<sup>ط</sup>

**“Mwenyezi Mungu Anajua yaliomo katika nafsi zao.”**

Wakiwa ni waumini kwa ndani kama inavyoonekana katika hali zao, basi wao wana malipo ya wema, na lau mtu yeyote anadai kuwa hao ni waovu baada ya kuamini kwao huyo atakuwa ni dhalimu, mwenye kusema asio na ujuzi nayo.

قَالُوا يَبْنُوهُ قَدْ جَدَلْتَنَا فَأَكْثَرْتَ جِدَالَنَا فَأْتِنَا بِمَا نَعِدُنَا إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ

﴿٣١﴾ قَالَ إِنَّمَا يَأْتِيكُمْ بِهِ اللَّهُ إِنْ شَاءَ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿٣٢﴾ وَلَا يَنْفَعُكُمْ نُصْحِي إِنْ

أَرَدْتُ أَنْ أَنْصَحَ لَكُمْ إِنْ كَانَ اللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يُغْوِيَكُمْ هُوَ رَبُّكُمْ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٣٣﴾

**32. Wakasema: Ewe Nuhu! Umejadiliana, na umekithirisha kutujadili. Basi tulettee hayo unayotuahidi, ukiwa miongoni mwa wasemao kweli.**

**33. Akasema: Mwenyezi Mungu Atakuleteeni akipenda. Wala nyinyi si wenye kumshinda.**

**34. Wala nasaha yangu haikufaini kitu nikitaka kukunasihini, ikiwa Mwenyezi Mungu Anataka kukuachieni mpotee. Yeye Ndiye Mola wenu Mlezi; na Kwake mtarejeshwa.**

**Watu wa Nuhu عليه السلام Kudai Waletewe Adhabu na Majibu ya Madai Hayo**

Allah تعالى Anasema Akielezea kuhusu watu wa Nuhu عليه السلام Kuharakisha waletewe mateso na Allah تعالى, Adhabu, na Ghadhabu Yake,

قَالُوا يَنْبُوحُ قَدْ جَدَلْتَنَا فَأَكْثَرْتَ جِدَالَنَا

**“Wakasema: Ewe Nuhu! Umejadiliana, na umekithirisha kutujadili...”**

Maana yake: Umehojiana nasi na umezidisha hilo, na sisi hatukufuati.

فَأْتَيْنَا بِمَا تَعِدُنَا

**“Basi tuletee hayo unayotuahidi...”** Maana yake: Miongoni mwa mateso na adhabu, tuapize kwa lolote unalolitaka na litujie hilo unalotuapizia,

إِنْ كُنْتُمْ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٣١﴾ قَالَ إِنَّمَا يَأْتِيكُمْ بِهِ اللَّهُ إِنْ شَاءَ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿٣٢﴾

**“Ukiwa miongoni mwa wasemao kweli. Akasema: Mwenyezi Mungu Atakuleteeni Akipenda. Wala nyinyi si wenye kumshinda.”**  
(11:32-33)

Maana yake: Hakika Ambaye Atakuadhibuni na Kuiharakisha kwenu adhabu, ni Allah تعالى Ambaye Hashindwi na jambo lolote.

وَلَا يَنْفَعُكُمْ نُصْحِي إِنْ أَرَدْتُ أَنْ أَنْصَحَ لَكُمْ إِنْ كَانَ اللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يُغْوِيَكُمْ

**“Wala nasaha yangu haikufaini kitu nikitaka kukunasihini, ikiwa Mwenyezi Mungu Anataka Kukuachieni mptee.”**

Maana yake: Ni jambo gani litakalofaa kwenu kuhusu wito wangu kwenu, kuwakhofisheni na kuwanasihini,

إِنْ كَانَ اللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يُغْوِيَكُمْ

**“...Ikiwa Mwenyezi Mungu Anataka Kukuachieni mptee...”** Maana yake: Kuwapoteza na Kuwaangamiza,

هُوَ رَبُّكُمْ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٣٣﴾

**“Yeye Ndiye Mola wenu Mlezi; na Kwake mtarejeshwa.”**

Maana yake: Yeye Ndiye Mwenye Kumiliki hatamu za mambo yote, Mwenye Kufanya Atakavyo.

Hakimu Mwadilifu Ambaye Hafanyi jeuri, ni Kwake Yeye Kuumba na Kuamrisha, na Yeye Ndiye Muanzishaji, Mrudishaji, Mmiliki wa dunia na akhera.

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَيْنَاهُ قُلْ إِنْ افْتَرَيْتُهُ فَعَلَىٰ إِجْرَامِي وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا تُجْرِمُونَ ﴿٣٥﴾

**35. Auudio wanasema: Amezua? Sema: Ikiwa nimeizua, basi kosa hilo ni juu yangu, na mimi sihusiki na makosa myatendayo.**

**Kutoka Nje ya Mada kwa Ajili ya Ubainifu wa Ukweli wa Mtume ﷺ**

Hayo ni maneno yaliyoingia katikati ya kisa hiki unakitilia mkazo, na kukithibitisha, Allah تعالى Anasema Kumuambia Muhammad ﷺ – hivi wanasema hawa makafiri wenye kupinga ameyazuwa haya na kuyaunda kutoka kwake mwenyewe,

قُلْ إِنْ افْتَرَيْتُهُ فَعَلَىٰ إِجْرَامِي

**“Sema: Ikiwa nimeizua, basi kosa hilo ni juu yangu.”**

Maana yake: Madhambi ya hilo yatakuwa juu yangu,

وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا تُجْرِمُونَ ﴿٣٦﴾

**“Na mimi sihusiki na makosa myatendayo.”**

Maana yake: Hilo si lenye kuundwa wala si lenye kuzuliwa kwa sababu mimi ninayajua mateso yaliyo kwa Allah تعالى kwa ajili ya mwenye kumzulia uongo.

وَأَوْحَىٰ إِلَىٰ نُوحٍ أَنَّهُ لَنْ يُؤْمِنَ مِنْ قَوْمِكَ إِلَّا مَنْ قَدْ ءَامَنَ فَلَا تَبْتَئِسْ بِمَا كَانُوا يَفْعَلُونَ ﴿٣٧﴾ وَأَصْنَعِ الْفُلَكَ بِأَعْيُنِنَا وَّوَحَيْنَا وَلَا تَخْطِبْنِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا إِلَيْهِمْ مَعْرِفُونَ ﴿٣٨﴾ وَيَصْنَعِ الْفُلَكَ وَكُلَّمَا مَرَّ عَلَيْهِ مَلَأَ مِنْ قَوْمِهِ سَخِرُوا مِنْهُ قَالَ إِنْ تَسَخَرُوا مِنِّي فَإِنَّا نَسَخَرُ مِنْكُمْ كَمَا تَسَخَرُونَ ﴿٣٩﴾ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٤٠﴾ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَمْرُنَا وَفَارَ التَّنُورُ قُلْنَا احْمِلْ فِيهَا

مِن كُلِّ زَوْجَيْنِ آتَيْنِ وَأَهْلَكَ إِلَّا مَن سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ وَمَنْ ءَامَنَ وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ

إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٣٦﴾

**36. Na akafunuliwa Nuhu akaambiwa: Hataamini yeyote katika watu wako ila wale waliokwisha amini. Basi usisikitike kwa waliyokuwa wakiyatenda.**

**37. Na unda jahazi mbele ya Macho Yetu na kwa mujibu wa ufunuo Wetu. Wala usinisemeze kuwatetea waliodhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa.**

**38. Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipita wakuu wa kaumu yake wakimkejeli. Yeye akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli na sisi tunakukejelini kama mnavyotukejeli.**

**39. Nanyi mtakuja jua ni nani itakayemfikia adhabu ya kumhizi, na itakayemteremkia adhabu ya kudumu.**

**40. Hata ilipokuja Amri Yetu, na tanuri ikafoka maji, Tulisema: Pakia humo wawili wawili, dume na jike, kutoka kila aina, na ahali zako, isipokuwa wale ambao imekwisha wapitia hukumu; na watu walioamini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.**

**Wahyi kwa Nuhu عليه السلام Kuhusu Hatima ya Watu Wake na Kuamrisha Kufanya Maandalizi kwa Jambo Hilo**

Allah تعالی Anaeleza kuwa Yeye Alipeleka wahyi kwa Mtume Nuhu عليه السلام wakati watu wake walipojiharakishia Mateso ya Allah تعالی na Adhabu Yake, Nuhu عليه السلام akawaapiza maafizo yake ambayo Allah تعالی Amesema kuhusiana nayo,

رَبِّ لَا تَذَرْ عَلَى الْأَرْضِ مِنَ الْكَافِرِينَ دَيَّارًا ﴿٣٧﴾

**“Mola wangu Mlezi! Usimuache juu ya ardhi mkaazi wake yeyote katika makafiri!” (71:26)**

Na Akasema,

فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَأَنْتَصِرْ ﴿٣٨﴾

**“Basi akamuomba Mola wake Mlezi akasema: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru!” (54:10)**

Wakati huo Allah تعالی Akampelekea wahyi,

أَنَّهُ لَنْ يُؤْمِرَ مِنْ قَوْمِكَ إِلَّا مَنْ قَدْ ءَامَنَ

**“Hakika mambo yalivyo hawataamini katika watu wako isipokuwa wale ambao wamekwisha amini...”**

Kwa hiyo usiwahuzunikie na wala jambo lao lisikushughulishie,

وَأَصْنَعِ الْفُلْكَ

**“Na unda jahazi...”** Maana yake: Safina,

بِأَعْيُنِنَا

**“...Mbele ya Macho Yetu...”** Maana yake: Kwa Kuona Kwetu,

وَوَحَيْنَا

**“Na kwa mujibu wa ufunuo Wetu...”**

Maana yake: Mafundisho Yetu kwako kwa kila ambacho utakifanya.

وَلَا تُخَاطَبُنِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا إِنَّهُمْ مُغْرَقُونَ ﴿٣١﴾

**“Wala usinisemeze kuwatetea waliodhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa”.**

Muhammad bin Is’haqa رحمه الله تعالى, ametaja kuhusu Taurati, kwamba Allah تعالی Alimuamrisha Kulitengeza jahazi kutokana na ubao wa msaji, na kulifanya Jahazi hilo urefu wake dhiraa themanini, na upana wake dhiraa hamsini, na kwamba ipakwe sehemu yake ya ndani na sehemu yake ya nje. Kwa sifa na afanye sehemu ya omo (mbele ya Jahazi) nyembamba – itakayokuwa inayakata maji, na urefu wake kwa kwenda juu ilikuwa ni dhiraa thelathini na ilikuwa na tabaka tatu: Kila tabaka ni dhiraa kumi, kwa hiyo tabaka la chini ni la wanyama, na tabaka la kati ni la watu na tabaka la juu ni la ndege, mlango wake katika upana wake una mfuniko, uliofunikwa juu yake<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Tabari 15/318.



وَيَصْنَعُ الْفُلُوكَ وَكُلَّمَا مَرَّ عَلَيْهِ مَلَأَ مِنْ قَوْمِهِ سَخِرُوا مِنْهُ

**“Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipita wakuu wa kaumu yake wakimkejeli.”**

Maana yake: Wanamcheza shere na wanayakadhibisha yale ambayo anawakamia nayo katika kughariki,

قَالَ إِنْ تَسْخَرُوا مِنَّا فَإِنَّا نَسْخَرُ مِنْكُمْ

**“Yeye akasema: Ikiwa nyinyi mnatukejeli na sisi tuna kukejelini kama mnavyo tukejeli...”**

Haya ni makamio makali na matisho yaliosisitizwa,

مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ

**“Ni nani itakayemfikia adhabu ya kumhizi.”**

Maana yake: Yenye kuendelea, Yenye kudumu milele.

وَيُخَلِّ عَلَيْهِ عَذَابٌ مُّهِمٌّ

**“Na itakayemteremkia adhabu ya kudumu.”**

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَمْرُنَا وَفَارَ التَّنُورُ قُلْنَا احْمِلْ فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ وَأَهْلَكَ إِلَّا مَنْ

سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ وَمَنْ ءَامَنَ وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ

**40. Hata ilipokuja Amri Yetu, na tanuri ikafoka maji, tulisema: Pakia humo wawili wawili, dume na jike, kutoka kila aina, na ahali wake, isipokuwa wale ambao imekwisha wapitia hukumu; na watu walioamini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.**

**Mwanzo wa Tufani, na Nuhu عليه السلام Kuchukua katika Jahazi Kila Jinsia Wawili.**

Hii ni ahadi kutoka kwa Allah تعالى kwa Nuhu عليه السلام, itakapokuja Amri ya Allah تعالى, miongoni mwa mvua zenye kufuatana, mvua ambayo haisimami wala haikatiki bali mvua hiyo ni kama Alivyosema Allah تعالى:

فَفَتَحْنَا أَبْوَابَ السَّمَاءِ بِمَاءٍ مُّثَهَّرٍ ﴿١١﴾ وَفَجَّرْنَا الْأَرْضَ عُيُونًا فَالْتَقَى الْمَاءُ عَلَىٰ أَمْرٍ قَدْ  
 قُدِّرَ ﴿١٢﴾ وَحَمَلْنَاهُ عَلَىٰ ذَاتِ الْأَلْوَحِ وَدُسِّرَ ﴿١٣﴾ تَجْرَىٰ بِأَعْيُنِنَا جَزَاءً لِّمَن كَانَ كُفِرَ ﴿١٤﴾

***“Basi Tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika. Na Tukazipasua ardhi kwa chemchem, yakakutana maji kwa jambo lililokadiriwa. Na Tukamchukua kwenye safina ya mbao na kamba. Ikawa inakwenda kwa Nadhari Yetu, kuwa ni malipo kwa alivyokuwa amekanushwa.” (54:11-14)***

Ama Kauli Yake Allah تعالى:

وَفَارَ التَّنُورُ

***“Na ardhi ikajaa maji”***

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: *At` tanuur* ni uso wa ardhi<sup>1</sup>, Maana yake: ardhi ilikuwa ni chemchemu zinazofurika, mpaka maji yakafurika kutoka katika matanuri ambayo ni mahali pa moto, maji yakawa yanafurika, na hii ndiyo kauli ya kundi kubwa la wanawazuoni waliotangulia na wanawazuoni waliokuja nyuma, basi wakati huo Allah تعالى Alimuamrisha Nuhu عليه السلام achukue pamoja naye katika jahazi lake kila jinsia mbili wawili, katika aina za viumbe wenye roho, pamesemwa na wasiokuwa hao miongoni mwa mimea miwili, kiume na kike. Imesemwa wa mwanzo kuingizwa katika wadudu ni sisimizi na wa mwisho kuingizwa katika wanyama ni punda. Iblisi akajishikamanisha na mkia wake akawa anataka kusimama basi akawa anamfanyia uzito kusimama, hali ya kuwa yeye amejishikamanisha na mkia wake. Nuhu عليه السلام akawa anamuambia: ‘Ole wako! Una nini? Ingia.’ Akitaka kusimama hawezi kusimama, akasema: ‘Ingia japokuwa Iblisi yuko pamoja nawe.’ Wakaingia katika Jahazi.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَهْلَكَ إِلَّا مَنْ سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ

**“...na ahali wake, isipokuwa wale ambao imekwishawapitia hukumu.”**

Maana yake: Wachukue katika hilo Jahazi watu wako wa nyumbani na jamaa zako isipokuwa yule ambaye imetangulia juu yake kauli ya adhabu miongoni mwao, katika wale ambao hawakumuamini Mwenyezi Mungu. Miongoni mwao alikuwa ni mtoto wake Yam, ambaye alijitenga peke yake, na mke wa Nuhu alikuwa kafiri, alimkufuru Allah تعالى na Mtume Wake.

Na Kauli Yake Allah تعالى :

وَمَنْ ءَامَنَ

**“...na watu walio amini...”** Maana yake: jamaa zako.

وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ

**“Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.”**

Maana yake: Watu wachache tu, pamoja na urefu wa muda na kukaa baina yao miaka elfu moja isipokuwa miaka hamsini. Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, walikuwa ni watu themanini pamoja na wake zao<sup>1</sup>.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Tabari 15/326.

\* وَقَالَ ارْكَبُوا فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ جَرَّهَا وَمُرْسَنَهَا ۗ إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٤١﴾ وَهِيَ تَجْرِي بِهِمْ فِي مَوْجٍ كَالْجِبَالِ وَنَادَى نُوحٌ ابْنَهُ وَكَانَ فِي مَعْرِلٍ يَبْنَىٰ أَرْكَبَ مَعَنَا وَلَا تَكُن مَعَ الْكَافِرِينَ ﴿٤٢﴾ قَالَ سَفَاوَىٰ إِلَىٰ جَبَلٍ يَعْصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ ۗ قَالَ لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَنْ رَجِمَ ۗ وَحَالٌ بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِينَ ﴿٤٣﴾ وَقِيلَ يَا أَرْضُ ابْلَعِي مَاءَكِ وَيَسْمَاءِ أَقْلِي وَغِيضَ الْمَاءِ وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَاسْتَوَتْ عَلَىٰ الْجُودِيِّ ۖ وَقِيلَ بُعْدًا لِلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾ وَنَادَىٰ نُوحٌ رَبَّهُ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ ابْنِي مِنْ أَهْلِي وَإِنَّ وَعْدَكَ الْحَقُّ وَأَنْتَ أَحْكَمُ الْحَاكِمِينَ ﴿٤٥﴾ قَالَ يَبْنَوحُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ ۖ إِنَّهُ عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ ۖ فَلَا تَسْطَلْنِ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۖ إِنِّي أَعْظَمُكَ أَنْ تَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٤٦﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ أَنْ أَسْأَلَكَ مَا لَيْسَ لِي بِهِ عِلْمٌ ۖ وَإِلَّا تَغْفِرْ لِي وَتَرْحَمْنِي أَكُن مِّنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٤٧﴾ قِيلَ يَبْنَوحُ أَهْبِطْ بِسَلْمٍ مِنَّا وَبَرَكَتٍ عَلَيْكَ وَعَلَىٰ أُمَمٍ مِّمَّنْ مَعَكَ ۗ وَأْمُرْ سُنْمِتُهُمْ ۖ ثُمَّ يَمْسُهُمْ مِثْنَا عَذَابُ الْيَوْمِ ﴿٤٨﴾ تِلْكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهَا إِلَيْكَ ۖ مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَا أَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ مِنْ قَبْلِ هَذَا ۖ فَاصْبِرْ ۖ إِنَّ الْعَقِيبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٩﴾

\* وَقَالَ ارْكَبُوا فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ جَرَّهَا وَمُرْسَنَهَا ۗ إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٤١﴾ وَهِيَ تَجْرِي بِهِمْ فِي مَوْجٍ كَالْجِبَالِ وَنَادَىٰ نُوحٌ ابْنَهُ وَكَانَ فِي مَعْرِلٍ يَبْنَىٰ أَرْكَبَ مَعَنَا وَلَا تَكُن مَعَ الْكَافِرِينَ ﴿٤٢﴾ قَالَ سَفَاوَىٰ إِلَىٰ جَبَلٍ يَعْصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ ۗ قَالَ لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَنْ رَجِمَ ۗ وَحَالٌ بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِينَ ﴿٤٣﴾

**41. Na akasema: Pandeni humo kwa Bismillahi, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kwenda kwake na kusi-mama kwake. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.**

**42. Ikawa inakwenda nao katika mawimbi kama milima. Na Nuhu akamuita mwanawe naye alikuwa mbali: Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi, wala usiwe pamoja na makafiri.**

**43. Akasema: Nitakimbilia mlimani unilinde na maji. (Nuhu) akasema: Leo hapana wa kulindwa na Amri ya Mwenyezi Mungu ila aliyemrehemu Mwenyewe. Na wimbi likawatenganisha, akawa katika waliozama.**

**Kupanda katika Jahazi na Kusafiri katika Mawimbi Makubwa Yenye Kutisha**

Allah تعالی Anasema: akielezea kuhusu Mtume Nuhu عليه السلام kwamba yeye aliwaambia wale ambao aliamrisha kuwachukua katika Jahazi pamoja naye,

أَرْكَبُوا فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ حَجَّيْنَهَا وَمُرْسِنَهَا

**“Pandeni humo kwa Bismillahi, Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, kwenda kwake na kusimama kwake.”**

Maana yake: Kwa Jina la Allah تعالی kutakuwa kupita kwake juu ya uso wa maji, na kwa Jina la Allah تعالی utakuwa ukomo wa kwenda kwake, nako ni kule kufunga nanga kwake. Abu Rajaail-Utwaaridy amesoma:

(بِسْمِ اللَّهِ مُجْرِيهَا وَمُرْسِيهَا)

**‘Bismillah Mujrihaa wa Mursiihaa.’<sup>1</sup>**

Na Allah تعالی Amesema:

فَإِذَا أَسْتَوَيْتَ أُنْتِ وَمَنْ مَعَكَ عَلَى الْفُلِّ فَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي نَجَّيْنَا مِنَ الْقَوْمِ

الظَّالِمِينَ ﴿٢٨﴾ وَقُلْ رَبِّ أَنْزِلْنِي مُنْزَلًا مُبَارَكًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ ﴿٢٩﴾

**“Basi utakapotulia wewe na walio pamoja nawe humo marikebuni, sema: Alhamdulillah Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, Aliyetuokoa na watu madhaalimu! Na sema: Mola wangu Mlezi! Niteremshe mteremsho wenye baraka, na Wewe ni Mbora wa wateremshaji.” (23:28-29)**

Na kwa sababu hii inasuniwa kusema: *Bismillahi* katika kuyaanza mambo, wakati wa kupanda juu ya Jahazi na mnyama, kama Alivyosema Allah تعالی:

<sup>1</sup> Tabari 15/328.

وَالَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلْكِ وَالْأَنْعَامِ مَا تَرْكَبُونَ ﴿١٢﴾ لِيَسْتَوُوا عَلَىٰ ظُهُورِهِمْ

**“Na Ambaye Ndiye Aliyeumba katika kila kitu jike na dume, na Akakufanyieni marikebu na wanyama mnaowapanda. Ili mkae vizuri migongoni mwao...” (43:12-13)**

Imekuja sunnah katika kuhimiza hilo, kama itakavyokuja katika Surat Zukhruf, Inshaa Allah.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ نَبِيَّ لَعَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٣﴾

**“Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”**

Yanasibihiana wakati wa kutaja Kuteswa kwa makafiri, kwa Kuwazamisha wote, ametaja kwamba Yeye ni Msamehevu mno, Mwingi wa Huruma, kama vile Kauli Yake Allah تعالى:

إِنَّ رَبَّكَ لَسَرِيعُ الْعِقَابِ ۖ وَإِنَّهُ لَعَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٤﴾

**“...Hakika Mola wako Mlezi ni Mwepesi wa Kuadhibu, na bila ya shaka ni Mwenye Maghfira, na Mwenye Kurehemu.” (7:167)**

Na Akasema:

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِّلنَّاسِ عَلَىٰ ظُلْمِهِمْ ۗ وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٥﴾

**“...Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa Kuadhibu.” (13:6)**

Na Aya nyingine zisizokuwa hizo ambazo Analinganisha ndani yake baina ya Rehma na Adhabu Yake. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَهِيَ تَجْرِي بِهِمْ فِي مَوْجٍ كَالْجِبَالِ

**“...Ikawa inakwenda nao katika mawimbi kama milima...”**

Maana yake: Jahazi linalokwenda nao juu ya uso wa maji, maji ambayo yamefunika ardhi yote mpaka likaelea juu ya vilele vya majabali, likapanda juu yake kwa kiasi cha dhiraa kumi na tano. Imesemwa: Maili themanini, na Jahazi hili linapita juu ya uso wa maji likiwa linakwenda kwa Amri ya Allah تعالیٰ, chini ya Kivuli Chake, Msaada Wake, Ulinzi na Neema Zake, kama Alivyosema Allah تعالیٰ:

إِنَّا لَمَّا طَغَا الْمَاءُ حَمَلْنَاكُمْ فِي الْجَارِيَةِ ﴿٤١﴾ لِنَجْعَلَهَا لَكُمْ تَذْكِرَةً وَتَعِبْنَا أُنْفُسَنَا وَعِيسَىٰ ﴿٤٢﴾

***“Maji yalipofurika Sisi Tulikupandisheni katika safina. Ili Tuyafanye hayo kuwa ni waadhi kwenu na kila sikio linalosikia liyahifadhi.”***  
(69:11-12) Na Allah تعالیٰ Akasema tena:

وَحَمَلْنَاهُ عَلَىٰ ذَاتِ الْأَوْحِ وَدُسِّرِ ﴿٤٣﴾ تَجْرَىٰ بِأَعْيُنِنَا جَزَاءً لِّمَن كَانَ كُفْرًا ﴿٤٤﴾ وَقَدْ تَرَكْنَاهَا آيَةً فَهَلْ مِن مَّدَكِرٍ ﴿٤٥﴾

***“Na Tukamchukua kwenye safina ya mbao na kamba. Ikawa inakwenda kwa Nadhari Yetu, kuwa ni malipo kwa alivyokuwa amekanushwa. Na bila ya shaka Tuliacha iwe ni Ishara. Lakini je, yupo anayekumbuka?”*** (54:13-15)

**Kisa cha Kuzamishwa Mtoto wa Nuhu عليه السلام Aliyekuwa Kafiri**

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَنَادَىٰ نُوحٌ أَبْنَاهُ

***“Na Nuhu akamuita mwanawe naye alikuwa mbali.”***

Huyu ndiye mtoto wa nne na jina lake ni Yam alikuwa kafiri, Baba yake alimuita wakati wa kupanda jahazi, ili aamini na apande pamoja na wao, na asizame mfano wanavyozama makafiri:

قَالَ سَاوِيَ إِلَىٰ جِبَلٍ يَّعَصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ

***“Akasema: Nitakimbilia mlimani unilinde na maji.”***

Aliamini kutokana na ujinga wake kwamba tufani haitafika katika vilele vya majabali na kwamba, yeye lau anajishikamanisha na kilele cha jabali hilo lingemuokoa na kuzama. Baba yake, Nuhu عليه السلام, akamuambia:

لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَنْ رَحِمَ<sup>٤</sup>

**“...Leo hapana wa kulindwa na Amri ya Mwenyezi Mungu ila aliyemrehemu mwenyewe...”**

Kwa maana: Leo hakuna kitu kitakachosalimika kutokana na Amri ya Allah تعالى:

وَحَالَ بَيْنَهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ الْمُغْرَقِينَ ﴿٥٠﴾

**“...Na wimbi likawatenganisha, akawa katika waliozama.”**

وَقِيلَ يَا أَرْضُ ابْلَعِي مَاءَكِ وَيَسْمَأِ أَقْلِي وَغِيضَ الْمَاءِ وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَاسْتَوَتْ عَلَى

الْجُودِيِّ<sup>٥١</sup> وَقِيلَ بَعْدًا لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٥١﴾

**44. Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako. Na Ewe mbingu! Jizuie. Basi maji yakadidimia chini, na Amri ikapitishwa, na (jahazi) likasimama juu ya (mlima) wa Al Juudiy. Na ikasemwa: Wapotelee mbali watu waliodhulumu!**

### Mwisho wa Tufani

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye Aliwazamisha watu wote wa ardhi isipokuwa watu wa Jahazi, Aliamrisha ardhi kumeza maji yake, ambayo yalichembuka kutoka humo, yakakusanyika juu yake, Akaiamrisha mbingu kujizuia kuteremsha maji,

وَغِيضَ الْمَاءِ

**“Basi maji yakadidimia chini...”**

Maana yake: Yakaanza kupungua.

وَقُضِيَ الْأَمْرُ

**“Na Amri ikapitishwa...”,** Maana yake: Watu wote wa ardhi wakamalizwa miongoni mwa wale ambao walikuwa wamemkufuru Allah تعالى, na hakubakia katika wao mtu yeyote.

وَاسْتَوَتْ

**“...na (jahazi) likasimama...”** Jahazi na wale waliokuwa ndani yake.



عَلَىٰ الْجُودِيِّ ط

*“likasimama juu ya (mlima) wa Al Juudiy...”*

Mujahid amesema: hilo ni jabali lililokuwa katika kisiwa, siku hiyo majabali yalishindana kwa urefu kuepuka kuzama, na yakarefuka sana, jabali hilo likanyenyekea kwa Allah تعالى Mwenye Kushinda, Mwenye Utukufu, kwa hiyo halikuzama. Jahazi la Nuhu عليه السلام<sup>1</sup> likafunga nanga juu yake. Qatada amesema: Lilikaa juu yake kwa Mwezi mmoja mpaka waliposhuka humo. Qatadah amesema: Kwa hakika Allah تعالى Alilibakisha jahazi la Nuhu عليه السلام juu ya jabali, katika ardhi ya kisiwa, ili liwe ni mazingatio na alama,<sup>2</sup> mpaka watu wa mwanzo wa ummah huu walilionga, kwani ni majahazi mangapi yaliyokuwepo baada yake ambayo yaliangamia yakawa chakavu?

Na Kauli Yake:

وَقِيلَ بَعْدًا لِلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٤﴾

*“Wapotelee mbali watu waliodhulumu!”*

Maana yake: Kuangamia na kuhasirika ni kwao, na kuwa mbali na rehma ya Allah تعالى kwani wao waliangamia mpaka wa mwisho wao, hakubaki katika wao mtu yoyote.

وَنَادَىٰ نُوحٌ رَبَّهُ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ أَبِي مِنِّي وَأَهْلِي مِنِّي وَأَنَا أَحْكَمُ الْحَاكِمِينَ  
 ﴿٤٤﴾ قَالَ يَبْنَوحُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنِّي أَهْلِكَ إِنَّهُ عَمَلٌ غَيْرُ صَالِحٍ فَلَا تَسْأَلْنِي مَا لَيْسَ لَكَ  
 بِهِ عِلْمٌ إِنِّي أَعْطَيْتُكَ أَنْ تَكُونَ مِنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٤٥﴾ قَالَ رَبِّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ  
 مَا لَيْسَ لِي بِهِ عِلْمٌ وَإِلَّا تَغْفِرْ لِي وَتَرْحَمْنِي أَكُن مِّنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٤٦﴾

**45. Na Nuhu alimuomba Mola wake Mlezi: Ee Mola Mlezi wangu!  
 Hakika mwanangu ni katika ahali wangu, na hakika ahadi Yako ni  
 haki. Na Wewe ni Mwenye haki kuliko mahakimu wote.**

<sup>1</sup> Tabari 15/337.

<sup>2</sup> Tabari 15/338.

**46. Akasema: Ewe Nuhu! Huyu si katika ahali wako. Mwendo wake si mwema. Basi usiniombe jambo usio na ujuzi nalo. Mimi Nakuwaidhi usije ukawa miongoni mwa wajinga.**

**47. Nuhu akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi najikinga Kwako nisikuombe nisio na ujuzi nalo. Na kama Hunisamehe na Ukanirehemu, nitakuwa katika walio khasiri.**

**Kurejea Kwenye Kisa cha Mtoto wa Nuhu عليه السلام na Kutaja Yaliyojiri Kati ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Nuhu عليه السلام Kuhusu Mtoto Wake**

Haya ni maulizo ya kutaka kuelewa na kufunuliwa kutoka kwa Nuhu عليه السلام kuhusu hali ya mtoto wake ambaye alizama,

فَقَالَ رَبِّ إِنِّي مِنَ أَهْلِ

**“Ee Mola Mlezi wangu! Hakika mwanangu ni katika ahali wangu...”**

Maana yake: Kwa hakika uliniahidi kuwaokoa watu wangu, na ahadi Yako ni ya kweli ambayo haikhalifu, vipi basi amezama na hali ya kuwa wewe ni Hakimu wa mahakimu wote?

قَالَ يَنْبُوحُ إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ

**“Akasema: Ewe Nuhu! Huyu si katika ahali wako.”** Maana yake: Si katika wale ambao Nilikuahidi kuwaokoa, kwa sababu Mimi Nilikuahidi kuokoka wale ambao wameamini katika watu wako. Na kwa sababu hiyo Amesema,

وَأَهْلِكَ إِلَّا مَنْ سَقَّ عَلَيْهِ الْقَوْلُ مِنْهُمْ

**“...Na watu wako wa nyumbani isipokuwa yule ambaye imetangulia juu yake kauli ya adhabu katika wao.” (11:40)**

Kwa hiyo mtoto huyu akawa ni katika wale ambao tamko lilitangulia juu yake, juu ya kuzama, kwa sababu ya ukafiri wake na kumpinga kwake Baba yake, ambaye ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Nuhu عليه السلام. Na Kauli Yake:

إِنَّهُ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ

**“Huyu si katika ahali zako.”**

Maana yake: Sio katika wale ambao Nimekuahidi kuokoka kwao. Na Abdurrazaq amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: Huyu ni mtoto wake, isipokuwa yeye alimpinga katika kutenda na kuazimia. Ikrima: amesema: Katika baadhi ya usomaji wa aya hii ni,

(إِنَّهُ عَمِلَ عَمَلًا غَيْرَ صَالِحٍ)

(Hakika yeye amefanya amali isiyokuwa njema)

Na hiana inaweza ikawa kwa namna nyingine. Na hakika imekuja katika Hadithi kwamba: “Mtume ﷺ amesoma hivyo: Na Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Asma binti Yazid رضي الله عنها amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ anasoma:

(إِنَّهُ عَمِلَ غَيْرَ صَالِحٍ)

(Kwa Hakika yeye ametenda yasiyokuwa mema)<sup>1</sup>.

قِيلَ يَنْبُوحُ أَهْبِطْ بِسَلَامٍ مِنَّا وَبَرَكَاتٍ عَلَيْكَ وَعَلَىٰ أُمَمٍ مِّمَّنْ مَعَكَ وَأُمَّمٌ سَنُنْتَعِبُهُمْ ثُمَّ

يَمْسُهُمْ مِنَّا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٤٨﴾

**48. Ikasemwa: Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo Kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja nawe. Na zitakuwapo kaumu Tutakazozistarehesha, na kisha zitashikwa na adhabu chungu itokayo Kwetu.**

### Kuamrisha Kushuka katika Jahazi kwa Amani na Baraka

Allah تعالى Anatoa maelezo kuhusu yale ambayo Nuhu عليه السلام aliambiwa wakati lilipofunga nanga jahazi, juu ya jabali la Juudy, katika kumsalimia yeye na wale waliokuwa pamoja naye, miongoni mwa waumini na juu ya kila muumini katika kizazi chake mpaka siku ya Kiyama.<sup>2</sup> Kama alivyosema Muhammad Bin Ka'ab: Ameingia katika salamu hii kila muumini mwanamume, na muumini mwanamke, mpaka siku ya Kiyama. Na vilevile ameingia katika adhabu na kustareheshwa kwa muda mfupi – kila kafiri mwanamume na kafiri mwanamke mpaka siku ya Kiyama. Na Muhammad Bin Is'haq amesema: Allah

<sup>1</sup> Tabari 15/343.

<sup>2</sup> Tabari 15/303.

تعالى Alipotaka kuzuia tufani Aliupeleka upepo juu ya uso wa ardhi, maji yakatulia na chemchem za ardhi zikaziba na milango ya mbingu (ikafungika). Allah تعالى Anasema.

وَقِيلَ يَا أَرْضُ ابْلَيْ مَاءَكَ

**“Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako.” (11:44)**

Maji yakawa yanapungua na yanazama, na jahazi likawa limelingana juu ya jabali la Juudy - katika madai ya watu wa Taurati - ni kwamba ilitokea katika mwezi wa saba: ndani ya siku kumi na saba zilizopita katika mwezi huo, na katika siku ya kwanza katika mwezi wa kumi vilele vya jabali vilionekana, na zilipopita baada ya hapo siku arobaini Nuhu عليه السلام alifungua dirisha la jahazi ambalo alipanda ndani yake, kisha alimtuma kunguru ili aone maji yamefanya nini, hakurejea, akamtuma njiwa manga, akarejea kwake, hapakuwa na nafasi kwa ajili ya kuweka miguu yake, (Nuhu) akamnyooshea njiwa mkono akamchukua akamwingiza, (ndani ya jahazi). Kisha zikapita siku saba, kisha akamtuma akamtazamie, akarejea wakati wa jioni na hali ya kuwa mdomoni mwake ana majani ya Zaituni, Nuhu عليه السلام akajua kwamba maji yamepungua juu ya uso wa ardhi. Kisha akakaa kwa muda wa siku saba, kisha akamtuma, hakurejea, Nuhu عليه السلام akajua kwamba ardhi imetokeza, na ulipotimia mwaka, tangu wakati Allah تعالى Alipopeleka tufani na wakati Nuhu عليه السلام alipomtuma njiwa manga, ikaingia siku moja katika mwezi wa kwanza katika mwaka wa pili uso wa ardhi ulidhihirika, na nchi kavu ikadhihirika pia, Nuhu عليه السلام akafunua kifunuko cha jahazi, ndani ya mwezi wa pili katika mwaka wa pili, katika siku ya ishirini na sita katika mwezi huo,

قِيلَ يَنْوُوحُ أَهْبِطْ بِسَلْمٍ مِّنَّا

**“Ikasemwa: Ewe Nuhu! Shuka kwa salama itokayo Kwetu.”**

تِلْكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهَا إِلَيْكَ ۗ مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَا أَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ مِنْ قَبْلِ هَذَا ۗ

فَأَصْبِرْ ۗ إِنَّ الْعَاقِبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿٤٥﴾

**49. Hizi ni katika khabari za ghaibu Tunazokufunulia. Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii. Basi subiri! Hakika Mwisho ni wa wachamungu.**

## Kuhadithia Visa vya Ghaibu, ni Dalili Juu ya Wahyi wa Allah تعالى kwa Mtume ﷺ

Allah تعالى Anamuambia Mtume wake ﷺ, Kisa hiki na mithili yake kuwa ni:

مِنَ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ

**“...ni katika khabari za ghaibu...”**

Kwa maana, ni katika khabari za mambo yaliyojificha zilizotangulia Tunazileta kwako kwa wahyi, juu ya njia Yake kana kwamba wewe unazona kwa macho,

نُوحِيهَا إِلَيْكَ

**“...Tunazokufunulia...”**

Maana yake: Tunakufundisha kupitia wahyi kutoka Kwetu kuja kwako.

مَا كُنْتَ تَعْلَمُهَا أَنْتَ وَلَا قَوْمُكَ مِنْ قَبْلِ هَذَا

**“...Hukuwa ukizijua wewe, wala watu wako, kabla ya hii...”**

Maana yake: Haikuwa kwako wala kwa yeyote katika watu wako ujuzi wake, mpaka aseme yule ambaye anakupinga kwamba wewe umejifundisha kwake. Bali amekupa wewe khabari Allah تعالى kulingana na usahihi wa jambo lenyewe, kama vinavyolishuhudia hilo vitabu vya Mitume waliokuwa kabla yako. Kwa hiyo subiri juu ya ukadhibishaji wa yule ambaye anakupinga katika watu wako, na maudhi yao kwako, kwani hakika Sisi Tutakunusuru na Tutakuinga kwa msaada Wetu, na Tutaufanya mwisho mwema ni wako na wafuasi wako, duniani na akhera. Kama Tulivyofanya kwa Mitume – namna Tulivyowanusuru juu ya adui zao,

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا

**“Kwa hakika Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na wale ambao wameamini.” (40:51)**

Allah تعالى Amesema:

---

<sup>1</sup> Tabari 15/338

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَلِمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧١﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿١٧٢﴾

***“Na bila ya shaka Neno Letu lilikwishatangulia kwa waja Wetu waliotumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa.”***  
**(37:171-172)**

Allah تعالیٰ Amesema:

فَاصْبِرْ إِنَّ الْعَاقِبَةَ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٧٣﴾

***“Na subiri hakika mwisho ni kwa ajili ya wacha Mungu.”***

\* \* \*

وَالِى عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۚ قَالَ يَنْفِقُونَ أَنْعَبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِّنْ إِلَهِ غَيْرُهُ ۗ إِنَّ أَنْتُمْ إِلَّا مُفْتَرُونَ ﴿٥٠﴾ يَنْفِقُونَ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۗ إِنَّ أَجْرِي إِلَّا عَلَى الَّذِي فَطَرَنِي ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥١﴾ وَيَنْفِقُونَ آسْتَفْعِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تَوْنُوا إِلَيْهِ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا وَيَزِدْكُمْ قُوَّةً إِلَى قُوَّتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا مُجْرِمِينَ ﴿٥٢﴾ قَالُوا يَهُودُ مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِي آلِهَتِنَا عَنْ قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٥٣﴾ إِنْ نَقُولُ إِلَّا اعْرَابًا مِّمَّا بَعْضُ آلِهَتِنَا يُسْوِئُهُ ۗ قَالَ إِنِّي أَشْهَدُ أَنَّ اللَّهَ وَآسَهِدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾ مِنْ دُونِهِ ۗ فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونَ ﴿٥٥﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ ۗ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا ۗ إِنَّ رَبِّي عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

وَالِى عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۚ قَالَ يَنْفِقُونَ أَنْعَبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِّنْ إِلَهِ غَيْرُهُ ۗ إِنَّ أَنْتُمْ إِلَّا مُفْتَرُونَ ﴿٥٠﴾ يَنْفِقُونَ لَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۗ إِنَّ أَجْرِي إِلَّا عَلَى الَّذِي فَطَرَنِي ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥١﴾ وَيَنْفِقُونَ آسْتَفْعِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تَوْنُوا إِلَيْهِ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا وَيَزِدْكُمْ قُوَّةً إِلَى قُوَّتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا مُجْرِمِينَ ﴿٥٢﴾

50. Na kwa kina A'adi Tulimtuma ndugu yao Hud. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu! Nyinyi hamna

*mungu isipokuwa Yeye. Nyinyi si chochote ila ni wazushi tu.*

51. Enyi watu wangu! Sikuombeni ujira kwa ajili ya haya. Haukuwa ujira wangu ila kwa Yule Aliyeniumba. Basi hamtumii akili?

52. Na enyi watu wangu! Muombeni msamaha Mola wenu Mlezi, kisha mtubie kwake. Atakuleteeni mbingu zenye kunyesha mvua ya kumiminika, na Atakuzidishieni nguvu juu ya nguvu zenu. Wala msigeuke mkawa wakosefu.

### Kisa cha Hud عليه السلام na Jamaa Zake 'Aad

Allah تعالى Anasema:



**"Na."** Hakika bila ya shaka Tulimtuma.

وَأِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا

**"Kwa kina A'adi Tulimtuma ndugu yao Hud."**

Hud عليه السلام alikuja kwao hali ya kuwaamrisha wao kumuabudu Allah عزوجل hali ya kuwa Yu Peke Yake, Hana mshirika, na kuwakataza kuabudu masanamu ambayo wameyazusha na wakayaundia majina ya miungu. Akawaeleza kwamba yeye hataki malipo yoyote kwao juu ya nasaha hizo na kufikisha kwake huko kutoka kwa Allah تعالى, yeye anataka thawabu yake kutoka kwa Allah تعالى ambaye Amemuumba.

أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥٠﴾

**"Basi hamtumii akili?"**

Mkamjua yule ambaye huwalingania kwenye jambo ambalo lina maslahi kwenu duniani na akhera bila malipo yoyote. Kisha aliwaamrisha kutaka msamaha ambako ndani yake kuna kusamehewa madhambi yaliyotangulia, na kwa kutubia kutokana na yale ambayo yanakuja, na mwenye kusifika na sifa hii, Allah تعالى Atamrahisishia riziki yake na Atayafanya mambo yake kuwa mepesi, na Atamhifadhia mambo yake, na kwa ajili hiyo Amesema:

يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُمْ مِدْرَارًا

**"Atakuleteeni mbingu zenye kunyesha mvua ya kumiminika."**

قَالُوا يَا هُودُ مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِي آلِهَتِنَا عَنْ قَوْلِكَ وَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٥١﴾ إِنْ نَقُولُ إِلَّا اعْتَرَاكَ بَعْضُ آلِهَتِنَا بِسُوءٍ ۗ قَالَ إِنِّي أُشْهِدُ اللَّهَ وَآسَئِدُ وَآتِي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٢﴾ مِنْ دُونِهِ ۗ فَكِيدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونَ ﴿٥٣﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ ۚ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِئَصْوَتِهَا ۚ إِنَّ رَبِّي عَلَىٰ صِرَاطٍ

مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٤﴾



**53. Wakasema: Ewe Hud! Hujatuletea dalili za wazi. Wala sisi hatuiachi miungu yetu kwa kufuata kauli yako. Na wala sisi hatukuamini wewe.**

**54. Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa. Akasema: Hakika mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnao wafanya washirika,**

**55. Mkamuacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula!**

**56. Hakika mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye Anamuendesha Atakavyo. Hakika Mola wangu Mlezi yuko juu ya Njia Iliyonyooka.**

**Mjadala Kati ya 'Aad na Hud عليه السلام.**

Allah عزوجل Anaeleza kuwa wao walimuambia Mtume wao,

مَا جِئْتَنَا بِبَيِّنَةٍ

**“Hujatuletea dalili za wazi.”**

Maana yake: Hoja na ushahidi juu ya yale ambayo unayadai,

وَمَا نَحْنُ بِتَارِكِي آلِهَتِنَا عَنْ قَوْلِكَ

**“Wala sisi hatuiachi miungu yetu kwa kufuata kauli yako.”**

Maana yake: Kwa kule tu kusema kwako: Waacheni, tuwaache?

وَمَا نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ

**“Na wala sisi hatukuamini wewe.”** wenye kukusadiki.

إِنْ نَقُولُ إِلَّا أَعْرَضْنَا عَنْ قَوْلِكَ بِسُوءٍ

**“Sisi tunasema: Baadhi katika miungu yetu imekusibu kwa baa.”**

Wanasema: Hatudhani isipokuwa baadhi ya waungu wetu wamekusibu kwa wazimu na kuharibikiwa akili kwa sababu ya kutukataza kwako kuwaabudu, na kuwatia kwako aibu.

قَالَ إِنِّي أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٥﴾ مِنْ دُونِهِ ط

**“...Akasema: Hakika mimi namshuhudisha Mwenyezi Mungu, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnaowafanya washirika” Mukamuacha Yeye...” (11:54-55)**

Anasema: Mimi nimeepukana na washirika wote na masanamu,

فَكَيْدُونِي جَمِيعًا

**“Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi,...”**Maana yake: nyinyi na waungu wenu, wakiwa waungu hao ni wa kweli.

ثُمَّ لَا تَنْظُرُونَ ﴿٥٦﴾

**“...na kisha msinipe muhula.”** Maana yake: kufumba na kufumbua. Na Kauli Yake:

إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ ۚ مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا

**“Hakika mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye Anamuendesha Atakavyo.”**

Maana yake: Kila kiumbe kipo chini ya Allah تعالى katika Kutenza nguvu Kwake, na Utawala Wake, na Yeye ni Hakimu Muadilifu, Ambaye Hafanyi dhulma katika Hukumu Yake, hakika Yeye Yuko juu ya njia iliyo nyooka.

Kwa hakika msimamo huu ni hoja nzito, na dalili ya nguvu juu ya ukweli aliokuja nao, na kubatilika yale ambayo wao wako juu yake katika kuabudu masanamu, ambayo hayanufaishi wala hayadhuru. Bali haya masanamu ni vitu visivyokuwa na uhai ambavyo havisikii wala havioni, havinusuru wala havifanyi uadui, hakika anayestahiki kutakasiwa ibada ni Allah تعالى Peke Yake Hana mshirika, ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme na Kufanya Atakalo, na hapana kitu chochote isipokuwa kiko chini ya Ufalme Wake, Kutenza Nguvu Kwake na Utawala Wake, kwa hiyo hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye na hapana Bwana asiyekuwa Yeye.

فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ إِلَيْكُمْ<sup>٥٧</sup> وَتَسْتَخْلِفُ رَبِّي قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّونَهُ شَيْئًا<sup>٥٨</sup> إِنَّ رَبِّي عَلَى كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ<sup>٥٩</sup> وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا هُودًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَنَجَّيْنَاهُمْ مِّنْ عَذَابٍ غَلِيظٍ<sup>٦٠</sup> وَتِلْكَ ءَادٌ جَحَدُوا بِبَايَتِ رَبِّهِمْ وَعَصَوْا رُسُلَهُمْ وَاتَّبَعُوا أَمْرَ كُلِّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ<sup>٦١</sup> وَأَتَّبَعُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةَ وَيَوْمِ أَلْقَيْنَاهُمْ<sup>٦٢</sup> آلَا إِنَّ ءَادًا كَفَرُوا رَبَّهُمْ<sup>٦٣</sup> آلَا بُعْدًا لِّعَادٍ قَوْمِ هُودٍ<sup>٦٤</sup> \* وَإِلَى ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًا<sup>٦٥</sup> قَالَ يَاقَوْمِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنِّ إِلَهِ غَيْرُهُ<sup>٦٦</sup> هُوَ أَنشَأَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا فَاسْتَغْفِرُوهُ ثُمَّ تَوْبُوا إِلَيْهِ<sup>٦٧</sup> إِنَّ رَبِّي قَرِيبٌ مُّجِيبٌ<sup>٦٨</sup> قَالُوا يَصْلِحْ قَدْ كُنْتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَذَا<sup>٦٩</sup> أَتَنْهِنَا أَنْ نَعْبُدَ مَا يَعْبُدُ آبَاؤُنَا وَإِنَّا لَفِي شَكِّ مِمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ<sup>٧٠</sup> مُرِيبٌ<sup>٧١</sup> قَالَ يَاقَوْمِ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَءَاتَانِي مِنْهُ رَحْمَةً فَمَنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُ<sup>٧٢</sup> فَمَا تَزِيدُونَنِي غَيْرَ تَخْسِيرٍ<sup>٧٣</sup>

فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ إِلَيْكُمْ<sup>٥٧</sup> وَتَسْتَخْلِفُ رَبِّي قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّونَهُ شَيْئًا<sup>٥٨</sup> إِنَّ رَبِّي عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ<sup>٥٩</sup> وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا هُودًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَنَجَّيْنَاهُمْ مِّنْ عَذَابٍ غَلِيظٍ<sup>٦٠</sup> وَتِلْكَ ءَادٌ جَحَدُوا بِبَايَتِ رَبِّهِمْ وَعَصَوْا رُسُلَهُمْ وَاتَّبَعُوا أَمْرَ كُلِّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ<sup>٦١</sup> وَأَتَّبَعُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةَ وَيَوْمِ أَلْقَيْنَاهُمْ<sup>٦٢</sup> آلَا إِنَّ ءَادًا كَفَرُوا رَبَّهُمْ<sup>٦٣</sup> آلَا بُعْدًا لِّعَادٍ قَوْمِ هُودٍ<sup>٦٤</sup>

57. Na ikiwa mtarudi nyuma, basi mimi nimekwisha kufikishieni niliyotumwa kwenu. Na Mola wangu Mlezi Atawaleta watu wengine badala yenu, wala nyinyi

hamumdhuru kitu Yeye. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kuhifadhi kila kitu.

58. Ilipofika Amri Yetu, Tulimuokoa Hud na walioamini pamoja naye, kwa rehema itokayo Kwetu. Na Tukawaokoa na adhabu ngumu.

59. Na hao ndio kina A'adi. Walizikanusha Ishara za Mola wao Mlezi, na wakawaasi Mitume wake, na wakafuata amri ya kila jabari mwenye inda.

**60. Na wakafuatishiwa laana katika dunia hii na Siku ya Kiyama. Basi tambueni mtanabahi! Hakika kina A'adi walimkufuru Mola wao Mlezi. Na tambueni mtanabahi kuwa hakika waliangamizwa kina A'adi, kaumu ya Hud.**

Hud عليه السلام anawaambia “Na ikiwa watarudi nyuma na niliyowaletea katika kumuabudu Allah تعالى Bwana wenu hali ya kuwa Yu Peke Yake, hana mshirika, kwa hakika hoja imesimama juu yenu kwa kukufikishieni ujumbe wa Allah تعالى ambao kwa huo Amenituma.”

وَدَسْتَخْلِفُ رَبِّي قَوْمًا غَيْرَكُمْ

**“Na Mola wangu Mlezi Atawaleta watu wengine badala yenu.”**

Ambao watamuabudu Yeye hali ya kuwa Yu Peke Yake Hana mshirika na Hatawajali nyinyi, kwa hakika nyinyi hamtamdhuru kwa ukafiri wenu bali litarejea balaa la kufanya hivyo juu yenu,

إِنَّ رَبِّي عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَفِيظٌ

**“Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kuhifadhi kila kitu.”**

Maana yake: Mwenye Kushuhudia, Mwenye Kuhifadhi maneno ya waja wake na matendo yao, Atawalipa juu yake, ikiwa ni kheri Atawalipa kheri na ikiwa ni shari Atawalipa shari.

**Kuangamizwa kwa Aadi na Kuokolewa Walioamini Miongoni Mwao**

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا

**“...Ilipofika Amri Yetu...”**

Nayo ni upepo usiyokuwa na kheri yoyote, Allah تعالى Akawaangamiza wao hadi wa mwisho wao, Akamuokoa Hud عليه السلام na wafuasi wake, na adhabu nzito sana, kwa Rehma na Upole Wake Allah تعالى.

وَتِلْكَ عَادٌ جَحَدُوا بِآيَاتِنَا رَبِّهِمْ

**“Na hao ndio kina A'adi. Walizikanusha Ishara za Mola wao Mlezi.”**

Walizikufuru na wakawaasi Mitume wa Allah تعالى, na hilo ni kwa sababu mwenye kumkufuru Mtume yeyote, kwa hakika amewakufuru Mitume wote, kwa sababu hapana tofauti yeyote kati ya yoyote miongoni mwao katika wajibu wa kuwaamini mitume wote.

Kwa hiyo 'Aadi walimkufuru Hud عليه السلام, kwa hiyo, kukufuru kwao kukawekwa katika nafasi ya kuwakufuru Mitume wote

وَاتَّبِعُوا أَمْرَ كُلِّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ ﴿٦١﴾

**“...na wakafuata amri ya kila jabari mwenye inda.”**

Waliacha kumfuata Mtume wao aliye muongofo wakaifuata amri ya kila muovu mkaidi, na kwa sababu hiyo walifuatishiwa laana duniani kutoka kwa Allah تعالى na kutoka kwa waja wake waumini kila wanapotajwa, na siku ya Kiyama itanadiwa juu yao, mbele za mashahidi,

أَلَا إِنَّ عَادًا كَفَرُوا رَبَّهُمْ ۗ

**“Hakika kina A’adi walimkufuru Mola wao Mlezi.”**

﴿٦١﴾ وَإِلَى ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًا ۚ قَالَ يَا قَوْمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ هُوَ أَنْشَأَكُمْ

مِنَ الْأَرْضِ وَأَسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا فَاسْتَغْفِرُوهُ ثُمَّ تَوْبُوا إِلَيْهِ ۗ إِنَّ رَبِّي قَرِيبٌ مُجِيبٌ ﴿٦٢﴾

**61. Na kina Thamud Tuliwapelekea ndugu yao Saleh. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye. Yeye Ndiye Aliyekuumbeni katika ardhi, na Akakuwekeni humo. Basi muombeni msamaha, kisha mtubu Kwake. Hakika Mola wangu Mlezi Yupo karibu, Anaitikia maombi.**

**Kisa cha Saleh عليه السلام na Thamuud**

Allah تعالى Anasema:



“**Na.**” hakika Tulipelekea kwa,

إِلَى ثَمُودَ

“...**kina Thamud...**” Na hao ni wale ambao walikuwa wanaishi katika miji ya Hijri kati ya Tabuuk na Madinah, na walikuwa ni baada ya ‘Aad. Allah تعالى Akampeleka,

أَخَاهُمْ صَالِحًا

“...**ndugu yao Saleh...**” Kutokana nao, akawaamrisha kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, kwa sababu hiyo Amesema:

هُوَ أَنشَأَكُم مِّنَ الْأَرْضِ

“...**Yeye Ndiye Aliyekuumbeni katika ardhi...**”

Maana yake: Ameanza Uumbaji wenu kutoka humo katika ardhi, humo Amemuumba Baba yenu Adamu,

وَأَسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا

“...**na Akakuwekeni humo...**” Maana yake: Amekufanyeni ni waimarishaji, mnaimarisha na mnaizalisha.

فَأَسْتَغْفِرُوهُ

“...**Basi muombeni msamaha...**” kwa madhambi yenu yaliyopita,

تُؤْمِنُوا تَوْبًا إِلَيْهِ

“...**kisha mtubu Kwake.**” katika muda mnaouelekea.

إِنَّ رَبِّي قَرِيبٌ مُّجِيبٌ ﴿٥٧﴾

“**Hakika Mola wangu Mlezi Yupo karibu.**”

Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۗ

**“Na waja wangu watakapokuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi Nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba” (2:186)**

قَالُوا يَنْصَلِحُ قَدْ كُنْتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَذَا أَتَنْهَنَّا أَنْ نَعْبُدَ مَا يَعْبُدُ آبَاؤُنَا وَإِنَّا لَفِي شَكِّ مِمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٦٢﴾ قَالَ يَنْفَوِمِ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي وَءَاتَنِي مِنْهُ رَحْمَةً فَمَنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُ فَمَا تَزِيدُونِي غَيْرَ تَخْسِيرٍ ﴿٦٣﴾

**62. Wakasema: Ewe Saleh! Hakika kabla ya haya ulikuwa unatarajiwa kheri kwetu. Je, unatukataza tusiwaabudu waliyokuwa wakiwaabudu baba zetu? Na hakika sisi tuna shaka na wasiwasi kwa hayo unayotuitia.**

**63. Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa ninazo dalili zilizo wazi kutokana na Mola wangu Mlezi, Naye Akawa kanipa rehema kutoka Kwake - je, ni nani atakayeninusuru kwa Mwenyezi Mungu nikimuasi? Basi nyinyi hamtanizidishia ila khasara tu.**

**Mjadala kati ya Saleh عليه السلام na Thamuud**

Allah تعالى Anataja jinsi maneno yalivyokuwa baina ya Saleh عليه السلام na watu wake, na jinsi ujinga na inadi ilivyokuwa katika kauli yao,

قَدْ كُنْتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَذَا

**“Hakika kabla ya haya ulikuwa unatarajiwa kheri kwetu.”**

Maana yake: Tulikuwa tunatarajia akili yako kabla hujasema uliyoyasema,

أَتَنْهَنَّا أَنْ نَعْبُدَ مَا يَعْبُدُ آبَاؤُنَا

**“Unatukataza tusiwaabudu waliyokuwa wakiwaabudu baba zetu?”**

Na ambayo watangulizi wetu walikuwa juu yake?

وَإِنَّا لَفِي شَكِّ مِمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٦٢﴾

**“Na hakika sisi tuna shaka na wasiwasi kwa hayo unayotuitia.”**

Maana yake: Shaka nyingi sana,

قَالَ يَاقَوْمِ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُمْ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّي

***“Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa ninazo dalili zilizo wazi kutokana na Mola wangu Mlezi.”***

Katika kile ambacho Amenituma kwenu, juu ya yakini na dalili ,

وَأَتَانِي مِنْهُ رَحْمَةٌ فَمَنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُ

***“...Naye Akawa kanipa rehema kutoka Kwake - je, ni nani atakayeninusuru kwa Mwenyezi Mungu nikimuasi?”***

Kwa maana, ningeacha kukulinganieni kwenye ukweli na kumuabudu Allah تعالیٰ Peke Yake, lau ningeacha hivyo, msingeninufaisha,

غَيْرَ تَخْسِيرٍ ﴿٦٣﴾

***“ila khasara tu.”***

Maana yake: Madhara na maafa.

\* \* \*



وَيَقُولُ هَذِهِ نَاقَةُ اللَّهِ لَكُمْ آيَةٌ فَذَرُوهَا تَأْكُلْ فِي  
 أَرْضِ اللَّهِ وَلَا تَمْسُوهَا بِسُوءٍ فَيَأْخُذَكُمْ عَذَابٌ قَرِيبٌ ﴿٦٤﴾  
 فَعَقَرُوهَا فَقَالَ تَمَتَّعُوا فِي دَارِكُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ ۖ ذَٰلِكَ  
 وَعْدٌ غَيْرُ مَكْدُوبٍ ﴿٦٥﴾ فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا صَالِحًا  
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَمِن خِزْيِ يَوْمِئِذٍ ۗ إِنَّ  
 رَبَّكَ هُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ ﴿٦٦﴾ وَأَخَذَ الَّذِينَ ظَلَمُوا  
 الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِيَرِهِمْ جَثِيمِينَ ﴿٦٧﴾ كَأَن لَّمْ  
 يَغْتَوَّأ فِيهَا ۗ أَلَا إِنَّ ثَمُودًا كَفَرُوا رَبَّهُمْ ۗ أَلَا بُعْدًا لِثَمُودَ  
 ﴿٦٨﴾ وَلَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُنَا إِبْرَاهِيمَ بِالْبُشْرَىٰ قَالُوا سَلَامًا  
 قَالَ سَلَامٌ ۗ فَمَا لَبِثَ أَن جَاءَ بِعِجْلٍ حَنِيذٍ ﴿٦٩﴾ فَلَمَّا رَأَىٰ  
 أَيْدِيَهُمْ لَا تَصِلُ إِلَيْهِ نَكِرَهُمْ وَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً ۗ قَالُوا  
 لَا تَخَفْ إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٠﴾ وَاتْرَأْتُهُ قَابِئَةً  
 فَضَحِكْتْ فَبَشَّرْنَاهَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ  
 ﴿٧١﴾ قَالَتْ يَبْئُوتَنِي ءَأُلْدُ وَأَنَا عَجُوزٌ وَهَٰذَا بَعْلٌ شَيْخًا  
 ۗ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٧٢﴾ قَالُوا أَتَعْجَبِينَ مِنْ أَمْرِ  
 اللَّهِ ۗ رَحِمْتُ اللَّهُ وَبَرَكَتُهُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ ۗ إِنَّهُ حَمِيدٌ  
 مَّجِيدٌ ﴿٧٣﴾

وَيَقُولُ هَذِهِ نَاقَةُ اللَّهِ لَكُمْ آيَةٌ فَذَرُوهَا تَأْكُلْ فِي  
 أَرْضِ اللَّهِ وَلَا تَمْسُوهَا بِسُوءٍ فَيَأْخُذَكُمْ عَذَابٌ  
 قَرِيبٌ ﴿٦٤﴾ فَعَقَرُوهَا فَقَالَ تَمَتَّعُوا  
 فِي دَارِكُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ ۖ ذَٰلِكَ وَعْدٌ  
 غَيْرُ مَكْدُوبٍ ﴿٦٥﴾ فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا  
 نَجَّيْنَا صَالِحًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ  
 بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَمِن خِزْيِ يَوْمِئِذٍ ۗ إِنَّ  
 رَبَّكَ هُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ ﴿٦٦﴾ وَأَخَذَ  
 الَّذِينَ ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ  
 فَأَصْبَحُوا فِي دِيَرِهِمْ جَثِيمِينَ ﴿٦٧﴾  
 كَأَن لَّمْ يَغْتَوَّأ فِيهَا ۗ أَلَا إِنَّ ثَمُودًا  
 كَفَرُوا رَبَّهُمْ ۗ أَلَا بُعْدًا  
 لِثَمُودَ ﴿٦٨﴾

64. Enyi watu wangu!  
 ngamia huyu wa Mwenyezi  
 Mungu ni Ishara kwenu. Basi  
 muacheni ale katika ardhi  
 ya Mwenyezi Mungu; wala

msimguse kwa ubaya, isije ikakuangamizeni adhabu iliyo karibu.

65. Wakamchinja. Basi (Saleh) akasema: Stareheni katika mji wenu muda wa siku tatu. Hiyo ni ahadi isiyokuwa ya uwongo.

**66. Basi ilipokuja Amri Yetu Tulimuokoa Saleh na wale walioamini pamoja naye kwa Rehema Yetu kutokana na hizaya ya siku ile. Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Kushinda.**

**67. Na ukelele uliwaangamiza wale waliodhulumu, wakapambazukiwa nao ni maiti majumbani mwao.**

**68. Kama kwamba hawakuwako huko. Hebu zingatieni! Hakika kina Thamud walimkufuru Mola wao Mlezi. Hebu zingatieni! Thamud wamepotelea mbali!**

Yametangulia meneno juu ya kisa hiki kwa ukamilifu, katika Surat Al-Aaraf kuanzia aya ya 83 - 88 kwa kiwango ambacho hatuhitaji kurudia tena hapa.

Na kwa Allah تعالى tu ninataka kuwezesha. Na Allah Ndiye Apaye ushindi.

وَلَقَدْ جَاءَتْ رُسُلْنَا إِبْرَاهِيمَ بِالْبَشِيرِ قَالُوا سَلَمًا قَالِ سَلَمٌ فَمَا لَبِثَ أَنْ جَاءَ بِعِجْلٍ حَنِينٍ ﴿٦٦﴾ فَلَمَّا رَأَىٰ أَيْدِيَهُمْ لَا تَصِلُ إِلَيْهِ نَكِرَهُمْ وَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً قَالُوا لَا تَخَفْ إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمِ لُوطٍ ﴿٦٧﴾ وَأَمْرُهُمْ قَائِمَةٌ فَضَحِكْتُمْ فَبَشَّرْنَاهَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ ﴿٦٨﴾ قَالَتْ يَبْئُوتَنِي أَيْدِي وَأَنَا عَجُوزٌ وَهَذَا بَعْلِي شَيْخًا إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٦٩﴾ قَالُوا اتَّعَجِبِينَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ رَحِمْتُ اللَّهُ وَبَرَكَّتْهُ عَلَيْهِمْ أَهْلَ الْبَيْتِ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ﴿٧٠﴾

**69. Na wajumbe wetu walimjia Ibrahim kwa bishara njema, wakasema: Salama! Naye akasema: Salama! Hakukaa ila mara akaleta ndama wa kuchoma.**

**70. Basi alipoona mikono yao haimfikilii aliwatilia shaka, na akawaogopa. Wakasema: Usiogope! Hakika sisi tumetumwa kwa kaumu ya Lut'.**

**71. Na mkewe alikuwa kasimama wima, akacheka. Basi Tukambashiria (kuzaliwa) Is-haq, na baada ya Is-haq Yaaqub.**

**72. Akasema: Je, hivyo mimi nizae, na hali yangu ni kikongwe na huyu mume wangu ni kizee? Hakika haya ni mambo ya ajabu!**

**73. Wakasema: Je, unastaajabia amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye Ndiye Msifiwa wa Kutukuzwa.**

**Ujio wa Malaika kwa Ibrahim عليه السلام na Kumpa Bishara ya Kuzaliwa Is-haq عليه السلام na Ya'aqub عليه السلام .**

Anasema Allah تعالى:

وَلَقَدْ جَاءَتْ رُسُلُنَا

**“Na wajumbe Wetu walimjia...”** Neno **“wajumbe Wetu”** hapa linamaanisha Malaika.

إِبْرَاهِيمَ بِالْبَشْرَى

**“Walimjia Ibrahim kwa Bishara Njema...”**

Pamesemwa wanampa khabari njema ya kuzaliwa Is-haq عليه السلام, na pamesemwa kwa kuangamizwa watu wa Lut عليه السلام, na Kauli Yake Allah تعالى inashuhudia maana ya kwanza.

فَلَمَّا ذَهَبَ عَنْ إِبْرَاهِيمَ الرَّوْعُ وَجَاءَتْهُ الْبَشْرَى مُجْتَدِلُنَا فِي قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٣﴾

**“Basi khofu ilipomuondoka Ibrahim, na ikawa ile bishara imemfikia, alianza kujadiliana nasi juu ya kaumu ya Lut,...”(11:74)**

قَالُوا سَلَامًا قَالَ سَلَامٌ

**“Wakasema: “Salaman.” Naye akasema, “Salamun”**

Maana yake: Amani iwe juu yenu. Wanawazuoni wa fasihi wamesema kwamba: majibu ya Ibrahim عليه السلام ni mazuri zaidi kuliko maamkizi yao, kwa sababu maamkizi ya Ibrahim **“Salamun”** yanafahamisha ithibati na kudumu.

فَمَا لَبِثَ أَنْ جَاءَ بِعِجْلٍ حَنِيفٍ ﴿٧٤﴾

**“...Hakukaa ila mara akaleta ndama wa kuchoma.”**

Kwa maana Ibrahim عليه السلام alienda haraka, akawaletea wageni ndama aliyechomwa kwa kubanikwa. Hivi ndivyo alivyopokea bin Abbasi, Qatadah na wengineo رضي الله عنهم. Kama Allah تعالى Asemavyo katika aya nyingine:

فَرَاغَ إِلَىٰ أَهْلِهِ فَجَاءَ بِعَجَلٍ سَمِينٍ ﴿٦٦﴾ فَقَرَّبَهُ إِلَيْهِمْ قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٦٧﴾

**“Akenda kwa ahali wake na akaja na ndama aliyenona. Akawakaribisha, akasema: Mbona hamli?” (51:26-27)**

Aya hii imekusanya adabu na taratibu nyingi za kukirimu ugeni.

فَلَمَّا رَأَىٰ أَيْدِيَهُمْ لَا تَصِلُ إِلَيْهِ نَكِرَهُمْ

**“Basi alipoona mikono yao haimfikilii aliwatilia shaka...”**

Alitishika na wao.

وَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً

**“...aliwatilia shaka na akawaogopa.”**

Kwa sababu, Malaika hawali chakula, wala kukitamani. Hivyo aliwaona wamechukia kwa sababu ya kuletewa chakula, na wakajitenga nacho kabisa, na kwa kuzingatia hilo, Ibrahim عليه السلام akatishika na ugeni huo.

وَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً

**“...aliwatilia shaka na akawaogopa.”**

Sudiyiyy amesema: Mwenyezi Mungu تعالى Alipowapeleka Malaika kwa watu wa Lut عليه السلام, walikuja na hali ya kuwa wanakwenda katika sura za wanamume vijana, mpaka wakashukia kwa Ibrahim عليه السلام wakamuomba wawe wageni wake, alipowaona aliwatukuza,

فَرَاغَ إِلَىٰ أَهْلِهِ فَجَاءَ بِعَجَلٍ سَمِينٍ ﴿٦٦﴾

**“Akenda kwa ahali wake na akaja na ndama aliyenona.” (51:26)**

Akamchinja kisha akamchoma katika mawe yenye moto, akawaletetea, akakaa pamoja nao, alipowasogezea yule ndama, alisema: ‘Hivi hamli?’ Wakasema, ‘Ewe Ibrahim kwa hakika sisi hatuli chakula isipokuwa kwa malipo.’ Akasema, ‘chakula hiki kina malipo.’ Wakasema, ‘ni yapi malipo yake?’ Akasema: ‘Mtalitaja Jina la Allah تعالى mwanzo wake, na mtamsifu mwisho wake.’ Jibril عليه السلام akamtazama Mikail عليه السلام akasema: ‘Ni haki kwa Allah تعالى Kumfanya huyu kuwa ni mwandani wake.’

<sup>1</sup> Tabari 15/384, 385.

فَأَمَّا رءَا أَيْدِيهِمْ لَا تَصِلُ إِلَيْهِ نَكِرَهُمْ

**“Basi alipoona mikono yao haimfikilii aliwatilia shaka...”**

Anasema: alipowaona hawali alifadhaika na akawaogopa, na Sara alipoona kwamba Ibrahim عليه السلام amekwisha wakirimu na yeye akasimama kuwahudumia, alicheka, akasema: ‘Ni ajabu ya wageni wetu hawa, tunawatumikia sisi wenyewe kwa kuwakirimu wao, wao hawali chakula chetu!’

Kauli Yake Allah تعالى Anaelezea kuhusu Malaika:

قَالُوا لَا تَخَفْ

**“Wakasema: Usiogope!”**

Maana yake: Walisema: ‘usituogope *hakika sisi*, ni malaika *tumetumwa kwa kaumu ya Lut*’ ili tuwaangamize, akacheka sana kwa kufurahia kuangamizwa kwao, kutokana na wingi wa uovu wao, na ukubwa wa ukafiri wao. Kwa sababu hiyo alilipwa kwa kupewa khabari njema ya kupata mtoto baada ya kukata tamaa. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمِنْ وَّرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ ﴿١٣١﴾

**“Na baada ya Is’haq Yaaqub.”**

Maana yake: Mtoto wake, atakuwa na mtoto, wajukuu na kizazi, kwani Yaaqub alimzaa Is’haq عليه السلام, kama alivyosema katika aya ya sura ya Baqarah:

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ

إِلَهَكَ وَإِلَهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِلَهًا وَاحِدًا وَنَحْنُ لَهُد مُسْلِمُونَ ﴿١٣١﴾

**“Je! Mlikuwapo yalipomfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is-haq, Mungu Mmoja tu, na sisi tunasilimu Kwake.” (2:133)**

<sup>1</sup> Tabari 15/389.

Na kutoka hapa wametoa dalili kwa aya hii, kuwa (dhabihu), mchinjwa ni Ismail عليه السلام, na kwamba inazuilika kuwa mchinjwa ni Is'haq عليه السلام, kwa sababu huyo Is'haq عليه السلام bishara yake imekuja kwamba atakuja mzaa Yaaqub عليه السلام, sasa vipi Ibrahim عليه السلام aamrishwe kumchinja hali ya kuwa yeye ni mtoto mdogo, na hali ya kuwa Yaaqub عليه السلام ambaye amehidiwa kupatikana kupitia kwake hajazaliwa bado? Na ahadi ya Allah تعالى ni ya kweli hairudi nyuma, kwa hiyo, siyo yeye Yaaqub عليه السلام aliyeamrishwa kuchinjwa na baba yake, wakati hali ni hii, kwa hiyo imelazimika awe ni Ismail عليه السلام. Na huu ni katika uchukuaji wa dalili uliyo mzuri mno na uliyo sahihi zaidi, na uliyo wazi mno, sifa njema ni za Allah تعالى.

قَالَتْ يَوَيْلَتِي ۖ أَلِدُ وَأَنَا عَجُوزٌ وَهَذَا بَعْلِي شَيْخًا

***“Akasema: Je, hivyo mimi nizae, na hali yangu ni kikongwe na mume wangu huyu ni kizee?”***

Ameyaigiza maneno yake katika aya hii kama alivyoigiza matendo yake katika aya nyingine,

فَأَقْبَلَتِ امْرَأَتُهُ فِي صَرَوةٍ فَصَكَتْ وَجْهَهَا وَقَالَتْ عَجُوزٌ عَقِيمٌ ﴿٥٩﴾

***“Ndipo mkewe akawaelekea, na huku anasema na akijipiga usoni kwa mastaajabu, na kusema: Mimi ni kikongwe na tasa!” (51:29)***

Kama ilivyo ada ya wanawake katika maneno na matendo yao katika kustaajabu,

قَالُوا أَتَعْجَبِينَ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ

***“Wakasema: Je, unastaajabia Amri ya Mwenyezi Mungu?”***

Kwa maana: Malaika wakasema: Usistajabu katika hili, kwa kuwa Yeye Anapotaka jambo huliambia kuwa likawa, usistajabu katika hili, japokuwa ukikongwe na tasa na mumeo ni mzee sana kwani Allah تعالى kwa Analolitaka ni Muweza.

رَحِمْتُ اللَّهُ وَبَرَكَتُهُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الْبَيْتِ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَجِيدٌ ﴿٦٠﴾

***“Rehma ya Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yenu enyi watu wa nyumba – ya Ibrahim – kwa hakika Yeye ni Mwingi wa Kusifiwa Mtukufu sana.”***

Maana yake: Yeye Ndiye Mwenye Kusifiwa katika Matendo Yake na Maneno Yake yote, Ndiye Mwenye Kutukuzwa katika Sifa Zake, na kwa sababu hiyo imethibitika katika sahihi ya Bukhari na Muslim, kwamba Masahaba walisema: ‘tumejua namna ya kukusalimia, je ni namna gani kukutakia rehma?’ Akasema:

«تُؤَلُّوا: اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ  
وَأَلِ إِبْرَاهِيمَ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلَى آلِ  
إِبْرَاهِيمَ إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ»

“Semeni Ee Mola wa Haki Mrehemu Muhammad ﷺ na jamaa za Muhammad ﷺ kama Ulivyomrehemu Ibrahimu عليه السلام na jamaa za Ibrahimu عليه السلام na Mbariki Muhammad ﷺ na jamaa za Muhammad ﷺ kama Ulivyowabariki jamaa za Ibrahim عليه السلام, hakika Wewe ni Mwingi na Kusifiwa Mtukufu sana.”<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Fat’hul al- Bari 6/469, na Muslim.

فَلَمَّا ذَهَبَ عَنْ إِبْرَاهِيمَ الرَّوْعُ وَجَاءَتْهُ الْبُشْرَىٰ مُجْبَدِلُنَا فِي قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٤﴾ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَحَلِيمٌ أَوَّهٌ مُّئْتَبٍ ﴿٧٥﴾ يَتَّبِعُهُمْ فِي كِبَرِهِمْ أُعْرِضْ عَنْ هَذَا ۖ إِنَّهُ قَدْ جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَإِنَّهُمْ لَأْتِيهِمْ عَذَابٌ غَيْرُ مَرْدُودٍ ﴿٧٦﴾ وَلَمَّا جَاءَتْ رُسُلُنَا لُوطًا سِيءَ بِهِمْ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا وَقَالَ هَذَا يَوْمٌ عَصِيبٌ ﴿٧٧﴾ وَجَاءَهُ قَوْمُهُ يُرْعَعُونَ إِلَيْهِ وَمِنْ قَبْلُ كَانُوا يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ ۗ قَالَ يَاقَوْمِ هَٰؤُلَاءِ بَنَاتِي هُنَّ أَطْهَرُ لَكُمْ ۖ فَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ وَلَا تَكْفُرُوا فِي صَيْفِي ۗ أَلَيْسَ مِنْكُمْ رَجُلٌ رَّشِيدٌ ﴿٧٨﴾ قَالُوا لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا لَنَا فِي بَنَاتِكِ مِنْ حَقٍّ وَإِنَّكَ لَتَعْلَمُنَّ مَا نُرِيدُ ﴿٧٩﴾ قَالَ لَوْ أَنَّ لِي بِكُمْ قُوَّةٌ أَوْ آوَىٰ إِلَيَّ رُكْنٌ شَدِيدٌ ﴿٨٠﴾ قَالُوا يَبْلُوطُ إِنَّا رُسُلُ رَبِّكَ لَنْ يَصْلُوَا إِلَيْكَ ۖ فَأَسْرِ بِأَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِنَ اللَّيْلِ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ أَحَدٌ ۖ إِلَّا أَمْرَاتِكَ ۖ إِنَّهُ مُصِيبُهَا مَا أَصَابَهُمْ ۗ إِنَّ مَوْعِدَهُمُ الصُّبْحُ ۗ أَلَيْسَ الصُّبْحُ بِقَرِيبٍ ﴿٨١﴾ فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا جَعَلْنَا عَلَيْهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ مَّنضُودٍ ﴿٨٢﴾ مُّسَوِّمَةً عِنْدَ رَبِّكَ وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ بِبَعِيدٍ ﴿٨٣﴾ \* وَإِلَىٰ مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۗ قَالَ يَنْفَوْرِمَ آعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِن إِلَهِ غَيْرُهُ ۖ وَلَا تَنْقُصُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ ۗ إِنِّي أَرَبُّكُمْ بِحَقِّ وَائِي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ مُّحِيطٍ ﴿٨٤﴾

فَلَمَّا ذَهَبَ عَنْ إِبْرَاهِيمَ الرَّوْعُ وَجَاءَتْهُ الْبُشْرَىٰ مُجْبَدِلُنَا فِي قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٤﴾  
 إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَحَلِيمٌ أَوَّهٌ مُّئْتَبٍ ﴿٧٥﴾  
 يَتَّبِعُهُمْ فِي كِبَرِهِمْ أُعْرِضْ عَنْ هَذَا ۖ إِنَّهُ قَدْ جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَإِنَّهُمْ لَأْتِيهِمْ عَذَابٌ غَيْرُ مَرْدُودٍ ﴿٧٦﴾

74. Basi khofu ilipo-muondoka Ibrahim, na ikawa ile bishara ime-mfikia, alianza kujadiliana nasi juu ya kaumu ya Lut'.

75. Hakika Ibrahim alikuwa mpole, ana huruma, na mwepesi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu.

76. (Akaambiwa): Ewe Ibrahim! Wachilia mbali haya! Kwa hakika amri ya Mola wako Mlezi ime-kwisha kuja, na hakika hao itawafikia adhabu isiyorudi nyuma.



**Mjadala wa Ibrahim عليه السلام Kuhusu Watu wa Lut عليه السلام**

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu Ibrahim عليه السلام kwamba yeye hofu ilipomuondoka, nao malaika, wakambashiria baada ya hapo kupata mtoto, wakamueleza kuhusu kuangamia kwa watu wa Lut عليه السلام. Alianza kusema, kama alivyosema Saeed Bin Jubair katika aya hii, amesema Jibril عليه السلام alipomjia yeye pamoja na malaika wengine, walimuambia:

﴿إِنَّا مُهْلِكُوا أَهْلَ هَذِهِ الْقَرْيَةِ﴾

***“Hakika sisi tutawaangamiza watu wa mji huu...”***

Na Ibrahim عليه السلام akawaambia, ‘hivi mnauangamiza mji ambao ndani yake kuna waumini mia tatu?’ Wakasema: ‘Hapana.’ Akasema, ‘hivi mnaungamiza mji ambao una waumini mia mbili?’ Wakasema: ‘Hapana.’ Akasema: ‘Hivi mnauangamiza mji ambao una waumini arobaini?’ Wakasema, ‘Hapana.’ Akasema, ‘thelathini?’ Wakasema, ‘hapana.’ Mpaka wakafikia watano. Wakasema, ‘Hapana.’ Akasema: ‘Je mnaonaje iwapo utakuwa humo mtu mmoja Muislam?’ Wakasema: ‘Hapana.’ Wakati huo Ibrahim عليه السلام akasema:

﴿إِنَّ فِيهَا لُوطًا قَالُوا فَأَلَيْكَ أَكْثَرُ مِنَّا أَنْتَ بَيْنَ يَدَيْنا لَنْجِيتَنَّهُ وَأَهْلَهُ إِلَّا أَمْرًا نَكْمُ﴾

***“Kwa hakika ndani ya Mji huo yumo Lut, wakasema: Sisi Tunawajua sana waliyomo humo kwa hakika Tutamuokoa yeye na watu wa nyumbani kwake isipokuwa mke wake.”***

Akawanyamazia na nafsi yake Ikatulia.<sup>1</sup>

Na Kauli Yake:

﴿إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَحَلِيمٌ أَوَّهٌ مُّنِيبٌ﴾

***“Hakika Ibrahim alikuwa mpole, ana huruma, na mwepesi wa kurejea kwa Mwenyezi Mungu.” (11:75)***

Alimsifu Ibrahim عليه السلام kwa sifa hizi nzuri, Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

﴿يَا إِبْرَاهِيمُ أَعْرِضْ عَنْ هَذَا إِنَّهُ قَدْ جَاءَ أَمْرٌ رَبِّكَ ط

***“Ewe Ibrahim! Wachilia mbali haya! Kwa hakika Amri ya Mola wako Mlezi imekwisha kuja.”***

<sup>1</sup> Tabari 15/402.

Maana yake: Hukumu kwao imekwisha tekelezwa, na tamko la kuangamizwa limethibitika juu yao, na kushuka shari ambayo hairudishwi kwa watu ambao ni waovu.

وَلَمَّا جَاءَتْ رُسُلُنَا لُوطًا سِيءَ بِهِمْ وَضَاقَ بِهِمْ ذَرْعًا وَقَالَ هَذَا يَوْمٌ عَصِيبٌ ﴿٧٤﴾  
 وَجَاءَهُ قَوْمُهُ يُهْرَعُونَ إِلَيْهِ وَمَنْ قَبْلُ كَانُوا يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ ﴿٧٥﴾ قَالَ يَبْقَوْمِ هَتُّوْا لِي بَنَاتِي  
 هُنَّ أَطْهَرُ لَكُمْ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَلَا تُخْزُونِ فِي ضَيْفِي ۗ أَلَيْسَ مِنْكُمْ رَجُلٌ رَّشِيدٌ ﴿٧٦﴾ قَالُوا  
 لَقَدْ عَلِمْتَمَا لَنَا فِي بَنَاتِكَ مِنْ حَقٍّ وَإِنَّكَ لَتَعْلَمُ مَا تُرِيدُ ﴿٧٧﴾

**77. Na wajumbe wetu walipokuja kwa Lut' aliwahuzunukia na akawaonea dhiki. Akasema: Hii leo ni siku ngumu!**

**78. Wakamjia kaumu yake mbiombio. Na kabla ya haya walikuwa wakitenda maovu. Yeye akasema: Enyi watu wangu! Hawa binti zangu, ndio wametakasika zaidi kwenu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu, wala msinihizi mbele ya wageni wangu. Hivyo, hamna hata mtu mmoja miongoni mwenu aliyeongoka?**

**79. Wakasema: Bila shaka umekwishajua hatuna haki juu ya binti zako, na unayajua tunayoyataka.**

### Ujio wa Malaika kwa Lut عليه السلام, Dhiki Iliyompata na Yaliyojiri Baina Yake na Watu Wake

Allah تعالى Anaeleza kufika kwa wajumbe wake miongoni mwa Malaika, baada ya kumfahamisha Ibrahim عليه السلام kuangamia kwao. Wakaachana naye, wakamueleza kuwa Allah تعالى Atawaangamiza watu wa Lut عليه السلام, usiku huu, wakaondoka kwake wakamuendea Lut عليه السلام na hali ya kuwa yeye kutokana na yale ambayo yamesemwa alikuwa katika ardhi yake. Na pamesemwa alikuwa nyumbani kwake, wakamuendea hali ya kuwa wako katika sura nzuri sana, za vijana wazuri wa nyuso, na hayo ni majaribio kutoka kwa Allah تعالى. Na ni Yake Yeye Hekima na Hoja kubwa. Jambo lao likamhuzunisha, nafsi yake ikapata dhiki, kwa sababu yao, akaogopea iwapo hatawakaribisha wakawa wageni wake, mmoja wa watu wake anaweza akawakaribisha na wakapatwa na ubaya,

وَقَالَ هَذَا يَوْمٌ عَصِيبٌ ﴿٧٤﴾

**“Hii leo ni siku ngumu!”**

Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine wamesema: Balaa lake ni kubwa,<sup>1</sup> na hilo ni kwa sababu yeye alijua atawalinda na hilo ni gumu juu yake. Qatadah ameeleza kwamba wao walimuendea akiwa katika ardhi yake,<sup>2</sup> wakamuomba awakaribishe akawaonea haya akatangulia mbele yao, akawaambia katikati ya njia kama mwenye kuwapa nyongo ili wamuondokee. Kwa hakika ninaapa kwa Allah تعالى, Enyi watu, ‘Mimi sijui juu ya uso wa ardhi hii, watu wa mji ambao ni waovu mno kuliko hawa.’ Kisha akaenda kidogo, kisha akayarudia maneno hayo kwao, mpaka akafikia mara nne. Qatadah amesema: ‘Walikuwa wameamrisha kwamba wasiwaangamize mpaka Mtume wao ashuhudie juu ya jambo hilo.’<sup>3</sup>

Na Kauli Yake:

يُرْعُونَ إِلَيْهِ

**“Wakamjia kaumu yake mbio mbio...”**

Maana yake: Wanakwenda harakaharaka kutokana na kulifurahia kwao hilo.

Na Kauli Yake:

وَمِنْ قَبْلُ كَانُوا يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ ۚ

**“Na kabla ya haya walikuwa wakitenda maovu.”**

Maana yake: Hiyo haikuacha kuwa ndio tabia yao, mpaka wakapatilizwa, hali ya kuwa wao wamo katika hali hiyo. Na Kauli Yake:

قَالَ يَنْقَوْمُ هَتُولَاءِ بَنَاتِي هُنَّ أَطْهَرُ لَكُمْ ۗ

**“Yeye akasema: Enyi watu wangu! Hawa binti zangu, ndio wametakasika zaidi kwenu.”**

Anawaelekeza kwa wanawake wao, kwani Mtume kwa Ummah yuko katika nafasi ya mzazi, akawaelekeza kwenye ambalo lina manufaa sana kwao duniani na akhera, kama alivyowaambia katika aya nyingine.

<sup>1</sup> Tabari 15/311.

<sup>2</sup> Tabari 15/408.

<sup>3</sup> Tabari 15/408.

أَتَأْتُونَ الذُّكْرَانَ مِنَ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٥﴾ وَتَذَرُونَ مَا خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ ۗ بَلْ أَنْتُمْ قَوْمٌ عَادُونَ ﴿١٦٦﴾

**“Je! Katika viumbe vyote mnawaingilia wanaume? Na mnaacha alichokuumbieni Mola wenu Mlezi katika wake zenu? Ama kweli nyinyi ni watu mnaoruka mipaka!” (26:165-166)**

Na Kauli Yake katika aya nyingine:

قَالُوا أَوْلَمْ نَنْهَكَ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٧٠﴾

**“Wakasema: Sisi hatukukukataza usimkaribishe yeyote?” (15:70)**

Maana: Hivi hatukukataza kuwakaribisha wageni wanamume?

قَالَ هَتُّؤُلَاءِ بَنَاتِي إِنْ كُنْتُمْ فَعَالِينَ ﴿٧١﴾ لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٢﴾

**“Akasema: Hawa binti zangu, ikiwa nyinyi ni watendaji. Naapa kwa umri wako! Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakihangaika ovyo.” (15:71-72)**

Na Amesema katika aya hii tukufu:

هَتُّؤُلَاءِ بَنَاتِي هُنَّ أَطْهَرُ لَكُمْ ۗ

**“Hawa binti zangu, ndio wametakasika zaidi kwenu.”**

Mujahid amesema: Hawakuwa binti zake, isipokuwa walikuwa katika umma wake, na kila Mtume ni Baba wa umma wake<sup>1</sup>, kama hivi imepokewa kutoka kwa Qatadah na watu wengine<sup>2</sup>. Na Kauli Yake,

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَلَا تُخْزُونِ فِي ضَيْفِي ۗ

**“Basi mcheni Mwenyezi Mungu, wala msinihizi mbele ya wageni wangu”.**

<sup>1</sup> Tabari 15/414.

<sup>2</sup> Tabari 15/413.

Maana yake: Yakubalini yale ambayo ninakuamrisheni, katika kutosheka na wanawake zenu.

أَلَيْسَ مِنْكُمْ رَجُلٌ رَّشِيدٌ ﴿٧٤﴾

**“Hivyo, hamna hata mtu mmoja miongoni mwenu aliyelongoka?”**

Maana yake: Ambaye ana kheri atakayeyakubali yale ambayo ninakuamrisheni? na akaacha yale ambayo ninakukatazeni?

قَالُوا لَقَدْ عَلِمْتَمَا لَنَا فِي بَنَاتِكَ مِنْ حَقٍّ

**“Wakasema: Bila shaka umekwisha jua hatuna haki juu ya binti zako...”**

Maana yake: Kwa hakika wewe unajua kwamba wanawake wetu hatuna haja nao na hatuwatamani.

وَإِنَّكَ لَتَعْلَمُ مَا نُرِيدُ ﴿٧٥﴾

**“...na unayajua tunayo yataka.”**

Maana yake: Sisi hatuna matakwa isipokuwa kwa wanamume, na wewe unalijua hilo, kwa hiyo kuna haja gani kurudia maneno katika hilo?

قَالَ لَوْ أَنَّ لِي بِكُمْ قُوَّةٌ أَوْ آوَىٰ إِلَىٰ رُكْنٍ شَدِيدٍ ﴿٧٦﴾ قَالُوا يَلُوطُ إِنَّا رُسُلُ رَبِّكَ لَنْ يَصِلُوا إِلَيْكَ فَأَسْرِبْ أَهْلَكَ بِقِطْعٍ مِّنَ اللَّيْلِ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ أَحَدٌ إِلَّا أَمْرَاتُكَ ۗ إِنَّهُ مُصِيبُهَا مَا أَصَابَهُمْ ۗ إِنَّ مَوْعِدَهُمُ الصُّبْحُ ۗ أَلَيْسَ الصُّبْحُ بِقَرِيبٍ ﴿٧٧﴾

**80. Akasema: Laiti ningelikuwa na nguvu kwenu, au nategemea kwenye nguzo yenye nguvu!**

**81. (Wajumbe) wakasema: Ewe Lut! Sisi ni wajumbe wa Mola wako Mlezi. Hawa hawatakufikia. Na wewe ondoka pamoja na ahali zako usiku ungalipo. Wala yeyote miongoni mwenu asitazame nyuma, isipokuwa mkeo, kwani yeye utamfika msiba utakaowafika hao. Hakika miadi yao ni asubuhi. Je, asubuhi si karibu?**

## Kushindwa kwa Lut عليه السلام na Kutamani Awe na Nguvu na Kuwaeleza Malaika Kumueleza Yeye Uhakika

Allah تعالى Anasema, akimuelezea Mtume wake Lut عليه السلام kwamba Lut عليه السلام aliwakemea kwa kauli yake:

قَالَ لَوْ أَنَّ لِي بِكُمْ قُوَّةٌ

**“Akasema: Laiti ningelikuwa na nguvu kwenu.”**

Maana yake: Ningekuwa nimekwisha kuwaadhibu na ningekuwa nimekwisha washikisha adabu mimi mwenyewe na jamaa zangu, na kwa sababu hii imekuja katika Hadithi kutoka kwa Abu Huraira عنه رضي الله kwamba, Mtume ﷺ amesema:

«رَحِمَهُ اللهُ عَلَى لُوطٍ لَقَدْ كَانَ يَأْوِي إِلَى رُكْنٍ شَدِيدٍ» يَعْنِي اللهُ عَزَّ وَجَلَّ «فَمَا بَعَثَ اللهُ بَعْدَهُ مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا فِي تَرْوَةٍ مِنْ قَوْمِهِ»

*“Rehma ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya Lut, alikuwa akitegemea nguvu kubwa”, Anamkusudia Mwenyezi Mungu wa Kushinda, Mwenye Kutukuka – “Mwenyezi Mungu Hakumpeleka baada yake Mtume yeyote, isipokuwa anakuwa katika nguvu kutoka kwa jamaa zake”<sup>1</sup>.*

Wakati huo walimueleza Malaika kwamba wao ni wajumbe wa Allah تعالى kwao na kwamba hao watu wake waovu hawatafika kwake,

قَالُوا يَلُوطُ إِنَّا رُسُلُ رَبِّكَ لَنْ يَصْلُوا إِلَيْكَ<sup>ط</sup>

**“Wajumbe wakasema: Ewe Lut! Sisi ni wajumbe wa Mola wako Mlezi. Hawa hawatakufikia.”**

Wakamuamrisha aende usiku na watu wake, mwisho wa usiku, na awaongoze watu wake,

وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ أَحَدٌ

**“Wala yeyote miongoni mwenu asitazame nyuma.”** Maana yake: Utakaposikia ambacho kimewashukia, na zisikufazaisheni sauti hizo zenye kutisha, isipokuwa endeleeni na safari yenu.

<sup>1</sup> Tirmidhy 3116.

إِلَّا أَمْرًا تَكُ

**"Isipokuwa mkeo."**

Wafasiri wengi wamesema, maana yake: Kuwa yeye hatakwenda na wala hataondoka pamoja nawe, bali atabakia nyumbani kwake na ataangamia.

Kadhaliika imetafsiriwa kwa maana ya: 'yeye atageuka nyuma.' Waliotafsiri hivi wamesema: 'kuwa yeye alitoka pamoja nao, na aliposikia kishindo aligeuka nyuma.' Akasema: 'Ee jamaa zangu!' Likamjia, jiwe kutoka mbinguni likamuuu."

Kisha malaika wakamjia Lut عليه السلام kumjulisha juu ya kuangamia watu wake, kwa sababu yeye aliwaambia: 'Waangamizeni sasa hivi', wakasema:

إِنَّ مَوْعِدَهُمُ الصُّبْحُ ۖ أَلَيْسَ الصُّبْحُ بِقَرِيبٍ ﴿٨٢﴾

**"Hakika miadi yao ni asubuhi. Je, asubuhi si karibu?"**

Haya yote yanafanyika hali ya kuwa watu wa Lut عليه السلام wamesimama mlangoni hawaondoki, wamekuja kwake harakaharaka kutoka kila upande na hali ya kuwa Lut عليه السلام amesimama mlangoni akiwa anawakinga, anawazuia na kuwakataza kuyaacha yale ambayo wao wamo ndani yake, na wao hawamkubalii, bali walikuwa wanamkaripia na kumtisha. Wakati huo akawatokea Jibril عليه السلام akazipiga nyuso zao kwa ubawa wake, akayafuta macho yao, wakarudi na hali ya kuwa hawaioni njia, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَقَدْ رَاوَدُوهُ عَن صَيْفِيهِ فَطَمَسْنَا أَعْيُنَهُمْ فَذُوقُوا عَذَابِي وَتُذِرِ ﴿٨٣﴾

**"Na walimtaka awape wageni wake. Tukayapofua macho yao, na Tukawaambia: Onjeni basi adhabu na maonyo yangu! ." (54:37)**

فَلَمَّا جَاءَ أُمَّرْنَا جَعَلْنَا عَلَيْهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ مَّنصُودٍ ﴿٨٤﴾

مُسَوَّمَةً عِندَ رَبِّكَ ۗ وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ بِبَعِيدٍ ﴿٨٥﴾

**82. Basi ilipofika Amri Yetu Tuliigeuza nchi juu chini, na Tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu uliokamatana wa Motoni.**

**83. Zilizotiwa alama kwa Mola wako Mlezi. Na haya hayako mbali na wenye kudhulumu wengineo.**

Kugeuzwa juu chini Kitongoji cha Watu wa Lut عليه السلام na Kuangamizwa Kwao

Allah تعالى Anasema:

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا

**“Basi ilipofika Amri Yetu.”**

Na hilo lilikuwa wakati wa jua kuchomoza.

جَعَلْنَا عَلَيْهَا

**“Tuliigeuza nchi juu...”** Nayo ni Sodoma,

سَافِلَهَا

**“...chini...”** Kama Kauli Yake, Allah تعالى:

فَغَشَّاهَا مَا غَشَّى

**“Vikaifunika vilivyofunika.” (53:54)**

Maana yake: Tulinyesheleza juu ya mji huo mawe ya udongo mkavu wa *Sijjiil*. Kwa lugha ya Kifursi, ni mawe ya udongo. Hayo ameyasema Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine.<sup>1</sup>

Na baadhi yao wamesema neno *Sijjil* – linatokana na neno - *Sanak*- nalo ni jiwe, na yote hayo yana maana ya udongo, amesema katika aya nyingine,

حِجَارَةً مِّنْ طِينٍ

**“Tuwatupie Mawe ya udongo.” (51:33)**

Maana yake: Udongo ambao umekuwa jiwe, kwa nguvu na ukali, baadhi yao wamesema: Yaliokaangwa. Bukhari amesema: *Sijjil*, maana yake: gumu, kubwa. *Sijjiil na sijjin* herufi mbili hizi (*laam*) na (*nuun*) ni ndugu wawili.<sup>2</sup>

Amesema, Tamim Bin Muqbil aliimba mashairi yake: “Na wapiganaji wa miguu wanazipiga panga kwa kujitolea, kupiga ambako wameshakula kiapo cha “*Sijjin*” ukakamavu.

<sup>1</sup> Tabari 15/434.

<sup>2</sup> Fat’hul al- Bari 8/202.



Na Kauli Yake:

مَنْضُودٍ

**“...uliokamatana.”**

Baadhi yao wamesema: yameandaliwa kutoka mbinguni. Maana yake: Yameandaliwa kwa ajili hiyo, wengine wamesema,

مَنْضُودٍ

**“...uliokamatana.”**

Maana yake: Yanafuata baadhi yao baadhi katika kuwashukia wao. Na Kauli Yake:

مُسُومَةٍ

**“Zilizotiwa alama...”**

Maana yake: Yametiwa alama, yamepigwa mhuri ya majina ya watu wake, kila jiwe limeandikwa juu yake jina la ambaye litamshukia. Qatada na Ikrima wamesema:

مُسُومَةٍ

**“Zilizotiwa alama...”**

Yamezungushwa, Yamenyunyiziwa rangi nyekundu<sup>1</sup>, wametaja kwamba mawe hayo yaliwashukia watu wa mji na wakazi wa viunga vilivyo pembezoni mwake, wakati mmoja wao anapokuwa mbele ya watu akiongea, ghafla humjia jiwe kutoka mbinguni likamdonokea baina ya watu, likamponda, mawe yakawa yanawafuata katika miji mingine mpaka yakawaangamiza hadi wa mwisho wao hakubakia katika wao mtu yeyote. Na Kauli Yake:

وَمَا هِيَ مِنَ الظَّالِمِينَ بَبَعِيرٍ

**“Na haya hayako mbali na wenye kudhulumu wengineo.”**

Maana yake: Haikuwa adhabu hiyo, kwa wale ambao wamejifananisha nao katika dhulma yao kuwa iko mbali nao. Na imekuja katika Hadithi iliyopokewa katika vitabu vya Hadithi kutoka kwa bn Abbas رضي الله عنهما, Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Maana yake: Ina athari na mabaki ya wekundu, Tabari 15/ 438.

«مَنْ وَجَدْتُمْوهُ يَعْمَلْ عَمَلٌ لُّوطٍ فَأَقْتُلُوا الْفَاعِلَ وَالْمَفْعُولَ بِهِ»

*“Mtakayempata anafanya matendo ya watu wa Lut, muuweni mwenye kufanya na mwenye kufanywa”.<sup>1</sup>*

❖ وَإِلَىٰ مَدْيَنَ أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۚ قَالَ يَنْفَوْرِمِ أَعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنِّ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ وَلَا تَنْقُصُوا الْمِكْيَالَ وَالْمِيزَانَ ۚ إِنَّي أُرْسِلُكُمْ بِخَيْرٍ وَإِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ

مُحِيطٍ ﴿٨٤﴾

**84. Na kwa watu wa Madyana Tuliwatumia ndugu yao Shua'ib. Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Mwenyezi Mungu. Nyinyi hamna Mungu ila Yeye, wala msipunguze vipimo na mizani. Mimi nakuoneni mmo katika hali njema, nami nakukhofieni adhabu ya Siku kubwa hiyo itakayokuzungukeni.**

**Kisa cha Mji wa Madyana na Wito wa Shu'aib عليه السلام**

Allah تعالى Anasema: Na kwa hakika Tulimpeleka kwa watu wa Madyana, ambao ni kabila la Waarabu, walikuwa wanaishi kati ya Hijazi na Sham karibu na Maana (jina la mji). Miji inayojulikana kwao kwa jina la Madyana, Allah تعالى Akawapeleka Mtume Shu'aib عليه السلام, alikuwa ni katika watukufu wao zaidi kinasaba. Kwa sababu hiyo amesema:

أَخَاهُمْ شُعَيْبًا ۚ

*“...ndugu yao Shua'ib.”*

Aliwaamrisha kumuabudu Allah تعالى Peke Yake asiye na mshirika, na aliwakataza kupunguza pishi na mizani.

إِنِّي أُرْسِلُكُمْ بِخَيْرٍ

*“Mimi nakuoneni mmo katika hali njema...”*

Maana yake: Katika maisha yenu na riziki yenu, na kwa hakika mimi ninakukhofieni kunyang'anywa neema ambazo mlizo nazo, kwa kuvunja kwenu maharamisho ya Allah تعالى,

<sup>1</sup> Abu Daawud 4,462, Tirmidhy 1,456.

إِنِّي أَرْسَلْتُكُمْ بِخَيْرٍ وَإِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ مُّحِيطٍ ﴿٧٤﴾

***"...nami nakukhofieni adhabu ya Siku kubwa hiyo itakayo kuzungukeni."***

Maana yake: Katika nyumba ya akhera.

\* \* \*

وَيَقَوْمٍ أَوْفُوا الْمَكَالَ وَالْمَيْرَاتِ بِالْقِسْطِ ۗ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٨٥﴾ بَقِيَّتُ اللَّهِ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ۗ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ ﴿٨٦﴾ قَالُوا يَشْعِيبُ أَسْلَوْنَاكَ تَأْمُرُنَا أَنْ نَتْرَكَ مَا يَعْبُدُ آبَاؤُنَا أَوْ أَنْ نَفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا نَشَاءُ ۗ إِنَّكَ لَأَنْتَ الْحَلِيمُ الرَّشِيدُ ﴿٨٧﴾ قَالَ يَنْقَوْمِرَ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ يَدَيْنِ مِنْ رَبِّي وَرَزَقَنِي مِنْهُ رِزْقًا حَسَنًا ۚ وَمَا أُرِيدُ أَنْ أَمْلِكُمْ إِلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَنْهُ ۗ إِنْ أُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ مَا اسْتَطَعْتُ ۗ وَمَا تَوْفِيقِي إِلَّا بِاللَّهِ ۗ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ ﴿٨٨﴾ وَيَنْقَوْمِرَ لَا يَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقِي أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ مَا أَصَابَ قَوْمَ نُوحٍ أَوْ قَوْمَ هُودٍ أَوْ قَوْمَ صَالِحٍ ۗ وَمَا قَوْمُ لُوطٍ مِنْكُمْ بِبَعِيدٍ ﴿٨٩﴾ وَأَسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ ۗ إِنَّ رَبِّي رَحِيمٌ وَدُودٌ ﴿٩٠﴾

وَيَقَوْمٍ أَوْفُوا الْمَكَالَ وَالْمَيْرَاتِ بِالْقِسْطِ ۗ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْتُوا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٨٥﴾ بَقِيَّتُ اللَّهِ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ۗ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ ﴿٨٦﴾

**85. Na enyi watu wangu! Timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu wala msiwakhini watu vitu vyao; wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu.**

**86. Alivyokubakishieni Mwenyezi Mungu ndiyo bora kwa ajili yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini. Wala mimi siye mlinzi wenu.**

Kwanza Anawakataza kupunguza pishi na mizani, wanapowapa watu, kisha Akawaamrisha kukamilisha pishi na mizani kwa uadilifu wakipokea na wakitoa, Akawakataza kufanya ufisadi katika ardhi, kwa hakika walikuwa wakifanya uhalifu njiani. Na Abu Jaafar Bin Jarir رحمه الله تعالى amesema:

بَقِيَّتُ اللَّهِ خَيْرٌ لَّكُمْ

**"Alivyokubakishieni Mwenyezi Mungu ndiyo bora kwa ajili yenu..."**

Maana yake: Kilichozi kwenu katika faida baada ya kukamilisha pishi na mizani ni bora kwenu kuliko kuchukua mali za watu<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Tabari 15/447.

Amesema: Na haya yamepokelewa kutokana na Ibni Abbas رضي الله عنهما.  
(Nimesema): Haya yanafanana<sup>1</sup> na Maneno ya Allah تعالى:

قُلْ لَا يَسْتَوِي الْخَبِيثُ وَالطَّيِّبُ وَلَوْ أَعْجَبَكَ كَثْرَةُ الْخَبِيثِ

**“Sema: Haviwi sawa viovu na vyema ujapo kutakupendeza wingi wa viovu...” (5:100)**

Isome aya hiyo mpaka mwisho wake. Na Kauli Yake,

وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ

**“Wala mimi siye mlinzi wenu”.**

Maana yake: Mimi si mwenye kuwachunga wala si mwenye kuwalinda. Maana yake: Fanyeni hayo kwa ajili ya Allah تعالى Mshindi Mtukuka. Msifanye hayo ili watu wawaone, bali fanyeni kwa ajili ya Allah عزوجل Mwenye Kushinda Mwenye Kutukuka.

قَالُوا يَنْشُعِبُ أَصْلُوتُكَ تَأْمُرُكَ أَنْ نَتْرَكَ مَا يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا أَوْ أَنْ نَفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا

دَشْتُوا إِنَّكَ لَأَنْتَ الْحَلِيمُ الرَّشِيدُ

**87. Wakasema: Ewe Shua'ib! Ni sala zako ndizo zinazokuamrisha tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu? Ama hakika wewe ni mstahamilivu kweli na mwongofu!**

**Majibu ya Watu wa Shuaib عليه السلام**

Wanamuambia kwa njia ya kumdhihaki - Allah تعالى Awalani:

أَصْلُوتُكَ

**“Ni sala zako?”** Al-Amash amesema: Maana yake: kisomo chako.

تَأْمُرُكَ أَنْ نَتْرَكَ مَا يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا

**“Ndizo zinazokuamrisha tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu?”**

<sup>1</sup> Tabari 15/447.

Maana yake: Masanamu.

أَوْ أَنْ نَفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا دَشَتُوا<sup>ط</sup>

**“Au kufanya katika mali zetu tunavyotaka?”**

Kwa hiyo, tuache kupunguza vipimo kwa sababu ya maneno yako, na hali ya kuwa hizo ni mali zetu na tunafanya katika mali zetu tunalolitaka. Al-Hassan amesema: katika Kauli Yake:

أَصَلَوْتُكَ تَأْمُرُكَ أَنْ نَتْرَكَ مَا يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا

**“Ni sala zako ndizo zinazokuamrisha tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu?”**

Ndiyo ninaapa kwa Allah تعالى kwa hakika maombi yake yanawaamrisha waache vile ambavyo walikuwa wanaviabudu wazee wao<sup>1</sup>. Na Thaury رحمه الله تعالى amesema, katika Kauli Yake:

أَوْ أَنْ نَفْعَلَ فِي أَمْوَالِنَا مَا دَشَتُوا<sup>ط</sup>

**“Au kufanya katika mali zetu tunavyotaka?”**

Wanakusudia zaka.

إِنَّكَ لَأَنْتَ الْحَلِيمُ الرَّشِيدُ ﴿٨٧﴾

**“Ama hakika wewe ni mstahamilivu kweli na mwongofu!”**

Ibn Abbas, Maymuun Bin Mahraan, Ibn Juraiji na Ibn Aslam<sup>2</sup> na Ibn Jariri رضي الله عنهم wamesema: wanayasema hayo maadui wa Allah تعالى kwa njia ya kucheza shere - Allah تعالى Awaadhibu, na Awalani, wawe mbali na rehma Yake – na Allah تعالى Amekwisha fanya hivyo<sup>3</sup>.

قَالَ يَفْقَوْمِ اٰرْءَيْتُمْ اِنْ كُنْتُمْ عَلٰى بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّيْ وَرَزَقْنِيْ مِنْهُ رِزْقًا حَسَنًا وَمَا اُرِيْدُ اَنْ

اُخَالَفَكُمْ اِلٰى مَا اَنْهَيْتُمْ عَنْهُ اِنْ اُرِيْدُ اِلَّا الْاِصْلَاحَ مَا اَسْتَطَعْتُ وَمَا تَوْفِيْقِيْ اِلَّا بِاللّٰهِ

عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَاِلَيْهِ اُنِيْبُ ﴿٨٨﴾

<sup>1</sup> Tabari 15/451.

<sup>2</sup> Tabari 15/453.

<sup>3</sup> Tabari 15/453.

**88. Akasema: Enyi watu wangu! Mnaonaje ikiwa ninayo dalili wazi inayotokana na Mola wangu Mlezi, na ikawa Yeye Ameniruzuku riziki njema kutoka Kwake? Wala mimi sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayokukatazeni. Sitaki ila kutengeneza kiasi ninavyo weza. Na sipati kuwezesha haya ila na Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye ninategemea, na Kwake Yeye naelekea.**

### **Majibu ya Shuaib عليه السلام kwa Watu Wake**

Anawaambia, Je mnaonaje enyi jamaa zangu,

عَلَىٰ بَيْنِ مِنِّي مِنِّي

**“Mnaonaje ikiwa ninayo dalili ya wazi inayotokana na Mola wangu Mlezi...”,**

Maana yake: Nikiwa nina uongofu ulio wazi katika lile ambalo ninawalingania:

وَرَزَقْنِي مِنْهُ رِزْقًا حَسَنًا

**“...na ikawa Yeye Ameniruzuku riziki njema kutoka Kwake?”**

Imesemwa: amekusudia utume, na imesemwa: amekusudia riziki ya halali, na inawezekana yote mawili. Na amesema Thawry:

وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَىٰ مَا أَنْتَهُكُمْ عَنْهُ

**“Wala mimi sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayokukatazeni.”**

Maana yake: Sitawakataza jambo na nikaenda kinyume kwa siri nikalifanya kwa kuwaficha nyinyi. Kama alivyosema Qatada katika Kauli Yake:

وَمَا أُرِيدُ أَنْ أُخَالِفَكُمْ إِلَىٰ مَا أَنْتَهُكُمْ عَنْهُ

**“Wala mimi sipendi kukukhalifuni nikafanya yale ninayokukatazeni.”**

Anasema: Sikuwa ninawakataza jambo na nikalitenda<sup>1</sup> mimi.

<sup>1</sup> Tabari 15/453.

إِنْ أُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ مَا اسْتَطَعْتُ

**“Sitaki ila kutengeneza kiasi ninavyo weza.”**

Maana yake: Katika lile ambalo ninawaamrisha, na ninalowakataza. Hakika si vinginevyo ninataka kutengemaa kwenu kwa juhudi yangu na uwezo wangu.

وَمَا تَوْفِيقِي

**“Na sipati kuwezesha...”**

Maana yake: Katika kupatia haki katika ninalolitaka,

إِلَّا بِاللَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ

**“...ila na Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye ninategemea...”**

Katika mambo yangu yote,

وَالَيْهِ أُيِّبُ

**“...na kwake Yeye naelekea”.**

Maana yake: Ninarejea. Hayo ameyasema Mujahid na wengine<sup>1</sup>.

وَيَقَوْمٍ لَا تَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقِي أَنْ يُصِيبَكُمْ مِثْلُ مَا أَصَابَ قَوْمَ نُوحٍ أَوْ قَوْمَ هُودٍ أَوْ قَوْمَ  
صَالِحٍ وَمَا قَوْمُ لُوطٍ مِنْكُمْ بِبَعِيدٍ ۝ وَأَسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ إِنَّ رَبِّي  
رَحِيمٌ وَدُودٌ

**89. Na enyi watu wangu! Kukhalifiana nami kusikupelekeeni hata mkasibiwa kama walivyosibiwa watu wa Nuhu, au watu wa Hud, au watu wa Saleh. Na watu wa Lut' si mbali nanyi.**

**90. Na ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi, tena tubuni kwake. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kurehemu na Mwenye Upendo.**

Anawaambia,

وَيَقَوْمٍ لَا تَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقِي

**“Na enyi watu wangu! Kukhalifiana nami kusikupelekeeni.”**

<sup>1</sup> Tabari 15/454.



Maana yake: Kunifanyia kwenu uadui na kunichukia kusiwachukue juu ya kuendelea na yale ambayo mmo ndani yake, miongoni mwa ukafiri na ufisadi, yatawapateni mfano wa yale yaliyowapata watu wa Nuuh عليه السلام, watu wa Hud عليه السلام, watu wa Saleh عليه السلام na watu wa Lut عليه السلام, miongoni mwa mateso na adhabu. Na Qatada amesema:

وَيَقَوْمٍ لَا تَجْرِمَنَّكُمْ شِقَاقِي

**“Na enyi watu wangu! Kukhalifiana nami kusikupelekeeni,...”**

Anasema: Kusikupelekeeni kutengana nami.<sup>1</sup> Assudiyi amesema: Kunifanyia kwenu uadui, kusikufanyeni kuendelea katika upotevu na ukafiri, ikakupateni adhabu ambayo imewapata wao. Na Kauli Yake:

وَمَا قَوْمٌ لُوطٍ مِّنْكُمْ بِبَعِيدٍ

**“Na watu wa Lut’ si mbali nanyi.”**

Imesemwa: Makusudio ni katika zama. Qatadah amesema: Anakusudia kwamba hakika waliangamia mbele yenu jana. Na imesemwa: Ni mahali, na inawezekana mawili yote.

وَأَسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ

**“Na ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi,...”**

Kutokana na madhambi yaliyotangulia,

ثُمَّ تَوْبُوا إِلَيْهِ

**“...tena tubuni Kwake.”**

Katika muda unaokuja mbele kwa matendo maovu. Na Kauli Yake:

إِنَّ رَبِّي رَحِيمٌ وَدُودٌ

**“Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kurehemu na Mwenye Upendo.”**

Kwa mwenye kurejea Kwake.

<sup>1</sup> Tabari 15/458.

قَالُوا يَدْعُبُ مَا نَفَقَهُ كَثِيرًا وَمَا تَقُولُ وَإِنَّا لَنَرَاكَ فِينَا  
 ضَعِيفًا ۖ وَلَوْلَا رَهْطُكَ لَرَجَمْنَاكَ ۖ وَمَا أَنْتَ عَلَيْنَا بَعِزٌّ ۙ ﴿٩١﴾  
 قَالَ يَنْقَوْمِ أَرْهَطَىٰ أَعَزُّ عَلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَاتَّخَذْتُمُوهُ  
 وَرَاءَكُمْ ظَهْرِيًّا ۗ إِنَّ رَبِّي بِمَا تَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ۙ ﴿٩٢﴾  
 وَيَنْقَوْمِ أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَاتِبِكُمْ إِنِّي عَمِلٌ ۗ سَوْفَ  
 تَعْلَمُونَ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ مُّخْزٍ بِهِ وَمَنْ هُوَ كَذِبٌ ۗ  
 وَأَرْتَقِبُوا إِنِّي مَعَكُمْ رَقِيبٌ ۙ ﴿٩٣﴾ وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا  
 شُعَيْبًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَأَخَذَتِ الَّذِينَ  
 ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِئْرِهِمْ جَئِشِينَ ۙ ﴿٩٤﴾  
 كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا ۗ أَلَا بُعْدًا لِّمَدْيَنَ كَمَا بَعَدَتِ ثَمُودُ ۙ ﴿٩٥﴾  
 وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ۙ ﴿٩٦﴾ إِلَىٰ  
 فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ فَاتَّبَعُوا أَمْرَ فِرْعَوْنَ ۗ وَمَا أَمْرُ فِرْعَوْنَ  
 بِرَشِيدٍ ۙ ﴿٩٧﴾ يَقْدُمُ قَوْمَهُ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فَأَوْرَدَهُمُ النَّارَ ۗ  
 وَبِئْسَ الْوَرْدُ الْمَوْرُودُ ۙ ﴿٩٨﴾ وَاتَّبِعُوا فِي هٰذِهِ لَعْنَةً وَيَوْمَ  
 الْقِيٰمَةِ ۗ بِئْسَ الرِّفْدُ الْمَرْفُودُ ۙ ﴿٩٩﴾

قَالُوا يَدْعُبُ مَا نَفَقَهُ كَثِيرًا وَمَا  
 تَقُولُ وَإِنَّا لَنَرَاكَ فِينَا ضَعِيفًا ۖ  
 وَلَوْلَا رَهْطُكَ لَرَجَمْنَاكَ ۖ وَمَا أَنْتَ  
 عَلَيْنَا بَعِزٌّ ۙ ﴿٩١﴾ قَالَ يَنْقَوْمِ  
 أَرْهَطَىٰ أَعَزُّ عَلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ  
 وَاتَّخَذْتُمُوهُ وَرَاءَكُمْ ظَهْرِيًّا ۗ إِنَّ  
 رَبِّي بِمَا تَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ۙ ﴿٩٢﴾

91. Wakasema: Ewe Shua'ibu! Mengi katika hayo unayoyasema hatu-yafahamu. Na sisi tuna-kuona huna nguvu kwetu. Lau kuwa si jamaa zako tungekupiga mawe, wala wewe si mtukufu kwetu.

92. Akasema: Enyi watu wangu! Kwani jamaa zangu ni watukufu zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu? Na Yeye mmemueka nyuma ya migongo yenu!

**Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kuyazunguka yote mnyoyatenda.**

**Majibu ya Watu ya Shuaib** عليه السلام

Wanasema:

قَالُوا يَدشُعِبُ مَا نَفَقَهُ

**“Ewe Shua’ibu! Mengi katika hayo unayoyasema hatuyafahamu...”**

Hatufahamu,

كثيراً

**“Mengi”**Katika maneno yako. Na Thauri amesema: Alikuwa anaitwa: Hatibu wa Mitume.<sup>1</sup> Sudy amesema:

وَإِنَّا لَنَرُكَ فِيْنَا ضَعِيفًا

**“Na sisi tunakuona huna nguvu kwetu.”**

Amesema: Wewe ni mmoja tu. Na Abuu Rawq amesema: Wanakusudia kuwa mnyonge kwa sababu jamaa zako hawako katika dini yako.

وَلَوْلَا رَهْطُكَ لَرَجِمْنَاكَ

**“Lau kuwa si jamaa zako tungekupiga mawe.”**

Maana yake: Jamaa zako, lau si ubora wao kwetu tungekupiga mawe, Imesemwa: Kwa mawe, na Imesemwa tungekutukana,

وَمَا أَنْتَ عَلَيْنَا بَعِزٌّ

**“Wala wewe si mtukufu kwetu.”** Maana yake: Wewe kwetu huna ubora wowote.**Majibu ya Shu’aibu** عليه السلام **kwa Jamaa Zake**

Anawaambia:

قَالَ يَنْقَوْمِ أَرْهَطِي - أَعَزُّ عَلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ

**“Akasema: Enyi watu wangu! Kwani jamaa zangu ni watukufu zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu?”**<sup>1</sup> Tabari 15/458.

Anasema: Mnaniacha kwa ajili ya heshima ya watu wangu? wala hamniachi kwa ajili ya kutukuza Utukufu wa Allah تعالى, kwa kutomfanyia mabaya Mtume wake?, na huku mkimtenga Yeye.

وَرَأَىٰ كُمْ ظَهْرِيًّا

**“Na Yeye mmemuweka nyuma ya migongo yenu!”**

Maana yake: mmemtupa nyuma yenu hamumuheshimu wala hamumtukuzi,

إِنَّ رَبِّي بِمَا تَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٧﴾

**“Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kuyazunguka yote mnayo yatenda”.**

Maana yake: Yeye Anajua matendo yenu yote, na Atawalipa kwayo.

وَيَنْقُورِ أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَاتِبِكُمْ إِنِّي عَمِلٌ ۗ سَوْفَ تَعْلَمُونَ ۗ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ مُّخْزٍ  
وَمَنْ هُوَ كَذِبٌ ۗ وَأَرْتَقِبُوا إِنِّي مَعَكُمْ رَقِيبٌ ﴿١٨﴾ ۗ وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجِيتَنَا شُعَيْبًا  
وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَأَخَذَتِ الَّذِينَ ظَلَمُوا الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِيَرِهِمْ  
جَنِّمِينَ ﴿١٩﴾ ۗ كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا ۗ أَلَا بُعْدًا لِّمَدْيَنَ كَمَا بَعَدَتِ ثَمُودُ ﴿٢٠﴾

**93. Na enyi watu wangu! Fanyeni (mtakayo) kwa tamkini yenu (mtakavyo); na mimi pia ninafanya (yangu kwa tamkini yangu). Karibuni hivi mtajua ni nani itakayemfikia adhabu ifedheheshayo na nani aliye mwongo. Na ngojeeni, mimi pia ninangoja pamoja nanyi.**

**94. Na ilipofika Amri Yetu, Tulimuokoa Shua'ib na wale walioamini pamoja naye kwa Rehema Yetu. Na ukelele uliwanyakua waliodhulumu, na wakapambaukiwa majumbani mwao wamekufa kifudifudi!**

**95. Kama kwamba hawakuwamo humo. Zingatia walivyoangamia watu wa Madyana, kama walivyoangamia watu wa Thamud!**

**Vitisho vya Shua'ib عليه السلام kwa Watu Wake**

Mtume Shuaib عليه السلام alipokata tamaa ya kuitikiwa alisema: Enyi jamaa zangu:

أَعْمَلُوا عَلَيَّ مَكَاتِبِكُمْ

**“Fanyeni (mtakayo) kwa tamkini yenu (mtakavyo)...”**

Maana yake: Fuataeni njia yenu, na haya ni matisho makali,

إِنِّي عَمِلٌ

**“...na mimi pia ninafanya (yangu kwa tamkini yangu).”** Kufuata njia yangu

سَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ يَأْتِيهِ عَذَابٌ مُخْتَلِفٌ وَمَنْ هُوَ كَذِبٌ

**“Karibuni mtajua ni nani itakayemfikia adhabu ya kumhizi, na nani aliye mwongo.”**

Maana yake: Kutoka kwangu na kutoka kwenu,

وَأَرْتَقِبُوا

**“Na ngojeni”** Maana yake: Ngojeeni,

إِنِّي مَعَكُمْ رَقِيبٌ

**“...mimi pia nina ngoja pamoja nanyi.”**

Amesema Allah تعالى:

وَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَّيْنَا شُعَيْبًا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِنَّا وَأَخَذَتِ الَّذِينَ ظَلَمُوا

الصَّيْحَةَ فَأَصْبَحُوا فِي دِيَارِهِمْ جَنِينَ

**“Na ilipofika Amri Tetu, Tulimuokoa Shua'ib na wale walioamini pamoja naye kwa Rehema Yetu. Na ukelele uliwanyakua waliodhulumu, na wakapambaukiwa majumbani mwao wamekufa kifudifudi!”**

Na Kauli Yake: Kifudifudi. Yaani waliotulia, hawana mtikisiko wowote. Hapa ametaja kuwa umewajia wao (ukelele), na katika Suratil A'araf aya ya 91,

(*mtetemeko*), na katika *Suratil Shu'araa*, (*Adhabu ya siku ngumu*) aya ya 189, hao ni umma mmoja. Siku ya adhabu yao mateso haya yote yalikusanyika kwao. Ametaja katika kila msemu yanayolingana nayo, katika Al-A'araaf waliposema:

لُنُخْرِجَنَّكَ يَشُعَيْبُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا

**“...Tutakutoa wewe pamoja na wale waliokuamini katika mji wetu...” (7:88)**

Katika Aya hii imenasibiana kutaja ‘*mtetemeko*’ kwa hiyo ardhi ikatetemeshwa kwao, ambayo wamedhulumu juu yake, wakataka kumtoa humo Mtume wao, na katika aya hii walipokosa adabu katika maneno yao kwa Mtume wao, ameutaja ‘ukelele’ ambao uliwachukua kidogokidogo na ukawazima. Na katika *Shu'araa*, waliposema:

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٨٧﴾

**“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni ikiwa wewe ni miongoni mwa wasema kweli.” (26:187)**

Allah تعالی Akasema,

فَأَخَذَهُمْ عَذَابٌ يَوْمِ الظُّلَّةِ إِنَّهُ كَانَ عَذَابٌ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٨٩﴾

**“Na ikawashika adhabu ya siku ya kivuli. Hakika hiyo ilikuwa adhabu ya siku kubwa.” (26:189)**

Hizi ni miongoni mwa siri za ndani sana – na ni za Allah تعالی tu Sifa Njema na Neema zenye kudumu.

Na Kauli Yake:

كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا

**“Kama kwamba hawakuwamo humo.”**

Maana yake: Hawakuishi katika miji yako kabla ya hapo.

أَلَا بُعْدًا لِّمَدْيَنَ كَمَا بَعَدَتِ ثَمُودُ ﴿١٩٠﴾

**“Zingatia walivyoangamia watu wa Madyana, kama walivyoangamia watu wa Thamud!”**

Na wa Thamud Walikuwa ni jirani zao, wako karibu na wao katika miji, walikuwa wanafanana nao katika ukafiri na uhalifu, walikuwa ni Waarabu mfano wao.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٦٦﴾ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِۦ فَاتَّبَعُوْا أَمْرَ  
فِرْعَوْنَ ۗ وَمَا أَمْرُ فِرْعَوْنَ بِرَشِيْدٍ ﴿٦٧﴾ يَقْدُمُ قَوْمَهُ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فَأَوْرَدَهُمُ النَّارَ  
وَيَتَسَّ الْوَرْدُ الْمَوْرُوْدُ ﴿٦٨﴾ وَأَتَّبَعُوْا فِي هٰذِهِ لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۗ يَتَسَّ الرَّفْدُ  
الْمَرْفُوْدُ ﴿٦٩﴾

**96. Na hakika Tulimtuma Musa pamoja na Ishara Zetu na uthibitisho uliowazi**

**97. Kwa Firauni na waheshimiwa wake. Lakini wao walifuata amri ya Firauni, na amri ya Firauni haikuwa yenye uwongofu.**

**98. Siku ya Kiyama atawatangulia watu wake na atawaingiza Motoni. Na muingio muovu ulioje huo!**

**99. Nao wamefuatishiwa laana hapa duniani na Siku ya Kiyama. Ni mabaya yalioje watakayopewa!**

**Kisa cha Mussa عليه السلام na Firauni**

Allah تعالى Anasema: hali ya kuelezea kupelekwa kwa Mussa عليه السلام na miujiza na dalili zilizowazi zenye kushinda, kwa Firauni Mfalme wa Waqibti na waheshimiwa wao,

فَاتَّبَعُوْا أَمْرَ فِرْعَوْنَ ۗ

**“Walifuata amri ya Firauni.”**

Maana yake: Utaratibu wake njia na mpango wake katika upotevu,

وَمَا أَمْرُ فِرْعَوْنَ بِرَشِيْدٍ ﴿٦٧﴾

**“...na amri ya Firauni haikuwa yenye uwongofu.”**

Maana yake: Hamna ndani yake uongofu wala mwongozo, isipokuwa ni ujinga upotevu, ukafiri na inadi. Na kama walivyokuwa wamemfuata hapa duniani,

na alikuwa kiongozi wao, hivyo hivyo atakuwa mbele yao siku ya kiyama kuelekea motoni. Atawaingiza motoni na watakuwa katika mabirika yake ya maangamivu na yeye atakuwa na fungu kubwa katika maangamivu hayo, katika adhabu kubwa. Kama Allah تعالى Alivyosema:

فَعَصَى فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيلاً ﴿٧٣﴾

**“Lakini Firauni alimuasi Mtume huyo, basi Tukamshika mshiko wa mateso.” (73:16)**

فَكَذَّبَ وَعَصَى ﴿٧٤﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَى ﴿٧٥﴾ فَحَشَرَ فَنَادَى ﴿٧٦﴾ فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَى ﴿٧٧﴾ فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْأَخْزَةِ وَالْأُولَى ﴿٧٨﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِمَن يَخْشَى ﴿٧٩﴾

**“Lakini alihakadhibisha na akaasi. Kisha alirudi nyuma, akaingia kufanya juhudi. Akakusanya watu akanadi. Akasema: Mimi ndiye mola wenu mlezi mkuu kabisa. Basi hapo Mwenyezi Mungu Akamshika Kumuadhibu kwa la mwisho na la mwanzo. Kwa hakika katika haya yapo mazingatio kwa wanaoogopa.” (79:21-29)**

Allah تعالى Amesema:

يَقْدُمُ قَوْمَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَأَوْرَدَهُمُ النَّارَ وَبِئْسَ الْوِرْدُ الْمَوْرُودُ ﴿٨٠﴾

**“Siku ya Kiyama atawatangulia watu wake na atawaingiza Motoni. Na muingio muovu ulioje huo! ”**

Hivyo ndivyo ilivyo hali ya wenye kufuatwa wanakuwa wenye fungu kubwa katika adhabu siku ya Kiyama, kama Allah تعالى Alivyosema:

لِكُلِّ ضِعْفٍ وَلَكِن لَّا تَعْلَمُونَ ﴿٨١﴾

**“...kila mmoja ana yongeza yake lakini hajui” (7:38)**

Na Allah تعالى Amesema Akielezea kuhusu makafiri kwamba wao wakiwa motoni watasema:

رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَّرَاءَنَا فَأَضَلُّونَا السَّبِيلَا ﴿٨٢﴾ رَبَّنَا ءَاتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ



***“Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwat’ii bwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio waliotupoteza njia. Mola wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili...” (33:67-68)***

Na Kauli Yake:

وَأَتَّبِعُوا فِي هَذِهِ لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ

***“Nao wamefuatishiwa laana hapa duniani na Siku ya Kiyama.”***

Maana yake: Tumewafuatishia nyongeza juu ya adhabu ya moto, laana duniani na siku ya Kiyama, msaada mbaya ambao umetolewa ni huo.

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ بِئْسَ الرِّفْدُ الْمَرْفُودُ

***“...na Siku ya Kiyama. Ni mabaya yalioje watakayopewa!”***

Mujahid amesema wataongezewa laana Siku ya Kiyama, kwa hiyo hizo ni laana mbili<sup>1</sup>.

Na Ali Bin Abi Twalha amesema kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما:

بِئْسَ الرِّفْدُ الْمَرْفُودُ

***“Ni mabaya yalioje watakayopewa!”***

Amesema: Laana ya dunia na akhera.<sup>2</sup> Na kama hivyo amesema Dhahak na Qatada<sup>3</sup>.

Na maneno hayo ni kama Kauli Yake:

وَجَعَلْنَاهُمْ أَيْمَةً يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يُنصَرُونَ ﴿١١﴾ وَأَتَّبَعْنَاهُمْ فِي

هَذِهِ الدُّنْيَا لَعْنَةً وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ هُمْ مِنَ الْمَقْبُوحِينَ ﴿١٢﴾

***“Na Tuliwafanya ni viongozi waitao kwenye Moto. Na Siku ya Kiyama hawatanusuriwa. Na Tukawafuatishia laana katika dunia hii, na Siku ya Kiyama watakuwa miongoni mwa wanaochusha.” (28:41-42)***

<sup>1</sup> Tabari 15/468.

<sup>2</sup> Tabari 15/469.

<sup>3</sup> Tabari 15/469,480.

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا ۖ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ

الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

***“Wanaoneshwa Moto asubuhi na jioni. Na itapofika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!” (40:46)***

\* \* \*

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْقُرَى نَقُصُّهُ عَلَيْكَ مِنْهَا قَائِمٌ  
 وَحَصِيدٌ ﴿١٠٠﴾ وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ فَمَا  
 أَغْنَتْ عَنْهُمْ آلِهَتُهُمُ الَّتِي يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ  
 لَمَّا جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ وَمَا زَادُوهُمْ غَيْرَ تَتْسِيرٍ ﴿١٠١﴾  
 وَكَذَلِكَ أَخْذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَى وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ  
 أَخْذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِمَنْ خَافَ  
 عَذَابَ الْآخِرَةِ ذَلِكَ يَوْمٌ تَجْمَعُ لَهُ النَّاسُ وَذَلِكَ يَوْمٌ  
 مَشْهُودٌ ﴿١٠٣﴾ وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مَعْدُودٍ ﴿١٠٤﴾ يَوْمٌ  
 يَأْتِ لَا تَكَلِّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَسَعِيدٌ  
 ﴿١٠٥﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ شَقُوا فِي النَّارِ هُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَشَهِيْقٌ  
 ﴿١٠٦﴾ خَلِيدِينَ فِيهَا مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ إِلَّا  
 مَا شَاءَ رَبُّكَ إِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِمَا يُرِيدُ ﴿١٠٧﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ  
 سَعِدُوا فِي الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ  
 وَالْأَرْضُ إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ عَطَاءٌ غَيْرَ مَجْدُوذٍ ﴿١٠٨﴾

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْقُرَى نَقُصُّهُ  
 عَلَيْكَ مِنْهَا قَائِمٌ وَحَصِيدٌ ﴿١٠٠﴾  
 وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ  
 فَمَا أَغْنَتْ عَنْهُمْ آلِهَتُهُمُ الَّتِي  
 يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ لَمَّا  
 جَاءَ أَمْرُ رَبِّكَ وَمَا زَادُوهُمْ غَيْرَ  
 تَتْسِيرٍ ﴿١٠١﴾

100. Hizi ni katika khabari za miji, Tunakusimulia. Mingine ipo bado na mingine imefyekwa.

101. Na Sisi hatukuwadhulumu, lakini wao wenyewe wamejidhulumu. Na miungu yao waliyokuwa wakiiomba badala ya Mwenyezi Mungu haikuwafaa kitu ilipokuja Amri ya Mola wako Mlezi. Na hiyo miungu haikuwazidi shia ila maangamizo tu.

### Kuonyeka Kutokana na Miji Iliyoangamizwa

Allah تعالی Alipotaja khabari za Mitume na yaliyowapitia pamoja na umma wao na jinsi Alivyowaangamiza makafiri, na jinsi Alivyowaokoa waumini Amesema:

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْقُرَى

“Hizi ni katika khabari za miji...”

Maana yake: Khabari za watu wa miji hiyo.

نَقُصُّهُ عَلَيْكَ مِنْهَا قَائِمٌ

**“Tunakusimulia, Mingingine ipo bado...”**

Maana yake: Imeimarika,

وَحَصِيدٌ

**“...na mingine imefyekwa.”**

Maana yake: Imeangamia,

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ

**“Na Sisi hatukuwadhulumu.”**

Maana yake: Tulipowaangamiza,

وَلَكِنْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ

**“lakini wao wenyewe wamejidhulumu.”**

Kwa sababu ya kuwakadhibisha kwao Mitume wetu na kuwakufuru.

فَمَا أَغْنَتْ عَنْهُمْ آلِهَتُهُمْ

**“Na miungu yao haikuwafaa kitu.”**

Masanamu yao ambayo wanayaabudu na wanayoyaomba.

مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ

**“..badala ya Mwenyezi Mungu haikuwafaa kitu...”**

Hayakuwanufaisha wala hayakuwaokoa ilipokuja Amri ya Allah تعالى, ya kuangamizwa kwao.

وَمَا زَادُوهُمْ غَيْرَ تَتْبِيبٍ

**“...haikuwazidishia ila maangamizo tu.”**

Mujaahidi, Qatadah na wengine wamesema: Ina maana: isipokuwa kukhasirika, na hilo ni kuwa kuangamia kwao na kuharibiwa kwao, ni kwa sababu ya kufuata miungu yao, kwa sababu hiyo wamepata hasara duniani na akhera<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Tabari 15/473.

وَكَذَلِكَ أَخْذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ ۗ إِنَّ أَخْذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿١٠٢﴾

**102. Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi Anapoikamata miji inapokuwa imedhulumu. Hakika mkamoto wake ni mchungu na mkali.**

Allah تعالى Anasema: na kama Tulivyowaangamiza madhalimu wa karne hizo, wenye kuwakadhibisha Mitume wetu, na hivyo hivyo Tutafanya kwa wale wanaofanana nao.

﴿١٠٢﴾ إِنَّ أَخْذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ

**“Hakika Mkamoto Wake ni mchungu na mkali.”**

Imekuja katika Sahihi Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Mussa رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ اللَّهَ لَيُنْبِئِي لِلظَّالِمِ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يُفْلِتْهُ»

**“Hakika Mwenyezi Mungu Anamchelewesha dhalimu mpaka Akimkamata hamponyoki”.**<sup>1</sup>

Kisha Mtume ﷺ akasoma:

وَكَذَلِكَ أَخْذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ

**“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi Anapoikamata miji inapo kuwa imedhulumu.”**

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّمَن خَافَ عَذَابَ الْآخِرَةِ ۗ ذَلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَّهُ النَّاسُ وَذَلِكَ يَوْمٌ

مَشْهُودٌ ﴿١٠٣﴾ وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مَّعْدُودٍ ﴿١٠٤﴾ يَوْمَ يَأْتِ لَا تَكَلِّمُنَّ نَفْسٌ إِلَّا

بِإِذْنِهِ ۗ فَمَنْهُمْ شَاقِقٌ وَسَعِيدٌ ﴿١٠٥﴾

**103. Hakika katika haya ipo ishara kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo Siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayoshuhudiwa.**

<sup>1</sup> Fat'hu all-Bari 8/205, na Muslim 4/1997.

**104. Na Sisi Hatuiakhirishi ila kwa muda unaohisabiwa.**

**105. Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa Idhini Yake Mwenyezi Mungu. Kati yao watakuwamo waliomo mashakani na wenye furaha.**

### Kuangamizwa kwa Miji ni Dalili ya Kusimama Kiyama

Allah تعالى Anasema: Hakika katika Kuwaangamiza Kwetu makafiri na Kuwaokoa Kwetu waumini,

لَايَةٌ

**“ipo ishara”** Maana yake: Maonyo na mazingatio juu ya ukweli wa Tunayoyaahidi huko akhera.

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

**“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi.” (40:51)** Na Allah تعالى Amesema:

فَأَوْحَىٰ إِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ لَنُهَلِكَنَّ الظَّالِمِينَ ﴿١٣﴾

**“Akawafunulia kwao kuwa Tutawaangamiza madhalimu.” (14:13),**

ذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَّهُ النَّاسُ

**“Hiyo ndiyo Siku itakayokusanyiwa watu...”**, Maana yake: Wa mwanzo na wa mwisho wao, kama ilivyo Kauli ya Allah تعالى,

وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾

**“Na Tukawafufua na hatukuacha miongoni mwao yoyote.” (18:47)**

وَذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُودٌ ﴿٥٧﴾

**“...na hiyo ndiyo Siku itakayoshuhudiwa.”** Maana yake: Siku kubwa itahudhuriwa na Malaika, na Mitume watakusanyika katika siku hiyo, na viumbe wote watakusanywa, miongoni mwa watu, majini, ndege, wanyama na wadudu, na Atahukumu ndani yake Muadilifu Ambaye:

وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مُّعَدَّدٍ ﴿٣٨﴾

**“Na Hatuicheleweshi isipokuwa kwa muda maalumu...”**

Maana yake: Kwa muda uliyowekwa hapaongezwi juu yake wala haupunguzwi.

Na Kauli Yake: **يَوْمَ يَأْتُ لَا تَكَلَّمُ نَفْسٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ**

**“Siku hiyo itakapofika, hatosema hata mtu mmoja ila kwa Idhini Yake”**

Maana yake: Siku ambayo kitapokuja Kiyama hatazungumza mtu yoyote isipokuwa kwa idhini ya Allah تعالیٰ, kama ilivyo katika Kauli Yake:

لَا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أَذِنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٩﴾

**“...Hawatasema ila Mwingi wa Rehema Aliyemruhusu, na atasema yaliyo sawa tu.” (78:38)**

وَحَشَعَتِ الْأَصْوَاتُ لِلرَّحْمَنِ

**“Na sauti zote zitamnyenyekea Arrahmani Mwingi wa Rehema.” (20:108)**

Imekuja katika Sahihi Bukhari na Muslim katika Hadithi ya maombezi:

«وَلَا يَتَكَلَّمُ بِؤْمِنِيذٍ إِلَّا الرُّسُلُ، وَدَعْوَى الرُّسُلِ بِؤْمِنِيذِ اللَّهِ! سَلِّمْ سَلِّمْ»

**“Na wala hawatasema siku hiyo isipokuwa Mitume, na dua ya mitume siku hiyo ni Ee! Mola, salimisha, salimisha.”<sup>1</sup>**

Na Kauli Yake: **فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَسَعِيدٌ ﴿٤٠﴾**

**“Kati yao watakuwamo waliomo mashakani na wenye furaha.”**

Hii inamaanisha siku hiyo ya mkusanyiko wa watu (siku ya Kiyama) kuna watakaokuwa na huzuni na kuna watakaofurahi.

فَرِيقٌ فِي الْجَنَّةِ وَفَرِيقٌ فِي السَّعِيرِ ﴿٤١﴾

**“Kundi moja litakuwa Peponi, na kundi jengine Motoni.” (42:7)**

<sup>1</sup> Fat'hul al-Bari 2/341, na Muslim 2/169.

Al-Hafidhi Abuu Ya'ala, amenukuu katika kitabu chake kutoka kwa Ibn Umar kutokana na Umar رضي الله عنه amesema: Ilipotemka ayah hii:

فَمِنْهُمْ شَقِيٌّ وَسَعِيدٌ ﴿١٠٦﴾

**“Kati yao watakuwamo waliomo mashakani na wenye furaha.”**

Nilimuuliza Mtume ﷺ nikasema: ‘Ewe Mtume, patakuwa na ishara ya kutujulisha (tuko katika pote lipi). Je itakuwa ni kutokana na jambo alilolifanya mtu, au jambo ambalo aliacha kulifanya?’ Akasema:

«عَلَىٰ شَيْءٍ قَدْ فُرغَ مِنْهُ يَا عُمَرُ! وَجَرَتْ بِهِ الْأَقْلَامُ، وَلَكِنْ كُلُّ مُبَسَّرٍ لِمَا خُلِقَ لَهُ»

*“Juu ya jambo ambalo limeshahitimishwa Ewe ‘Umar na kalamu zimethibitisha isipokuwa kila mmoja amerahisishiwa lile ambalo ameumbiwa nalo.”<sup>1</sup>*

Kisha Allah تعالى Amebainisha hali ya waovu na hali ya wema, kwa Kusema:

فَأَمَّا الَّذِينَ شَقُوا فِي النَّارِ هُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَشَهِيقٌ ﴿١٠٧﴾ خَالِدِينَ فِيهَا مَا دَامَتِ

السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ إِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيدُ ﴿١٠٨﴾

**106. Ama wale wa mashakani hao watakuwamo Motoni wakiyayatika na kukoroma.**

**107. Watadumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipo kuwa Apendavyo Mola wako Mlezi. Hakika Mola wako Mlezi Hutenda Apendavyo.**

**Hali ya Waovu na Hatima Yao**

Allah تعالى Anasema:

هُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَشَهِيقٌ ﴿١٠٧﴾

**“Motoni wakiyayatika na kukoroma.”**

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما : *Zafiir*, ni sehemu katika koo; na *Shahiiq*: ni katika kifua, yaani kupumua kwao ni *Zafiir*, na kuchukuliwa nafsi zao ni *Shahiiq*.<sup>2</sup> Hii ni kutokana na adhabu inayowasibu.

<sup>1</sup> Tirmidhy 3111.

<sup>2</sup> Tabari 15/480.



Tunajilinda na adhabu hiyo,

خَلْدِيْنَ فِيْهَا مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ

**“Watadumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi,”**

Amesema Imamu Abuu Ja`afar Bin Jariri رحمه الله تعالى ni katika utaratibu wa Waarabu wanapotaka kulisifia jambo kwa kudumu milele wanasema: “Jambo hili litadumu kudumu kwa mbingu na ardhi’. Kadhalika wanasema: ‘Jambo hili litabaki kwa muda wa kupishana kwa usiku na mchana’, ‘Na muda wakeshapo wazungumzao usiku kucha’, ‘Na muda wanyama watikisapo masikio yao’, Misemo yote hiyo humaanisha, milele. Kwa hiyo, Allah تعالى Ambaye Zimetukuka Sifa Zake Amewasemesha, kwa matamshi ambayo huelewa baina yao, Akisema:

خَلْدِيْنَ فِيْهَا مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ

**“Watadumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi.”**

Ninasema: Inawezekana kuwa makusudio ya muda wa kudumu mbingu na ardhi ni uanishaji tu, kwa sababu hapana budi katika ulimwengu wa akhera kuwepo kwa mbingu na ardhi, kama Alivyosema Allah تعالى:

يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ

**“Siku zitakapobadilishwa mbingu na ardhi...” (14:48)**

Na kwa ajili hiyo amesema Al-Hassanul-Basry رحمه الله تعالى katika Kauli Yake,

مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ

**“Muda wa kudumu mbingu na ardhi,...”**

Amesema: Mbingu zisizokuwa mbingu hizi na ardhi isiyokuwa ardhi hii, kwa hiyo muda wa kudumu mbingu hiyo na ardhi hiyo.

Na Kauli Yake,

إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ إِنَّ رَبَّكَ فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيدُ

**“...isipokuwa apendavyo Mola wako Mlezi. Hakika Mola wako Mlezi Hutenda Apendavyo.”**

<sup>1</sup> Tabari 15/481.

Maneno hayo ni kama maneno yake:

﴿١٢٨﴾ أَلْتَأْتُونَكُمْ خَلِيدِينَ فِيهَا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ

***“Moto ndiyo makazi yao watakaa milele humo, isipokuwa kile Atakachokitaka Mwenyezi Mungu hakika Bwana wako ni Mwenye Hekima sana Mjuzi mno...” (6:128).***

Imesemwa: Hakika kutolewa motoni ni kwa wenye kuasi, miongoni mwa watu wa kumpwekesha Allah تعالى, katika wale ambao Atawatoa Allah تعالى motoni kwa maombezi ya wenye kuombea, miongoni mwa Malaika, Mitume na waumini. Hadi mpaka watawaombea wenye madhambi makubwa kisha itakuja Rehema ya Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu, itamtoa motoni yule ambaye hakufanya kheri kabisa, ambaye alisema siku moja tu katika zama: *“Hapana Mola anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu.”* Kama zilivyokuja katika hilo Hadithi Sahihi, ambazo zimepokewa kwa wingi kutoka kwa Mtume ﷺ zenye madhumuni hayo. Katika Hadithi za Anas, Jabir, Abu Saeed, Abu Huraira na wengine رضي الله عنهم miongoni mwa maswahaba. Na wala hatabakia motoni baada ya hapo isipokuwa yule ambaye imepasa juu yake kukaa humo milele, na wala hana namna ya kuepukana nao. Rai hii ndiyo ambayo wanawazuoni wengi wa zamani na wa sasa wameitolea hukumu juu yake, katika kuifasiri aya hii tukufu,

﴿١٠٨﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ سَعِدُوا فَبِئْسَ الْجَنَّةِ خَلِيدِينَ فِيهَا مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ إِلَّا مَا شَاءَ

رَبُّكَ عَطَاءٌ غَيْرَ مَجْدُودٍ ﴿١٠٨﴾

***108. Na ama wale waliobahatika, wao watakuwamo Peponi wakidumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipokuwa Apendavyo Mola wako Mlezi. Hicho ni kipawa kisio na ukomo.***

**Hali ya Watu Wema na Hatima Yao**

Allah تعالى Anasema: ﴿١٠٨﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ سَعِدُوا

***“Na ama wale waliobahatika,...”*** Hao ni wafuasi wa Mitume,

﴿١٠٨﴾ فَبِئْسَ الْجَنَّةِ

***“watakuwamo Peponi,...”*** Maana yake: makazi yao ni Peponi,

خَلِيدِينَ فِيهَا

“...*wakidumu humo*,...” Maana yake: Watakaa humo milele,

مَا دَامَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ إِلَّا مَا شَاءَ رَبُّكَ

**“Muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipokuwa Apendavyo Mola wako Mlezi...”**

Maana ya kuwachuja hapa ni kwamba, kudumu kwao katika yale ambayo wao wamo ndani yake miongoni mwa neema, hali kuwa jambo lenye kupasa kwa dhati yake, bali hilo limeegemezwa kwenye matakwa ya Allah تعالى. Kwa hiyo ni haki Yake Kuwaneemesha wao wakati wote, na kwa sababu hiyo wanafahamishwa kumtakasa na kumsifu kama wanavyofahamishwa kupumua<sup>1</sup>. Addhahak na Al-Hassanul-Basry wamesema: hilo ni katika haki ya wenye kuasi, wenye kumpwekesha Allah تعالى ambao walikuwa motoni kisha wakatolewa humo baada ya hapo. Kwa Kauli Yake,

عَطَاءٌ غَيْرَ مَجْدُودٍ

**“Hicho ni kipawa kisio na ukomo.”**

Maana yake: Kisichokatwa, ameyasema hayo Mujahidi, Ibn Abbas na Abul-Aalya, na wengine<sup>2</sup>. Ili asije akadhania mwenye kudhania, baada ya kutaja kwake *matakwa*, kwamba kuna kukatika au kutatiza au kitu chochote, bali Amewajibisha kuwa jambo hilo ni la kudumu na la kutokatika. Kama Alivyobainisha hapa kwamba, adhabu ya watu wa motoni ndani ya moto itakuwa ya kudumu, inarudishwa kwenye Matakwa Yake, na kwamba Yeye kwa Uadilifu na Hekima Yake, Amewaadhibu na kwa sababu hiyo Amesema:

إِنَّ رَبَّكَ فَعَالٌ لِّمَا يُرِيدُ

**“Hakika mola wako Anafanya Atakalo...”**

Kama Alivyosema:

لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ

**“Haulizwi alifanyalo wao wanaulizwa.” (21:23)**

<sup>1</sup> Muslimu 4/2181.

<sup>2</sup> Tabari 15490.

Kwa hiyo hapa nyoyo zimeburudika na makusudio yamepatikana kwa Kauli Yake,

عَطَاءٌ غَيْرَ مَجْدُوذٍ ﴿١٠٨﴾

**“Hicho ni kipawa kisio na ukomo,...”**

Imekuja katika sahihi mbili:

«يُؤْتَى بِالْمَوْتِ فِي صُورَةٍ كَبِشٍ أَمْلَحَ فَيَذْبَحُ بَيْنَ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ، ثُمَّ يُقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ! خُلُودٌ فَلَا مَوْتَ، وَيَا أَهْلَ النَّارِ! خُلُودٌ فَلَا مَوْتَ»

*“Yataletwa mauti siku ya kiama katika sura ya kondoo aliyenona, atachinjwa baina ya pepo na moto kisha kutasemwa: “Enyi watu wa peponi, mtakaa humo milele bila kufa, na nyie watu wa motoni mtakaa humo milele bila kufa.”<sup>1</sup>*

Na katika sahihi vilevile: kutasemwa:

«فَيَقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ! إِنَّ لَكُمْ أَنْ تَعِيشُوا فَلَا تَمُوتُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تَسِيبُوا فَلَا تَهْزَمُوا تَسْقَمُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تَصِحُّوا فَلَا تَنْعَمُوا فَلَا تَبْأَسُوا أَبَدًا»

*“Enyi watu wa peponi mtaishi milele wala hamtakufa, na nyinyi mtakuwa vijana na hamtazeeka milele, na kwamba mtakuwa na afya hamtaugua milele, na kuwa mtastarehe, hamtapata tabu milele”<sup>2</sup>*

\* \* \*

<sup>1</sup> Fat’hul Bari 8/282, na Muslim 4/2188.

<sup>2</sup> Muslimu 4/2182.

فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّمَّا يَعْبُدُ هَتُولَاءِ ۚ مَا يَعْبُدُونَ إِلَّا كَمَا  
يَعْبُدُ ءَابَاؤُهُمْ مِّن قَبْلُ ۗ وَإِنَّا لَمُوفُونَ ۚ نَصَبْنَاهُمْ غَيْرَ  
مَنْقُوصٍ ۗ ۝۱۰۹ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَآخْتَلَفَ فِيهِ  
ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ۚ وَإِنَّهُمْ لَفِي  
شَكٍّ مِّنْهُ مُرِيبٍ ۗ ۝۱۱۰ وَإِنَّ كُلًّا لَّمَّا لَيُؤْفِقِينَ رَبِّكَ  
أَعْمَلَهُمْ ۚ إِنَّهُمْ بِمَا يَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ۗ ۝۱۱۱ فَاسْتَقَمَ كَمَا  
أُمِرْتَ وَمَن تَابَ مَعَكَ وَلَا تَطْغَوْا ۚ إِنَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ  
بَصِيرٌ ۗ ۝۱۱۲ وَلَا تَزْكُتُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَمَا تَمْسِكُمُ النَّارُ  
وَمَا لَكُم مِّن دُونِ اللَّهِ مِن أَوْلِيَاءِ تُرْمَلُونَ ۗ ۝۱۱۳  
وَأَقْرِ الصَّلَاةَ طَرَفِي الْبَهَارِ وَزُلْفَا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ إِنَّ أَحْسَنْتَ  
يُذْهِبْنَ السَّيِّئَاتِ ۚ ذَلِكَ ذِكْرِي لِلذَّاكِرِينَ ۗ ۝۱۱۴ وَأَصْبِرْ  
فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ۗ ۝۱۱۵

فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّمَّا يَعْبُدُ هَتُولَاءِ ۚ  
مَا يَعْبُدُونَ إِلَّا كَمَا يَعْبُدُ  
ءَابَاؤُهُمْ مِّن قَبْلُ ۗ وَإِنَّا لَمُوفُونَ  
نَصَبْنَاهُمْ غَيْرَ مَنْقُوصٍ ۗ ۝۱۰۹  
وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ فَآخْتَلَفَ  
فِيهِ ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ  
لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ۚ وَإِنَّهُمْ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ  
مُرِيبٍ ۗ ۝۱۱۰ وَإِنَّ كُلًّا لَّمَّا لَيُؤْفِقِينَ  
رَبِّكَ أَعْمَلَهُمْ ۚ إِنَّهُمْ بِمَا يَعْمَلُونَ  
خَبِيرٌ ۗ ۝۱۱۱

109. Basi usiwe na shaka juu ya wanayoyaabudu hao. Hawaabudu ila kama walivyoabudu baba zao

zamani. Na hakika Sisi Tutawatimilizia fungu lao bila ya kupunguzwa.

110. Na kwa yakini Tulimpa Musa Kitabu; zikazuka khitilafu ndani yake. Na lau kuwa si neno lililokwishatangulia kutoka kwa Mola wako Mlezi, bila ya shaka ingelihukumiwa baina yao. Na hakika wao wamo katika shaka juu yake inayo wahangaisha.

111. Na hakika Mola wako Mlezi Atawatimilizia malipo ya vitendo vyao. Hakika Yeye Anayo khabari ya wayatendayo.

## Kumshirikisha Allah تعالی ni Upotevu Usio na Shaka Ndani Yake

Allah تعالی Anasema:

فَلَا تَكُ فِي مِرْيَةٍ مِّمَّا يَعْبُدُ هَتُولًا ۚ

**“Basi usiwe na shaka juu ya wanayoyaabudu hao,...”**

Maana yake: Washirikina, kwani kumshirikisha Allah تعالی ni batili, ujinga na upotevu, kwa kuwa wao, wanaabudu ambavyo vimeabudiwa na baba zao huko nyuma. Maana yake: wao hawana ushahidi katika lile ambalo wao wamo ndani yake, isipokuwa kufuata wazazi wao katika mambo ya ujinga, na Allah تعالی Atawalipa wao juu ya hayo malipo yaliyo kamili, na Atawaadhibu adhabu ambayo Haadhibu adhabu hiyo yeyote, na ikiwa wana mema, kwa hakika Allah تعالی Amekwishawalipa wao katika dunia kabla ya akhera. Na Kauli Yake,

وَإِنَّا لَمُوفُونَ مِمَّا نَصَبْتُمْ غَيْرَ مَنقُوصٍ ﴿١٠٩﴾

**“Na hakika Sisi Tutawatimilizia fungu lao bila ya kupunguzwa.”**

Abdul Rahman Ibn Zaid Bin Aslam amesema: Tutawalipa kwa ukamilifu fungu lao katika adhabu, bila kupunguzwa<sup>1</sup>. Kisha Allah تعالی Ametaja kwamba Yeye Amempa Musa عليه السلام kitabu, watu wakatofautiana ndani yake, kuna waliokiamini na kuna waliokikufuru. Kwa hiyo wewe una kigezo kutokana na wale waliotangulia kabla yako miongoni mwa Mitume, Ee Muhammad ﷺ, kwa hiyo kukadhibisha kwao kusikuchukize na hilo lisikufadhaishe.

وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ۚ

**“Na lau kuwa si neno lilokwishatangulia kutoka kwa Mola wako Mlezi, bila ya shaka ingelihukumiwa baina yao.”**

Ibn Jariri رحمه الله تعالی amesema: Lau si yale ambayo yametangulia kwa kucheleweshewa kwake adhabu mpaka muda maalumu, Allah تعالی Angehukumu baina yao. Na inawezekana kuwa makusudio ya maneno ni kwamba Hamuadhibu yeyote isipokuwa baada ya kusimama hoja juu yake, na kumpelekea Mjumbe<sup>2</sup>, kama Alivyosema:

<sup>1</sup> Tabari 15/492.

<sup>2</sup> Tabari 15/493.

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ تَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٠٩﴾

**“Na hatukuwa wenye kuadhibu mpaka Tumepeleka Mjumbe.” (17:15)**

Allah تعالیٰ Amesema katika aya nyingine.

وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ لَكَانَ لِزَامًا وَأَجَلٌ مُّسَبًّى ﴿١١٠﴾ فَاصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ  
وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ غُرُوبِهَا ۖ وَمِنْ أَثَارِ اللَّيْلِ فَسَبِّحْ وَأَطْرَافَ  
النَّهَارِ لَعَلَّكَ تَرْضَىٰ ﴿١١١﴾

**“Lau si maneno yaliyotangulia kutoka kwa Bwana wako kungekuwa kuangamizwa ni kwenye kuwalazimu hapa duniani na muda uliyowekwa kwao, kwa hiyo subiri juu ya yale wanayoyasema.” (20:129-130)**

Kisha Allah تعالیٰ Ameeleza kwamba: Yeye Atawakusanya watu wa mwanzo na wa mwisho katika umati mbalimbali, na Atawalipa kutokana na matendo yao yakiwa mema watalipwa wema na yakiwa maovu watalipwa uovu. Kwa hiyo Amesema:

وَإِنْ كُلاًّ لَّمَّا لِيُوقِيَهُمْ رَبُّكَ أَعْمَلَهُمْ ۗ إِنَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١١٢﴾

**“Na hakika Mola wako Mlezi Atawatimilizia malipo ya vitendo vyao. Hakika Yeye Anayo khabari ya wayatendayo,”**

Maana yake: Anajuwa sana matendo yao yote, matukufu yake na duni, makubwa na madogo yake. Katika aya hii kuna visomo vingi, maana zake zinarejea kwenye hayo ambayo tumeyataja, kama ilivyo katika Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَإِنْ كُلٌّ لَّمَّا جَمِيعٌ لَدَيْنَا مُحْضَرُونَ ﴿١١٣﴾

**“Na hakika wote wao juu Yake watahudhurishwa.” (36:32)**

فَأَسْتَقِمْ كَمَا أُمِرْتَ وَمَنْ تَابَ مَعَكَ وَلَا تَطْغَوْا ۗ إِنَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١١٤﴾ وَلَا  
تَرْكَبُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا فَتَمَسَّكُمْ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ثُمَّ لَا  
تُنصَرُونَ ﴿١١٥﴾

**112. Basi, simama sawasawa kama ulivyoamrishwa, wewe na wale wanaoelekea kwa Mwenyezi Mungu pamoja nawe; wala msikiuke mipaka. Hakika Yeye Anayaona yote myatendayo.**

**113. Wala msiwategemee wanaodhulumu, usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa.**

### **Amri ya Kusimama Thabiti Katika Njia Iliyonyooka**

Allah تعالی Anamuamrisha Mtume wake ﷺ na waja wake, waumini kuthibiti na kudumu juu ya msimamo. Na hilo ni katika msaada mkubwa sana juu ya kupata ushindi dhidi ya maadui, na kupinga ubaya, na Allah تعالی Amekataza kupetuka mpaka, kwani kufanya hivyo ni uhalifu, hata kama anayefanyiwa uhalifu huo ni mtu mshirikina. Allah تعالی Amefahamisha kwamba Yeye Anaona sana matendo ya waja, na wala Haghafiliki na kitu chochote, na Kwake hakuna kinachojificha. Kauli Yake:

وَلَا تَرْكُنُوا إِلَى الَّذِينَ ظَلَمُوا

**“Wala msiwategemee wanaodhulumu,...”**

Amesema Ali Bin Abii Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه: Msiwafanyie ulaini. Na amesema Ibn Jariri رحمه الله تعالی kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه: Msipondokee kwa wale ambao wamedhulumu;<sup>1</sup> na kauli hii ni *Hasan*. Maana yake: Msitake msaada kwa wale ambao wamedhulumu, kwani mtakuwa kana kwamba mmeyaridhia matendo yao.

فَتَمَسَّكُمُ النَّارُ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِنْ أَوْلِيَاءَ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ ﴿١١٣﴾

**“...Usije ukakuguseni Moto. Wala nyinyi hamna walinzi badala ya Mwenyezi Mungu, wala tena hamtasaidiwa.”**

Maana yake: Nyinyi hamna msaidizi asiyekuwa Yeye atakayekuoeni, wala mnusuru atakaye kunusuruni, na pia atakayewavua na adhabu Yake.

<sup>1</sup> Tabari 15/501.



وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفِي النَّهَارِ وَزُلْفًا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ إِنَّ أَحْسَنَتِ يُدْهِمِنَ السَّيِّئَاتِ ۚ ذَٰلِكَ ذِكْرِي  
لِلذَّاكِرِينَ ۝ وَأَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ۝

**114. Na shika Sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizokaribu na mchana. Hakika mema huondoa maovu. Huu ni ukumbusho kwa wanaokumbuka.**

**115. Na subiri, kwani Mwenyezi Mungu Hapotezi ujira wa wanaofanya wema.**

### Amri ya Kusimamisha Sala

Amesema Aly Bin Abii Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما:

وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفِي النَّهَارِ

**“Na shika Sala katika ncha mbili za mchana...”**

Amesema anakusudia asubuhi na magharibi<sup>1</sup>. Na kama hivyo amesema Al-Hassan na Abdurahman Bin Zaid Bin Aslam<sup>2</sup>. Amesema Al-Hassan katika upokezi wa Qatada na Dhahaak na wengine: Ni asubuhi na Al-Asri, amesema Mujahid: Ni asubuhi mwanzoni mwa mchana na adhuhuri na alasri mwisho wake. Na kama hivyo, amesema Muhammad Bin Kaab, Al-Quradhy na Adh-Dhahaak katika mapokezi kutoka kwake.

وَزُلْفًا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ

**“...na nyakati za usiku.”**

Amesema Ibn Abbas na Mujahid na Hassan na wengine: Anakusudia Sala ya Isha. Hassan amesema katika mapokezi ya Ibn Mubaarak kutokana na Mubarak Bin Fadhalah kutokana naye:

وَزُلْفًا مِّنَ اللَّيْلِ ۚ

**“...na nyakati za usiku.”** Anakusudia Magharibi na Isha. Mtume ﷺ amesema,

<sup>1</sup> Tabari 15/503.

<sup>2</sup> Tabari 15/503.

«هُمَا زُلْفَا اللَّيْلِ : الْمَغْرِبُ وَالْعِشَاءُ»

*“Hizo ni nyakati mbili za usiku: Magharibi na Isha.”*

Na kama hivyo amesema Mujahid, Muhammad Ibn Kaab, Qatada na Adh-Dhahaak: Hakika masaa hayo ni Sala ya Magharibi na Isha. Na huenda ikawa kushuka kwa aya hii kulikuwa kabla ya kufaradhihwa Sala tano katika usiku wa Israai, kwani ilikuwa inapasa Sala mbili tu. Sala kabla ya kuchomoza jua na Sala kabla ya kuzama kwake. Na katikati ya usiku ni kisimamo, juu yake Mtume ﷺ na juu ya umma wake. Kisha kikafutwa katika haki ya umma wake, na ukathibiti wajibu juu yake, kisha na yeye akafutiwa pia, katika Kauli nyingine. Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi

### Mema Yanafuta Maovu

Kauli Yake,

إِنَّ الْحَسَنَاتِ يُذْهِبْنَ أَلْسَفَاتِ

*“Hakika mema huondoa maovu.”*

Anasema: Hakika kufanya mema hufuta madhambi yaliyotangulia, kama ilivyokuja katika Hadithi ambayo ameipokea Imamu Ahmad na watu wa Sunan kutoka kwa kiongozi wa waumini Ali Bin Abii Talib رضي الله عنه kuwa amesema: Nilikuwa nikisikia kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa Allah تعالى Huninufaisha mimi kwa Analolitaka Kuninufaisha nalo, na mtu yeyote anaponihadithia kutoka kwa Mtume ﷺ, humtaka aape na akiniapia ninamsadikisha. Na Abubakar رضي الله عنه akanihadithia, na amesema kweli Abubakar رضي الله عنه, kwamba yeye amemsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَا مِنْ مُسْلِمٍ يُذِيبُ ذَنْبًا فَيَتَوَضَّأُ وَيُصَلِّي رَكَعَتَيْنِ إِلَّا عُفِرَ لَهُ»

*“Hapana Muislamu yoyote anayefanya makosa akatawadha na akasali raka mbili isipokuwa atasamehewa.”<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 1/9, na Abuu Dawuud 2/180. na Tuhfatul- Ahwahdy 8/357. na Nasaai katika Alkubraa 6/109. na Ibnu Maajah 1/446.

Na imekuja katika sahihi mbili kutoka kwa kiongozi wa waumini Uthman Bin Affaan رضي الله عنه, kwamba yeye alitawadha kama alivyotawadha Mtume ﷺ kisha akasema: 'kama hivi nilimuona Mtume ﷺ anatawadha.'

Kisha akasema tena:

«مَنْ تَوَضَّأَ وَضُوءِي هَذَا ثُمَّ صَلَّى رَكْعَتَيْنِ لَا يُحَدِّثُ فِيهِمَا نَفْسَهُ غَيْرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ  
ذَنْبِهِ»

*"Mwenye kutawadha kama kutawadha kwangu huku, kisha akasali raka mbili haimuzungumzishi ndani ya raka mbili hizo nafsi yake, husamehewa madhambi yake yaliyotangulia."*<sup>1</sup>

Na imekuja katika Sahihi za Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ,

«أَرَأَيْتُمْ لَوْ أَنَّ بَابَ أَحَدِكُمْ نَهْرًا غَمْرًا، يَغْتَسِلُ فِيهِ كُلَّ يَوْمٍ خَمْسَ مَرَّاتٍ، هَلْ يُبْقِي  
مِنْ دَرَرِهِ شَيْئًا؟»

*"Je mnaonaje lau katika mlango wa mmoja wenu kuna mto wenye maji mengi, anaoga katika mto huo, kila siku mara tano, je kitabaki kitu katika uchafu wake?"*

Wakasema: 'Hapana Ee Mtume ﷺ.' Akasema:

«كَذَلِكَ الصَّلَاةُ الْخَمْسُ يَمْحُو اللَّهُ بِهِنَّ الذُّنُوبَ وَالْخَطَايَا»

*"Ni hivyo hivyo Sala tano Anafuta Mwenyezi Mungu kwa Sala hizo madhambi na makosa."*<sup>2</sup>

Na amepokea Muslim katika Sahihi yake kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kwamba, Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«الصَّلَاةُ الْخَمْسُ، وَالْجُمُعَةُ إِلَى الْجُمُعَةِ، وَرَمَضَانَ إِلَى رَمَضَانَ، مُكْفَرَاتٌ لِمَا  
بَيْنَهُنَّ مَا اجْتَنِبْتَ الْكَبَائِرُ»

<sup>1</sup> Fat'hul Bari 1/320.

<sup>2</sup> Bukhary 528, na Muslim 667.

*“Sala tano, na Ijumaa mpaka Ijumaa nyingine, na Ramadhani mpaka Ramadhani nyingine, hufuta madhambi yaliyo kati yao, pindi yatakapoepukwa madhambi makubwa.”<sup>1</sup>*

Na Bukhari amepokea kutoka kwa Ibn Mas‘uud رضى الله عنه kwamba, mtu mmoja alim-busu mwanamke, akamuendea Mtume ﷺ akamueleza, Allah تعالى Akateremsha,

وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفِي النَّهَارِ وَزُلْفَا مِنْ اللَّيْلِ إِنَّ أَحْسَنْتَ يُذْهِبَنَّ السَّيِّئَاتِ

***“Na shika Sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizokaribu na mchana. Hakika mema huondoa maovu.” (11:114)***

Mtu yule akasema: ‘Ee Mtume ﷺ Je ujumbe huu ni wangu mimi tu?’ Akasema:

«لِجَمِيعِ أُمَّتِي كُلِّهِمْ»

*“Ni wa umati wangu wote.”<sup>2</sup>*

Kama hivi amenukuu Imamu Bukhary katika kitabu cha Sala na akabainisha katika tafsiri kwa mfano wake<sup>3</sup>.

Na Imamu Ahmad amepokea kutoka kwa Ibni Abbas رضى الله عنهما kwamba mtu mmoja alimuendea Umar رضى الله عنه akasema: ‘Kwa hakika mwanamke mmoja alikuja akiwa anataka kununua kitu, nikamwingiza katika mfereji nikamfanya tendo lisilokuwa la kuingilia.’ Akasema: ‘Ole wako, huenda akawa amepotea katika njia ya Allah تعالى.’ Akasema: ‘Ndiyo.’ Akasema: ‘Muendee Abubakri رضى الله عنه muulize.’ Amesema: ‘Akamuendea akamuuliza.’ akasema: ‘Huenda akawa amepotea katika njia ya Allah?’ Akasema mfano wa yale aliyoyasema Umar رضى الله عنه. Kisha akamuendea Mtume ﷺ akamuambia mfano wa hayo akasema:

«فَلَعَلَّهَا مُنِيَّةً فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

*“Huenda akawa amepotea katika njia ya Mwenyezi Mungu.”*

<sup>1</sup> Muslim 1/209.

<sup>2</sup> Fat’hul Bari 2/12.

<sup>3</sup> Fat’hul- Bari 8/206.

Ikashuka Qur'an,

وَأَقِمِ الصَّلَاةَ طَرَفِي النَّهَارِ وَزُلْفَا مِنْ اللَّيْلِ إِنَّ الْحَسَنَاتِ يُذْهِبْنَ السَّيِّئَاتِ

***“Na shika Sala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizokaribu na mchana. Hakika mema huondoa maovu.”***

Akasema: ‘Ee Mjumbe ﷺ msamaha huo ni wangu mimi tu au wa watu wote?’ Umar رضي الله عنه akapiga kifua chake kwa mkono wake na akasema: ‘Hapana, faida hii si ya peke yako! Bali msamaha huo ni kwa ajili ya watu wote.’ Mtume ﷺ akasema:

«صَدَقَ عُمَرُ»

*“Umar Amesema kweli”<sup>1</sup>*

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ahmad 1/245.

فَلَوْلَا كَانَ مِنَ الْقُرُونِ مِن قَبْلِكُمْ  
 أُولُوا بَقِيَّةَ يَهُودَ عَنِ الْفَسَادِ فِي  
 الْأَرْضِ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّنْ أُجِيبْنَا مِنْهُمْ  
 الَّذِينَ ظَلَمُوا مَا أَتَرَفُوا فِيهِ وَكَانُوا  
 مُجْرِمِينَ ﴿١١٦﴾ وَمَا كَانَ رَبُّكَ  
 لِيُهْلِكَ الْقُرَى بِظُلْمٍ وَأَهْلِهَا  
 مُصْلِحُونَ ﴿١١٧﴾ وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ  
 النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَا يَزَالُونَ  
 مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٨﴾ إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ  
 وَلِذَلِكَ خَلَقَهُمْ وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ  
 لِأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ  
 الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٩﴾ وَكُلًّا  
 نَقَّصُ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِ  
 الرُّسُلِ مَا نُنْتِثُ بِهِ فُؤَادَكَ ۗ وَجَاءَكَ فِي  
 هَذِهِ الْحَقِّ وَمَوْعِظَةٌ وَذِكْرَى  
 لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٠﴾ وَقُلْ لِلَّذِينَ لَا  
 يُؤْمِنُونَ أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ  
 إِنَّا عَمِلُونَ ﴿١٢١﴾ وَانْتَظِرُوا إِنَّا  
 مُنْتَظِرُونَ ﴿١٢٢﴾ وَاللَّهُ غَيْبُ  
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَيْهِ  
 يُرْجَعُ الْأُمُورُ كُلُّهُ ۖ فَاعْبُدْهُ  
 وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ۗ وَمَا رَبُّكَ  
 بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٢٣﴾

فَلَوْلَا كَانَ مِنَ الْقُرُونِ مِن قَبْلِكُمْ  
 أُولُوا بَقِيَّةَ يَهُودَ عَنِ الْفَسَادِ فِي  
 الْأَرْضِ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّنْ أُجِيبْنَا مِنْهُمْ  
 الَّذِينَ ظَلَمُوا مَا أَتَرَفُوا فِيهِ  
 وَكَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿١١٦﴾ وَمَا كَانَ  
 رَبُّكَ لِيُهْلِكَ الْقُرَى بِظُلْمٍ وَأَهْلِهَا  
 مُصْلِحُونَ ﴿١١٧﴾

**116. Basi mbona hawa-  
 kuwamo katika watu wa  
 kabla yenu wenye vyeo na  
 wasaa wanaokataza uhari-  
 bifu katika nchi, isipokuwa  
 wachache tu, ambao ndio  
 Tuliowaokoa? Na walio-  
 dhulumu walifuata starehe  
 zao, na wakawa ni wako-  
 sefu.**

**117. Wala hakuwa Mola  
 wako Mlezi wa kuihiliki miji**

**kwa dhulma tu na hali watu wake ni watenda mema.**

### Hapana Budi Liwepo Kundi Linalokataza Machafu

Allah تعالیٰ Anasema: 'Kwa nini yasipatikane kutokana na karne zilizopita mabaki katika watu wa kheri? Wanakataza Yaliyokuwa Yanatuka kati yao, miongoni mwa shari na mambo machafu, na uharibifu katika ardhi?'

إِلَّا قَلِيلًا

"...isipokuwa wachache tu..."

Maana yake: Walipatikana miongoni mwao, kutokana na aina hii, wachache, hawakuwa wengi na hao ndiyo ambao Allah تعالى Aliwaokoa wakati wa kushuka ghadhabu Yake na kuja mateso Yake kwa ghafla. Na kwa sababu hii Allah تعالى Ameuamrisha umma huu, Mtukufu kupatikana ndani yake watu ambao wataamrisha mema na watakataza maovu, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ

الْمُقْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

***“Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania kheri na unaoamrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio waliofanikiwa.”(3:104)***

Na imekuja katika Hadithi:

«إِنَّ النَّاسَ إِذَا رَأَوْا الْمُنْكَرَ فَلَمْ يُغَيِّرُوهُ أَوْشَكَ أَنْ يَعْصِمَهُمُ اللَّهُ بِعِقَابٍ»

*“Kwa hakika watu watakapoliona jambo baya kisha wasilikataze Mwenyezi Mungu Anakaribia Kuwaenezea wao adhabu.”<sup>1</sup>*

Na kwa sababu hiyo Amesema Allah تعالى:

فَلَوْلَا كَانَ مِنَ الْقُرُونِ مِنْ قَبْلِكُمْ أُولُوا بَقِيَّةٍ يَنْهَوْنَ عَنِ الْفَسَادِ فِي الْأَرْضِ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّنْ أَنْجَيْنَا مِنْهُمْ

***“Basi mbona hawakuwamo katika watu wa kabla yenu wenye vyeo na wasaa wanaokataza uharibifu katika nchi, isipokuwa wachache tu, ambao ndio Tuliowaokoa?”***

Na Kauli Yake:

وَاتَّبَعَ الَّذِينَ ظَلَمُوا مَا أُتْرِفُوا فِيهِ

***“Na waliodhulumu walifuata starehe zao...”***

Maana: Katika waliokuwa nayo miongoni mwa maasi na munkari, na wasigeuke katika kuwaonya hao, hadi adhabu ilipowajia ghafla na,

<sup>1</sup> Ibnu Majaah 2/1327.

وَكَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿١١٦﴾

*"...na wakawa ni wakosefu."*

Kisha Allah تعالى Ameerza kwamba Yeye Hakuangamiza mji wowote isipokuwa watu wake wamedhulumu nafsi zao, na adhabu Yake haijauendea mji wowote mwema mpaka watakapokuwa watu wake wao ndiyo madhalimu, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ ۗ

*"Na Sisi hatukuwadhulumu, lakini wao wenyewe wamejidhulumu..."*  
(11:101)

Akasema:

وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿١١٧﴾

*"...Wala Mola wako Mlezi si Mwenye Kuwadhulumu waja." (41:46)*

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٨﴾ إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ  
وَلِذَلِكَ خَلَقَهُمْ ۗ وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٩﴾

**118. Na Mola wako Mlezi Angelipenda Angewafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitilafiana,**

**119. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu; na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu Amewaumba. Na litatimia neno la Mola wako Mlezi: Kwelikweli Nitaijaza Jahannam kwa majini na watu pamoja.**

**Allah تعالى Hakuifanya Imani Ikubalike na Watu Wote wa Ardhi**

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye Anaweza Kuwafanya watu wote kuwa umma mmoja miongoni mwa imani na ukafiri. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مَن فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا ۗ

*"Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi..." (10:99)*



Na Kauli Yake:

وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٦﴾ إِلَّا مَنْ رَّحِمَ رَبُّكَ ۗ

**"...Lakini hawaachi kukhitilafiana. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu..."**

Maana yake: Wala tofauti haitaacha kuwepo baina ya watu, katika dini, itikadi mila, tabia, madhehebu na rai zao. Kama Kauli Yake Allah تعالى:

إِلَّا مَنْ رَّحِمَ رَبُّكَ ۗ

**"Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu,..."**

Hii ina maana: Isipokuwa wale waliorehemewa katika wafuasi wa Mitume, ambao wameshikamana na yale ambayo wameamrisha, katika dini. Wamepewa khabari kuhusu hiyo dini na Mitume wa Allah تعالى ambao walipelekwa kwao. Na huo haukuacha kuwa ndiyo mwendo wao mpaka Mtume ﷺ akawa wa mwisho wa Mitume na Manabii. Wakamfuata wakamkubali na wakamsaidia, wakafuzu na kupata mafanikio ya dunia na akhera, kwa sababu wao ndiyo kikundi chenye kuokoka kama ilivyokuja katika Hadithi iliyopokewa katika vitabu vya mapokezi na Sunan na kwa njia zinavyopana nguvu hizo zenyewe.

«إِنَّ الْيَهُودَ افْتَرَقَتْ عَلَى إِحْدَى وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، وَإِنَّ النَّصَارَى افْتَرَقَتْ عَلَى اثْنَتَيْنِ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، وَسَتَفْرُقُ هَذِهِ الْأُمَّةُ عَلَى ثَلَاثٍ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، كُلُّهَا فِي النَّارِ إِلَّا فِرْقَةً وَاحِدَةً»

*"Kwa hakika Mayahudi wamegawanyika katika vikundi sabini na moja na hakika Manaswara wamegawanyika katika makundi sabini na mbili na utagawanyika umma huu katika makundi sabini na tatu, yote yataingia motoni isipokuwa kikundi kimoja tu."*

Wakauliza, 'ni kina nani hao Ee Mtume?' Akasema:

«مَا أَنَا عَلَيْهِ وَأَصْحَابِي»

*"Ni wale watakaofuata yale ambayo mimi na masahaba wangu tuko juu yake."<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 2/332, na Abuu Daawuud 5/4, Tuhfatul Ahwahdy 7/397, Ibnu Maajah 2/1322.

Al-Hakimu amepokea kutoka katika kitabu chake *Al-Mustadrak* pamoja na nyongeza<sup>1</sup> hii. Na Kauli Yake,

وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٦﴾

**“Na litatimia neno la Mola wako Mlezi kwelikweli Nitaijaza Jahannam kwa majini na watu pamoja.”**

Allah تعالى Anaeleza kwamba: Imetangulia katika Hukumu Yake na Makadirio Yake, na kwa Elimu Yake iliyokamilika, na Hekima Yake yenye kupenya kwamba katika viumbe Wake kuna watakaostahiki pepo na katika wao kuna watakaostahiki moto. Na kwamba hapana budi kuijaza Jahannam kutokana na viumbe hivi wawili, majini na watu. Yeye Ana Hoja kubwa na Hekima iliyotimia. Imekuja katika sahihi Bukhari na Muslim, kutoka kwa Abu Huraira kuwa amesema: Mtume ﷺ amesema:

«اخْتَصَمَتِ الْجَنَّةُ وَالنَّارُ فَقَالَتِ الْجَنَّةُ: مَا لِي لَا يَدْخُلُنِي إِلَّا ضُفْنَاءُ النَّاسِ وَسَقَطُهُمْ وَقَالَتِ النَّارُ: أُورِثُ بِالْمُتَكَبِّرِينَ وَالسُّجَّيرِينَ. فَقَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ لِلْجَنَّةِ: أَنْتِ رَحْمَتِي أَرْحَمُ بِكَ مِنْ أَشَاءِ، وَقَالَ لِلنَّارِ: أَنْتِ عَذَابِي أَنْتِمْ بِكَ مِنْ أَشَاءِ، وَلِكُلِّ وَاحِدَةٍ مِنْكُمَا يَلُؤِمَا، فَأَمَّا الْجَنَّةُ فَلَا يَزَالُ فِيهَا فَضْلٌ، حَتَّى يُنْبِئَ اللَّهُ لَهَا خَلْقًا يُسْكِنُ فَضْلَ الْجَنَّةِ، وَأَمَّا النَّارُ فَلَا تَزَالُ تَقُولُ: هَلْ مِنْ مَزِيدٍ حَتَّى يَضَعَ عَلَيْهَا رَبُّ الْعِزَّةِ قَدَمَهُ فَتَقُولُ: قَطُّ قَطُّ وَعِزَّتِكَ»

*“Pepo na Moto zilizozana, Pepo ilisema: ‘Nina nini, kwanini kwangu hawaingii, isipokuwa wanyonge katika watu na duni wao.’ Na Moto ukasema: ‘Nimependelewa wenye kibri na wababe.’ Mwenyezi Mungu Mwenye Kushinda na Kutukuka Akaiambia pepo: “Wewe ni Rehema Yangu Nitamrehemu kwako Nimtakaye.’ Akauambia Moto, ‘wewe ni Adhabu Yangu, Nitamuadhibu kwako Nimtakaye.” Na kila mmoja miongoni mwenu ana hadhi yake, ama pepo haitaacha kuwa na nyongeza ndani yake, mpaka Mwenyezi Mungu Aumbe viumbe watakao ishi katika nyongeza ya pepo; ama moto hautaacha kusema: ‘Je kuna nyongeza?’ Mpaka Mwenyezi Mungu, Mola wa Utukufu Auwekee Unyayo Wake, hapo utasema: ‘Basi, basi, naapa kwa Utukufu Wako.’<sup>2</sup>*

<sup>1</sup> Haakim: 1/129.

<sup>2</sup> Fat’hul Bari, 13/444, na Muslim, 4/2186.

وَكُلًّا نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِ الرُّسُلِ مَا نُثَبِّتُ بِهِ فُؤَادَكَ ۗ وَجَاءَكَ فِي هَذِهِ الْحَقُّ  
وَمَوْعِظَةٌ وَذِكْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٠﴾

**120. Na yote Tunayokusimulia katika khabari za Mitume ni ya kukupa nguvu moyo wako. Na katika haya imekuja haki na mawaidha na ukumbusho kwa Waumini.**

### Hitimisho

Allah تعالى Anasema: Khabari zote ambazo Tunazisimulia kwako (Muhammad ﷺ) miongoni mwa khabari za Mitume waliotangulia kabla yako, pamoja na umati wao na namna mahojiano na majadiliano yalivyopita kwao. Na yale ambayo Mitume waliyavumilia katika kukadhibishwa na maudhi, na namna Allah تعالى Alivyolinusuru kundi Lake la waumini na maadui Wake makafiri Akawatelekeza. Yote hayo ni katika mambo ambayo Tunaimarisha kwayo moyo wako. Maana yake: Moyo wako ewe! Muhammad ﷺ, ili iwe kwako ni kigezo cha ndugu zako waliopita miongoni mwa Mitume. Na Kauli Yake,

وَجَاءَكَ فِي هَذِهِ الْحَقُّ

**“Na katika haya imekuja haki...”**

Maana yake: Sura hii. Hayo ameyasema Ibn Abbas رضي الله عنهما na Mujaahid, na kundi katika wanawazuoni waliotangulia, nayo ni sahihi. Anakusudia katika sura hii ambayo imekusanya visa vya Mitume na namna Allah تعالى Alivyowaokoa na wale walioamini pamoja nao, na Akawaangamiza makafiri. Ndani yake vimekuja visa vya haki na khabari ya kweli, na maonyo ambayo makafiri wataacha kwayo maovu yao, na maonyo ambayo watawaadhika kwayo waumini.

وَقُلْ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَاتِبِكُمْ إِنَّا عَمِلُونَ ﴿١٢١﴾ وَأَنْتُمْ مُنْتَظِرُونَ ﴿١٢٢﴾

**121. Na waambie wale wasioamini: Fanyeni muwezavyo, nasi pia tunafanya.**

**122. Na ngojeni, na sisi tunangoja.**

Allah تعالى Anasema Akimuamrisha Mjumbe Wake, awaambie wale ambao

hawayaamini yale ambayo amekuja nayo kutoka kwa Bwana wake, kwa njia za kuwatisha,

أَعْمَلُوا عَلَىٰ مَكَانَتِكُمْ

*“Fanyeni muwezavyo,...”*

Maana yake: Juu ya njia yenu na utaratibu wenu,

إِنَّا عَمِلُونَ ﴿١١٦﴾

*“...nasi pia tunafanya.”*

Maana yake: Juu ya njia yetu na utaratibu wetu,

وَأَنْتَظِرُونَ إِنَّا مُنْتَظِرُونَ ﴿١١٧﴾

*“Na ngojeni, na sisi tunangoja.”* Maana yake:

فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَنْ تَكُونُ لَهُ عَنقَبَةُ الدَّارِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١١٨﴾

*“...Mtakujajua nani atakuwa na makazi mema mwishoni. Hakika hawafaulu madhaalimu...”* (6:135)

Allah تعالی Alimtekelezea Mjumbe Wake ﷻ Ahadi Yake, Akamnusuru na Akampa nguvu, na Akayafanya maneno yake kuwa yaliyo juu, na maneno ya ambao wamekufuru, yakawa chini.

Na Allah تعالی ni Mwenye Kushinda na Mwingi wa Hekima,

وَلِلَّهِ غَيْبُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَيْهِ يُرْجَعُ الْأَمْرُ كُلُّهُ فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ ۗ وَمَا رَبُّكَ

بِغَيْفٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١١٩﴾

**123. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyofichikana katika ardhi na mbingu, na mambo yote yatarejezwa Kwake. Basi muabudu Yeye na umtegemee Yeye. Na Mola wako Mlezi Haghafiliki na yale mnayogatenda.**

Anaeleza Allah تعالی kwamba Yeye ni Mjuzi wa mambo yaliyojificha ya mbingu na ardhi na kwamba ni Kwake Yeye tu marejeo na Atampa kila mtendaji matendo yake siku ya hesabu; ni Kwake Yeye tu Kuumba na Kuamrisha. Kwa

hiyo, Allah تعالی Amewaamrisha kumuabudu Yeye tu na kumtegemea. Kwani Yeye Anamtosha mwenye kumtegemea na akarejea Kwake. Na Kauli Yake:

وَمَا رَبُّكَ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١١٦﴾

***“Na Mola wako Mlezi Haghafiliki na yale mnayoyatenda.”***

Maana yake: Kwake hakifichiki chochote ambacho wanaokukadhibisha kwako juu Yake, ewe Muhammad ﷺ, bali Yeye ni Mjuzi wa hali zao, na Atawalipa kwa hilo utimilifu wa malipo katika dunia na akhera, na Atakunusuru wewe na kundi lako duniani na akhera.

Mwisho mwa tafsiri ya Suratu Hud عليه السلام, kuhimidiwa ni kwa Allah تعالی na Kuneemesha.

\* \* \*

**Tafsiri ya Suratu Yusuf**  
**Sura ya 12**  
**Iliteremshwa Makkah**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

**سُورَةُ يُسُوفِ**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّ ۙ تِلْكَ ءَايَةُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿١﴾ إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ قُرْآنًا  
 عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢﴾ نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ أَحْسَنَ  
 الْقَصَصِ بِمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ هَذَا الْقُرْآنَ وَإِن كُنْتَ مِنْ  
 قَبْلِهِ لَمِنَ الْغَافِلِينَ ﴿٣﴾ إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ  
 إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي  
 سَاجِدِينَ ﴿٤﴾ قَالَ يَبْنَؤُكَ لَا تَقْصُصْ رُؤْيَاكَ عَلَيَّ  
 إِخْوَتَكَ فَيَكِيدُوا لَكَ كَيْدًا ۗ إِنَّ الشَّيْطَانَ لِلْإِنْسَانِ عَدُوٌّ  
 مُّبِينٌ ﴿٥﴾ وَكَذَلِكَ نَجْتَبِئُكَ رُؤْيَاكَ وَنُعَلِّمُكَ مِنْ تَأْوِيلِ  
 الْأَحَادِيثِ وَيُنَبِّئُكَ بِنِعْمَتِهِ عَلَيْكَ وَعَلَىٰ آلِ يَعْقُوبَ كَمَا  
 أَتَمَّهَا عَلَىٰ أَبَوَيْكَ مِنْ قَبْلُ ۖ إِنزَاهِمَ ۖ وَإِسْحَاقَ ۚ إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ  
 حَكِيمٌ ﴿٦﴾

الرَّ ۙ تِلْكَ ءَايَةُ الْكِتَابِ الْمُبِينِ ﴿١﴾  
 إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ  
 تَعْقِلُونَ ﴿٢﴾ نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ  
 أَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ  
 هَذَا الْقُرْآنَ وَإِن كُنْتَ مِنْ قَبْلِهِ  
 لَمِنَ الْغَافِلِينَ ﴿٣﴾

1. Alif Lam Raa. Hizi ni Aya za Kitabu kinachobainisha.
2. Hakika Sisi Tumeite-remsha Qur’ani kwa Kiarabu ili mpate kuzingatia.
3. Sisi Tunasimulia simulizi nzuri kwa kukufunulia Qur’ani hii. Na ijapokuwa kabla ya haya ulikuwa miongoni mwa wasiojua.

### Sifa za Qur'ani

Ama maneno kuhusu herufi za mkato yametangulia mwanzoni mwa *Surat Al-Baqarah*. Na Kauli Yake,

تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ

**“Hizi ni Aya za Kitabu.”**

Maana yake: Hizi ni aya za kitabu nacho ni Qur'ani yenye kubainisha. Maana yake: iliyowazi ambayo inaweka wazi mambo yaliyojificha, kuyafafanua na kuyabainisha.

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ قُرْءَانًا عَرَبِيًّا لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢﴾

**“Hakika Sisi Tumeiteremsha Qur'ani kwa Kiarabu ili mpate kuzingatia.” (12:2)**

Na hilo ni kwa sababu, lugha ya Waarabu ni fasaha zaidi kuliko lugha nyingine, na ni bainifu na pana zaidi, na ndio lugha inayobainisha maana ambazo zinasimama katika nafsi. Na kwa sababu hiyo Ameteremsha Kitabu Kitukufu zaidi ya vitabu vingine kwa lugha tukufu zaidi juu ya Mtukufu zaidi wa Mitume, kupitia ubalozi wa Mtukufu zaidi wa Malaika. Na hilo lilikuwa katika eneo tukufu mno katika ardhi, na kuteremshwa kwake kulianza katika mwezi Mtukufu zaidi wa miezi ya mwaka, nao ni mwezi wa Ramadhani. Kwa hiyo kitabu kimekamili kwa njia zote na kwa sababu hiyo Allah تعالیٰ Amesema:

لَخُنُ نَقْصُ عَلَيْكَ أَحْسَنَ الْقَصَصِ بِمَا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ هَذَا الْقُرْءَانَ

**“Sisi Tunasimulia simulizi nzuri kwa Kukufunulia Qur'ani hii...” (12:3)**

Maana yake: Kwa sababu ya Kukufunulia Kwetu wewe Qur'ani hii.

### Sababu ya Kushuka kwa Aya hii (12:3)

Imekuja katika sababu ya kushuka aya hii, yale ambayo ameyapokea Ibn Jariir kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: Masahaba waliuliza: ‘Ee Mtume ﷺ tunakuomba utusimulie, ikashuka,

لَخُنُ نَقْصُ عَلَيْكَ أَحْسَنَ الْقَصَصِ

**“Sisi Tunakusimulia simulizi nzuri.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Tabari 15/552.

Kuna Hadithi inayoendana na kutajwa kwa Aya hii tukufu, inayosifia Qur'an na kuonesha kuwa inatosheleza pasi na kuhitajika kitabu kingine chochote. Imam Ahmad amenukuu riwaya kutoka kwa Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه kuwa "Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alikuja kwa Mtume ﷺ akiwa na kitabu alichokichukua kutoka kwa Watu waliopewa Kitabu. 'Umar رضي الله عنه akaanza kumsomea Mtume ﷺ, naye akakasirika. Akasema,

«أَمْ نَبْرُكُونَ فِينَا يَا ابْنَ الْخَطَّابِ؟ وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَمَّا جِئْتُمْ بِهَا بَيْضَاءَ نَفِيَّةً، لَا تَسْأَلُوهُمْ عَنْ شَيْءٍ فَيُخْبِرُوكُمْ بِحَقِّ فَتَكْذِبُونَ، أَوْ بِبَاطِلٍ فَتُصَدِّقُونَهُ، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَوْ أَنَّ مُوسَى كَانَتْ حَيًّا مَا وَسِعَهُ إِلَّا أَنْ يُبْعِنِي»

*"Kwani una mashaka nacho ewe Ibn Al-Khattab? Naapa kwa Ambaye uhai wangu uko Mkononi Mwake! Nimekuleteeni nyeupe. Msiwaulize jambo, na wao wakakujulisheni kweli mkaikataa, au upotovu mkausadiki. Naapa kwa Ambaye uhai wangu uko Mkononi Mwake! Kama Musa angekuwa hai, asingekuwa na hiari isipokuwa kunifuata."*<sup>1</sup>

Imam Ahmad pia alinukuu riwaya kutoka kwa 'Abdullah bin Thabit رضي الله عنه ambaye alisema, "Umar رضي الله عنه alikuja kwa Mjumbe ﷺ na kusema, 'Ewe Mtume! Nilipita kwa ndugu yangu wa (kabila la) Quraydhah, akaniandikia maneno ya kina kutoka katika Taurati, je, nikusomee?' Uso wa Mjumbe ﷺ ukabadilika (kwa hasira). Nikamuambia ('Umar رضي الله عنه), 'Huo ni uso wa Mjumbe wa Allah?' 'Umar رضي الله عنه akasema, 'Tumeridhia Allah تعالى kuwa ni Mola wetu Mlezi, Uislamu kuwa Dini yetu na Muhammad ﷺ kuwa Mtume wetu.' Basi hasira ya Mtume ﷺ ikashuka, na akasema,

«وَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ، لَوْ أَصْبَحَ فِيكُمْ مُوسَى ثُمَّ اتَّبَعْتُمُوهُ وَتَرَكْتُمُونِي لَضَلَلْتُمْ، إِنَّكُمْ حَطَّيْتُمْ مِنَ الْأَمْرِ، وَأَنَا حَطَّيْتُكُمْ مِنَ النَّبِيِّينَ»

*"Naapa kwa Ambaye nafsi ya Muhammad iko Mkononi Mwake, kama Musa angetokea kuwa pamoja nanyi mkamfuata, na kuniacha mimi, basi mngepotea. Hakika, mna hadhi kwa mataifa kwa sababu ya mimi na mimi nina hadhi kwenu katika Mitume."*<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Ahmad 3:387,

<sup>2</sup> Ahmad 4:266, Angalia Al-Irwa' namba 1589.



إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي

سَجْدِينَ ﴿١٠﴾

**“Yusuf alipomuambia baba yake: Ewe babaangu! Hakika mimi nimeota nyota kumi na moja, na jua, na mwezi. Nimeota zikinisujudia.”(12:4)**

### Ndoto ya Yusuf عليه السلام

Allah تعالى Anasema watajje watu wako Ee Muhammad ﷺ katika kusimulia kwako kisa cha Yusuf عليه السلام wakati alipomuambia baba yake. Na baba yake ni Ya'aqub Bin Ishaqa Bin Ibrahim عليه السلام. Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: ‘Ndoto za Mitume ni Wahy!’.”

Wafasiri wa Qur’ani wamezungumza katika kuifasiri ndoto hii, kwamba zile nyota kumi na moja ni maelezo yenye kuwaelezea ndugu zake, walikuwa ni kumi na moja mbali na yeye, na jua na mwezi ni maelezo yenye kuwaelezea mama na baba yake. Haya yamepokewa kutoka kwa Ibn Abbas, Dhahaak, Qatada na Sufyani Thawry na Abdirrahmani bin Zaidi bin Aslam رضي الله عنهم. Na tafsiri yake ilitokea baada ya miaka arobaini. Na imesemwa miaka themanini, na hilo ni wakati alipowanyanyua wazazi wake juu ya kiti cha enzi, ndugu zake wakiwa mbele yake.

إِذْ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ رَأَيْتُهُمْ لِي

سَجْدِينَ ﴿١٠﴾ قَالَ يَبْنَئِي لَأَقْصُصَ رُؤْيَاكَ عَلَىٰ إِخْوَتِكَ فَيَكِيدُوا لَكَ كَيْدًا ۗ إِنَّ

الشَّيْطَانَ لِلْإِنْسَانِ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿١١﴾

**4. Yusuf alipomuambia baba yake: Ewe babaangu! Hakika mimi nimeota nyota kumi na moja, na jua, na mwezi. Nimeota zikinisujudia.**

**5. (Baba) akasema: Ewe mwanangu! Usiwasimulie nduguzo ndoto yako, wasije wakakufanyia vitimbi. Hakika Shet’ani ni adui aliye dhaahiri kwa mwanaadamu.**

<sup>1</sup> Tabari 15/554.

## Amri ya Ya'aqub عليه السلام kwa Yusuf عليه السلام Kuificha Ndoto kwa Tahadhari ya Hila za Shetani

Allah تعالى Anasema Akielezea maneno ya Ya'aqub عليه السلام kwa mtoto wake Yusuf عليه السلام, wakati alipomsimulia yale ambayo aliyaona katika ndoto hii. Ambayo tafsiri yake ni ndugu zake kunyenyekea kwake na kumtukuza yeye, kutukuza kukubwa kulikozidi, wakati wakiporomoka kwake hali ya kusujudu kwa kumtukuza, kumheshimu na kumkirimu. Ya'aqub عليه السلام akaogopa kumzungumzia mtu yeyote katika ndugu zake ndoto hii, kwani watamhusudu juu ya hilo, watamfanyia hila, kutokana na husuda waliyo nayo kwake. Kwa sababu hiyo Ya'aqub عليه السلام amesema na kumuambia Yusuf عليه السلام,

لَا تَقْصُصْ رُؤْيَاكَ عَلَىٰ إِخْوَتِكَ فَيَكِيدُوا لَكَ كَيْدًا<sup>ط</sup>

***"Usiwasimulie nduguzo ndoto yako, wasije wakakufanyia vitimbi."***

Maana yake: Watakuufanyia njama watakuangamiza kwa njama hizo, na kwa sababu hiyo imethibitika Hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا رَأَىٰ أَحَدُكُمْ مَا يُحِبُّ فَلْيُحَدِّثْ بِهِ، وَإِذَا رَأَىٰ مَا يَكْرَهُ فَلْيَتَحَوَّلْ إِلَىٰ جَنْبِ الْآخَرِ، وَلْيَتَمَلَّصْ عَنِ بَسَائِرِهِ ثَلَاثًا، وَلْيَسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنْ شَرِّهَا، وَلَا يُحَدِّثْ بِهَا أَحَدًا فَإِنَّهَا لَنْ تَضُرَّهُ»

*"Atakapoota mmoja wenu ndoto nzuri na awaeleze watu na atakapoota ndoto ambayo anaichukia na ageuke kulalia ubavu wake mwingine, na ateme mate kushotoni kwake mara tatu, na amtake hifadhi Mwenyezi Mungu na shari yake na asimzungumzie ndoto hiyo mtu yoyote, kwani ndoto hiyo haitamdhuru."<sup>1</sup>*

Na imekuja katika Hadithi nyingine ambayo ameipokea Imamu Ahmad na baadhi ya watu wa Hadithi kutokana na upokezi wa Mu'awiya Bin Haida Qushairy رضي الله عنه, kwamba yeye amesema, Mtume ﷺ amesema,

«الرُّؤْيَا عَلَىٰ رَجُلٍ طَائِرٌ مَا لَمْ تُعْبَرْ، فَإِذَا عُبِرَتْ وَقَعَتْ»

*"Ndoto iko mguuni mwa ndege muda wa kuwa haijafasiriwa ikifasiriwa inatokea."*

<sup>1</sup> Tabari 15/557.

Kwa hivyo, mtu anapaswa kuacha kutumaini neema inayokuja, ila mpaka imfikie na kujulikana. Mtume ﷺ amesema,

«اسْتَعِينُوا عَلَىٰ قَضَاءِ الْحَوَائِجِ بِكَيْتَمَانِهَا، فَإِنَّ كُلَّ ذِي نِعْمَةٍ مَّخْسُودٌ»

*“Jisaidieni kwa kukidhi haja kwa kuzifanya siri, kwani kila mwenye neema huhusudiwa.”*

وَكَذَلِكَ سَجَّيْتِكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ مِن تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ وَيُتِمُّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَعَلَىٰ آئِلِ

يَعْقُوبَ كَمَا أَتَمَّهَا عَلَىٰ أَبَوَيْكَ مِن قَبْلُ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦﴾

**6. Na kadhaalika Mola wako Mlezi Atakuteua na Atakufundisha tafsiri ya mambo. Na Atatimiza neema Zake juu yako na juu ya ukoo wa Yaa'qub, kama Alivyowatimizia hapo zamani baba zako Ibrahim na Is-haq. Hakika Mola wako Mlezi ni Mjuzi Mwenye Hikima.**

**Tafsiri ya Ndoto ya Yusuf** عليه السلام

Allah تعالى Anasema Akielezea maneno ya Ya'aqub عليه السلام kwa mtoto wake Yusuf عليه السلام: Kuwa kama Alivyokuteuwa Mola wako Akakuonesha nyota hizi pamoja na jua na mwezi vinakusujudia,

وَكَذَلِكَ سَجَّيْتِكَ رَبُّكَ

***“Na kadhaalika Mola wako Mlezi Atakuteuwa.”***

Maana yake: Anakuchagua na Kukuteua kwa ajili ya utume wake,

وَيُعَلِّمُكَ مِن تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ

***“...na Atakufundisha tafsiri ya mambo.”***

Mujahid amesema na wengine: Maana yake: kufasiri ndoto,

وَيُتِمُّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ

***“Na Atatimiza neema Zake juu yako.”***

Maana yake: Kwa kukupa utume na kukuletea Wahyi. Na kwa sababu hiyo amesema:

كَمَا أَتَمَّهَا عَلَىٰ أَبَوَيْكَ مِن قَبْلُ إِبْرَاهِيمَ

*"..kama Alivyowatimizia hapo zamani baba zako Ibrahim."*

Naye ni mwandani,

وَإِسْحَاقَ

*"Na Is'haqa."* Mtoto wake.

إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١١﴾

*"Hakika Mola wako Mlezi ni Mjuzi Mwenye Hikima."*

Maana yake: Anajua sana mahali Anapoweka ujumbe Wake, kama Alivyosema katika aya nyingine.

\* \* \*

\* لَقَدْ كَانَ فِي يُوسُفَ وَإِخْوَتِهِ ءَايَاتٍ لِّلسَّالِئِينَ ﴿٧﴾ إِذْ قَالُوا لِيُوسُفُ وَأَخُوهُ أَحَبُّ إِلَيْنَا مِنَّا وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّ أَبَانَا لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾ اقْتُلُوا يُوسُفَ أَوْ آطْرَحُوهُ أَرْضًا يَخْلُ لَكُمْ وَجْهَ أَبِيكُمْ وَتَكُونُوا مِن بَعْدِهِ قَوْمًا صَالِحِينَ ﴿٩﴾ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ لَا تَقْتُلُوا يُوسُفَ وَأَلْقُوهُ فِي غَيَابَتِ الْجُبِّ يَلْتَقِطْهُ بَعْضُ السَّيَّارَةِ إِن كُنْتُمْ فَاعِلِينَ ﴿١٠﴾ قَالُوا يَا أَبَانَا مَا لَكَ لَا تَأْتِنَا عَلَى يُوسُفَ وَإِنَّا لَهُ لَنَنْصِحُونَ ﴿١١﴾ أَرْسَلَهُ مَعَنَا غَدًا يَرْتَعِ وَيَلْعَبْ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٢﴾ قَالَ إِنِّي لَيَحْزُنُنِي أَنَّ تَذْهَبُوا بِهِ وَأَخَافُ أَن يَأْكُلَهُ الذِّئْبُ وَأَنْتُمْ عَنْهُ غَافِلُونَ ﴿١٣﴾ قَالُوا لَئِن أَكَلَهُ الذِّئْبُ وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّا إِذًا لَّخَسِرُونَ ﴿١٤﴾ فَلَمَّا ذَهَبُوا بِهِ وَاجْتَمَعُوا أَن يُجْعَلُوهُ فِي غَيَابَتِ الْجُبِّ وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِ لَتُنَبِّئَنَّهُمْ بِأَمْرِهِمْ هَذَا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٥﴾ وَجَاءَ وَ أَبَاهُمْ عِشَاءً يَبْكُونَ ﴿١٦﴾ قَالُوا يَا أَبَانَا إِنَّا ذَهَبْنَا نَسْتَبِقُ وَتَرَكْنَا يُوسُفَ عِندَ مَتَاعِنَا فَأَكَلَهُ الذِّئْبُ وَمَا أَنتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا وَلَوْ كُنَّا صَادِقِينَ ﴿١٧﴾ وَجَاءَهُ عَلَى قَمِيصِهِ بِدَمٍ كَذِبٍ ﴿١٨﴾ قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنفُسُكُمْ أَمْرًا فَصَبِرْ حَمِيلًا ﴿١٩﴾ وَاللَّهُ الْمُسْتَعَانُ عَلَى مَا تَصِفُونَ ﴿٢٠﴾

\* لَقَدْ كَانَ فِي يُوسُفَ وَإِخْوَتِهِ ءَايَاتٍ لِّلسَّالِئِينَ ﴿٧﴾ إِذْ قَالُوا لِيُوسُفُ وَأَخُوهُ أَحَبُّ إِلَيْنَا مِنَّا وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّ أَبَانَا لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾ اقْتُلُوا يُوسُفَ أَوْ آطْرَحُوهُ أَرْضًا يَخْلُ لَكُمْ وَجْهَ أَبِيكُمْ وَتَكُونُوا مِن بَعْدِهِ قَوْمًا صَالِحِينَ ﴿٩﴾ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ لَا تَقْتُلُوا يُوسُفَ وَأَلْقُوهُ فِي غَيَابَتِ الْجُبِّ يَلْتَقِطْهُ بَعْضُ السَّيَّارَةِ إِن كُنْتُمْ فَاعِلِينَ ﴿١٠﴾

7. Kwa yakini katika Yusuf na nduguze ziko ishara kwa wanaouliza.

8. Pale waliposema: Hakika Yusuf na nduguye wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi, hali sisi ni kikundi chenye nguvu. Hakika baba yetu yumo katika upotofu wa dhaahiri.

9. Muueni Yusuf, au mtupeni nchi mbali ili uso

wa baba yenu ukuelekeeni nyinyi. Na baada ya haya mtakuwa watu wema.

10. Akasema msemaji kati yao: Msimuuwe Yusuf. Lakini mtumbukizeni ndani ya kisima. Wasafiri watakuja mwokota; kama nyinyi mna sharti ya kufanya jambo.

**Kuna Ishara Ndani ya Kisa cha Yusuf** عليه السلام

Allah تعالى Anasema: Kwa hakika katika kisa cha Yusuf عليه السلام na khabari zake pamoja na ndugu zake kuna ishara nyingi. Maana yake: Mazingatio na mafunzo mengi kwa wenye kuulizia kuhusu hilo, wale wenye kutaka kuelewa kwa hakika hiyo ni khabari ya ajabu sana ambayo inastahiki kutolewa khabari.

إِذْ قَالُوا لِيُوسُفُ وَأَخُوهُ أَحَبُّ إِلَيْنَا مِمَّا

***“Pale waliposema: Hakika Yusuf na nduguye wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi.”***

Maana yake: Walipoapa katika wanayoyadhania, tunaapa kwa Allah تعالى. Yusuf عليه السلام na ndugu yake, wanamkusudia Bin Yamin, alikuwa ni ndugu yake kwa baba na mama,

أَحَبُّ إِلَيْنَا مِمَّا وَنَحْنُ عُصْبَةٌ

***“Wanapendwa zaidi na baba yetu kuliko sisi, hali sisi ni kikundi chenye nguvu.”***

Maana yake: kikundi, basi kwa vipi kawapenda hao watu wawili zaidi kuliko kundi?

إِنَّ أَبَانَا لَفِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿١٧﴾

***“Hakika baba yetu yumo katika upotofu wa dhaahiri.”***

Wanakusudia katika kuwapa kipaumbele wawili hao kuliko sisi, na kuwapenda kwake wawili hao zaidi kuliko sisi,

أَقْتُلُوا يُوسُفَ أَوْ اطْرَحُوهُ أَرْضًا يَخْلُ لَكُمْ وَجْهَ أَبِيكُمْ

***“Muueni Yusuf, au mtupeni nchi ya mbali ili uso wa baba yenu ukuelekeeni nyinyi.”***

Wanasema: Huyu anayependwa zaidi na baba yenu kuliko nyinyi muepusheni na uso wa baba yenu ili mbaki nyinyi tu peke yenu, ima kwa kumuua au kumtupa katika ardhi yoyote miongoni mwa ardhi za mbali.

Kwa kufanya hivyo mtapumzika naye na mtapata nafasi kwa baba yenu.

وَتَكُونُوا مِنْ بَعْدِهِ قَوْمًا صَالِحِينَ ﴿١٤﴾

**“Na baada ya haya mtakuwa watu wema.”**

Wakadhamiria toba kabla ya dhambi.

قَالَ قَائِلٌ مِنْهُمْ

**“Akasema msemaji kati yao.”**

Qatada na Muhammad bin Ishaqa wamesema: Na mkubwa wao jina lake lilikuwa: ni Ruwaibil.<sup>1</sup> Assudiy amesema: Ambaye aliyasema hayo ni Yahudha, Mujahid amesema: huyo ni Sham`uun Al-Swafa.

لَا تَقْتُلُوا يُوسُفَ

**“Msimuue Yusuf.”**

Maana yake: Msifikie kumfanyia uadui na kumchukia kiasi cha kutaka kumuua.

Na hawakuwa na njia ya kumuua kwa sababu Allah تعالی Alikuwa Anataka kwake jambo, ambalo hapana budi kutekelezwa na kutimizwa kwake, katika kupelekewa Wahyi wa Utume. Na pia kumthibitisha katika ardhi ya Misri na kutawala katika ardhi hiyo. Allah تعالی Akawaepusha kumfanyia kitendo hicho kwa meneno ya Ruwaibil kuhusu yeye. Na akapendekeza kwamba wamtumbukize, katika maficho ya kisima, katika kina chake cha chini zaidi,

يَلْتَقِطُهُ بَعْضُ السَّيَّارَةِ

**“Watamuokota baadhi ya wasafiri...”**

Maana yake: Wapita njia katika wasafiri, ili wapumzike naye, na hapana haja ya kumuua.

إِنْ كُنْتُمْ فَعَلِينَ ﴿١٥﴾

**“...kama nyinyi mna sharti ya kufanya jambo.”**

Maana yake: Mkiwa mmeazimia juu yake mnayosema. Muhammad bin Is-haq bin Yasari amesema: Waliazimia jambo kubwa la kuvunja udugu na kumuudhi mzazi, na kuacha kumuhurumia mtoto mdogo ambaye hana hatia yoyote.

<sup>1</sup> Tabari 15/564, 565.

Vilevile kumhurumia mtu mzima, kikongwe, mwenye haki, heshima, ubora na fadhila zake, mbele ya Allah تعالى. Pamoja na haki ya mzazi kwa mtoto wake, na azma yao ya kutaka kutenganisha kati ya mtoto kipenzi na baba yake kikongwe, mwenye upendo wa juu, kwa mtoto wake. Bado Allah تعالى Anawasamehe wao, na Yeye ni Mwenye Huruma kuliko viumbe vyote. Kwani wamebeba jambo kubwa sana. Amepokea Ibn Abuu Hatim kutokana na njia ya Salma Ibn Al-Fadhli kutokana na yeye.

قَالُوا يَا أَبَانَا مَا لَكَ لَا تَأْمَنَّا عَلَى يُوسُفَ وَإِنَّا لَهُ لَنَنْصِحُونَ ﴿١١﴾ أَرْسَلَهُ مَعَنَا غَدًا يَرْتَعِ وَيَلْعَبُ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٢﴾

**11. Wakasema: Ewe baba yetu! Una nini hata hutuamini kwa Yusuf? Na hakika sisi ni wenye kumtakia kheri!**

**12. Mpeleke kesho pamoja nasi, ale kwa furaha na acheze; na bila ya shaka sisi tutamhifadhi**

**Ndugu Zake Yusuf عليه السلام Waomba Ruhusa kwa Baba Yao ya Kutaka Kutoka na Yusuf عليه السلام**

Wakati walipokula njama juu ya kumkamata na kumtupa kisimani kama alivyotoa pendekezo hilo ndugu yao mkubwa Ruwaibili, walimuendea Baba yao Ya'aqub عليه السلام wakasema: 'Hivi una nini!'

لَا تَأْمَنَّا عَلَى يُوسُفَ وَإِنَّا لَهُ لَنَنْصِحُونَ ﴿١١﴾

**"Una nini hata hutuamini kwa Yusuf? Na hakika sisi ni wenye kumtakia kheri!"**

Na huku ni kuweka msisitizo kuhusu ombi lao kuwa wao wanakusudia kinyume cha hivyo. Kwa sababu ndani ya nyoyo zao kumejaa husuda kutokana na mapenzi ya Baba yao kwake,

أَرْسَلَهُ مَعَنَا

**"Mpeleke kesho pamoja nasi."**

Maana yake: Tuachie sisi.

غَدًا يَرْتَعِ وَيَلْعَبُ

**"Ale kwa furaha na acheze."**



Wamesoma baadhi yao kwa kisomo (cha) *'yarta`a wayal`ab'* wengine wamesoma (na) *'narti`a wanal`ab.'* Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما aende na achangamke.<sup>1</sup> Na kama hivyo amesema Qatada na Adh-Dhahaak na Assudiy na watu wengine.<sup>2</sup>

وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٣﴾

***"Na hakika sisi ni wenye kumtakia kheri!"***

Wanasema: Na sisi tutamhifadhi tutamlinda kwa ajili yako.

قَالَ إِنِّي لَيَحْزُنُنِي أَنْ تَذْهَبُوا بِهِ وَأَخَافُ أَنْ يَأْكُلَهُ الذِّئْبُ وَأَنْتُمْ عَنْهُ غَافِلُونَ ﴿١٤﴾

قَالُوا لَئِنْ أَكَلَهُ الذِّئْبُ وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّا إِذًا لَّخَسِرُونَ ﴿١٥﴾

**13. Akasema: Kwa hakika inanihuzunisha kwamba nyinyi mwende naye, na ninaogopa asije mbwa mwitu akamla nanyi mmeghafilika naye.**

**14. Wakasema: Ikiwa mbwa mwitu atamla na hali sisi ni kundi lenye nguvu kabisa, basi bila ya shaka sisi tutakuwa khasarani.**

**Ya'aqub عليه السلام Anawajibu Ombi Lao**

Allah تعالى Anasema Akimuelezea Mtume wake Ya'aqub عليه السلام kwamba yeye aliwaambia watoto wake katika kuwajibu yale ambayo waliyaomba kuhusu kuwakabidhi wao Yusuf عليه السلام pamoja na wao kwenda machungani katika jangwa,

إِنِّي لَيَحْزُنُنِي أَنْ تَذْهَبُوا بِهِ

***"Kwa hakika inanihuzunisha nyinyi kuenda naye."***

Maana yake: Inakuwa vigumu juu yangu kutengana naye, muda wa nyie kwenda naye, mpaka atakaporudi. Na hilo linatokana na kuvuka mpaka kwa mapenzi yake kwake, kutokana na yale ambayo anayaona kwake miongoni mwa kheri kubwa, sifa za utume, na ukamilifu wa maumbile na tabia. Kauli Yake:

<sup>1</sup> Tabari 15/570.

<sup>2</sup> Tabari 15/571.

وَأَخَافُ أَنْ يَأْكُلَهُ الذِّئْبُ وَأَنْتُمْ عَنْهُ غٰفِلُونَ ﴿٧﴾

**“...na ninaogopa asije mbwa mwitu akamla nanyi mmeghafilika naye.”**

Anasema: Ninaogopea hamtashughulika naye kutokana urushaji wenu mishale na kuchunga kwenu, atajiwa na mbwa mwitu amle, na hali ya kuwa nyinyi hamuelewi. Wakachukua tamko hilo kutoka mdomoni mwake, wakalifanya ndiyo udhuru wao katika ambalo wamelifanya. Wakasema wakimjibu kupitia tamko hilo wakati huu:

لَيْنَ أَكَلَهُ الذِّئْبُ وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّا إِذًا لَّخٰسِرُونَ ﴿٨﴾

**“...Ikiwa mbwa mwitu atamla na hali sisi ni kundi lenye nguvu kabisa, basi bila ya shaka sisi tutakuwa khasarani.”**

Wanasema: Iwapo mbwa mwitu atamshambulia na akamla miongoni mwetu, na hali ya kuwa sisi ni kikundi, hakika sisi wakati huo tutakuwa tumeangamia.

فَلَمَّا ذَهَبُوا بِهَا وَاجْتَمَعُوا أَن يَجْعَلُوهُ فِي غَيْبَتِ آجُتٍ ۖ وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِ لَتُنَبِّئَهُمْ بِأَمْرِهِمْ

هٰذَا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

**15. Basi walipomchukua na wakakubaliana wamtumbukize ndani ya kisima, Tulimfunulia Yusuf: Hapana shaka yoyote utakuja waambia kwa jambo lao hili, na wala wao hawatambui.**

**Yusuf عليه السلام Anatupwa Ndani ya Kisima**

Allah تعالى Anasema Ndugu zake Yusuf عليه السلام walipomchukua machoni mwa baba yake, huku wakidai kuwa watamchunga.

وَاجْتَمَعُوا أَن يَجْعَلُوهُ فِي غَيْبَتِ آجُتٍ ۖ

**“...Na wakakubaliana wamtumbukize ndani ya kisima.”**

Katika maneno haya kuna ukuzaji wa yale ambayo wamefanya. Kwa hakika wao walikubaliana wote juu ya kumtupa ndani ya kisima hicho. Dhahiri ilivyo ni kwamba walimchukua kutoka kwa Baba yake, huku wakimtukuza na kumtoa wasiwasi kwa kumpa maneno ya furaha. Panasemwa kwamba Yaaqub عليه السلام wakati alipowakabidhi alimkumbatia na akambusu na akamuombea. Assudiy

na wengine wametaja kwamba mambo yalivyokuwa ni kwamba hapakuwa kati ya kumtukuza kwao na kati ya kuonesha maudhi kwake isipokuwa ni kiasi cha kuondoka kwao tu machoni pa baba yake. Na wakajificha naye, kisha wakaanza kumfanyia maudhi kwa maneno. Miongoni mwa matusi na mfano wake, na kwa vitendo miongoni mwa kumpiga na mfano wake. Kisha wakaenda naye kwenye kisima hicho ambacho walipatana kumtupa humo, wakamfunga kwa kutumia kamba, na hali ya kuwa ndoo yake imefungwa na kamba hiyo, alikuwa pindi anapotegemea kwa mmoja wao humpiga makofi na kumtukana na pindi anapojishikamanisha na ukingo wa kisima wanaipiga mikono yake kisha wakamkatia kamba katika nusu ya masafa. Akaangukia katika maji, yakamwenea maji, akapanda kwenye jiwe ambalo lilikuwa katikati yake. Jiwe hilo linaitwa (*al-rraghuufah*) akasimama juu yake<sup>1</sup>.

Na Kauli Yake:

﴿وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِ لَتُنَبِّئَنَّهُمْ بِأَمْرِهِمْ هَذَا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ﴾

***“Tulimfunulia (Yusuf): Hapana shaka yoyote utakuja waambia kwa jambo lao hili, na wala wao hawatambui.”***

Allah تعالى Anasema hali ya Kutaja Upole Wake, Rehma Yake, Kunufaisha Kwake na Kuteremsha Kwake wepesi katika hali ya uzito, hakika Yeye Alimfunulia Yusuf عليه السلام katika hali hiyo ya haki, ili Auburudishe moyo wake na Authubutishe, kwa hakika wewe hutapatwa na huzuni kutokana na lile ambalo umo ndani yake. Kwa hakika wewe katika hilo una faraja na matokeo mazuri. Allah تعالى Atakunusuru juu yao, Atakuweka juu na Atainyanyua daraja yako, na utawaeleza lile ambalo wamekufanyia katika kitendo hiki.

Na Kauli Yake,

﴿وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ﴾

***“...na wala wao hawatambui.”***

Na amesema Ibn Abbas عليه السلام: Utawapa habari ya kitendo chao hiki walichokufanyia wewe hali ya kuwa wao hawakujui wala hawakutambui<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Tabari 15/574.

<sup>2</sup> Tabari 15/577.

وَجَاءُوا أَبَاهُمْ عِشَاءً يَبْكُونَ ﴿١٦﴾ قَالُوا يَا أَبَانَا إِنَّا ذَهَبْنَا نَسْتَبِقُ وَتَرَكْنَا يُوسُفَ عِنْدَ  
 مَتْعِنَا فَاكَلَهُ آلُ زَيْبٍ ۗ وَمَا أَنْتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا وَلَوْ كُنَّا صَادِقِينَ ﴿١٧﴾ وَجَاءُوا عَلَى  
 قَمِيصِهِ بِدَمٍ كَذِبٍ ۗ قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا ۗ فَصَبْرٌ حَمِيلٌ ۗ وَاللَّهُ الْمُسْتَعَانُ  
 عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١٨﴾

16. Wakaja kwa baba yao usiku wakilia.

17. Wakasema: Ewe baba yetu! Hakika tulikwenda kushindana na tukamuacha Yusuf penye vitu vyetu. Basi mbwa mwitu akamla. Lakini wewe hutuamini ijapokuwa tunasema kweli.

18. Wakaja na kanzu yake ina damu ya uwongo. Akasema: Bali nafsi zenu zimekushawishini kutenda kitendo. Lakini subira ni njema; na Mwenyezi Mungu Ndiye wa Kuombwa msaada kwa haya mnayo yaeleza.

### Hila za Ndugu Zake Yusuf عليه السلام kwa Baba Yao

Allah تعالى Anasema Akielezea kuhusu jambo ambalo walilitegemea ndugu zake Yusuf عليه السلام baada ya kumtupa katika kina cha shimo la kisima, kwamba wao walirejea kwa Baba yao katika kiza cha usiku hali ya kuwa wanalia. Na wanaonesha masikitiko na malalamiko juu ya Yusuf عليه السلام, na wanaonesha kuwa wana huzuni kubwa sana kwa baba yao. Na walisema kwa kuomba msamaha kutokana na lile ambalo limetokea katika madai yao:

إِنَّا ذَهَبْنَا نَسْتَبِقُ

“*Hakika tulikwenda kushindana.*” Maana yake: tunarushiana,

وَتَرَكْنَا يُوسُفَ عِنْدَ مَتْعِنَا

“*Na tukamuacha Yusuf penye vitu vyetu.*” Maana: nguo na mizigo yetu,

فَاكَلَهُ آلُ زَيْبٍ ۗ

“*Basi mbwa mwitu akamla.*” Na hilo ndilo ambalo alikuwa amelilogopa na kulitahadharisha. Na Kauli Yake:

وَمَا أَنْتَ بِمُؤْمِنٍ لَّنَا وَلَوْ كُنَّا صَادِقِينَ ﴿١٧﴾

**“Lakini wewe hutuamini ijapokuwa tunasema kweli.”** Maelezo yenye upole mkubwa kuthibitisha lile ambalo wanalifanyia hila. Wanasema: Na sisi tunajua kuwa wewe hutuamini - na hali ndio hii iwapo utatuamini. Vipi utatuamini na hali ya kuwa wewe una tutuhumu katika jambo hilo? Kwa sababu wewe ulichelea yeye kuliwa na mbwa mwitu, na imetokea kweli ameliwa. Kwa hiyo wewe umesamehewa kwa kutuona sisi kwako ni waongo, kwa sababu ya jambo hili lililotokea, na makubaliano yetu mazuri tuliyoafikiana pamoja katika jambo hili.

وَجَاءُوا عَلَىٰ قَمِيصِهِ بِدَمٍ كَذِبٍ ﴿١٨﴾

**“Wakaja na kanzu yake, ina damu ya uwongo.”** Maana yake: Damu ya uongo iliyotumiwa. Na hili ni katika matendo ambayo wanatilia mkazo kwamba hawakufanya njama wala hila juu yake. Na ni kwamba wao walimkusudia mtoto wa kondoo wakati wa kuzaliwa kwake, katika yale ambayo ameyataja Mujahidi na Assudiy na wengine, wakamchinja wakaipakaza nguo ya Yusuf عليه السلام kwa damu yake<sup>1</sup> hali ya kuwa wakimaanisha hivyo ndivyo walivyoipata kanzu yake, ambayo Yusuf عليه السلام alivaa wakati akiliwa, na imepatwa na damu yake. Isipokuwa katika uwongo wao huu walisahau kuirarua hiyo kanzu. Na kwa sababu hiyo kitendo hiki hakikuwa na mashiko, hakikiona Mtume Yaaqub عليه السلام, bali aliwaambia hali ya kupinga maneno yao, akawaeleza ambalo limethibitika katika nafsi yake, miongoni mwa kubabaisha kwao.

بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا فَصَبِرُوا حَمِيمًا ﴿١٩﴾

**“Bali nafsi zenu zimekushawishini kutenda kitendo. Lakini subira ni njema.”**

Maana yake: Nitasubiri subira nzuri juu ya jambo hili ambalo mmepatana juu yake mpaka Atakapoliondoa Allah تعالى kwa Msaada Wake na Upole Wake,

وَاللَّهُ الْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿٢٠﴾

**“...na Mwenyezi Mungu Ndiye wa Kuombwa msaada kwa haya mnayoyaeleza.”**

Maana yake: Yale ambayo mnayataja miongoni mwa uongo na hila.

<sup>1</sup> Tabari 15/580.

وَجَاءَتْ سَيَّارَةٌ فَأَرْسَلُوا وَارِدَهُمْ  
 فَأَدَّتْ دَلْوَهُ<sup>ط</sup> قَالَ يَبِئْسَ تِجَارَةً  
 هَذَا غُلْمٌ<sup>ع</sup> وَأَسْرُوهُ بَضْعَةً<sup>ع</sup> وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِمَا  
 يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾ وَشَرَوْهُ بِثَمَنٍ  
 بَخْسٍ دَرَاهِمَ مَعْدُودَةٍ وَكَانُوا فِيهِ  
 مِنَ الزَّاهِدِينَ ﴿٢٠﴾ وَقَالَ الَّذِي  
 اشْتَرَاهُ مِنْ مِصْرَ لِمَرْأَتِهِ  
 أَكْرِمِي مَثْوَاهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا  
 أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا<sup>ع</sup> وَكَذَٰلِكَ  
 مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ  
 وَلِنُعَلِّمَهُ مِنْ تَأْوِيلِ  
 الْأَحَادِيثِ<sup>ع</sup> وَاللَّهُ غَالِبٌ  
 عَلَىٰ أَمْرِهِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ  
 النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢١﴾  
 وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ<sup>ع</sup> آتَيْنَاهُ  
 حُكْمًا وَعِلْمًا<sup>ع</sup> وَكَذَٰلِكَ  
 نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٢٢﴾ وَرَوَدَتْهُ  
 الْأَيُّهُ<sup>ع</sup> وَقَالَتْ هَيْتَ لَكَ<sup>ع</sup>  
 قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ<sup>ط</sup> إِنَّهُ رَبِّي  
 أَحْسَنَ مَثْوَىٰ<sup>ط</sup> إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ  
 الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾ وَلَقَدْ هَمَّتْ  
 بِهِ<sup>ط</sup> وَهَمَّ بِهَا لَوْلَا  
 أَنَّ رَجُلًا<sup>ع</sup> بَرَّهَنَ رَبِّي<sup>ع</sup>  
 كَذَٰلِكَ لِنَصْرِفَ عَنْهُ  
 السُّوءَ وَالْفَحْشَاءَ<sup>ع</sup> إِنَّهُ  
 مِنْ عِبَادِنَا الْمُتْلِصِينَ ﴿٢٤﴾

وَجَاءَتْ سَيَّارَةٌ فَأَرْسَلُوا وَارِدَهُمْ  
 فَأَدَّتْ دَلْوَهُ<sup>ط</sup> قَالَ يَبِئْسَ تِجَارَةً  
 هَذَا غُلْمٌ<sup>ع</sup> وَأَسْرُوهُ بَضْعَةً<sup>ع</sup> وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِمَا  
 يَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾ وَشَرَوْهُ بِثَمَنٍ  
 بَخْسٍ دَرَاهِمَ مَعْدُودَةٍ وَكَانُوا فِيهِ  
 مِنَ الزَّاهِدِينَ ﴿٢٠﴾

**19. Ukafika msafara, wakamtuma mchota maji wao, naye akatumbukiza ndoo yake. Alisema: Kheri Inshallah! Huyu hapa mvulana! Wakamficha ili kumfanya ni bidhaa. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa wanayoyatenda.**

**20. Na wakamuza kwa thamani duni, kwa akali ya pesa. Wala hawakuwa na haja naye.**

### Yusuf عليه السلام Anaokolewa Kutoka Kisimani na Anauzwa Kama Mtumwa

Allah تعالى Anasema Akielezea yale yaliyompitia Yusuf عليه السلام wakati walipomtupa ndugu zake na wakamuacha katika shimo hilo hali ya kuwa peke yake mpweke, akakaa kisimani Yusuf عليه السلام siku tatu. Katika yale ambayo ameyasema Abuu Bakr Bin Ayyash, na ameyasema Muhammad bin Is'haqa. Walipomtupa ndugu zake walikaa pembezoni mwa kisima siku yao hiyo wakitazama nini atafanya na lile atakalofanyiwa. Akampelekea Mwenyezi Mungu wasafiri wakashukia karibu ya kisima kile wakamtuma mchota maji

wao alipokwenda kwenye kisima hicho na akaiteremsha ndoo yake ndani ya kisima kile alijishikamatisha Yusuf عليه السلام na ndoo ile akamtoa, na akafurahi mchota maji na kwa sababu hiyo akasema:

يُبَشِّرِي هَذَا غُلْمًا

**“Kheri Inshallah! Huyu hapa mvulana!”**

Na amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na Kauli Yake,

وَأَسْرُوهُ بِضَعَّةٍ

**“Wakamficha ili kumfanya ni bidhaa.”**

Anawakusudia ndugu zake Yusuf عليه السلام walilificha jambo lake na wakaficha kuwa ni ndugu yao na alilificha Yusuf عليه السلام jambo lake kwa kuogopea kumuua ndugu zake na akachagua kuuzwa, wakalitaja hilo ndugu zake kwa mchota maji nao akawaita wenzake.

يُبَشِّرِي هَذَا غُلْمًا

**“Kheri Inshallah! Huyu hapa mvulana!”**

Anauzwa, ndugu zake wamemuza.<sup>1</sup>

Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿٦٠﴾

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa wanayoyatenda.”**

Inaeleza kuwa Allah تعالى Aliyajua waliyoyafanya nduguze Yusuf عليه السلام, na wale waliomnunua. Alikuwa na Uwezo wa Kuwazuia vitendo vyao, lakini kwa Hekima Yake kamilifu. Alijaalia vingine. Aliwaacha wafanye vile ili Maamuzi Yake yatawale na Aliyoyataka yaweze kutimia.

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٦١﴾

**“...Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (7:54)**

<sup>1</sup> Tabari 16:6

Hii inamkumbusha Mtume ﷺ, kuwa Allah تعالى Anayajua waliyomtendea watu wake dhidi yake na kuwa Ana Uwezo wa Kuwazuia. Hata hivyo, Aliamua Kuwapa muda kidogo, halafu Akampa ushindi Muhammad ﷺ na Kumfanya awe juu yao, kama Alivyompa ushindi Yusuf عليه السلام na Alivyomjaalia kuwa juu ya nduguze. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَشَرَوْهُ بِثَمَنٍ بَخْسٍ دَرَاهِمَ مَعْدُودَةٍ

**“Na wakamuza kwa thamani duni, kwa akali ya pesa...”**

Maana yake: Nduguze Yusuf عليه السلام walimuza kwa bei ya chini mno. Kwa mujibu wa Mujahid na 'Ikrimah, neno 'Bakhs' linamaanisha iliyo pungufu mno.<sup>1</sup> Kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine,

فَلَا يَخَافُ يَخْسًا وَلَا رَهَقًا ﴿١٣﴾

**“...Basi mwenye kumuamini Mola wake Mlezi basi haogopi kupunjwa wala kudhulumiwa.” (72:13)**

Inamaanisha kuwa nduguze Yusuf عليه السلام walimuza kwa bei ndogo mno. Tena hakuwa na thamani kwao, ambapo kama watu wa msafara wangemtaka bure bila ya malipo, wangewapa bure! Ibn 'Abbas, Mujahid na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم walisema,

وَشَرَوْهُ

**“...Na wakamuza...”** Inakusudia nduguze Yusuf عليه السلام.<sup>2</sup> Walimuza Yusuf عليه السلام kwa bei ya chini mno, kama ilivyoashiriwa na kauli ifuatayo ya Allah تعالى,

دَرَاهِمَ مَعْدُودَةٍ

**“... kwa akali ya pesa....”**, Dirhamu ishirini, kwa mujibu wa 'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه.<sup>3</sup> Sawa na hayo yalisemwa na Ibn 'Abbas, Nawf Al-Bikali, As-Suddi, Qatadah na 'Atiyah Al-'Awfi رضي الله عنهم, aliyeongeza kuwa waligawana Dirhamu hizo, kila mmoja alipata Dirhamu mbili,<sup>4</sup> Adh-Dhahhak رضي الله عنه amesema kuhusu Aya,

<sup>1</sup> Tabari 16:12.

<sup>2</sup> Tabari 16:14-17.

<sup>3</sup> Tabari 16:12.

<sup>4</sup> Tabari 16:14.



وَكَاثُوا فِيهِ مِنَ الزَّاهِدِينَ ﴿١٩﴾

“... *Wala hawakuwa na haja naye.*”

“Hayo ni kwa sababu wao hawakuwa wakiujua utume wake (Yusuf عليه السلام) pamoja na daraja yake Tukufu kwa Allah تعالى.”

وَقَالَ الَّذِي اشْتَرَاهُ مِنْ مِصْرَ لِمَرْأَتِهِ أَكْرِي مَثْوَاهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا  
وَكَذَلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ وَلِنُعَلِّمَهُ مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ عَلِيمٌ  
أَمْرِهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٢٠﴾ ۗ وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ ءَاتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا  
وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿٢١﴾

**21. Na yule aliyemnunua huko Misri alimuambia mkewe: Mtengenezee makaazi ya hishima huyu; huenda akatufaa au tukamfanya mwenetu. Na kama hivyo Tulimuweka Yusuuf katika nchi ili Tumfundishe kufasiri mambo. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kushinda katika jambo Lake, lakini watu wengi hawajui.**

**22. Na alipofikilia utu uzima Tulimpa hukumu na ilimu. Na kama hivi Tunawalipa wanaotenda mema.**

**Yusuf عليه السلام Akiwa Misri**

Allah تعالى Anaeleza Upole Wake juu ya Yusuf عليه السلام kwamba Yeye Alimuandaa kwa ajili yake yule mtu aliyemnunua kutoka Misri mpaka akaweza kumshughulikia, kumkirimu na akamuagiza mke wake kufanya hivyo baada ya kuhisi ishara za kheri kwake.

أَكْرِي مَثْوَاهُ عَسَىٰ أَنْ يَنْفَعَنَا أَوْ نَتَّخِذَهُ وَلَدًا

“*Yatukuze makazi yake huenda akatufaa au tukamfanya mtoto.*”

Na yule mtu aliyemnunua pale Misri alikuwa ni Mheshimiwa, mwenye cheo cha uwaziri. Na amesema Abuu Ishaqa kutoka kwa Abuu ‘Ubayda kutoka kwa na Abdallah bin Mas’ud رضي الله عنهم kwamba yeye amesema: Wachambuzi zaidi wa mambo kwa njia ya kuyapima ni watu watatu: Mtawala wa Misri wakati aliposema kumuambia mke wake,

أَكْرَبِي مَثَوْنَهُ عَسَىٰ

**“Yatukuze makazi yake...”**

Na mwanamke aliyemuambia baba yake,

يَتَأْتِي أَشْتَجِرَهُ

**“...Ee Baba yangu mwajiri...” (28:26)**

Na Abubakri Al-Swiddiq رضى الله عنه wakati alipomfanya kiongozi ‘Umar bin Al-Khattab رضى الله عنه. Allah تعالى Anasema: kama tulivyomuokoa Yusuf عليه السلام, kwa ndugu zake,

وَكَذَلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ

**“...Kama hivyo Tulimpa cheo Yusuf katika ardhi...”**

Anakusudia ardhi ya nchi ya Misri.

وَلِنُعَلِّمَهُمُ مِنَ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ

**“Na ili Tumfundishe kufasiri ndoto.”**

Amesema Mujahid na Assudiy huko ni kufasiri ndoto.

وَاللَّهُ غَالِبٌ عَلَىٰ أَمْرِهِ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushinda, Juu ya Mambo Yake.”**

Maana yake: Akilitaka jambo, basi Utashi Wake Haurudishwi, Haupingwi, wala Hauzuiwi bali Yeye Ndiye Mwenye Kushinda kila kiwacho. Amesema Saeed bin Jubair katika Kauli Yake:

وَاللَّهُ غَالِبٌ عَلَىٰ أَمْرِهِ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushinda katika mambo Yake.”**

Maana yake: Ni Mfanyaji sana wa yale Anayoyataka. Na Kauli Yake:

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

**“Isipokuwa watu wengi hawaelewi.”**

Anasema: Hawaielewi Hekima Yake katika Kuumba Kwake, na Kufanya Kwake Upole na Kutenda Kwake lile Analolitaka. Na Kauli Yake.

وَلَمَّا بَلَغَ

**“Na alipofikia utu uzima.”**

Yaani: Yusuf عليه السلام,

أَشَدَّهُ

**“Ukamilifu wake.”**

Maana yake: Alipoikamilisha akili yake na umbile lake.

ءَاتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا

**“Tulimpa utume na elimu.”**

Anakusudia: Utume kwamba yeye alimpa huo utume kati ya hao watu,

وَكَذَلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴿١٧﴾

**“Na kama hivyo Tunawalipa watu wema.”**

Maana yake: Hakika yeye alikuwa mwema kutokana na matendo yake kwa kumtii Allah تعالى.

وَرَاوَدَتْهُ الْإِنْسِي فِي بَيْتِهَا عَنْ نَفْسِهِ وَعَلَّقَتْ الْأَبْوَابَ وَقَالَتْ هَيْت لَكَ قَالَ مَعَاذَ

اللَّهِ إِنَّهُ رَبِّي أَحْسَنَ مَثْوَايَ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١٨﴾

**23. Na yule bibi wa nyumba aliyokuwamo Yusuf alimtamani kinyume cha nafsi yake, na akafunga milango. Akamuambia: Njoo! Yusuf akasema: Audhubillahi! Najikinga na Mwenyezi Mungu. Bwana wangu huyu kaniweka katika maskani nzuri, na hakika wenye kudhulumu hawatengenekwi.**

## Mapenzi ya Mke wa Mtwala wa Misri kwa Yusuf عليه السلام na Kumfanyia Kwake Vituko

Allah تعالى Anaeleza kuhusu mke wa Mheshimiwa ambaye Yusuf عليه السلام alikuwa akiishi nyumbani mwake, pale Misri na alikuwa mume wake amemuusia juu ya Yusuf عليه السلام na kumkirimu. Mwanamke yule akamtaka Yusuf عليه السلام, pasina Yusuf عليه السلام kumtaka yeye. Maana alimfanyia hila nafsi yake na akamuita kwake. Na hilo ni kwa sababu ya kuwa mwanamke yule alimpenda Yusuf عليه السلام mapenzi makubwa sana. Kwa sababu ya uzuri wa Yusuf عليه السلام na utanashati wake. Hilo likamfanyia kujipamba kwa ajili yake na akamfungia milango na akamuita kwake.

وَقَالَتْ هَيْتَ لَكَ<sup>ع</sup>

**“Na akasema njoo.”**

Akajizuilia na jambo hilo kujizuilia kwa nguvu sana na,

قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ إِنَّهُ رَبِّي أَحْسَنَ مَقْوَلًا<sup>ط</sup>

**“Akasema: Nataka Hifadhi kwa Mwenyezi Mungu hakika Yeye ni Bwana wangu ameyafanya mazuri makazi yangu.”**

Na walikuwa wanalitumia tamko “Rabi” kwa maana ya “Bwana” na Mtu mkubwa, maana hakika mume wako ni Bwana wangu ameyafanya mazuri makazi yangu. Kwa maana, mashukio yangu, na amenifanyia wema kwa hiyo sitamlipa kwa kumfanyia uchafu kwa mke wake,

إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الظَّالِمُونَ ﴿١٢٠﴾

**“Kwa hakika hawafanikiwi madhalimu.”**

Ameyasema hayo Mujahid na Assudiy na Muhammad bin Is’haqa na wengine. Kwa hakika wametofautiana wasomaji wa Qur’ani katika kauli yake:

هَيْتَ لَكَ<sup>ع</sup>

**“Hayta laka.”**

‘Njoo’ Wameyasoma maneno hayo wasomaji wengi kwa fataha ya *he*, na Sekna ya *Ye* na Fataha ya *te* maana wamesoma ‘Hayta’. Amesema Ibn Abbas, na

Mujahid na wengine رضي الله عنهم maana yake ni kwamba yule mwanamke anamuita kwenye nafsi yake<sup>1</sup>. Na amesema Al-Bukhary na Ikrima.

هَيْتَ لَكَ<sup>ع</sup>

*“Haytal aka.”*

Maana yake: Njoo kwa lugha ya Kihaurani. Na kama hivyo amelitaja hilo pamoja na kukatika njia ya upokezi wake<sup>2</sup>. Na wamesoma wasomaji wengi (*Hii tu Laka*) kwa kuweka kasra ya *he* na *l* na *dhumma* ya *‘te’* (*Hiitu*) kwa maana ya kuwa nimejiandaa kwa ajili yako kutokana na kauli ya msomaji: Nimejiandaa kwa jambo (*Hiitu Bil-amri*). Na katika wale ambao kimepokewa kutoka kwake kisomo hiki ni Ibn Abbas na Abu Abdirrahman Al-Ssulamy na Abu Waili na Ikrima na Qatada na wote رضي الله عنهم wameyafasiri maneno hayo kwa maana ya: ‘Nimejiandaa kwa ajili yako.’

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهِ<sup>ط</sup> وَهَمَّ بِهَا لَوْلَا أَنْ رَأَى بُرْهَانَ رَبِّهِ<sup>ع</sup> كَذَلِكَ لَتَصْرِفَ عَنْهُ السُّوءَ

وَالْفَحْشَاءَ<sup>ع</sup> إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُخْلَصِينَ ﴿٢٤﴾

**24. Na hakika yule mwanamke alimtamani, na Yusuf angelimtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi. Hayo yamekuwa hivyo ni kwa ajili Tuepushe kwake uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja Wetu waliosafishwa.**

Pamesemwa muradi wa kutamani Yusuf عليه السلام kwa yule mwanamke ni mawazo ya mazungumzo ya nafsi. Ameyapokea maana haya Al-Baghawi kutoka kwa baadhi ya wahakiki, kisha ameileta Al-Baghawli hapa hadithi ya Abdirazzaq kutoka kwa Maamar kutoka kwa Humam kutoka kwa Abuu Huraira رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema ,

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: إِذَا هَمَّ عَبْدِي بِحَسَنَةٍ فَاكْتُبُوهَا لَهُ حَسَنَةً، فَإِنْ عَمِلَهَا فَاكْتُبُوهَا لَهُ بِعَشْرِ أَمْثَالِهَا، وَإِنْ هَمَّ بِسَيِّئَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْهَا فَاكْتُبُوهَا حَسَنَةً، فَإِنَّمَا تَرَكْنَاهَا مِنْ جَرَائِي، فَإِنْ عَمِلَهَا فَاكْتُبُوهَا بِمِثْلِهَا»

<sup>1</sup> Tabari 16:27.

<sup>2</sup> Fat’hul Bari 8:214.

*“Mwenyezi Mungu Mtukufu Amesema : atakapokusudia mja Wangu kufanya jema basi muandikieni jema, iwapo atalitenda basi muandikieni mema kumi mfano wake; na atakapolikusudia ovu na asilitende, muandikieni jema moja; hakika hapana jambo jengine, ameliacha kwa sababu Yangu, iwapo atalitenda liandikeni kwa mfano wake.”<sup>1</sup>*

Na Hadithi hii, imethibitishwa katika Sahih<sup>2</sup> ya Bukhari na Muslim, na ina matamko mengi, tamko hili ni katika matamko hayo. Ama ishara ambayo aliiona ndani yake pana kauli nyingi, amesema Ibn Jarir رحمه الله تعالى usawa ni kusemwa: ni kwamba yeye alizona ishara za Allah تعالى zina mkataza na lile ambalo alilikusudia. Na inawezekana kuwa ishara hiyo ni sura ya Ya'qub عليه السلام na inawezekana kuwa ni sura ya Malaika. Na inawezekana kuwa kile ambacho alikiona ni uthibitisho wa makatazo hayo kuhusu jambo hilo. Na hapana hoja ya mkato katika uainishaji kitu chochote katika yote hayo yaliyosemwa. Kauli sahihi zaidi kuachwa bila ya kuhusisha lolote katika hayo kama Alivyosema Allah تعالى katika Kauli Yake,

كَذَلِكَ لِيَتَصَرَّفَ عَنْهُ الشُّوْءُ وَالْفَحْشَاءُ<sup>3</sup>

***“Jambo limekuwa hivyo ili Tumuondolea ubaya na uchafu.”***

Maana yake: Kama Tulivyomuonesha dalili iliyomuepusha na lile ambalo alikuwa ndani yake, kama hivyo Tunamkinga na ubaya na uovu katika mambo yake yote.

إِنَّهُ مِنْ عِبَادِنَا الْمُخْلَصِينَ

***“Hakika yeye ni katika waja Wetu waliyoteuliwa.”***

Maana yake: Waliochaguliwa waliotakaswa – waliochaguliwa, walioteuliwa walio bora, Rehma za Mwenyezi Mungu na Amani Yake ziwe juu yake.<sup>3</sup>

\* \* \*

<sup>1</sup> Al-Baghawi 2:420

<sup>2</sup> Fat'hul Bari 13:473 Muslim 1:117.

<sup>3</sup> Tabari 16:49.

وَأَسْتَبَقَا الْبَابَ وَقَدَّتْ قَمِيصَهُ مِنْ دُبُرٍ وَأَلْفَيَا سَيِّدَهَا لَدَا  
 الْبَابِ ۗ قَالَتْ مَا جَزَاءُ مَنْ أَرَادَ بِأَهْلِكَ سُوءًا إِلَّا أَنْ يُسْجَنَ  
 أَوْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٥﴾ قَالَ هِيَ رَوَدَّتْنِي عَنْ نَفْسِي ۖ وَشَهِدَ  
 شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا إِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدٌّ مِّنْ قَبْلٍ فَصَدَقَتْ  
 وَهُوَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٢٦﴾ وَإِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدٌّ مِّنْ دُبُرٍ  
 فَكَذَبَتْ وَهُوَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٧﴾ فَلَمَّا رَأَى قَمِيصَهُ قُدًّا مِنْ  
 دُبُرٍ قَالَ إِنَّهُ مِنْ كَيْدِكُنَّ ۖ إِنَّ كَيْدَكُنَّ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾ يُوسُفُ  
 أَعْرَضَ عَنْ هَذَا ۖ وَاسْتَغْفِرِي لِذَنبِكِ ۖ إِنَّكَ كُنْتَ مِنَ  
 الْخَاطِئِينَ ﴿٢٩﴾ \* وَقَالَ نِسْوَةٌ فِي الْمَدِينَةِ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ  
 تُرَاوِدُ فَتْنَهَا عَنْ نَفْسِهِ ۖ قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا ۗ إِنَّا لَنَرْنَاهَا فِي  
 ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٣٠﴾ فَلَمَّا سَمِعَتْ بِمَكْرِهِنَّ أَرْسَلَتْ إِلَيْهِنَّ  
 وَأَعْتَدَتْ لَهُنَّ مُتَّكًا وَآتَتْ كُلَّ وَاحِدَةٍ مِّنْهُنَّ سِكِّينًا وَقَالَتْ  
 أَخْرِجْ عَلَيَّهِنَّ ۖ فَلَمَّا رَأَيْتَهُنَّ أَكْبَرْتَهُنَّ وَقَطَّعْنَ أَيْدِيَهُنَّ وَقُلْنَ حَاشَ  
 لِلَّهِ مَا هَذَا بَشَرًا إِنْ هَذَا إِلَّا مَلَكٌ كَرِيمٌ ﴿٣١﴾ قَالَتْ  
 فَذَلِكُنَّ الَّذِينَ لَمْتُنِّي فِيهِ ۖ وَلَقَدْ رَوَدَّتُّهُ عَنْ نَفْسِهِ  
 فَاسْتَعْصَمَ ۖ وَلَئِن لَّمْ يَفْعَلْ مَا ءَامُرُهُ لَيُسْجَنَنَّ وَلَيَكُونًا مِّنَ  
 الصَّغِيرِينَ ﴿٣٢﴾ قَالَ رَبِّ السِّجْنُ أَحَبُّ إِلَيَّ مِمَّا يَدْعُونَنِي  
 إِلَيْهِ ۖ وَإِلَّا تَصْرِفْ عَنِّي كَيْدَهُنَّ أَصُبُ ۖ إِلَيْهِنَّ وَأَكُن مِّنَ  
 الْجَاهِلِينَ ﴿٣٣﴾ فَاسْتَجَابَ لَهُ رَبُّهُ فَصَرَفَ عَنْهُ كَيْدَهُنَّ ۗ  
 إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٤﴾ ثُمَّ بَدَأَ لَهُمْ مِنْ بَعْدِ مَا رَأَوُا  
 الْأَيَّاتِ لَيَسْجُنُنَّهُ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٣٥﴾

وَأَسْتَبَقَا الْبَابَ وَقَدَّتْ قَمِيصَهُ مِنْ  
 دُبُرٍ وَأَلْفَيَا سَيِّدَهَا لَدَا الْبَابِ ۗ  
 قَالَتْ مَا جَزَاءُ مَنْ أَرَادَ بِأَهْلِكَ  
 سُوءًا إِلَّا أَنْ يُسْجَنَ أَوْ عَذَابٌ  
 أَلِيمٌ ﴿٢٥﴾ قَالَ هِيَ رَوَدَّتْنِي عَنْ  
 نَفْسِي ۖ وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا  
 إِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدٌّ مِّنْ قَبْلٍ  
 فَصَدَقَتْ وَهُوَ مِنَ الْكَاذِبِينَ ﴿٢٦﴾  
 وَإِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدٌّ مِّنْ دُبُرٍ  
 فَكَذَبَتْ وَهُوَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٧﴾  
 فَلَمَّا رَأَى قَمِيصَهُ قُدًّا مِنْ دُبُرٍ  
 قَالَ إِنَّهُ مِنْ كَيْدِكُنَّ ۖ إِنَّ كَيْدَكُنَّ  
 عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾ يُوسُفُ أَعْرَضَ عَنْ  
 هَذَا ۖ وَاسْتَغْفِرِي لِذَنبِكِ ۖ إِنَّكَ  
 كُنْتَ مِنَ الْخَاطِئِينَ ﴿٢٩﴾

25. Na wote wawili  
 wakakimbilia mlangoni, na  
 mwanamke akairarua  
 kanzu yake Yusuf kwa  
 nyuma. Na wakamkuta  
 bwana wake mlangoni.  
 Mwanamke akasema:  
 Hapana malipo ya mwenye

***kutaka kumfanyia maovu mkeo isipokuwa kufungwa au kupewa adhabu chungu.***

***26. Yusuf akasema: Yeye ndiye aliyenitaka bila ya mimi kumtaka. Na shahidi aliyekuwa katika jamaa za mwanamke alisema: Ikiwa kanzu yake imechanwa mbele basi mwanamke amesema kweli, naye Yusuf ni katika waongo.***

***27. Na ikiwa kanzu yake imechanwa nyuma, basi mwanamke amesema uwongo, naye Yusuf ni katika wakweli.***

***28. Basi yule bwana alipoona kanzu yake imechanwa kwa nyuma, alisema: Hakika haya ni katika vitimbi vyenu wanawake. Bila ya shaka vitimbi vyenu ni vikuu.***

***29. Yusuf! Wachilia mbali haya. Na wewe, mwanamke, omba msamaha kwa dhambi zako. Kwa hakika wewe ni katika waliofanya makosa.***

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu hali ya wakati walipotoka wakiwa wanaushindania mlango, Yusuf عليه السلام anakimbia na mwanamke anamtaka arudi nyumbani. Akamuwahi katikati na akaishika kanzu yake kwa nyuma yake, akairarua, mraruo mbaya sana. Panasemwa kwamba kanzu ilimwanguka na aliendelea Yusuf عليه السلام hali ya kukimbia na kwenda zake, hali ya kuwa mwanamke yuko nyuma yake. Wakakutana na Bwana wake, mume wa mwanamke huyo, mbele za mlango. Wakati huo mwanamke alitoka katika lile ambalo alikuwemo ndani yake kwa vitimbi na vituko vyake na akamuambia mume wake kwa kujinasua na kumsingizia Yusuf عليه السلام, kuwa alitaka kum-baka:

مَا جَزَاءُ مَنْ أَرَادَ بِأَهْلِكَ سُوءًا

***“Ni malipo gani ya mtu ambaye ametaka kwa mke wako ubaya?”***

Maana yake: Uchafu,

إِلَّا أَنْ يُسَجَّنَ

***“Isipokuwa ni kufungwa.”*** Maana yake: kutiwa jela,

أَوْ عَذَابٍ أَلِيمٍ

***“Au adhabu yenye kuumiza.”***



Maana yake: Atapigwa pigo kubwa lenye kuumiza. Wakati huo Yusuf عليه السلام alipata ushindi kwa kunusurika na kufanya vitendo vichafu, na alijitakasa na lile ambalo alimsingizia kwalo miongoni mwa kutaka kum-baka.

قَالَ

**“Akasema.”**

Hali ya kuwa mwema mkweli,

هِيَ رَاوَدَتْنِي عَنْ نَفْسِي

**“Yeye ndiye aliyenitaka mimi kuitaka nafsi yangu.”**

Na akataja kwamba mwanamke huyo alimfuata nyuma hali ya kuwa anamvutia kwake mpaka akararua kanzu yake.

وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا إِن كَانَ قَمِيصُهُ قُدِّمَ مِنْ قَبْلِ

**“Na akashuhudia shahidi katika watu wa mwanamke – kwa kusema ikiwa kanzu yake imekatwa kwa mbele.”**

Maana yake: Kwa mbele yake,

فَصَدَقَتْ

**“...huyo mwanamke amesema kweli.”**

Maana yake: Katika maneno yake kwamba Yusuf عليه السلام amemtaka kutenda naye zinaa. Kwa sababu kama Yusuf عليه السلام atakuwa wakati alipomuita na akamkatalia alimsukuma katika kifua chake, mwanamke akaichana kanzu yake, kwa hiyo aliyoyasema yatakuwa sahihi.

وَإِنْ كَانَ قَمِيصُهُ قُدِّمَ مِنْ دُبُرٍ فَكَذَبَتْ وَهُوَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٦﴾

**“Na ikiwa kanzu yake imekatwa kwa nyuma mwanamke atakuwa mrongo na yeye atakuwa miongoni mwa watu wa kweli.”**

Na hilo litakuwa kama lilivyotokea wakati alipomkimbia na akawa anamfuata na aliikamata kanzu yake kwa nyuma yake ili amrudishe kwake, matokeo yake akaichana kanzu yake. Kwa hakika wametofautiana wapokezi wa kisa hiki kuhusu huyo shahidi. Je shahidi huyo ni mdogo au mkubwa? Amepokea Abdurazzaq kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا

**“Na akashuhudia shahidi katika watu wake.”**

Amesema: Alikuwa mwenye ndevu. Na amesema Thauri kutoka kwa Jabir kutoka kwa Abuu Mulaika, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, alikuwa katika watu wanaomhusu mfalme. Na kama hivi, amesema Mujahid na Ikrimah na Al-Hassan na Qatada na Assudiy na Muhammad bin Ishaqa na wengine kwamba, alikuwa mwanamume. Na amesema Al-Awfi kutokana na Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake,

وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا

**“Na akashuhudia shahidi katika watu wake.”**

Amesema: Alikuwa mtoto mdogo<sup>1</sup> katika rika la ulezi. Na kama hivi pamepokewa kutoka kwa Abuu Huraira na Hilali Bin Yasaf na Al-Hassan na Saeed bin Jubair na Adhahak bin Muzahim: Kwamba yeye alikuwa mtoto mdogo katika nyumba<sup>2</sup> ile. Na ameichagua kauli hii Ibn Jariri رحمه الله تعالى. Na Kauli Yake,

فَلَمَّا رَأَىٰ قَمِيصَهُ قُدَّ مِنْ دُبُرٍ

**“Alipoiona kanzu yake imekatwa kwa nyuma.”**

Maana yake: Alipohakikisha mume wake ukweli wa Yusuf عليه السلام na urongo wa mkewe katika lile ambalo amemsingizia kwalo Yusuf عليه السلام.

قَالَ إِنَّهُ مِنْ كَيْدِكُنَّ

**“Alisema hakika uzushi huu ni katika vitimbwi vyenu.”**

Maana yake: Hakika huu uzushi na upakaziaji ambao umeichafua heshima ya kijana huyu, kwa wanawake ni miongoni mwa vituko vyenu.

إِنَّ كَيْدِكُنَّ عَظِيمٌ

**“Kwani vituko vyenu ni vikubwa sana.”**

Kisha akasema akimuamrisha Yusuf عليه السلام kuyaficha yale ambayo yametokea:

<sup>1</sup> Tabari 16:56.

<sup>2</sup> Tabari 16:54-55.

يُوسُفُ أُعْرِضْ عَن هَذَا<sup>ع</sup>

**“Ee Yusuf yapuuze haya.”**

Maana yake: Yaachilie mbali. Maana: Usiyataje kwa mtu yeyote.

وَأَسْتَغْفِرِي لِدُنُوبِكِ<sup>ط</sup>

**“Nawe taka msamaha kwa makosa yako.”**

Maneno haya alimuambia mke wake na huyu mume alikuwa mlaini wa tabia na mwepesi wa kusamehe. Ni kwamba yeye alimsamehe mkewe kwa sababu alijua kuwa ni vigumu mwanamke yeyote kuweza kuvumilia hayo. Akamuambia: Taka msamaha wa dhambi zako. Maana: Ambazo umezifanya wewe miongoni mwa kutaka ubaya kwa kijana huyo na kumsingizia jambo ambalo yeye hahusiki nalo.

إِنَّكَ كُنْتَ مِنَ الْخَاطِئِينَ ﴿٣٠﴾

**“Kwa hakika wewe ulikuwa ni katika wenye makosa.”**

\* وَقَالَ نِسْوَةٌ فِي الْمَدِينَةِ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ تُرَاوِدُ فَتَاهَا عَن نَّفْسِهِ<sup>ط</sup> قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا إِنَّا لَنَرَاهَا فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٩﴾ فَلَمَّا سَمِعَتْ بِمَكْرِهِنَّ أَرْسَلَتْ إِلَيْهِنَّ وَأَعْتَدَتْ لَهُنَّ مُتَكًا وَءَاتَتْ كُلَّ وَاحِدَةٍ مِّنْهُنَّ سِكِّينًا وَقَالَتِ اخْرُجْ عَلَيْهِنَّ<sup>ط</sup> فَلَمَّا رَأَيْنَهُ أَكْبَرْتَهُ وَقَطَّعْنَ أَيْدِيَهُنَّ وَقُلْنَ حَاشَ لِلَّهِ مَا هَذَا بَشَرًا إِنْ هَذَا إِلَّا مَلَكٌ كَرِيمٌ ﴿٣٠﴾ قَالَتْ فَذَلِكُنَّ الَّذِينَ لُمْتُنَّنِي فِيهِ<sup>ط</sup> وَلَقَدْ رَاوَدْتُهُ عَن نَّفْسِهِ فَاسْتَعْصَمَ<sup>ط</sup> وَلَئِن لَّمْ يَفْعَلْ مَا آمُرُهُ لَيَسْجَنَنَّ وَلَيَكُونَا مِنَ الصَّاغِرِينَ ﴿٣١﴾ قَالَ رَبِّ السِّجْنُ أَحَبُّ إِلَيَّ مِمَّا يَدْعُونَنِي إِلَيْهِ<sup>ط</sup> وَإِلَّا تَصْرِفْ عَنِّي كَيْدَهُنَّ أَصْبُ إِلَيْهِنَّ وَأَكُن مِّنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٣٢﴾ فَاسْتَجَابَ لَهُ رَبُّهُ فَصَرَفَ عَنْهُ كَيْدَهُنَّ<sup>ع</sup> إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٣﴾

**30. Na wanawake wa mjini wakawa wanasema: Mke wa Mheshimiwa anamtamani mtumishi wake! Hakika amesalitika kwa mapenzi. Sisi hakika tunamuona yumo katika upotovu ulio dhaahiri.**

**31. Aliposikia yule bibi masengenyo yao aliwaita, na akawawekea matakia ya kuegemea, na akampa kila mmoja wao kisu. Akamuambia Yusuf: Tokeza mbele yao. Basi walipomuona waliona ni kitu kikubwa kabisa, na wakajikata mikono yao. Wakasema: Hasha Lillahi! Huyu si mwanaadamu. Hakuwa huyu ila ni Malaika Mtukufu.**

**32. Yule bibi akasema: Huyu basi ndiye huyu mliyenilaumia! Na kweli mimi nilimtaka naye akakataa. Na asipofanya ninayomuamrisha basi hapana shaka atafungwa gerezani, na atakuwa miongoni mwa walio chini kabisa.**

**33. Yusuf akasema: Ee Mola Mlezi wangu! Nastahabu kifungo kuliko haya anayoniitia. Na usiponiondoshea vitimbi vya wanawake mimi nitamili kwao, na nitakuwa katika wajinga.**

**34. Basi Mola wake Mlezi Akamuitikia, na Akamuondoshea vitimbi vyao. Hakika Yeye ni Msikizi Mjuzi.**

**Habari Zinawafikia Wanawake wa Mji Ambao Nao Wanakula Njama Dhidi ya Yusuf عليه السلام**

Allah تعالى Anaeleza kuwa habari za yaliyojiri kati ya mke wa Mheshimiwa na Yusuf عليه السلام zilienea katika mji. Yaani, Misri, na watu wakazijadili,

﴿ وَقَالَ نِسْوَةٌ فِي الْمَدِينَةِ ﴾

**“Na wanawake wa mjini wakawa wanasema.”**

Kama vile wake wa wakuu na wana wa wafalme, wakasema, kwa kumkemea na kumkosoa mke wa ‘Aziz, Mheshimiwa.

أَمْرَأَتِ الْعَزِيزِ تُرَاوِدُ فَتْلَهَا عَنِ نَفْسِهِ ط

**“...Mke wa Mheshimiwa anamtamani mtumishi wake!”**

Anamhadaa mtumishi wake amuingilie kimwili,

قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا ط

**“...Hakika amesalitika kwa mapenzi...”** Penzi limejaa moyoni mwake,

إِنَّا لَنَرْنَهَا فِي صَلَٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٢٥﴾

**“...Sisi hakika tunamuona yumo katika upotovu ulio dhaahiri.”**

Kwa kumpenda na kujaribu kumshawishi mtumishi wake.

فَلَمَّا سَمِعَتْ بِمَكْرِهِنَّ

**“Alipo sikia yule bibi masengenyo yao.”**

Hususani kauli yao, “anampenda mno.” Muhammad bin Is’haq رحمه الله تعالى amesema, “Walisikia uzuri wa Yusuf عليه السلام, wakataka kumuona, wakasema hayo ili wamuone,

أَرْسَلَتْ إِلَيْهِنَّ

**“...aliwaita...”** Aliwaalika nyumbani kwake,

وَأَعْتَدَتْ لَهُنَّ مُتَّكًا

**“... na akawawekea matakia ya kuegemea...”**

Ibn ‘Abbas, Said bin Jubayr, Mujahid, Al-Hasan, As-Suddi na wengine رضي الله عنهم walisema kuwa aliandaa chumba na makochi, mito (ya kuegemea) na chakula kilichohitaji visu vya kukatia, kama vile machungwa.<sup>1</sup> Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

وَأَتَتْ كُلَّ وَاحِدَةٍ مِّنْهُنَّ سِكِّينًا

**“...na akampa kila mmoja wao kisu...”**

Kama sehemu ya mpango wake wa kisasi chake kwa hila zao za kutaka kumuona Yusuf عليه السلام.

وَقَالَتْ أَخْرِجْ عَلَيْنَّ

**“...Akamuambia Yusuf tokeza mbele yao...”**

Kwani alimuomba abakie katika sehemu nyingine ya nyumba.

فَلَمَّا رَأَيْتَهُ أُكْبِرْتَهُ

**“Basi walipomuona waliona ni kitu kikubwa kabisa.”**

<sup>1</sup> Tabari 16:71-72.

Walifikiria sana na kustaajabia walichokiona. Wakajikata mikono yao kwa kushangaa uzuri wake, huku wakidhani kuwa walikuwa wakikata machungwa kwa visu vyao. Hivyo, walijikata mikono kwa visu walivyokuwa navyo, kwa mujibu wa taarifa za *Tafsir*.<sup>1</sup>

Wengine walisema kuwa walipotulia, na baada ya machungwa kuwekwa mbele yao, huku akimpa kisu kila mmoja, mke wa 'Aziz Mheshimiwa aliwauliza, "Mngependa kumuona Yusuf عليه السلام?" Wakaitikia, "Ndiyo." Akaagiza aje mbele yao, walipomuona walianza kujikata mikono. Akaagiza awe anapitapita, ili wamuone pande zote, na akarejea huku wakiendelea kujikata. Walipoumia, walipiga kelele. Akawauliza, "Mmefanya hayo kwa kumuona mara moja tu, basi kwanini nilaumiwe?"

وَقَطَّعْنَ أَيْدِيَهُنَّ وَقُلْنَ حَسْبَ اللَّهِ مَا هَذَا بَشَرًا إِنْ هَذَا إِلَّا مَلَكٌ كَرِيمٌ ﴿١٦٨﴾

**"...na wakajikata mikono yao. Wakasema: Hasha Lillahi! Huyu si mwanaadamu. Hakuwa huyu ila ni Malaika Mtukufu..."**

Wakamuambia, "Hatutakulaumu baada ya kuona tuliyoyaona." Hawakupata kumuona yeyote kama Yusuf عليه السلام hapo kabla. Kwani yeye alipewa nusu ya uzuri wote. Hadithi sahihi inaeleza kuwa Mtume ﷺ alimkuta Nabii Yusuf عليه السلام, wakati wa safari ya Usiku wa *Isra*<sup>2</sup> katika mbingu ya tatu na akasema,

«فَإِذَا هُوَ قَدْ أُعْطِيَ شَطْرَ الْحُسْنِ»

"Yeye alipewa nusu ya uzuri wote."

Imesimuliwa kutoka kwa Mujahidi kutoka kwa Rabiah Al-Jurashi amesema: "Uzuri umegawanywa sehemu mbili Yusuf عليه السلام na mama yake."

مَا هَذَا بَشَرًا

**"Huyu si mwanaadamu."<sup>3</sup>**

Kisha wakasema,

<sup>1</sup> Tabari 16:76-78.

<sup>2</sup> Safari ya usiku kutoka Makkah mpaka Jerusalem, kisha mbinguni, halafu kurejea Makkah.

<sup>3</sup> Muslim 1:146.

<sup>4</sup> Tabari 16:84.

إِنَّ هَذَا إِلَّا مَلَكٌ كَرِيمٌ ﴿٢٥﴾ قَالَتْ فَذَلِكُنَّ الَّذِي لُمْتُنَّنِي فِيهِ ۖ

**“...Hakuwa huyu ila ni Malaika Mtukufu. Yule bibi akasema: Huyu basi ndiye huyu mliyenilaumia!”**

Alisema maneno hayo ili waone udhuru walichokifanya, kwani mwenye kuuona uzuri huo, anastahiki kupendwa, akaungama kwa kusema.

وَلَقَدْ رَاودْنَاهُ عَنْ نَفْسِهِ فَاسْتَعْصَمَ ۖ

**“Na kweli mimi nilimtaka naye akakataa.”**

Kunitii. Wanazuoni wengine walisema kuwa wanawake walipouona uzuri wa Yusuf عليه السلام, aliwaeleza uzuri wake wa ndani zaidi ambao hawakuwa wakiujua, nao ni utanashati na staha. Halafu akamtishia,

وَلَيْن لَّمْ يَفْعَلْ مَاءَ امْرَأَةٍ لَّيْسَجَنَّ وَلْيَكُونَا مِنَ الصَّاغِرِينَ ﴿٢٦﴾

**“Na asipofanya ninayo muamrisha basi hapana shaka atafungwa gerezani, na atakuwa miongoni mwa walio chini kabisa.”**

Hayo ni pale Nabii Yusuf عليه السلام alipojikinga kwa Allah تعالى dhidi ya shari yao na hila zao,

قَالَ رَبِّ اللَّيْسَجُنُّ أَحَبُّ إِلَيَّ مِمَّا يَدْعُونَنِي إِلَيْهِ ۖ

**“...Akasema: Ee Mola Mlezi wangu! Nastahabu kifungo kuliko haya anayo niitia...”**

Mambo ya zinaa,

وَأَلَّا تَصْرِفَ عَنِّي كَيْدَهُنَّ أَصْبُ إِلَيْهِنَّ ۖ

**“Na usiponiondoshea vitimbi vya wanawake mimi nitamili kwao.”**

Yusuf عليه السلام alimuomba Allah تعالى: Ukiniacha nami nikajitegemea, basi mimi sina uwezo, wala siwezi kujidhuru wala kujinufaisha, isipokuwa ukitaka Wewe. Hakika, Wewe unahitajiwa na kila kitu, na tunakutegemea Wewe Peke Yako kwa kila jambo, Usiniache peke yangu, kisha,

أَصْبُ إِلَيْهِنَّ وَأَكُن مِّنَ الْجَاهِلِينَ ﴿٢٧﴾ فَاسْتَجَابَ لَهُ رَبُّهُ ۖ

**“...na nitakuwa katika wajinga. Basi Mola wake Mlezi akamuitikia.”**

Yusuf عليه السلام, aliepushwa na makosa kwa Utashi wa Allah تعالى, na Alimuokoa dhidi ya kukubali ushawishi wa mke wa Mheshimiwa 'Aziz'. Alichagua jela, badala ya kukubali wito wake haramu. Hii inadhihirisha daraja ya juu kabisa katika hali hii, kwani Yusuf عليه السلام alikuwa kijana, aliye balebale, mzuri na mkamilifu kiutu. Mke wa mkuu wake mwenyewe alimtaka, na alikuwa mke wa Mheshimiwa 'Aziz wa Misri. Yeye pia alikuwa mzuri na tajiri, pia alikuwa na nafasi ya juu katika jamii. Yusuf عليه السلام alikataa yote hayo na akachagua jela, kwani alimcha Allah تعالى na alitumaini kupata malipo Yake. Imenukuliwa katika Sahihi Mbili kuwa Mtume ﷺ amesema,

«سَبْعَةٌ يُظِلُّهُمُ اللَّهُ فِي ظِلِّهِ يَوْمَ لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّهُ: إِمَامٌ عَادِلٌ، وَنِسَاءٌ نَشَأَ فِي عِبَادَةِ اللَّهِ، وَرَجُلٌ قَلْبُهُ مُعَلَّقٌ بِالْمَسْجِدِ إِذَا خَرَجَ مِنْهُ حَتَّى يَعُودَ إِلَيْهِ، وَرَجُلَانِ تَحَابَّا فِي اللَّهِ، اجْتَمَعَا عَلَيْهِ وَتَفَرَّقَا عَلَيْهِ، وَرَجُلٌ نَصَدَّقَ بِصَدَقَةٍ فَأَخْفَاهَا حَتَّى لَا تَعْلَمَ شِمَالُهَا مَا أَنْفَقَتْ يَمِينُهُ، وَرَجُلٌ دَعَتْهُ امْرَأَةٌ ذَاتُ مَنْصِبٍ وَجَمَالٍ فَقَالَ: إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ، وَرَجُلٌ ذَكَرَ اللَّهَ خَالِيًا فَفَاضَتْ عَيْنَاهُ»

*“Allah Atawapa kivuli watu saba, katika Siku ambapo hakutakuwa na kivuli kingine isipokuwa Chake Yeye: Mtawala muadilifu, kijana aliyekulia katika kumuabudu Allah, mtu ambaye moyo wake umefungamana na Masjid, tangu anapotoka katika Masjid mpaka anaporejea, watu wawili waliopendana kwa ajili ya Allah na kuachana kwa ajili ya Allah tu, Mtu anayetoa sadaka kisiri kiasi kwamba mkono wake wa kushoto haujui kinachotolewa na mkono wa kulia; mtu anayekataa wito, wa mwanamke mzuri wa uzao wa heshima, kwa ajili ya kuzini naye na akasema: “Ninamcha Allah”. Na mwenye kumkumbuka Allah katika faragha kisha macho yake yakabubujika machozi.”<sup>1</sup>*

ثُمَّ بَدَأَ هُمْ مِّنْ بَعْدِ مَا رَأَوْا الْآيَاتِ لَيْسَ جُنَّتَهُ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٣٥﴾

**35. Basi ikawadhihirikia baada ya kuona Ishara kuwa wamfungue kwa muda.**

<sup>1</sup> Fat'hul Bari 2:168, Muslim 2:715



**Yusuf عليه السلام Anafungwa Bila Uthibitishaji wa Haki**

Allah تعالى Anasema kisha ikawadhihirikia wao maslahi katika lile ambalo waliliona kwamba wamfungwe kwa muda fulani. Na hilo, ni baada ya kujua kutohusika kwake na machafu. Zikadhihiri alama mbalimbali nazo ni zile zenye kufahamisha juu ya ukweli wake. Katika kujichunga na machafu na usafi wake. Wao (Allah تعالى Ndiye Mjuzi) hawakuwa na kisingizio kingine ila waliamua kumfunga yalipoenea mazungumzo ya kumsingizia kwamba yeye alimtaka mke wa Mheshimiwa pasi na kuwa yule mwanamke kumtaka yeye, na kwamba wao walimfunga kwa kisingizio hicho. Na kwa sababu hiyo wakati alipomtaka Mfalme Mkuu atoke gerezani alikataa kutoka, mpaka lile alilosingiziwa liwe wazi. Na alipothibitishiwa kuwa ni mtu msafi ndio alitoka gerezani akiwa hana tuhuma yoyote, mwenye heshima kamili (Rehema za Mwenyezi Mungu na Amani Yake ziwe juu yake).



وَدَخَلَ مَعَهُ السِّجْنَ فَتَيَانٍ ۗ قَالَ أَحَدُهُمَا إِنِّي أَرَانِي أَعْصِرُ  
 خَمْرًا ۗ وَقَالَ الْآخَرُ إِنِّي أَرَانِي أَحْمِلُ فَوْقَ رَأْسِي خُبْرًا  
 تَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْهُ ۗ نَبِّئْنَا بِتَأْوِيلِهِ ۗ إِنَّا نَرَاكَ مِنَ  
 الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٦﴾ قَالَ لَا يَأْتِيكُمَا طَعَامٌ تُزْزَقَانِيَهُ إِلَّا  
 نَبِّأْتُكُمَا بِتَأْوِيلِهِ قَبْلَ أَنْ يَأْتِيَكُمَا ۗ ذَلِكُمْ مِمَّا عَلَّمَنِي  
 رَبِّي ۗ إِنِّي تَرَكْتُ مِلَّةَ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ  
 كَافِرُونَ ﴿٣٧﴾ وَأَتَّبَعْتُ مِلَّةَ آبَائِي إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ  
 وَيَعْقُوبَ ۗ مَا كَانَ لَنَا أَنْ نَشْرِكَ بِاللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ۗ ذَلِكُمْ  
 مِنْ فَضْلِ اللَّهِ عَلَيْنَا وَعَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا  
 يَشْكُرُونَ ﴿٣٨﴾ يَبْصُرِي السِّجْنَ ۗ أَرْبَابٌ مُتَفَرِّقُونَ  
 خَيْرٌ أَمِ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٣٩﴾ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِهِ  
 إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ مِمَّا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا  
 مِنْ سُلْطَانٍ ۗ إِنَّ الْحَكْمَ إِلَّا لِلَّهِ ۗ أَمَرَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ۗ  
 ذَلِكُمْ الدِّينَ الْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٠﴾  
 يَبْصُرِي السِّجْنَ ۗ أَمَّا أَحَدُكُمَا فَيَسْقِي رَبَّهُ خَمْرًا ۗ وَأَمَّا  
 الْآخَرُ فَيُصَلِّبُ فَتَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْ رَأْسِهِ ۗ قُضِيَ الْأَمْرُ  
 الَّذِي فِيهِ تَسْتَفْتِيَانِ ﴿٤١﴾ وَقَالَ لِلَّذِي ظَنَّ أَنَّهُ نَاجٍ  
 مِثْمَا أذْكُرَنِي عِنْدَ رَبِّكَ فَأَدْنَسَهُ الشَّيْطَانُ ذِكْرَ رَبِّهِ  
 فَلَبِثَ فِي السِّجْنِ بِضْعَ سِنِينَ ﴿٤٢﴾

وَدَخَلَ مَعَهُ السِّجْنَ فَتَيَانٍ ۗ قَالَ  
 أَحَدُهُمَا إِنِّي أَرَانِي أَعْصِرُ خَمْرًا ۗ  
 وَقَالَ الْآخَرُ إِنِّي أَرَانِي أَحْمِلُ فَوْقَ  
 رَأْسِي خُبْرًا تَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْهُ ۗ نَبِّئْنَا  
 بِتَأْوِيلِهِ ۗ إِنَّا نَرَاكَ مِنَ  
 الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٦﴾

**36. Wakaingia gerezani pamoja naye vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika mimi nimeota nakamua mvinyo. Na mwingine akasema: Mimi nimeota nimebeba mikate juu ya kichwa changu, na ndege wanaila. Hebu tuambie tafsiri yake, kwani sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.**

**Wafungwa Wawili Wana- muomba Yusuf عليه السلام Kuwafasiria Ndoto Zao**

Qatadah amesema alikuwa mmoja wao ni mwandazi wa Mfalme na mwingine alikuwa mtengenezaji wa mikate<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Tabari 16:95.

Kisha ni kwamba wao waliota ndoto wakataka tafsiri yake.

قَالَ لَا يَايَّتِكُمْ طَعَامٌ تُرْزَقَانِيهِ إِلَّا نَبَأْتُكُمْ بِتَأْوِيلِهِ قَبْلَ أَنْ يَأْتِيَكُمَا ۚ ذَلِكُمَا مِمَّا  
 عَلَّمَنِي رَبِّي ۚ إِنِّي تَرَكْتُ مِلَّةَ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَهُمْ بِالْآخِرَةِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٣٧﴾ وَأَتَّبَعْتُ  
 مِلَّةَ آبَائِي ۖ إِنَّهُمْ إِسْرَافُونَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۚ مَا كَانَ لَنَا أَنْ نَشْرِكَ بِاللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ۚ ذَلِكَ  
 مِنْ فَضْلِ اللَّهِ عَلَيْنَا وَعَلَى النَّاسِ وَلَئِنْ أُكْثِرَ النَّاسُ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٣٨﴾

**37. Akasema: Hakitakufikilieni chakula mtakachopewa ila nitakuambieni hakika yake kabla hakijakufikieni. Haya ni katika yale Aliyonifundisha Mola wangu Mlezi. Hakika mimi nimeacha mila ya watu wasiomuamini Mwenyezi Mungu, na wakawa hawaiamini Akhera.**

**38. Na nimefuata mila ya baba zangu, Ibrahim, na Is-haq, na Yaa'qub. Hatuna haki ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote. Hiyo ni katika fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yetu na juu ya watu; lakini watu wengi hawashukuru.**

**Wito wa Yusuf عليه السلام kwa Wafungwa Wawili Wampwekeshe Mwenyezi Mungu Kabla ya Kufasiri Ndoto Zao**

Yusuf عليه السلام anawaeleza kwamba wao wakati wowote watakapoota katika usingizi ndoto yoyote, kwa hakika yeye anajua tafsiri yake, atawaeleza tafsiri yake kabla ya kutuka kwake, na kwa sababu hiyo amesema:

لَا يَايَّتِكُمْ طَعَامٌ تُرْزَقَانِيهِ إِلَّا نَبَأْتُكُمْ بِتَأْوِيلِهِ

**“Hakitawajia chakula chochote ambacho, mtaruzukiwa isipokuwa nitawaeleza tafsiri yake.”**

Amesema Mujahid: Anasema:

لَا يَايَّتِكُمْ طَعَامٌ تُرْزَقَانِيهِ

**“Hakitawajia chakula chochote ambacho mnaruzukiwa.”**

Katika siku yenu,

إِلَّا نَبَأْتُكُمَا بِتَأْوِيلِهِ قَبْلَ أَنْ يَأْتِيَكُمَا<sup>٤</sup>

***“Isipokuwa nitawaelezeni tafsiri yake kabla ya kuwajieni.”***

Na kama hivyo amesema Assudiy<sup>1</sup>. Kisha akasema: Na hili hakika si vingine, jambo hili ni katika mafunzo ya Allah تعالی kwangu kwa sababu mimi nimejipusha na mila ya makafiri wanaomkufuru Allah تعالی na siku ya mwisho, ambao hawataraji malipo wala adhabu huko akhera.

وَاتَّبَعْتُ مِلَّةَ آبَائِي إِبْرَاهِيمَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ<sup>٥</sup>

***“Na nimeifuata mila ya Baba zangu: Ibrahim na Is’haq na Yaaqub”***

Yusuf عليه السلام anasema: Nimehama njia ya ukafiri na ushirikina na nimefuata njia ya hawa Mitume - Rehema za Allah تعالی na Amani ziwe juu yao wote, na hivi ndivyo inavyokuwa hali ya mwenye kufuata njia ya uongofu na njia ya Mitume, na akaipa nyongo njia ya waliopotea. Kwani, Allah تعالی Huongoza moyo wake na Humfundisha mambo ambayo hakuwa anayajua na Humfanya kuwa ni kiongozi anayefuatwa katika kheri na mwenye kulingania kwenye njia ya uongofu.

مَا كَانُوا لَنَا أَنْ نُشْرِكَ بِاللَّهِ مِنْ شَيْءٍ<sup>٤</sup> ذَلِكَ مِنْ فَضْلِ اللَّهِ عَلَيْنَا وَعَلَى النَّاسِ

***“Hakukuwa kunatufalia kumshirikisha na Mwenyezi Mungu kitu chochote hiyo ni Fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yetu na juu ya watu.”***

Upwekesho huu ni kukiri kwamba hapana Mola anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Peke Yake hana mshirika.

مِنْ فَضْلِ اللَّهِ عَلَيْنَا

***“...Na katika wema wa Mwenyezi juu yetu...”***

Ameleta wahyi kwetu na Ametuamrisha kwayo.

وَعَلَى النَّاسِ

***“Na juu ya watu.”***

Kwani Ametufanya ni walinganiaji kwao kwenye jambo hilo.

<sup>1</sup> Tabari 16:100.

وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٣٦﴾

**“Isipokuwa watu wengi hawashukuru.”**

Hawaelewi neema za Allah تعالی juu yao kwa Kuwapeleka Mitume kwao bali ni kwamba,

بَدَلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ﴿٣٧﴾

**“...wameibadili neema ya Mwenyezi Mungu kuwa ni kukufuru na wakawatumbukiza watu wao katika nyumba ya maangamivu.”**  
(14:28)

يَصْلِحِي السَّجْنَ ءَأَرْتَابٌ مُتَفَرِّقُونَ خَيْرٌ أَمِ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٣٨﴾ مَا تَعْبُدُونَ  
مِنْ دُونِهِ ءِإِلَّا أَسْمَاءٌ سَمِيَّتُوهَا أَنْتُمْ وءَابَاؤُكُمْ مِمَّا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ ءِإِنِ  
الْحُكْمُ ءِإِلَّا لِلَّهِ ءِأَمْرٌ ءِأَلَّا تَعْبُدُوا ءِإِلَّا ءِإِيَّاهُ ءِذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا

يَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾

**39. Enyi wafungwa wenzangu wawili! Je, mabwana wengi wanaofarikiana wao kwa wao ni bora au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye Nguvu?**

**40. Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyoyapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo Dini Iliyonyooka. Lakini watu wengi hawajui.**

Kisha Yusuf عليه السلام aliwaelekea vijana wawili kwa kuwasemesha na kuwalingania kumuabudu Allah تعالی Peke Yake Asiyeye na mshirika na kuachana na miungu mingine miongoni mwa masanamu wanayoyaabudu jamaa zao akasema:

ءَأَرْتَابٌ مُتَفَرِّقُونَ خَيْرٌ أَمِ اللَّهُ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٣٨﴾

**“Hivi waungu mbali mbali ni bora au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye Kutenza Nguvu.”**

Maana yake: Yule ambaye kimenyenyekea Kwake kila kitu kutokana na Utukufu Wake, na Ukubwa wa Ufalme Wake. Yusuf عليه السلام kisha aliwawekea wazi kwamba masanamu ambayo wanayaabudu na ambayo wanayaita kuwa waungu, hakika hapana jambo jengine ni ujinga kutoka kwao na uhitaji wenye kutokana na wao wenyewe, wameupokea waliokuja nyuma kutoka kwa waliotangulia, na halina hilo mategemeo yoyote mbele ya Allah تعالى na kwa sababu hiyo amesema:

مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطَانٍ

***“Hakuteremsha Mwenyezi Mungu kwa hayo Masanamu hoja yoyote.”***

Maana yake: Hoja na ushahidi wowote, kisha akawaeleza kwamba kuhukumu na kuyafanya mambo na matakwa na ufalme, vyote hivyo ni vya Allah تعالى. Na Amewaamrisha waja Wake wote wasimuabudu yoyote asiyekuwa yeye.

Kisha Allah تعالى Amesema:

ذَلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ

***“Hiyo ndiyo Dini Iliyonyooka.”***

Maana yake: Hili ambalo ninawalinganieni kwalo, miongoni mwa kumpwekesha Allah تعالى na Kumtakasia matendo, kufanya hivyo ndiyo dini iliyonyooka ambayo Ameerisha Allah تعالى kuifuata, na Ameteremsha kwa dini hiyo hoja na ushahidi, dini ambayo Anaipenda na Anairidhia.

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٣﴾

***“Isipokuwa watu wengi hawaelewi.”***

Maana: Kwa sababu hiyo wamekuwa wengi wao wanamshirikisha Allah تعالى.

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

***“Na hawakuwa watu wengi ijapokuwa na pupa juu ya kuwa waumini si wenye kuamini.” (12:103)***

Yusuf عليه السلام alipomaliza kuwalingania alianza kufasiri ndoto yao, akasema:

يَنْصَلِحِي السِّجْنَ أَمَا أَحَدُكُمَا فَيَسْقِي رَبَّهُ خَمْرًا<sup>ط</sup> وَأَمَا الْآخَرُ فَيُصَلِّبُ فَتَأْكُلُ الطَّيْرُ  
 مِنْ رَأْسِهِ<sup>ع</sup> قُضِيَ الْأَمْرُ الَّذِي فِيهِ تَسْتَفْتِيَانِ ﴿٤١﴾

**41. Enyi wafungwa wenzangu wawili! Ama mmoja wenu atamnyweshwa bwana wake mvinyo. Na ama mwengine atasulubiwa, na ndege watamla kichwa chake. Imekwisha katwa hukumu ya hilo jambo mlilokuwa mkiuliza.**

### Kufasiri Ndoto

Yusuf عليه السلام alisema,

يَنْصَلِحِي السِّجْنَ أَمَا أَحَدُكُمَا فَيَسْقِي رَبَّهُ خَمْرًا<sup>ط</sup>

**“Enyi wafungwa wenzangu wawili! Ama mmoja wenu atamnyweshwa bwana wake mvinyo.”**

Kumuambia aliyeota ndotoni kwamba alikuwa akikamua mvinyo. Hakumuambia hayo moja kwa moja, bali, ili kupunguza huzuni za yule mwingine. Ndio sababu hakusema maneno moja kwa moja,

وَأَمَا الْآخَرُ فَيُصَلِّبُ فَتَأْكُلُ الطَّيْرُ مِنْ رَأْسِهِ<sup>ع</sup>

**“Na ama mwengine atasulubiwa, na ndege watamla kichwa chake.”**

Ambayo ni tafsiri ya ndoto ya yule aliyeota kuwa amebeba mkate kichwani kwake. Yusuf عليه السلام aliwaambia kuwa uamuzi wa suala lao tayari umechukuliwa na utapita. Haya ni kwa sababu ndoto imefungamana na mguu wa ndege, inapokuwa bado kufasiriwa. Ikishafasiriwa, inakuwa kweli. Ath-Thawri رضي الله عنه alisema kwamba ‘Umarah bin Al-Qa’qa رضي الله عنه alisimulia kuwa Ibrahim alisema, ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Walipomuambia maneno yao, na yeye kuwafasiria ndoto zao, walijibu, ‘Hatujaona chochote.’ Haya ni pindi waliposema,

قُضِيَ الْأَمْرُ الَّذِي فِيهِ تَسْتَفْتِيَانِ

**“Imekwisha katwa hukumu ya hilo jambo mlilokuwa mkiuliza.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:108.

Ufahamu wa hayo ni kwamba anayedai kuwa ameota ndoto na akapewa tafsiri yake, atafungamana na tafsiri yake, na Allah تعالى Anajua zaidi. Kuna Hadithi tukufu aliyokusanya Imam Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Mu'awiyah bin Haydah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الرُّؤْيَا عَلَى رِجْلِ طَائِرٍ مَا لَمْ تُعْبَرْ، فَإِذَا عُبِرَتْ وَقَعَتْ»

*“Ndoto imefungamana na mguu wa ndege, madam haijafasiriwa. Ikifasiriwa, inatimia.”<sup>1</sup>*

وَقَالَ لِلَّذِي ظَنَّ أَنَّهُ نَاجٍ مِّنْهُمَا اذْكُرْنِي عِنْدَ رَبِّكَ فَأَنَسَهُ الشَّيْطَانُ ذِكْرَ رَبِّهِ  
فَلَبَسَ فِي السِّجْنِ بِضَعِّ سِنَّينَ ﴿٤٢﴾

**42. Na akamuambia yule aliyejua kuwa atavuka katika wale wawili: Nikumbuke kwa bwana wako. Lakini Shet’ani alimsahaulisha kumtaja kwa bwana wake. Basi Yusuf akakaa gerezani miaka kadhaa.**

**Yusuf عليه السلام Anamuomba Mkamuaji Mvinyo wa Mfalme Ataje Shauri Lake kwa Mfalme**

Yusuf عليه السلام alijua kuwa mkamuaji mvinyo angenusurika. Kwa hali ya usiri, ili wasiwasi wa yule mwingine kuwa angesulubiwa usiwe mkubwa, alisema,

أَذْكُرْنِي عِنْدَ رَبِّكَ

**“Nikumbuke kwa bwana wako.”**

Kwa kumuomba amueleze mfalme habari zake. Mtu huyo alisahau ombi la Yusuf عليه السلام na hakumtaja mfalme habari zake, hila za kishetani, ili Mtume wa Allah تعالى asitoke jela. Hii ni tafsiri sahihi ya,

فَأَنَسَهُ الشَّيْطَانُ ذِكْرَ رَبِّهِ

**“Lakini Shet’ani alimsahaulisha kumtaja kwa bwana wake.”**

Hiyo inamkusudia yule aliyenusurika. Kama walivyoeleza Mujahid, Muhammad bin Ishaq na wengine wengi.<sup>2</sup> Ama kuhusu, ‘miaka michache’, au, ‘bidh’a’ kwa

<sup>1</sup> Ahmad 4:10.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:113.



Kiarabu, inamaanisha baina ya mitatu na tisa, kwa mujibu wa Mujahid na Qatadah.<sup>1</sup> Wahb bin Munabbih alisema, "Ayub عليه السلام aliugua kwa miaka saba, Yusuf عليه السلام alikaa jela miaka saba na Bukhtanassar (Nebukad nezza - Mfalme wa Babil) aliteswa miaka saba."<sup>2</sup>



---

<sup>1</sup> At-Tabari 16:115.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:114

وَقَالَ الْمَلِكُ إِنِّي أَرَى سَبْعَ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ يَأْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَسَبْعَ سُنبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَتٍ ۗ يَأْتِيهَا الْمَلَأُ أَفْتُونًا فِي رُءُوسِنَّ إِن كُنْتُمْ لِلرُّءْيَا تَعْبُرُونَ ﴿٤٣﴾ قَالُوا أَضْغَنْتُ أَحْلَمَ ۗ وَمَا نَحْنُ بِتَأْوِيلِ الْأَحْلَمِ بِعَلِيمِينَ ﴿٤٤﴾ وَقَالَ الَّذِي نَجَا مِنْهُمَا وَادَّكَرَ بَعْدَ أُمَّةٍ أَنَا أُنَبِّئُكُمْ بِتَأْوِيلِهِ فَأَرْسِلُونِ ﴿٤٥﴾ يُوسُفُ أَيُّهَا الصِّدِّيقُ أَفْتِنَا فِي سَبْعِ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ يَأْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَسَبْعِ سُنبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَتٍ لَعَلِّي أَرْجِعُ إِلَى النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٤٦﴾ قَالَ تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَأْبًا فَمَا حَصَدْتُمْ فَذَرُوهُ فِي سُنْبُلَيْهِ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٤٧﴾ ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ سَبْعٌ شِدَادًا يَأْكُلْنَ مَا قَدَّمْتُمْ هُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّا حُصِنْتُمْ ﴿٤٨﴾ ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَامٌ فِيهِ يُغَاثُ النَّاسُ وَفِيهِ يَعْصِرُونَ ﴿٤٩﴾ وَقَالَ الْمَلِكُ أَتُتُونِي بِهِ ۗ فَلَمَّا جَاءَهُ الرَّسُولُ قَالَ أَرْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَسْتَلْهُ مَا بَالُ النِّسْوَةِ الَّتِي قَطَعْتَ أَيْدِيَّ ۗ إِنَّ رَبِّي بِكَيْدِهِمْ عَلِيمٌ ﴿٥٠﴾ قَالَ مَا خَطْبُكُمْ إِذْ رَوَدْتُمُنِّي يُونُسَ عَنِ نَفْسِهِ ۗ قُلْنَ حَاشَ لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِنْ سُوءٍ ۗ قَالَتِ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ الْقَنْعَنُ حَضَحَصَ الْحَقُّ أَنَا رَوَدْتُهُ عَنْ نَفْسِهِ وَإِنَّهُ لَمِنَ الصِّدِّيقِينَ ﴿٥١﴾ ذَلِكَ لِيَعْلَمَ أَنِّي لَمْ أَخُنْهُ بِالْغَيْبِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي كَيْدَ الْخَائِبِينَ ﴿٥٢﴾ \* وَمَا أُبْرِئُ نَفْسِي ۗ إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۗ إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٣﴾

وَقَالَ الْمَلِكُ إِنِّي أَرَى سَبْعَ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ يَأْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَسَبْعَ سُنبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَتٍ ۗ يَأْتِيهَا الْمَلَأُ أَفْتُونًا فِي رُءُوسِنَّ إِن كُنْتُمْ لِلرُّءْيَا تَعْبُرُونَ ﴿٤٣﴾ قَالُوا أَضْغَنْتُ أَحْلَمَ ۗ وَمَا نَحْنُ بِتَأْوِيلِ الْأَحْلَمِ بِعَلِيمِينَ ﴿٤٤﴾ وَقَالَ الَّذِي نَجَا مِنْهُمَا وَادَّكَرَ بَعْدَ أُمَّةٍ أَنَا أُنَبِّئُكُمْ بِتَأْوِيلِهِ فَأَرْسِلُونِ ﴿٤٥﴾ يُوسُفُ أَيُّهَا الصِّدِّيقُ أَفْتِنَا فِي سَبْعِ بَقَرَاتٍ سِمَانٍ يَأْكُلُهُنَّ سَبْعٌ عِجَافٌ وَسَبْعِ سُنبُلَاتٍ خُضْرٍ وَأُخَرَ يَابِسَتٍ لَعَلِّي أَرْجِعُ إِلَى النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٤٦﴾ قَالَ تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَأْبًا فَمَا حَصَدْتُمْ فَذَرُوهُ فِي سُنْبُلَيْهِ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٤٧﴾ ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ سَبْعٌ شِدَادًا يَأْكُلْنَ مَا قَدَّمْتُمْ هُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِمَّا حُصِنْتُمْ ﴿٤٨﴾ ثُمَّ يَأْتِي مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَامٌ فِيهِ يُغَاثُ النَّاسُ

وَفِيهِ يَعْصِرُونَ ﴿٥٣﴾

**43. Na siku moja mfalme alisema: Hakika mimi nimeota ng'ombe saba wanene wanaliwa na ng'ombe saba waliokonda. Na mashuke saba mabichi na mengine makavu. Enyi waheshimiwa! Niambieni maana ya ndoto zangu, ikiwa nyinyi mnaweza kuagua ndoto.**

**44. Wakasema: Hizi ni ndoto zilizoparaganyika, wala sisi sio wenye kujua tafsiri ya ndoto hizi.**

**45. Hapo akasema yule aliyeokoka katika wale wawili akakumbuka baada ya muda: Mimi nitakuambieni tafsiri yake. Basi nitumeni.**

**46. Yusuf! Ewe mkweli! Tueleze nini maana ya ng'ombe saba wanene kuliwa na ng'ombe saba waliokonda. Na mashuke saba mabichi na mengine makavu, ili nirejee kwa watu wapate kujua.**

**47. Akasema: Mtalima miaka saba kwa juhudi. Mtachovuna kiwacheni katika mashuke yake, isipokuwa kidogo mtachokula.**

**48. Kisha itakuja baadaye miaka saba ya shida itakayo kula kile mlichoiwekea isipokuwa kidogo mtachokihifadhi.**

**49. Kisha baada ya haya utakuja mwaka ambao katika mwaka huo watu watasaidiwa, na watakamua.**

### **Ndoto ya Mfalme wa Misri**

Ndoto hii aliyoiota Mfalme wa Misri, Allah تعالیٰ Alijaalia kuwa ni sababu ya Yusuf عليه السلام kutoka jela, na heshima yake kuwa imehifadhiwa. Mfalme alishtuka na kutafuta tafsiri yake. Alikusanya makuhani, wakuu wa dola na wasaidizi wake wengine, akawaomba wamfasirie. Hawakujua tafsiri yake na kwa udhuru, walisema,

أَضَعْتُ أَحْلَمِ

**"Hizi ni ndoto zilizo paraganyika."** Ndiyo uliyoota,

وَمَا نَحْنُ بِتَأْوِيلِ الْأَحْلَمِ بِعَلَمِينَ

**"...wala sisi sio wenye kujua tafsiri ya ndoto."** Walisema, kama ingekuwa maono badala ya ndoto tu zilizoparaganyika za uongo, tungeijua tafsiri yake. Yule mtu aliyenusurika kati ya wale wawili wenzake Yusuf عليه السلام kule gerezani, alikumbuka. Shaytan alifanya hila ili kumfanya asahau ombi la Yusuf

عليه السلام, asimtajie mfalme habari yake. Sasa, miaka kadhaa baadaye imeshapita, amekumbuka baada ya kusahau na akamueleza mfalme na watu wake,

أَنَا أَنبِئُكُمْ بِتَأْوِيلِهِ

**“Mimi nitakuambieni tafsiri yake.”** Ndoto hiyo,

فَأَرْسِلُونِ

**“Basi nitumeni.”** Kwa Yusuf عليه السلام, mtu mkweli. Wakampeleka, na akamuambia Yusuf عليه السلام,

يُوسُفُ أَيُّهَا الصَّادِقُ أَفْتِنَا

**“Yusuf! Ewe mkweli! Tueleze...”** na akamsimulia ndoto ya mfalme.

### Tafsiri ya Yusuf عليه السلام Kuhusu Ndoto ya Mfalme.

Haya ni pindi Yusuf عليه السلام alipomfasiria ndoto, bila ya kumkosoa mtu huyo kwa kusahau ombi lake alilompa. Wala hakuweka sharti kuwa aachiliwe kabla ya kufasiri. Bali, alisema,

تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَأْبًا

**“Mtalima miaka saba kwa juhudi.”** Mtapata kiasi cha kawaida cha mvua na rutuba kwa miaka saba mfululizo. ‘Alifasiri kwamba ng’ombe ni miaka, kwa sababu ng’ombe hulima shamba lenye kutoa matunda na nafaka, ambazo zinawakilisha mashuke ndotoni. Kisha akawashauri mambo ya kufanya katika kipindi cha miaka hiyo ya rutuba,

فَمَا حَصَدْتُمْ فَذَرُوهُ فِي سُنْبُلِهِ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تَأْكُلُونَ

**“Mtacho vuna kiwacheni katika mashuke yake, isipo kuwa kidogo mtacho kula.”**

Alisema, ‘Mavuno yenu katika miaka hiyo saba ya rutuba, muyaache katika mashuke yake ili kuyahifadhi vyema. Hilo litasaidia kuyafanya yakae kwa muda mrefu yakiwa na afya, isipokuwa kiasi mnachohitaji kwa chakula, ambacho hakitakiwi kuwa kingi. Acheni kutumia kwa fujo, ili kinachobakia mkitumie katika kipindi cha miaka saba ya ukame utakaofuata baada ya miaka saba ya rutuba.’ Hayo yaliwakilishwa na ng’ombe saba wembamba wanaokula ng’ombe saba wanene. Katika kipindi cha miaka saba ya ukame, watakula kutoka katika

mavuno yaliyokusanywa wakati wa miaka saba ya rutuba, ambayo imewakilishwa na mashuke makavu ndotoni. Yusuf عليه السلام aliwaambia kuwa wakati wa miaka hiyo, mashuke yaliyobakia hayatatoa chochote na kila watakachojaribu kupanda, hakitaleta mavuno, akasema,

يَأْكُلْنَ مَا قَدَّمْتُمْ هُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تَحْصُونَ

**“...itakayo kula kile mlichoiwekea isipokuwa kidogo mtacho kihifadhi.”**

Aliwapa bishara kuwa baada ya miaka mfululizo ya ukame, utafuata mwaka wa rutuba, ambapo kwa wakati huo, watu watapata mvua na ardhi itazalisha kwa wingi. Hapo watu watachuja mvinyo na mafuta kama kawaida.

وَقَالَ الْمَلِكُ أَتُوتَنِي بِهِ فَمَا جَاءَهُ الرَّسُولُ قَالَ أَرْجِعْ إِلَىٰ رَبِّكَ فَسَأَلَهُ مَا بَأْسَ اللَّيْسَةِ  
 الَّتِي قَطَعْنَا أَيَدِيَهُنَّ إِنَّ رَبِّي بِكَيْدِهِنَّ عَلِيمٌ ﴿٥٠﴾ قَالَ مَا خَطْبُكُنَّ إِذْ رَاوَدْتُنَّ يُوسُفَ عَنِ  
 نَفْسِهِ ۗ قُلْنَ حَاشَ لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِنْ سُوءٍ ۗ قَالَتِ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ الْقَنْعَنُ حَضَخَصَّ  
 الْحَقُّ أَنَا رَاوَدْتُهُ عَنْ نَفْسِهِ وَإِنَّهُ لَمِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٥١﴾ ذَلِكَ لِيَعْلَمَ أَنِّي لَمْ أَخُنْهُ  
 بِالْغَيْبِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي كَيْدَ الْخَائِبِينَ ﴿٥٢﴾ وَمَا أُبْرِئُ نَفْسِي ۗ إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ  
 بِالسُّوءِ ۗ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۗ إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥٣﴾

**50. Na mfalme akasema: Mleteni kwangu! Basi mjumbe alipomjia Yusuf alisema: Rejea kwa bwana wako ukamuulize khabari ya wale wanawake waliojikata mikono yao. Hakika Mola wangu Mlezi Anazijua vyema hila zao.**

**51. Mfalme alisema: Mlikuwa mna nini mlipomtaka Yusuf kinyume na nafsi yake? Wakasema: Hasha Lillahi! Sisi hatukujua ubaya wowote kwake. Mke wa Mheshimiwa akasema: Sasa haki imedhiri. Mimi ndiye niliyemtaka kinyume na nafsi yake, na hakika yeye ni katika wakweli.**

**52. Hayo ni apate kujua ya kwamba mimi sikumfanyia khiyana nyuma yake; na ya kwamba Mwenyezi Mungu Haziongoi hila za makhaini.**

**53. Nami sijitoi lawamani. Kwa hakika nafsi ni mno kuamrisha maovu, isipokuwa ile ambayo Mola wangu Mlezi Aliyoihemu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu.**

**Mfalme Anachunguza Yaliyojiri Baina ya Mkewe Azizi, Wanawake wa Mji na Yusuf** عليه السلام

Allah تعالى Anatusimulia kuwa baada ya mfalme kufikishiwa tafsiri ya ndoto yake aliipenda tafsiri ya Yusuf عليه السلام na akahisi kuwa ilikuwa kweli, akatambua ubora wa Yusuf عليه السلام na ujuzi wake wa kutafsiri ndoto, na ubora wa tabia zake juu ya watu wa nchi yake, akasema:

أَتْتُونِي بِهِ

**“Mleteni kwangu!”** ‘Mtoeni jela na mumlete.’ Mjumbe alipomuendea na kumfikishia habari za kuachiliwa. Kwa heshima, Yusuf عليه السلام alikataa kutoka jela mpaka mfalme na raia wake watamke kuwa hakuwa na hatia na isafishwe heshima yake, kwa kukana mashtaka ya mke wa Mheshimiwa ‘Aziz dhidi yake. Alitaka wajue kuwa kifungo chake kilikuwa ni dhuluma na ulipizaji kisasi, na si kwamba alitenda kosa hilo alilopachikwa. Alisema:

أَرْجِعْ إِلَىٰ رَبِّكَ

**“Rejea kwa bwana wako.”** Sunna ya Mtume wetu ﷺ imemsifu Nabii Yusuf عليه السلام na imetaja ubora na utukufu wake, cheo na uvumilivu wake rehma za Allah تعالى na amani yake ziwe juu yake. Imekuja katika Musnad na Sahihi Mbili zimenukuu kuwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema,

«نَحْنُ أَحَقُّ بِالشُّكِّ مِنْ إِبْرَاهِيمَ إِذْ قَالَ،»

*“Sisi tuna haki zaidi ya kuwa na shaka kuliko Ibrahim, wakati aliposema,”*

رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ

**“Mola wangu, nioneshe unavyofufua wafu.”**

«وَيَرْحَمُ اللَّهُ لَوْطًا لَقَدْ كَانَ يَأْوِي إِلَىٰ رُكْنٍ شَدِيدٍ، وَلَوْ لَبِثْتُ فِي السُّجْنِ  
يُوسُفُ لَأَجَبْتُ الدَّاعِيَ»

*"Na Allah amrehemu Lut, kwa hakika alikuwa anaegemea kwenye nguzo madhubuti, na kama mimi ningekaa jela kama muda aliokaa Yusuf ningeitikia (wito wa) muitaji."*<sup>1</sup>

Katika riwaya nyingine iliyoandikwa na Ahmad kutoka kwa Abu Huraira عليه السلام, Mtume ﷺ alisema kuhusu kauli ya Yusuf رضي الله عنه

فَسَأَلَهُ مَا بَأْسُ النَّسْوَةِ الَّتِي قَطَعْنَ أَيْدِيَهُنَّ إِنَّ رَبِّي بِكَيْدِهِنَّ عَلِيمٌ

***"...ukamuulize khabari ya wale wanawake waliojikata mikono yao. Hakika Mola wangu Mlezi Anazijua vyema hila zao."***

Mtume ﷺ akasema:

«لَوْ كُنْتُ أَنَا، لَأَسْرَعْتُ الْإِجَابَةَ وَمَا ابْتَغَيْتُ الْعُذْرَةَ»

*"Ningekuwa mimi ningeharakisha kuitika, nisingetafuta udhuru."*<sup>2</sup>

Na Kauli Yake Allah تعالى:

قَالَ مَا حَطَبُكُمْ إِذْ رَأَوْتُنَّ يُوسُفَ عَنْ نَفْسِهِ

***"Mlikuwa mna nini mlipomtaka Yusuf kinyume na nafsi yake?"***

Mfalme aliwakusanya wanawake waliojikata mikono yao walipokaribishwa nyumbani kwa mkewe 'Aziz. Aliwauliza wote ingawa kauli yake ilimuelekea mke wa Mheshimiwa 'Aziz. Aliwauliza hivi,

مَا حَطَبُكُمْ

***"Mlikuwa mna nini."*** Mna kisa gani kuhusu,

إِذْ رَأَوْتُنَّ يُوسُفَ عَنْ نَفْسِهِ

***"Mlipo mtaka Yusuf kinyume na nafsi yake?"*** Katika siku ya karamu,

قُلُوبَ حَشَى لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِنْ سُوءٍ

***"Wakasema: Hasha Lillahi! Sisi hatukujua ubaya wowote kwake."***

<sup>1</sup> Ahmad 4:326, Fat'hul Al-Bari 8:216, Muslim 1:133.

<sup>2</sup> Ahmad 4:346.

Wanawake walimjibu mfalme, *Hasha Lillahi!* Yusuf عليه السلام kuwa na hatia ya hilo, tunaapa kwa Allah تعالى, kamwe hatukujua juu yake ubaya wowote.

قَالَتْ امْرَأَتُ الْعَزِيزِ اَلْكُنْ حَصْحَصَ

***“Mke wa Mheshimiwa akasema: Sasa haki imedhihiri.”***

Au ukweli umewabainikia wote, kwa mujibu wa Ibn Abbas, Mujahid na wengine رضي الله عنهم<sup>1</sup>. Pia maana ya *Has’hasa* ni kuwa, umebainika na kuwa wazi,

اَنَا رَاوَدْتُهُ عَن نَفْسِهِ وَاِنَّهُ لَمِنَ الصّٰدِقِيْنَ

***“Mimi ndiye niliyemtaka kinyume na nafsi yake, na hakika yeye ni katika wakweli.”***

Pale Yusuf عليه السلام aliposema,

هِيَ رَاوَدْتَنِي عَن نَفْسِي

***“Yeye ndiye aliyenitaka bila ya mimi kumtaka..”***

ذٰلِكَ لِيَعْلَمَ اَنِّي لَمْ اَخُنُّهُ بِالْغَيْبِ

***“Hayo ni apate kujua ya kwamba mimi sikumfanyia khiyana nyuma yake.”***

Mke wa Mheshimiwa ‘Aziz alisema, ‘Mimi mwenyewe ninakiri hili ili mume wangu ajue kwamba sikumfanyia hiana nyuma yake na kwamba jambo hilo halikutokea. Nilim-bembeleza kijana huyu, na yeye alikataa, nami ninakiri hivyo ili ajue kuwa mimi sikuwa na hatia.

وَاَنَّ اللّٰهَ لَا يَهْدِي كَيْدَ الْخٰتِئِيْنَ ﴿٤٣﴾ \* وَمَا اُبْرِيْ نَفْسِي

***“...na ya kwamba Mwenyezi Mungu haziongoi hila za makhaini. Nami sijitoi lawamani.”***

Mwanamke huyo anasema, “Sijitoi lawamani, kwani nafsi hutamani na hutamani, na hayo ndiyo yalijonifanya nimbembeleze.”

<sup>1</sup> At-Tabari 16:138.



الْنَفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي

***“Kwa hakika nafsi ni mno kuamrisha maovu, isipokuwa ile ambayo Mola wangu Mlezi Aliyoihemu.”***

Ambayo Allah تعالى Ameikinga.

إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَحِيمٌ

***“Hakika Mola wangu Mlezi ni Msamehevu na Mwenye Kurehemu.”***

Ufahamu huo ndio wa kutosheleza na unaofaa kwa muendelezo wa habari na maana ya maneno ya Kiarabu. Al-Mawardi ameeleza hayo katika tafsiri yake, kwa kuiunga mkono, pia imependelewa na Imamu Abul-'Abbas Ibn Taymiyya رحمه الله تعالى aliyeandikia kitabu.

Ilisemekana kuwa Yusuf عليه السلام ndiye aliyesema:

ذَلِكَ لِيَعْلَمَ أَنِّي لَمْ أَخُنْهُ

***“Hayo ni apate kujua ya kwamba mimi sikumfanyia khiyana.”***

Kwa mkewe,

بِالْغَيْبِ

***“...nyuma yake.”*** Alisema, ‘Nilimrudisha mjumbe ili Mfalme akague kosa langu na Mheshimiwa ‘Aziz awe na uhakika kwamba, mimi ni Mtukufu.

أَنِّي لَمْ أَخُنْهُ

***“...mimi sikumfanyia khiyana.”*** kwa mkewe.

بِالْغَيْبِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي كَيْدَ الْخَائِبِينَ

***“...nyuma yake na ya kwamba Mwenyezi Mungu haziongoi hila za makhaini.”***

Hayo ndio maelezo pekee yaliyotolewa na Ibn Jarir At-Tabari رحمه الله تعالى, na Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى, lakini rai ya mwanzo ina nguvu zaidi na imedhiri zaidi kwa sababu ni muendelezo wa aliyoyasema mke wa Mheshimiwa ‘Aziz mbele ya Mfalme. Yusuf عليه السلام hakuwepo kabisa katika muda huo, kwa kuwa aliachiliwa baadaye na kuletwa kwa Mfalme kwa amri yake.

وَقَالَ الْمَلِكُ أَتُتُونِي بِهَذِهِ أَسْتَخْلِصُكَ لِنَفْسِي ۗ فَلَمَّا كَلَّمَهُ  
 قَالَ إِنَّكَ آلْيَوْمَ لَدَيْنَا مَكِينٌ أَمِينٌ ﴿٥٤﴾ قَالَ أَجْعَلْنِي عَلَى  
 خَزَائِنِ الْأَرْضِ ۗ إِنِّي حَفِيظٌ عَلَيْكُمْ ﴿٥٥﴾ وَكَذَلِكَ مَكَّنَّا  
 لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ يَتَّبِعُونَ ۗ إِنَّهَا خَيْرٌ مِّمَّا يَشَاءُونَ ۗ نُصِيبُ بِرَحْمَتِنَا  
 مَن نَّشَاءُ ۗ وَلَا نُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٦﴾ وَلَا أَجْرَ  
 الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٥٧﴾ وَجَاءَ إِخْوَتُهُ  
 يُوسُفَ فَدَخَلُوا عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ ﴿٥٨﴾  
 وَلَمَّا جَهَّزَهُم بِجَهَّازِهِمْ قَالَ أَتُتُونِي بِأَخٍ لَّكُم مِّنْ أُمَّيْكُم  
 ۗ أَلَا تَرَوْنَ أَنِّي أُوفِي الْكَيْلَ وَأَنَا خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ ﴿٥٩﴾ فَإِن  
 لَّمْ تَأْتُونِي بِهَذَا فَلَا كَيْلَ لَكُمْ عِنْدِي وَلَا تَقْرَبُونِ ﴿٦٠﴾  
 قَالُوا سَتَرُوهُ عَنْهُ ءَابَاؤُهُ وَاتَّخَذُوا لِيُوسُفَ إِفْتِيصًا  
 وَجَعَلُوا بَصُرَتِهِمْ فِي رِحَابِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَعْرِفُونَهَا إِذَا انْقَلَبُوا إِلَى  
 أَهْلِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٦١﴾ فَلَمَّا رَجَعُوا إِلَىٰ أَبِيهِمْ  
 قَالُوا يَا أَبَانَا مُنِعَ مِنَّا الْكَيْلُ فَأَرْسِلْ مَعَنَا آخَانًا نَّكَتَلْ  
 وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٦٢﴾ قَالَ هَلْ ءَامَنُكُمْ عَلَيْهِ إِلَّا  
 كَمَا ءَامَنُكُمْ عَلَىٰ أَخِيهِ مِن قَبْلُ ۗ فَاللَّهُ خَيْرٌ حَافِظًا ۗ وَهُوَ  
 أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٦٣﴾

وَقَالَ الْمَلِكُ أَتُتُونِي بِهَذِهِ أَسْتَخْلِصُكَ  
 لِنَفْسِي ۗ فَلَمَّا كَلَّمَهُ قَالَ إِنَّكَ آلْيَوْمَ  
 لَدَيْنَا مَكِينٌ أَمِينٌ ﴿٥٤﴾ قَالَ أَجْعَلْنِي  
 عَلَىٰ خَزَائِنِ الْأَرْضِ ۗ إِنِّي حَفِيظٌ  
 عَلَيْكُمْ ﴿٥٥﴾

**54. Basi mfalme akasema:**  
*Mleteni kwangu, awe wangu mwenyewe khasa. Basi alipomsemeza alinena: Hakika wewe leo ume-kwisha tamakani kwetu na umeaminika.*

**55. Yusuf akasema:** *Nifanye mshika khazina za nchi. Kwani hakika mimi ni mlinzi mjuzi.*

**Yusuf عليه السلام Amepewa Cheo cha Hadhi ya Juu na Mfalme wa Misri**

Allah تعالى Anaeleza kuwa Mfalme alipotambua Yusuf kwa yale aliyoshitakiwa, alisema,

أَتُتُونِي بِهَذِهِ أَسْتَخْلِصُكَ لِنَفْسِي ۗ

**“Mleteni kwangu, awe wangu mwenyewe khasa.”** Kwamba nimfanye katika wasaidizi na washirika wangu wa karibu.

فَلَمَّا كَلَّمَهُ

**"Basi alipomsemeza."**

Mfalme alipomsemesha Yusuf عليه السلام na kugundua zaidi ubora, uwezo mkubwa, uhodari, tabia njema na maadili mema, alimuambia:

إِنَّكَ الْيَوْمَ لَدَيْنَا مَكِينٌ أَمِينٌ

**"Hakika wewe leo umekwisha tamakani kwetu na umeaminika."**

Mfalme alimuambia Yusuf عليه السلام, 'Umepata heshima ya juu kwetu na umeaminiwa kikamilifu.' Yusuf عليه السلام akasema:

أَجْعَلَنِي عَلَىٰ خَزَائِنِ الْأَرْضِ إِنِّي حَفِيظٌ عَلِيمٌ

**"Nifanye mshika khazina za nchi. Kwani hakika mimi ni mlinzi mjuzi."**

Yusuf عليه السلام alieleza sifa zake, kwani hilo linaruhusiwa pindi uwezo wa mtu hautambuliki na kuna haja ya kufanya hivyo. Alisema kuwa yeye ni,

حَفِيظٌ

**"ni mlinzi."** Mlinzi mwaminifu,

عَلِيمٌ

**"...mjuzi."**

Mwenye elimu na busara kwa kazi anayoaminiwa. Yusuf عليه السلام alimuomba mfalme amteue awe waziri wa fedha katika nchi, mwenye majukumu katika mavuno na maghala, ambapo wangekusanya mavuno kwa ajili ya miaka ya njaa aliyowaambia kuwa yangewakumba. Alitaka awe msimamizi, ili aweze kutumia mavuno kwa uangalifu na kwa njia bora zaidi. Mfalme alimkubalia Yusuf عليه السلام kwa sababu alitamani sana kumueka Yusuf عليه السلام karibu naye zaidi na kumpa heshima. Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

وَكَذَلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ يَتَّبِعُونَ مِنْهَا حَيْثُ يَشَاءُ ۗ نُنِيبُ بِرَحْمَتِنَا مَنْ نَشَاءُ ۗ وَلَا

نُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٧﴾ وَلَا جُرْأَلَاءَ خَيْرٌ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٥٨﴾

**56. Basi namna hivi Tukampa Yusuf cheo katika nchi; anakaa humo popote anapopenda. Tunamfikishia Rehema Zetu Tumtakaye, wala hatupuuzi malipo ya wafanyao mema.**

**57. Na hakika malipo ya Akhera ni bora zaidi, kwa walioamini na wakawa wachamungu.**

### Utawala wa Yusuf عليه السلام katika Misri

Halafu Allah تعالى Akasema:

وَكَذَلِكَ مَكَّنَّا لِيُوسُفَ فِي الْأَرْضِ

**“Basi namna hivi Tukampa Yusuf cheo katika nchi.”** Huko Misri,

يَتَّبِعُوا مِنَّا حَيْثُ يَشَاءُ

**“Anakaa humo popote anapopenda.”**

As-Suddi, ‘Abdur-Rahman bin Zaid, bin Aslam wamesema: kuwa maana ya sehemu hii ya Aya inamaanisha, “Huko anafanya atakavyo.”<sup>1</sup> Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema inamaanisha, “Alikuwa anakwenda kwa uhuru nchini baada ya kufungwa jela, alipokuwa na dhiki na udhalili wa utumwa.”<sup>2</sup> Allah تعالى Anasema,

نُصِيبُ بِرَحْمَتِنَا مَن نَّشَاءُ وَلَا نُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ

**“Tunamfikishia Rehema Zetu Tumtakaye, wala hatupuuzi malipo ya wafanyao mema.”**

Allah تعالى Anasema hapa, Hatutaipoteza subira ya Yusuf juu ya udhia wa nduguze na kufungwa jela kwa sababu ya mke wa ‘Aziz, na kwa sababu hiyo Allah تعالى, Atampa malipo kwa Kumpa msaada na ushindi,

وَلَا نُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٥٧﴾ وَلَا أَجْرَ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٥٨﴾

**“Wala hatupuuzi malipo ya wafanyao mema. Na hakika malipo ya Akhera ni bora zaidi, kwa walioamini na wakawa wachamungu.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:151-152.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:151.

Allah عليه السلام Anaeleza kuwa yale Aliyomhifadhia Mtume Wake Yusuf huko Akhera ni makubwa, mengi na matukufu sana kuliko mamlaka Aliyompa duniani. Kama Alivyosema Allah عليه السلام kuhusu Sulaiman:

هَذَا عَطَاؤُنَا فَامْنُنْ أَوْ أَمْسِكْ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٩﴾ وَإِنَّ لَهُ عِنْدَنَا لَزُلْفَىٰ وَحُسْنَ مَقَابٍ ﴿٤٠﴾

***“Hichi ndicho kipawa Chetu. Basi toa au zuia, bila ya hisabu. Na hakika yeye Kwetu Sisi ana cheo cha kukaribishwa Kwetu, na pahala pazuri pa kurejea.” (38:39-40).***

Yusuf عليه السلام aliteuliwa na Ar-Rayyan bin Al-Walid, Mfalme wa Misri wa enzi hizo kuwa Waziri wa fedha, na kuondoka kwa Mheshimiwa 'Aziz (aliyemnunua na mume wa mwanamke aliyemtaka kimapenzi). Mfalme alisilimu mikononi mwa Yusuf عليه السلام kwa mujibu wa Mujahid.

وَجَاءَ إِخْوَتُهُ يُوسُفَ فَدَخَلُوا عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ ﴿٥٨﴾ وَلَمَّا جَهَّزَهُم بِجَهَّازِهِمْ قَالِ اتُّنُونِي بِأَخٍ لَّكُمْ مِّنْ أَبِيكُمْ ؕ أَلَا تَرَوْنَ أَنِّي أُوفِي الْكَيْلَ وَأَنَا خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ ﴿٥٩﴾ فَإِن لَّمْ تَأْتُونِي بِهِ فَلَا كَيْلَ لَكُمْ عِنْدِي وَلَا تَقْرُبُونِ ﴿٦٠﴾ قَالُوا سَتَرُوهُ عَنْهٗ أَبَاهُ وَإِنَّا لَفَاعِلُونَ ﴿٦١﴾ وَقَالَ لِفِتْيَانِهِ اجْعَلُوا بِضْعَتَهُمْ فِي رِحَالِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَرْفُؤْنَهَا إِذَا أَنْقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمْ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٦٢﴾

***58. Wakaja ndugu zake Yusuf, na wakaingia kwake. Yeye akawajua na wao hawakumjua.***

***59. Na alipowatengenezea tayari haja yao alisema: Nileteeni ndugu yenu kwa baba. Je! Hamuoni ya kwamba mimi ninatimiza kipimo, nami ni mbora wa kukirimu?***

***60. Na msiponiletea basi hampati kipimo chochote kwangu, wala msinikurubie.***

***61. Wakasema: Sisi tutamrairai baba yake; na bila ya shaka tutafanya hayo.***

***62. Na Yusuf akawaambia watumishi wake: Tieni bidhaa zao katika mizigo yao, ili wazione watakaporudi kwa watu wao wapate kurejea tena.***

### Nduguze Yusuf عليه السلام Wanasafiri Wanakwenda Misri

As-Suddi, Muhammad bin Ishaq na wengine wengi, wamesema kuwa sababu ya nduguze Yusuf عليه السلام kuja Misri, ni kwamba, baada ya Yusuf عليه السلام kuwa waziri wa Misri, na ikapita miaka saba ya neema, ilifuatia miaka saba ya ukame ulioenea katika Misri yote. Ukame pia ulifika katika eneo la Kan'aani, alipokuwa akiishi baba yake Yusuf عليه السلام, Mzee Yakubu عليه السلام na wanawe. Nabii Yusuf عليه السلام alikusanya na kuhifadhi vyema mazao ya watu, na ukusanyaji uliwasaidia sana watu. Hili pia lilimruhusu Yusuf عليه السلام kuwapa watu waliokuja kuhemea kutoka maeneo mengi, kwa ajili yao wenyewe na familia zao, akawa hamzidishii mtu kupita mzigo wa ngamia mmoja kwa mwaka, na Yusuf عليه السلام alikuwa hashibishi nafsi yake, na yeye, mfalme na wasaidizi wao walikula mlo mmoja tu, wa mchana, mpaka watu walipojikimu kwa walichokua nacho kwa miaka saba iliyobakia, Yusuf عليه السلام akawa ni Rehema ya Allah تعالى kwa watu wa Misri.

Nduguze Yusuf عليه السلام walikuwa miongoni mwa watu waliokuja Misri kununua chakula, kwa amri ya baba yao. Walijua kuwa 'Aziz wa Misri alikuwa anawauzia watu chakula kwa bei nafuu, wakachukua bidhaa za kubadilishana na chakula. Walikuwa watu kumi, kwa sababu Yakubu عليه السلام alibakia na mwanaye Binyamin ndugu yake Yusuf عليه السلام. Alikuwa akimpenda zaidi Binyamin baada ya Yusuf عليه السلام kutoweka.

Nduguze Yusuf عليه السلام walipoingia kwa Yusuf عليه السلام akiwa katika heshima yake, uongozi wake na ukubwa wake, aliwatambua mara tu alipowaona. Hata hivyo, hawakumjua kwa sababu wao waliondokana naye alipokuwa angali mdogo, wakamuuzua kwa wasafiri, na hawakujua alipoelekea, na hawakudhani kuwa Yusuf عليه السلام angekuwa waziri ndio maana hawakumjua, ilhali yeye aliwajua. As-Suddi alisema kuwa alianza kuongea na nduguze na kuwauliza, "Jambo gani limekuleteni katika nchi yangu?" Wakasema, "Ewe Mheshimiwa 'Aziz, tumekuja kununua chakula." Akasema, "Huenda nyinyi ni wapelelezi." Wakasema, "Tunajikinga kwa Allah تعالى" Akasema, "Mnatoka wapi?" Wakasema, "Tumetoka katika nchi ya Kanaani na Baba yetu ni Yakubu عليه السلام, Mtume عليه السلام akasema: "Je, ana watoto wengine wasiokuwa nyinyi?" Wakasema, "Ndiyo tulikuwa watoto kumi na wawili, mdogo wetu alifariki jangwani, na alikuwa anapendwa sana na baba yake, akabaki ndugu yake wa baba mmoja mama mmoja, baba yetu amemzuia ili aliwazike naye." Yusuf عليه السلام akaamuru kuwa nduguze waheshimiwe na wakaruhusiwa kubakia.

وَلَمَّا جَهَّزَهُم بِجَهَّازِهِمْ

**“Na alipowatengenezea tayari haja yao.”**

Aliwakamilishia kipimo chao, na akawabebesha mizigo yao, akasema: ‘Nileteeni ndugu yenu huyo mliyemtaja ili nijue ukweli wa mliyosema.’

أَلَا تَرَوْنَ أَنِّي أُوْفِي الْكَيْلَ وَأَنَا خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ

**“Je! Hamuoni ya kwamba mimi nina timiza kipimo, nami ni mbora wa kukirimu?”**

Anawashawishi warejee tena kwake, kisha akawatisha.

فَإِنْ لَّمْ تَأْتُونِي بِهٖ فَلَا كَيْلَ لَكُمْ عِنْدِي

**“Na msiponiletea basi hampati kipimo chochote kwangu.”**

Msipokuja naye mtapokuja mara ya pili, basi hamtapewa chakula.

وَلَا تَقْرُبُونِ ﴿٥٤﴾ قَالُوا سُرُوْدُ عَنْهُ أَبَاهُ وَإِنَّا لَفَاعِلُونَ ﴿٥٥﴾

**“...wala msinikurubie. Wakasema: Sisi tutamrairai baba yake; na bila ya shaka tutafanya hayo.”**

Tutaharakisha kuja naye, vyovyote iwezekanavyo na tutajitahidi kwa kila namna, ili ujue ukweli wa tulichokisema.

وَقَالَ لِفِتْيَانِهِ

**“Akawaambia watumishi wake.”**

Au watumwa wake:

أَجْعَلُوا بِضَاعَهُمْ

**“Tieni bidhaa zao,”**

Au bidhaa walizokuja nazo ili kubadilishana na chakula.

فِي رِحَالِهِمْ

**“...katika mizigo yao,”**

Hali ya kuwa hawajui,

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

“...wapate kurejea tena.”

Ilisemekana kuwa Yusuf عليه السلام alifanya hivyo kwa sababu alichelea kuwa huenda nduguze hawakuwa na bidhaa zingine za kuleta kubadilisha kwa chakula.

فَلَمَّا رَجَعُوا إِلَىٰ أَبِيهِمْ قَالُوا يَا أَبَانَا مُنِعَ مِنَّا الْكَيْلُ فَأَرْسِلْ مَعَنَا آخَانَ نَكْتَلْ وَإِنَّا لَهُ  
لَحَافِظُونَ ﴿٦٣﴾ قَالَ هَلْ ءَامَنُكُمْ عَلَيْهِ إِلَّا كَمَا ءَامَنُتُمْ عَلَىٰ أَخِيهِ مِن قَبْلُ فَاللَّهُ خَيْرٌ  
حَافِظًا ۖ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّحِيمِينَ ﴿٦٤﴾

**63. Basi waliporejea kwa baba yao, walisema: Ewe baba yetu! Tumenyimwa chakula zaidi, basi mpeleke nasi ndugu yetu ili tupate kupimiwa; na yakini sisi tutamlinda.**

**64. Je, nikuaminini kwa huyu ila kama nilivyokuaminini kwa nduguye zamani? Lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa Kulinda, Naye Ndiye Mbora wa Kurehemu kuliko wenye kurehemu wote.**

**Nduguze Yusuf عليه السلام Wanaomba Idhini kwa Baba Yao Ya'aqub عليه السلام Ili Waende Misri Pamoja na Mdogo wao, Binyamin**

Allah تعالى Anasema kuwa waliporejea kwa baba yao.

قَالُوا يَا أَبَانَا مُنِعَ مِنَّا الْكَيْلُ

“Ewe baba yetu! Tumenyimwa chakula zaidi.”

Baada ya mara hii iwapo hutatutuma pamoja na ndugu yetu Binyamin hatutapimiwa, kwa hiyo mtume pamoja nasi tutapimiwa.

وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ

“Na yakini sisi tutamlinda.”

Usihofie usalama wake, kwani hakika atarejea kwako, na yafuatayo ndiyo waliyomuambia baba yao Yaakub عليه السلام kuhusu Yusuf عليه السلام,



أَرْسَلُهُ مَعَنَا غَدًا يَرْتَع وَيَلْعَبُ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿١٢﴾

***“Mpeleke kesho pamoja nasi, ale kwa furaha na acheze; na bila ya shaka sisi tutamhifadhi.” (12:12)***

Ndio sababu Nabii Yaakub عليه السلام aliwaambia,

هَلْ ءَامَنُكُمْ عَلَيْهِ إِلَّا كَمَا ءَامَنُكُمْ عَلَىٰ أَخِيهِ مِن قَبْلُ ۗ

***“Je, nikuaminini kwa huyu ila kama nilivyokuaminini kwa nduguye zamani.”***

Aliwauliza, ‘Je, mtamfanyia kingine isipokuwa kama mliyomfanyia ndugu yake, Yusuf عليه السلام siku za nyuma, mlipomchukua kutoka kwangu na mkamtengana nisha nami?’

فَأَلَّهُ خَيْرٌ حَافِظًا ۗ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّحِيمِينَ ﴿١٣﴾

***“Lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa Kulinda.”***

Yaakub عليه السلام alisema, ‘Allah تعالى Ana Rehema nyingi kwangu, kuliko wote wenye kurehemu, Anaurehemu uzee wangu, unyonge wangu na hamu yangu kwa mwanangu. Ninamuomba Allah تعالى Amrejeshe kwangu, na Amruhusu awe pamoja nami. Kwani kwa hakika, Yeye ni Mwingi wa Rehema kuliko wote wenye kurehemu.’

\* \* \*

وَلَمَّا فَتَحُوا مَتَاعَهُمْ وَجَدُوا بِضْعَتَهُمْ زُدَّتْ إِلَيْهِمْ ط قَالَوا  
 يَتَّابَانَا مَا نَبَغِي ط هِنْدِه بِضْعَتُنَا زُدَّتْ إِلَيْنَا وَنَمِيرُ أَهْلَنَا  
 وَخَفِظُ أَحَانَا وَنَزْدَادُ كَيْلِ بَعِيرٍ ط ذَلِكَ كَيْلُ يَسِيرٍ ﴿٦٥﴾  
 قَالَ لَنْ أُرْسِلَهُ مَعَكُمْ حَتَّى تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِنْ آلِهِ  
 لَتَأْتُنِي بِهِ إِلَّا أَنْ تُحَاطَ بِكُمْ ط فَلَمَّا ءَاتَوْهُ مَوْثِقَهُمْ قَالَ  
 اللَّهُ عَلَى مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٦٦﴾ وَقَالَ يَبْنَى لَأ تَدْخُلُوا مِنْ  
 بَابِ وَاحِدٍ وَأَدْخُلُوا مِنْ أَبْوَابٍ مُتَفَرِّقَةٍ ط وَمَا أَغْنَى عَنْكُمْ  
 مِنْ آلِهِ مِنْ شَيْءٍ ط إِنْ أَحْكَمْتُ إِلَّا لِلَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ  
 فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٦٧﴾ وَلَمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ  
 أَمَرَهُمْ أَبُوهُمْ مَا كَانَ يُغْنِي عَنْهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ  
 إِلَّا حَاجَةٌ فِي نَفْسِ يَعْقُوبَ قَضَاهَا وَإِنَّهُ لَذُو عِلْمٍ لَمَّا  
 عَلَّمْنَاهُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾ وَلَمَّا  
 دَخَلُوا عَلَى يُوسُفَ ءَاوَىٰ إِلَيْهِ أَخَاهُ ط قَالَ إِنِّي أَنَا أَخُوكَ  
 فَلَا تَبْتَئِسْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٩﴾ فَلَمَّا جَهَّزَهُمْ  
 بِجَهَّازِهِمْ جَعَلَ السِّقَايَةَ فِي رَحْلِ أَخِيهِ ثُمَّ أَذِنَ مُؤَدِّنٌ  
 أَيُّهَا الْعَبِيرُ إِنَّكُمْ لَسَّرِقُونَ ﴿٧٠﴾ قَالُوا وَقَبِلُوا عَلَيْهِمْ مَاذَا  
 تَفْقَدُونَ ﴿٧١﴾ قَالُوا نَفَقْدُ صَوَاعَ الْمَلِكِ وَلِمَنْ جَاءَ  
 بِهِ جَمْلُ بَعِيرٍ وَأَنَا بِهِ زَعِيمٌ ﴿٧٢﴾

وَلَمَّا فَتَحُوا مَتَاعَهُمْ وَجَدُوا بِضْعَتَهُمْ زُدَّتْ إِلَيْهِمْ ط قَالَوا  
 يَتَّابَانَا مَا نَبَغِي ط هِنْدِه بِضْعَتُنَا زُدَّتْ إِلَيْنَا وَنَمِيرُ أَهْلَنَا  
 وَخَفِظُ أَحَانَا وَنَزْدَادُ كَيْلِ بَعِيرٍ ط ذَلِكَ كَيْلُ يَسِيرٍ ﴿٦٥﴾  
 قَالَ لَنْ أُرْسِلَهُ مَعَكُمْ حَتَّى تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِنْ آلِهِ  
 لَتَأْتُنِي بِهِ إِلَّا أَنْ تُحَاطَ بِكُمْ ط فَلَمَّا ءَاتَوْهُ مَوْثِقَهُمْ قَالَ  
 اللَّهُ عَلَى مَا نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٦٦﴾

**65. Na walipo fungua mizigo yao wakakuta bidhaa zao wamerudishiwa. Waka sema: Ewe baba yetu! Tutake nini zaidi? Hizi bidhaa zetu tumerudishiwa. Wacha tuwalettee watu wetu chakula, na tuta mlinda ndugu yetu, na tutaongeza shehena ya ngamia. Na hicho ni kipimo kidogo.**

**66. Akasema: Sitampeleka nanyi mpaka mnipe ahadi kwa Mwenyezi Mungu kwamba lazima mtamre-**

**jeza kwangu, ila ikiwa mmezungukwa. Basi walipo mpa ahadi yao alisema: Mwenyezi Mungu Ndiye Mtegemewa kwa tuyasemayo.**

### Wanakuta Fedha Zao Zimerejeshwa Katika Mifuko Yao

Anasema Allah تعالى, nduguze Yusuf عليه السلام walipofungua mifuko yao walikuta bidhaa zao, kwani Yusuf عليه السلام aliwaamrisha vijana wake wazirejeshe katika mizigo yao.

قَالُوا يَا أَبَانَا مَا نَبْغِي

**“Wakasema: Ewe baba yetu! Tutake nini zaidi?”**

Tutaomba nini kingine?

هَذِهِ بِضَعْتُنَا رُدَّتْ إِلَيْنَا

**“Hizi bidhaa zetu tumerudishiwa.”**

Qatadah alitoa rai (kuwa walisema), “Tuombe nini kingine, bidhaa zetu tumerejeshewa na Mheshimiwa ‘Aziz ametupa mzigo wa kutosha tuliotaka?”<sup>1</sup> Kisha wakasema,

وَنَمِيرُ أَهْلَنَا

**“Wacha tuwalettee watu wetu chakula.”**

Kama utatutuma pamoja na ndugu yetu safari ijayo tutakapokwenda kununua chakula kwa ajili ya familia yetu,

وَنَحْفَظُ أَخَانَا وَنَزِدَادُ كَيْلٍ بَعِيرٍ

**“Na tutamlinda ndugu yetu, na tutaongeza shehena ya ngamia.”**

Kwani Yusuf عليه السلام alimpa kila mtu nafaka za kutosha kubebwa na ngamia mmoja.

ذَلِكَ كَيْلٌ يَسِيرٌ

**“Na hicho ni kipimo kidogo.”** Walitamka maneno hayo ili hali yao iwe ya kuvutia zaidi, kwa kusema kuwa kumchukua ndugu yao kutafaa kuwezesha kupatikana kiasi hicho.

قَالَ لَنْ أَرْسَلَهُ مَعَكُمْ حَتَّى تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِنَ اللَّهِ

**“Akasema: Sitampeleka nanyi mpaka mnipe ahadi kwa Mwenyezi Mungu.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:162.

Mpaka muape kwa Allah تعالى kwa kiapo kizito,

لَتَأْتَنِي بِيَمِّهِ إِلَّا أَنْ سَخَّطَ بِكُمْ<sup>ط</sup>

**“Lazima mtamrejeza kwangu, ila ikiwa mmezungukwa.”**

Isipokuwa mtakaposhindwa nyote na mkashindwa kumuokoa,

فَلَمَّا آتَوْهُ مَوْتُهُمْ

**“Basi walipompa ahadi yao alisema,”**

Alitilia mkazo zaidi kwa kusema:

اللَّهُ عَلَىٰ مَا نَقُولُ وَكِيلٌ

**“Mwenyezi Mungu Ndiye Mtegemewa kwa tuyasemayo.”**

Ibn Is’haq رحمه الله تعالى amesema, “Yaakub عليه السلام alifanya hivyo kwa sababu hakuwa na hiari isipokuwa kuwatuma kwenda kuleta chakula muhimu cha kujikimu. Hivyo akamtuma Binyamin pamoja nao.”<sup>1</sup>

وَقَالَ يَبْنَئِي لَا تَدْخُلُوا مِن بَابٍ وَاحِدٍ وَأَدْخُلُوا مِن أَبْوَابٍ مُّتَفَرِّقَةٍ وَمَا أُغْنِي عَنْكُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ۗ إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٦٧﴾ وَلَمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ أَمَرَهُمْ أَبُوهُمْ مَا كَانَ يُغْنِي عَنْهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا حَاجَةٌ فِي نَفْسِ يَعْقُوبَ قَضَاهَا وَإِنَّهُ لَذُو عِلْمٍ لِّمَا عَلَّمْتَهُ وَلَبِئْنَ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾

**67. Na akasema: Enyi wanangu! Msiingie mlango mmoja, bali ingieni kwa milango mbali mbali. Wala mimi sikufaeni kitu mbele ya Mwenyezi Mungu. Hukumu haiko ila kwa Mwenyezi Mungu tu. Juu Yake Yeye mimi nimetegemea, na juu Yake Yeye wategemee wanaotegemea.**

**68. Na walipoingia kama alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa ni haja tu iliyokuwa katika nafsi ya Yaa'qub aliitimiza. Na hakika yeye alikuwa na ilimu kwa sababu Tulimfundisha; lakini watu wengi hawajui.**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:164.

## Yaakub عليه السلام Anawaamrisha Watoto Wake Waingie Misri Kupitia Milango Tofauti

Allah تعالی Anasema kuwa Yaakubu عليه السلام aliwaagiza wanaye, pindi alipomtuma Binyamin pamoja nao kwenda Misri, waingie milango tofauti, badala ya wote kuingia kwenye mlango mmoja. Ibn Abbas, Muhammad bin Ka'ab, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, As-Suddi na wengine wengi رضي الله عنهم walisema kuwa aliwaogopea kijicho, kwa sababu walikuwa ni wazuri, wenye mapambo mazuri, na mandhari ya kuvutia. Hivyo, alichelea watu kuwafanyia kijicho, kwani huwa kinadhuru, kwa kudura za Allah تعالی na humshusha mpanda farasi shujaa kutoka juu ya farasi wake. Kisha akasema,

وَمَا أَعْنِي عَنْكُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ ط

***"Wala mimi sikufaeni kitu mbele ya Mwenyezi Mungu."***

Maana yake: Kujilinda huku hakurudishi Makadiri ya Allah تعالی na Hukumu Yake, kwani Allah تعالی Akitaka jambo Hapingwi wala Hazuiwi.

إِنَّ الْحُكْمَ إِلَّا لِلَّهِ ط عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٦٧﴾ وَلَمَّا دَخَلُوا مِنْ حَيْثُ أَمَرَهُمْ أَبُوهُمْ مَا كَانَ يُغْنِي عَنْهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا حَاجَةً فِي نَفْسِ يَعْقُوبَ قَضَلَهَا ء

***"Hukumu haiko ila kwa Mwenyezi Mungu tu. Juu Yake Yeye mimi nimetegemea, na juu Yake Yeye wategemee wanaotegemea. Na walipoingia kama alivyowaamrisha baba yao, haikuwafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa ni haja tu iliyokuwa katika nafsi ya Yaa'qub aliitimiza."***

Wamesema haja yenyewe ni kuondoa kupatwa kwao na kijicho.

وَإِنَّهُ لَذُو عِلْمٍ لِمَا عَلَّمْنَاهُ

***"Na hakika yeye alikuwa na ilimu kwa sababu Tulimfundisha."***

Alikuwa na elimu aliyoitumia, kwa mujibu wa Qatadah na Ath-Thauri.<sup>1</sup> Ibn Jariri رحمه الله تعالی amesema: Kuwa sehemu hii ya Aya inamaanisha kuwa ana elimu Tuliyomfundisha.

<sup>1</sup> At-Tabari 16:168.

وَلَيْكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

*"Lakini watu wengi hawajui."*<sup>1</sup>

وَلَمَّا دَخَلُوا عَلَى يُوسُفَ ءَاوَىٰ ۖ إِلَيْهِ أَخَاهُ ۗ قَالَ إِنِّي أَنَا أَخُوكَ فَلَا تَبْتَئِسْ بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾

**69. Na walipoingia kwa Yusuf alimchukua nduguye akasema: Mimi hakika ni nduguye. Basi usihuzunike kwa waliyokuwa wakiyafanya.**

**Yusuf عليه السلام Anamliwaza Bin Yamin**

Allah تعالى Anaeleza kuwa nduguze Yusuf عليه السلام walimuendea pamoja na nduguye Binyamin na yeye akawaalika kwake kama wageni wa heshima, akawapa zawadi na kuwafanyia ukarimu na wema, akakaa faragha na ndugu yake na kumsimulia yaliyompata, akajua kwamba alikuwa ndugu yake, akamuambia:

فَلَا تَبْتَئِسْ

*"Usihuzunike..."* Usiyahuzunikie waliyonifanyia. Akamuamuru Binyamin asiwaambie hayo na asiwaambie kuwa Mheshimiwa 'Aziz ni ndugu yake, Yusuf عليه السلام. Akapanga naye mbinu ya kumfanya abakie Misri na kupata heshima na ukarimu mkubwa.

فَلَمَّا جَهَّزَهُمْ بِجَهَّازِهِمْ جَعَلَ السَّقَايَةَ فِي رَحْلِ أَخِيهِ ثُمَّ أَذَّنَ مُؤَذِّنٌ أَيَّتُهَا الْعَيْرُ انْكُم لَسِرْقُونَ ﴿٦٧﴾ قَالُوا وَأَقْبَلُوا عَلَيْهِمْ مَاذَا تَفْقَدُونَ ﴿٦٨﴾ قَالُوا نَفَقْدُ صَوَاعَ الْمَلِكِ وَلَمَن جَاءَ بِهِ حِمْلُ بَعِيرٍ وَأَنَا بِهِ زَعِيمٌ ﴿٦٩﴾

**70. Na alipokwisha watengenezea mahitaji yao akakitia kikopo cha kunywa maji katika mzigo wa nduguye huyo, kisha mnadi akanadi: Enyi wasafiri! Hapana shaka nyinyi ni wezi!**

**71. Wakasema nao wamewakabili: Kwani mmepoteza nini?**

**72. Wakasema: Tumepoteza kopo la mfalme. Na atayelileta atapewa shehena nzima ya ngamia. Nami ni mdhamini wa hayo.**

<sup>1</sup> Kama hapo juu

## Yusuf عليه السلام Anaweka Bakuli lake la Dhahabu Kwenye Mzigo wa Ndugu Yake; Mbinu Iliyotumika Abakie Misri

Baada ya Yusuf عليه السلام kuwapa chakula, aliwaagiza baadhi ya vijana wake kuweka bakuli la fedha (kwenye mzigo wa Bin Yamin), kwa mujibu wa wanazuoni wengi. Wengine walisema kuwa bakuli la mfalme lilikuwa limetengenezwa kwa dhahabu. Ibn Zaid amesema kuwa mfalme alikuwa analitumia kunywa vinywaji,<sup>1</sup> na baadaye alilitumia kupimia nafaka kwa kuwa chakula kilikuwa haba kwa wakati huo, kwa mujibu wa Ibn Abbas na Mujahid na Qatadah na Adh-Dhahhak na Abdur-Rahman Bin Zaid رضي الله عنهم.<sup>2</sup> Shu'bah amesema kuwa Abu Bishri ameeleza kuwa Sa'id Bin Jubayr alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, kipimo cha mfalme kilikuwa cha fedha na alikitumia kwa ajili ya kunywa.<sup>3</sup> Yusuf عليه السلام aliliweka bakuli hilo kwenye mzigo wa Bin Yamin huku hawatambui, halafu mtu akatangaza,

أَيُّهَا الْعَيْرُ إِنَّكُمْ لَسَرِقُونَ

**“Enyi wasafiri! Hapana shaka nyinyi ni wezi!”**

Wakamtazama mtangazaji huyo na wakamuuliza,

مَاذَا تَفْقَدُونَ ﴿٦٦﴾ قَالُوا نَفَقَدُ صُوعَ الْمَلِكِ

**“Kwani mmepoteza nini? Wakasema: Tumepoteza kopo la mfalme.”**

Alilokuwa akilitumia kupimia nafaka.

وَلَمَنْ جَاءَ بِهِ حِمْلُ بَعِيرٍ

**“Na atayelileta atapewa shehena nzima ya ngamia.”**

Kama zawadi.

وَأَنَا بِهِ زَعِيمٌ

**“Nami ni mdhamini wa hayo.”**

Yakuhakikisha zawadi inatolewa.

<sup>1</sup> At-Tabari 16:172.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:173.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:176.

قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا جِئْنَا لِنُفْسِدَ فِي الْأَرْضِ وَمَا  
 كُنَّا سَارِقِينَ ﴿٧٣﴾ قَالُوا فَمَا جَزَاؤُهُ إِنْ كُنْتُمْ كَذِبِينَ  
 ﴿٧٤﴾ قَالُوا جَزَاؤُهُ مَنْ وُجِدَ فِي رَحْلِهِ فَهُوَ جَزَاؤُهُ  
 كَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٧٥﴾ فَبَدَأَ بِأَوْعِيَّتِهِمْ قَبْلَ  
 وَعَاءِ أَخِيهِ ثُمَّ اسْتَخْرَجَهَا مِنْ وَعَاءِ أَخِيهِ كَذَلِكَ كِدْنَا  
 لِيُوسُفَ ۗ مَا كَانَ لِيَأْخُذَ أَخَاهُ فِي دِينِ الْمَلِكِ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ  
 اللَّهُ ۗ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَن نَّشَاءُ ۗ وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ  
 ﴿٧٦﴾ \* قَالُوا إِنْ يَسْرِقْ فَقَدْ سَرَقَ أَخٌ لَهُ مِنْ قَبْلُ  
 فَأَسْرَهَا يُوسُفُ فِي نَفْسِهِ وَلَمْ يُبَدِّهَا لَهُمْ ۗ قَالَ أَنْتُمْ شَرُّ  
 مَكَانًا ۗ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَصِفُونَ ﴿٧٧﴾ قَالُوا يَا أَيُّهَا  
 الْعَزِيزُ إِنَّ لَهُ أَبًا شَيْخًا كَبِيرًا فَخُذْ أَحَدَنَا مَكَانَهُ ۗ إِنَّا  
 نَرْنَكَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٧٨﴾ قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ أَنْ نَأْخُذَ  
 إِلَّا مَنْ وَجَدْنَا مَتَّعَيْنًا عِنْدَهُ ۗ إِنَّا إِذَا لَطَلِمُونَ ﴿٧٩﴾

قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا جِئْنَا  
 لِنُفْسِدَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كُنَّا سَارِقِينَ  
 ﴿٧٣﴾ قَالُوا فَمَا جَزَاؤُهُ إِنْ كُنْتُمْ  
 كَذِبِينَ ﴿٧٤﴾ قَالُوا جَزَاؤُهُ مَنْ  
 وُجِدَ فِي رَحْلِهِ فَهُوَ جَزَاؤُهُ ۗ كَذَلِكَ  
 نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٧٥﴾ فَبَدَأَ  
 بِأَوْعِيَّتِهِمْ قَبْلَ وَعَاءِ أَخِيهِ ثُمَّ  
 اسْتَخْرَجَهَا مِنْ وَعَاءِ أَخِيهِ ۗ كَذَلِكَ  
 كِدْنَا لِيُوسُفَ ۗ مَا كَانَ لِيَأْخُذَ  
 أَخَاهُ فِي دِينِ الْمَلِكِ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ  
 اللَّهُ ۗ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مَن نَّشَاءُ ۗ  
 وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ ﴿٧٦﴾

**73. Wakasema: Wallahi! Mnajua vyema kwamba**

*sisi hatukuja kufanya uharibifu katika nchi hii, wala sisi si wezi.*

**74. Wakasema: Basi malipo yake yatakuwa nini ikiwa nyinyi ni waongo?**

**75. Wakasema: Malipo yake ni yule ambaye ataonekana nalo yeye huyo ndiye malipo yake. Hivi ndivyo tunavyowalipa madhaalimu.**

**76. Basi akaanza kwenye mizigo yao kabla ya mzigo wa nduguye. Kisha akakitoa katika mzigo wa nduguye. Hivi ndivyo Tulivyompangia Yusuf. Hakuweza kumzuia nduguye kwa sharia ya mfalme isipokuwa alivyotaka Mwenyezi Mungu. Tunawatukuza kwenye vyeo Tuwatakao; na juu ya kila ajuae yupo ajuae zaidi.**



Baada ya Yusuf عليه السلام kumtuhumu wizi nduguye, walisema,

تَاللَّهِ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا جِئْنَا لِنُفْسِدَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كُنَّا سَارِقِينَ

**“Wakasema: Wallahi! Mnajua vyema kwamba sisi hatukuja kufanya uharibifu katika nchi hii, wala sisi si wezi.”**

‘Tangu ulipotujua, kutokana na tabia zetu, umejua wazi kuwa,

مَا جِئْنَا لِنُفْسِدَ فِي الْأَرْضِ وَمَا كُنَّا سَارِقِينَ

**“...hatukuja kufanya uharibifu katika nchi hii, wala sisi si wezi.”**

Walisema kuwa wizi si tabia yetu, kama ulivyojua. Watu wa Yusuf عليه السلام wakasema,

جَزَاءُ

**“Basi malipo yake yatakuwa nini...”**

Kama ni mmoja wenu?

إِنْ كُنْتُمْ كٰذِبِينَ

**“Ikiwa nyinyi ni waongo?”**

Waliwauliza, ‘Apewe adhabu gani, kama ni mmoja wenu?’

قَالُوا جَزَاءُ مَنْ وُجِدَ فِي رَحْلِهِ فَهُوَ جَزَاءُ<sup>٤</sup> كَذٰلِكَ نَجْزِي الظَّٰلِمِينَ ﴿٧٦﴾

**“Wakasema: Malipo yake ni yule ambaye ataonekana nalo yeye huyo ndiye malipo yake. Hivi ndivyo tunavyowalipa madhaalimu.”**

Ndivyo ilivyokuwa sheria ya Nabii Ibrahim عليه السلام kwamba mwenye kuiba hukabidhiwa kwa yule aliyeibiwa kuwa mtumwa wake. Hivyo ndivyo alivyotaka Yusuf عليه السلام na ndio sababu alianza kuvipekuwa vyombo vyao kabla ya chombo cha ndugu yake ili kufanikisha lengo lake.

ثُمَّ اسْتَخْرَجَهَا مِنْ وِعَاءِ أَخِيهِ

**“Kisha akakitoa katika mzigo wa nduguye.”**

Hivyo Yusuf عليه السلام alimchukua Binyamin kama mtumwa, kwa mujibu wa hukumu yao na ndiyo sheria waliyokuwa wakiamini. Kwa hivyo, Allah تعالى Akasema,

كَذَّالِكِ كَدْنَا لِيُوسُفَ ط

**“Hivi ndivyo Tulivyompangia Yusuf.”**

Huo ndio ubunifu mzuri unaopendwa na Allah تعالی, kwa sababu ndani yake kuna hekima na huwanufaisha wote.

Na Kauli Yake:

مَا كَانَ لِيَأْخُذَ أَخَاهُ فِي دِينِ الْمَلِكِ

**“Hakuweza kumzuia nduguye kwa sharia ya mfalme...”**

Kama mtumwa, kwa sababu hiyo haikuwa sheria ya mfalme wa Misri, kwa mujibu wa Adh-Dhahhak na wanazuoni wengine wengi.<sup>1</sup> Allah تعالی Alimruhusu Yusuf عليه السلام tu kumchukua nduguye kama mtumwa baada ya nduguye kuafiki kwanza, na alijua kuwa hiyo ilikuwa sheria yao. Ndiyo sababu Allah تعالی Alimsifu kwa Kusema,

تَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مِّنْ دُشَاءٍ ط

**“Tunawatukuza kwenye vyeo Tuwatakao.”**

Kama ilivyo katika Aya nyingine,

يَرْفَعُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ

**“Mwenyezi Mungu Atawainua walioamini miongoni mwenu.”**  
(58:11)

Kisha Allah تعالی Akasema,

وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ

**“...na juu ya kila ajuaye yupo ajuaye zaidi.”**

Al-Hassan Al-Basri رحمه الله تعالی amesema, “Hakuna mjuzi, isipokuwa yupo mwingine ajuae zaidi mpaka inaishia kwa Allah تعالی.<sup>2</sup> Kwa kuongezea, Abdur-Razzaq رحمه الله تعالی alinukuu kuwa Sa'id bin Jubayr رحمه الله تعالی alisema, “Tulikuwa

<sup>1</sup> At-Tabari 16:188.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:193.

pamoja na Ibn Abbas رضي الله عنهما, mtu mmoja akasimulia Hadithi ya kushangaza, alisema: 'Sifa njema Zinamstahiki Allah تعالى. Na juu ya kila mjuzi pana mjuzi zaidi." Ibn Abbas رضي الله عنهما akamjibu,,: 'Umesema maneno mabaya sana! Allah تعالى Ndiye Ajuaye yote na Ujuzi Wake uko juu ya kila ajuaye.'<sup>1</sup> Simak amesimulia kutoka kwa Ikrimah kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema.

وَفَوْقَ كُلِّ ذِي عِلْمٍ عَلِيمٌ

*"...na juu ya kila ajuaye yupo ajuaye zaidi."*

"Huyu ana elimu zaidi ya mwingine na Allah تعالى Yuko juu ya wote."<sup>2</sup> Masimulizi sawa na hayo yamesimuliwa na 'Ikrimah.<sup>3</sup> Qatadah amesema, "Juu ya kila mwenye elimu yupo mwenye elimu zaidi mpaka elimu yote inaishia kwa Allah تعالى.' Kwa hakika, elimu zote zimeanzia kwa Allah تعالى wasomi hujifundisha, na elimu zote zitarejea Kwake. 'Abdallah bin Mas'ud رضي الله عنهما aliisoma Ayah hiyo kama ifuatavyo,

(وَفَوْقَ كُلِّ عَالِمٍ عَلِيمٌ)

"Na juu ya kila ajuaye Yupo Ajuaye Zaidi (Allah تعالى)."<sup>4</sup>

قَالُوا إِن يَسْرِقَ فَقَدْ سَرَقَ أَخٌ لَهُ مِنْ قَبْلُ فَأَسْرَهَا يُوسُفُ فِي نَفْسِهِ وَلَمْ يُبْدِهَا لَهُمْ  
قَالَ أَنْتُمْ شَرُّ مَكَانٍ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَصِفُونَ ﴿٧٧﴾

**77. Wakasema: Ikiwa huyu ameiba, basi nduguye vile vile aliiba zamani. Lakini Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake wala hakuwaonesha. Akawaambia: Nyinyi mko katika hali mbaya zaidi, na Mwenyezi Mungu Anajua zaidi hayo mnayosingizia.**

<sup>1</sup> Abdur-Razzaq 2:327.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:192.

<sup>3</sup> Kama hapo juu.

<sup>4</sup> At-Tabari 16:193.

**Ndugu wa Yusuf عليه السلام Walimtuhumu kwa Wizi**

Nduguze Yusuf عليه السلام walipoona kipimo kimetolewa katika mzigo wa Bin Yamin, walisema,

إِنْ يَسْرِقَ فَقَدْ سَرَقَ أَخٌ لَهُ مِنْ قَبْلُ

**“Ikiwa huyu ameiba, basi nduguye vile vile aliiba zamani.”**

Walijaribu kujitoa katika hatia ya Binyamin, kwa kusema kuwa amefanya kama alivyofanya ndugu yake huko nyuma, yaani Yusuf عليه السلام. Kauli ya Allah تعالى,

فَأَسْرَهَا يُوسُفُ فِي نَفْسِهِ

**“Lakini Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake...”**Maana: Maneno aliyoyasema baada ya hapo,

أَنْتُمْ شَرُّ مَكَّانًا وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَصِفُونَ

**“Nyinyi mko katika hali mbaya zaidi, na Mwenyezi Mungu Anajua zaidi hayo mnayosingizia.”**

Yusuf عليه السلام alijisemea hayo moyoni bila kuyatamka kwa sauti kwa kukusudia kufanya siri moyoni mwake kabla ya kutaja. Al-Awfi ametaarifu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

فَأَسْرَهَا يُوسُفُ فِي نَفْسِهِ

**“Yusuf aliyaweka siri moyoni mwake...”** Aliyahifadhi katika nafsi yake.

أَنْتُمْ شَرُّ مَكَّانًا وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَصِفُونَ

**“Nyinyi mko katika hali mbaya zaidi, na Mwenyezi Mungu Anajua zaidi hayo mnayosingizia.”**

قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ إِنَّ لَهُ أَبًا شَيْخًا كَبِيرًا فَخُذْ أَحَدَنَا مَكَانَهُ إِنَّا نَرَاكَ مِنَ

الْمُحْسِنِينَ ﴿٧٦﴾ قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ أَنْ نَأْخُذَ إِلَّا مَنْ وَجَدْنَا مَتَّعْنَا عِنْدَهُ إِنَّا إِذَا

لَطَلِمُونَ ﴿٧٧﴾

**78. Wakasema: Ewe Mheshimiwa! Huyu anaye baba mzee sana. Kwa hivyo mchukue mmoja wetu badala yake. Hakika sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.**

**79. Akasema: Mwenyezi Mungu Apishe mbali kumshika yeyote yule isipokuwa tuliyemkuta naye kitu chetu. Hivyo basi tutakuwa wenye kudhulumu.**

**Ndugu wa Yusuf عليه السلام Watoa Pendekezo la Kutiwa Hatiani Mtu Mwingine Badala ya Bin Yamin na Wanakataliwa.**

Ilipoamuliwa kuwa Bin yamin abakie kwa mujibu wa sheria yao, nduguze Yusuf عليه السلام walianza kusihi wahurumiwe,

قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ إِنَّ لَهُ أَبًا شَيْخًا كَبِيرًا

**“Wakasema: Ewe Mheshimiwa kwa hakika huyu anaye baba mzee sana.”**

Anampenda sana na analiwazika naye kwa sababu ya mwanaye aliyemkosa.

فَخُذْ أَحَدَنَا مَكَانَهُ

**“Kwa hiyo mchukue mmoja wetu badala yake.”**

Badala ya Bin Yamin kubakia,

إِنَّا نَرْنَكَ مِنَ الْمُحْسِنِينَ

**“Hakika sisi tunakuona wewe ni katika watu wema.”**

Watenda mema, waadilifu na wenye kukubali kheri.

قَالَ مَعَاذَ اللَّهِ أَنْ نَأْخُذَ إِلَّا مَنْ وَجَدْنَا مَتَّعِنَا بِهِ

**“Akasema: Mwenyezi Mungu Apishe mbali kumshika yeyote yule isipokuwa tuliyemkuta naye kitu chetu.”**

Kulingana na hukumu na adhabu yake,

إِنَّا إِذَا لَطَمُوا

**“Hivyo basi tutakuwa wenye kudhulumu.”** Maana: Iwapo tutamchukua aliye mzima kwa sababu ya mgonjwa.

فَلَمَّا اسْتَيْسَسُوا مِنْهُ خَلَصُوا نَجِيًّا ۗ قَالَ كَبِيرُهُمْ أَلَمْ  
 تَعْلَمُوا أَنَّ أَبَاكُمْ قَدْ أَخَذَ عَلَيْكُمْ مَوْثِقًا مِنَ اللَّهِ وَمِنْ  
 قَبْلُ مَا فَرَطْتُمْ فِي يُوسُفَ ۗ فَلَنْ أَرْجِعَ الْأَرْضَ حَتَّى يَأْذَنَ لِي  
 أَبِي أَوْ يَحْكُمَ اللَّهُ لِي ۗ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿٨٠﴾ أَرْجِعُوا إِلَيَّ  
 أَبِيكُمْ فَقُولُوا يَا أَبَانَا إِنَّ أَبْنَتَكَ سَرَقَتْ وَمَا شَهِدْنَا إِلَّا بِمَا  
 عَلَّمْنَا وَمَا كُنَّا لِلْغَيْبِ حَافِظِينَ ﴿٨١﴾ وَسَلِّ الْقَرْيَةَ الَّتِي  
 كُنَّا فِيهَا وَالْعَيْرَ الَّتِي أَقْبَلْنَا فِيهَا ۗ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٨٢﴾  
 قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا ۗ فَصَبْرٌ حَمِيلٌ ۗ عَسَى اللَّهُ  
 أَنْ يَأْتِيَنِي بِهِمْ جَمِيعًا ۗ إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٨٣﴾  
 وَتَوَلَّى عَنْهُمْ وَقَالَ يَا أَسْفَىٰ عَلَىٰ يُوسُفَ وَأَبْطِضتْ عَيْنَاهُ  
 مِنَ الْحُزَنِ فَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٨٤﴾ قَالُوا تَاللَّهِ تَفْتُونَا تَذَكُرُ  
 يُوسُفَ حَتَّى تَكُونَ حَرَضًا أَوْ تَكُونَ مِنَ الْهَالِكِينَ ﴿٨٥﴾  
 قَالَ إِنَّمَا أَشْكُوا بِنِّي وَحُزْنِي إِلَى اللَّهِ وَاعْلَمُ مِنَ  
 اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨٦﴾

فَلَمَّا اسْتَيْسَسُوا مِنْهُ خَلَصُوا نَجِيًّا ۗ  
 قَالَ كَبِيرُهُمْ أَلَمْ تَعْلَمُوا أَنَّ  
 أَبَاكُمْ قَدْ أَخَذَ عَلَيْكُمْ مَوْثِقًا مِنَ اللَّهِ  
 وَمِنْ قَبْلُ مَا فَرَطْتُمْ فِي يُوسُفَ ۗ فَلَنْ  
 أَرْجِعَ الْأَرْضَ حَتَّى يَأْذَنَ لِي أَبِي أَوْ  
 يَحْكُمَ اللَّهُ لِي ۗ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ  
 ﴿٨٠﴾ أَرْجِعُوا إِلَيَّ أَبِيكُمْ فَقُولُوا  
 يَا أَبَانَا إِنَّ أَبْنَتَكَ سَرَقَتْ وَمَا شَهِدْنَا  
 إِلَّا بِمَا عَلَّمْنَا وَمَا كُنَّا لِلْغَيْبِ  
 حَافِظِينَ ﴿٨١﴾ وَسَلِّ الْقَرْيَةَ الَّتِي  
 كُنَّا فِيهَا وَالْعَيْرَ الَّتِي أَقْبَلْنَا فِيهَا ۗ  
 وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٨٢﴾

80. Walipokata tamaa naye wakenda kando kunong'ona. Mkubwa wao akasema: Je! Hamjui ya kwamba baba

yenu amechukua ahadi kwenu kutokana na Mwenyezi Mungu, na kabla ya hapo mlimkosa katika agano lenu juu ya Yusuf? Basi mimi sitotoka nchi hii mpaka baba yangu anipe ruhusa au Mwenyezi Mungu Anihukumie. Na Yeye Ndiye Mbora wa mahakimu.

81. Rudini kwa baba yenu, na muambieni: Ee baba yetu! Mwanao ameiba. Na sisi hatutoi ushahidi ila kwa tunayoyajua. Wala sisi hatukuwa wenye kuhifadhi mambo ya ghaibu.

82. Na waulize watu wa mji tuliokuwako, na msafara tuliokuja nao. Na hakika sisi tunasema kweli.

## Ndugu Zake Yusuf عليه السلام Kushauriana Kwao kisiri na Ushauri Aliowapa Mkubwa Wao

Allah تعالى Anatueleza kuwa nduguze Yusuf عليه السلام walikata tamaa ya kuweza kufanikisha kuachiliwa Bin Yamin, ingawa walimuahidi baba yao na kuapa kuwa wangemrejsha. Walishindwa kutimiza ahadi yao kwa baba yao, kwa hivyo,

خَلَّصُوا

“...wakenda kando...” Mbali na watu

يَحْيَا

“Kunong’ona,” Baina yao,

قَالَ كَبِيرُهُمْ

“Mkubwa wao akasema...”

Jina lake, kama tulivyosema, ni Rubil au Yahudha. Ndiye aliyewashauri kumtupa Yusuf عليه السلام kisimani, badala ya kumuua. Rubil akawaambia,

أَلَمْ تَعْلَمُوا أَنَّ أَبَاكُمْ قَدْ أَخَذَ عَلَيْكُمْ مَوْثِقًا مِنَ اللَّهِ

“Je! Hamjui ya kwamba baba yenu amechukua ahadi kwenu kutokana na Mwenyezi Mungu.”

Kuwa mtamrudisha kwake? Lakini mlishindwa kutimiza ahadi, na kabla ya hapo mlisababisha Yusuf عليه السلام apotezane na baba yake.

فَلَنْ أَبْرَحَ الْأَرْضَ

“Basi mimi sitotoka nchi hii.” Sitaondoka Misri.

حَتَّى يَأْذَنَ لِي أَبِي

“...mpaka baba yangu anipe ruhusa...” Ya kurejea kwake (baba) huku akiwa radhi kwangu,

أَوْ يَحْكُمَ اللَّهُ لِي

“Au Mwenyezi Mungu Anihukumie.” Kwa panga, au ilisemekana, kwa kuniwezesha kufanikisha kuachiliwa huru kwa ndugu yangu.

وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ

**“Na Yeye Ndiye Mbora wa mahakimu.”**

Kisha akawaamrisha wamueleze baba yao kuhusu yaliyotokea ili uwe udhuru wao kwa yaliyompata, na wamuoneshe kuwa hawakuwa na makosa. Rubil aliwaambia (kuwa wamuambie baba yao),

وَمَا كُنَّا لِلْغَيْبِ حَافِظِينَ

**“Wala sisi hatukuwa wenye kuhifadhi mambo ya ghaibu.”**

Au, hatukujua kuwa mwanao ameiba, kwa mujibu wa Qatadah na Ikrima.<sup>1</sup> Abdur-Rahman bin Zaid Bin Aslam amesema kuwa inamaanisha, ‘Hatukujua kuwa Binyamin aliiba kitu cha mfalme, bai sisi tulieleza tu adhabu ya mwizi.’

وَسَأَلَ الْقَرْيَةَ الَّتِي كُنَّا فِيهَا

**“Na waulize watu wa mji tulio kuwako.”**

Imekusudiwa Misri,<sup>1</sup> kwa mujibu wa Qatadah,<sup>2</sup> au mji mwingine.

وَالْعِيرَ الَّتِي أَقْبَلْنَا فِيهَا<sup>ط</sup>

**“Na msafara tuliokuja nao.”**

Kuhusu ukweli, uaminifu, ulinzi na uangalizi wetu.

وَإِنَّا لَصَادِقُونَ

**“Na hakika sisi tunasema kweli.”**

Kwa tuliyokueleza kwamba Binyamin aliiba na akafanywa mtumwa kama fidia.

<sup>1</sup> At-Tabari 16:211-212.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:210.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:212.



قَالَ بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا ۖ فَصَبْرٌ جَمِيلٌ ۗ عَسَىٰ اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَنِي بِهِمْ جَمِيعًا ۚ إِنَّهُ هُوَ  
 الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿٨٤﴾ وَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَا أَسْفَىٰ عَلَىٰ يُونُسَ ۖ وَأَبْيَضَّتْ عَيْنَاهُ مِنَ  
 الْحُزَنِ فَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٨٥﴾ قَالُوا تَاللَّهِ تَفْتُنَا تَذَكَّرُ يُونُسَ ۖ حَتَّىٰ تَكُونَ حَرَضًا أَوْ تَكُونَ  
 مِنَ الْهَالِكِينَ ﴿٨٦﴾ قَالَ إِنَّمَا أَشْكُوا بَنِي وَحُرِّيَ إِلَى اللَّهِ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا  
 تَعْلَمُونَ ﴿٨٧﴾

**83. Akasema: Bali nafsi zenu zimekushawishini kwenye jambo fulani. Subira ni njema! Asaa Mwenyezi Mungu Akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye Hikima.**

**84. Naye akajitenga nao, na akasema: Ah! Masikini Yusuf! Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni aliyokuwa akiizuia.**

**85. Wakasema: Wallahi! Huachi kumkumbuka Yusuf mpaka uwe mgonjwa au uwe katika waliohiliki.**

**86. Akasema: Hakika mimi namshitakia Mwenyezi Mungu sikitiko langu na huzuni yangu. Na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua nyinyi.**

### Yaakub عليه السلام Anapata Habari za Kuhuzunisha

Mtume Yaakub عليه السلام aliwakariria wanaye maneno yaleyale walipomletea damu ya uongo katika kanzu ya Yusuf عليه السلام,

بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا ۖ فَصَبْرٌ جَمِيلٌ ۗ

**“Bali nafsi zenu zimekushawishini kwenye jambo fulani. Subira ni njema!”**

Muhammad Bin Is’haq رحمه الله تعالى amesema, “Waliporejea kwa Yaakub عليه السلام na kumuambia yaliyotokea, hakuwaamini na alidhani kuwa kitendo kicho kinakariri waliyomfanyia Yusuf عليه السلام, akasema:

بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْرًا ۖ فَصَبْرٌ جَمِيلٌ ۗ

**“Bali nafsi zenu zimekushawishini kwenye jambo fulani. Subira ni njema!”**

Wengine wamesema: Kwa kuwa kitendo hiki kimekuja baada ya yale waliyofanya hapo zamani (kwa Yusuf عليه السلام), walipewa hukumu sawa na ile ya tukio la awali. Kwa hivyo, kauli ya Yakubu عليه السلام hapa inafaa,

بَلْ سَوَّلَتْ لَكُمْ أَنْفُسُكُمْ أَمْراً فَصَبْرٌ جَمِيلٌ

***“Bali nafsi zenu zimekushawishini kwenye jambo fulani. Subira ni njema!”***

Kisha akamuomba Allah تعالى Amrejeshee wanaye watatu: “Yusuf, Bin'yamin na Rubil.”<sup>1</sup> Rubil alibakia Misri kusubiri Uamuzi wa Allah تعالى kuhusu jambo hilo, ama baba yake amridhie au amchukue nduguye kisiri, kwa sababu hiyo amesema:

عَسَى اللَّهُ أَنْ يَأْتِيَنِي بِهِمْ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ

***“Asaa Mwenyezi Mungu Akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi.”***

Wa huzuni yangu.

الْحَكِيمُ

***“Mwenye Hikima.”***

Katika Maamuzi, Hukumu na Kudura. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَتَوَلَّى عَنْهُمْ وَقَالَ يَا سَفَىٰ عَلَىٰ يُوسُفَ

***“Naye akajitenga nao, na akasema: Ah! Masikini Yusuf!”***

Aliwapa mgongo wanaye, akakumbuka huzuni yake ya zamani, Yusuf عليه السلام.

يَا سَفَىٰ عَلَىٰ يُوسُفَ

***“...Ah! Masikini Yusuf!”***

Huzuni mpya ya kuwakosa wanaye wawili, Bin'yamin na Rubil. Abdur-Razzaaq amesimulia kuwa Ath-Thawri alisema kuwa Sufyani Al-'Usfuri alisema kuwa Sa'id bin Jubayr alisema, “Umma huu peke yake (wa Muhammad ﷺ) ndio uliopewa Al-Istirja.<sup>2</sup> Kwani hamkusikia kauli ya Yaakub عليه السلام,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:214.

<sup>2</sup> Kusema: “Sisi ni wa Allah تعالى na Kwake tutarejea.”

يَتَأْسَفَىٰ عَلَىٰ يُونُسَ وَأَبْيَضَتْ عَيْنَاهُ مِنَ الْحُزْنِ فَهُوَ كَظِيمٌ

**“Ah! Masikini Yusuf! Na macho yake yakawa meupe kwa huzuni aliyokuwa akiizuia.”<sup>2</sup>**

Yaakub عليه السلام alizuia huzuni zake na hakumlalamikia kiumbe yeyote, kwa mujibu wa Qatadah na wengine,<sup>3</sup> Adh-Dhahhak pia alisema, ‘Yaakub عليه السلام alihuzunika.<sup>4</sup> Wanaye Yaakub عليه السلام walimhurumia, na wakasema kwa huzuni na huruma,

تَاللَّهِ تَفْتَتُوا تَذَكُرُ يُونُسَ

**“Wallahi! Huachi kumkumbuka Yusuf,”**

Hutaacha kumkumbuka Yusuf عليه السلام,

حَتَّىٰ تَكُونَ حَرَضًا

**“Mpaka uwe mgonjwa.”**

Mpaka ukose nguvu.

أَوْ تَكُونَ مِنَ الْهَالِكِينَ

**“Au uwe katika waliohiliki.”**

Walisema, ‘Ukiendelea hivyo, tunahofia kuwa utakufa kwa huzuni.”

قَالَ إِنَّمَا أَشْكُوا بَنِي وَحُرِّيَّ إِلَى اللَّهِ

**“Akasema: Hakika mimi namshitakia Mwenyezi Mungu sikitiko langu na huzuni yangu.”**

Walipomuambia hayo, aliwaambia,

إِنَّمَا أَشْكُوا بَنِي وَحُرِّيَّ

**“Hakika mimi namshitakia sikitiko langu na huzuni yangu.”** Kwa majanga yaliyonikumba,

<sup>1</sup> Abdur-Razzaq 2:227.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:216.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:218.

إِلَى اللَّهِ

“... *namshitakia Mwenyezi Mungu,*” Peke Yake,

وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

“*Na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua nyinyi.*”

Nina tumaini heri zote, kutoka kwa Allah تعالى. Ibn Abbas رضي الله عنهما ametoa rai juu ya maana ya Aya,

وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

“*Na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua nyinyi.*”

Ndoto aliyoota Yusuf عليه السلام ni ya kweli na kwa hakika, Allah تعالى Ataitimiza.<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 16:227.

يَنْبِيَّ أَذْهَبُوا فَتَحَسَّسُوا مِنْ يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَأْيِسُوا مِنْ رُوحِ اللَّهِ إِنَّهُ لَا يَأْيِسُ مِنْ رُوحِ اللَّهِ إِلَّا الْكَافِرُونَ ﴿٧٧﴾ فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَيْهِ قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ مَسْنَا وَأَهْلْنَا الضُّرَّ وَجِئْنَا بِبِضْعَةٍ مُزَجَّجَةٍ فَأَوْفِ لَنَا الْكَيْلَ وَتَصَدَّقْ عَلَيْنَا إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي الْمُتَصَدِّقِينَ ﴿٧٨﴾ قَالَ هَلْ عَلِمْتُمْ مَا فَعَلْتُمْ بِيُوسُفَ وَأَخِيهِ إِذْ أَنْتُمْ جَاهِلُونَ ﴿٧٩﴾ قَالُوا أَءِنتَ لَا تَأْتِيكَ الْيُوسُفَ قَالَ أَنَا يُوسُفُ وَهَذَا أَخِي قَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْنَا إِنَّهُ مَنْ يَتَّقِ وَيَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٠﴾ قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ ءَاثَرَكَ اللَّهُ عَلَيْنَا وَإِنْ كُنَّا لَخَطِئِينَ ﴿٨١﴾ قَالَ لَا تَثْرِبَ عَلَيْكُمْ أَيُّومًا طَغَى يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٨٢﴾ أَذْهَبُوا بِقَمِيصِي هَذَا فَأَلْقُوهُ عَلَى وَجْهِ أَبِي يَأْتِ بَصِيرًا وَأْتُونِي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٣﴾ وَلَمَّا فَصَلَتِ الْعِيرُ قَالَ أَبُوهُمْ إِنِّي لَأَجِدُ رِيحَ يُوسُفَ لَوْلَا أَنْ تَفَنَّدُونَ ﴿٨٤﴾ قَالُوا تَاللَّهِ إِنَّكَ لَفِي ضَلَالِكَ الْقَدِيمِ ﴿٨٥﴾ فَلَمَّا أَنْ جَاءَ الْبَشِيرُ أَلْقَاهُ عَلَى وَجْهِهِ فَارْتَدَّ بَصِيرًا قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨٦﴾ قَالُوا يَا بَنَاتَنَا اسْتَعْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ﴿٨٧﴾ قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٨٨﴾

يَنْبِيَّ أَذْهَبُوا فَتَحَسَّسُوا مِنْ يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَأْيِسُوا مِنْ رُوحِ اللَّهِ إِنَّهُ لَا يَأْيِسُ مِنْ رُوحِ اللَّهِ إِلَّا الْكَافِرُونَ ﴿٧٧﴾ فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَيْهِ قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ مَسْنَا وَأَهْلْنَا الضُّرَّ وَجِئْنَا بِبِضْعَةٍ مُزَجَّجَةٍ فَأَوْفِ لَنَا الْكَيْلَ وَتَصَدَّقْ عَلَيْنَا إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي الْمُتَصَدِّقِينَ ﴿٧٨﴾

**87. Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na faraja ya Mwenyezi Mungu. Hakika hawakati tamaa na faraji ya Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri.**

**88. Basi walipoingia kwa Yusuf walisema: Ewe Mheshimiwa! Imetupata shida, sisi na watu wetu. Na tumeleta mali kidogo. Basi tupimie kipimo na fanya kama unatupa sadaka. Hakika Mwenyezi Mungu Huwalipa watoao sadaka.**

## Yakubu عليه السلام Anawaamuru Wanaye Wapeleleze kuhusu Yusuf عليه السلام na Nduguye

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yaakub عليه السلام aliwataka wanaye warejee na wapeleleze habari 'Tahassus' (kwa wema) za Yusuf عليه السلام na nduguye Binyamin, na sio Tajassus (kupeleleza kwa ubaya). Aliwahamasisha, akawapa bishara na kuwaamrisha wasikate tamaa na Rehma za Allah تعالى, Aliwaambia kuwa makafiri ndio wenye kukata tamaa na Rehma za Allah تعالى.

## Nduguze Yusuf عليه السلام Wanasimama Mbele Yake

Kisha Allah تعالى Akasema,

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَيْهِ

**"Basi walipoingia kwa Yusuf..."**

Waliporejea Misri na wakaingia kwa Yusuf عليه السلام,

قَالُوا يَا أَيُّهَا الْعَزِيزُ مَسَّنَا وَأَهْلَنَا الضُّرُّ

**"...walisema: Ewe Mheshimiwa! Imetupata shida, sisi na watu wetu."**

Kwa sababu ya ukame na uhaba wa chakula.

وَجَعَلْنَا بِيضَنَّهُ مُزَجَّلَةً

**"Na tumeleta mali kidogo."**

Maana yake: Tumeleta pesa za kununulia chakula, lakini ni chache, kwa mujibu wa Mujahid, Al-Hassan na wengine wengi.<sup>1</sup> Allah تعالى Ameeleza kuwa waliongeza kusema,

فَأَوْفٍ لَنَا الْكَيْلَ

**"Basi tupimie kipimo."** Kwa pesa hizi chache tulizoleta, utupe kipimo kamili kama hapo awali. Ibn Masud رضي الله عنه, ameisoma Aya hiyo kwa namna inayomaanisha, "Tupe kipimo kamili juu ya ngamia wetu na uwe mwenye kutupa sadaka."<sup>2</sup> Ibn Jurayji amesema, "Tupe sadaka kwa kuturejeshea ndugu yetu."<sup>3</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 16:238.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:228.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:243.

Sufyani bin Uayyana alipoulizwa kama sadaka ilikatazwa kwa Mtume yeyote kabla ya Mtume wetu ﷺ, alisema, "Hamkusikia Aya?"

فَأَوْفِرْنَا لَنَا الْكَيْلَ وَتَصَدَّقْ عَلَيْنَا إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي الْمُتَصَدِّقِينَ

**"Basi tupimie kipimo na fanya kama unatupa sadaka Hakika Mwenyezi Mungu Huwalipa watoao sadaka."**<sup>1</sup>

Ameikusanya Ibn Jarir At-Tabari رحمه الله تعالى.

قَالَ هَلْ عَلِمْتُمْ مَا فَعَلْتُمْ بِيُوسُفَ وَأَخِيهِ إِذْ أَنْتُمْ جَاهِلُونَ ﴿٨٧﴾ قَالُوا أءَنْتَ لَأَنْتَ يُوسُفُ قَالَ أَنَا يُوسُفُ وَهَذَا أَخِي قَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْنَا إِنَّهُ مَنْ يَتَّقِ وَيَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٨﴾ قَالُوا تَاللَّهِ لَقَدْ ءَاثَرَكَ اللَّهُ عَلَيْنَا وَإِنْ كُنَّا لَخَطِئِينَ ﴿٨٩﴾ قَالَ لَا تَثْرِبَ عَلَيْكُمْ أَيُّومَ يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٩٠﴾

**89. Akasema: Je! Mmejua mliyomfanyia Yusuf na nduguye mlipokuwa wajinga?**

**90. Wakasema: Kumbe wewe ndiye Yusuf? Akasema: Mimi ndiye Yusuf, na huyu ni ndugu yangu. Mwenyezi Mungu Ametufanyia hisani. Hakika anayemcha Mungu na akasubiri, basi Mwenyezi Mungu Haachi ukapotea ujira wa wafanyao mema.**

**91. Wakasema: Wallahi! Mwenyezi Mungu Amekufadhilisha wewe kuliko sisi, na hakika sisi tulikuwa wenye kukosa.**

**92. Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu Atakusameheni, naye ni Mwingi wa Kurehemu kuliko wote wanao rehemu.**

**Yusuf عليه السلام Anajitambulisha kwa Nduguze na Kuwasamehe**

Allah تعالى Anasema kuwa nduguze Yusuf عليه السلام walipomuelezea majanga, taabu, dhiki, uhaba wa chakula kufuatia ukame uliowakumba, na akakumbuka huzuni ya baba yake kwa kuwapoteza wanaye wawili, alimhurumia na kumsikitikia baba yake na nduguze. Alijihisi hivyo, hususani kwa kuwa alikuwa akifurahia ufalme, mamlaka na nguvu, basi alilia na akawadhihirishia, pale alipowauliza,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:242.

هَلْ عَلِمْتُمْ مَا فَعَلْتُ بِيُوسُفَ وَأَخِيهِ إِذْ أَنْتُمْ جَاهِلُونَ

**“Akasema: Je! Mmejua mliyomfanyia Yusuf na nduguye mlipokuwa wajinga?”**

Maana yake: Mlipomtenganisha Yusuf عليه السلام na nduguye,

إِذْ أَنْتُمْ جَاهِلُونَ

**“Mlipokuwa wajinga?”** Kilichosababisha mfanye hayo ni ujinga wenu kuhusu dhambi kubwa mliyokaribia kuifanya, inaonekana, Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi, kuwa Yusuf عليه السلام alijitambulisha kwao kwa amri ya Allah تعالى. Kama alivyojificha dhidi yao mara mbili za mwanzo walipokutana, kwa amri ya Allah تعالى. Janga lilipoongezeka zaidi, Allah تعالى Alitoa Msaada Wake kutokana na dhiki hiyo, kama Alivyo sema Allah تعالى:

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾

**“Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi. Hakika pamoja na uzito upo wepesi.” (94:5-6)**

Hapo ndipo wakamuambia Yusuf عليه السلام,

أُوَيْسُفُ لَأَنْتَ لَأَنْتَ يُوسُفُ

**“Kumbe wewe ndiye Yusuf?”**

Kwa mshangao kwa sababu walikuwa wakikutana kwa zaidi ya miaka miwili huku wakiwa hawamjui kwa hakika. Lakini yeye aliwajua wao na habari zao. Kwa hivyo, wakauliza kwa mshangao,

أُوَيْسُفُ لَأَنْتَ لَأَنْتَ يُوسُفُ قَالَ أَنَا يُوسُفُ وَهَذَا أَخِي

**“Kumbe wewe ndiye Yusuf? Akasema: Mimi ndiye Yusuf, na huyu ni ndugu yangu.”**

Kisha Yusuf عليه السلام akasema,

قَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَيْنَا

**“Mwenyezi Mungu Ametufanyia hisani,”** kwa kutokusanya baada ya kutengana kwa muda wote huo.



إِنَّهُ مَنْ يَتَّقِ وَيَصْبِرْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿٨٧﴾ قَالُوا تَأَلَّه لَقَدْ ءَاثَرَكَ اللَّهُ عَلَيْنَا

***“Hakika anayemcha Mungu na akasubiri, basi Mwenyezi Mungu Haachi ukapotea ujira wa wafanyao mema. Wakasema: Wallahi! Mwenyezi Mungu Amekufadhilisha wewe kuliko sisi.”***

Kwa kukiri ubora wa Yusuf عليه السلام, kubarikiwa uzuri, tabia, utajiri, ufalme, mamlaka, na juu ya yote, utume. Walikiri kosa lao na wakakubali kuwa walimkosea.

قَالَ لَا تَتْرِبَ عَلَيْكُمُ الْيَوْمَ

***“Leo hapana lawama juu yenu.”***

Aliwaambia, Leo hamtalaumiwa wala kukaripiwa, nami sitakukumbusheni baada ya leo kuhusu kosa mlilonifanyia. Kisha aliwafanyia ukarimu mkubwa zaidi kwa kuwaomba Rehema za Allah تعالى.

يَغْفِرُ اللَّهُ لَكُمْ وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

***“Mwenyezi Mungu Atakusameheni, naye ni Mwingi wa Kurehemu kuliko wote wanao rehemu.”***

أَذْهَبُوا بِقَمِيصِي هَذَا فَأَلْقُوهُ عَلَى وَجْهِ أَبِي يَأْتِ بَصِيرًا وَأْتُونِي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٨﴾  
 ﴿٨٩﴾ وَلَمَّا فَصَلَتِ الْعِيرُ قَالَ أَبُوهُمْ إِنِّي لَأَجِدُ رِيحَ يُوسُفَ لَوْلَا أَنْ تُفَنِّدُونِ ﴿٩٠﴾  
 قَالُوا تَأَلَّه إِنَّكَ لَفِي ضَلَالِكَ الْقَدِيمِ ﴿٩١﴾

***93. Nendeni na kanzu yangu hii na mumuekee usoni baba yangu, atakuwa mwenye kuona. Na mje nao watu wenu wote wa nyumbani.***

***94. Na ulipoondoka tu msafara baba yao alisema: Hakika mimi nasikia harufu ya Yusuf, lau kuwa hamtanituhumu.***

***95. Wakasema: Wallahi! Hakika bado ungali katika upotovu wako wa zamani.***

Ya'kubu عليه السلام Anapata Harufu ya Yusuf عليه السلام kwenye Kanzu

Anasema: Chukueni kanzu yangu hii,

فَأَلْقُوهُ عَلَىٰ وَجْهِ أَبِي يَأْتِ بَصِيرًا

***“Na mumuekee usoni baba yangu, atakuwa mwenye kuona.”***

Kwani, alipofuka kutokana na kulia sana.

وَأَتُونِي بِأَهْلِكُمْ أَجْمَعِينَ

***“Na mje nao watu wenu wote wa nyumbani.”***

Watoto wote wa Ya'kubu عليه السلام,

وَلَمَّا فَصَلَتِ الْعِيرُ

***“Na ulipoondoka tu msafara...”*** Kutoka Misri

قَالَ أَبُوهُمْ

***“...baba yao alisema...”***

Ya'kub عليه السلام aliwaambia wanawe waliokuwa wamebakia naye.

إِنِّي لَأَجِدُ رِيحَ يُوسُفَ ۖ لَوْلَا أَن تَفْنَدُونَ

***“Hakika mimi nasikia harufu ya Yusuf, lau kuwa hamtanituhumu.”***

Mtadhania nimeharibikiwa akili kwa uzee. 'Abdur-Razzaq amesimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Msafara ulipoondoka Misri, upepo ulivuma, ukampelekea Yaakubu عليه السلام harufu ya kanzu ya Yusuf عليه السلام.” Akasema,

إِنِّي لَأَجِدُ رِيحَ يُوسُفَ ۖ لَوْلَا أَن تَفْنَدُونَ

***“Hakika mimi nasikia harufu ya Yusuf, lau kuwa hamtanituhumu.”***

“Aliipata harufu yake kutokea masafa ya mwendo wa siku nane.”<sup>1</sup> Riwaya kama hiyo imepokewa kupita kwa Sufyani Thauri na Shu'ubah na wengine waliosimulia kutoka kwa Abu Sinan.<sup>2</sup> Yaakub عليه السلام akawaambia,

<sup>1</sup> 'Abdur-Razzaq 2:329.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:250.

لَوْلَا أَن تَفْقَهُوا

**“Lau kuwa hamtanituhumu.”**

Ibn Abbas, Mujahid, Ataa, Qatadah na Sa'id bin Jubair رضي الله عنهم, wamesema, “Kama hamtanidhanja mpumbavu.”<sup>1</sup> Mujahid na Al-Hassan walisema: Kuwa inamaanisha, “Kama hamtaniona mzee.”<sup>2</sup> Jibu lao lilikuwa,

إِنَّكَ لَفِي ضَلَالِكَ الْقَدِيمِ

**“Wallahi! Hakika bado ungali katika upotovu wako wa zamani.”**

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, ‘umo katika kosa lako la zamani.’<sup>3</sup> Qatadah amesema, walimaanisha, ‘kwa sababu unampenda sana Yusuf عليه السلام, hutamsahau.’ Wakamuambia baba yao maneno makali yasiyofaa kumuambia yeye, wala Mtume.<sup>4</sup> Maneno sawa na hayo yalisemwa na As-Suddi na wengine.<sup>5</sup>

فَلَمَّا أَن جَاءَ الْبَشِيرُ أَلْقَاهُ عَلَىٰ وَجْهِهِ فَارْتَدَّ بَصِيرًا ۗ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَّكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٩٦﴾ قَالُوا يَا أَبَانَا اسْتَغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ﴿٩٧﴾ قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي ۗ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٩٨﴾

**96. Basi alipofika mbashiri na akaiweka kanzu usoni pake alirejea kuona. Akasema: Je! Sikukuambieni kuwa mimi najua ya Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi?**

**97. Wakasema: Ee baba yetu! Tuombe msamaha kwa dhambi zetu. Hapana shaka sisi tulikuwa na makosa.**

**98. Akasema: Nitakuja kuombeeni msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Maghufira na Mwenye Kusamehe.**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:253

<sup>2</sup> At-Tabari 16:255.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:257.

<sup>4</sup> At-Tabari 16:257.

<sup>5</sup> At-Tabari 16:257.

**Yahudha Analeta Kanzu ya Yusuf عليه السلام na Habari Njema**

Ibn Abbas na Ad-Dhahhak رضي الله عنهما wamesema

الْبَشِيرُ

"...mbashiri..." Mjumbe, Mujahid na As-Suddi wamesema, Yahudha bin Yaakub ndiye aliyekuwa na habari njema.<sup>1</sup> As-Suddi aliongeza, "Aliileta (kanzu ya Yusuf عليه السلام) kwa sababu yeye ndiye aliyeyleta kanzu ya Yusuf عليه السلام iliyokuwa na damu, hivyo alitaka kufuta kosa kwa kitendo chema cha kuleta kanzu ya Yusuf عليه السلام na kuiweka usoni mwa baba yake. Macho ya baba yake yakarudia kuona."<sup>2</sup> Ya'kubu عليه السلام akawaambia wanaye,

قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ إِنِّي أَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٩٦﴾

**"Je! Sikukuambieni kuwa mimi najua ya Mwenyezi Mungu msiyo yajua nyinyi?" (12:96)**

Kuwa Allah تعالى Atamrudisha Yusuf عليه السلام kwangu, na kwamba,

لَأَجِدُ رِيحَ يُوسُفَ لَوْلَا أَن تَفَنِّدُونَ

**"...Hakika mimi nasikia harufu ya Yusuf, lau kuwa hamtanituhumu."**

**Nduguze Yusuf عليه السلام Wanasikitika na Kujuta**

Hayo ni pale nduguze Yusuf عليه السلام walipomuambia kwa unyenyekevu,

قَالُوا يَا أَبَانَا اسْتَغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا إِنَّا كُنَّا خَاطِئِينَ ﴿٩٧﴾ قَالَ سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي

إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٩٨﴾

**"Ee baba yetu! Tuombee msamaha kwa dhambi zetu. Hapana shaka sisi tulikuwa na makosa. Akasema: Nitakuja kuombeeni msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Maghufira na Mwenye Kusamehe." (12:97-98)**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:258.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:259.

Kwa maana: mwenye kutaka toba Kwake Humsamehe yeye. 'Abdullah bin Masud, Ibrahim At-Taymi, Amri Bin Qays, Ibn Jurayj na wengine wamesema: aliwachelewesha mpaka usiku wa manane.<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 16:262

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَى يُوسُفَ ءَاوَىٰ إِلَيْهِ أَبَوَيْهِ وَقَالَ ادْخُلُوا  
 مِصْرَ إِن شَاءَ اللَّهُ ءَامِنِينَ ﴿٩٩﴾ وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ  
 وَخَرُّوا لَهُ سُجَّدًا ۗ وَقَالَ يَا أَبَتِ هَذَا تَأْوِيلُ رُؤْيَايَ مِن  
 قَبْلُ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّي حَقًّا ۗ وَقَدْ أَحْسَنَ بِي إِذْ أَخْرَجَنِي مِنَ  
 السِّجْنِ وَجَاءَ بِكُم مِّنَ الْبَدْوِ مِن بَعْدِ ۚ أَن نُّزِعَ الشَّيْطَانُ  
 مِنِّي وَيَنبَغِ إِحْوَىٰ ۗ إِنَّ رَبِّي لَطِيفٌ لِّمَا يَشَاءُ ۗ إِنَّهُ هُوَ  
 الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾ \* رَبِّ قَدْ ءَاتَيْتَنِي مِنَ الْمَلِكِ  
 وَعَلَّمَنِي مِمَّا تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ ۗ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ  
 أَنْتَ وَلِيِّّ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ تَتَوَفَّيْ مُسْلِمًا وَآلِحِقِنِي  
 بِالصَّلَاحِينَ ﴿١٠١﴾ ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۗ وَمَا  
 كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ أَتَوْا أَمْرَهُمْ وَهُمْ مَحْكُورُونَ ﴿١٠٢﴾ وَمَا  
 أَكْثَرَ النَّاسَ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾ وَمَا تَسْأَلُهُمْ  
 عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۗ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾

فَلَمَّا دَخَلُوا عَلَى يُوسُفَ ءَاوَىٰ إِلَيْهِ  
 أَبَوَيْهِ وَقَالَ ادْخُلُوا مِصْرَ إِن شَاءَ  
 اللَّهُ ءَامِنِينَ ﴿٩٩﴾ وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى  
 الْعَرْشِ وَخَرُّوا لَهُ سُجَّدًا ۗ وَقَالَ  
 يَا أَبَتِ هَذَا تَأْوِيلُ رُؤْيَايَ مِن قَبْلُ  
 قَدْ جَعَلَهَا رَبِّي حَقًّا ۗ وَقَدْ أَحْسَنَ  
 بِي إِذْ أَخْرَجَنِي مِنَ السِّجْنِ وَجَاءَ  
 بِكُم مِّنَ الْبَدْوِ مِن بَعْدِ ۚ أَن نُّزِعَ  
 الشَّيْطَانُ مِنِّي وَيَنبَغِ إِحْوَىٰ ۗ إِنَّ  
 رَبِّي لَطِيفٌ لِّمَا يَشَاءُ ۗ إِنَّهُ هُوَ  
 الْعَلِيمُ الْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾

99. Na walipoingia kwa Yusuf aliwakumbatia wazazi wake na akasema: Ingieni Misri, Inshallah, mmo katika amani.

100. Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi. Na wote wakaporomoka kumsujudia. Na akasema: Ewe baba yangu! Hii ndiyo tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani. Na Mwenyezi Mungu Ameijaalia iwe kweli. Na Mwenyezi Mungu Amenifanyia wema kunitoa gerezani, na kukuleteni kutoka jangwani baada ya Shet'ani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mpole kwa Alitakalo. Bila ya shaka Yeye ni Mjuzi Mwenye Hikima.

**Yusuf عليه السلام Anawakaribisha Wazazi Wake, Ndoto Yake Inatimia**

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yaakub عليه السلام alikwenda kwa Yusuf عليه السلام nchini Misri. Yusuf عليه السلام aliwaomba nduguze wailete familia yao yote, na wote wakaondoka kwao, wakaiacha Kanaan, wakaenda Misri. Yusuf عليه السلام alipopewa khabari za kukaribia kwao, alienda kuwalaki, Mfalme aliwaagiza wana wa mfalme na waheshimiwa waongozane na Yusuf عليه السلام, ili kumlaki Yaakub عليه السلام. Yusuf عليه السلام aliambia familia yake baada ya kuingia kwake na kuwachukua yeye mwenyewe.

وَقَالَ آدْخُلُوا مِصْرَ إِن شَاءَ اللَّهُ ءَامِنِينَ

**“...na akasema: Ingieni Misri, Inshallah, mmo katika amani.”**

Maana: Aliwaambia, ‘Ingieni Misri’, yaani, ‘Muishi Misri’, na akaongeza, ‘Allah تعالى Akipenda, kwa usalama’ kulinganisha na taabu na njaa iliyowataabisha.

Allah تعالى Akasema,

ءَاوَىٰ إِلَيْهِ أَبْوَيْهِ

**“...aliwakumbatia wazazi wake.”**

As-Suddi na Abdur-Rahman bin Zaid Bin Aslam wamesema kuwa wazazi wake walikuwa baba yake na shangazi yake,<sup>1</sup> kwani mama yake alishafariki zamani.<sup>2</sup> Muhammad Bin Is’haq رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى wamesema baba yake na mama yake walikuwa hai. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema kuwa hakukuwa na ushahidi kuwa mama yake alishafariki kabla ya hapo, bali Qur’an inashuhudia kuwa alikuwa hai. Rai hii ina maana dhahiri na inayofaa ambayo kisa hiki kinaithibitisha.<sup>3</sup> Allah تعالى Akasema,

وَرَفَعَ أَبْوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ

**“Na akawapandisha wazazi wake kwenye kiti cha enzi.”**

Aliwakalisha kitandani alipokuwa amekaa, kwa mujibu wa Ibn Abbas, Mujahid رضي الله عنهما.<sup>4</sup> Allah تعالى Amesema,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:267.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:269.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:267.

<sup>4</sup> Kama hapo juu.

وَحَرُّوا لَهُ سُجَّدًا<sup>ط</sup>

**“Na wote wakaporomoka kumsujudia.”** Wazazi wake na nduguze walimsujudia, nao walikuwa kumi na mmoja.

وَقَالَ يَتَأْتِبِ هَذَا تَأْوِيلُ رُءْيَايَ مِنْ قَبْلُ

**“Na akasema: Ewe baba yangu! Hii ndiyo tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani.”**

Kwa maana, aliyomsimulia baba yake huko nyuma,

إِنِّي رَأَيْتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوْكَبًا

**“Hakika mimi nimeota nyota kumi na moja...”**

Katika sheria za Mitume hawa na waliotangulia, watu waliruhusiwa kuwasujudia wenye mamlaka wanapokutana nao. Sheria hii iliruhusiwa kwa Adam mpaka ‘Isa (Rehema na amani za Allah تعالى ziweifikie wote), lakini baadaye ilikatazwa kisheria. Uislamu umefanya kuwa wa kusujudiwa ni Allah تعالى Peke Yake. Ishara ya kauli hiyo ilikusanywa na Qatadah na wanazuoni wengine.<sup>1</sup> Muadh رضي الله عنه alipokwenda Sham,<sup>2</sup> akawakuta watu wanawasujudia Maaskofu wao. Aliporejea (Al-Madinah) alimsujudia Mtume ﷺ, naye akamuuliza,

«مَا هَذَا يَا مُعَاذُ؟»

**“Hiki ni nini, ewe Muadhi?”**

Akajibu, “Nimewaona wanawasujudia maaskofu wao na wewe una haki zaidi ya kusujudiwa, ewe Mtume ﷺ.” Akasema:

«لَوْ كُنْتُ أَمِيرًا أَحَدًا أَنْ يَسْجُدَ لِأَحَدٍ، لَأَمَرْتُ الْمَرْأَةَ أَنْ تَسْجُدَ لِزَوْجِهَا لِعِظَمِ حَقِّهِ عَلَيْهَا»

**“Lau ningekuwa mwenye kumuamrisha yeyote kumsujudia mwingine ningemuamrisha mwanamke kumsujudia mumewe kutokana na ukubwa wa haki yake juu yake.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:269.

<sup>2</sup> Shamu ya Kale, ambayo kwa sasa ni Syria, Lebanon, Palestina na Jordan.

<sup>3</sup> Ibn Majah 1:595.



Kwa hivyo, hilo liliruhusiwa katika sheria zilizopita, kama tulivyosema. Hiyo ndiyo sababu wao (Yaakub عليه السلام, mkewe na wanaye) walimsujudia Yusuf عليه السلام, ambaye wakati huohuo alisema,

يَتَأْتِبَ هَذَا تَأْوِيلُ رُؤْيَايَ مِنْ قَبْلُ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّي حَقًّا<sup>ط</sup>

***“Ewe baba yangu! Hii ndiyo tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani. Na Mwenyezi Mungu Ameijaalia iwe kweli.”***

Kutumia neno *Ta’wil’*, kueleza mambo yalivyoishia, baadaye Allah تعالى Alisema katika Aya nyingine:

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ<sup>ع</sup> يَوْمَ يَأْتِي تَأْوِيلَهُ<sup>ط</sup>

***“Je, lipo wanalolingojea isipokuwa matokeo yake? Siku yatapo fika matokeo yake...” (7:53)***

Maana yake: Katika Siku ya Kiama, itakuja heri au shari waliyoahidiwa. Yusuf عليه السلام amesema,

قَدْ جَعَلَهَا رَبِّي حَقًّا<sup>ط</sup>

***“Na Mwenyezi Mungu Ameijaalia iwe kweli.”***

Kwa kutaja kuwa Allah تعالى Amembariki kwa kumtimizia ndoto yake,

وَقَدْ أَحْسَنَ بِي إِذْ أَخْرَجَنِي مِنَ السِّجْنِ وَجَاءَ بِكُمْ مِنَ الْبَدْوِ

***“Na Mwenyezi Mungu Amenifanyia wema kunitoa gerezani, na kukuleteni kutoka jangwani,...”***

Ambapo waliishi maisha ya kibedui na walifuga mifugo, kwa mujibu wa Ibn Jurayj na wengine.<sup>1</sup> Alisema kuwa walikuwa wakiishi mahali palipoitwa Arava, Ghur katika ardhi ya Palestina huko Sham. Yusuf عليه السلام akasema,

مِنْ بَعْدِ أَنْ تَرَعَ الشَّيْطَانُ بَيْنِي وَبَيْنَ إِخْوَتِي<sup>ع</sup> إِنَّ رَبِّي لَطِيفٌ لِمَا يَشَاءُ<sup>ع</sup>

***“...baada ya Shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mpole kwa Alitakalo.”***

<sup>1</sup> At-Tabari 16:276.

Kwani Allah تعالى Anapotaka jambo, Hutanguliza visababishi vyake, kisha Analifanya litokee na kurahisisha kutokea.

إِنَّهُ هُوَ الْعَلِيمُ

**"Bila ya shaka Yeye ni Mjuzi."**

Wa maslahi ya waja wake,

الْحَكِيمُ

**"Mwenye Hikima."**

Katika Kauli, Matendo, Hukumu, Kudura Zake na Analolichagua na Kulitaka.

رَبِّ قَدْ ءَاتَيْتَنِي مِنَ الْمَلِكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ ۚ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ  
أَنْتَ وَلِيٌّ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۖ تُوَفِّي مُسْلِمًا وَالْحَقِيقِي بِالصَّالِحِينَ ﴿١٠١﴾

**101. Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika Umenipa utawala, na Umenifunza tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe Ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema**

**Yusuf عليه السلام Anamuomba Allah تعالى Amfishe Hali ya Kuwa Muislamu**

Hii ni dua ya Yusuf عليه السلام Mkweli, kwa Mola Wake Mlezi, baada ya Allah تعالى Kumneemesha kwa Kumuunganisha tena na wazazi na nduguze, baada ya kupewa utume na ufalme. Alimuomba Mola wake Mlezi kwamba kama Alivyoitimiza neema yake duniani aendelee nayo huko akhera. Alimuomba amfishe hali ya kuwa ni Muislamu, kama alivyoosema Adh-Dhahhak, na kumuunganisha na watu wa daraja la wema, nao ni Manabii na Mitume, Rehema za Allah تعالى na Amani yake ziwafikie.<sup>1</sup> Inawezekana kwamba Yusuf عليه السلام aliomba dua hii wakati wa kufariki kama ilivyo katika Sahihi Mbili kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba Mtume ﷺ alikuwa ananyanyua kidole chake wakati wa kufariki huku anasema:

اللَّهُمَّ فِي الرَّيْبِ الْأَعْلَى، ثَلَاثًا

**"Ee Mola wangu wa haki Nipe ithibati katika hali ya umauti, kwa Rafiki Aliye Juu."**<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Fat'hul Bari 7:743

Pia inawezekana ilikuwa muda mrefu kabla ya wakati wa kufariki, aliomba kufa akiwa Muislamu na kuungana na watu wema.

ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۗ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ أَجْمَعُوا أَمْرَهُمْ وَهُمْ يَمْكُرُونَ ﴿١٠٢﴾  
 وَمَا أَكْثَرَ النَّاسَ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾ وَمَا تَسْأَلُهُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ ۗ إِنْ هُوَ إِلَّا  
 ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾

**102. Hizi ni katika khabari za ghaibu Tulizokufunulia. Na hukuwa pamoja nao walipoazimia shauri yao, walipofanya njama zao wakizua vitimbi.**

**103. Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.**

**104. Wala wewe huwaombi ujira kwa haya. Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.**

**Kisa hiki ni Wahyi wa Allah** تعالی

Allah تعالی Anamsimulia Muhammad ﷺ habari za nduguze Yusuf عليه السلام na jinsi Allah تعالی Alivyomnyanyua juu yao na Akamfanyia mwisho mwema, ushindi, mamlaka, hekima (yaani utume), ingawa walitaka kumdhuru na kumuua. Allah تعالی Amesema, 'Kisa hiki na vingine kama hiki ni katika mambo ya ghaibu, ewe Muhammad,

نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۗ

**"...Tulizokufunulia."**

Na Tunakufundisha, ewe Muhammad ﷺ kwa sababu vina mazingatio kwako, na onyo kwa anayekupinga.

Kisha Allah تعالی Akasema,

وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ

**"Na hukuwa pamoja nao."**

Hukuwepo mbele yao na hukuwaona,

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 7:643.

إِذْ أَجْمَعُوا أَمْرَهُمْ

**“...walipoazimia shauri yao.”**

Ili wamtupe Yusuf عليه السلام kisimani,

وَهُمْ مَمْكُرُونَ

**“...wakizua vitimbi.”** Dhidi yake.

Tumekujulisha hayo kwa Wahyi Tuliokuteremshia. Kama alivyosema:

وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يُلْقُونَ أَقْلَامَهُمْ

**“...nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao...” (3:44)** na,

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الْغَرْبِيِّ إِذْ قَضَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ الْأَمْرَ

**“Wala wewe hukuwa upande wa magharibi Tulipompa Musa amri...”** mpaka,

وَمَا كُنْتَ بِجَانِبِ الطُّورِ إِذْ نَادَيْنَا

**“Wala hukuwa kando ya mlima Tuliponadi.” (28:46)**

Na Kauli Yake,

وَمَا كُنْتَ ثَاوِيًا فِي أَهْلِ مَدْيَنَ تَتْلُوا عَلَيْهِمْ ءَايَاتِنَا

**“Wala hukuwa mkaazi na watu wa Madyana ukiwasomea Aya Zetu.” (28:45)**

Allah تعالى Anasema kuwa Muhammad ﷺ ni Mjumbe Wake na kuwa Amemfundisha habari za yaliyopita, zenye mafunzo kwa watu, ili wapate usalama katika mambo yao ya kidini na ya kidunia. Lakini watu wengi hawakuamini na hawataamini.

Kwa hivyo Allah تعالى Akasema,

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٢٧﴾

**“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.”**

Akasema katika Aya hiyohiyo,

وَأِنْ تُطِيعْ أَكْثَرَ مَنْ فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

**“Na ukiwatii wengi katika hawa waliomo duniani watakupoteza na Njia ya Mwenyezi Mungu.” (6:116) Na,**

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُمْ مُؤْمِنِينَ

**“Hakika katika haya zipo Ishara. Lakini wengi wao hawakuwa wenye kuamini.” (26:8)**

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمَا تَسْأَلُهُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ

**“Wala wewe huwaombi ujira kwa haya.”**

Allah تعالى Anasema, ‘Wewe, ewe Muhammad, huwaombi ujira kwa nasaha zako na kuwalingania kwenye heri na uongofu malipo yoyote. Badala yake, unalifanya hilo kwa kutaka radhi za Allah تعالى na kuwanasihi viumbe Wake.”

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ

**“Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.”**

Wanakumbuka, wanaongoka na wanajiokoa kwa Qur’an duniani na akhera.

\* \* \*

وَكَايِن مِّنْ آيَةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَمُرُونَ عَلَيْهَا  
 وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُونَ ﴿١٠٥﴾ وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا  
 وَهُمْ مُشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾ أَفَأَمِنُوا أَنْ تَأْتِيَهُمْ غَشِيَةٌ مِّنْ عَذَابِ  
 اللَّهِ أَوْ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٠٧﴾ قُلْ  
 هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُوا إِلَى اللَّهِ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي  
 وَسُبْحَانَ اللَّهِ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٨﴾ وَمَا أَرْسَلْنَا  
 مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُّوحِي إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ ۗ أَفَلَمْ  
 يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ  
 قَبْلِهِمْ ۗ وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ  
 ﴿١٠٩﴾ حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِّبُوا  
 جَاءَهُمْ نَصْرُنَا فَنُجِّيَ مَنْ نَّشَاءُ ۗ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُنَا عَنِ الْقَوْمِ  
 الْمُجْرِمِينَ ﴿١١٠﴾ لَقَدْ كَانَتْ فِي قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِأُولِي  
 الْأَلْبَابِ ۗ مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَىٰ وَلَكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي  
 بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ كُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ  
 يُؤْمِنُونَ ﴿١١١﴾

وَكَايِن مِّنْ آيَةٍ فِي السَّمَوَاتِ  
 وَالْأَرْضِ يَمُرُونَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا  
 مُعْرِضُونَ ﴿١٠٥﴾ وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ  
 بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾ أَفَأَمِنُوا  
 أَنْ تَأْتِيَهُمْ غَشِيَةٌ مِّنْ عَذَابِ اللَّهِ أَوْ  
 تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً وَهُمْ لَا  
 يَشْعُرُونَ ﴿١٠٧﴾

105. Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia, na hali ya kuwa wanazipuuzwa.

106. Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina.

107. Je! Wanaaminisha kuwa haitowajia adhabu ya Mwenyezi Mungu ya kuwagubika, au haitawafikia Saa ya Kiyama kwa ghafla, na hali hawatambui?

## Watu Wanapuuzwa Kutafakari Ishara Zilizoa Mbele Yao

Allah تعالى Anaeleza kuwa watu wengi hawafikirii ishara zinazothibitisha kuwa Yeye ni Mmoja tu, Muumba mbingu na ardhi, nyota zing'aazo na sayari na viumbe vingine vizungukavyo. Na vyote vimedhalilishwa na Allah تعالى. Kuna sehemu nyingi zilizokaribiana ardhini, zenye rutuba, mashamba, milima migumu, bahari na mawimbi yanayogongana, na majangwa mapana. Kuna

viumbe hai wengi na wasio hai, milima, mimea na matunda yanayofanana maumbo, lakini hutofautiana kwa ladha, harufu, rangi na sifa. Hivyo, kutakasika dhidi ya upungufu ni kwa Allah تعالی Mmoja, Wa Pekee, Aliyeumba viumbe vyote, wa Pekee kwa kudumu, na Mkusudiwa kwa Majina na Sifa. Kauli Yake:

﴿ وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ﴾

**“Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina.”**

Ibn Abbas رضي الله عنهما ametoa rai, “Wana imani ndogo, kwani wanapoulizwa, ‘Nani kaumba ardhi? Ni nani kaumba milima?’ Wanajibu, ‘Ni Allah تعالی’ wanasema hayo huku wanamshirikisha Allah تعالی.”<sup>1</sup> Rai sawa na hiyo ilisemwa na Mujahid, Ataa, Ikrimah As-Sha’bi, Qatada, Adh-Dhahhak na ‘Abdur-Rahman bin Zaid bin Aslam.<sup>2</sup> Katika *Sahih* kumeandikwa kuwa washirikina walikuwa wanasema katika *Talbiyah* yao, ‘Tunakuitikia hali ya kuwa huna mshirika isipokuwa mshirika yule unayemiliki lakini yeye hamiliki.”<sup>3</sup> Allah تعالی Amesema katika Aya nyingine,

﴿ إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴾

**“Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa.” (31:13)**

Hiyo ndiyo Shiriki kubwa sana, kumshirikisha Allah تعالی katika ibada. Imeanikwa katika Sahihi Mbili kuwa ‘Abdallah bin Mas’uud رضي الله عنه alisema, ‘Ewe Mtume! Ni dhambi gani kubwa zaidi?’ Akasema:

﴿ أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً وَهُوَ خَلَقَكَ ﴾

**“Ni unapomuekea Allah mshindani, na hali ya kuwa Yeye Ndiye Aliyekuumba.”<sup>4</sup>**

Al-Hassan Basri رحمه الله تعالی ametoa rai kuhusu Kauli Yake,

<sup>1</sup> Tabari 16:292.

<sup>2</sup> Kama hapo juu.

<sup>3</sup> Muslim 2:843.

<sup>4</sup> *Fat’hul Al-Bari* 8:350, Muslim 1:90.

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾

**“Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina.”**

Huyo ni mnaifiki, akifanya mema ni kwa kuwaonesha watu na yeye anaabudu sanamu huku akifanya hayo. Al-Hassan alikuwa akirejea katika Kauli ya Allah

تعالى:

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كَسَالَى يُرَاءُونَ  
النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٠٧﴾

**“Hakika wanaafiki wanamkhadaa Mwenyezi Mungu, na hali ni Yeye Ndiye Mwenye Kuwakhadaa wao. Na wanapoinuka kusali huinuka kwa unyong’onyo, wanajionesha kwa watu tu, wala hawamd hukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.” (4:142)**

Na kuna Shirki nyingine iliyojificha ambayo wengi hawajui, kama alivyopokea Hammad bin Salamah amesimulia kuwa `Asim bin Abi Najud alisema kuwa Urwa alisema kuwa Hudhaifa رضي الله عنه alimzuru mgonjwa na akaona kamba imefungwa mkononi mwake, akaitoa huku akisoma,

وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ﴿١٠٦﴾

**“Na wengi katika wao hawamuamini Allah pasi na kuwa ni washirikina.”**

Hadithi kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما iliyoandikwa na At-Tirmidhi ambaye alisema ni Hasan, Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ حَلَفَ بِغَيْرِ اللَّهِ فَقَدْ أَشْرَكَ»

**“Mwenye kuapa kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu kwa hakika ameshirikisha.”<sup>1</sup>**

Imamu Ahmad na Abu Dawud, na wengine wamesimulia kutoka kwa Ibn Mas‘uud رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

<sup>1</sup> Tuhfat Al-Ahwadhi 5:135



«إِنَّ الرُّقْمَ وَالشَّمَانِمَ وَالنُّزْلَةَ شِرْكٌ»

"Hakika kinga na hirizi na kinga za uchawi vyote hivyo ni shirki."<sup>1</sup>

Na riwaya nyingine iliyoandikwa na Ahmad na Abu Dawud Mtume ﷺ amesema,

«الطَّيْرَةُ شِرْكٌ وَمَا مِثْلُهَا، وَلَكِنَّ اللَّهَ يُذْهِبُهُ بِالتَّوَكُّلِ»

"Kuhisi Mkosi ni shirki na hakuna yoyote katika sisi isipokuwa anao lakini Allah Anaundoa kwa kutawakali."<sup>2,3</sup>

Kauli Yake,

أَفَأَمِينُوا أَنْ تَأْتِيَهُمْ غَشِيَةٌ مِّنْ عَذَابِ اللَّهِ

**"Je! Wanaaminisha kuwa haitowajia adhabu ya Mwenyezi Mungu ya kuwagubika,"**

Hivi wamejiaminisha hawa washirikina kwa Allah تعالى kuwajia wao jambo litakalowafunika kutoka mahali wasipopajua, kama Alivyosema Allah تعالى:

أَفَأَمِينُ الَّذِينَ مَكَرُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ يَخْسِفَ اللَّهُ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٠٥﴾ أَوْ يَأْخُذَهُمْ فِي تَقْلُبِهِمْ فَمَا هُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿١٠٦﴾ أَوْ يَأْخُذَهُمْ عَلَى تَخَوُّفٍ فَإِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠٧﴾

**"Je! Wameaminisha wanaofanya vitimbi vya uovu kwamba Mwenyezi Mungu Hatawadidimiza katika ardhi, na haitawafika adhabu kutoka wasipopajua? Au Hatawashika katika nyendo zao, na wala hawataponyoka? Au Hatawashika kwa kitisho na Kuwapunguza kidogo kidogo? Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye Huruma, Mwenye Kurehemu."** (Suratu Nnahi:45-47) Na,

أَفَأَمِينُ أَهْلِ الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا بَيْنَمَا وَهُمْ نَائِمُونَ ﴿١٠٨﴾ وَأَمِينُ أَهْلِ الْقُرَىٰ أَنْ يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا ضُحًى وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿١٠٩﴾ أَفَأَمِينُوا مَكَرَ اللَّهِ؟ فَلَا يَأْمَنُ مَكَرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١١٠﴾

<sup>1</sup> Ahmad 1:381, Abu Dawud 4:212, Ibn Majah 2:1167. *Ar-Ruqya* ni kusoma dua kwa kutumia Qu'an. *At-Tamaim* ni Kitendo cha kuweka hirizi shingoni mwa watoto kwa kutaka kuwakinga dhidi ya kijicho. *At-Tiwalah* ni namna ya uchawi unaofanywa na wale wanaodai kuwa wanaweza kumfanya mwanamke azidi kupendwa na mumewe na kinyume chake.

<sup>2</sup> Kumtegemea na kumtumaini Yeye.

<sup>3</sup> Ahmad 1:389, Abu Dawud 4:230

***“Je, watu wa mijini wameaminisha ya kuwa adhabu Yetu haitawafika usiku, nao wamelala? Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa adhabu Yetu haitawafika mchana, nao wanacheza? Je, wamejiaminisha na Mipango ya Mwenyezi Mungu? Kwani hawajiaminishi na Mipango ya Mwenyezi Mungu ila watu wenye kukhasiri.”***

قُلْ هٰذِهِ سَبِيْلِيْ اَدْعُوْا اِلٰى اَللّٰهِ عَلٰى بَصِيْرَةٍ اَنَا وَمَنْ اَتَّبَعَنِ ۗ وَسُبْحٰنَ اَللّٰهِ وَمَا اَنَا مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ ﴿١٠٨﴾

**108. Sema: Hii ndiyo Njia yangu - ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa kujua - mimi na wanaonifuata. Na Ametakasika Mwenyezi Mungu! Wala mimi si katika washirikina.**

### **Njia ya Mtume ﷺ**

Allah تعالى Anamuagiza Mjumbe wake ﷺ awaambie wanadamu na majini kwamba hii ni njia Yake. Kwa maana: Njia, mfumo, njia na Sunnah yake, kwa kudumu katika kulingania kwenye shahada kwamba hapana anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى Peke Yake, Asiye na mshirika. Mtume ﷺ analingania kwenye shahada hii kwa uhakika kabisa na ushahidi imara. Anawalingania kwenye njia hii, na wafuasi wake wanalingania kwenye alilolingania Mtume ﷺ kwa uhakika na ushahidi, ima wa kiakili au wa kidini.

وَسُبْحٰنَ اَللّٰهِ

***“Na Ametakasika Mwenyezi Mungu!”***

Sehemu hii inamaanisha, ninamtakasa Allah تعالى, ninamtukuza na kuwa Yeye hana mshirika au mwenye kufanana Naye au mwenye kulingana Naye au mtoto au mzazi au mke au msaidizi au mshauri.

Kila Sifa njema na Utukufu ni wa Allah تعالى, na Ametakasika dhidi ya yote wanayomnasibisha nayo.

تَسْبِيْحٌ لِّهٖ السَّمٰوٰتِ السَّبْعُ وَالْاَرْضُ وَمَنْ فِيْهِنَّ ۗ وَاِنْ مِنْ شَيْءٍ اِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهٖ ۗ وَلٰكِنْ لَا تَفْقَهُوْنَ تَسْبِيْحَهُمْ ۗ اِنَّهٗ كَانَ حَلِيْمًا غَفُوْرًا ﴿١٠٩﴾

***“Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Maghfira.” (17:44)***

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ ۗ أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ  
فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا ۗ أَفَلَا  
تَعْقِلُونَ ﴿١١١﴾

**109. Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipokuwa wanaume Tuliowafunulia wahyi miongoni mwa watu wa mijini. Je! Hawatembei katika ardhi wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao? Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wamchao Mungu. Basi hamfahamu?**

### Mitume Wote ni Wanadamu Wanaume

Allah تعالی, Anaeleza kuwa aliwatuma Mitume wake wanamume tu, si wanawake. Kama Aya hii inavyoeleza waziwazi, kwamba Allah تعالی Hakumpa mwanamke yeyote katika mabinti wa Adam, wahyi wa kidini na sheria. Hii ni imani ya *Ahlu-Sunnah wal-Jama'ah*. Sheikh Abu Al-Hassan Ali bin Ismail Ash'ari رحمه الله تعالی alisema kuwa rai ya *Ahlu-Sunnah wal-Jama'ah* ni kwamba hakuna Mtume ﷺ katika wanawake. Allah تعالی Anataja kuwa mwanamke mtukufu zaidi ni Maryam bint I'mran, Aliposema:

مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ كَأَنَّا  
يَأْكُلَانِ الطَّعَامَ ۗ

***“Masih mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume. Wamekwisha pita Mitume kabla yake. Na mama yake ni mwanamke mkweli. Wote wawili walikuwa wakila chakula.” (5:75)***

Hizo ndio sifa bora alizopewa na Allah تعالی, angekuwa Mtume, Allah تعالی Angetaja hilo pindi Alipoeleza sifa na heshima na utukufu wake. Kwa hiyo yeye ni muumini mkweli kwa mujibu wa Qur'an.

### Mitume Walikuwa Wanadamu, Si Malaika

Adh-Dhahhak ameeleza kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رَجَالًا

**“Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipokuwa wanaume...”**

Hawakuwa katika watu wa mbinguni (malaika) kama mlivyodai.<sup>1</sup> Kauli hii ya Ibn Abbas رضي الله عنهما inapata nguvu kutokana na Kauli Yake:

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ<sup>١</sup>

**“Na hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakenda masokoni.”**  
(25:20)

وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوا خَالِدِينَ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ صَدَقْنَاهُمُ الْوَعْدَ فَأَنْجَيْنَاهُمْ<sup>٢</sup> وَمَنْ نَشَاءُ وَأَهْلَكْنَا الْمُسْرِفِينَ ﴿٢١﴾

**“Wala Hatukuwafanya miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele. Kisha Tukawatimizia miadi, na Tukawaokoa wao na Tuliowataka, na Tukawateketeza walio pita mipaka.”**(21:8-90) Na,

قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَاٍ مِنَ الرُّسُلِ

**“Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume.”** (46:9)

Halafu Allah تعالى Akasema,

مِّنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ<sup>٣</sup>

**“...miongoni mwa watu wa mijini.”**

Kwa maana: Watu wa mijini, si kwamba walikuwa ni watu wa mashambani (mabedui) ambao ni watu makatili na wasiokuwa na murua mzuri.

<sup>1</sup> Ad-Dur Al-Manthur 5:595.

**Kujifunza Kutokana na Matukio Yaliyotangulia**

Kauli ya Allah تعالى،

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ

**“Je! Hawatembei katika ardhi.”**

Anakusudia hawa wenye kukukadhibisha wewe ewe Muhammad! katika ardhi

فَيَنْظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَنقَبَةُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

**“Wakaona jinsi ulivyokuwa mwisho wa waliokuwa kabla yao?”**

Kwa maana: Katika umati uliowakadhibisha Mitume wao, namna Allah تعالى Alivyowaangamiza, wao na makafiri mfano wao, kama Kusema Kwake:

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَتَكُونُ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا

**“Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia...” (22:46)**

Watakaposikiliza habari za watu hao wataona kuwa Allah تعالى Amewaangamiza makafiri Akawaokoa waumini, na huu ndio ulikuwa utaratibu wa Allah تعالى kwa viumbe Wake, na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

وَلَدَارُ الْآخِرَةِ خَيْرٌ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا

**“Na hakika nyumba ya Akhera ni bora kwa wamchao Mungu.”**

Kwa maana, kama Tulivyo waokoa waumini duniani, kama hivyo Tumewaandikia kuokoka huko Akhera, na akhera ni bora kuliko dunia. Ni kama katika Aya nyingine,

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾ يَوْمَ لَا

يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ ۗ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٥٢﴾

**“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku watapo simama Mashahidi, Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makaazi mabaya kabisa.” (40:51-51)**

Ameinasibisha nyumba na akhera, akasema: 'Na hakika nyumba ya Akhera', kama inavyosemwa: Swala ya kwanza, na msikiti wa Ijumaa, na mwaka wa kwanza, na, mwanzo wa usiku wa jana, na siku ya Alkhamisi.

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ وَطُنُّوْا أَهْمَ قَدْ كُذِّبُوا جَاءَهُمْ نَصْرُنَا فَنُجِّيَ مَنْ نَشَاءُ ۗ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُنَا عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١١٠﴾

**110. Hata Mitume walipokata tamaa na wakaona kuwa wamekadhibishwa, hapo ikawajia Nusura Yetu, wakaokolewa tuwatakao. Na Adhabu Yetu haitowawacha kaumu ya wakosefu.**

**Mitume wa Allah تعالى Walinusuriwa katika Nyakati za Dhiki Sana**

Allah تعالى Anataja kwamba Nusura Yake Hushuka juu ya Mitume Wake (Rehema za Allah تعالى na Amani Yake ziwe juu yao wote) kipindi chenye dhiki mno na kutaraji msaada wa Allah تعالى. Kama ilivyo Kauli Yake nyingine,

وَزُلْزِلُوا حَتَّىٰ يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ مَتَىٰ نَصْرُ اللَّهِ ۗ

**"...na wakatikiswa hata Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Lini nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja?" (2:214)**

Ama kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

كُذِّبُوا

**"Wamekadhibishwa."**

Kuna visomo viwili, kimoja kwa *shadda* (wamewasaliti). Hivyo ndivyo alivyokuwa akisoma Aishah رضي الله عنها. Al-Bukhari amesema kuwa Urwa Bin Zubair alisimulia kuwa alimuuliza 'Aishah رضي الله عنها kuhusu maana ya Aya ifuatayo,

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ

**"Hata Mitume walipokata tamaa...,"**

Je, ni kudanganywa au kusalitiwa?" 'Aishah رضي الله عنها akajibu, "walisalitiwa." 'Urwah akasema: 'Nikasema, 'Walikuwa na hakika kuwa wafuasi wao waliwasaliti basi kwanini limetumika neno 'dhana (*dhwannu*)?' Akajibu, 'Ndiyo, walikuwa na hakika kuwa waliwasaliti.' Nikasoma,

وَوَظَّنُوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِّبُوا

**“...na wakaona kuwa wamekadhibishwa...”**

Akasema: ‘Najikinga kwa Allah تعالى, Mitume hawakuwa na shaka kwa Mola wao Mlezi juu ya hilo.’ Nikasema: ‘Kwa hiyo Aya hii inamaanisha nini?’ Akajibu, ‘Inawahusu wafuasi wa Mitume waliomuamini Mola wao Mlezi na wakasadikisha Mitume wao, muda wa mtihani wao ukawa mrefu na nusura ya Allah تعالى ikachelewa, (Mpaka Mitume wakakata tamaa) kwa waliowapinga wao katika kaumu zao, na wakawa na mashaka, hata wafuasi wao nao wamewapinga, ikawajia wao nusura ya Allah تعالى. Urwa akasema: Nikamuambia Aisha رضي الله عنها: ‘huwenda (wamedanganywa Mitume)?’ Kwa kisomo cha (*Qad Kudhibuu*).“ Aisha رضي الله عنها akasema, ‘Najilinda kwa Allah تعالى na dhana hiyo.’ Ibn Jurayj amesimulia kuwa Ibn Abi Mulaikah alisema, “Ibn Abbas رضي الله عنهما ameisoma aya hiyo”,

وَوَظَّنُوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِّبُوا

**“...na wakaona kuwa wamekadhibishwa,”** Abdullah Ibn Abi Mulaikah akasema: Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما aliniambia, walikuwa ni binadamu, kisha akasoma:

حَتَّى يَقُولَ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ مَتَى نَصْرُ اللَّهِ ۗ أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ ﴿٢١٤﴾

**“...Mpaka Mtume na walioamini pamoja naye wakasema: Lini Nusura ya Mwenyezi Mungu itakuja?” (2:214)**

Ibn Jurayj amesema, ‘na Ibn Abi Mulaikah aliniambia, Urwa amenieleza kutoka kwa Aisha رضي الله عنها, kwamba alitofautiana naye katika hilo, na alilikataa na kusema Allah تعالى Hakumuahidi Muhammad ﷺ, jambo lolote isipokuwa anakuwa amekwisha kujua kwamba jambo hilo litakuwa mpaka alipokufa. Isipokuwa ni kwamba balaa halikuacha kuwa kwa Mitume mpaka wakadhani kwamba wale walio pamoja nao katika waumini wamewakadhibisha. Ibn Abi Mulaikah amesema katika Hadithi ya Urwa, Aishah رضي الله عنها alikuwa akisoma aya hiyo kama hivi,

(وَوَظَّنُوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِّبُوا)

(Na wakadhani kuwa wamesalitiwa.)<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Tabari 16:307

Na aina ya pili ya usomaji ni ule usiokuwa na *Shadda*, na kuna rai tofauti kuhusu maana yake. Tumeeleza maana aliyotoa Ibn Abbas رضي الله عنهما. Ibn Mas'ud رضي الله عنهما amesema, alivyosimulia Sufyan Ath-Thauri رحمه الله تعالى kutoka kwake, kuwa aliisoma Aya hivi,

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ وَطُنُّوْا أَهْمَمَ قَدْ كُذِبُوا

***“Hata Mitume walipokata tamaa na wakaona kuwa wamekadhibishwa...”***

Abdullah ametoa rai juu ya hilo kuwa huu ndio usomaji unaochukiza. Ibn Abbas رضي الله عنهما pia alitoa rai juu ya Aya:

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ وَطُنُّوْا أَهْمَمَ قَدْ كُذِبُوا

***“Hata Mitume walipokata tamaa na wakaona kuwa wamekadhibishwa...”***

Amesema: walipokata tamaa Mitume kujibiwa na watu wao. Na watu hao wakadhani kwamba Mitume wamewadanganya, nusura ili waja juu ya hilo,

فَنَجَّيَ مِنْ كُذْبَاءِ

***“...wakaokolewa Tuwatakao.”***

Ibn Jarir At-Tabari رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Ibrahim bin Abi Hamzah (Hurrah) Al-Jazari, “Kijana wa Kikuraishi alimuuliza Sa'id bin Jubayr, ‘Ewe Abu ‘Abdullah! Unasomaje neno hili, kwani ninapolikuta, ninatamani kuwa nisingeisoma Surah hii,

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ وَطُنُّوْا أَهْمَمَ قَدْ كُذِبُوا

***“Hata Mitume walipokata tamaa na wakaona kuwa wamekadhibishwa...”***

Akasema ‘Ndiyo, mpaka Mitume walipokata tamaa kwa kukubaliwa na watu wao, na wale waliopelekewa Mitume watakapodhani kuwa Mitume hawakuwa wakweli.’ Adh-Dhahhak bin Muzahim amesema, “Sijaona mtu anayedai ana elimu lakini anashindwa kuitikia wito, mpaka leo! Kama ningesafiri mpaka Yemen ili kupata maelezo haya, lingekuwa jambo dogo tu kwa hili.” Ibn Jarir



رحمَهُ اللهُ تَعَالَى amesimulia kwamba Muslim bin Yasaar alimuuliza bin Jubayr kuhusu Aya hiyohiyo na akatoa jibu hilohilo. Muslim alisimama na kumkumbatia Said bin Jubayr رحمه الله تعالى huku akimuambia, "Allah تعالى Akufariji kama ulivyonifariji."<sup>1</sup> Hayo yamesimuliwa kutoka kwa Said bin Jubayr رحمه الله تعالى kupitia isnadi mbalimbali. Hii pia ni *Tafsir* ambayo Mujahid bin Jabir رحمه الله تعالى na wanazuoni wengi wa Salaf waliieleza kuhusu Aya hiyo. Hata hivyo, baadhi ya wanazuoni wamesema kuhusiana na aya hiyo,

وَطَنُوا أَنَّهُمْ قَدْ كُذِّبُوا

**"...na wakaona kuwa wamekadhibishwa."**

inawalenga waumini waliowafuata Mitume, ilhali wengine wamesema kuwa inawalenga makafiri katika umma za Mitume. Kwa maana: 'Na makafiri walidhani kuwa Mitume hawakuwa wakiahidi ahadi ya kweli juu ya ushindi.'" Ibn Jariri رحمه الله تعالى amesimulia kuwa Tamiim bin Hadhlam amesema: "Nilimsikia Abdullah bin Mas'uud رضي الله عنه akitoa rai juu ya Aya hii,

حَتَّىٰ إِذَا اسْتَيْسَسَ الرُّسُلُ

**"Hata Mitume walipo kata tamaa,"**

Ya watu wao kuwaamini, na pale mambo yalipochelewa walidhani kwamba Mitume wao hawakuwa na ahadi ya kweli.<sup>2</sup>

لَقَدْ كَانَتْ فِي قَصَصِهِمْ عِبْرَةٌ لِأُولِي الْأَلْبَابِ ۗ مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَىٰ وَلَٰكِن تَصَدِيقَ

الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ كُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١١١﴾

**111. Kwa hakika katika hadithi zao limo zingatia kwa wenye akili. Si maneno yaliyo zuliwa, bali ni ya kusadikisha yaliyo kabla yake, na ufafanuzi wa kila kitu, na ni uwongofu na rehema kwa kaumu yenye kuamini.**

<sup>1</sup> Tabari 16:304.

<sup>2</sup> Tabari 16:303.

### Zingatia kwa Wenye Akili

Allah تعالى Anaeleza hapa kuwa habari za Mitume na watu wao na namna Tulivyowanusuwa waumini na kuwaangamiza makafiri ni,

عِبْرَةٌ لِأُولَى الْأَلْبَابِ

**“...zingatio kwa wenye akili.”** Akili salama.

مَا كَانَ حَدِيثًا يُفْتَرَىٰ

**“Si maneno yaliyozuliwa.”**

Allah تعالى Anasema haya kuwa hii Qur'an haiwezi kuwa imezushwa, bali kwa hakika imetoka kwa Allah تعالى,

وَلَكِن تَصَدِّيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ

**“...bali ni ya kusadikisha yaliyo kabla yake,...”**

inakusudia vitabu vilivyotangulia kuteremshwa, ambavyo Qur'an inasadikisha yaliyo sahihi na kukanusha yaliyoongezwa, yaliyobadilishwa na yaliyopotoshwa na watu. Qur'an inakubali na kufuta yote Aliyotaka Allah تعالى kuwa hivyo katika Vitabu hivyo,

وَتَفْصِيلَ كُلِّ شَيْءٍ

**“...na ufafanuzi wa kila kitu,”**

Kwa maana: Mambo ya halali, ya haramu, yanayopendekezwa na ya karaha. Qur'an inashughulikia mambo ya kiibada, ya faradhi na Sunna, inakataza haramu na kukemea ya makuruhu. Qur'an inazungumzia mambo makubwa yaliyopo na yajayo kwa ujumla na kwa undani. Qur'an inatueleza kuhusu Mola Mlezi, na kuhusu Majina Yake na Sifa Zake na inatufundisha kuwa Allah تعالى Ametakasika dhidi ya kufanana kwa namna yoyote na viumbe. Kwa hivyo, Qur'an ni,

وَهُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

**“...mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini,...”**

Mwongozo unaongoza nyoyo kutoka katika upotovu na kuzielekeza kwenye uongofu, na kutoka katika kupinda na kuzielekeza kwenye unyoofu, wanatafuta rehema za Mola wao Mlezi wa viumbe humu duniani na siku ya Kurejea.

Tunamuomba Allah تعالی Atujaalie tuwe miongoni mwao duniani na Akhera, siku ambayo waliofuzu watakuwa na nyuso nyeupe zenye kumemetuka, ilhali wenye nyuso nyeusi watapata hasara.

Mwisho wa Surat Yusuf, ni Zake Allah تعالی Sifa Njema na Kuneemesha ni Kwake, na matumaini yetu yote na kutegemea ni Kwake Yeye tu.



## Tafsiri ya Suratu Ar-ra'ad

### Sura ya 13

#### Iliteremshwa Makkah

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

### سُورَةُ الرَّاعِدِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْمَرَّةَ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ ۗ وَالَّذِي أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ  
 الْحَقُّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ اللَّهُ الَّذِي  
 رَفَعَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۗ ثُمَّ أَسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۗ  
 وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۗ كُلٌّ لِحَجْرٍ لِّأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ يُدَبِّرُ  
 الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ ﴿٢﴾  
 وَهُوَ الَّذِي مَدَّ الْأَرْضَ وَجَعَلَ فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنْهَارًا ۗ وَمِنْ كُلِّ  
 الشَّجَرِ جَعَلَ فِيهَا زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ ۗ يُغْشَىٰ اللَّيْلَ أَلْهَابًا ۗ إِنَّ فِي  
 ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٣﴾ وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ  
 مُّتَجَدِّدَاتٌ وَجَنَّاتٌ مِّنْ أَعْنَابٍ وَزُرْعٌ وَنَخِيلٌ صِنَوَانٌ وَغَيْرُ  
 صِنَوَانٍ يُسْقَىٰ بِمَاءٍ وَحِدٍ وَنُفِضِلُ بَعْضَهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي  
 الْأَكْمَالِ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٤﴾ \*  
 وَإِن تَعَجَّبْتَ فَعَجَبٌ قَوْمُهُمْ ءَإِذَا كُنَّا تُرَابًا ءَأِنَّا لِنَافِثٍ خَلْقٍ  
 جَدِيدٍ ۗ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۗ وَأُولَٰئِكَ الْأَغْلَالُ فِي  
 أَعْنَاقِهِمْ ۗ وَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٥﴾

الْمَرَّةَ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ ۗ وَالَّذِي  
 أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ وَلَكِنَّ  
 أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١﴾

1. Alif Lam Mym Ra.  
 (A.L.M.R.) Hizi ni Ishara za  
 Kitabu. Na uliyo teremshiwa  
 kutoka kwa Mola wako  
 Mlezi ni Haki. Lakini wengi  
 wa watu hawaamini.

Qur'ani ni Maneno ya  
 Mwenyezi Mungu عزوجل

Ama maneno juu ya hizi herufi zilizokatwa mwanzoni mwa sura mbalimbali yametangulia mwanzoni mwa Surat Al-Baqarah. Na tumetanguliza kwamba kila Sura iliyoanzwa kwa herufi hizi basi pana ndani yake ushindi wa Qur'ani na kwamba kushuka kwake kutoka kwa Allah تعالى ni haki hapana shaka ndani yake na kwa sababu hiyo Amesema:

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ ۚ

**“Hizi ni aya za kitabu.”** Maana yake: Hizi ni aya za kitabu, nacho ni Qurani kisha Ameungia juu ya hilo uungaji wa sifa. Amesema:

وَالَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكَ

**“Na kile ambacho kimeteremshwa kwako.”**

Maana yake: Ee Muhammad ﷺ.

مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ

**“...kutokana na Bwana wako ni ukweli.”**

Maneno haya ni habari ambayo kimetangulia chenye kutolewa habari nacho ni Kauli Yake.

وَالَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ

**“Na kile ambacho kimeteremshwa kwako.”**

Na Kauli Yake:

، وَلَئِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠﴾

**“Isipokuwa watu wengi hawaamini.”**

Kama vile Kauli Yake:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١١﴾

**“Na wengi wa watu si wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.” (12:103)**

Kwa Maana pamoja na ubainifu huu na uwazi wote huu wengi hawataki kuamini kwa sababu ya uovu, ukaidi na unafiki.

اللَّهُ الَّذِي رَفَعَ السَّمَوَاتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا ۖ ثُمَّ أَسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ۗ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ

لِكُلِّ نَجْمٍ مَجْرَىٰ لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ ﴿١٢﴾

**2. Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona, kisha Akakaa juu ya Kiti cha Enzi (‘Arshi), na Amefanya jua na mwezi vimtii, kila kimoja kinakwenda kwa kiwango maalumu. Anayapanga mambo, na Anazipambanua Ishara ili mpate kuwa na yakini kukutana na Mola wenu Mlezi.**

## Kuweka Wazi Ukamilifu wa Uweza wa Mwenyezi Mungu Mtukufu

Anaeleza Allah تعالى, kuhusu Ukamilifu wa Uwezo Wake na Ukubwa wa Ufalme Wake, kwamba Yeye kwa Idhini Yake na Amri Yake Amezinyanyua mbingu pasi na nguzo, bali isipokuwa kwa Idhini Yake na Amri Yake, na Kudhalilisha Kwake Amezinyanyua Kuziepusha na ardhi umbali ambao hazipatwi na haufikiwi upeo wake. Kwani mbingu iliyo karibu na dunia inaizunguka ardhi yote na vilivyo pembezoni mwake, miongoni mwa maji na hewa, katika pande zake zote na maeneo yake yote, zimenyanyuka juu yake katika kila upande kwa usawa na umbali, uliyo kati ya mbingu na kati ya ardhi, kwa kila upande ni mwendo wa miaka mia tano na hiyo yenyewe kipenyo chake ni mwendo wa miaka mia tano. Kisha mbingu ya pili inaizunguka mbingu ya dunia na vile ambavyo imevikusanya na kati yao katika umbali wa mwendo miaka mia tano, na kina chake yenyewe ni miaka mia tano, kadhalika kama hivyo mbingu ya tatu na ya nne na ya tano na ya sita na ya saba.<sup>1</sup>

Kama Alivyosema Allah تعالى:

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ

***“Mwenyezi Mungu ni Yule Ambaye Ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hizo...”***

Na Kauli Yake:

بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرْوِيهَا

***“...bila ya nguzo mnazoziona...”***

Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas, Mujahid, Al-Hassan, Qatadah na wengine رضي الله عنهم, kwamba wamesema mbingu zina nguzo ila hazionekani.<sup>2</sup>

Na amesema Iyasi bin Muawiya mbingu juu ya ardhi ni mfano wa kuba, anakusadia pasi na nguzo, na kama hivyo pamepokelewa kutoka kwa Qatadah na maelezo hayo ndiyo yanayokubaliana na mtiririko wa maneno. Na uwazi kutokana na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Hii inatokana na riwaya sahihi kutoka kwa Ibn Mas'ud. Angalia *Al-'Ulu (Mukhtasir)* uk. 103. na *Al-Majma'* 1:86. Pia kuna riwaya dhaifu inayonasibishwa katika kauli ya Mtume akizungumzia hayo hayo. Imenukuliwa na At-Tirmidhi 2:525, na wengine pia.

<sup>2</sup> Tabari 16:324.

وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ<sup>ط</sup>

**“Na Amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa Idhini Yake...” (22:65)**

Tukienda juu ya mafundisho ya aya hii<sup>1</sup>, itakuwa Kauli Yake:

تَرَوْنَهَا<sup>ط</sup>

**“Mnayoiona,...”**

Ni kutilia mkazo kuwa hakuna. Maana yake: Hizo mbingu zimenyanyuliwa pasi na nguzo kama mnavyoziona na huu ndiyo ukamilifu sana katika uwezo.

### Kulingana Sawa

Na Kauli Yake:

ثُمَّ أَسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ<sup>ط</sup>

**“...Kisha Amekaa juu ya kiti cha Enzi (‘Arshi)..”**

Imetangulia tafsiri yake katika *Surat Al-Aaraf*, (7:54) na kwa tafsiri yake itapita kama ilivyokuja pasi na kueleza namna yake, wala kufananiza, wala kusema hakuwa juu ya sifa hiyo, wala kutoa mfano. Ametukuka Allah تعالیٰ Kutukuka kukubwa sana.

### Kudhalilishwa kwa Jua na Mwezi na Kwenda Kwao

Na Kauli Yake:

وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلًّا يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَبًّى<sup>ط</sup>

**“Na Amefanya jua na mwezi vimtii, kila kimoja kinakwenda kwa kiwango maalumu.”**

Pamesemwa: Makusudiwa ni kwamba jua na mwezi vinakwenda na vitakaposimama, ndio dalili ya kufika kwa Kiyama. Kama katika Kauli Yake Allah تعالیٰ:

<sup>1</sup> Tabari 16:325.

وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا ۗ

**“Na jua linakwenda kwa kiwango chake...” (36:38)**

Pamesemwa: Makusudiwa mpaka matulizano yao, na matulizano haya ni chini ya Arshi, katika sehemu inayaandamia tumbo la ardhi katika upande mwingine, kwani jua na mwezi na nyota nyingi zitatapofika hapo, zinakuwa mbali sana na Arshi.

Kutokana na kauli Sahihi ambayo zinasimama juu yake dalili, ni kuwa katika sehemu inayouandamia ulimwengu katika upande huu, na haikuwa ni yenye kuanguka kama zilivyo Sayari nyingine kwa sababu ina vishikizo na wapo wachukuzi ambao wanaichukua, na hali hii haipo kwa sayari nyingine za duara, na hili liko wazi kwa mwenye kuyazingatia yale ambayo zimekuja aya na hadithi Sahihi kuyazungumzia.

Na ni za Allah تعالى Peke Yake Sifa Njema na Kuneemesha. Na Amelitaja jua na mwezi kwa sababu hivyo viwili ni vyenye kuonekana sana katika sayari saba ambazo ni tukufu na kubwa sana katika vilivyothibiti, kwa kudhalilishwa sayari na nyota nyingine ndogondogo ni kwa njia nyepesi na uhakika zaidi kama Alivyotanabahisha Allah تعالى kwa Kauli Yake:

لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ ۚ إِنَّ كُنْتُمْ إِيَّاهُ

تَعْبُدُونَ ﴿٤١﴾

**“...Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Mwenyezi Mungu Aliye viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu.” (41:37)**

Pamoja na kwamba Yeye Ameliweka wazi hilo kwa Kauli Yake:

وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ مُسَخَّرَاتٌ بِأَمْرِ ۙ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ

الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

**“...Na jua, na mwezi, na nyota vimetiishwa kwa Amri Yake. Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (7:54)**



Na Kauli Yake,

يُفْضِلُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ بِلِقَاءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ ﴿١٣﴾

**“...na Anazipambanua Ishara ili mpate kuwa na yakini kukutana na Mola wenu Mlezi.”**

Maana yake: Anabainisha wazi ishara na dalili mbalimbali zenye kufahamisha kwamba hapana Mola anayestahiki kuabudiwa asiyekuwa kwa haki ila Yeye, na kwamba Atalirudisha umbile wakati wowote Atakapotaka kama Alivyolianza.

وَهُوَ الَّذِي مَدَّ الْأَرْضَ وَجَعَلَ فِيهَا رَواسِيَ وَأَنْهَارًا وَمِنْ كُلِّ الْأَنْمَاتِ جَعَلَ فِيهَا رِزْقَيْنِ  
 اثْنَيْنِ يُغْشَى اللَّيْلَ النَّهَارَ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٤﴾ وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ  
 مُتَجَوِّزَاتٌ وَجَنَّاتٌ مِّنْ أَعْنَابٍ وَزُرْعٌ وَنَخِيلٌ وَصِنَوَانٌ وَعُغْبُرٌ صِنَوَانٍ يُسْقَى بِمَاءٍ وَاحِدٍ  
 وَنُفْضِلُ بَعْضَهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِي الْأَكْلِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٥﴾

**3. Na Ndiye Aliyeitandaza ardhi na Akaweka humo milima na mito. Na katika kila matunda Akafanya dume na jike. Huufunika usiku juu ya mchana. Hakika katika haya zimo Ishara kwa watu wanaofikiri.**

**4. Na katika ardhi vimo vipande vilivyokaribiana, na zipo bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende yenye kuchipua kwenye shina moja na isiochipua kwenye shina moja, nayo inatiliwa maji yale yale. Na Tunaifanya baadhi yao bora kuliko mengine katika kula. Hakika katika hayo zimo ishara kwa watu wanaotia mambo akilini.**

**Ishara za Allah تعالیٰ katika Ardhi**

Alipoutaja Allah تعالیٰ Ulimwengu wa juu Ameanza Kutaja Uweza Wake na Hekima Yake na Kuutengeneza Kwake ulimwengu wa chini Amesema:

وَهُوَ الَّذِي مَدَّ الْأَرْضَ

**“Na Ndiye Aliyeitandaza ardhi...”**

Maana yake: Ameifanya pana, imenyooka katika urefu na upana na Ameithibitisha milima imara na mirefu, na Amepitisha katika ardhi mito na mifereji na chemchem ili Anywesheleze vile Alivyoviweka ardhini, miongoni mwa matunda yenye kutofautiana rangi, maumbile, ladha na harufu.

مِنْ كُلِّ زَوْجَيْنِ آتَيْنِ

**“Katika kila umbile pana namna mbili.” (11:40)**

Maana yake: katika kila umbile pana pea mbili.

يُغْشَى اللَّيْلَ اللَّهَارُ

**“Anaufunika usiku kwa mchana.”**

Maana yake: Amekifanya kila kimoja katika viwili hivyo kumtafuta mwingine, utafutaji wa haraka sana, kikiondoka hiki, kinakifunika hiki na kikimalizika hiki kinakuja kingine. Anafanya Atakavyo katika zama kama Anavyofanya Atakavyo katika mahali na wakazi wa mahali hapo.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١٦﴾

**“Hakika pana katika yote hayo alama nyingi za uwezo wa Mwenyezi Mungu – kwa watu wanaofikiri.”**

Maana yake: Wanazifikiria neema za Allah تعالی na Hukumu Yake na Dalili Yake. Kauli Yake:

وَفِي الْأَرْضِ قِطْعٌ مُّتَجَوِّزَاتٌ

**“Na katika ardhi vimo vipande vilivyokaribiana...”**

Maana yake: Ardhi zinakaribiana baadhi yake na baadhi, pamoja na kuwa kipande hiki ni kizuri kinaotesha yenye kuwafaa watu na kingine cha chumvi hakioteshi kitu chochote. Kama hivi amepokea Ibn Abbas na Mujahid, Saeed bin Jubair, Ad-dhahak na wengine رضي الله عنهم.<sup>1</sup> Na kunaingia katika ayah hii kutofautiana kwa rangi ya maeneo mbalimbali ya ardhi mchanga huu mweupe na mwengine wa manjano au mweusi. Na ardhi hii ina mawe na hii ni nyepesi,

<sup>1</sup> Tabari 16:331-333.

na hii ni ya mchanga, hii ni nzito na hii ni laini. Na vipande vyote hivyo vipo sehemu moja lakini kila kimoja kina sifa yake – ambayo haifanani na sifa ya kingine na haya yote ni katika yanayomfahamisha Allah تعالى Mwenye Kufanya Analolitaka, hapana Mola Mwenye kustahiki kuabudiwa kwa haki ila Yeye.

وَجَنَّتٌ مِّنْ أَعْنَابٍ وَزُرْعٌ وَنَخِيلٌ

**“Na zipo bustani za mizabibu, na mimea mingine, na mitende.”**

Inawezekana kuwa maneno haya katika kanuni ya sarufi ya kiarabu yameunganishwa na neno “*Jannaatu*” kwa hivyo yatakuwa matamko *Zar’un* na *Nakhiylun*. Ni yenye kutiwa alama ya *Dhumma* (U) na inawezekana yakawa maneno haya yameunganishwa na Zabibu “*A’anabin*” kwa hiyo matamko (*Zar’i* na *Nakhiylun*) yatakuwa na alama ya kasri (i) na kwa sababu hiyo limesomwa kwa njia zote mbili na kundi katika maimamu. Na Kauli Yake:

صِنَوَانٌ وَعَيْتُرٌ صِنَوَانٍ

**“Yenye kuchipua kwenye shina moja na isiochipua kwenye shina moja.”**

*Al-Swinwan* ni mashina yaliyokusanyika katika maoteo mamoja kama vile komamanga na Tini, na baadhi ya mitende na mfano wa hayo. Na yasiyokuwa *Al-Swinwan* ni mimea iliyokuwa juu ya shina moja tu kama ilivyo baki ya miti na kutokana na maana hayo, ameitwa Ami wa mtu kwa jina la ‘*Swinwa*’ akimaanisha ni shina moja na baba yake kama ilivyokuja katika Hadithi Sahihi kwamba Mtume ﷺ alisema kumuambia ‘Umar رضي الله عنه:

«أَمَا شَعَرْتَ أَنَّ عَمَّ الرَّجُلِ صِنْرٌ أَبِيهِ»

**“Hivi huelewi kwamba Ami wa mtu ni shina moja na Baba yake?”<sup>1</sup>**

Na Kauli Yake:

يُسْقَى بِمَاءٍ وَاحِدٍ وَتُفَضَّلُ بَعْضَهَا عَلَى بَعْضٍ فِي الْأَكْلِ<sup>٢</sup>

**“Nayo inatiliwa maji yale yale. Na Tunaifanya baadhi yao bora kuliko mengine katika kula.”**

<sup>1</sup> Muslim 2:677.



## Kukanusha Uhai Baada ya Kufa ni Jambo la Ajabu

Allah تعالی Anasema Akimuambia Mtume wake Muhammad ﷺ,

✽ وَإِنْ تَعَجَّبْ

**“Na ukistaajabu.”**

Kutokana na kukadhibisha kwa Washirikina hawa kuhusu kurejea akhera – pamoja na zile dalili ambazo wanazishuhudia miongoni mwa alama mbalimbali za Kuwepo kwa Allah تعالی Kutakata ni Kwake. Na pia dalili Zake kwa viumbe Wake juu ya kwamba Yeye ni Muweza juu ya lile ambalo Analitaka. Na pamoja na yale ambayo wanakiri kwayo miongoni mwa kuwa Yeye Ameanza Kuumba viumbe, Akavipatisha baada ya kuwa havikuwa ni vitu vyenye kutajwa.

Kisha wao baada ya yote hayo wanaikadhibisha taarifa Yake, kwamba Yeye Ataurejesha ulimwengu katika umbile jipya.

Na kwa hakika wamekiri na wameshuhudia mambo ambayo ni ya ajabu sana kuliko yale ambayo wameyakadhibisha. Basi kustaajabu kwao ni kwa kauli yao.

أَءِذَا كُنَّا تُرَابًا أَوْ إِنَّا لَفِي خَلْقٍ جَدِيدٍ

**“Hivi pindi tukiwa mchanga tutakuwa katika umbile jipya?”**

Na kwa hakika amejua kila mjuzi na mwenye akili kwamba Kuumbwa kwa mbingu na ardhi ni jambo kubwa sana kuliko Kuumbwa kwa watu. Na kwamba kwa Mwenye Kuanza Kuumba kulirejesha umbo ni rahisi sana Kwake.

Kama Alivyosema:

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَكُنْ لِيَّ خَلْقِهِنَّ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ مُنْحَىٰ  
الْمَوْتِ بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤٦﴾

**“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”**  
(46:33)

Kisha Amewasifu wale wenye kupinga haya kwa Kusema:

أُولَئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ وَأُولَئِكَ الْأَعْلَىٰ فِي أَعْنَاقِهِمْ

***“Hao ndio waliomkufuru Mola wao Mlezi. Na hao ndio wataokuwa na makongwa shingoni mwao, ...”***

Maana yake: Watakokotwa kwayo ndani ya moto:

وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٣﴾

***“Hao ndiyo watu wa motoni wao humo wataishi milele.”***

Maana yake: Watakaa humo milele, hawatahamishwa kutoka motoni na hawataondoka.

\* \* \*

وَدَسْتَعَجِلُونَكَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ وَقَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمُ  
 الْمَثَلَتُ وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ وَإِنَّ  
 رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٦﴾ وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا  
 أَنْزَلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ وَلِكُلِّ قَوْمٍ  
 هَادٍ ﴿٧﴾ اللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنثَىٰ وَمَا تَغِيضُ  
 الْأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ كُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٨﴾  
 عَلِيمٌ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْكَبِيرِ الْمُتَعَالِ ﴿٩﴾ سَوَاءٌ  
 مِنْكُمْ مَنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ  
 بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٠﴾ لَهُ مُعَقِّبَاتٌ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ  
 وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا  
 بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِقَوْمٍ سُوءًا  
 فَلَا مَرَدَّ لَهُ وَمَا لَهُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ وَالٍ ﴿١١﴾

وَدَسْتَعَجِلُونَكَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ  
 وَقَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمُ الْمَثَلَتُ وَإِنَّ  
 رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ  
 وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٦﴾

6. Na wanakuhimiza ulete maovu kabla ya mema, hali ya kuwa zimekwisha pita kabla yao adhabu za kupigiwa mfano. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa Kuadhibu.

Makafiri Wanataka Adhabu Iwapate Haraka

Allah تعالى Anasema:

وَدَسْتَعَجِلُونَكَ

“Na wanakuhimiza.”

Maana yake: Hawa wenye kukadhibisha.

بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ

“Ulete maovu kabla ya mema.”

Maana yake: Wanaitaka haraka adhabu kama Alivyowaelezea katika Kauli Yake:

وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ ﴿١٢﴾ لَوْ مَا تَأْتِينَا بِالْمَلَكَةِ إِنْ كُنْتَ

مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٣﴾ مَا نُنزِلُ الْمَلَكَةَ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَا كَانُوا إِذًا مُنظَرِينَ ﴿١٤﴾

**“Na walisema: Ewe uliyeteremshiwa Ukumbusho! Hakika wewe ni mwendawazimu. Mbona hutuletei Malaika ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli? Sisi hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya haki, na hapo hawatapewa muhula.” (15:6-8)**

Maana yake: Adhabu Yetu na Hesabu Yetu. Kama Alivyosema Akiwaelezea:

وَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ

**“Na wanakuhimiza waletewe adhabu...” (29:53-54).**

Amesema Allah تعالى:

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ

**“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itakayotokea.” (70:1)**

Na Amesema tena:

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا الْحَقُّ

**“Wasioamini huihimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanaoamini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli...” (42:18)**

Na Kauli Yake,

وَقَالُوا رَبَّنَا عَجِّلْ لَنَا قِطْنَا

**“Mola wetu Mlezi! Tuletee upesi sehemu yetu ya adhabu.”**

Maana yake: Adhabu yetu na hesabu yetu. Allah تعالى Amesema kuwa waliomba kama ifuatavyo,

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِنَّ كَارِبَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ

**“Na waliposema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako...”**

Walikuwa makafiri waasi na sugu kiasi kwamba, walimuomba Mtume ﷺ awalettee adhabu ya Allah تعالى. Allah تعالى Akajibu,

وَقَدْ خَلَّتْ مِنْ قَبْلِهِمُ الْمَثَلُتُ

**“...hali ya kuwa zimekwisha pita kabla yao adhabu za kupigiwa mfano.”**



Maana yake: Tulishawaadhibu umma uliotangulia, na Tukawapa fundisho na mfano kwa wenye kutafakari maangamizo yao.

Isingekuwa Stahmala na Maghufira Yake, basi Allah تعالى Angewaadhibu haraka, kwa hakika. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهَرِهَا مِنْ دَابَّةٍ

**“Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwachukulia watu kwa waliyoyachuma, basi Asingelimuacha juu ya ardhi hata mnyama mmoja.”**

Na Amesema katika Aya hii Tukufu,

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِّلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ

**“Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao.”**

Maana yake: Hakika Yeye Allah تعالى ni Mwenye Kusamehe na Kutupilia mbali na Kuwasitiri watu pamoja na kuwa wao wanadhulumu na wanakosea usiku na mchana. Kisha Ameikutanisha hukumu hii na kwamba Yeye ni mkali wa mateso ili yalingane sawa matarajiwa na khofu, kama Alivyosema Allah تعالى:

فَإِن كَذَّبُوكَ فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٧﴾

**“Wakikukanusha basi wewe sema: Mola Mlezi wenu ni Mwenye Rehema iliyoenea. Wala haizuiliki Adhabu Yake kwa watu wakhalifu.” (7:147)**

إِنَّ رَبَّكَ لَسَرِيعُ الْعِقَابِ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ

**“Hakika Mola wako Mlezi ni Mwepesi wa Kuadhibu, na bila ya shaka ni Mwenye Maghufira, na Mwenye Kurehemu.” (A’raf: 167)**

نَبِيَّ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٥﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ ﴿١٦﴾

**“Waambie waja Wangu ya kwamba Mimi Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu. Na kwamba Adhabu Yangu ndio Adhabu iliyo chungu!” (15:49-50)**

Kuna Aya nyingine nyingi zenye kueleza hofu na matumaini,

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ وَلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ ﴿٦﴾

**7. Na wale waliokufuru husema: Mbona hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Hakika wewe ni Mwonyaji, na kila kaumu ina wa kuwaongoa.**

### Washirikina Wataka Waletewe Muujiza na Majibu Yao

Allah تعالى Anasema Akiwaeleza washirikina wanaosema kwa kukanusha na inadi, kwa nini hatuletewi muujiza kutoka kwa Bwana Wake, kama walivyopelekewa Mitume wa Kwanza. Kama ambavyo walionesha ukaidi wa kutaka mlima swafa uwe wa dhahabu, na Awaondolee majabali na Afanye mahali pake nyasi na mito. Allah تعالى Amesema:

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوَّلُونَ

**“Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha.” (17:59)**

Allah تعالى Amesema:

إِنَّمَا أَنْتَ مُنذِرٌ

**“Hakika wewe ni Mwonyaji.”** Maana yake: Hakika hapana jambo jingine ni juu yako kufikisha ujumbe wa Allah تعالى ambao Amekuamrisha kwao.

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

**“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye.” (2:272)**

Na Kauli Yake,

وَلِكُلِّ قَوْمٍ هَادٍ

**“...na kila kaumu ina wa kuwaongoa.”**

Amesema Ali Bin Abii Twalha<sup>1</sup> kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: Ina maana, kila watu wana mlinganiaji. Kama Ilivyo Kauli Yake,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:357.

وَأَنَّ مِنْ أُمَّةٍ إِلَّا حَلَا فِيهَا نَذِيرٌ

**“Na hapana umma wowote ila ulipata mwonyaji kati yao.” (35:24)**

Na kwa Kauli hii amesema Qatadah na Abdurrahman Bin Zaid.<sup>1</sup>

اللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنثَىٰ وَمَا تَغِيضُ الْأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ ۗ وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٨٨﴾ عَلِيمُ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ الْكَبِيرُ الْمُتَعَالِ ﴿٨٩﴾

**8. Mwenyezi Mungu Anajua mimba abebayo kila mwanamke, na kinachopunguka na kuzidi matumboni. Na kila kitu Kwake ni kwa kipimo.**

**9. Yeye Ndiye Mwenye Kujua yanayoonekana na yasioonekana; Mkuu Aliyetukuka.**

**Mjuzi wa Mambo Yaliyojificha ni Allah تعالى Pekee**

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Ukamilifu wa Elimu Yake ambayo Haijifichi juu yake kitu chochote. Na kwamba Yeye Amevizunguka kwa elimu vile vinavyochukuliwa na wenye mimba katika kila wanawake na wanyama.

Kama Allah تعالى Alivyosema:

وَيَعْلَمُ مَا فِي الْأَرْحَامِ ۗ

**“Na Anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi.” (31:34)**

Maana yake: Vile ambavyo imevichukua mifuko hiyo iwapo, mwanamume au mwanamke, mzuri au mbaya, muovu au mwema, mwenye umri mrefu au mfupi kama Alivyosema Allah تعالى:

هُوَ أَعْلَمُ بِكُمْ إِذْ أَنْشَأَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ وَإِذْ أَنْتُمْ أَجِنَّةٌ

**“...Naye Anakujueni sana tangu Alipokuumbeni kutoka kwenye ardhi, na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu.” (53:32)**

<sup>1</sup> At-Tabari: 16:356.

Na Allah تعالى Amesema:

تَخْلُقُكُمْ فِي بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ خَلَقًا مِّنْ بَعْدِ خَلْقِ فِي ظُلُمَاتٍ ثَلَاثٍ

**“Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu.” (39:6)**

Maana yake: Amewaumbeni hali baada ya hali, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِّن طِينٍ ﴿٦﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿٧﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظْمًا فَكَسَوْنَا الْعِظْمَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿٨﴾

**“Na kwa yakini Tumemuumba mtu kutokana na asili ya udongo. Kisha Tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha Tukaiumba tone kuwa damu iliyoganda, na Tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha Tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama. Kisha Tukamfanya kiumbe mwengine. Basi Ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.” (23:12-14)**

Na imekuja katika Sahihi ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Ibn Masuud رضي الله عنهما, Amesema: Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ خَلْقَ أَحَدِكُمْ يُجْمَعُ فِي بَطْنِ أُمِّهِ أَرْبَعِينَ يَوْمًا، ثُمَّ يَكُونُ عَلَقَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَكُونُ مُضْغَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَنْعَثُ اللَّهُ إِلَيْهِ مَلَكًا فَيُؤَمِّرُ بِأَرْبَعِ كَلِمَاتٍ، يَكْتُبُ رِزْقَهُ، وَعُمُرَهُ، وَعَمَلَهُ، وَشَقِيَّ أَوْ سَعِيدًا،

**“Kwa hakika umbile la mmoja wenu linakusanywa tumboni mwa mama yake, kwa muda wa siku arubaini. Kisha linakuwa pande la damu, mfano wa hivyo, kisha linakuwa pande la nyama mfano wa hivyo, kisha Anampeleka Mwenyezi Mungu kwake malaika anaamrisha kuandika matamko manne: Kuandika riziki yake, umri wake, matendo yake na muovu au mwema.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 11:486, Muslim 4:2036.

Na imekuja katika Hadithi nyingine:

«فَيَقُولُ الْمَلَكُ: أَيُّ رَبِّ أَدَّكَرْتُ أَمْ أَنْتَى؟ أَيُّ رَبِّ أَشَقِيَّيْ أَمْ سَعِيدِيَّ؟ فَمَا الرِّزْقُ؟ فَمَا الأَجَلُ؟ فَيَقُولُ اللهُ: وَيَكْتُبُ الْمَلَكُ»

*“Atasema Malaika: Ee Bwana ni mwanamume au mwanamke? Ee Bwana ni muovu au mwema? Ni ipi riziki yake? Ni upi muda wake? Atasema Mwenyezi Mungu na ataandika malaika.”<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake تعالَى:

وَمَا تَغِيضُ الأَرْحَامُ وَمَا تَزْدَادُ<sup>ع</sup>

**“...na kinachopunguka na kuzidi matumboni.”**

Al-Bukhari ameandika kuwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما amesema, Mtume ﷺ amesema:

«مَفَاتِيحُ الغَيْبِ خَمْسٌ، لَا يَعْلَمُهُنَّ إِلاَّ اللهُ: لَا يَعْلَمُ مَا فِي غَدِ إِلاَّ اللهُ، وَلَا يَعْلَمُ مَا تَغِيضُ الأَرْحَامُ إِلاَّ اللهُ، وَلَا يَعْلَمُ مَنْ يَأْتِي المَطَرُ أَحَدٌ إِلاَّ اللهُ، وَلَا تَدْرِي نَفْسٌ بِأَيِّ أَرْضٍ تُمُوتُ، وَلَا يَعْلَمُ مَنْ تَقُومُ السَّاعَةُ إِلاَّ اللهُ»

*“Funguo za mambo yaliyojificha ni tano: Hajui mambo ya kesho isipokuwa Mwenyezi Mungu na hajui kupungua kwa mifuko ya uzazi isipokuwa Mwenyezi Mungu na hajui mtu yeyote lini itakuja mvua isipokuwa Mwenyezi Mungu na hajui nafsi yeyote ni katika ardhi gani itakufa, na hajui mtu ni lini kitasimama Kiyama isipokuwa Mwenyezi Mungu.”<sup>2</sup>*

Na amesema Al-Awafi رضي الله عنهما kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه,

وَمَا تَغِيضُ الأَرْحَامُ

**“...na kinachopunguka matumboni.”**

Anakusudia kipomoko.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 11:486, Muslim 4:2038.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 8:225.

وَمَا تَزِدَادُ<sup>ط</sup>

**“...na kuzidi matumboni.”**

Anasema: Kilichozi mfuko wa uzazi katika mimba juu ya kilichopungua mpaka ukakizaa hali ya kutimia, na hilo ni kwamba katika wanawake, wapo ambao huchukua mimba kwa miezi sita, wengine huchukua kwa miezi tisa, na wapo wanaozidi hapo, na wapo wa pungufu ya hapo. Kwa hiyo huko kupungua na kuongezeka ndiko alikokutaja Allah تعالى, na yote hayo ni kwa Elimu Yake Allah تعالى.<sup>1</sup> Amesema Qatadah:

وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِمِقْدَارٍ

**“Na kila kitu Kwake ni kwa kipimo.”**

Kwa muda uliopangwa. Allah تعالى Amehifadhi riziki za viumbe wake na muda wao na wa kila kitu. Na imekuja katika Hadithi Sahihi, kwamba mmoja wa mabinti za Mtume ﷺ alikwenda kumhabarisha Mjumbe kuwa mwanaye alikaribia kufariki na angependa awepo. Mtume ﷺ akamtuma mjumbe kumuambia:

«إِنَّ لِلَّهِ مَا أَخَذَ، وَلَهُ مَا أُعْطِيَ، وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ بِأَجَلٍ مُّسَمًّى، فَمُرُّهَا فَلْتَنْصِبْ  
وَلْتَحْتَسِبْ»

*“Kwa hakika ni cha Allah Alichochukua na ni Chake Alichotoa na kila kitu Kwake, kina muda uliowekwa, hivyo muamrisheni asubiri na ataraji thawabu.”<sup>2</sup>*

عَلِمُوا الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ

**“...Yeye Ndiye Mwenye Kujua yanayoonekana na yasioonekana;...”**

Anajua yote wanayoona waja na wasiyoyaona, na hakijifichi Kwake kitu chochote

الْكَبِيرُ

**“Mkuu.”** Aliye Mkubwa sana.

<sup>1</sup> Tabari 16:359.

<sup>2</sup> Al-Bukhari 7385, An-Nasai katika *Al-Kubra* 1570, Ibn Majah 188, At-Tabari 5:28.

## الْمُتَعَالِ

“Aliyetukuka.” Juu ya vyote.

قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**“Mwenyezi Mungu Amekizunguka kila kitu Kukijua vilivyo kwa ilimu Yake.” (65:12)**

Na Amekitenza nguvu kila kitu kwa hiyo zimenyenyekea Kwake shingo na wamenyenyekea Kwake waja kwa hiari na kwa lazima.

سَوَاءٌ مِنْكُمْ مَنْ أَسَرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ ﴿١٢﴾  
 لَهُدُ مُعَقِّبَتٌ مِّنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا  
 بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ ۗ وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ ۗ وَمَا لَهُمْ مِنْ  
 دُونِهِ مِنْ وَالٍ ﴿١٣﴾

**10. Ni sawa anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhihirisha, na anayejibanza usiku na anayetembea jahara mchana.**

**11. Kila mtu analo kundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao. Na Mwenyezi Mungu Anapowatakiwa watu adhabu hakuna cha kuzuia wala hawana mlinzi yeyote badala Yake.**

**Elimu ya Allah تعالى Imekizunguka kila Chenye Kuonekana na Kilichojificha**

Allah تعالى Ameerza kuhusu Elimu Yake Kuzunguka viumbe Wake wote, na kwamba ni sawa miongoni mwao mwenye kuyaficha maneno yake na mwenye kuyadhihirisha, kwani Yeye Anayasikia na hakuna kinachojificha Kwake kitu chochote. Kama ilivyo Kauli Yake

وَإِنْ تَجَهَّرَ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿١٤﴾

**“Na ukinyanyua sauti kwa kusema, basi hakika Yeye Anajua siri na duni kuliko siri.” (20:7) na**

وَيَعْلَمُ مَا تُخْفُونَ وَمَا تُعْلِنُونَ

**“...na Anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza.” (27:25)**

Aishah رضي الله عنها amesema Kutakata ni kwa Yule ambaye Umekunjuka Usikivu Wake sauti zote. Wallahi, yule mwanamke aliyejadiliana na Mtume ﷺ kuhusu mumewe, Khawla Binti Thaalaba رضي الله عنها alikuja kumshitaki, kwa Mtume ﷺ, mume wake na hali ya kuwa mimi niko ubavuni mwa nyumba. Na kwa hakika baadhi ya maneno ya mwanamke huyo yalikuwa yakinipita. Allah تعالى Akateremsha:

قَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّتِي تُجَادِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِي إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَا إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿١٥﴾

**“Mwenyezi Mungu Amekwishasikia usemi wa mwanamke anayejadiliana nawe juu ya mumewe, na anamshitakia Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anayasikia majibizano yenu. Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.” (58:1)<sup>1</sup>**

Na Kauli Yake:

وَمَنْ هُوَ مُسْتَخَفٌّ بِآيَاتِنَا

**“...na anayejibanza usiku...”**

Maana yake: Mwenye kujificha katika maficho ya nyumba yake, katika kiza cha usiku:

وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ

**“...na anayetembea jahara mchana.”**

Maana yake: Mwenye kuonekana, mwenye kwenda katika weupe wa mchana na mwangaza wake, kwani yote mawili hayo yamo katika Elimu ya Allah تعالى kwa usawa. Kama ilivyo katika Kauli Yake;

أَلَا حِينَ يَسْتَغْشُونَ ثِيَابَهُمْ

**“Jueni kuwa wanapojigubika nguo zao...” (11:5)**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 11:502.



وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦١﴾

***“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilichowazi.” (10:61)***

### **Malaika Wenye Kulinda**

Na Kauli Yake:

لَهُمْ مُعَقِّبَاتٌ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِمْ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ

***“Kila mtu analo kundi la malaika mbele yake na nyuma yake linamlinda kwa Amri ya Mwenyezi Mungu.”***

Maana yake: Mja ana Malaika wanaopishana juu yake, kuna walinzi usiku na kuna walinzi mchana wanaomlinda na mambo mabaya na matukio mbalimbali. Kama wanavyopishana malaika wengi kwa ajili ya kuyahifadhi matendo miongoni mwa kheri au shari. Kuna Malaika wa usiku na kuna malaika wa mchana, wawili wanakuwa upande wa kulia na kushoto, wanayaandika matendo, wa upande wa kulia anaandika matendo mema na wa kushoto anaandika matendo maovu. Na kuna malaika wawili wengine wanamuhifadhi na wanamlinda, mmoja nyuma yake na mwengine mbele yake. Kwa hiyo mja anakuwa kati ya malaika wanne wakati wa mchana na wanne wengine wakati wa usiku, hali ya kuwa wanabadilishana, wanamlinda na wanaandika kama ilivyokuja katika hadithi Sahihi:

«يَتَعَاقِبُونَ فِيكُمْ مَلَائِكَةٌ بِاللَّيْلِ وَمَلَائِكَةٌ بِالنَّهَارِ، وَيَجْمَعُونَ فِي صَلَاةِ الصُّبْحِ وَصَلَاةِ الْعَصْرِ، فَيَضَعُونَ إِلَيْهِ الَّذِينَ بَاتُوا فِيكُمْ فَيَسْأَلُهُمْ وَهُمْ أَعْلَمُ بِكُمْ: كَيْفَ تَرَكْتُمْ عِبَادِي؟ فَيَقُولُونَ: أَتَيْنَاهُمْ وَهُمْ يُصَلُّونَ، وَتَرَكْنَاهُمْ وَهُمْ يُصَلُّونَ»

*“Malaika wa usiku na wa mchana huwa wanashika zamu kwenu, na wanakusanyika katika Sala ya asubuhi na alasiri. Basi hupanda kumuendea Allah, wale wa zamu ya usiku kwenu, Naye Huwauliza, ilhali Yeye Anakujueni zaidi, ‘Mmewaachaje waja wangu?’ Nao wanajibu, ‘Tumewaendea hali ya kuwa wanasali, na tumewaacha hali ya kuwa wanasali.’”<sup>1</sup>*

Na amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Abdillah رضى الله عنه amesema: Amesema Mtume ﷺ:

«مَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا وَقَدْ وَكَّلَ بِهِ قَرِينٌ مِنَ الْجِنِّ وَقَرِينُهُ مِنَ الْمَلَائِكَةِ»

*“Hapana katika nyinyi mtu yeyote isipokuwa ametegemezwa kwake mwambata wake katika majini na mwambata wake katika malaika.”*

Wakasema, ‘na wewe Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?’ Akasema

«وَأَيُّهَا، وَلَكِنَّ اللَّهَ أَعَانَنِي عَلَيْهِ، فَلَا يَأْمُرُنِي إِلَّا بِخَيْرٍ»

*“Na mimi isipokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu Amenisaidia juu yake kwa hiyo haniamrishi isipokuwa kheri.”<sup>2</sup>*

Hadithi hii imenukuliwa na Imam Muslim pekee.<sup>3</sup> Na ameipokea Ibnu Abuu Hatim kutoka kwa Ibrahim amesema: Allah تعالى Alipeleka wahyi kwa Mtume mmoja katika Mitume wa Bani Israili kwamba waambie watu wako: ‘Kwa hakika haiwi kwa watu wa kijiji wala wa mjini wanaokuwa juu ya utii wa Allah تعالى kisha wakageuka kutoka katika utii wakaenda kwenye maasia, isipokuwa Allah تعالى Hubadilisha yale wanayoyapenda na Kuwapa ambayo wanayachukia, kisha akasema: Uthibitisho wa hilo umo katika kitabu cha Allah تعالى,

«إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّى يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ»

***“Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao.”***

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 13:426.

<sup>2</sup> Ahmad 1:401.

<sup>3</sup> Muslim na. 2:2814.

هُوَ الَّذِي يُرِيكُمُ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنْذِرُ  
 السَّحَابَ الثِّقَالَ ﴿١٢﴾ وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ  
 وَالْمَلَأْتِكُمْ مِنْ خِفَّتِهِ وَيُرْسِلُ الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَنْ  
 يَشَاءُ وَهُمْ يُجَادِلُونَ فِي اللَّهِ وَهُوَ شَدِيدُ الْحَالِ ﴿١٣﴾  
 لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ  
 لَهُمْ بِشَيْءٍ إِلَّا كَبْسِطٍ كَفْبِهِ إِلَى الْمَاءِ لِيَبْلُغَ فَاهُ وَمَا هُوَ  
 بِبَلِيغٍ ۚ وَمَا دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿١٤﴾ وَاللَّهُ  
 يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَظِلَالُهُمْ  
 بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿١٥﴾ قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ  
 قُلِ اللَّهُ ۚ قُلْ أَفَأَتَّخِذْتُمْ مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ لَا يَمْلِكُونَ  
 لِأَنْفُسِهِمْ نَفْعًا وَلَا ضَرًّا ۚ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَى  
 وَالْبَصِيرُ أَمْ هَلْ تَسْتَوِي الظُّلُمَاتُ وَالنُّورُ ۚ أَمْ جَعَلُوا لِلَّهِ  
 شُرَكَاءَ خَلَقُوا كَخَلْقِهِ فَتَشَبَّهُهُ الْخَلْقُ عَلَيْهِمْ ۚ قُلِ اللَّهُ خَلِقُ  
 كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿١٦﴾

هُوَ الَّذِي يُرِيكُمُ الْبَرْقَ خَوْفًا  
 وَطَمَعًا وَيُنْذِرُ السَّحَابَ الثِّقَالَ  
 ﴿١٢﴾ وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ  
 وَالْمَلَأْتِكُمْ مِنْ خِفَّتِهِ وَيُرْسِلُ  
 الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَنْ يَشَاءُ وَهُمْ  
 يُجَادِلُونَ فِي اللَّهِ وَهُوَ شَدِيدُ  
 الْحَالِ ﴿١٣﴾

12. Yeye Ndiye Anayeku-  
 onesheni umeme kwa khofu  
 na tamaa, na Huyaleta  
 mawingu mazito.

13. Na radi inamtakasa  
 Mwenyezi Mungu kwa  
 kumhimidi, na Malaika pia,  
 kwa kumkhofu. Naye Hupe-  
 leka mapigo ya radi yaka-  
 mpata Amtakaye. Nao  
 wanabishana juu ya  
 Mwenyezi Mungu. Na Yeye  
 ni Mwenye Adhabu kali!

**Mawingu, Umeme na Radi na Sauti ya Radi ni katika Uwezo wa Allah** تعالى

Anaeleza Allah تعالى, kwamba Yeye Ndiye Aliyeidhalilisha radi, nayo ni ile inayoonekana miongoni mwa mwangaza wenye kumweka katikati ya mawingu. Na amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى, kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما aliandika kwa Abu Al Jald عنه رضي الله عنهما akimuuliza kuhusu radi akasema radi ni maji.<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Tabari: 16:387.

Na Kauli Yake تعالى:

خَوْفًا وَطَمَعًا

**"...kwa khofu na tamaa,"**

Amesema Qatada: Hofu ni kwa msafiri - anaogopa maudhi Yake na taabu Yake; na tamaa ni kwa mkazi - anataraji kupata baraka Zake na manufaa Yake na anatumai kupata riziki ya Allah تعالى.

وَيُنشِئُ السَّحَابَ الثِّقَالَ

**"...na Huyaleta mawingu mazito."**

Maana yake: Anayaumba umbo jipya, na kutokana na wingi wa maji yake yamekuwa mazito, yamekaribia katika ardhi. Amesema Mujahid: Mawingu mazito ni yale yenye maji.<sup>1</sup> Allah تعالى Amesema:

وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ

**"Na radi inamtakasa Mwenyezi Mungu kwa kumhimidi."**

Kama ilivyo Kauli Yake nyingine:

وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ

**"Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake." (17:44)**

Imam Ahmad ameandika kuwa Ibrahim bin Said amesema, "Baba yangu aliniambia kuwa alikuwa amekaa ubavuni mwa Humaid bin Abdirrahman msikitini, akapita mtu wa Bani Ghifar aliyempa ujumbe Hamid, na alipokuja alisema: 'Ee mtoto wa ndugu yangu mpe nafasi baina yangu na wewe, kwani huyo alifuatana na Mtume ﷺ. Hivyo akasogea hadi akakaa baina yangu na yeye. Humaid akamuambia, "Ni Hadithi gani uliyoisimulia kutoka kwa Mtume?" Basi mtu huyo wa Ghifar akasema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akiwa anasema:

«إِنَّ اللَّهَ يُنْشِئُ السَّحَابَ فَيَنْطِقُ أَحْسَنَ التَّنْقِيهِ، وَيَضْحَكُ أَحْسَنَ الضَّحِكِ»

**"Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anayaumba mawingu yanatamka kutamka kuzuri sana na yanacheka kucheka kuzuri sana."<sup>2</sup>**

<sup>1</sup> Tabari 16:388.

<sup>2</sup> Ahmad 5:435.

Na maana yake, Allah تعالی Ndiye Mjuzi sana, ni kwamba kutamka kwa *Raad* na kucheka kwake ni mmweko. Na amesema Mussa bin Ubayda kutoka kwa Saad bin Ibrahim amesema: Allah تعالی Huleta mvua, hapana kitu kizuri sana kwa kucheka katika mvua na hapana kitu chenye kuliwaza sana kwa kutamka kwa mvua. Kucheka kwake ni mmweko na kutamka kwake ni Radi.

### Kuomba Wakati wa Radi

Imam Ahmad ameandika kutoka kwa Salim kutoka kwa Baba yake, amesema. Alikuwa Mtume ﷺ pindi anapoisikia Radi na Sauti yake husema:

«اللَّهُمَّ لَا تَقْتُلْنَا بِغَضَبِكَ، وَلَا تُهْلِكْنَا بِعَذَابِكَ، وَعَافِنَا قَبْلَ ذَلِكَ»

*“Ee Mola wangu wa haki Usituuwe kwa Ghadhabu Yako, na Usituangamize kwa Adhabu Yako na tuondolee Machukivu Yako kabla ya hapo.”<sup>1</sup>*

Na amepokea maneno hayo Attirmidhy, na Al-Bukhari katika Al-Adab, na Annasai katika Al-Yaumu wal Llayla na Al-Hakimu katika *Al-Mustadrak*.<sup>2</sup> Na imepokea kutoka kwa Abdillah bin Azubair رضي الله عنه kwamba yeye alikuwa wakati anapoisikia *Raad* huacha mazungumzo na husema: Kutakata ni kwa Yule Ambaye inamtakasa *Raad* pamoja na Kumsifu, na Malaika kutokana na kumwogopa Yeye. Alikuwa anasema: Kwa hakika hayo ni makamio makubwa kwa watu wa ardhini. Amepokea Imam Malik رحمه الله تعالی katika Al-Muwatta na Al Bukhari رحمه الله تعالی katika kitabu *Al-Adab*.<sup>3</sup> Na amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«قَالَ رَبُّكُمْ عَزَّ وَجَلَّ: لَوْ أَنَّ عِبِيدِي أَطَاعُونِي لِأَسْقَيْتُهُمُ الْمَطَرَ بِاللَّيْلِ، وَأَطْلَعْتُ عَلَيْهِمُ الشَّمْسَ بِالنَّهَارِ، وَلَمَّا أَسْمَعْتُهُمْ صَوْتَ الرَّعْدِ»

*“Amesema Bwana wenu: Lau kwamba waja Wangu wangenitii Ningewanyweshwa mvua usiku na Ningewachomozea jua mchana na Nisingewasikilizisha sauti ya Radi.”<sup>4</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 2:100.

<sup>2</sup> Ahmad 2:359.

<sup>3</sup> *Tuhfat Al-Ahwadhi* 9:412, *Al-Adab Al-Mufrad* 187, An-nasai katika *Al-Kubra* 6:230, Al-Hakim 4:286.

<sup>4</sup> *Al-Muwatta* 2:992, Al-Bukhari katika *Al-Adab Al-Mufrad* na. 724.

Na Kauli ya Allah تعالى:

وَأَرْسِلْ الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَنْ يَشَاءُ

***“Naye Hupeleka mapigo ya radi yakampata Amtakaye.”***

Huwapelekea Adhabu Anaowataka. Na Raad zitakithiri katika zama za mwisho.

Na amepokea Al-Hafidhi –Abu Al-Qasim Attabarani رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwamba Arbad bin Qaysi bin Jaz’i bin Jalid bin Jaafar bin Kallab na Amir bin Attufal bin Maliki walifika Madina kwa Mtume ﷺ na kuashiria kwake na hali ya kuwa amekaa, wakakaa mbele yake, akasema Aamir Bin Attufail, ‘Ee Muhammad ﷺ utanipa nini iwapo nitasilimu.’ Akasema Mtume ﷺ:

لَكَ مَا لِلْمُسْلِمِينَ وَعَلَيْكَ مَا عَلَيْهِمْ

*“Ni haki yako yale ambayo ni haki ya Waislamu wote na ni juu yako yale ambayo yako juu ya Waislamu wote.”*

Akasema Aamir bin Attufail: ‘Jee utalifanya hilo kuwa ni jambo langu baada yako? Iwapo nitasilimu?’ Mtume ﷺ akasema;

لَيْسَ ذَلِكَ لَكَ وَلَا لِقَوْمِكَ، وَلَكِنَّ لَكَ أَعْتَةَ الْخَيْلِ

*“Halikuwa hilo ni lako wewe wala la jamaa zako isipokuwa ni zako hatamu za farasi.”*

Aamir akasema: ‘Mimi hivi sasa nimo katika hatamu za farasi wa Najad, nipe mimi vijiji na ni yako wewe miji.’ Akakataa Mtume ﷺ. Watu hao wawili walipokuwa wakiondoka kwa Mtume ﷺ, Aamir alisema, “Wallah! Nitaijaza (Al-Madinah) farasi na watu (wakorofi kwa Waislamu).” Mtume ﷺ akajibu:

يَتَنَعَكَ اللَّهُ

*“Atakuzuia wewe Mwenyezi Mungu.”*

Alipotoka Arbad na Aamir alisema Aamir: ‘Ee Arbad mimi nitamshughulisha Muhammad kwa mazungumzo na wewe mpige kwa upanga, kwani watu watakapomuua Muhammad hawatazidisha jambo lingine isipokuwa kuridhia kupewa malipo (Dia) na watavivichukia vita, kwa hiyo tutawapa malipo.’ Akasema Arbad: ‘Fanya.’ Wakaja wakiwa wanarejea kwake, akasema Aamir. ‘Ee Muhammad – simama pamoja nami nikusemeshe.’ Akasimama pamoja

naye Mtume ﷺ, wakakaa wakiwa wamechegemea ukuta, na akasimama pamoja naye Mtume ﷺ huku akimsemesha. Akachomoa Arbad upanga, alipouweka mkono wake juu ya upanga, ulikauka mkono wake juu ya mpini wa upanga. Kwa hiyo hakuweza kuuchomoa upanga, akachelewa Arbad juu ya Aamir kumpiga kwa upanga. Akageuka Mtume ﷺ akamuona Arbad na yale aliyokuwa anayafanya. Mtume ﷺ akawaondokea. Walipotoka Aamir na Arbad kutoka mbele ya Mtume ﷺ mpaka walipokuwa mahali paitwapo Al-Harra – Harra Waqim - walishuka, akawatokea Saad bin Muadhi na Usaid Bin Hudhair wakawaambia: ‘Simameni enyi maadui wa Allah تعالی. Allah تعالی Amewalaani.’ Akasema Aamir, ‘ni nani huyo Ee Saad?’ Akasema, ‘huyu ni Usaid Ibni Al-Hudhair, Al-Kataib. Wawili hao wakatoka mpaka walipokuwa mahali paitwapo Arraqmi. Allah تعالی Akamtumia Arbad Radi yenye sauti kali ikamuua. Na alitoka Aamir mpaka alipokuwa mahali paitwapo Al-Kharim, Allah تعالی Akamtumia upele ukamkamata, ukafika usiku akiwa katika nyumba ya mwanamke katika Bani Salul, akawa anaushika upele wake ukiwa katika umbo la duara huku anasema: ‘Ugonjwa wa tauni kama ugonjwa wa tauni ya ngamia.’ Na alikuwa katika nyumba ya Mwanamke wa ukoo wa Salul na akapenda afie nyumbani mwake. Akatoka kisha akampanda farasi wake akaenda naye mpaka akafa juu yake hali ya kuwa anarudi kwake. Allah تعالی akateremsha (Aya hizi 13:8-11) kwa watu wawili hao,

اللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَحْمِلُ كُلُّ أُنثَىٰ

**“Mwenyezi Mungu Anajua mimba abebayo kila mwanamke,”** Mpaka,

وَمَا لَهُمْ مِّنْ دُونِهِ مِّنْ وَّالٍ

**“...wala hawana mlinzi yeyote badala Yake.”**

Amesema: Wale Malaika wanaopishana kutokana na amri ya Allah تعالی wanamlinda Muhammad ﷺ. Kisha Akamtaja Arbadi na kile alichomuua kwacho, Akasema:

وُزِّيْلُ الصَّوْعِقِ

**“Naye Hupeleka mapigo ya radi...”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> At-Tabarani 10:379-381. Hadithi inayoeleza sehemu ya kisa hiki imeandkwa na Al-Bukhari, na 4091. Haielezi kauli za Mtume ﷺ.

وَهُمْ مُجْتَدِلُونَ فِي اللَّهِ

**“Na wanabishana juu ya Mwenyezi Mungu.”**

Wanatia shaka Utukufu Wake na kwamba hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye.

وَهُوَ شَدِيدُ الْحَالِ

**“Na Yeye ni Mwenye adhabu kali!”**

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: Ana adhabu kali kwa anayeruka mipaka na kukaidi na kuendelea katika ukafiri wake.<sup>1</sup> Na aya hii inafanana na Kauli Yake

وَمَكْرُوا مَكْرًا وَمَكْرَنَا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٠﴾ فَأَنْظِرْ كَيْفَ كَانَ عَنَقِبَةُ  
مَكْرِهِمْ أَنَا دَمَرْنَاهُمْ وَقَوْمَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥١﴾

**“Basi wakapanga mipango yao, na Sisi Tukapanga mipango Yetu, na wao hawatambui. Basi angalia ulivyokuwa mwisho wa mipango yao, ya kwamba Tuliwaangamiza wao pamoja na watu wao wote.”**  
(27:50-51)

Na imepokewa kutoka kwa Ali رضي الله عنه,

وَهُوَ شَدِيدُ الْحَالِ

**“Na Yeye ni Mwenye adhabu kali!”**

Maana yake: mkali wa mashiko.<sup>2</sup>

لَهُ دَعْوَةُ الْحَقِّ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ لَا يَسْتَجِيبُونَ لَهُمْ بِشَيْءٍ إِلَّا كَبْسِطٍ كَفِيٍّ إِلَى  
الْمَاءِ لِيَبْلُغَ فَاهُ وَمَا هُوَ بِبَالِغِهِمْ وَمَا دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ ﴿٥١﴾

**14. Wa kuombwa kweli ni Yeye tu. Na hao wanaowaomba badala Yake hawawajibu chochote; bali ni kama mwenye kunyoosha viganja vyake kwenye maji ili yafike kinywani mwake, lakini hayafiki. Na maombi ya makafiri hayako ila katika upotovu.**

<sup>1</sup> Tabari 16:394.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:396.



## Kuonesha Mfano wa Kushindwa kwa Miungu ya Washirikina

Ali Bin Abii Talib رضي الله عنه amesema,

لَهُ دَعْوَةٌ أَحَقُّ<sup>ط</sup>

**“Wa kuombwa kweli ni Yeye tu.”**

Amesema: ni upwekeshaji. Amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى.<sup>1</sup> Wamesema Ibn Abbas, Qatada na Malik رضي الله عنهم kutoka kwa Muhammad bin Munkadiri رضي الله عنه.

لَهُ دَعْوَةٌ أَحَقُّ<sup>ط</sup>

**“Wa kuombwa kweli ni Yeye tu.”**

Hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى.<sup>2</sup>

وَالَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِهِ

**“Na hao wanaowaomba badala Yake...”**

Na mfano wa wale ambao wanawaabudu waungu wasiokuwa Allah تعالى .

Kauli ya Allah تعالى,

كَبَسِطَ كَفِّهِ إِلَى الْمَاءِ لِيَبْلُغَ فَاهُ

**“...ni kama mwenye kunyoosha viganja vyake kwenye maji ili yafike kinywani mwake,”**

Ali Bin Abii Talib رضي الله عنه amesema. Ni kama mfano wa anayechukua maji kutoka ukingoni mwa kisima kwa mkono wake na hali ya kuwa yeye hayapati milele kwa mkono wake sasa vipi yatafika mdomoni mwake.<sup>3</sup>

Na Mujahid amesema,

كَبَسِطَ كَفِّهِ

**“...ni kama mwenye kunyoosha viganja vyake...”**

<sup>1</sup> At-Tabari: 16:398.

<sup>2</sup> Kama hapo juu.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:400.

Anayaita maji kwa ulimi wake na anayatolea ishara wala hayamwendei milele.<sup>1</sup> Na maana ya maneno hayo, ni kwamba yule ambaye anaukunjua mkono wake kuuelekeza kwenye maji, ima atakuwa ni mwenye kuyakamata na ima atakuwa ni mwenye kuyashika kwa umbali kama ambavyo yeye hanufaiki na maji ambayo hayakufika mdomoni mwake. Mdomo ambao ameufanya kuwa ni mahali pa kunywea kwake hivyo hivyo hawa washirikina ambao wanamuabudu pamoja na Allah تعالى mwingine asiyekuwa Yeye, hawatanufaika na waungu hao milele duniani wala huko akhera.

Na kwa sababu hiyo Amesema:

وَمَا دُعَاءُ الْكَافِرِينَ إِلَّا فِي ضَلَالٍ

*“Na maombi ya makafiri hayako ila katika upotovu.”*

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَظِلَّلُهُمْ بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿١٥﴾

**15. Na viliomo mbinguni na katika ardhi vinamsujudia Mwenyezi Mungu tu vikitaka visitake. Na pia vivuli vyao asubuhi na jioni.**

**Kila Kitu Kinamsujudia Allah تعالى**

Allah تعالى Anaeleza Kuhusu Utukufu Wake na Ufalme Wake Ambaye Umekiteza nguvu kila kitu, na kimenyenyekeza kila kitu Kwake. Na kwa sababu hiyo kinamsujudia kila kitu kwa utiifu hasa waumini na kwa lazima makafiri.

وَظِلَّلُهُمْ بِالْغُدُوِّ

*“Na pia vivuli vyao asubuhi...”*

Kwa maana: Wakati wa asubuhi.

وَالْآصَالِ

*“... na jioni.”*

Kwa maana: Mwisho wa mchana. Kama Alivyosema Allah تعالى:

<sup>1</sup> Tabari 16:400.

أَوَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِنْ شَيْءٍ يَتَفَيَّؤُا ظِلَالُهُ عَنِ الَّيْمِينِ وَالشَّمَائِلِ سُجَّدًا لِلَّهِ وَهُمْ

دَاخِرُونَ ﴿٤٨﴾

**“Je! Hawavioni vitu Alivyo viumba Mwenyezi Mungu - vivuli vyao vinaelekea kushotoni na kuliani, kumsujudia Mwenyezi Mungu na vikinyenyekea? (16:48).**

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ قُلِ اللَّهُ ۗ قُلْ أَفَاتَّخَذْتُمْ مِنْ دُونِهِ أَوْلِيَاءَ لَا يَمْلِكُونَ

لأنفُسِهِمْ نَفْعًا وَلَا ضَرًّا ۗ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ أَمْ هَلْ تَسْتَوِي الظُّلُمَاتُ

وَالنُّورُ ۗ أَمْ جَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ خَلَقُوا كَخَلْقِهِ فَتَشَبَهَ الْخَلْقَ عَلَيْهِمْ ۗ قُلِ اللَّهُ خَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ

وَهُوَ الْوَاحِدُ الْقَهَّارُ ﴿٤٩﴾

**16. Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu na ardhi? Sema: Mwenyezi Mungu. Sema: Basi je, mnawafanya wenginewe badala Yake kuwa ni walinzi, nao hawajifai wenyewe kwa jema wala baya? Sema: Hebu kipofu na mwenye kuona huwa sawa? Au hebu huwa sawa giza na mwangaza? Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika walio umba kama Alivyo umba Yeye, na viumbe hivyo vikawadanganyikia? Sema: Mwenyezi Mungu Ndiye Muumba wa kila kitu. Na Yeye ni Mmoja Mwenye Kushinda!**

### Kuthibitisha Tawhidi ya Allah تعالى

Allah تعالى Anathibitisha kwamba hapana wa kuabudiwa isipokuwa Yeye, kwa sababu wao wanakiri kwamba Allah تعالى Ndiye aliyumba mbingu na ardhi, na Ndiye Mlezi Wake na Mpangaji wa mambo Yake na wao pamoja na hivyo wanawafanya kinyume cha Allah تعالى, waungu wengine ambao wanawaabudu, hali ya kuwa waungu hao hawazimiliki nafsi zao wala wale wanaowaabudu, kwa njia ya manufaa wala madhara. Maana yake: Hayapatikani kwao manufaa yoyote wala hawawaondolei madhara yoyote. Jee analingana sawa na yule anayewaabudu waungu hao pamoja na Allah تعالى na yule anayemuabudu Allah تعالى Pekee Asiyekuwa na mshirika, hivyo yeye hayupo katika nuru ya Mola wake Mlezi? Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Anasema,

قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الْأَعْمَىٰ وَالْبَصِيرُ أَمْ هَلْ تَسْتَوِي الظُّلُمَاتُ وَالنُّورُ ۗ أَمْ جَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ خَلَقُوا كَخَلْقِهِمْ فَتَشَبَّهُ الْخَلْقُ عَلَيْهِمْ ۗ

**“Sema: Hebu kipofu na mwenye kuona huwa sawa? Au hebu huwa sawa giza na mwangaza? Au wamemfanyia Mwenyezi Mungu washirika walioumba kama Alivyoumba Yeye, na viumbe hivyo vikawadanganyikia?”**

Maana yake: Hivi wamefanya hawa washirikina pamoja na Allah تعالى waungu wengine wanalingana na Allah تعالى na wanafanana Naye katika kuumba, kwa hiyo wakawa wameumba kama Kuumba Kwake. Kwa hiyo likatatiza umbile juu yao wakawa hawajui kwamba viumbe hivyo vimeumbwa kama wao? Maana yake: Mambo hayako hivyo, kwani Allah تعالى hafanani Naye kitu chochote na hakilingani Naye na Hana mwenza, wala anayelingana Naye, Hana msaidizi na wala Hana mtoto wala Hana mke. Ametukuka Allah تعالى na huku Kutukuka Kukubwa sana, hakika si vingine washirikina hawa wamemuabudu Allah تعالى pamoja na miungu mingine hali ya kuwa wao wanakiri kwamba miungu hiyo ni viumbe Wake na waja Wake, kama walivyokuwa wanasema katika kuitikia kwao *Talbiyah*.

Tunakuitikia Wewe hali ya kuwa huna mshirika, isipokuwa mshirika ambaye yeye ni milki yake Unammiliki na vile anavyovimiliki, na kama alivyoeleza Allah تعالى kuhusu wao Katika Kauli Yake:

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

**“Sisi hatuwaabudu ila wapate kutujongeza tu kumkaribia Mwenyezi Mungu.” (39:3)**

Allah تعالى Akakanusha hilo kwao ilipokuwa wameliitakidi hilo, na Yeye Allah تعالى Haombi mtu yeyote mbele Yake isipokuwa kwa Amri Yake:

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ ۗ

**“Wala uombezi mbele yake hautafaa kitu, isipokuwa kwa Aliyempa idhini.” (34:23)**

وَكَم مِّن مَّلَكٍ فِي السَّمَوَاتِ

**“Na wako Malaika wangapi mbinguni” (53:26) na**

إِن كُنتُمْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَاكِ الرَّحْمَنُ عَبْدًا ﴿٣٣﴾ لَقَدْ أَحْصَيْنَاهُمْ وَعَدَّهُمْ  
عَدًّا ﴿٣٤﴾ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٣٥﴾

**“Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Arrahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao Atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.” (19:93-95)**

Watakapokuwa wote ni waja kwanini wanaabudu wengine, baadhi yao kuwaabudu pasi na dalili wala hoja yoyote? Bali ni kutokana na maoni na uzushi. Kisha Amewapeleka Mitume Wake kutoka wa kwanza wao mpaka wa mwisho wao wakiwa wanawakemea hayo na wanawakataza kumuabudu asiyekuwa Allah تعالى. Wakawakadhibisha, likathibiti juu yao tamko la adhabu bila ya shaka.

وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤١﴾

**“Na Mola wako Mlezi hamdhulumu yeyote.” (18:49).**

\* \* \*

أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَالَتْ أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا فَاحْتَمَلَ  
 السَّيْلُ زَبَدًا رَابِيًا ۖ وَمِمَّا يُوقِدُونَ عَلَيْهِ فِي النَّارِ ابْتِغَاءَ  
 حُلِيِّهِ أَوْ مَتَعِ زَيْدٌ مِثْلَهُ ۗ كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْحَقَّ  
 وَالْبَاطِلَ ۗ فَأَمَّا الزُّبَدُ فَيَذْهَبُ جُفَاءً ۗ وَأَمَّا مَا يَنْفَعُ النَّاسَ  
 فَيَمْكُثُ فِي الْأَرْضِ ۗ كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ ﴿١٧﴾  
 لِلَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمُ الْحَسَنَىٰ ۗ وَالَّذِينَ لَمْ يَسْتَجِيبُوا  
 لَهُ لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ  
 لَافْتَدَوْا بِهِ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ السُّوءُ الْحِسَابِ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ  
 وَيُنْسَىٰ إِلَهُادُ ﴿١٨﴾ \* أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّ مَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ مِنَ  
 رَبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ ۗ إِنَّمَا يَنْذَرُكُمُ أَوْلُوا الْأَلْبَابِ ﴿١٩﴾  
 الَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَلَا يَنْقُضُونَ الْعِمَّةَ ﴿٢٠﴾ وَالَّذِينَ  
 يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ  
 وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ﴿٢١﴾ وَالَّذِينَ صَبَرُوا ابْتِغَاءَ وَجْهِ  
 رَبِّهِمْ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً  
 وَدَبَّرُوا بِأَلْحَسَنَةِ السَّيِّئَةِ أُولَٰئِكَ هُمُ عُقَى الدَّارِ ﴿٢٢﴾  
 جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ  
 وَذُرِّيَّاتِهِمْ ۗ وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾  
 سَلَّمَ عَلَيْهِمْ بِمَا صَبَرُوا ۗ فَبِعَمِّ عُقَى الدَّارِ ﴿٢٤﴾

أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَالَتْ  
 أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا فَاحْتَمَلَ السَّيْلُ زَبَدًا  
 رَابِيًا ۖ وَمِمَّا يُوقِدُونَ عَلَيْهِ فِي النَّارِ  
 ابْتِغَاءَ حُلِيِّهِ أَوْ مَتَعِ زَيْدٌ مِثْلَهُ ۗ  
 كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْحَقَّ وَالْبَاطِلَ ۗ  
 فَأَمَّا الزُّبَدُ فَيَذْهَبُ جُفَاءً ۗ وَأَمَّا مَا  
 يَنْفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُثُ فِي الْأَرْضِ ۗ  
 كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ ﴿١٧﴾

**17. Ameteremsha maji kutoka mbinguni. Na mabonde yakamiminika maji kwa kadiri yake. Na mafuriko yakachukua mapovu yaliyokusanyika juu yake. Na kutokana na wanavyoyayusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo hutokea povu vile vile. Namna hivyo Mwenyezi Mungu ndivyo Anavyopiga mifano ya Haki na batili. Basi lile povu linapita kama takataka tu basi. Ama kinachowafaa watu hubakia kwenye**

**ardhi. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyopiga mifano.**

### Mifano Miwili ya Kubaki Haki na Kutoweka Batili

Aya hii Tukufu imekusanya mifano miwili iliyopigwa kwa ajili ya haki katika kuthibiti kwake na kubaki kwake, na batili katika kumalizika kwake na kutoweka kwake. Allah تعالى Amesema,

أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً

**“Ameteremsha maji kutoka mbinguni.”**

Maana yake Mvua.

فَسَأَلَتْ أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا

**“Na mabonde yakamiminika maji kwa kadiri yake.”**

Maana yake: Lilichukua kila jangwa sehemu yake, jangwa kubwa limesheheni maji mengi, na dogo limesheheni kwa kiasi chake.

Hiyo ni ishara ya nyoyo na kutofautiana kwake, kuna ambazo zina elimu nyingi na kuna ambazo hazikubeba elimu nyingi, bali hupatwa na dhiki hizo elimu.

فَأَحْتَمَلَ السَّيْلُ زَبَدًا رَابِيًا

**“Na mafuriko yakachukua mapovu yaliyokusanyika juu yake.”**

Maana yake: Mapovu yakaja juu ya uso wa maji ambayo yametirizika kutoka majangwani. Haya povu ni mfano. Na Kauli Yake

وَمِمَّا يُوقِدُونَ عَلَيْهِ فِي النَّارِ ابْتِغَاءَ حُلِيٍّ أَوْ مَتَعٍ زَبَدٌ مِّثْلَهُ

**“Na kutokana na wanavyoyayusha katika moto kwa kutaka mapambo au vyombo hutokea povu vile vile.”**

Huu ndiyo mfano wa pili nao ni kile ambacho kinafuliwa katika moto miongoni mwa dhahabu au fedha kwa kutaka kipambo. Maana yake: Ili kifanywe kipambo cha shaba au chuma, hufanyia kuwa kitu cha kutumiwa kwani hicho hukikalia juu povu.

كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْحَقَّ وَالْبَاطِلَ

**“Namna hivyo Mwenyezi Mungu ndivyo Anavyopiga mifano ya Haki na batili.”**

Maana yake: Vitakapokusanyika viwili hivyo, hapana kuthibiti kwa batili na haina kudumu kama ambavyo povu halithibiti pamoja na maji na wala pamoja na dhahabu na fedha. Na mfano wao katika vile ambavyo vinafuliwa katika moto bali huondoka na humalizika. Na kwa sababu hiyo Amesema:

فَأَمَّا الزُّبْدُ فَيَذْهَبُ جُفَاءً<sup>ط</sup>

***“Basi lile povu linapita kama takataka tu basi.”***

Maana yake: Hapana manufaa kwalo bali hutawanyika na husambaratika na huenda katika pambizo mbili za jangwa na huambatana na miti na hulipeperusha upepo. Na hivyo hivyo uchafu wa fedha, dhahabu, chuma na shaba huondoka na hakirudi kutokana nayo kitu chochote, hakubakii kitu chochote isipokuwa maji na dhahabu. Hiyo na mfano wake, hubaki chenye kufaa.

Kwa sababu hiyo Amesema:

وَأَمَّا مَا يَنْفَعُ النَّاسَ فَيَمُكُّ فِي الْأَرْضِ<sup>ط</sup> كَذَلِكَ يَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ

***“Ama kinachowafaa watu hubakia kwenye ardhi. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyopiga mifano.”***

Kama Alivyosema Katika Aya Nyingine,

وَتِلْكَ الْأَمْثَلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ<sup>ط</sup> وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٤٣﴾

***“Na hiyo ni mifano Tunawapigia watu, na hawaifahamu ila wenye ilimu.” (29:43)***

Baadhi ya wanawazuoni waliotangulia wanasema: Nilikuwa ninapousoma mfano katika Qur’ani nikawa sikuufahamu hulia juu ya nafsi yangu kwa sababu Allah تعالى Anasema:

وَمَا يَعْقِلُهَا إِلَّا الْعَالِمُونَ ﴿٤٣﴾

***“...na hawaifahamu ila wenye ilimu.” (29:43)***

Amesema Ali bin Abii Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake Allah تعالى:



أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَالَتْ أَوْدِيَةٌ بِقَدَرِهَا

***“Ameteremsha maji kutoka mbinguni. Na mabonde yakamiminika maji kwa kadiri yake.”***

Huu ni mfano Ameupiga Allah تعالى, zimechukua kutokana na mfano huo nyoyo kwa kiasi cha yakini na shaka yake, haifai kuwa na shaka. Allah تعالى huwanufaisha watu wake kwa yakini.

Hayo ndiyo madhumuni ya Kauli Yake.

فَأَمَّا الزَّبَدُ

***“Basi lile povu...”*** Nalo ni shaka,

فَيَذَهِبُ جُفَاءً<sup>ط</sup> وَأَمَّا مَا يَنْفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُتُ فِي الْأَرْضِ<sup>ع</sup>

***“...linapita kama takataka tu basi. Ama kinachowafaa watu hubakia kwenye ardhi. ”***

Nacho ni yakini na kama ambavyo huwekwa kipambo motoni huchukuliwa usafi wake na huachwa uchafu wake katika moto. Ni kama hivyo Anakubali Allah تعالى Yakini na Anaacha shaka.<sup>1</sup>

### **Qur'an na Sunna Imesheheni Mifano Mingi ya Maji na Moto**

Kwa hakika Allah تعالى Kutakata ni Kwake na Ametukuka, mwanzoni mwa Surat Al-Baqarah Amepiga mifano miwili kuhusu wanafiki: wa moto na wa maji: na mifano hiyo ni Kauli Yake:

مَثَلُهُمْ كَمَثَلِ الَّذِي اسْتَوْقَدَ نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهُ

***“Mfano wao ni kama mfano wa aliyekoka moto, na ulipotanda mwangaza wake kote kote,...”*** (2:17). Kisha Akasema:

أَوْ كَصَيْبٍ مِنَ السَّمَاءِ فِيهِ ظُلُمَاتٌ وَرَعْدٌ وَنَرَقٌ

***“Au ni kama mvua kubwa itokayo mbinguni, ina giza na radi na umeme:...”*** (2:19)

<sup>1</sup> Tabari 16:410.

Na kama hivyo Amewapigia mifano makafiri katika *Surat Annur*, mifano miwili mmoja ni katika Kauli Yake:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُوهُمْ كَسَرَابٍ

**“Na waliokufuru vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi),...” (24:39)**

Na mangati hakika hapana jambo jingine yanapatikana katika joto kali na kwa sababu hiyo imekuja katika Sahihi ya Bukhari na Muslim,

«قِيلَ لِلْيَهُودِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ: فَمَا تُرِيدُونَ؟ فَيَقُولُونَ: أَيُّ رَبَّنَا عَطَيْنَا فَاسْتِنَا. فَيَقَالُ: أَلَا تَرِيدُونَ؟ فَيَرِدُونَ النَّارَ فَإِذَا هِيَ كَسَرَابٍ يَخْطِمُ بَعْضُهَا بَعْضًا»

*“Patasemwa kuambiwa Mayahudi Siku ya Kiyama mnataka nini? Watasema: ‘Ee Bwana wetu tumepatwa na kiu tunaomba Utupe maji’ wataambiwa, ‘hivi hamvuki?’ Watauvuka moto ghafla watauona huo moto kama mangati, yanayavunja baadhi yake kuvunja mengine.”<sup>1</sup>*

Kisha Amesema Allah تعالى katika mfano mwingine.

أَوْ كَطَلَمْتٍ فِي بَحْرِ لَيْجٍ

**“Au ni kama giza katika bahari kuu,...” (24:40)**

Katika Sahihi Mbili kumeandikwa kuwa Abu Musa Al-Ashary رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ مَثَلَ مَا بَعَثَنِي اللَّهُ بِهِ مِنَ الْهُدَى وَالْعِلْمِ، كَمَثَلِ غَيْثٍ أَصَابَ أَرْضًا، فَكَانَ مِنْهَا طَائِفَةٌ قَبِلَتِ الْمَاءَ فَأَنْبَتَتِ الْكَلَّاءَ وَالْعُشْبَ الْكَثِيرَ، وَكَانَتْ مِنْهَا أَجَادِبٌ أُمْسَكَتِ الْمَاءَ، فَفَنَعَ اللَّهُ بِهَا النَّاسَ، فَشَرِبُوا، وَرَعَوْا، وَسَقَوْا، وَزَرَعُوا، وَأَصَابَتْ طَائِفَةٌ مِنْهَا أُخْرَى، إِنَّمَا هِيَ قَيْعَانٌ لَا تُمْسِكُ مَاءً وَلَا تُنْبِتُ كَلًّا، فَذَلِكَ مَثَلُ مَنْ قَفَّ فِي دِينِ اللَّهِ وَنَفَعَهُ اللَّهُ بِمَا بَعَثَنِي وَنَفَعَ بِهِ، فَعَلِمَ وَعَلَّمَ، وَمَثَلُ مَنْ لَمْ يَرْفَعْ بِذَلِكَ رَأْسًا وَلَمْ يَقْبَلْ هُدَى اللَّهِ الَّذِي أُرْسِلْتُ بِهِ»

<sup>1</sup> *Fat’hul Al-Bari* 8:98, *Muslim* 4:168.

*“Kwa hakika mfano wa kile ambacho Amenipeleka mimi Mwenyezi Mungu kwa hicho miongoni mwa uongofu na elimu, ni kama mfano wa mvua iliyoipata ardhi. Ikawa katika hiyo ardhi sehemu inayohifadhi maji, ikaotesha majani na nyasi nyingi; na ikawa katika ardhi hiyo sehemu ngumu zilizoyazuia maji, akawanufaisha Mwenyezi Mungu kwa maeneo hayo watu, wakanywa na wakawachunga wanyama na wakawanyweshwa na wakalima. Ikayapata katika hiyo ardhi maeneo mengine, hakika maeneo hayo ni majangwa hayazui maji na hayaoteshi majani. Huo ni mfano wa mtu ambaye amefahamu katika Dini ya Mwenyezi Mungu na Akamnufaisha yeye Mwenyezi Mungu kutokana na kile ambacho Amenipeleka Mwenyezi Mungu kwacho. Akaelewa na akawaeleweshwa watu na pia huu ni mfano wa yule ambaye hakunyanyua kwa jambo hilo kichwa na hakuukubali uongofu wa Mwenyezi Mungu ambao nimepelekwa kwao.”<sup>1</sup>*

Huu ni mfano wa maji. Na amesema katika hadithi nyingine aliyoiandika Imam Ahmad kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ kwamba amesema:

«مَثَلِي وَمَثَلِكُمْ كَمَثَلِ رَجُلٍ اسْتَوْدَدَ نَارًا فَلَمَّا أَضَاءَتْ مَا حَوْلَهُ، جَعَلَ الْفَرَاشُ وَهَيْهِ الدَّوَابُّ الَّتِي يَقَعْنَ فِي النَّارِ يَقَعْنَ فِيهَا، وَجَعَلَ يَحْجِرُهُنَّ وَيَغْلِبُنَّهُ فَيَفْتَحِمْنَ فِيهَا - قَالَ -: فَذَلِكُمْ مَثَلِي وَمَثَلِكُمْ، أَنَا آخِذٌ بِحُجْرِكُمْ عَنِ النَّارِ، هَلُمَّ عَنِ النَّارِ، فَتَغْلِبُونِي، فَتَفْتَحِمُونِ فِيهَا»

*“Mfano wangu na mfano wenu ni kama mfano wa mtu ambaye ameuwasha moto, ulipoviangazia vilivyo pambizoni mwake wakawa vipepeo na wadudu wale ambao hutumbukia motoni wakawa wanatumbukia ndani yake na akawa anawazuia na wanamshinda, wakawa wanatumbukia ndani ya moto. Huo ni mfano wangu na mfano wenu, mimi ninaikamata mikando iliyo viunoni mwenu nikiwazuia na moto, nikiwaambia njooni huku muepukane na moto mnanishinda (mnaniponyoka) mnatumbukia ndani ya moto.”<sup>2</sup>*

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 1:211, Muslim 4:1788.

<sup>2</sup> Ahmad 2:312.

Pia Sahihi Mbili zimeandika Hadithi hii.<sup>1</sup> Huu ni mfano wa moto.

لِلَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ الْحُسْنَىٰ وَالَّذِينَ لَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُ لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ  
جَمِيعًا وَمِثْلَهُ مَعَهُ لَافْتَدَوْا بِهِمْ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ السُّوءُ الْحِسَابِ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٧﴾

**18. Waliomuitikia Mola wao Mlezi watapata wema. Na wasio  
muitikia, hata wangelikuwa navyo vyote viliomo katika ardhi na  
mfano wa hivyo, bila ya shaka wangelivitoa kujikombolea! Hao  
watapata hisabu mbaya kabisa, na makao yao ni Jahannamu. Na  
hapo ni pahala pabaya mno!**

### Malipo ya Wema na Waovu

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu mwisho wa watu wema na watu waovu:

لِلَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِرَبِّهِمْ

**“Waliomuitikia Mola wao Mlezi...”**

Wamemtii Allah تعالیٰ na Mtume wake na wakanyenyekea kwenye maamrisha  
Yake na wakazisadikisha khabari Zake zilizopita na zinazokuja. Wanastahiki  
hao,

الْحُسْنَىٰ

**“...watapata wema.”**

Maana yake: Malipo mazuri kama Alivyosema Allah تعالیٰ:

قَالَ أَمَّا مَنْ ظَلَمَ فَسَوْفَ نُعَذِّبُهُ ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ رَبِّهِ فَيُعَذِّبُهُ عَذَابًا نَّكَرًا ﴿١٨﴾ وَأَمَّا مَنْ  
ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَهُ جَزَاءُ الْحُسْنَىٰ ۖ وَسَنَقُولُ لَهُ مِنْ أَمْرِنَا يُسْرًا ﴿١٩﴾

**“Akasema: Ama aliyedhulumu basi Tutamuadhibu, na kisha  
atarudishwa kwa Mola wake Mlezi Amuadhibu adhabu  
isiyojulikana. Na ama aliyeamini na akatenda mema basi atapata  
malipo mazuri. Nasi Tutamuambia lilio jepesi katika Amri Yetu.”  
(18:87-88)**

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 11:323, Muslim 4:1790.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا أَحْسَنَىٰ وَزِيَادَةً

**“Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi.” (10:26)**

Kisha Akasema,

وَالَّذِينَ لَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُ

**“Na wasiomuitikia,...”** Hawakumtii Allah تعالى,

لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا

**“...hata wangelikuwa navyo vyote viliomo katika ardhi...”**

Maana yake: Katika nyumba ya akhera watakapoulizwa katika *Naqir*<sup>1</sup> na *Qitmir*,<sup>2</sup> makubwa na madogo. Kwa hakika, watakaoulizwa kwa kina katika Siku ya Hukumu, ataadhibiwa. Kisha, Allah تعالى Akasema,

أُولَئِكَ هُمْ سُوءَ الْحِسَابِ

**“Hao watapata hisabu mbaya kabisa,...”**

Huko Akhera wataulizwa juu ya matendo yanayolingana kwa udogo na tundu ya kokwa ya tende au ganda lake, kikubwa na kidogo. Na atakayeulizwa sana kuhusu hesabu yake ataadhibiwa. Na kwa sababu hiyo Amesema:

وَمَا أُولَئِكَ بِمَنِّي وَبِئْسَ الْإِلَهَادُ

**“...na makao yao ni Jahannamu. Na hapo ni pahala pabaya mno!”**

أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَىٰ ۚ إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٩﴾

**19. Je! Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu? Wenye akili ndio wanaozingatia.**

<sup>1</sup> Doa dogo nyuma ya kokwa ya tende.

<sup>2</sup> Utando mwembamba unaozunguka kokwa ya tende.

## Halingani Muumini na Kafiri

Allah تعالى Anasema Halingani sawa anayejua katika watu kwamba yale

أُنزِلَ إِلَيْكَ

“...yaliyoteremshwa kwako ...” Ee Muhammad ﷺ,

مِنْ رَبِّكَ

“...kutoka kwa Mola wako Mlezi...”

Ndiyo haki isiyo na shaka ndani yake wala hamna utata au kutofautiana ndani yake, bali yote hayo ni kweli, husadikisha baadhi yake baadhi nyingine, hakuna mgongano ndani yake. Kwa hiyo habari zake zote ni za ukweli na maamrishi yake na makatazo yake ni ya uadilifu. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا

**“Na yametimia maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu.”**  
(6:115)

Maana yake: Ukweli katika kutoa habari na uadilifu katika kutaka. Kwa hiyo halingani sawa mwenye kuthibitisha ukweli wa yale ambayo umekuja nayo, Ee Muhammad ﷺ na yule ambaye ni kipofu, asiyeongoka kwenye kheri yoyote na wala haifahamu. Hata kama angeifahamu asingeinyenyekea wala kuisadikisha na kuifuata. Kama ilivyo Kauli Yake Allah تعالى:

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ الْفَائِزُونَ

**“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.”** (59:20)

Allah تعالى Amesema katika Aya hii Tukufu,

أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَى

**“Je! Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu?”**

Maana yake: Hivi huyo ni kama huyu, hapana usawa. Na Kauli Yake:

إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ

*“Wenye akili ndio wanaozingatia,...”*

Maana yake: Hakika hapana jambo jingine wanaonyeka na kupata mazingatio na kuelewa na wanaelewa wenye akili zilizosalimika, zilizo nzima tu. Namuomba Allah تعالی Atufanye miongoni mwao.

الَّذِينَ يُوفُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَلَا يَنْقُضُونَ الْمِيثَاقَ ﴿١٧﴾ وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ  
يُوصَلَ وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ وَيَخَافُونَ سُوءَ الْحِسَابِ ﴿١٨﴾ وَالَّذِينَ صَبَرُوا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ  
وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً وَيَدْرُءُونَ بِالْحَسَنَةِ السَّيِّئَةَ أُولَئِكَ  
هُمْ عُقْبَى الدَّارِ ﴿١٩﴾ جَنَّتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ  
وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢٠﴾ سَلَّمَ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَبِعَمِّ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢١﴾

**20. Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wala hawavunji maagano.**

**21. Na wale ambao huyaunga Aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanaikhofu hisabu mbaya.**

**22. Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao Mlezi, na wakashika Sala, na wakatoa, kwa siri na kwa uwazi, katika Tulivyo wapa; na wakayaondoa maovu kwa wema. Hao ndio watakaopata malipo ya Nyumba ya Akhera.**

**23. Nayo ni Bustani za milele, wataziingia wao na walio wema miongoni mwa baba zao, na wake zao, na vizazi vyao. Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango.**

**24. (Wakiwaambia) Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyosubiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera.**

### Sifa za Watu Wema Zitakazowaingiza Peponi

Allah تعالى Anasema kuwa wenye sifa hizi bora wana mwisho mzuri na kupata nyumba ya neema. Na huo ni mwisho mwema na kunusurika katika dunia na akhera.

الَّذِينَ يُوفُونَ بَعْدَهُ وَاللَّهُ وَلَا يَنْقُضُونَ الْمِيثَاقَ ﴿١٧﴾

***“Wale ambao wanatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu, wala hawavunji maagano.”***

Hawakuwa kama wanafiki ambao anapoahidi mmoja wao anavunja ahadi, akigombana anafanya uovu, akizungumza hudanganya na akiaminiwa hufanya khiana.

وَالَّذِينَ يَصِلُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ

***“Na wale ambao huyaunga Aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe,...”***

Miongoni mwa kuunga udugu na kuwafanyia wema hao ndugu na pia kuwafanyia wema mafukara na wenye haja, na kufanya wema.

وَيَخْشَوْنَ رَبَّهُمْ

***“...na wanamkhofu Mola Wao Mlezi.”***

Maana yake: Katika yale wanayoyatenda na yale wanayoyaacha katika matendo, wanamchungu Allah تعالى katika mambo hayo na wanaogopa ubaya wa hesabu katika Akhera. Na kwa ajili hiyo, Amewaamrisha usawa na unyoofu katika harakati zao na matulivu yao na hali zao zote zinazowahusu wao tu na zile zinazowahusu watu wengine.

وَالَّذِينَ صَبَرُوا أَبْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِمْ

***“Na ambao husubiri kwa kutaka radhi ya Mola wao Mlezi,”***

Maana yake: Wamesubiri kwa kuepukana na mambo yaliyoharamishwa na madhambi, wakaziepusha nafsi zao na mambo hayo kwa ajili ya Allah تعالى, kwa kutaka radhi Yake na malipo Yake.

وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ

***“...na wakashika Sala,”***



Kwa mipaka yake na nyakati zake, rukuu zake, sijida zake na unyenyekevu wake, juu ya utaratibu wa kisheria unaokubalika.

وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ

**“...na wakatoa katika Tulivyowapa:...”**

Maana yake: Kwa wale ambao hupasa juu yao kuwapa, miongoni mwa wake, jamaa na watu kando miongoni mwa mafukara na wenye haja na maskini.

سِرًّا وَعَلَانِيَةً

**“...kwa siri na kwa uwazi,...”**

Maana yake: Katika siri na kudhihirisha, haikuwazua wao na kuyafanya hayo hali yoyote ile, nyakati za usiku na za mchana.

وَيَذَرُهُمْ بِالْحَسَنَةِ الْسَّيِّئَةِ

**“...na wakayaondoa maovu kwa wema.”**

Maana yake: Kwa hiyo pindi anapowaudhi wao mtu yeyote, wanamkabili kwa wema, kwa kusubiri, kwa uvumilifu na kwa kusamehe na kupuuza. Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

أَدْفَعْ بِأَلْتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿١٧﴾ وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَمَا يُلْقِنَهَا إِلَّا ذُو حِظٍّ عَظِيمٍ ﴿١٨﴾

**“Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu. Lakini hawapewi wema huu ila wanaosubiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa.” (41:34-35).**

Kwa ajili hiyo ameelezea kuhusu hawa watu wema wenye sifa hizi nzuri kwamba wana mafikio mazuri katika nyumba ya akhera. Kisha akalifasiri hilo kwa Kauli Yake,

جَنَّاتُ عَدْنٍ

**“Nayo ni Bustani za milele,...”** Na neno *Aden* maana yake ni ukazi. Maana katika bustani za ukazi watakaa milele humo. Na Kauli Yake:

وَمَنْ صَلَحَ مِنْ آبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّتِهِمْ<sup>ط</sup>

**“...na walio wema miongoni mwa baba zao, na wake zao, na vizazi vyao.”**

Allah تعالی Atawakusanya pamoja na wapenzi wao katika bustani hizo miongoni mwa wazazi wao na wake na watoto katika waliofaa kuingia Peponi, katika waumini ili watulize macho yao, kwa hao wapenzi, kiasi kwamba, itanyanyuliwa daraja ya aliye chini kupelekwa ya aliye juu. Kwa neema za Allah تعالی na hisani Zake pasi na kumpunguzia daraja yake ya juu.

Kama Alivyosema Allah تعالی:

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتِهِمْ

**“Na walioamini na dhuriya wao wakawafuata kwa Imani Tutawakutanisha nao dhuriya wao,...” (52:21).**

Na Kauli Yake تعالی:

وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢١﴾ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٢﴾

**“Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango. (Wakiwaambia) Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyosubiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera.”**

Maana yake: Wataingia juu yao Malaika kutokea hapa na hapa ili kuwapongeza kwa kuingia kwao peponi. Wakati wa kuingia kwao peponi watawaendea malaika na kuwasalimia, hali ya kuwapongeza kwa waliyoyapata kutoka kwa Allah تعالی kama vile kusogezwa na kuneemeshwa na kukaa katika nyumba ya amani, katika ujirani na watu wa kweli na Manabii na Mitume walio Watukufu. Na amepokea Imam Ahmad رحمه الله تعالی, kutoka kwa Abdillahi bin Amri bin Al-Asi رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba yeye amesema

«هَلْ تَذَرُونَ أَوَّلَ مَنْ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مِنْ خَلْقِ اللَّهِ؟»

**“Je mnamjua wa kwanza kuingia peponi katika viumbe wa Allah?”**

Wakasema Allah تعالی na Mjumbe wake wanajua zaidi akasema

«أَوَّلُ مَنْ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مِنْ خَلْقِ اللَّهِ الْفُقَرَاءُ الْمُهَاجِرُونَ الَّذِينَ تُسَدُّ بِهِمُ الثُّغُورُ، وَتَقَى بِهِمُ الْمَكَارَهُ، وَيَمُوتُ أَحَدُهُمْ وَحَاجَتُهُ فِي صَدْرِهِ، لَا يَسْتَطِيعُ لَهَا قَضَاءً، فَيَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى لِمَنْ يَشَاءُ مِنْ مَلَائِكَتِهِ: ائْتُوهُمْ فَحَيِّوهُمْ، فَقَالُوا الْمَلَائِكَةُ: نَحْنُ سُكَّانُ سَمَاوَاتِكُمْ، وَخَيْرَتُكَ مِنْ خَلْقِكَ، أَفَتَأْمُرُنَا أَنْ نَأْتِيَ هَؤُلَاءِ وَنُسَلِّمَ عَلَيْهِمْ؟ فَيَقُولُ: إِنَّهُمْ كَانُوا عِبَادًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا، وَتُسَدُّ بِهِمُ الثُّغُورُ، وَتَقَى بِهِمُ الْمَكَارَهُ، وَيَمُوتُ أَحَدُهُمْ وَحَاجَتُهُ فِي صَدْرِهِ لَا يَسْتَطِيعُ لَهَا قَضَاءً - قَالَ - : فَاتَّيَبَهُمُ الْمَلَائِكَةُ عِنْدَ ذَلِكَ فَيَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ»

*“Watu wa kwanza kuingia peponi katika viumbe wa Mwenyezi Mungu ni mafukara waliohama ambao hufanywa wao walinzi katika ngome na kinga dhidi ya shari zinazoogopewa kutoka kwa maadui. Na anakufa mmoja wao na hali ya kuwa shida yake imo kifuani mwake, hawezi kuikidhi. Kisha Mwenyezi Mungu Atamuambia Amtakaye katika malaika Wake, ‘Nendeni mkawasalimie.’ Watasema malaika, ‘Sisi ni wakazi wa mbingu yako, na wabora wa viumbe wako hivi unatuamrisha tuwaendee hawa na tuwasalimie?’ Atasema: ‘Hakika wao walikuwa waja wakiniabudu, hawanishirikishi na mimi kitu chochote; hufanywa walinzi sehemu za hatari na huzikinga na mambo yenye kuchukiza, na anakufa mmoja wao na hali ya kuwa shida yake iko kifuani kwake, hawezi kuikidhi.’ Amesema, ‘watawaendea wao malaika wakati huo na wataingia kwao, katika kila mlango.”*

Wakisema:

سَلِّمٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿١٦٨﴾

***“Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyosubiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera.”<sup>1</sup>***

\* \* \*

<sup>1</sup> Ahmad 2:168.

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ  
 مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ ۗ أُولَٰئِكَ  
 لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٢٥﴾ اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ  
 يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ وَفَرِحُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا  
 فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَاعٌ ﴿٢٦﴾ وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ  
 عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ ۗ قُلْ إِنَّمَا اللَّهُ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي  
 إِلَيْهِ مَنْ أُنَابَ ﴿٢٧﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ  
 اللَّهِ ۗ أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾ الَّذِينَ  
 ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ طُوبَىٰ لَهُمْ وَحَسُنَ مَا فِي مَقَابِرِهِمْ ﴿٢٩﴾  
 كَذَٰلِكَ أَرْسَلْنَاكَ فِي أُمَّةٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهَا أُمَمٌ لَتَتْلُوَا  
 عَلَيْهِمُ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ ۗ قُلْ هُوَ  
 رَبِّي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ مَتَابِ ﴿٣٠﴾ وَلَوْ  
 أَنَّ قُرْءَانَ سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ أَوْ قُطِعَتْ بِهِ الْأَرْضُ أَوْ كُفِّرَ بِهِ  
 أَلْمُوتَىٰ ۗ بَلْ لِلَّهِ الْأَمْرُ جَمِيعًا ۗ أَفَلَمْ يَأْتِصِلِ الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 أَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَهَدَى النَّاسَ جَمِيعًا ۗ وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا تُصِيبُهُمْ بِمَا صَنَعُوا قَارِعَةٌ أَوْ تَحُلُّ قَرِيبًا مِّن دَارِهِمْ  
 حَتَّىٰ يَأْتِيَ وَعْدَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُخْلِفُ الْعَاهِدَ ﴿٣١﴾

وَالَّذِينَ يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ  
 مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ  
 بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ فِي  
 الْأَرْضِ ۗ أُولَٰئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ وَهُمْ  
 سُوءُ الدَّارِ ﴿٢٥﴾

**25. Na wale wanaovunja  
 ahadi ya Mwenyezi Mungu  
 baada ya kuzifunga, na  
 wanakata Aliyoamrisha  
 Mwenyezi Mungu yaungwe,  
 na wanafanya ufisadi katika  
 nchi: hao ndio watakaopata  
 laana, na watapata Nyumba  
 mbaya.**

**Sifa za Watu Waovu  
 Zitakazowafanya Wapate  
 Laana na Mafikio Mabaya**

Hii ndiyo hali ya watu waovu na sifa zao na utajua marejeo yao huko akhera, inavyotofautiana na mafikio ya waumini. Kama ambavyo watu wabaya sifa zao zilikuwa kinyume na sifa za waumini. Kwani walikuwa wanatekeleza ahadi ya

Allah تعالی, wanakiunga kile ambacho Ameamrisha Allah تعالی kiungwe na hawa.

يَنْقُضُونَ عَهْدَ اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مِيثَاقِهِ وَيَقْطَعُونَ مَا أَمَرَ اللَّهُ بِهِمْ أَنْ يُوصَلَ وَيُفْسِدُونَ  
 فِي الْأَرْضِ ۗ

***“Na wale wanaovunja ahadi ya Mwenyezi Mungu baada ya kuzifunga, na wanakata Aliyoamrisha Mwenyezi Mungu yaungwe, na wanafanya ufisadi katika nchi.”***

Kama ilivyothibiti katika Hadithi.

«آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا أُؤْتِيَ خَانًا»

*“Alama za mnafiki ni tatu: akizungumza anasema uwongo na akiahidi anavunja ahadi na akiaminiwa anafanya khiana.”<sup>1</sup>*

Katika upokezi mwingine.

«وَإِذَا عَاهَدَ غَدَرَ وَإِذَا خَاصَمَ فَجَرَ»

*“Na pindi akitoa ahadi anafanya khiana na akigombana anafanya uovu.”<sup>2</sup>*

Kwa sababu hiyo Amesema:

أُولَئِكَ لَهُمُ اللَّعْنَةُ

***“...hao ndio watakaopata laana,...”***

Laana ni kuwekwa mbali na Rehma za Allah تعالى.

وَهُمْ سُوءُ الدَّارِ

***“...na watapata Nyumba mbaya.”***

Nao ni matokeo na mwisho mbaya.

وَمَا لَهُمْ جَهَنَّمَ<sup>ط</sup> وَيَسَّ إِلِهَادُ

***“...na makao yao ni Jahannamu. Na hapo ni pahala pabaya mno!”***  
**(13:18)**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 1:111.

<sup>2</sup> Kama hapo juu.

اللَّهُ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ وَفَرِحُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي  
الْآخِرَةِ إِلَّا مَتْنَعٌ ﴿٢٦﴾

**26. Mwenyezi Mungu Humkunjulia riziki Amtakaye, na Humkunjia kwa kipimo. Na wamefurahia maisha ya dunia. Na uhai wa dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila ni starehe ndogo.**

**Ukunjufu wa Riziki na ufinyo Wake Vimo Mikononi mwa Allah تعالى**

Allah تعالى Anataja kuwa Yeye Ndiye Anayemkunjulia riziki Amtakaye na Anaifinya kwa Amtakaye kwa sababu ya Hekima na Uadilifu Wake. Suala la makafiri kufurahia waliyopewa duniani ni kupewa muda tu. Kama Alivyosema:

أَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ مِن مَّالٍ وَبَيْنَ ۙ نُسَارِعُ هُم فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٦﴾

**“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)**

Kisha akadharau maisha ya dunia kulinganisha na vile ambavyo Allah تعالى Amewawekea waja Wake waumini katika nyumba ya akhera. Kwa hiyo Amesema:

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتْنَعٌ

**“Na uhai wa dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila ni starehe ndogo.”**

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

قُلْ مَتْنَعُ الدُّنْيَا قَلِيلٌ ۗ وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقَىٰ ۗ وَلَا تُظْلَمُونَ فَتِيلًا

**“Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kumchamungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende.” (4:77)<sup>1</sup> na**

بَلْ تُؤْتُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾ وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٧﴾

**“Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia! Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.” (87:16-17)**

<sup>1</sup> Utando mwembamba unaozunguka kokwa ya tende.

Na amepokea Imam Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Al-Mustanirad ndugu wa Banii Fihri amesema: Mtume ﷺ amesema

«مَا الدُّنْيَا فِي الآجِرَةِ إِلَّا كَمَا يَجْعَلُ أَحَدُكُمْ إِصْبَعَهُ هَذِهِ فِي النَّيْمِ، فَلْيَنْظُرْ بِمَ تَرْجِعُ»

*“Haikuwa dunia kwa akhera ila kama anavyotia mmoja wenu kidole chake katika huu mkondo (wa maji) na atazame kinarudi na nini?”*

Na alishiria kwenye kidole cha shahada.<sup>1</sup> Amepokea Hadithi hii Muslim katika Sahihi yake.<sup>2</sup> Na imekuja katika Hadithi nyingine ni kwamba Mtume ﷺ alimpitia mtoto wa mbuzi mdogo wa masikio, aliyekufa akasema:

«وَاللَّهِ لَلدُّنْيَا أَمْرٌ عَلَى اللَّهِ مِنْ هَذَا عَلَى أَهْلِهِ جِئِنَ أَلْقَوْهُ»

*“Naapa kwa Allah kwa hakika dunia ni nyonge sana kwa Mwenyezi Mungu kuliko mbuzi huyu kwa wenyewe wakati walipomtupa.”<sup>3</sup>*

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْلَا نُزِّلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِنْ رَبِّهِ قُلْ إِنَّ اللَّهَ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ أُنَابَ ﴿٢٧﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ طُوبَى لَهُمْ وَحُسْنُ مَقَابٍ ﴿٢٩﴾

**27. Na wanasema waliokufuru: Kwa nini hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi. Sema: Hakika Mwenyezi Mungu Humuacha kupotea amtakaye, na Humuongoa anayeelekea Kwake,**

**28. Wale walioamini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!**

**29. Wale walioamini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.**

<sup>1</sup> Ahmad 4:228.

<sup>2</sup> Ahmad 4:2193.

<sup>3</sup> Muslim na. 29:57.

**Washirikina Kutaka Miujiza na Majibu Juu Yao**

Allah تعالی Anaelezea: **لَوْلَا**

**“Kwa nini...”** Maana hivi kwa nini

**أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ**

**“...hakuteremshiwa muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi.”**

Kama Kauli Yao,

**فَلْيَأْتِنَا بَيِّنَاتٍ كَمَا أُرْسِلَ الْآءِلُونَ ﴿٥﴾**

**“Basi atuletee miujiza kama walivyotumwa wale wa mwanzo.” (21:5)**

Yameshatangulia maelezo ya aya hii mara nyingi, kwamba Allah تعالی Anaweza kuyajibu waliyoyaomba. Ipo Hadithi inayoeleza kuwa Allah تعالی Alimpelekea wahyi Mtume wake ﷺ pindi walipomtaka awageuzie mlima wa Swafa uwe dhahabu na awapitishie chemchem na ayaondoe majabali yaliyozunguka mji wa Makka, na badala yake aoteshe majani na bustani. “Ee Muhammad ukiomba hayo Nitawapa kama wakikufuru Nitawaadhibu adhabu ambayo sitamuadhibu yeyote katika walimwengu, na ukitaka Nitawafungulia mlango wa toba na rehma.’ Mtume ﷺ akasema:

**«بَلْ نَنْفَعُ لَهُمْ بَابَ التَّوْبَةِ وَالرَّحْمَةَ»**

**“Bali Utawafungulia mlango wa toba na rehma.”<sup>1</sup>**

Akamuambia:

**قُلْ إِنْ أَلَّهَ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ أُنَابَ**

**“Hakika Mwenyezi Mungu Humuacha kupotea amtakaye, na Humuongoa anayeelekea Kwake,...”**

Allah تعالی Anaeleza kuwa Yeye Hupoteza au Kuongoa, ama kwa Kumpeleka Mtume ﷺ pamoja na miujiza waliyotaka ama laa. Hakika, kuongoka au kupotea hakuhusiani na kuwepo au kukosekana miujiza. Kama Alivyosema:

**وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَن قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠١﴾**

**“Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini.” (10:101)**

<sup>1</sup> Kuna Hadithi yenye maneno sawa na hayo iliyoandikwa na Ahmad 1:242.



إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١١٦﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿١١٧﴾

**“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwishathibitika juu yao, hawataamini, Ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.” (10:96-97)**

وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا مَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ يَجْهَلُونَ ﴿١١٨﴾

**“Na lau kuwa Tungeliwateremshia Malaika, na maiti wakazungumza nao, na Tukawakusanyia kila kitu mbele yao, bado wasingeliamini, ila Mwenyezi Mungu Atake. Lakini wengi wao wamo ujingani.” (6:111)**

Hapa Allah تعالى Anasema,

قُلْ إِنَّ اللَّهَ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي إِلَيْهِ مَنْ أُنَابَ

**“Sema: Hakika Mwenyezi Mungu Humuacha kupotea Amtakaye, na Humuongoa anayeelekea Kwake.”**

Kwa maana: Anamuongoza Kwake mwenye kurejea kwa Allah تعالى na akarejea Kwake na akataka msaada Kwake na akanyenyekea mbele Yake.

**Utulivu wa Moyo wa Muumini kwa Sababu ya Kumtaja Allah تعالى**

Na Kauli Yake:

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَطَهَّرُوا قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ

**“Wale walioamini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu.”**

Maana yake: Zinakuwa nzuri na zinategemea upande wa Allah تعالى na zinatulizana wakati wa kumtaja na zinamridhia Akiwa ni Mtawalia wa mambo yao na Mwenye Kuwanusuru, na kwa sababu hiyo Amesema:

أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ ﴿١٣﴾

**“...Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!”**

Maana na yeye anastahiki hilo.

### **Kuweka Wazi Maana ya Neno “Tubaa”**

Na Kauli Yake:

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ طُوبَىٰ لَهُمْ وَحُسْنُ مَقَابٍ ﴿١٤﴾

**“Wale walioamini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.”**

Amesema Ibn Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: Inamaanisha kufurahi na kuridhia kwa macho.<sup>1</sup> Amesema Ikrima: ‘Ni bora sana walilopewa.’<sup>2</sup> Adh-Dhahhak amesema, “Furaha kwao.”<sup>3</sup> Amesema Ibrahim Annakhai, ‘Ni kheri kwao.’<sup>4</sup> Amesema Qatadah: ‘Ni tamko la Kiarabu: *Tubaa Laka*, yaani, Umepata kheri.’<sup>5</sup> Na katika upokezi Mwingine, (kheri zote ni zao) wema ni wao.”<sup>6</sup>

وَحُسْنُ مَقَابٍ

**“...na marejeo mazuri.”** Maana hizo za *Tubaa* ni moja, hazipingani.

Imam Ahmad عنه رضي الله عنه amemnukuu Abu Sa’id Al-Khudri عنه رضي الله عنه kuwa kuna mtu aliuliza, “Ewe Mtume! *Tubaa* ni kwa aliyekuona na kukuamini.” Mtume ﷺ akasema,

«طُوبَى لِمَنْ رَأَىٰ وَأَمَّنَ بِي، وَطُوبَى لِمَنْ طُوبَى ثُمَّ طُوبَى لِمَنْ آمَنَ بِي وَلَمْ يَرِنِّي»

**“*Tubaa* ni kwa aliyeniona na kuniamini. Na *Tubaa* zaidi na *Tubaa* zaidi na *Tubaa* zaidi kwa ambaye hakuniona na akaniamini.”**

Mtu mmoja akauliza, ‘*Tubaa* ni nini?’ Mtume ﷺ akasema,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:435.

<sup>2</sup> Kama hapo juu.

<sup>3</sup> Kama hapo juu.

<sup>4</sup> Al-Baghawi 3:18.

<sup>5</sup> At-Tabari 16:435.

<sup>6</sup> Kama hapo juu.

«شَجْرَةٌ فِي الْجَنَّةِ مَسِيرُهَا مِائَةٌ عَامٍ ثَابَتْ أَهْلُ الْجَنَّةِ تَخْرُجُ مِنْ أَكْمَامِهَا»

*"Ni mti wa peponi ambao masafa ya kipenyo chake ni miaka mia moja. Nguo za watu wa Peponi zinatokana na magamba yake."<sup>1</sup>*

Al-Bukhari na Muslim wameandika kuwa Sahl bin Saad رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ شَجْرَةً يَسِيرُ الرَّابُّ فِي ظِلِّهَا مِائَةَ عَامٍ لَا يَقْطَعُهَا»

*"Hakika peponi kuna mti anakwenda mwenye kupanda katika kivuli chake miaka mia moja hakikatiki kivuli chake."<sup>2</sup>*

Amesema, nikamueleza An-Numan bin Abii Ayyashi Al-Zarqi رضي الله عنه akasema: Ameniambia Abu Said Al-Khudry رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ شَجْرَةً يَسِيرُ الرَّابُّ الْجَرَادَ الْمُضْمَرَ السَّرِيعَ مِائَةَ عَامٍ مَا يَقْطَعُهَا»

*"Hakika peponi, kuna miti anakwenda mwenye kupanda farasi, aliyepewa mazoezi ya kukimbia, anayekwenda mbio miaka mia haukati mti huo."<sup>3</sup>*

Na imekuja katika Sahihi ya Muslim kutokana na Abu Dharr رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema kuwa Allah تعالى amesema:

«يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَجْرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجَنَّتُمْ قَامُوا فِي صَعِيدٍ وَاحِدٍ فَسَأَلُونِي فَأَعْطَيْتُ كُلَّ إِنْسَانٍ مَسْأَلَتَهُ مَا تَقْصَمُ ذَلِكَ مِنْ مُلْكِي شَيْئًا إِلَّا كَمَا يَنْقُصُ الْمِخْيَطُ إِذَا أُدْخِلَ فِي الْبَحْرِ»

*"Enyi waja wangu! Lau kama wa mwanzoni wenu mpaka wa mwishoni, wanadamu na majini wangesimama katika uwanja mmoja na wakaniomba, Ningempa kila mmoja bila ya kupungua chochote katika milki Yangu, bali kama inachopunguzwa na sindano inapotumbukizwa baharini."<sup>4</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 3:71.

<sup>2</sup> Al-Bukhari na. 6552, Muslim na. 2827.

<sup>3</sup> Muslim 4:1994.

Na amesema Khaliki bin Maadan, ‘Hakika peponi kuna mti unaoitwa *Tubaa* una viwele, vyote vitawanyonyesha watoto wadogo wa watu wa peponi na kwa hakika kipomoko – mtoto aliyeporomoka tumboni mwa mama yake – cha mwanamke kitakuwa katika mto katika mito ya peponi anageukageuka humo mpaka kisimame Kiyama, atafufuliwa hali ya kuwa ni Mtu mwenye miaka arobaini.’ Ameyapokea Ibn Abii Hatima.

كَذَلِكَ أَرْسَلْنَاكَ فِي أُمَّةٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهَا أُمَمٌ لَّتَتْلُوا عَلَيْهِمُ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَهُمْ  
يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ ۗ قُلْ هُوَ رَبِّي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ مَتَابِ ﴿٣٠﴾

**30. Ndio kama hivi Tumekutuma kwa umma ambao wamekwisha pita kabla yao umati nyengine, ili uwasomee Tunayokufunulia, na wao wanamkufuru Rahmani, Mwingi wa Rehema! Sema: Yeye Ndiye Mola Wangu Mlezi. Hapana mungu isipokuwa Yeye. Juu yake nimetegemea, na Kwake ndio marejeo yangu!**

**Makusudio ya Kupelekwa kwa Mtume ﷺ ni Kusoma Aliyofunuliwa Kwake na Kisha Kuyahubiri**

Allah تعالیٰ Anasema: na kama Tulivyokupeleka Ee Muhammad ﷺ katika umma huu;

لَتَتْلُوا عَلَيْهِمُ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ

**“...ili uwasomee Tunayokufunulia,”**

Maana yake: Unawafikishia ujumbe wa Allah تعالیٰ, kama hivyo Tulipeleka katika ummati uliopita ambao ulimkufuru Allah تعالیٰ, na kwa hakika walikadhibishwa Mitume waliokuwa kabla yako. Kwa hiyo una wewe kutokana na wao kigezo, na kama Tulivyoitusha adhabu Yetu na mateso Yetu kwa hao, na watahadhari hawa na kushuka mateso kwao kwani kukukadhibisha wewe ni jambo kubwa sana kuliko kukadhibishwa wengine katika Mitume. Amesema Allah تعالیٰ,

تَاللَّهِ لَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ

**“Wallahi! Sisi Tulituma Mitume kwa umati uliokuwa kabla yako,”**  
(16:63)

Allah تعالیٰ Amesema katika Aya nyingine,

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأَوْدُوا حَتَّىٰ أَتَاهُمْ نَصْرُنَا وَلَا مُبَدِّلَ  
لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ وَلَقَدْ جَاءَكَ مِن نَّبِيِّئِكَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٣٤﴾

**“Na hakika walikanushwa Mitume wa kabla yako. Nao wakavumilia kule kukanushwa, na kuudhiwa, mpaka ilipowafikia nusura Yetu. Na hapana wa kubadilisha Maneno ya Mwenyezi Mungu. Na bila ya shaka zimekuja baadhi ya khabari za Mitume hao.” (6:34)**

Maana yake: Tulivyowanusuru na Tukafanya mwisho mwema kwao na wafuasi wao duniani na akhera. Na Kauli Yake تعالی:

وَهُمْ يَكْفُرُونَ بِالرَّحْمَنِ ۗ

**“...na wao wanamkufuru Rahmani, Mwingi wa Rehema!”**

Maana huu umma ambao Tume kupoleka kwao unamkufuru Allah تعالی hawakubali kwa sababu wao walikuwa wanaona vibaya kumsifu Allah تعالی kwa kusema *Arrahmanir Rahim* – Mwenye Kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye Kuneemesha neema ndogo ndogo. Na kwa sababu hiyo waliona vibaya siku ya mkataba wa Hudaibiya<sup>1</sup> kuandika *Bismillahir Rahmanir Rahim* na wakasema: Hatujui ni kitu gani *Arrahmanir Rahim* ameyasema hayo Qatada na hadithi imo katika Sahihi ya Al-Bukhari.<sup>2</sup> Na amesema Allah تعالی:

قُلْ أَدْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ ۗ أَيًّا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۗ

**“Sema: Muombeni Allah (Mwenyezi Mungu), au muombeni Rahman (Mwingi wa Rehema), kwa jina lolote mnalomwita. Kwani Yeye ana majina mazuri mazuri.” (17:10)**

Na imekuja katika Sahihi ya Muslim kutoka kwa Abdillahi bin ‘Umar رضي الله عنه amesema. Mtume ﷺ amesema

«إِنَّ أَحَبَّ الْأَسْمَاءِ إِلَى اللَّهِ تَعَالَى عَبْدُ اللَّهِ وَعَبْدُ الرَّحْمَنِ»

**“Hakika linalopendeza sana katika majina kwa Allah تعالی ni Abdillahi na Abdurrahman – mja wa Mwenyezi Mungu.”<sup>3</sup>**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:446.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Bari 5:390.

<sup>3</sup> Muslim 3:1682.

قُلْ هُوَ رَبِّي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

**“Sema: Yeye ndiye Mola wangu Mlezi. Hapana mungu isipokuwa Yeye.”**

Maana yake: Huyu ambaye mnamkufuru, mimi ninamuamini, na ninaukubali Kwake Ubwana na Uungu, Yeye Ndiye Bwana wangu hapana Mola anayestahiki kuabudiwa asiyekuwa Yeye,

عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ

**“Juu yake nimetegemea,”**

Katika mambo yangu yote.

وَالِيهِ مَتَابِ

**“...na Kwake ndio marejeo yangu!”**

Kwa maana: Narejea Kwake na kutubu, kwani Yeye Peke Yake Ndiye Anayestahiki hayo, na si mwingine.

وَلَوْ أَنَّ قُرْءَانَ سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ أَوْ قُطِعَتْ بِهِ الْأَرْضُ أَوْ كُفِّرَ بِهِ الْمَوْتَىٰ ۗ بَلْ لِلَّهِ الْأَمْرُ جَمِيعًا ۗ أَفَلَمْ يَأْتِسَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَن لَّوِيَشَاءَ اللَّهُ لَهْدَىٰ النَّاسَ جَمِيعًا ۗ وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا تُصِيبُهُم بِمَا صَنَعُوا قَارِعَةٌ أَوْ تَحُلُّ قَرِيبًا مِّن دَارِهِمْ حَتَّىٰ يَأْتِيَ وَعْدَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُخَلِّفُ الْمِيعَادَ ﴿٣١﴾

**31. Na kama ingelikuwa Qur’ani ndiyo inayoendeshewa milima, na kupasuliwa ardhi, na kusemeshewa wafu, (basi ingelikuwa Qur’ani hii). Bali mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Je, hawajajua walioamini kwamba lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa bila ya shaka Angeliwaongoa watu wote? Wala waliokufuru hawaachi kusibiwa na balaa kwa waliyoyatenda, au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao, mpaka ifike Ahadi ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Havunji miadi Yake.**

### Ubora wa Qur'an na Kuikanusha kwake Makafiri

Allah تعالى Anasema katika Kuisifu Qur'ani ambayo Amemteremshia Muhammad ﷺ kwa Kuifanya bora juu ya baki ya vitabu vilivyoteremshwa kabla yake,

وَلَوْ أَنَّ قُرْءَانًا سُيِّرَتْ بِهِ الْجِبَالُ

***“Na kama ingelikuwa Qur'ani ndiyo inayoendesheba milima,...”***

Maana yake: Lau pangukuwa katika vitabu vilivyopita kitabu yanakwenda kwa kitabu hicho majabali kutoka katika sehemu zake. Au Ardhi ingeliweza kupasuliwa vipande, au wanasemeshwa kwa kitabu hicho wafu katika makaburi yao, ingekuwa Qur'ani hii ndiyo yenye sifa hiyo kinyume cha vitabu vingine. Au hadhi hiyo ingekuwa bora zaidi kwa Qur'an, kutokana na yaliyomo ndani yake miongoni mwa miujiza, ambayo watu na majini kwa pamoja iwapo watakusanyika juu ya kuleta mfano wake, au sura moja tu mfano wake wasingethubutu kufanya hivyo. Na pamoja na hayo hawa mushirikina wanaikufuru na wanaikanusha.

بَلِ لِلَّهِ الْأَمْرُ جَمِيعًا<sup>١</sup>

***“Bali mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu.”*** Maana yake: Marejeo ya mambo yote ni kwa Allah تعالى, na ambalo Analitaka Allah تعالى linakuwa, na ambalo Hakulitaka haliwi ambaye kapotezwa na Allah تعالى hapana wa kumuongoza na Yule ambaye Ameongozwa na Allah تعالى hana wa kumpoteza. Na jina Qur'an hutumiwa wakati mwingine kumaanisha vitabu vilivyotangulia kwa sababu Qur'ani Tukufu imechukuliwa kutokana na vitabu vyote. Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema,

«خَفِنْتُ عَلَى دَاوُدَ الْقِرَاءَةَ فَكَانَ يَأْمُرُ بِدَائِيهِ أَنْ تُسْرَجَ، فَكَانَ يَقْرَأُ الْقُرْآنَ مِنْ قَبْلِ أَنْ تُسْرَجَ دَائِيهِ، وَكَانَ لَا يَأْكُلُ إِلَّا مِنْ عَمَلِ يَدَيْهِ»

*“Kulirahisishwa kwa Dawud kusoma kwa hiyo alikuwa akiamrisha kutandikwa mnyama wake na alikuwa hali isipokuwa kutokana na kazi ya mikono yake alikuwa akisoma Qur'an (Zaburi) kabla ya kutandikwa mnyama wake.”<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 2:314.

Ampewekeka katika kuithibitisha hadithi hii Al-Bukhari.<sup>1</sup> Na makusudio ya Qur'ani katika hadithi hii ni Zabur. Na Kauli Yake:

أَفَلَمْ يَأْتِيسِ الَّذِينَ ءَامَنُوا

**“Je, hawajajua walioamini...”** Maana yake: Hawakukata tamaa na kuamini viumbe wote na wakaelewa na wakahakikisha,

أَنْ لَّوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَهَدَى النَّاسَ جَمِيعًا

**“...lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa bila ya shaka Angeliwaongoa watu wote?”**

Kwa hakika hakuna huko hoja wala muujiza mkubwa sana na wala wenye manufaa sana katika akili na nafsi kuliko Qur'ani hii, ambayo lau ingeteremshwa juu ya Mlima, ungeuona yenye kunyenyekea unapasukapasuka kutokana na kumuogopa Allah تعالى. Na imethibiti katika Hadithi Sahihi kwamba Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا وَقَدْ أُوتِيَ مَا آمَنَ عَلَىٰ مِنْهُ النَّبِيُّ، وَإِنَّمَا كَانَ الَّذِي أُوتِيَهُ وَحْيًا  
أَوْحَاهُ اللَّهُ إِلَيْهِ، فَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَكْثَرَهُمْ تَابِعًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*“Hapana Mtume yeyote isipokuwa amepewa yale ambayo wameamini juu ya mfano wake watu na hakika hapana jambo jengine kile ambacho nimepewa ni wahyi Aliyouleta Mwenyezi Mungu kwangu, kwa hiyo ninataraji kuwa nitakuwa mwingi wao sana kwa wafuasi siku ya Kiyama.”<sup>2</sup>*

Maana yake: Ni kwamba miujiza ya kila Mtume imekwisha kwa kufa kwake Mtume huyo, na Qur'ani hii ni hoja itakayobakia nyakati zote, hayamaliziki maajabu yake, na haitetereki pamoja na wingi wa kupingwa kwake, na wanazuoni hawakinaiki nayo. Qur'ani Tukufu ndiyo ukweli na si mzaha, mwenye kuiacha miongoni mwa wajeuri atamhilikisha Allah تعالى, na mwenye kuutafuta uongofu kutoka katika isiyokuwa Qur'ani atampoteza Allah تعالى. Na Kauli Yake:

بَلْ لِلَّهِ الْأَمْرُ جَمِيعًا

**“Bali mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu.”**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:248.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:619.



Ibnu Abbas رضي الله عنهما amesema: Maana yake: Hafanyi katika hayo isipokuwa lile Analolitaka, Asilolitaka Halifanyi.<sup>1</sup> Ameyapokea Ibn Is'haq رحمه الله تعالى kwa upokezi wake kutokana naye, na ameyasema hayo Ibnu Jarir رحمه الله تعالى vilevile. Na Kauli Yake:

وَلَا يُزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا تُصِيبُهُمْ بِمَا صَنَعُوا قَارِعَةٌ أَوْ تَحُلُّ قَرِيبًا مِّن دَارِهِمْ

**“Wala waliokufuru hawaachi kusibiwa na balaa kwa waliyoyatenda, au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao,”**

Maana yake: Kwa sababu ya kukadhibisha kwao hayataacha kuwa mabalaa yanawapata duniani au yanawapata walio pembezoni mwao ili waonyeke na wapate mazingatio kama alivyosema Allah تعالى,

وَلَقَدْ أَهَلَكْنَا مَا حَوْلَكُم مِّنَ الْقُرَىٰ وَصَرَّفْنَا الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٧﴾

**“Na hakika Tuliangamiza miji ilio jirani zenu, na Tulizitumia Ishara ili wapate kurejea.” (46:27) na,**

أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا أَفَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٢٨﴾

**“Je, hawaoni ya kwamba Sisi Tunaifikia ardhi Tukiipunguza ncha zake? Basi je! Hao ni wenye kushinda?” (21:44)**

Qatadah alisimulia kuwa Al-Hasan alitoa rai kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

أَوْ تَحُلُّ قَرِيبًا مِّن دَارِهِمْ

**“...au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao,”**

“Inaashiria balaa.”<sup>2</sup> Hii ni maana ya wazi hapa. Al-'Awfi amesema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema,

تُصِيبُهُمْ بِمَا صَنَعُوا قَارِعَةٌ

**“...hawaachi kusibiwa na balaa kwa waliyoyatenda,”**

Adhabu inayowashukia kutoka mbinguni.

أَوْ تَحُلُّ قَرِيبًا مِّن دَارِهِمْ

**“...au ikawateremkia karibu na nyumbani kwao,”**

<sup>1</sup> At-Tabari: 16:447.

<sup>2</sup> At-Tabari: 16:459.

Mtume ﷺ anapopiga kambi karibu na eneo lao na kuwapiga.” Rai sawa na hiyo imesimuliwa kutoka kwa Mujahid na Qatadah. Na amesema Ikrimah: Katika upokezi mwingine kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.

قَارِعَةً

“...bala...”

Mateso. Kila mmoja wao amesema,

حَتَّىٰ يَأْتِيَ وَعْدُ اللَّهِ

“...mpaka ifike Ahadi ya Mwenyezi Mungu...”

Anakusudia ufunguzi wa Makkah. Amesema Al-Hassan Al-Basry رحمه الله تعالى: Siku ya Kiyama. Na Kauli Yake:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَخْلِفُ الْمِيعَادَ

“**Hakika Mwenyezi Mungu Havunji miadi Yake.**”

Maana yake: Havunji Ahadi Yake kwa Mitume Wake, kwa Kuwanusuru wao na wafuasi wao duniani na akhera,

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ مُخْلِفًا وَعْدِهِمْ رُسُلَهُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ ذُو انْتِقَامٍ ﴿١٤﴾

**“Basi usimdhania Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye Kuwavunjia Ahadi Yake Mitume Wake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushinda, na ni Mwenye Kulipiza.” (14:47)**

\* \* \*

وَلَقَدْ آسَفْنَاهُ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ  
فَأَمَلَيْتُ لِلَّذِينَ كَفَرُوا ثُمَّ أَخَذْتُهُمْ<sup>ط</sup>  
فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ﴿٣٢﴾

**32. Na hakika walifanyiwa  
kejeli Mitume waliokuwa  
kabla yako. Na nikawavutia  
muda wale waliokufuru,  
kisha nikawashika! Basi  
ilikuwaje Adhabu Yangu!**

**Kuliwazwa kwa Mitume wa  
Allah** تعالی

Allah تعالی Anasema Akimli-  
waza Mtume Wake ﷺ kwa  
sababu ya kukadhibisha  
kwa waliyomkadhibisha  
katika jamaa zake,

وَلَقَدْ آسَفْنَاهُ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ

**“Na hakika walifanyiwa  
kejeli Mitume waliokuwa  
kabla yako.”**

Maana yake: Una wewe  
kwao kigezo.

وَلَقَدْ آسَفْنَاهُ بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَأَمَلَيْتُ لِلَّذِينَ كَفَرُوا ثُمَّ  
أَخَذْتُهُمْ<sup>ط</sup> فَكَيْفَ كَانَ عِقَابِ ﴿٣٢﴾ أَفَمَن هُوَ قَابِئًا عَلَىٰ  
كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ قُل سَمُّوهُمْ ؕ أَمْ  
تُنَبِّئُونَهُ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي الْأَرْضِ أَمْ بَطَّيِرُ مِن الْقَوْلِ ؕ  
بَلْ زُيِّنَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مَكْرَهُمْ وَصَدُّوا عَنِ السَّبِيلِ ؕ وَمَن  
يُضَلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن هَادٍ ﴿٣٣﴾ هُمْ عَذَابٌ فِي الْحَيَاةِ  
الدُّنْيَا ۖ وَعَذَابٌ الْآخِرَةِ أَشَقُّ ۖ وَمَا لَهُم مِّنَ اللَّهِ مِن وَّاقٍ ﴿٣٤﴾  
\* مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ ۖ تَجْرَىٰ مِن تَحْتِهَا  
الْأَنْهَارُ ۖ أَكْثُهَا دَائِمٌ وَظِلُّهَا ۚ تِلْكَ عُقْبَى الَّذِينَ اتَّقَوْا<sup>ط</sup>  
وَعُقْبَى الْكَافِرِينَ النَّارُ ﴿٣٥﴾ وَالَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ  
يَفْرَحُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ ۖ وَمِنَ الْأَحْزَابِ مَن يُنْكِرُ  
بَعْضَهُ ؕ قُلْ إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ وَلَا أُشْرِكَ بِهِ ؕ إِلَيْهِ  
أَدْعُوا وَإِلَيْهِ مَوَابٍ ﴿٣٦﴾ وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ حُكْمًا عَرَبِيًّا<sup>ع</sup>  
وَلَيْنِ اتَّبَعَتْ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ  
اللَّهِ مِن وَّالِيٍّ وَلَا وَاقٍ ﴿٣٧﴾

فَأَمَلَيْتُ لِلَّذِينَ كَفَرُوا

**“Na nikawavutia muda wale waliokufuru,”**

Maana yake: Niliwapa muda na Nikawachelewesha.

ثُمَّ أَخَذْتُهُمْ<sup>ط</sup>

**“Kisha Nikawashika!”**

Kwa Kuwaadhibu wao adhabu kubwa, bila shaka umeona jinsi Nilivyowafanya na Kuwaadhibu wao baada ya Kuwapa muda. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَكَأَيِّن مِّن قَرِيْبَةٍ أَمَلَيْتُهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ لِّمَا أُخَذْتُهَا وَإِلَى الْمَصِيْرِ ﴿٣٦﴾

**“Na miji mingapi Niliipa muda na hali ilikuwa imedhulumu, na kisha Nikaitia Mkononi? Na Kwangu Mimi ndio marudio yote.” (22:48)**

Na imekuja katika sahihi ya Bukhary na Muslim.

إِنَّ اللَّهَ لِيَمْلِكُ لِلظَّالِمِ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يَفْلِتْهُ

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Anampa muda dhalimu mpaka Atakapomkamata Hamuachii.”

Kisha Akasema Allah تعالى،

وَكَذَٰلِكَ أَخَذْنَا مِنْكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿٣٧﴾

**“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi Anapoikamata miji inapokuwa imedhulumu. Hakika Mkamato Wake ni mchungu na mkali.” (11:102).<sup>1</sup>**

أَفَمَن هُوَ قَابِئُ عَلَىٰ كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ ۗ وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ قُلْ سَمُّوهُمْ ۗ أَمْ تُنَبِّئُونَهُ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي الْأَرْضِ ۗ أَمْ يَبْظَهَرُ مِنَّا الْقَوْلُ ۗ بَلْ زَيْنَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مَكْرَهُمْ وَصَدُّوا عَنِ السَّبِيلِ ۗ وَمَن يُضِلِّ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن هَادٍ ﴿٣٨﴾

**33. Je! Ni nani anayeisimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma? Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu kuwa na washirika! Sema watajeni. Au ndio mnampa khabari ya yale asiyojajua katika ardhi; au ni maneno matupu? Bali waliokufuru wamepambiwa vitimbi vyao na wamezuiliwa njia. Na ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha apotee basi hana wa kumuongoa.**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:205, Muslim 4:1997.

## Hapana Ushirika kati ya Allah تعالى na Waungu wa Washirikina kwa Hali Yoyote

Allah تعالى Anasema:

أَفَمَنْ هُوَ قَائِمٌ عَلَىٰ كُلِّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ

**“Je! ni nani anayeisimamia kila nafsi kwa yale iliyoyachuma?”**

Maana yake: Mwenye Kuhifadhi, Mwenye Kujua sana, Mwenye Kuchunga juu ya kila nafsi iliyoyambwa, Anayajua yale ambayo wanayatenda wenye kutenda miongoni mwa kheri na shari, na Halijifichi Kwake jambo lolote lenye kujificha.

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ

**“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo.” (10:61) na,**

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا

**“Na halidondoki jani ila Analijua.” (6:59)**

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَىٰ اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي كِتَابٍ

مُسَبِّحِينَ

**“Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye Anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.” (11:6)**

سَوَاءٌ مِنْكُمْ مَنْ أَسْرَ الْقَوْلَ وَمَنْ جَهَرَ بِهِ وَمَنْ هُوَ مُسْتَخْفٍ بِاللَّيْلِ وَسَارِبٌ بِالنَّهَارِ

**“Ni sawa anayeficha kauli yake kati yenu na anayeidhirisha, na anayejibanza usiku na anayetembea jahara mchana.” (13:10)**

يَعْلَمُ الْسِّرِّ وَالْأَخْفَىٰ

**“Yeye anajua siri na duni kuliko siri.” (20:7) na,**

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ

**“Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona mnayoyatenda.” (57:4)**

Hivi yule ambaye yuko hivyo, atakuwa kama masanamu mnayoyaabudu? Hayasikii, hayaoni, hayaelewi na hayamiliki manufaa kwa nafsi yake, wala kwa wanayoyaabudu na hapana kuondolewa madhara kwa hayo masanamu wala kwa wale ambao wanayaabudu? Na yameondolewa majibu hayo kwa kutosheka na mafahamisho ya mtiririko wa maneno juu yake. Nayo ni Kauli Yake:

وَجَعَلُوا لِلَّهِ شُرَكَاءَ

**“Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu kuwa na washirika!”**

Kwa maana: Wameyaabudu masanamu pamoja na Allah تعالى.

قُلْ سَمُوهُمُ

**“Sema watajeni.”** Maana: Tufahamisheni juu ya waungu hao, na wawawekeni wazi ili wajulikane kwani waungu hao hawana hakika yoyote. Na kwa sababu hiyo Amesema:

أَمْ تَتَذَكَّرُونَ ۗ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي الْأَرْضِ

**“Au ndio mnampa khabari ya yale asiyoyajua katika ardhi;”**

Kwa maana: Jambo ambalo halipo? Kwa sababu lingekuwa lipo, katika ardhi Angelijua kwa sababu Yeye Halijifichi Kwake jambo lolote lenye kujificha.

أَمْ يَظَاهِرُونَ مِنَ الْقَوْلِ

**“...au ni maneno matupu?”**

Amesema Mujahidi ni dhana katika maneno.<sup>1</sup> Na amesema Adh-Dhahaak na Qatadah: Ni batili katika maneno.<sup>2</sup> Maana: Hakika si vingine mliyaabudu masanamu haya kutokana na dhana yenye kutokana na nyinyi, kwamba masanamu hayo yanadhuru na yananufaisha na mmeyaita kuwa ni waungu.

<sup>1</sup> At-Tabari 16:466.

<sup>2</sup> Kama hapo juu.

إِنَّ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمِيئُوهَا أَنْتُمْ وَءَابَاؤُكُمْ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ بِهَا مِنْ سُلْطٰنٍ ۚ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنفُسُ ۗ وَلَقَدْ جَاءَهُمْ مِنْ رَبِّهِمْ آهْدٰى ﴿٣٢﴾

***“Hayo hayakuwa ila ni majina mliyowapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu Hakuleta uthibitisho wowote juu ya hayo. Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa yakini uwongofu ulikwishawafikia kutoka kwa Mola wao Mlezi.” (53:23)***

Allah تعٰلى Akasema tena,

بَلْ زُيِّنَ لِلذِّينِ كَفْرُوهَا مَكْرُهُمْ

***“Bali waliokufuru wamepambiwa vitimbi vyao...”***

Mujahidi amesema, maneno yao.<sup>1</sup> Maana: Yale ambayo wao wako juu yake miongoni mwa upotevu na kuwaita watu kwenye huo upotevu, nyakati za usiku na ncha za mchana. Kama vile ilivyo Kauli Yake Allah تعٰلى:

وَقِيضْنَا لَهُمْ قُرْءَانَ فَرِيضُوا لَهُمْ

***“Na Tukawawekea marafiki, na wakawapambia...” (41:25)***

Allah تعٰلى Akasema tena,

وَصُدُّوهَا عَنِ السَّبِيلِ ۗ

***“...na wamezuiliwa njia.”***

Mwenye kuisoma aya hiyo kwa *fatha* ya *Swad- na kuwa Swaddu*. Maana yake itakuwa ni walipopambiwa yale ambayo wao wamo ndani yake, na kwamba hayo ni ukweli, waliwaita watu kwenye mambo hayo na wakawazuia watu katika kuifuata njia ya Mitume. Na mwenye kuisoma aya hiyo kwa *Dhumma* ya *Swad - na kuwa Swuddu*. Italeta maana: Kwa sababu ya kupambiwa kwao miongoni mwa usahihi wa lile ambalo wao wamo ndani yake, walizuiliwa kwa sababu hiyo na njia ya Allah تعٰلى. Na kwa sababu hiyo Amesema:

وَمَنْ يُضَلِلِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ هَادٍ

***“Na ambaye Mwenyezi Mungu Amemuacha apotee basi hana wa kumuongoa.”***

<sup>1</sup> At-Tabari 16:467.

Kama Alivyosema:

وَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَنْ تَمْلِكَ لَهُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا

**“Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu Anataka kumfitini huwezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu.” (5:41) na,**

إِنْ تَحَرَّصَ عَلَىٰ هُدُنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ يُضِلُّ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿١٦﴾

**“Hata ukiwa na pupa ya kutaka kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Hamuongoi yule anaye shikilia kupotea. Wala hawatapata wa kuwanusuru.” (16:37)**

هُمَّ عَذَابٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَقُّ ۖ وَمَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَاقٍ ﴿١٧﴾ \*  
مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعِدَ الْمُتَّقُونَ ۖ تَجْرَىٰ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۖ أُكُلُهَا دَائِمٌ وَظِلُّهَا ۚ تِلْكَ عُقْبَى الَّذِينَ اتَّقَوْا وَعُقْبَى الْكَافِرِينَ النَّارُ ﴿١٨﴾

**34. Wanayo adhabu katika maisha ya dunia, na adhabu ya Akhera hapana shaka ni nzito zaidi. Na wala hawatakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu.**

**35. Mfano wa Bustani waliyoahidiwa wachamungu, kati yake inapita mito, matunda yake ni ya daima, na pia kivuli chake. Huu ndio mwisho wa wale waliojilinda. Na mwisho wa makafiri ni Moto.**

### Kuiweka Wazi Adhabu ya Makafiri na Malipo ya Watu Wema

Hapa Allah تعالیٰ Anataja adhabu ya makafiri na malipo ya watu wema baada ya Kuelezea kufuru na shirki waliokuwa wakiifanya.

هُمَّ عَذَابٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Wanayo adhabu katika maisha ya dunia.”**

Maana yake: Mikononi mwa waumini kwa kuwaua na kuwateka.

وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ

**“...na adhabu ya Akhera hapana shaka...”** Maana yake: Adhabu ambayo itawapata huko mbele pamoja na udhalili huu katika dunia



أَشَقُّ

“...**ni nzito zaidi.**”Maana yake: Kuliko hii kwa uchungu zaidi. Kama alivyosema Mtume ﷺ akiwaambia watu wawili wenye kulaaniana,<sup>1</sup>

«إِنَّ عَذَابَ الدُّنْيَا أَهْرَنُ مِنْ عَذَابِ الآخِرَةِ»

“Kwa hakika adhabu ya dunia ni nyepesi sana kuliko adhabu ya akhera.”<sup>2</sup>

Na hayo ni kama alivyosema Mtume ﷺ kwani adhabu ya dunia inamalizika, na ya Akhera ni yenye kudumu na ya milele katika moto, na adhabu hiyo ukilinganisha na ya dunia ni zaidi ya mara sabini, kuna minyororo ya kufungiwa ambayo hauingii akilini, wingi na ugumu wake. Kama Alivyosema Allah تعالى:

فَيَوْمَئِذٍ لَا يُعَذِّبُ عَذَابُهُ أَحَدًا ۖ وَلَا يُوثِقُ وِثْقَهُ أَحَدًا ﴿٢٦﴾

“**Basi siku hiyo hataadhibu yeyote namna ya kuadhibu Kwake. Wala hatafunga yeyote kama kufunga Kwake.**” (89:25-26) na.

بَلْ كَذَّبُوا بِالسَّاعَةِ ۖ وَأَعْتَدْنَا لِمَنْ كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا ﴿٢٥﴾ إِذَا رَأَتْهُمْ مِنْ مَكَانٍ  
بَعِيدٍ سَمِعُوا لَهَا تَغَيُّظًا وَزَفِيرًا ﴿٢٦﴾ وَإِذَا أَلْقَا مِنْهَا مَكَانًا ضَيِّقًا مُقَرَّبِينَ دَعَوْا هُنَالِكَ  
ثُبُورًا ﴿٢٧﴾ لَا تَدْعُوا آيَوْمَ ثُبُورًا وَاحِدًا ۖ وَادْعُوا ثُبُورًا كَثِيرًا ﴿٢٨﴾ قُلْ أَدْرَاكُمْ أَهْلَ  
جَنَّةِ الآخِرَةِ الَّتِي وَعَدَ الْمُتَّقُونَ ؕ كَانَتْ لَهُمْ جَزَاءً وَمَصِيرًا ﴿٢٩﴾

“**Bali wanaikanusha Saa (ya Kiyama). Na Sisi Tumemuandalia Moto mkali kabisa huyo mwenye kuikanusha Saa. Ule Moto ukiwaona tangu mahali mbali wao watasikia hasira yake na mngurumo wake. Na watakapotupwa humo mahali dhiki, hali wamefungwa, wataomba wafe. Msiombe kufa mara moja tu, bali mfe mara nyingi! Sema: Je! Haya ni bora au Pepo ya milele, ambayo wameahidiwa wachamungu, iwe kwao malipo na marejeo?**” (25:11-15)

<sup>1</sup> Laana huapizwa inapoaminika kuwa mwana ndoa amezini na hakuna mashahidi. Angalia Tafsiri ya Surat An-Nur na. 7.

<sup>2</sup> Muslim 2:1131.

Kadhhalika Amesema,

مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعِدَ الْمُتَّقُونَ<sup>ط</sup>

**“Mfano wa Bustani waliyoahidiwa wachamungu,”**

Maana yake: Maelezo na sifa zake,

تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ<sup>ط</sup>

**“...kati yake inapita mito.”** Maana yake: Inapita katika pande zake na pembezoni mwake, na mahali popote watakapotaka watu wake, wataivuta kwa nafasi popote watakapo namna wanavyotaka, kama ilivyo Kauli Yake Allah

تعالى، مَثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وَعِدَ الْمُتَّقُونَ<sup>ط</sup> فِيهَا أَنْهَارٌ مِنْ مَاءٍ غَيْرِ آسِنٍ وَأَنْهَارٌ مِنْ لَبَنٍ لَمْ يَتَغَيَّرَ طَعْمُهُ وَأَنْهَارٌ مِنْ خَمْرٍ لَذَّةٍ لِلشَّارِبِينَ وَأَنْهَارٌ مِنْ عَسَلٍ مُصَفًّى<sup>ط</sup> وَهُمْ فِيهَا مِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ

**“Mfano wa Pepo walioahidiwa wachamungu ina mito ya maji yasiyovunda, na mito ya maziwa isiyoharibika ladha yake, na mito ya mvinyo yenye ladha kwa wanywao, na mito ya asali iliyosafishwa. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda, na maghufira kutoka kwa Mola wao Mlezi.” (47:15)**

Na Kauli Yake تعالى،

أَكُلُهَا دَائِمًا وَظِلُّهَا<sup>ط</sup>

**“...matunda yake ni ya daima, na pia kivuli chake.”**

Kwani peponi kuna vyakula, matunda na vinywaji visivyokwisha. Imeandikwa katika Sahihi Mbili kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika kuelezea Sala ya kupatwa kwa jua na katika hilo walisema: ‘Ee Mtume ﷺ tumekuona umechuma kitu katika masimamo yako haya kisha tumekuona umetafuna akasema,

«إِنِّي رَأَيْتُ الْجَنَّةَ - أَرَأَيْتُ الْجَنَّةَ - فَتَنَّاوَلْتُ مِنْهَا عُشْرًا، وَلَوْ أَخَذْتَهُ لَأَكَلْتُمْ مِنْهُ مَا بَقِيَ الدُّنْيَا»

**“Kwa hakika mimi nimeiona Pepo - au nimeoneshwa Pepo nikachuma humo Peponi kole na lau ningelichukua mngékula katika kole hilo muda wa kubaki kwa dunia.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 2:271, Muslim 2:626.

Imam Muslim ameandika kuwa Jabir bin Abdillah رضي الله عنهما amesema: Mtume  
 𐤃𐤁𐤀 amesema,

«يَأْكُلُ أَهْلُ الْجَنَّةِ وَيَشْرَبُونَ، وَلَا يَتَمَخَّطُونَ وَلَا يَتَغَوَّطُونَ، وَلَا يَبُولُونَ، طَعَامُهُمْ  
 جُشَاءٌ كَرِيحِ الْمِسْكِ، وَيُلْهَمُونَ التَّنْبِيحَ وَالتَّقْدِيرَ كَمَا يُلْهَمُونَ التَّنَسُّمَ»

*“Watakula watu wa Peponi ndani ya Pepo, watakunywa humo, hawatapenga kamasi, hawatakunya na hawatakojoa; chakula chao kitatoka katika hali ya kucheua, ni kama harufu nzuri ya miski na watafundishwa Kumtakasa Mwenyezi Mungu na Kumtukuza kama wanavyofahamishwa kupumua.”* Hadith ameinukuu Muslim.<sup>1</sup>

Kadhalika Imam Ahmad na Annasai wamenukuu kutoka kwa Thumana bin Uqbah kuwa amemsikia Zaid bin Arqam رضي الله عنه, amesema: Alikuwa mtu mmoja katika watu wa kitabu akasema: ‘Ee Abal Qasim unadai kwamba watu wa Peponi watakula na watakunywa?’ Akasema

«تَعَمُّ، وَالَّذِي تَفَسَّرَ مُحَمَّدٌ بِيَدِهِ، إِنَّ الرَّجُلَ مِنْهُمْ لَيُعْطَى قُوَّةَ مِائَةِ رَجُلٍ فِي الْأَكْلِ  
 وَالشُّرْبِ وَالْجَمَاعِ وَالشَّهْوَةِ»

*“Ndiyo, naapa kwa Mwenyezi Mungu Ambaye nafsi ya Muhammad imo katika Uwezo Wake hakika mtu katika wao atapewa nguvu za watu mia katika kula, kunywa, kuingilia na matamano.”*

Akasema, ‘Kwa hakika anayekula na kunywa anakuwa na haja na hamna Peponi uchafu.’ Akasema:

«تَكُونُ حَاجَةٌ أَحَدِهِمْ رَشْحًا يَبْيِضُ مِنْ جُلُودِهِمْ كَرِيحِ الْمِسْكِ تَبْضُرُ بَطْنَهُ»

*“Itakuwa haja ya mmoja wao ni jasho litakalomiminika kutoka katika ngozi zao kama vile harufu ya miski, (baada ya kutoka hilo jasho) litarudi tumbo lake ndani.”*

Ameipokea Imam Ahmad na An-Nisai.<sup>2</sup> Na kwa hakika Allah تعالى Amesema :

﴿وَفِيكَهَّ كَثِيرًا ۖ لَا مَقْطُوعَةَ وَلَا مَمْنُوعَةَ ۗ﴾

**“Na matunda mengi, Hayatindikii wala hayakatazwi.” (56:32-33)** na,

<sup>1</sup> Muslim na. 2835.

<sup>2</sup> Ahmad 4:367, An-Nasai katika *Al-Kubra* 1178.

وَدَانِيَةً عَلَيْهِمْ ظِلُّلُهَا وَذُلِّلَتْ قُطُوفُهَا تَذْلِيلًا ﴿١٤﴾

**“Na vivuli vyake vitakuwa karibu yao, na mashada ya matunda yataning’inia mpaka chini.” (76:14)**

Kivuli cha Peponi ni cha milele na hakipungui. Kama Alivyosema Allah تعالى،

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا  
أَبَدًا هُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُطَهَّرَةٌ وَنُدْخِلُهُمْ ظِلًّا ظَلِيلًا ﴿٥٧﴾

**“Na wale walioamini na wakatenda mema Tutawaingiza katika Pepo zipitazo mito kati yake kwa kudumu humo milele. Huko watakuwa na wake waliotakasika, na Tutawaingiza katika vivuli vizuri kweli.” (4:57)**

Na mara nyingi hukutanisha Allah تعالى kati ya sifa ya Pepo na sifa za moto, ili Awavute watu Peponi na Awahadharishe na moto; na kwa sababu hiyo kwa yote ambayo aliyotaja kuhusu Pepo, alisema baada ya hapo:

تِلْكَ عُقْبَى الَّذِينَ اتَّقَوْا وَعُقْبَى الْكَافِرِينَ النَّارُ

**“Huu ndio mwisho wa wale waliojilinda. Na mwisho wa makafiri ni Moto.”**

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine،

لَا يَسْتَوِي أَصْحَابُ النَّارِ وَأَصْحَابُ الْجَنَّةِ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ هُمْ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾

**“Hawawi sawa watu wa Motoni na watu wa Peponi. Watu wa Peponi ndio wenye kufuzu.” (59:20)**

وَالَّذِينَ ءَاتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَفْرَحُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمِنَ الْأَحْزَابِ مَنْ يُحِبُّكَ بَعْضُهُمْ  
قُلْ إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ وَلَا أُشْرِكَ بِهِ إِلَيْهِ أَدْعُوا وَإِلَيْهِ مَقَابِلُ ﴿٢١﴾ وَكَذَلِكَ  
أَنْزَلْنَاهُ حُكْمًا عَرَبِيًّا وَلَئِنْ اتَّبَعْتَ أَهْوَاءَهُمْ بَعْدَمَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ  
وَلِيٍّ وَلَا وَاقِرٍ ﴿٢٢﴾

**36. Na Tuliowapa Kitabu wanafurahia uliyoteremshiwa. Na katika makundi mengine wapo wanaoyakataa baadhi ya haya. Sema: Nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu, na wala**

*nisimshirikishe. Kuendea Kwake Yeye ndiyo ninaita, na Kwake Yeye ndio marejeo yangu.*

**37. Na ndio kama hivi Tumeiteremsha Qur'ani kuwa ni hukumu kwa lugha ya Kiarabu. Na ukifuata matamano yao baada ya kukujia ilimu hii, hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu.**

**Watu Wakweli Katika Waliopewa Kitabu Wanafurahia Aliyoteremshiwa Muhammad ﷺ kwa Uthibitisho wa Vitabu Vyao**

Allah تعالیٰ Anasema:

وَالَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ

**“Na Tuliowapa Kitabu...”** Nao ni wale ambao wanasimama na mafunzo ya vitabu hivyo.

يَفْرَحُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ

**“...wanafurahia uliyoteremshiwa.”**

Miongoni mwa Qur'ani kutokana na yaliyomo katika vitabu vyao miongoni mwa ushahidi mwingi juu ya ukweli wake na kumbashiria yeye. Kama Alivyosema Allah تعالیٰ:

وَالَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِ

**“Wale Tuliowapa Kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa,”**  
(2:121) na,

قُلْ ءَامِنُوا بِهِمْ أَوْ لَا تُوْمِنُوا

**“Sema: laminini au msiiamini.” (17:107)** mpaka

إِنْ كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٠٨﴾

**“Hakika ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe!” (17:108)**

Maana yake: Kwa hakika yamekuwa yale ambayo ametuahidi kwayo Allah تعالیٰ katika vitabu vyetu miongoni mwa kupelekwa kwa Muhammad ﷺ ni haki na ni kweli na ni jambo lenye kutekelezwa. Hapana budi litakuwa. Kutakasika ni Kwake. Ni ukweli ulioje wa Ahadi Zake, kwa hiyo ni Zake Sifa Njema hali ya kuwa Peke Yake,

وَيَحْزَنُونَ لِلَّذِينَ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعًا ﴿٣٦﴾

**“Na huanguka kifudufudi na huku wanalia, na inawazidisha unyenyekevu.” (17:109)** Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمِنَ الْأَحْزَابِ مَن يُنْكِرُ بَعْضَهُ<sup>٤</sup>

**“Na katika makundi mengine wapo wanaoyakataa baadhi ya haya.”**

Maana yake: Na katika makundi kuna wanaokadhibisha baadhi ya yale ambayo yameteremshwa kwake na amesema Mujahid,

وَمِنَ الْأَحْزَابِ

**“Na katika makundi...”** Maana yake: Makundi ni Manaswara.

مَن يُنْكِرُ بَعْضَهُ<sup>٤</sup>

**“...wapo wanaoyakataa baadhi ya haya.”** Maana yake: baadhi ya yaliyokujia miongoni mwa haki. Na kama hivyo amesema Qatadah na Abdurrahman Ibn Zaidi Bin Aslam.<sup>1</sup> Ni kama Alivyosema Allah تعالى:

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَن يُؤْمِنُ بِاللَّهِ

**“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu.” (3:199)**

Kisha Allah تعالى Akasema,

قُلْ إِنَّمَا أُمِرْتُ أَنْ أَعْبُدَ اللَّهَ وَلَا أُشْرِكَ بِهِ<sup>٥</sup>

**“Sema: Nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu, na wala nisimshirikishe.”**

Maana yake: Hakika nimepelekwa kwa kumuabudu Allah تعالى hali ya kuwa Peke Yake hana mshirika kama Alivyowapeleka Mitume kabla yangu.

إِلَيْهِ أَدْعُوا

**“Kuendea Kwake Yeye ndiyo ninaita.”** Kwenye njia Yake ninawalingania watu.

<sup>1</sup> Tabari 16:474. Maana: Allah تعالى Ameyafanya hayo, imeelezwa katika Aya nambari 31.

وَأَلَيْهِ مَقَاب

**“...na Kwake Yeye ndio marejeo yangu.”**

Maana yake: Marejeo yangu na hatima yangu. Na Kauli Yake تعالى:

وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ حُكْمًا عَرَبِيًّا

**“Na ndio kama hivi Tumeiteremsha Qur’ani kuwa ni hukumu kwa lugha ya Kiarabu.”**

Maana yake: Kama Tulivyowapeleka kabla yake Mitume na Tukateremsha juu yao vitabu kutoka mbinguni, kama hivyo Tumeteremsha juu yako Qur’ani hali ya kuwa imetengezwa vizuri ikiwa katika lugha ya Kiarabu. Tumekutukuza kwa Qur’ani Tukufu hiyo na Tumekufanya bora juu ya wasio kuwa wewe. Kwa sababu ya kitabu hiki kinachoyaweka wazi mambo na kilicho wazi ambacho,

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤١﴾

**“Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Msifiwa.” (41:42)**

Na Kauli Yake:

وَلِيْنَ أَتَّبَعَتْ أَهْوَاءَهُمْ

**“Na ukifuata matamano yao...”** Maana yake: Rai zao,

بَعْدَ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ

**“...baada ya kukujia ilimu hii...”**

Kutoka kwa Allah تعالى, kila Sifa Njema ni Kwake.

مَا لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَلَا وَاقٍ ﴿٤٢﴾

**“...hutakuwa na rafiki wala mlinzi mbele ya Mwenyezi Mungu.”**

Na hayo ni kemeo kwa wajuzi kwa kufuata njia za watu wa upotovu, baada kuifuata Sunna ya Mtume ﷺ na njia yake ambayo amekuja nayo bora ya Rehma na Amani ziwe juu yake.

\* \* \*

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ وَجَعَلْنَا لَهُمْ أَزْوَاجًا وَذُرِّيَّةً  
 وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِبَيِّنَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ لِكُلِّ أَجَلٍ  
 كِتَابٌ ﴿٣٨﴾ يَمْحُوا اللَّهُ مَا يَشَاءُ وَيُثَبِّتُ<sup>ط</sup> وَعِنْدَهُ أُمُّ  
 الْكِتَابِ ﴿٣٩﴾ وَإِنْ مَا تُرِيدُكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ  
 تَتَوَفَّيْنَاكَ فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٤٠﴾ أَوَلَمْ  
 يَرَوْا أَنَّا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا<sup>ع</sup> وَاللَّهُ يَحْكُمُ لَا  
 يُعْقَبُ لِحُكْمِهِ<sup>ع</sup> وَهُوَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤١﴾ وَقَدْ مَكَرَ  
 الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَلِلَّهِ الْمَكْرُ جَمِيعًا<sup>ط</sup> يَعْلَمُ مَا تَكْسِبُ كُلُّ  
 نَفْسٍ<sup>ط</sup> وَسِعِلَّمُ الْكُفْرَ لِمَنْ عُقِيَ الدَّارِ ﴿٤٢﴾ وَيَقُولُ  
 الَّذِينَ كَفَرُوا لَسْتَ مُرْسَلًا قُلْ كَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي  
 وَبَيْنَكُمْ وَمَنْ عِنْدَهُ عِلْمُ الْكِتَابِ ﴿٤٣﴾

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلًا مِّن قَبْلِكَ  
 وَجَعَلْنَا لَهُمْ أَزْوَاجًا وَذُرِّيَّةً<sup>ع</sup> وَمَا كَانَ  
 لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِبَيِّنَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ<sup>ط</sup>  
 لِكُلِّ أَجَلٍ كِتَابٌ ﴿٣٨﴾ يَمْحُوا  
 اللَّهُ مَا يَشَاءُ وَيُثَبِّتُ<sup>ط</sup> وَعِنْدَهُ أُمُّ  
 الْكِتَابِ ﴿٣٩﴾

**38. Na hakika Sisi Tulikwisha watuma Mitume kabla yako, na Tukajaalia wawe na wake na dhuriya. Na haiwi kwa Mtume kuleta miujiza isipo kuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Kila kipindi kina hukumu yake.**

**39. Mwenyezi Mungu Hufuta na Huthibitisha Ayatakayo. Na asili ya hukumu zote iko Kwake.**

**Mitume Walikuwa Wanadamu**

Allah تعالى Anasema: Na kama Tulivyokupeleka wewe Ee Muhammad kuwa Mjumbe binadamu, ndivyo pia Tulivyowapeleka Mitume kabla yako hali ya kuwa ni binadamu, wanakula, wanakwenda sokoni. Na wanawajamii wake zao, na wana watoto. Na Tumewajaalia wao wake na watoto. Na kwa hakika Amesema Allah تعالى Kumuambia, Mtukufu wa Mitume na wa mwisho wao,

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ

**“Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi.”  
 (18:110)**



Imeandikwa katika Sahihi Mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَمَا أَنَا فَأَصُومُ وَأُفْطِرُ، وَأَقْرُمُ وَأَنَا، وَأَكُلُ اللَّحْمَ، وَأَتَزَوَّجُ النِّسَاءَ، فَمَنْ رَغِبَ  
عَنْ سُئِي فَلَيْسَ مِنِّي»

*“Ama mimi ninafunga na ninafungua, na ninasimama kwa ibada usiku na ninalala, na ninakula nyama na ninaoa wanawake, kwa hiyo mwenye kwenda kinyume na mwenendo wangu basi huyo si katika mimi.”<sup>1</sup>*

Mtume ﷺ Yeyote Hawezi Kuleta Miujiza Isipokuwa kwa Amri ya Allah تعالی

Kauli Yake:

وَمَا كَانَ لِرَسُولٍ أَنْ يَأْتِيَ بِغَايَةٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ<sup>٥</sup>

***“Na haiwi kwa Mtume kuleta miujiza isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu.”***

Maana yake: Hawezi kuwatendea watu wake, jambo ambalo ni kinyume na mazoea yao isipokuwa atakapoidhinishwa katika jambo hilo na Allah تعالی, jambo hilo halifanyi yeye, bali ni Allah تعالی, Anafanya Analolitaka na Anahukumu lile ambalo Analolitaka.

لِكُلِّ أَجَلٍ كِتَابٌ

***“Kila kipindi kina hukumu yake.”***

Maana kila muda uliyowekwa una maandishi yaliyoandikwa huhusu muda huo na kila kitu kilicho mbele yake, kina kiasi chenye kujulikana.

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِنَّ ذَلِكَ فِي كِتَابٍ<sup>٥</sup> إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ

يَسِيرٌ ﴿٧٠﴾

***“Je! Hujui kwamba Mwenyezi Mungu Anayajua yaliomo mbinguni na katika ardhi? Hakika hayo yamo Kitabuni. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.” (22:70).***

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 9:5, Muslim 2:1020.

**Mambo Yanayoyofutwa na Kuondoshwa Katika Kadari ya Allah تعالى**

Kauli ya Allah تعالى:

يَمْحُوا اللَّهُ مَا يَشَاءُ

**“Mwenyezi Mungu Hufuta Ayatakayo.”** Katika mambo.

وَيُثَبِّتُ<sup>ع</sup>

**“...na Huthibitisha...”**

Anakusudia hadi yote yaliyoondoshwa na Qur’ani ambayo Ameiteremsha Allah تعالى juu ya Mjumbe ﷺ. Na amesema Mujahid:

يَمْحُوا اللَّهُ مَا يَشَاءُ وَيُثَبِّتُ<sup>ع</sup>

**“Mwenyezi Mungu Hufuta na Huthibitisha Ayatakayo.”**

Isipokuwa Maisha na kifo na hali mbaya na njema, hivyo havibadiliki.<sup>1</sup> Na amesema Mansur nilimuuliza Mujahid nikasema: ‘Je, unayaonaje maombi ya mmoja wetu?’ Anasema: ‘Ee Mola wangu wa haki, likiwa jina langu limo katika watu wema basi lithibitisha katika hao watu wema, na likiwa katika waovu basi lifute kuliepusha nao na lifanye katika watu wema?’ Akasema: ‘Vizuri.’ Kisha nikakutana naye baada ya hapo kwa muda wa mwaka au zaidi nikamuuliza kuhusu hilo, akasema:

إِنَّا أَنْزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةٍ مُبَارَكَةٍ<sup>ع</sup>

**“Hakika Tumekiteremsha katika usiku uliobarikiwa.” (44:3)**

Amesema: yanahukumiwa katika usiku wa cheo mambo yatakayojiri katika mwaka wote miongoni mwa riziki au masaibu, kisha Hutanguliza Anachokitaka na Anakichelewesha, Anachokitaka. Ama maandishi ya wema na waovu hiyo ni yenye kuthibiti hayabadiliki.<sup>2</sup> Na amesema Al-Aamashi kutoka kwa Abii Wail, Shaqiq bin Salama kwamba yeye mara nyingi alikuwa anaomba kwa maombi haya; ‘Ee Mola wangu wa haki ukiwa Umetuandika hali ya kuwa waovu,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:479.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:480.

yafute hayo na tuandike hali ya kuwa wema. Na ukiwa Umetuandika hali ya kuwa wema basi tuthibitisha kwani Wewe Unafuta unachokitaka na Unakithibitisha, na mbele Yako kuna mama wa vitabu vyote, na maandishi yote.<sup>1</sup>

Na amepokea Ibn Jariri. Kauli kama hiyo, zimepokewa kutoka kwa Umar bin Al-Khattab, na Ibn Mas'ud رضي الله عنهما. Maana ya kauli hizo ni kwamba katika Kadari, Anafuta Allah تعالى Anayoyataka katika hayo na mengine Huyaacha kama yalivyo. Hili linathibitishwa, na thibitisho zaidi ni Alichonukuu Imam Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Thabwan alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيُحْرَمُ الرِّزْقَ بِالدَّنْبِ يُصِيبُهُ، وَلَا يَرُدُّ الْقَدَرَ إِلَّا الدُّعَاءُ، وَلَا يَزِيدُ فِي  
الْعُمْرِ إِلَّا الْبِرُّ»

*“Kwa hakika mtu hunyimwa riziki kwa madhambi anayoyatenda na hayarudishi makadirio (Qadar) isipokuwa maombi na hauongezi umri wa mtu isipokuwa wema.”*

Ameipokea Annasai na Ibn Majah.<sup>2</sup> Na imethibiti katika Hadithi sahihi kwamba kuunga udugu kunaongeza umri.<sup>3</sup>

Na imekuja Hadithi nyingine inayothibitisha kuwa dua na kadari zinakinzana baina ya mbingu na Ardhi.

Na amesema Al -Aufi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake:

يَمْحُوا اللَّهُ مَا يَشَاءُ وَيُثَبِّتُ<sup>ط</sup> وَعِنْدَهُ أُمُّ الْكِتَابِ ﴿٥٦﴾

***“Mwenyezi Mungu Hufuta na Huthibitisha Ayatakayo. Na asili ya hukumu zote iko Kwake.”***

Anasema huyo ni mtu ambaye anatenda matendo muda mrefu ya kumtii Allah تعالى kisha anarejea kwenye kumuasi Allah تعالى, kwa hiyo anakufa juu ya upotevu, hivyo ndivyo Yeye Anavyofuta. Na yale ambayo Anayathibitisha, ni mtu anayetenda maasi, kwa hakika imetangulia kwake kheri, mpaka akafa na

<sup>1</sup> At-Tabari 16:481.

<sup>2</sup> Ahmad 5:227, Ibn Majah na. 90.

<sup>3</sup> Muslim na. 2557.

hali ya kuwa yeye yuko katika kumtii Allah تعالى, huyo ndiye ambaye Anamthibitisha.<sup>1</sup> Imepokewa kutoka kwa Saeed Bin Jubair kwamba aya hiyo ni kwa maana ya,

فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٤﴾

***“Kisha Anamsamehe amtakaye na Anamuadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”(2:284)<sup>2</sup>***

وَإِن مَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَقَّيَنَّكَ فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿٢٨٥﴾  
 أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا ۗ وَاللَّهُ يَحْكُمُ لَا مُعَقَّبَ لِحُكْمِهِ ۗ وَهُوَ  
 سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٢٨٦﴾

**40. Na ikiwa Tukikuonesha baadhi ya Tuliyoahidi au Tukakufisha kabla yake, juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hisabu.**

**41. Je! Hawakuona kwamba Tunaifikia ardhi Tukiipunguza nchani mwake? Na Mwenyezi Mungu Huhukumu, na hapana wa kupinga Hukumu Yake, Naye ni Mwepesi wa Kuhisabu**

**Ni Juu ya Mtume Kufikisha na ni Juu ya Allah تعالى Kuhesabu**

Allah تعالى Anasema Akimuambia Mjumbe wake ﷺ,

وَإِن مَّا نُرِيَنَّكَ

***“Na ikiwa Tukikuonesha...”***

Ee Muhammad ﷺ baadhi ya yale ambayo Tunawaahidi maadui zake, miongoni mwa kudhalilishwa na kuteswa hapa duniani.

أَوْ نَتَوَقَّيَنَّكَ

***“...au Tukakufisha...”*** Kwa maana: Kabla ya hilo.

<sup>1</sup> At-Tabari 16:483.

<sup>2</sup> Al-Qurtubi 9:331.

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ

**“...juu yako wewe ni kufikisha ujumbe.”**

Maana yake: Hakika hapana jambo jingine Tumekupeleka ili uwafikishie ujumbe wa Allah تعالى na kwa hakika umefanya lile ambalo umeamrisha.

وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ

**“...na juu Yetu ni hisabu.”**

Kwa maana: Hesabu na malipo yao kama Alivyosema Allah تعالى,

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ﴿٣٨﴾ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ﴿٣٩﴾ إِلَّا مَنْ تَوَلَّى وَكَفَرَ ﴿٤٠﴾  
فِيُعَذِّبُهُ اللَّهُ الْعَذَابَ الْأَكْبَرَ ﴿٤١﴾ إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٤٢﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُمْ ﴿٤٣﴾

**“Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia. Lakini anayerudi nyuma na kukataa, Basi Mwenyezi Mungu Atamuadhibu kwa adhabu iliyo kubwa kabisa! Hakika ni Kwetu Sisi ndio marejeo yao. Kisha hakika ni juu Yetu Sisi hisabu yao!” (88:21-26)**

Kisha Allah تعالى Akasema,

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا

**“Je! Hawakuona kwamba Tunaifikia ardhi Tukiipunguza nchani mwake?”**

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, ‘Hivi hawaoni kwamba Sisi Tunamfungulia Muhammad ﷺ ardhi baada ya ardhi.’<sup>1</sup> Na amesema Al-Hassan na Adh - Dhahak huko ni kupata ushindi kwa Waislamu juu ya Mushrikina.<sup>2</sup> Kama ilivyo Kauli Yake:

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِنَ الْقُرَىٰ

**“Na hakika Tuliangamiza miji ilio jirani zenu,...” (46:27)**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:493.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:494.

وَقَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَلِلَّهِ الْمَكْرُ جَمِيعًا ۗ يَعْلَمُ مَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ ۗ وَسِعِلَّمُ الْكُفْرَ  
لِمَنْ عُقِيَ الدَّارِ ﴿٤٢﴾

**42. Na walipanga waliokuwa kabla yao, lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Mipango yote. Yeye Anajua inayochuma kila nafsi. Na makafiri watajua ni ya nani nyumba ya mwisho Akhera!**

**Vituko vya Makafiri na Karipio Juu ya Hilo**

Allah تعالی Anasema:

وَقَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

**“Na walipanga waliokuwa kabla yao,”**

Waliwafanyia vituko Mitume wao na wakataka kuwatoa katika miji yao Akawalipa Allah تعالی vituko vyao na Akaufanya mwisho mwema ni wa wale wenye kumcha Allah تعالی. Kama ilivyo Kauli Yake:

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ ۗ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ ۗ وَاللَّهُ خَيْرٌ الْمَكْرِينَ ﴿٤٣﴾

**“Na (kumbuka Ee Nabii Muhammad) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakutoe (kwa hali mbaya katika makka); na wakafanya hila (zao barabara). Na Mwenyezi Mungu Akazipitundua hila hizo. Na Mwenyezi Mungu ni M-bora wa kupindua hila. (za watu wabaya).” (8:30) na,**

وَمَكْرُوا مَكْرًا وَمَكْرَنَا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٤﴾ فَأَنْظِرْ كَيْفَ كَانَ عَنِيبَةً  
مَكْرِهِمْ أَنَا دَمَرْنَاهُمْ وَقَوْمَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٥﴾

**“Basi wakapanga mipango yao, na Sisi Tukapanga Mipango Yetu, na wao hawatambui. Basi angalia ulivyokuwa mwisho wa mipango yao, ya kwamba Tuliwaangamiza wao pamoja na watu wao wote.” (27:50-51)**

Kisha Allah تعالی Akasema.

يَعْلَمُ مَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ ۗ

**“Yeye Anajua inayochuma kila nafsi.”**

Kwa maana: Yeye Peke Yake Anajua siri na fikra zilizojificha. Na Atamlipa kila mmoja kulingana na vitendo vyake. Na aina nyingine ya usomaji,

(وَسِعَتْ كَافِرًا)

(Na kafiri atajua...) Kafiri (*kafir*) ataelewa,

الْكُفْرُ

**"Na makafiri..." Kuffar (makafiri).**

لِمَنْ عَقَى الدَّارِ

**"...ni ya nani nyumba ya mwisho Akhera!"**

Maana yake: Mzunguuko na mwisho utakuwa wa nani ni wao au ni wa Mitume? Hapana bali mwisho mwema ni wa wafuasi wa Mitume duniani na akhera. Ni za Allah تعالى tu Sifa Njema na Neema.

وَيَقُولُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَسْتَ مُرْسَلًا قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ وَمَنْ عِنْدَهُ

عِلْمُ الْكِتَابِ ﴿٤٣﴾

**43. Na waliokufuru wanasema: Wewe hukutumwa. Sema: Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi, na pia yule mwenye ilimu ya Kitabu.**

**Anatosha Mwenyezi Mungu na Wale Ambao Iko Mbele Zao Elimu ya Kitabu kuwa Mashahidi wa Ujumbe wa Mtume ﷺ**

Allah تعالى Anasema wanakukadhibisha hawa makafiri na wanasema:

لَسْتَ مُرْسَلًا

**"Wewe hukutumwa."** Maana yake: Hakukupeleka Allah تعالى.

قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ

**"Sema: Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi."**

Maana yake: Tegemeo langu ni Allah تعالى na Yeye Ndiye Mwenye Kushuhudia baina yangu na nyinyi, ni Mwenye Kushuhudia juu yangu kwa niliyoyafikisha kutoka Kwake miongoni mwa ujumbe, na ni Mwenye Kushuhudia juu yenu enyi wenye kukadhibisha katika mnachokijua miongoni mwa uzushi. Na Kauli Yake.

وَمَنْ عِنْدَهُ عِلْمٌ الْكِتَابِ

**“...na pia yule mwenye ilimu ya Kitabu.”**

Pamesemwa kuwa aya hii ilimshukia Abdillahi bin Salaam, ameyasema hayo Mujahid<sup>1</sup> na kauli hii ni ngeni kwa sababu aya hii imeshuka Makkah na Abdillahi bin Salaam, hakika si vinginevyo, alisilimu mwanzoni mwa kufika kwa Mtume ﷺ Madina. Na kauli yenye nguvu katika maneno haya ni ile aliyosema Al-Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema hao ni Mayahudi na Manaswara.<sup>2</sup> Na amesema Qatadah: Katika wao ni Ibn Salaam, Salman na Tamim Addaari.<sup>3</sup> Na kauli Sahihi katika maelezo haya ni kwamba,

وَمَنْ عِنْدَهُ

**“...na pia yule mwenye...”**

Ni jina linalokusanya wanawazuoni wa watu wa kitabu, ambao wanaikuta sifa ya Mtume Muhammad ﷺ na maelezo yake katika vitabu vyao vilivyotangulia, miongoni mwa ishara mbalimbali za Mitume wao kuhusu yeye Muhammad ﷺ. Kama Anavyosema Allah تعالى:

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ۚ فَسَأَكْتُمِبَا لِلَّذِينَ يُتَّقُونَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَالَّذِينَ هُمْ  
بِعَابَتِنَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٨﴾ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا  
عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ

**“...Na Rehema Yangu imeenea kila kitu. Lakini Nitawaandikia khasa wanao mchamungu, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara Zetu. Ambao kwamba wanamfuata huyo**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:502.

<sup>2</sup> Kama hapo juu.

<sup>3</sup> Tabari 16:503.



***Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, .... (7:156-157) na,***

أَوَلَمْ يَكُنْ لَهُمْ آيَةٌ أَنْ يَعْلَمَهُرُ غُلَمَتُوا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٧٧﴾

***“Je! Haikuwa kwao ni Ishara kwamba wanayajua haya wanazuoni wa Wana wa Israili?” (26:197)***

Katika zile aya ambazo ndani yake pana maelezo yanayowahusu wanawazuoni wa Wana Israili, kwamba wao wanalielewa jambo hilo kutokana na vitabu vyao vilivyoteremshwa.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya Suratu Ar-Raad. Na ni za Allah تعالى tu Sifa Njema na Kuneemesha.

\* \* \*

## Tafsiri ya Suratu Ibrahim

### Sura ya 14

#### Iliteremshwa Makkah

#### سُورَةُ إِبْرَاهِيمَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّ كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ  
إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ رَبِّهِمْ إِلَى صِرَاطٍ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿١﴾ اللَّهُ  
الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَوَيْلٌ  
لِلْكَافِرِينَ مِنْ عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يَسْتَحِبُّونَ  
الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ  
وَيَبْغُونَهَا عِوَجًا ۗ أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٣﴾ وَمَا أَرْسَلْنَا  
مِنْ رُسُلٍ إِلَّا بِلِسَانٍ قَوْمِهِمْ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ فَيُضِلُّ اللَّهُ  
مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤﴾ وَلَقَدْ  
أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا أَنْ أَخْرِجْ قَوْمَكَ مِنَ  
الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَذَكِّرْهُمْ بِآيَاتِنَا ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ  
لَآيَاتٍ لِكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٥﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّ كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ  
النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ بِإِذْنِ  
رَبِّهِمْ إِلَى صِرَاطٍ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿١﴾  
اللَّهُ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا  
فِي الْأَرْضِ ۗ وَوَيْلٌ لِّلْكَافِرِينَ مِنْ  
عَذَابٍ شَدِيدٍ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يَسْتَحِبُّونَ  
الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ  
وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَيَبْغُونَهَا  
عِوَجًا ۗ أُولَٰئِكَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٣﴾

1. Alif Lam Ra. (A.L.R.) Hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha kwako ili uwatoe watu kwenye giza uwapeleke kwenye muwangaza, kwa idhini ya Mola wao Mlezi, uwafikishe kwenye Njia ya Mwenye Nguvu, Msifiwa.

2. Naye ni Mwenyezi Mungu Ambaye ni Vyake Yeye vyote viliomo katika mbingu na ardhi. Na ole wao makafiri kwa adhabu kali!

3. Wale wanaofadhilisha maisha ya dunia kuliko Akhera, na wanawazuilia watu wasifuate njia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotisha. Hao wamepotelea mbali.

## Taarifa Juu ya Qur'an Tukufu na Makusudio Yake, na Adhabu Kali ni ya Mwenye Kwenda Kinyume Nayo

Yametangulia maelezo juu ya herufi za mkato mwanzoni mwa sura mbalimbali.

كَتَبْنَا أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ

**"Hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha kwako..."**

Maana yake: hiki ni kitabu Tumekiteremsha kwako Ee Muhammad ﷺ nacho ni Qur'ani Tukufu ambayo ni kitabu kitukufu sana ambacho Amekiteremsha Allah kutoka mbinguni kwa Mtume ﷺ Aliyempeleka katika ardhi kwa watu wake wote Waarabu wao na Waajemi wao.

لُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

**"...ili uwatoe watu kwenye giza uwapeleke kwenye mwangaza,..."**

Maana yake: Kwa hakika Tumekupeleka Ee, Muhammad ﷺ pamoja na Kitabu hiki ili uwatoe watu katika lile ambalo wao wamo ndani yake miongoni mwa upotevu uwapeleke kwenye uongofu. Kama Alivyosema Allah تعالى:

اللَّهُ وَلِيُّ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُخْرِجُهُمْ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَوْلِيَاؤُهُمُ  
الطَّاغُوتُ يُخْرِجُونَهُمْ مِنَ النُّورِ إِلَى الظُّلُمَاتِ

**"Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Huwatoa gizani na Kuwaingiza mwangazani. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni Mashetani. Huwatoa kwenye mwangaza na kuwaingiza gizani." (2:257) na**

هُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ عَلَىٰ عَبْدِهِ ءَايَاتٍ بَيِّنَاتٍ لِّيُخْرِجَكُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

**"Yeye Ndiye Anayemteremshia mja wake Aya zinazobainisha wazi ili Akutoeni gizani muingie kwenye nuru." (57:9)**

Na Kauli Yake تعالى،

بِإِذْنِ رَبِّهِمْ

**"...kwa idhini ya Mola wao Mlezi."**

Yeye Humuongoza aliyepangiwa kuongoka, mikononi mwa Mjumbe wake ﷺ aliyepolekwa kwa Amri Yake kuwaongoza,

إِلَىٰ صِرَاطِ الْعَزِيزِ

**“...kwenye njia ya Mwenye Nguvu,...”** Mwenye Kushinda Asiyezuiwa na hashindani bali Yeye Ndiye Mwenye Kukitenza nguvu kila kisichokuwa Yeye.

الْحَمِيدِ

**“Msifiwa,”** Maana yake: Mwenye Kusifiwa katika Vitendo Vyake vyote na Maneno Yake na Sheria Yake na Maamrisho Yake na Makatazo Yake Ambaye ni Mkweli katika Kutoa habari. Na Kauli Yake.

اللَّهُ الَّذِي لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ

**“Naye ni Mwenyezi Mungu Ambaye ni Vyake Yeye vyote vilimo katika mbingu na ardhi.”**

Wamesoma baadhi ya wanazuoni **“Allahu”** kwa kuweka irabu ya (*dhuma*) mwisho wa neno **“Allahu”** hali wamesoma wengine juu ya kufuatishia **“Allahi”** kwa kuweka irabu ya *kasra*, ikiwa ni sifa na kivumishi ya tamko tukufu (Allah تعالى) kama Alivyosema Allah تعالى:

قُلْ يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ اِنِّي رَسُوْلُ اللّٰهِ اِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

**“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliyetumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi.” (7:158).**

Na Kauli Yake,

وَوَيْلٌ لِّلْكَافِرِيْنَ مِنْ عَذَابٍ شَدِيْدٍ

**“Na ole wao makafiri kwa adhabu kali!”** Maana yake: Maangamivu ni yao siku ya Kiyama kwa sababu wamekwenda kinyume na wewe Ee Muhammad ﷺ na wamekukadhibisha. Kisha Amewaeleza kwamba wao wanayapenda maisha ya dunia juu ya akhera. Maana wanayatanguliza na wanayapa kipaumbele juu ya akhera na wanatenda kwa ajili ya dunia na wameisahau akhera na wameiacha nyuma ya migongo yao

وَيَصُدُّوْنَ عَن سَبِيْلِ اللّٰهِ

**“...na wanawazuilia watu wasifuate njia ya Mwenyezi Mungu,...”** Nayo ni kuwafuata Mitume.

وَيَبْغُوهَا عِوَجًا ۗ

"...*na wanataka kuipotosha.*" Maana yake: Wanapenda njia ya Allah تعالى iwe kombo yenye kupondoka, yenye kwenda upande. Na njia hiyo ni yenye kunyooka katika dhati yake, haidhuru, mwenye kwenda kinyume nayo wala mwenye kuiacha. Kwa hiyo wao kwa kutaka hilo, wamo katika ujinga na upotevu ulio mbali na ukweli, hawatarajiwi kwa hali hiyo kuwa watatengenekewa.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَّسُولٍ إِلَّا بِلِسَانٍ قَوْمِهِ لِيُبَيِّنَ لَهُمْ فَيُضِلُّ اللَّهُ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٤﴾

**4. Wala hatukumtuma Mtume ila kwa ulimi wa kaumu yake ili apate kuwabainishia. Basi Mwenyezi Mungu Humuacha akapotea amtakaye, na Akamuongoa amtakaye. Naye ni Mtukufu Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.**

**Kila Mtume ﷺ Amepelekwa kwa Lugha ya Watu Wake Ili Uwe Wazi Uongofu au Upotevu**

Huu ni katika upole wa Allah تعالى kwa viumbe Wake, kwamba Anawapelekea Mitume miongoni mwao kwa lugha zao ili wafahamu kutokana na wao yale wanayoyataka, na ujumbe uliofunuliwa kwao. Na Kauli Yake,

فَيُضِلُّ اللَّهُ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ

**"Basi Mwenyezi Mungu Humuacha akapotea Amtakaye, na akamuongoa Amtakaye."**

Baada ya kuweka wazi na kusimamisha hoja juu yao, Allah تعالى Humpoteza amtakaye na Kumuepusha na uongofu, na Humuongoza amtakaye kwenye ukweli.

وَهُوَ الْعَزِيزُ

**"Naye ni Mtukufu Mwenye Nguvu..."**

Ambaye Analolitaka linakuwa na ambalo Hakulitaka haliwi.

الْحَكِيمُ

**"Mwenye Hikima."** Katika Matendo Yake kwa hiyo Humpoteza anayestahiki kupotezwa, na Anamuongoza anayestahiki hilo, na kwa hakika ulikuwa huu

ndiyo utaratibu Wake kwa viumbe Wake kwamba Yeye Hakumpeleka Mtume katika umma isipokuwa anakuwa kwa lugha yao, kwa hiyo Amemhusisha kila Mtume kuufikisha ujumbe wake kwa umati wake kinyume cha watu wengine. Na Amemhusisha Muhammad bin Abdillahi ﷺ aeneze ujumbe wake kwa watu wote kama ilivyothibitika katika sahihi ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Jabir رضي الله عنه, Mtume ﷺ amesema,

أَعْطَيْتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ،  
وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا، وَأَجَلْتُ لِي الْعَنَابِمْ وَلَمْ تُحَلِّ لِأَحَدٍ قَبْلِي،  
وَأَعْطَيْتُ الشَّفَاعَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ يَبْعُثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً وَيُبْعِثُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً<sup>1</sup>

*“Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa Mtume yeyote wa kabla yangu. Nimenusuriwa kwa khofu mwendo wa mwezi, na imefanywa kwangu ardhi kuwa msikiti na ni kitu cha kujitwahaishia kilicho safi, na zimehalalishwa kwangu ngawira na hazikuhalalishwa kwa yeyote kabla yangu; na nimepewa uombezi, na alikuwa Mtume anapelekwa kwa watu wake tu na nimepelekwa kwa watu wote.”<sup>1</sup>*

Allah تعالى Amesema,

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

**“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote,”  
(7:158)**

Sema enyi watu hakika mimi ni Mjumbe wa Allah kwenu nyote.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ بِآيَاتِنَا أَنْ أَخْرِجْ قَوْمَكَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ وَذَكِّرْهُمْ  
بِآيَاتِ اللَّهِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ ﴿٥٠﴾

**5. Na Tulimtuma Musa pamoja na miujiza Yetu, Tukamuambia:  
Watoe watu wako kwenye giza uwapeleke kwenye mwangaza.  
Na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu. Hakika katika hayo  
zipo ishara kwa kila mwenye kusubiri akashukuru.**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 1:519, Muslim 1:370.

### Kisa cha Musa عليه السلام na Watu Wake

Allah تعالى Anasema, 'Kama Tulivyokutuma (ewe Muhammad ﷺ) na kukuteremshia Kitabu ili uwatoe watu gizani kwenda kwenye nuru.' Pia Tulimtuma Musa عليه السلام kwa Bani Israili pamoja na aya Zetu. Amesema Mujahid hiyo ni ile miujiza tisa.

أَنْ أُخْرِجَ قَوْمَكَ

**“Watoe watu wako...”** Maana yake: Tulimuamrisha hali ya kusema:

أَنْ أُخْرِجَ قَوْمَكَ مِنْ أَلْظُلْمَتِ إِلَى الْنُورِ

**“Watoe watu wako kwenye giza uwapeleke kwenye mwangaza.”**

Maana yake: Walinganie kwenye kheri ili uwatoe katika giza walilomo, kama vile ujinga na upotevu, kwenda kwenye nuru ya uongofu na busara ya imani.

وَذَكِّرْهُمْ بِأَيِّمِ اللَّهِ

**“Na uwakumbushe siku za Mwenyezi Mungu.”**

Maana yake: Misaada Yake na Neema Zake juu yao katika Kuwatoa wao katika kutekwa na Firauni na kuteza nguvu kwake na dhulumu yake, na Kuwaokoa wao na adui wao, na Kupasua bahari na Kuwafunika wingu na Kuwateremshia Manna na Salwa na neema nyingine nyingi. Ameyasema hayo Mujahid na Qatada na wengine.<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّكُلِّ صَبَّارٍ شَكُورٍ

**“Hakika katika hayo zipo ishara kwa kila mwenye kusubiri akashukuru.”**

Maana yake: Katika Tuliowafanyia wapenzi wetu Bani Israili. Tulipowaokoa mikononi mwa Firauni, na Tukawaokoa dhidi ya adhabu ya kudhalilisha. Ni fundisho kwa anayefanya subira wakati wa shida, na mwenye kushukuru wakati wa neema. Kama alivyosema Qatadah: Mja bora ni anayesubiri anapoonjwa na anashukuru anapopewa.<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Muslim 4:2295.

<sup>2</sup> Muslim 4:1995.

Imeandikwa katika Sahihi kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَمْرَ الْمُؤْمِنِ كُلَّهُ عَجَبٌ، لَا يَقْضِيهِ اللَّهُ لَهُ قَضَاءٌ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، إِنْ أَصَابَتْهُ  
ضُرٌّ صَبَرَ، فَكَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ سُرَّةٌ شَكَرَ، فَكَانَ خَيْرًا لَهُ»

*“Kwa hakika mambo ya muumini yote yanastaajibisha, Allah تعالى Hahukumu Hukumu Yoyote isipokuwa inakuwa Kheri kwake, yakimpata madhara ana subiri, na hiyo inakuwa ni kheri kwake; na ikimpata furaha anashukuru na inakuwa ni kheri kwake.”<sup>1</sup>*

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Muslim 4:2295.



وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ اذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ  
 أَخْرَجَكُمْ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ  
 وَيَدْمِغُونَ أُنْبَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ ۗ وَفِي  
 ذَلِكَ بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ ﴿٦﴾ وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكُمْ  
 لَئِن شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ ۖ وَلَئِن كَفَرْتُمْ إِنَّ عَذَابِي  
 لَشَدِيدٌ ﴿٧﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ إِنَّ تَكْفُرُوا أَنْتُمْ فِي الْأَرْضِ  
 جَمِيعًا فَإِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٨﴾ أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبُؤُا  
 الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ ۗ وَالَّذِينَ  
 مِن بَعْدِهِمْ لَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا اللَّهُ ۗ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ  
 فَرَدُّوا أُنْدِيَهُمْ فِي أَقْوَاهِهِمْ وَقَالُوا إِنَّا كَفَرْنَا بِمَا أُرْسِلْتُمْ  
 بِهِ وَإِنَّا لَفِي شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَنَا إِلَيْهِ مُرِيبٌ ﴿٩﴾

### 6. Na Musa alipowaambia

*watu wake: Kumbukeni Neema ya Mwenyezi Mungu Aliyokujaalieni, pale Alipokuoieni kutokana na watu wa Firauni waliokupeni adhabu mbaya kabisa, wakiwachinja wenenu wanaume, na wakiwawaacha hai wanawake. Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa unaotoka kwa Mola wenu Mlezi.*

**7. Na Alipotangaza Mola wenu Mlezi: Mkishukuru Nitakuzidishieni; na Mkikufuru, basi Adhabu Yangu ni Kali.**

**8. Na Musa alisema: Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitoshia, Msifiwa.**

Allah تعالیٰ Anasema Akimuelezea Musa عليه السلام wakati Alipowakumbusha watu wake, kuhusu Misaada ya Allah تعالیٰ kwao na Neema Zake juu yao, Alipowaokoa na jamaa za Firauni dhidi ya mateso na udhalilishaji wao. Pindi walipokuwa wanawachinja wale wanaowakuta miongoni mwa watoto wao wa kiume, na

wanawaacha watoto wao wa kike, Akawaokoa wao Allah تعالى na mambo hayo na hii ni neema kubwa sana. Na kwa sababu hii Amesema:

وَفِي ذَٰلِكُمْ بَلَاءٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَظِيمٌ

**“Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa unaotoka kwa Mola wenu Mlezi.”**

Maana yake: Neema kubwa kutoka Kwake kuja Kwenu. Katika jambo hilo nyinyi mnashindwa kusimama kwa kuishukuru neema hiyo. Na pamesemwa: na katika yale ambayo walikuwa Anawafanyia nyinyi watu wa Firauni miongoni mwa matendo hayo,

بَلَاءٌ

**“...mtihani...”**

Maana yake: Majaribu makubwa na inawezekana kuwa makusudiwa ya majaribu haya. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi Sana.

Kama ilivyo Kauli Yake Allah تعالى،

وَيَلَوْنَهُمْ بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿١٦٨﴾

**“Na Tukawajaribu kwa Mema na Mabaya ili Wapate Kurejea.”**  
**(7:168)**

Na Kauli Yake:

وَإِذْ تَأَذَّرَ رَبُّكُمْ

**“Na Alipotangaza Mola Wenu Mlezi...”**

Maana yake: Amewatangazia na Akawafahamisha Ahadi Yake kwenu. Na Inawezekana maana yake: Na kumbuka alipoapa Bwana wenu na kiapo cha Ushindi Wake katika mambo na Utukufu Wake na Ukubwa Wake.

Kama ilivyo katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِذْ تَأَذَّرَ رَبُّكَ لِيَبْعَثَنَّ عَلَيْهِمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ

**“Na pale Alipotangaza Mola wako Mlezi Kwamba Hapana Shaka Atawaletea Watu ambao watawaadhibu Kwa Adhabu Mbaya Mpaka Siku ya Kiyama.” (7:167)**

Iwapo mtashukuru Neema Zangu kwenu Nitawaongezea.

لَيْنِ شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ

**“Mkishukuru Nitakuzidishieni;...”**

Maana yake: Mkizikufuru neema na mkazifunika na mkazikanusha,

إِنَّ عَذَابِي لَشَدِيدٌ

**“...basi Adhabu Yangu ni Kali.”**

Hilo ni kwa Kuziondoshwa hizo neema kwenu na Kuwaadhibu kwa sababu ya Kuzikufuru neema. Na imekuja katika Hadithi.

«إِنَّ الْعَبْدَ لَيَحْرَمُ الرِّزْقَ بِالدَّنْبِ بِصِيئِهِ»

*“Kwa hakika mja hunyimwa riziki kwa sababu ya madhambi anayoyapata.”*

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَقَالَ مُوسَىٰ إِنَّ تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأَرْبُ اللَّهِ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ

**“Na Musa alisema: Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitosha, Msifiwa.”**

Maana: Yeye ni Mwenye Kujitosha si Mwenye kuhitaji shukurani za waja Wake na Yeye ni Mwenye Kusifu, Mwenye Kusifiwa hata wakufuru wale watakaomkufuru. Kama ilivyo Kauli Yake.

إِنَّ تَكْفُرُوا فَأَرْبُ اللَّهِ غَنِيٌّ عَنْكُمْ

**“Mkikufuru Basi Mwenyezi Mungu si Mwenye Haja Nanyi,...” (39:7)**

Na Kauli Yake تعالى,

فَكْفُرُوا وَتَوَلَّوْا وَأَسْتَفَعَى اللَّهُ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَمِيدٌ

**“Basi wakakufuru, na wakageuka upande. Mwenyezi Mungu Akawa Hana haja nao. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, si Mhitaji, naye ni Msifiwa.” (64:6)**

Imekuja katika sahihi Muslim kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ

katika yale anayoyapokea kutoka kwa Bwana wake Allah تعالى, amesema:

«يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَخْرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجِئْتُمْ كَانُوا عَلَىٰ أَنفَىٰ قَلْبِ رَجُلٍ وَاحِدٍ مِّنْكُمْ، مَا زَادَ ذَلِكَ فِي مُلْكِي شَيْئًا، يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَخْرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجِئْتُمْ كَانُوا عَلَىٰ أَنْفَجِرَ قَلْبِ رَجُلٍ وَاحِدٍ مِّنْكُمْ، مَا نَقَصَ ذَلِكَ فِي مُلْكِي شَيْئًا، يَا عِبَادِي لَوْ أَنَّ أَوْلَكُمْ وَأَخْرَكُمْ وَإِنْسَكُمْ وَجِئْتُمْ قَامُوا فِي صَعِيدٍ وَاحِدٍ، فَسَأَلُونِي، فَأَعْطَيْتُ كُلَّ إِنْسَانٍ مَّسْأَلَتَهُ، مَا نَقَصَ ذَلِكَ مِنْ مُلْكِي شَيْئًا إِلَّا كَمَا يَنْقُصُ الْمِخْيَطُ إِذَا أُدْخِلَ الْبَحْرَ»

*“Enyi waja Wangu! Lau kama wa mwanzo mpaka wa mwisho wenu, wanadamu na majini wenu wangekuwa katika moyo wa mchamungu zaidi kuliko nyinyi, basi hilo lisingezidisha chochote katika Ufalme Wangu. Enyi waja Wangu! Lau kama wa mwanzo na mpaka wa mwisho wenu, wanadamu na majini wenu, wangekuwa katika moyo wa muovu zaidi kuliko nyinyi, basi hilo lisingepunguza chochote katika Ufalme Wangu. Enyi waja Wangu! Lau kama wa mwanzo mpaka wa mwisho wenu, wanadamu na majini wenu, wangesimama katika uwanja mmoja, kisha wakaniomba, Ningempa kila mmoja alichokiomba, hakitapunguza chochote Katika Ufalme Wangu, bali ni kama inavyopunguza sindano inavyotumbukizwa baharini.”<sup>1</sup>*

Kwa hiyo Kutakasika ni Kwake na Kutukuka na Kujitosha na Kusifiwa Sana.

أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَبَأُ الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ ۗ وَالَّذِينَ مِن بَعْدِهِمْ لَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا اللَّهُ ۗ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَرَدُّوا أَيْدِيَهُمْ فِي أَفْوَاهِهِمْ وَقَالُوا إِنَّا كَفَرْنَا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ وَإِنَّا لَفِي شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَنَا إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٩﴾

**9. Je! Hazikukufikieni khabari za walio kabla yenu? Kaumu ya Nuhu, na A’adi, na Thamud, na walio baada yao, ambao hapana awajuaye ila Mwenyezi Mungu? Mitume wao waliwajia kwa hoja zilizowazi, na wao wakarudisha mikono yao kwenye vinywa vyao, wakasema: Hakika sisi tumeyakataa hayo mliyotumwa, na hakika sisi tuna shaka kubwa na mnyotuitia.**

<sup>1</sup> Muslim 4:1994.

**Ukadhibishaji wa Umma za Mwanzo kwa Mitume Wao na Yaliyopita Kati Yao**

Hii ni habari mpya kutoka kwa Allah تعالیٰ kwa Umma huu, kwani Allah تعالیٰ Ametusimulia habari za watu wa Nuh عليه السلام na Aad na Thamud na wasiokuwa hao katika umati mbalimbali, ambao waliwakadhibisha Mitume katika wale ambao hakuna anayejua idadi yao isipokuwa Allah تعالیٰ.

جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ

**“Mitume wao waliwajia kwa hoja zilizowazi,”**

Maana yake: Na hoja na dalili dhahiri zenye nguvu. Na amesema Ibn Is’haqa رحمه الله تعالیٰ kutoka kwa Amri bin Maymoun kuwa Abdillah amesema kuhusu Kauli Yake:

لَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا اللَّهُ

**“...ambao hapana awajuae ila Mwenyezi Mungu.”**

Wamesema urongo walioeleza nasabu za Mitume.<sup>1</sup> Amesema Urwa Bin Az-Zubair رضي الله عنه hatujamkuta yeyote anayejua nasaba ya watu walio baada ya Ma’ddi bin Adnan.<sup>2</sup>

Na Kauli Yake تعالیٰ:

فَرَدُّوا أَيْدِيَهُمْ فِي أَفْوَاهِهِمْ

**“...na wao wakarudisha mikono yao kwenye vinywa vyao,”**

Pamesemwa: Maana yake ni kwamba wao waliashiria mdomoni kwa Mitume, kwa kuwaamrisha kuwanyamazia wao wakati walipowalingania kwa Allah تعالیٰ.

Na pamesemwa: Bali waliweka mikono yao juu ya midomo yao, kwa kuwakadhibisha Mitume. Na pamesemwa: Kuwa bali huo ni msemo unaoelezea kuhusu kunyamaza kwao na kuacha kuwajibu Mitume.

Na pamesemwa: Waliiuma mikono kwa uchungu. Na amesema Mujahidi na Muhammad bin Kaab, na Qatada: Maana yake ni kwamba wao waliwakadhibisha na wakarudisha juu yao maneno yao kwa midomo yao.<sup>3</sup>

Ninasema: Na tafsiri ya Mujahid inapata nguvu. Kwa ukamilifu wa maneno:

<sup>1</sup> At-Tabari 16:528.

<sup>2</sup> Tafsir Al-Qurtubi 9:344.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:534.

وَقَالُوا إِنَّا كَفَرْنَا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ وَإِنَّا لَفِي شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَنَا إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٦﴾

**“...wakasema: Hakika sisi tumeyakataa hayo mliyo tumwa, na hakika sisi tunayo shaka kubwa na mnayo tuitia.”**

Na amesema Al-Awfi kutokana na Ibn Abbas رضي الله عنهما: walipoyafikia Maneno ya Allah تعالى, walistaajabu na wakarudisha mikono yao midomoni mwao.<sup>1</sup>

وَقَالُوا إِنَّا كَفَرْنَا بِمَا أُرْسِلْتُمْ بِهِ

**“...wakasema: Hakika sisi tumeyakataa hayo mliyo tumwa nayo...”**

Wanasema hatuwasadikishi katika yale ambayo mmekuja nayo kwani tunayo katika hayo shaka yenye nguvu sana.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 16:533.

\* قَالَتْ رُسُلُهُمْ أَفِي اللَّهِ شَكٌّ فَاطِرِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ  
 يَدْعُوكُمْ لِيَغْفِرَ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُؤَخَّرَكُمْ إِلَىٰ  
 أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ قَالُوا إِنَّ أَنتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا تُرِيدُونَ أَن  
 تَصُدُّونَا عَمَّا كَانَتْ يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا فَآتُونَا بُسُلَتِنِ ۚ  
 قَالَتْ لَهُمْ رُسُلُهُمْ إِن نَّحْنُ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلَكُمْ وَلَٰكِن  
 اللَّهُ يَمُنُّ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَمَا كَان لَنَا أَن  
 نَأْتِيَكُم بِسُلْطٰنٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ  
 الْمُؤْمِنُونَ ۝ وَمَا لَنَا أَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَىٰ اللَّهِ وَقَدْ  
 هَدٰنَا سُبُلَنَا ۗ وَلَنَصْبِرَنَّ عَلَىٰ مَا ءَادٰتُمُونَا ۗ وَعَلَىٰ اللَّهِ  
 فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُتَوَكِّلُونَ ۝ وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِرُسُلِهِمْ  
 لَنُخْرِجَنَّكُمْ مِّنْ أَرْضِنَا أَوْ لَنَعُودَنَّ فِي مِلَّتِنَا فَأَوْحَىٰ  
 إِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ لَنَبْلَنَّكَنَّ أَظْلَمٰلِيۢمِينَ ۝ وَلَنَسْكَنَنَّكُمْ  
 الْأَرْضَ مِنۢ بَعْدِهِمْ ۗ ذٰلِكَ لِمَن خَافَ مَقَامِي وَخَافَ  
 وَعَمِدِ ۝ وَأَسْتَفْتِحُوا وَخَابَ كُلُّ جَبَّارٍ عَمِيدٍ ۝  
 مِنۢ مَّرَآئِهِم جَهَنَّمُ يُسْقٰى مِنْ مَّآءٍ صٰدِيۢرٍ ۝ يَتَجَرَّعُهُ  
 وَلَا يَكَادُ يُسِيغُهُ ۗ وَيَأْتِيهِ الْمَوْتُ مِنۢ كُلِّ مَكَانٍ وَمَا هُوَ  
 بِمَعْتَرٍ ۗ وَمِنۢ مَّرَآئِهِم عَذَابٌ غٰلِيظٌ ۝

\* قَالَتْ رُسُلُهُمْ أَفِي اللَّهِ شَكٌّ فَاطِرِ  
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ يَدْعُوكُمْ لِيَغْفِرَ  
 لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ وَيُؤَخَّرَكُمْ  
 إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ قَالُوا إِنَّ أَنتُمْ  
 إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا تُرِيدُونَ أَن تَصُدُّونَا  
 عَمَّا كَانَتْ يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا فَآتُونَا  
 بُسُلَتِنِ ۚ قَالَتْ لَهُمْ  
 رُسُلُهُمْ إِن نَّحْنُ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلَكُمْ  
 وَلَٰكِن اللَّهُ يَمُنُّ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِنْ  
 عِبَادِهِ ۗ وَمَا كَان لَنَا أَن نَأْتِيَكُم  
 بِسُلْطٰنٍ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَعَلَىٰ اللَّهِ  
 فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ۝ وَمَا  
 لَنَا أَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَىٰ اللَّهِ وَقَدْ  
 هَدٰنَا سُبُلَنَا ۗ وَلَنَصْبِرَنَّ عَلَىٰ مَا  
 ءَادٰتُمُونَا ۗ وَعَلَىٰ اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ  
 الْمُتَوَكِّلُونَ ۝

10. Mitume wao waka-sema: Ati pana shaka na

Mwenyezi Mungu, Muumba mbingu na ardhi? Yeye Anakuiteni Apate  
 Kukufutieni madhambi yenu, na Akupeni muhula mpaka muda uliowekwa.  
 Wakasema: Nyinyi si chochote ila ni wanaadamu kama sisi. Mnataka  
 kutuzuilia na waliyokuwa wakiabudu baba zetu. Basi tuleteeni hoja iliowazi.

**11. Mitume wao wakawaambia: Sisi kweli si chochote ila ni wanaadamu kama nyinyi. Lakini Mwenyezi Mungu Humfanyia hisani amtakaye katika waja wake. Wala sisi hatuwezi kuleta uthibitisho ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na juu ya Mwenyezi Mungu ndio wategemee Waumini.**

**12. Na tuna nini hata tusimtegemee Mwenyezi Mungu, na Hali Yeye Ametuongoa kwenye njia zetu. Na hapana shaka sisi tutayavumilia hayo maudhi mnayotuudhi. Na Juu ya Mwenyezi Mungu Wategemee Wanaotegemea.**

### Majadiliano Kati ya Mtume ۞ na Makafiri

Allah تعالی Anaeleza kuhusu yaliyopita kati ya makafiri na Mitume wao miongoni mwa majadiliano, na hilo ni kwa hakika kwamba umati wao, wakati ulipowakabili Mitume kwa kutia shaka katika waliyokuja nayo miongoni mwa kumuabudu Allah تعالی hali ya kuwa Peke Yake Hana Mshirika. Mitume walisema.

أَفِي اللَّهِ شَكٌّ

**“Ati pana shaka na Mwenyezi Mungu.”**

Kuhusu Uungu Wake na Haki Yake Yeye Pekee ya Kuabudiwa, kwa Kuwa Ndiye Muumbaji Pekee wa Viumbe Wote? Hakika, Yeye Pekee Anastahiki Kuabudiwa, bila ya mshirika. Mataifa mbalimbali yalikiri na yanakiri kuwepo Muumbaji, isipokuwa wanamshirikisha na wengine wanaowadhania kuwa watawafaa au kuwasogeza sana kwa Allah تعالی. Na waliwaambia Mitume wa Allah تعالی,

يَدْعُوكُمْ لِيَغْفِرَ لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبِكُمْ

**“Yeye Anakuiteni Apate Kukufutieni Madhambi Yenu.”**

Maana yake: Katika Akhera.

وَيُؤَخِّرَكُمْ إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ

**“...na Akupeni Muhula mpaka muda Uliowekwa.”**

Maana yake: Hapa duniani kama Alivyosema Allah تعالی:



وَأَنْ أَسْتَغْفِرُوا رَبُّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ يُمَتِّعْكُمْ مَتَاعًا حَسَنًا إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى وَيُؤْتِ كُلَّ ذِي فَضْلٍ فَضْلَهُ ۗ

**“Na ili mumuombe msamaha Mola wenu Mlezi, kisha mtubie Kwake. Atakustarehesheni starehe nzuri mpaka muda maalumu. Na Atampa kila mwenye fadhila, fadhila yake.” (11:3)**

Umma wao ukashikilia kuhoji kuhusu Mtume wao baada ya kulazimika kukiri ushahidi wa kwanza kuwa Allah Peke Yake Ndiye Aliyeumba kila kitu.

### **Makafiri Hawaukubali Utume wa Mitume kwa Sababu ni Wanadamu**

Na majumuisho ya maneno yao walisema:

إِنْ أَنتُمْ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا

**“Nyinyi si chochote ila ni wanaadamu kama sisi.”**

Maana: Vipi tukufuateni kwa maneno yenu tu ilhali hatujaona miujiza yoyote?

فَأَتُونَا بِسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ

**“Basi tuleteeni hoja iliowazi.”**

Maana yake: Miujiza iitakayotushawishi tuwakubali.

قَالَتْ لَهُمْ رُسُلُهُمْ إِنْ نَحْنُ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ

**“Mitume wao wakawaambia: Sisi kweli si chochote ila ni wanaadamu kama nyinyi.”**

Maana yake: Ni sahihi kwamba sisi ni watu mfano wenu katika ubinadamu.

وَلٰكِنَّ اَللّٰهَ يَمُنُّ عَلٰى مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهٖ ۗ

**“Lakini Mwenyezi Mungu Humfanyia Hisani Amtakaye Katika Waja Wake.”**

Maana yake: Kwa Ujumbe na Utume,



**aliwaletea Wahyi: Hakika Tutawaangamiza Waliोधhulumu!**

**14. Na Tutakuwekeni katika Ardhi baada yao. Haya ni kwa anayeogopa kusimamishwa mbele Yangu, na Akaogopa Maonyo Yangu.**

**15. Na wakaomba ushindi, na akashindwa kila jabari mkaidi,**

**16. Ambaye nyuma yake ipo Jahannamu, na atanywishwa maji ya usaha.**

**17. Awe anayagugumia, wala hawezi kuyameza. Na mauti yawe yanamjia kutoka kila upande, naye wala hafi. Na zaidi ya hayo ipo adhabu nyengine kali vile vile.**

**Mataifa Yasiyomuamini Allah تعالیٰ Kuwatishia Kuwatoa Mitume Yao, Allah تعالیٰ Anawapa Bishara Mitume yake.**

Anaeleza Allah تعالیٰ kuhusu yale ambayo umati uliokufuru uliwakamia na kuwaapiza kwayo Mitume wao, miongoni mwa kuwatoa katika ardhi yao na kuwakataa mbele ya macho yao kama walivyosema watu wa Shuaibu عليه السلام kwa Shuaibu عليه السلام mwenyewe na kwa wafuasi wake:

لُنْخَرِجَنَّكَ يَشْعَبُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا

**“Ewe Shua’ib! Tutakutoa wewe pamoja na wale waliokuamini katika mji wetu.” (7:88)**

Tutakutoa Ee Shuaibu عليه السلام na wale ambao wameamini pamoja na wewe katika mji wetu. Na kama walivyosema watu wa Luut عليه السلام,

أَخْرَجُوا ءَالَ لُوطٍ مِّن قَرْيَتِكُمْ

**“Wafukuzeni wafuasi wa Lut’i katika mji wenu.” (27:56)** Na Amesema Allah تعالیٰ Akiwaelezea washirikina wa Kikuraishi:

وَإِنْ كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا وَإِذًا لَا يَلْبَثُونَ خِلاَفَكَ إِلَّا

قَلِيلًا ﴿٢٧﴾

**“Na walitaka kukukera ili uitoke nchi. Na Hapo wao wasingelibakia humo ila kwa muda mchache tu.” (17:76)** Na Kauli Yake,

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ ۚ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ ۗ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿١٤﴾

**“Na walipokupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu Akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa Mipango.” (8:30)**

Na ilikuwa katika kitendo chake Allah تعالى ni kwamba Yeye Alimpa nguvu Mjumbe Wake na Akamnusuru na Akamfanyia wepesi wa kutoka kwake Makkah kupata watu wa kumnusuru na wasaidizi, na askari wanaoipigania Dini ya Allah تعالى . Na hakuacha kuwa Allah تعالى Anampandisha kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine mpaka Akamfungulia Makkah ambayo alitolewa na Akammakinisha hapo Makkah licha ya maadui zake wa Makka kuchukia. Watu wa Ulimwenguni wakaingia katika Dini ya Allah تعالى makundi kwa makundi na likapata ushindi neno la Allah تعالى juu ya dini zingine, Mashariki ya ardhi na Magharibi yake katika muda mfupi sana. Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

فَأَوْحَىٰ إِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ لَنَبِّحَنَّهُم بِظُلْمِهِمْ ۖ وَلَنُنشِئَنَّكُمْ الْآرَضَ مِنْ بَعْدِهِمْ ﴿١٣﴾

**“Basi Mola wao Mlezi Aliwaletea wahyi: Hakika Tutawaangamiza waliodhulumu! Na Tutakuwekeni katika ardhi baada yao.” (14:13,14)**

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَمَتْنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿١٨﴾ وَإِنَّ جُنَدَنَا لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿١٩﴾

**“Na bila ya shaka Neno Letu lilikwishatangulia kwa waja Wetu waliotumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa. Na kwamba jeshi Letu ndilo litakaloshinda.” (37:171-173)**

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾

**“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.” (58:21)**

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزُّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ

**“Na Hakika Tulikwisha andika katika Zaburi baada ya Kumbukumbu.” (21:105)**

قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللَّهِ وَاصْبِرُوا إِنَّ الْأَرْضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ

وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٠٥﴾

**“Musa akawaambia watu wake: Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu, na subirini. Hakika ardhi ni ya Mwenyezi Mungu. Naye Humrithisha amtakaye katika waja Wake. Na mwisho ni wa wachamungu.” (7:128) na,**

وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضَعُونَ مَشْرِقَ الْأَرْضِ وَمَغْرِبَهَا الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا وَدَمَرْنَا مَا كَانِ يَصْنَعُ

فِرْعَوْنَ وَقَوْمَهُ وَمَا كَانُوا يَعْرِشُونَ ﴿١٣٧﴾

**“Na Tukawarithisha watu waliokuwa wanadharauliwa mashariki na Magharibi ya ardhi Tuliyoibariki. Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyosubiri. Na Tukayaangamiza aliyokuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyokuwa wakiyajenga.” (7:137)**

Kisha Allah تعالى Akasema,

ذَٰلِكَ لِمَنْ خَافَ مَقَامِي وَخَافَ وَعِيدِ

**“Haya ni kwa anayeogopa kusimamishwa mbele Yangu, na akaogopa maonyo Yangu.”**

Maana yake: Maonyo Yangu kwa mwenye kuogopa mbele Yangu Siku ya Kiyama. Na akayaogopa makemeo Yangu, nayo ni Matisho Yangu na Adhabu Yangu. Kama Alivyosema Allah تعالى:

فَأَمَّا مَنْ طَغَىٰ ﴿١٣٧﴾ وَعَٰثِرَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا ﴿١٣٨﴾ فَإِنَّ الْجَحِيمَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿١٣٩﴾ وَأَمَّا مَنْ

خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿١٤٠﴾ فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿١٤١﴾

**“Basi ama yule aliyezidi ujeuri, na akakhiari maisha ya dunia, Kwa hakika Jahannamu ndiyo makaazi yake! Na ama yule anayeogopa**

***kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizulia nafsi yake na matamano. Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake!” (79:37-41)***

وَلَمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّاتٍ ۝٤١

***“Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi atapata Bustani mbili.” (55:46)***

وَأَسْتَفْتَحُوا

***“Na wakaomba ushindi.”*** Maana yake: Wakaomba nusra Mitume kwa Bwana wao dhidi ya watu wao, ameyasema haya, Ibn Abbas, Mujahid na Qatada رضي الله عنهم.<sup>1</sup> Na amesema Abdulrahman bin Zaia na Bin Aslam, umma zilijipiza zenyewe.<sup>2</sup> Kama washirikina walivyosema,

اللَّهُمَّ إِنْ كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِنَ السَّمَاءِ أَوْ أُنْتِنَا

بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ۝٣٢

***“Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyo chungu.” (8:32)***

Inawezekana kuwa maana zote mbili hapa ni sahihi, maana, Mtume kutaka nusura dhidi ya watu wao au wao wenyewe kujiombea balaa kama ambavyo wao walitaka nusura juu ya nafsi zao. Siku ya vita vya Badr, Mtume ﷺ naye akaomba msaada, na Amesema Allah تعالى Kuwaambia washirikina:

إِنْ تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ ۖ وَإِنْ تَنْهَوْا فَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ ۖ

***“Kama mnataka hukumu basi hukumu imekwisha kujieni. Na mkiacha itakuwa ndio kheri kwenu.” (8:19)***

Allah تعالى Anajua zaidi. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَحَابَ كُلُّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ

***“...na akashindwa kila jabari mkaidi...”*** Waliokuwa na kiburi na wakauasi ukweli. Allah تعالى Anasema katika Aya nyingine,

<sup>1</sup> At-Tabari 16:544-545.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:545.

أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيدٍ ﴿٢٤﴾ مَنَّاعٍ لِلْخَيْرِ مُعْتَدٍ مُّرِيبٍ ﴿٢٥﴾ الَّذِي جَعَلَ مَعَ  
 اللَّهُ إِلَهًا ءَاخَرَ فَأَلْقِيَاهُ فِي الْعَذَابِ الشَّدِيدِ ﴿٢٦﴾

**“Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inda, akatazaye kheri, arukaye mipaka, mwenye kutia shaka, aliyeweka mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Basi mtupeni katika adhabu kali.” (50:24-26)**

Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّهُ يُؤْتِي بِجَهَنَّمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، فَتَنَادِي الْخَلَائِقَ، فَقَوْلُ: إِنِّي وَكَلْتُ بِكُلِّ جَبَّارٍ عَنِيدٍ»

*“Jahanamu italetwa Siku ya Kiama na itawatangazia viumbe kwa kusema, ‘Nimepewa majukumu kwa kila muasi mkaidi.’<sup>1</sup>*

Maana yake: Mtu huyo amepata hasara wakati Mitume walipojitahidi kumuomba kumnyenyekeka na kuelekea kwa Allah تعالى, Mwenye Uwezo Mkubwa. Na Kauli Yake:

مِّنْ وَرَائِهِمْ جَهَنَّمُ

**“...nyuma yake ipo Jahannamu...”** Maana yake: Mbele ya shupavu huyo mwenye kupinga pana moto – Jahannamu. Maana moto huo ni wake, unamlindilia atakaa humo milele Siku ya Kiyama, na ataoneshwa juu ya moto huo asubuhi na jioni mpaka Siku ya Kiyama.

وَيُسْقَىٰ مِنْ مَّاءٍ صَدِيدٍ

**“...na atanywishwa maji ya usaha.”**

Maana yake: Ndani ya moto hana yeye kinywaji chochote isipokuwa maji ya moto na usaha, kuna yaliopitiliza, na kuna ya baridi yaliyopitiliza na yanatoa harufu ya uvundo. Kama Alivyosema

هَذَا فَلْيَذُوقُوهُ حَمِيمٌ وَعَسَاقٌ ﴿٥٧﴾ وَءَاخِرُ مِنْ شَكْلِهِمْ أَزْوَاجٌ ﴿٥٨﴾

**“Ndio hivi! Basi na wayaonje maji ya moto na ya usaha! Na adhabu nyenginezo za namna hii.” (38:57-58)**

Na amesema Mujahid na Ikrima, *Swadid* ni usaha na damu.<sup>2</sup>

<sup>1</sup> At-Tirmidhi na. 2573, 2374.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:548.

Allah تعالیٰ Anasema:

وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ ﴿١٥﴾

“...*na wakinyweshwa maji yanayo chemka ya kuwakata matumbo yao?*” (47:15) na,

وَأِنْ يَسْتَعِثُّوا يُعَاثُوا بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوهَ

“*Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyotibuka. Yatakawababua nyuso zao.*” (18:29)

Na kama hivyo amepokea Ibnu Jariri رحمه الله تعالى. Na Kauli Yake:

يَتَجَرَّعُهُ

“*Awe Anayagugumia,...*” Atayapitisha kooni na hali ya kuwa hapendi, kwani atayanywa kwa kutenzwa nguvu na kulazimishwa, hatayaweka mdomoni mwake mpaka Malaika atampiga kwa nyundo ya chuma. Kama Alivyosema Allah تعالیٰ:

وَهُمْ مَقْمَعٌ مِنْ حَدِيدٍ ﴿٢١﴾

“*Na kwa ajili yao yatakuwapo marungu ya chuma.*” (22:21)

Na Akasema,

وَلَا يَكَادُ يُسِغُهُ

“...*wala hawezi kuyameza.*”

Maana yake: Hawezi kuyameza kwa sababu ya ubaya wa ladha yake na rangi yake na harufu yake na umoto wake, au ubaridi wake ambao hauwezekani.

وَيَأْتِيهِ الْمَوْتُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ

“*Na mauti yawe yanamjia kutoka kila upande,...*”

Maana yake: Utakuwa na maumivu kwake mwili wake wote na viungo vyake vyote. Amesema Amri bin Maymoun bin Mihran katika kila mfupa na mshipa.<sup>1</sup>

Na amesema Adh-Dhahak kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما:

وَيَأْتِيهِ الْمَوْتُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ

“*Na mauti yawe yanamjia kutoka kila upande,...*”

<sup>1</sup> Ad-Dur Al-Manthur 5:16.



Amesema: Namna mbalimbali za adhabu ambazo Atamuadhibu Yeye Allah تعالى kwa adhabu hizo Siku ya Qiyama katika moto wa Jahannamu, hapana katika namna hizo namna yoyote isipokuwa yatamjia mauti kutokana na namna hiyo. Lau angekuwa anakufa isipokuwa yeye hatakufa kwa sababu Allah تعالى Amesema:

لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِّنْ عَذَابِهَا

**“...hawahukumiwi wakafa, wala hawatapunguziwa Adhabu Yake.” (35:36)<sup>1</sup>**

Na maana ya maneno ya Ibn Abbas رضي الله عنهما ni kwamba hapana namna yoyote katika namna hizo katika adhabu, isipokuwa itakapompata inahukumilia afe kutokana na adhabu hiyo, lau angekuwa afadhali anakufa, wala hafi ili awekwe katika adhabu yenye kudumu na mateso, na kwa sababu hiyo Amesema Allah:

وَيَأْتِيهِ الْمَوْتُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ وَمَا هُوَ بِمَيِّتٍ

**“Na mauti yawe yanamjia kutoka kila upande, naye wala hafi.”** Maana: Baada ya hali hiyo ana adhabu nyingine nzito. Maana: Yenye uchungu mkubwa, ngumu na nzito kuliko ile iliyokuwa huko nyuma. Inatisha sana na ina uchungu mno. Na haya ni kama Alivyosema Allah تعالى kuhusu mti wa A-zzaqum:

وَمِنْ وَرَائِهِ عَذَابٌ غَلِيظٌ

**“Na zaidi ya hayo ipo adhabu nyengine kali vile vile.”**

إِنَّهَا شَجَرَةٌ تَخْرُجُ فِي أَصْلِ الْجَحِيمِ ۖ طَلْعُهَا كَأَنَّهُ زُرُّوسٌ الشَّيْطَانِ ۖ فَلْيَأْتِهِمْ  
لَا يَكُونُ مِنْهَا فَمَا لُفُونَ مِنْهَا الْبُطُونَ ۖ ثُمَّ إِنَّ لَهُمُ عَلَيْهَا لَشَوْبًا مِّنْ حَمِيمٍ ۖ ثُمَّ إِنَّ  
مَرَجِعَهُمْ لِآلِ الْجَحِيمِ ۖ

**“Hakika huo ni mti unaotoka katikati ya Jahannamu. Mashada ya matunda yake kama kwamba vichwa vya mashet’ani. Basi hakika bila ya shaka hao watayala hayo, na wajaze matumbo. Kisha juu yake wanyweshwe mchanganyo wa maji ya moto yaliyochemka. Kisha hakika marejeo yao bila ya shaka yatakuwa kwenye Jahannamu.” (37:64-68)**

<sup>1</sup> Ad-Dur Al-Manthur 5:16.

Allah تعالی Ameeleza kwamba wao watakuwa wakila *Zaqqum* na mara nyingine wanywe maji ya moto na mara nyingine watarudishwa motoni, tunaomba hifadhi kwa Allah تعالی na adhabu hiyo. N a kama hivyo Amesema Allah تعالی.

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٤٣﴾ يَطُوفُونَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ ءَانِ ﴿٤٤﴾

**"Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikanusha. Watakuwa wakiizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayochemka." (55:43-44)**

إِنَّ شَجَرَةَ الزَّقُّومِ ﴿٤٥﴾ طَعَامُ الْأَثِيمِ ﴿٤٦﴾ كَالْمُهْلِ يَغْلِي فِي الْبُطُونِ ﴿٤٧﴾ كَغَلِيِّ الْحَمِيمِ ﴿٤٨﴾ خَذُوهُ فَأَعْتَلُوهُ إِلَىٰ سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٤٩﴾ ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِنْ عَذَابِ الْحَمِيمِ ﴿٥٠﴾ ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٥١﴾ إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٥٢﴾

**"Hakika Mti wa Zaqqum, ni chakula cha mwenye dhambi. Kama shaba iliyoyayushwa, hutokota matumboni. Kama kutokota kwa maji ya moto. (Itasemwa:) Mkamateni na mtupeni katikati ya Jahannamu! Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji yanayochemka. Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu! Hakika haya ndiyo mliyokuwa mkiyatilia shaka." (44:43-50)**

وَأَصْحَابُ الشَّيْطَانِ مَا أَصْحَابُ الشَّيْطَانِ ﴿٥٣﴾ فِي سُمُومٍ وَحَمِيمٍ ﴿٥٤﴾ وَظِلٍّ مِّنْ تَحْمُومٍ ﴿٥٥﴾ لَا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ﴿٥٦﴾

**"Na watu wa kushotoni; je ni yepi ya wa kushotoni? Katika upepo wa moto, na maji yanayochemka, na kivuli cha moshi mweusi, si cha kuburudisha wala kustarehesha." (56:41-44) na,**

هَذَا وَلِيُّكَ يَأْتِيكُم مِّنْ هُنَا فَلَْيَذُقُوهُ ﴿٥٧﴾ هَذَا فَلَْيَذُقُوهُ ﴿٥٨﴾ وَإِنَّ لِلطَّيغِينَ لَشَرَّ مَنَابٍ ﴿٥٩﴾ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا فَبِئْسَ الْمَهَادُ ﴿٦٠﴾ هَذَا فَلَْيَذُقُوهُ ﴿٦١﴾ حَمِيمٌ وَغَسَّاقٌ ﴿٦٢﴾ وَآخِرُ مِنْ شَكْلِهِمْ أَزْوَاجٌ ﴿٦٣﴾

**"Ndio hivi! Na hakika wenye kuasi bila ya shaka watapata marudio maovu kabisa. Nayo ni Jahannamu! Wataingia humo. Nacho hicho ni kitanda kiovu mno cha kulalia. Ndio hivi! Basi na wayaonje maji ya moto na ya usaha! Na adhabu nyenginezo za namna hii." (38:55-58)**

Na nyingine nyingi zisizokuwa hizo miongoni mwa aya zenye kufahamisha juu namna nyingi za adhabu juu yao na kukaririka kwake na namna zake na miundo yake mbalimbali katika ambayo hayadhibiti isipokuwa Allah تعالى. Ikiwa ni malipo yanayolingana na makosa yao.

وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٤٦﴾

**“...wala Mola wako Mlezi si Mwenye Kuwadhulumu waja.” (41:46)**

\* \* \*

مَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۗ أَعْمَلُهُمْ كَرَمَادٍ اشْتَدَّتْ بِهِ  
 الرِّيحُ فِي يَوْمٍ عَاصِفٍ ۗ لَا يَقْدِرُونَ مِمَّا كَسَبُوا عَلَىٰ شَيْءٍ  
 ۗ ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَالُ الْبَعِيدُ ﴿١٨﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ  
 خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۗ إِنْ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ  
 بِخَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٩﴾ وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿٢٠﴾ وَرَبُّوْا  
 لِلَّهِ جَمِيعًا ۖ فَقَالَ الضُّعُفَتُوْا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا ۖ إِنَّا كُنَّا لَكُمْ  
 تَبَعًا ۖ فَهَلْ أَنتُمْ مُّعْتَدُونَ ۗ عَنَّا مِّنْ عَذَابِ اللَّهِ مِن شَيْءٍ ۗ  
 قَالُوا لَوْ هَدَّيْنَا اللَّهُ لَهَدَيْتُكُمْ ۗ سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَجْرَعْنَا أَمْ  
 صَبَرْنَا مَا لَنَا مِنْ مَّحِيسٍ ﴿٢١﴾ وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ  
 الْأَمْرُ إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ ۖ وَوَعَدْتُكُمْ  
 فَأَخْلَفْتُكُمْ ۗ وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ ۖ إِلَّا أَنْ  
 دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي ۗ فَلَا تَلُومُونِي ۖ وَلُومُوا أَنفُسَكُمْ ۗ مَا  
 أَنَا بِمُصْرِخِكُمْ ۖ وَمَا أَنتُمْ بِمُصْرِخِي ۗ إِنِّي كَفَرْتُ بِمَا  
 أَشْرَكْتُمُونِ مِن قَبْلُ ۗ إِنَّ الظَّٰلِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ  
 ﴿٢٢﴾ وَأُدْخِلَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحٰتِ جَنَّٰتٍ  
 تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ ۗ تَحِيَّاتٌ  
 فِيهَا سَلَامٌ ﴿٢٣﴾

مَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۗ  
 أَعْمَلُهُمْ كَرَمَادٍ اشْتَدَّتْ بِهِ الرِّيحُ فِي  
 يَوْمٍ عَاصِفٍ ۗ لَا يَقْدِرُونَ مِمَّا  
 كَسَبُوا عَلَىٰ شَيْءٍ ۗ ذَٰلِكَ هُوَ  
 الضَّلَالُ الْبَعِيدُ ﴿١٨﴾

**18. Mfano wa walio-  
 mkufuru Mola wao Mlezi -  
 vitendo vyao ni kama jivu  
 linalopeperushwa kwa  
 nguvu za upepo katika siku  
 ya mdharuba. Hawawezi  
 kupata chochote katika  
 waliyoyafanya. Huko ndiko  
 kupotelea mbali!**

**Mfano wa Matendo ya  
 Makafiri**

Huu ni mfano Ameupiga Allah wa matendo ya makafiri ambao wamemu-abudu pamoja na Yeye asiyekuwa Yeye na wakawakadhibisha Mitume Wake. Na wakayajenga matendo yao juu ya usiokuwa msingi sahihi, yakaporomoka na

wakayakosa, wakati ambao wanayahitajia sana. Kwa hiyo Amesema Allah

تعالى:

مَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِرَبِّهِمْ ۗ أَعْمَلُهُمْ

**“Mfano wa waliomkufuru Mola wao Mlezi - vitendo vyao...”**

Maana yake: Mfano wa matendo yao Siku ya kiyama pindi watakapotaka malipo yao kwa Allah تعالى, kwa sababu wao kuwa juu ya jambo, kwa hiyo hawakukuta kitu chochote na hawakukuta pato lolote, isipokuwa kama lile linalopatikana kwa majivu pindi unapovuma upepo mkali.

فِي يَوْمٍ عَاصِفٍ

**“...katika siku ya mdharuba.”**

Maana yake: Yenye upepo mkali sana, kimbunga kikali sana, kwa hiyo hawakuweza kuambulia kitu chochote katika matendo yao ambayo wameyachuma duniani. Isipokuwa kama wanavyoweza kuambulia majivu haya katika siku hii.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَنْثُورًا ﴿٣٣﴾

**“Na Tutayaendea yale waliyoyatenda katika vitendo vyao, tuvifanye kama mavumbi yaliyotawanyika.” (25:33)**

مَثَلُ مَا يُنْفِقُونَ فِي هَذِهِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَثَلِ رِيحٍ فِيهَا صِرٌّ أَصَابَتْ حَرْثَ قَوْمٍ

ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ فَأَهْلَكَتَهُ ۗ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ وَلَٰكِن أَنفُسُهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٣٤﴾

**“Mfano wa vile wanavyovitoa katika uhai wao wa duniani ni kama upepo ambao ndani yake ipo baridi ya barafu, ukalisibu shamba la watu waliodhulumu nafsi zao, ukaliteketeza. Na Mwenyezi Mungu Hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao.” (3:117) na,**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُبْطِلُوا صَدَقَاتِكُمْ بِالْمَنِّ وَالْأَذَىٰ كَالَّذِي كَانَتِ يَفُوقُ مَالَهُ رِثَاءَ النَّاسِ

وَلَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ فَمَثَلُهُ كَمَثَلِ صَفْوَانٍ عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابَهُ وَابِلٌ فَتَرَكَهُ

صَلْدًا ۗ لَا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِّمَّا كَسَبُوا ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٥﴾

**“Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anayetoa mali yake kwa kuwaonesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano**

**wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyochuma. Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri.” (2:264)**

ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَلُ الْبَعِيدُ

**“Huko ndiko kupotelea mbali!”**

Maana yake: Mahangaiko yao na matendo yao yako juu ya msingi usiokuwa mnyoofu, mpaka wameyakosa malipo yao wakati wanayahitajia sana.

ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَلُ الْبَعِيدُ

**“Huko ndiko kupotelea mbali!”**

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ إِنَّ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ وَيَأْتِ بِخَلْقٍ جَدِيدٍ  
وَمَا ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ بِعَزِيزٍ ﴿٢٦٤﴾

**19. Huoni kuwa Mwenyezi Mungu Ameziumba Mbingu na Ardhi kwa Haki? Akitaka Atakuondoeni na Alete Viumbe wapya!**

**20. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si jambo gumu.**

### Ushahidi wa Uhai Baada ya Mauti

Allah تعالی Ameerza kuhusu Uwezo Wake wa Kurejesha viwiliwili Siku ya Kiama, kwamba Ameumba Mbingu na Ardhi, ambazo ni jambo kubwa kuliko Kuumbwa watu. Naye Ndiye Ambaye Ameweza Kuziumba Mbingu hizi pamoja na kunyanyuka kwake, upana wake, ukubwa wake, na vilivyomo ndani yake, miongoni mwa nyota zenye kuthibiti, sayari, harakati mbalimbali, na alama mbalimbali zenye kushinda. Naye Ndiye Muumba wa Ardhi hii pamoja na vilivyomo ndani yake, miongoni mwa maeneo yaliyo tambarare, sehemu za miinuko, sehemu kavu, Majangwa, Bahari, Miti, Mimea, Wanyama pamoja na kutofautiana namna zake, manufaa yao, maumbile yake na rangi zake.

أُولَٰئِكَ يَرَوْنَ أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزِمْنَهُنَّ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ  
الْمَوْتَىٰ بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٦٥﴾

**“Je! Hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, Aliyeziumba Mbingu na Ardhi, na Hakuchoka kwa Kuziumba, kuwa ni Muweza wa Kuwafufua wafu? Kwani? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.”**  
(46:33)

أَوَلَمْ يَرَ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِن نُّطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴿٧٦﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا  
وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۗ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٧﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۗ  
وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٨﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُم مِّنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا فَإِذَا أَنتُم مِّنْهُ  
تُوقَدُونَ ﴿٧٩﴾ أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَىٰ أَن يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ بَلَىٰ  
وَهُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ﴿٨٠﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَن يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨١﴾  
فَسُبْحٰنَ الَّذِي بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٢﴾

**“Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi Tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri! Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake, akasema: ‘Ni nani huyo atakayeihisha mifupa nayo imekwisha mung’unyika?’ Sema: Ataihuisha Huyo Huyo Aliyeiumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila Kuumba. Aliyekujaalieni kupata moto kutokana na mti wa kijani nanyi mkawa kwa huo mnawasha. Kwani Aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye Ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa. Basi Ametakasika Yule Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu; na Kwake Yeye mtarejeshwa.”** (36:77-83)

Maana yake: Si jambo kubwa wala lenye kuzuilika bali ni jepesi Kwake iwapo mtakwenda kinyume na maamrishi Yake kuwaondosha na kuwaleta wengine wakiwa hawako juu ya sifa zenu.

Kama Alivyosema katika Aya nyingine:

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اٰنْتُمْ الْفُقَرَاءُ اِلَى اللّٰهِ ۗ وَاللّٰهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿١٠٢﴾ اِن يَشَآءُ يَدْهَبْكُمْ  
وَيَاْتِ بِخَلْقٍ جَدِيْدٍ ﴿١٠٣﴾ وَمَا ذٰلِكَ عَلَى اللّٰهِ بِعَزِيْزٍ ﴿١٠٤﴾

***“Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kujitoshwa, Msifiwa. Akitaka Atakuondoeni na Alete viumbe vipya. Na hilo si gumu kwa Mwenyezi Mungu.” (35:15-17)***

وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ

***“Na mkigeuka Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.” (47:38)***

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَن يَرْتَدَّ مِنكُمْ عَن دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهَ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ

***“Enyi mlioamini! Atakaye iacha miongoni mwenu Dini Yake, basi Mwenyezi Mungu Atakuja leta watu Anaowapenda nao Wanampenda,...” (5:54) na***

إِن يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ أَيُّهَا النَّاسُ وَيَأْتِ بِآخَرِينَ ۗ وَكَانَ عَلَىٰ ذَٰلِكَ قَدِيرًا ﴿٤١﴾

***“Akitaka Atakuondoeni, enyi watu! Na Awalete wengineo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa Hayo.” (4:133).***

وَبَرَزُوا لِلَّهِ جَمِيعًا فَقَالَ الضُّعَفَاءُ لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنتُمْ مُّعْتَدُونَ

عَنَّا مِن عَذَابِ اللَّهِ مِن شَيْءٍ ۗ قَالُوا لَوْ هَدَّيْنَا اللَّهُ لَهَدَيْتَنَا اللَّهُ هَدَىٰنَا لَكُم سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَجْرَعْنَا أَمْ

صَبَرْنَا مَا لَنَا مِن مَّحِيصٍ ﴿٤٢﴾

***21. Na wote watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu. Wanyonge watawaambia waliotakabari: Sisi tulikuwa wafuwasi wenu; ‘basi hebu hamtuondolei kidogo hivi katika adhabu ya Mwenyezi Mungu?’ Watasema: ‘Lau Mwenyezi Mungu Angeli tuongoa basi hapana shaka nasi tungelikuongoeni. Ni mamoja kwetu tukipapatika au tukisubiri; hatuna pa kukimbilia.***



## Wasioamini na Wakubwa Wao na Wafuasi Wao Watabishana Wakiwa Motoni

Anasema Allah تعالى:

وَبَرُّوْا

**“Na wote watahudhuria...”**

Viumbe wote, wema na waovu, watakusanyika mbele ya Allah تعالى katika sehemu iliyo wazi katika ardhi, napo ni mahali ambapo hapana hapo kitu chochote kinachomfunika mtu yoyote.

فَقَالَ الضُّعْفُوْا

**“Wanyonge watawaambia...”**

Nao ni wale wafuasi kuwaambia viongozi wao na mabwana zao na wakubwa wao,

لِّلَّذِيْنَ اَسْتَكْبَرُوْا

**“Waliotakabari...”**

Na kumuabudu Allah تعالى hali yakuwa Peke Yake hana mshirika na pia kuwakubali Mitume waliowaambia.

اِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا

**“Sisi tulikuwa wafuwasi wenu.”**

Maana yake: Wakati wowote na vyovyote, mtakavyotumrisha tunafuata na tunafanya.

فَهَلْ اَنْتُمْ مُّغْنُوْنَ عَنَّا مِنْ عَذَابِ اللّٰهِ مِنْ شَيْءٍ

**“...basi hebu hamtuondolei kidogo hivi katika adhabu ya Mwenyezi Mungu?”**

Maana: Hivi mtatuondolea sisi kitu chochote katika Adhabu ya Allah تعالى kama mlivyokuwa mnatauhidi na mnatupa tamaa. Watasema viongozi wao:

لَوْ هَدٰنَا اللّٰهُ هَدٰيَتِكُمْ

**“Lau Mwenyezi Mungu Angelituongoa basi hapana shaka nasi tungelikuongoeni.”**

Isipokuwa yamethibiti kwetu maneno ya Bwana Wetu na yametangulia kwetu na kwenu makadirio ya Allah تعالى, na yamethibiti Maneno ya adhabu juu ya makafiri.

سَوَاءٌ عَلَيْنَا أَجْرَعْنَا أَمْ صَبَرْنَا مَا لَنَا مِنْ مَّحِصٍ

**“Ni mamoja kwetu tukipapatika au tukisubiri; hatuna pa kukimbilia.”**

Maana yake: Hatuna sisi uokofu na lile ambalo tumo ndani yake tukisubiri Juu Yake au tukilalamika kutokana nalo. (Mimi, Ibn Kathir) Ninasema: Dhahiri inaonesha yakuwa maneno haya yatajadiliwa motoni, baada ya kuingia kwao humo, kama Alivyosema Allah تعالى:

وَإِذْ يَتَحَاجُّونَ فِي النَّارِ فَيَقُولُ الضُّعْفَتُو لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُنَّا لَكُمْ تَبَعًا فَهَلْ أَنْتُمْ مُغْنُونَ عَنَّا نَصِيبًا مِنَ النَّارِ ﴿١٧﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا إِنَّا كُلٌّ فِيهَا إِنَّ اللَّهَ قَدْ حَكَمَ بَيْنَ الْعِبَادِ ﴿١٨﴾

**“Na watapohojiana huko Motoni, wanyonge watawaambia waliojitukuza: Hakika sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi je, hamtuondolei sehemu ya Moto huu? Watasema waliojitukuza: Hakika sote sisi tumo humo humo! Kwani Mwenyezi Mungu kisha Hukumu Baina ya waja!”**

قَالَ أَدْخُلُوا فِي أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ مِنَ الْجِنَّ وَالْإِنْسِ فِي النَّارِ كُلَّمَا دَخَلَتْ أُمَّةٌ لَعَنَتْ أُخْتَهَا حَتَّى إِذَا آذَرُكُوا فِيهَا جَمِيعًا قَالَتْ أَخْرَبْنَاهُمْ لِأَوْلَادِهِمْ رَبَّنَا هَتُّوْنَا أَضَلُّونَا فَقَاتِهِمْ عَذَابًا ضِعْفًا مِنَ النَّارِ قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٍ وَلَكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾ وَقَالَتْ أَوْلَادُهُمْ لِأَخْرَبْنَاهُمْ فَمَا كَانَ لَكُمْ عَلَيْنَا مِنْ فَضْلٍ فذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٢٠﴾

**“Mwenyezi Mungu Atasema: Ingieni Motoni pamoja na umma uliopita kabla yenu wa majini na watu. Kila utakapoingia umma utawalaani wenzake. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa mwisho wao watawasema wa mwanzo wao: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya Motoni marudufu. Atasema: Itakuwa kwenu nyote marudufu, lakini nyinyi hamjui**

tu. Na wa mwanzo wao watawaambia wa mwisho wao: Basi nyinyi pia hamkuwa na ubora kuliko sisi. Basi onjeni adhabu kwa sababu ya mliyokuwa mkiyachuma.” (7:38-39) na,

رَبَّنَا إِنَّا أَطَعْنَا سَادَتَنَا وَكُبَرَاءَنَا فَأَضَلُّنَا الْسَّبِيلَ ﴿٣٨﴾ رَبَّنَا ءَاتِهِمْ ضِعْفَيْنِ مِنَ الْعَذَابِ وَالْعَنِيمَ لَعْنَا كَبِيرًا ﴿٣٩﴾

“Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tuliwatii mabwana zetu na wakubwa wetu; nao ndio waliotupoteza njia. Mola wetu Mlezi! Wape wao adhabu mara mbili, na uwalaani laana kubwa.” (33:67-68)

Na ama kuhasimiana kwao katika uwanja wa mkusanyiko, Amesema Allah تعالى:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ مَوْقُوفُونَ عِنْدَ رَبِّهِمْ يَرْجِعُ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ الْقَوْلِ يَقُولُ الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لَوْلَا أَنتُمْ لَكُنَّا مُؤْمِنِينَ ﴿٣٨﴾ قَالَ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا لِلَّذِينَ اسْتَضَعُّوا أَنَحْنُ صَدَدْنَاكُمْ عَنِ الْهُدَىٰ بَعْدَ إِذْ جَاءَكُمْ ۗ بَلْ كُنْتُمْ مُجْرِمِينَ ﴿٣٩﴾ وَقَالَ الَّذِينَ اسْتَضَعُّوا لِلَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُمْ أُنْدَادًا ۗ وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ وَجَعَلْنَا الْأَغْلَالَ فِي أَعْنَاقِ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ هَلْ نُجِزُونَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٤٠﴾

“Na ungelikiwaona madhaalimu wataposimamishwa mbele ya Mola wao Mlezi, wakirudishiana maneno wao kwa wao! Wanyonge wakiwaambia waliotakabari: ‘Lau kuwa si nyinyi, bila ya shaka tungelikuwa Waumini sisi.’ Waliotakabari watawaambia wanyonge: ‘Kwani sisi ndio tuliokuzuieni na uwongofu baada ya kukujieni? Bali nyinyi wenyewe ni wakosefu.’ Na wanyonge watawaambia waliotakabari: ‘Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika.’ Nao wataficha majuto watakapoiona adhabu. Na Tutaweka makongwa shingoni mwao waliokufuru. Kwani wanalipwa ila kwa waliyokuwa wakiyatenda?” (34:31-33)

وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ الْأَمْرُ إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتُكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ<sup>ط</sup>  
 وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِنْ سُلْطَانٍ إِلَّا أَنْ دَعَوْتُكُمْ فَاسْتَجَبْتُمْ لِي<sup>ط</sup> فَلَا تُلُومُونِي وَلُومُوا  
 أَنْفُسَكُمْ<sup>ط</sup> مَا أَنَا بِمُصْرِخِكُمْ وَمَا أَنْتُمْ بِمُصْرِخِيَّ<sup>ط</sup> إِنِّي كَفَرْتُ بِمَا أَشْرَكْتُمُونِ  
 مِنْ قَبْلُ<sup>ط</sup> إِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٢﴾ وَأَدْخَلَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا  
 الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ<sup>ط</sup> تَحِيَّاتٌ فِيهَا سَلَامٌ ﴿٢٣﴾

**22. Na Shet'ani atasema itapokatwa hukumu: Hakika Mwenyezi Mungu Alikuahidini ahadi ya kweli. Nami nalikuahidini; lakini sikukutimizieni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipokuwa nilikuiteni, nanyi mkaniitikia. Basi msinilaumu mimi, bali jilaumuni wenyewe. Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu, wala nyinyi hamuwezi kuwa watetezi wangu. Hakika mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha na Mwenyezi Mungu. Hakika madhaalimu watakuwa na adhabu chungu.**

**23. Na walioamini na wakatenda mema wataingizwa katika bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo kwa idhini ya Mola wao Mlezi. Maamkio yao humo yatakuwa: Salaam!**

### Iblisi Atawakana Wafuasi Wake Siku ya Kiama

Anaeleza Allah تعالی Kuhusu yale Aliyowaambia kwayo Iblisi wafuasi wake baada ya Kuhukumu kwa Allah تعالی kati ya waja wake, Akawatia waumini peponi na Akawaweka makafiri katika vidato vya moto. Atasimama kwao Iblisi – Laana ya Allah تعالی iwe juu yake, siku hiyo hali ya kuwa mtoa hotuba ili awaongezee huzuni. Kwenye huzuni yao, na kuwahadaa wao zaidi na kuwaongezea masikitiko: Amesema:

إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Alikuahidini ahadi ya kweli.”**

Maana yake: Juu ya ndimi za Mitume Wake, na Amewaahidi katika kuwafuata wao ndio kuokoka na kusalimika na ili iwe ahadi ya kweli. Na ama mimi nimewaahidini nikavunja ahadi yangu kwenu, kama alivyosema Allah تعالی:

يَعِدُّهُمْ وَيُؤْمِنُهُمْ<sup>ط</sup> وَمَا يَعِدُّهُمْ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿١٢٠﴾

***“Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shet’ani hawaahidi ila udanganyifu.”(4:120)***

وَمَا كَانَ لِيَ عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ

***“Na sikuwa na mamlaka juu yenu.”***

Maana yake: Sikuwa nina mamlaka juu yenu katika lile ambalo nimewalingania kwalo na dalili wala hoja yoyote, katika lile ambalo nimewaahidi kwalo.

إِلَّا أَن دَعَوْتُمْ فَأَسْتَجِبْتُ لِي<sup>ط</sup>

***“...isipokuwa nilikuiteni, nanyi mkaniitikia.”***

Kwa kufanya hivyo yaeleweni hayo. Na kwa hakika walisimamisha Mitume hoja na dalili sahihi juu ya ukweli wa lile walilokujieni nalo, mkawapinga, mkawa katika lile ambalo nyinyi mmo ndani yake:

فَلَا تَلُومُونِي

***“Basi msinilaumu mimi,”*** leo

وَلُومُوا أَنفُسَكُمْ<sup>ط</sup>

***“...bali jilaumuni wenyewe.”***

Kwani makosa ni yenu kwa kuwa nyinyi mmezipinga hoja na mmenifuata mimi kwa kule kuwaiteni kwenye batili.

مَا أَنَا بِمُصْرِخِكُمْ

***“Mimi siwezi kuwa mtetezi wenu.”***

Maana yake: Mwenye kuwanufaisha na mwenye kuwaokoa na lile ambalo nyinyi mmo ndani yake.

وَمَا أَنْتُمْ بِمُصْرِخِي<sup>ط</sup>

***“...wala nyinyi hamuezi kuwa watetezi wangu.”***

Wenye kunifaa kwa kuniokoa dhidi ya lile ambalo mimi nimo ndani yake miongoni mwa adhabu na mateso.

إِنِّي كَفَرْتُ بِمَا أَشْرَكْتُمُونَ مِنْ قَبْلُ<sup>1</sup>

**“Hakika mimi nilikataa tangu zamani kunishirikisha na Mwenyezi Mungu.”**

Qatada amesema: Maana: Kwa sababu ya kunishirikisha huko nyuma.<sup>1</sup> Na Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: Kwa hakika mimi nimekanusha kuwa mshirika wa Allah تعالى.<sup>2</sup> Na haya aliyoyasema ndiyo yenye nguvu. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ  
دُعَائِهِمْ غَنِيُونَ ﴿٥﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٦﴾

**“Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao. Na ambao watu watakapokusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.” (46:5-6) na,**

كَلَّا<sup>٣</sup> سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا

**“Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao.” (19:82)**

Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الظَّالِمِينَ

**“Hakika madhaalimu...”**

Maana yake: Katika kuuchukua kwao ukweli na kuifuata kwao batili, wana adhabu yenye kuumiza. Na dhahiri ya mtiririko wa aya ni kwamba hotuba ya Iblisi, itakuwa baada ya kuingia motoni, kama tulivyokwisha tanguliza. Na amesema Aamier Al-Shaaby watasimama mahatibu wawili siku ya Kiyama mbele ya hadhira ya watu. Atasema Allah تعالى kumuambia Issa Mwana wa Maryam عليه السلام:

<sup>1</sup> At-Tabari 16:564.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:561.

ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ اتَّخِذُونِي وَأُمَّيَ إِلَهَيْنِ مِنْ دُونِ اللَّهِ<sup>ط</sup>

**“Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu?” (5:116) mpaka,**

قَالَ اللَّهُ هَذَا يَوْمٌ يَنْفَعُ الصَّادِقِينَ صِدْقُهُمْ<sup>ط</sup>

**“Hii ndiyo Siku ambayo wasemao kweli utawafaa ukweli wao.” (5:119)**

Amesema atasimama Iblisi – Allah تعالى Amemlaani atasema:

وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِنْ سُلْطٰنٍ اِلَّا اَنْ دَعَوْتُكُمْ فَاَسْتَجِبْتُمْ لِي<sup>ط</sup>

**“Na sikuwa na mamlaka juu yenu, isipokuwa nilikuiteni, nanyi mkaniitikia.”<sup>1</sup>**

Kisha wakati Alipotaja Allah تعالى mwisho wa waovu, na ile hali ambayo wamekuwa juu yake miongoni mwa fedheha na mateso, na Akataja msemaji wao ni Iblisi. Kisha Ameunganisha hali ya mwisho wa watu wema, Amesema:

وَأُدْخِلَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحٰتِ جَنَّٰتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

**“Na walioamini na wakatenda mema wataingizwa katika bustani zipitazo mito kati yake,...”**

Zinapita popote watakapo na namna waitakayo,

خٰلِدِينَ فِيهَا

**“...wadumu humo...”**

Watakaa milele hawabadiliki na hawaondoki.

بِإِذْنِ رَبِّهِمْ تَحِيَّاتٌ فِيهَا سَلَامٌ<sup>ط</sup>

**“...kwa Idhini ya Mola Wao Mlezi. Maamkio yao humo yatakuwa: Salaam!”**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:562.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا وَفُتِحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلَامٌ عَلَيْكُمْ

**"...mpaka watakapofikilia, nayo milango yake imekwisha funguliwa. Walinzi wake watawaambia: Salaam Alaikum, Amani iwe juu yenu!" (39:73)**

وَالْمَلَائِكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿١٣﴾ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ

**"Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango (Wakiwaambia) Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu," (13:23-24)**

وَيُلَقَّوْنَ فِيهَا حَيًّا وَسَلَامًا

**"...na watakuta humo maamkio na salamu." (25:75)**

دَعْوَتُهُمْ فِيهَا سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ۗ وَآخِرُ دَعْوَتُهُمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ

الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

**"Wito wao humo utakuwa: Subhanaka Llahumma "Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu!" Na maamkio yao humo ni "Salama". Na mwisho wa wito wao ni: Alhamdulillah Rabbil A'lamiin "Kuhimidiwa Kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote." (10:10)**

\* \* \*



أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ  
 أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ ﴿٢٤﴾ تُوْتِي أَكْلَهَا كُلَّ  
 حِينٍ بِإِذْنِ رَبِّهَا ۗ وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ  
 يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٥﴾ وَمِثْلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ  
 آجَتْتُ مِنْ فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٢٦﴾ يُثْبِتُ اللَّهُ  
 الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي  
 الْآخِرَةِ ۗ وَيُضِلُّ اللَّهُ الظَّالِمِينَ ۚ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ﴿٢٧﴾  
 \* أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ  
 دَارَ النَّوَارِ ﴿٢٨﴾ جَهَنَّمَ يَصَلُّونَهَا ۗ وَيَنْسَوْنَ الْفَرَآءَ ﴿٢٩﴾  
 وَجَعَلُوا لِلَّهِ أُنْدَادًا لِيُضِلُّوا عَنْ سَبِيلِهِ ۗ قُلْ تَمَتَّعُوا فَإِنَّ  
 مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ ﴿٣٠﴾ قُلْ لِعِبَادِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 يُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُنْفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً مِّنْ  
 قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خِلَالَ ﴿٣١﴾ اللَّهُ الَّذِي  
 خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ  
 بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۗ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْفُلُوكَ لِيَتَّجِرَ  
 فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ ۗ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْأَنْهَارَ ﴿٣٢﴾ وَسَخَّرَ لَكُمُ  
 الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبَيْنِ ۗ وَسَخَّرَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ ﴿٣٣﴾  
 وَءَاتَاكُمْ مِّنْ كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ ۗ وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ لَا  
 تُحْصُونَهَا ۗ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَظُلُومٌ كَفَّارٌ ﴿٣٤﴾

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً  
 طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ  
 وَفَرْعُهَا فِي السَّمَاءِ ﴿٢٤﴾ تُوْتِي  
 أَكْلَهَا كُلَّ حِينٍ بِإِذْنِ رَبِّهَا ۗ  
 وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ  
 يَتَذَكَّرُونَ ﴿٢٥﴾ وَمِثْلُ كَلِمَةٍ  
 خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ آجَتْتُ مِنْ  
 فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ ﴿٢٦﴾

24. Hebu hukuona vipi  
 Mwenyezi Mungu Alivyo-  
 piga mfano wa neno zuri?  
 Ni kama mti mzuri, mizizi  
 yake ni imara, na matawi  
 yake yako mbinguni.

25. Hutoa Matunda yake  
 kila wakati kwa idhini ya  
 Mola wake Mlezi. Na  
 Mwenyezi Mungu Huwa-  
 pigia watu mifano ili  
 wapate kukumbuka.

26. Na mfano wa neno ovu  
 ni kama mti muovu,  
 uliong'olewa juu ya ardhi.  
 Hauna imara.

## Mfano wa Tamko la Uislamu na Tamko la Ukafiri

Amesema Ali bin Aby Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake,

مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً

**“...Alivyo piga mfano wa neno zuri?”**

Ambalo ni kushuhudia kwamba hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki asiyekuwa Allah تعالى:

كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ

**“Ni kama mti mzuri.”** Naye ni muumini.

أَصْلُهَا ثَابِتٌ

**“...mizizi yake ni imara.”**

Inaashiria kuwa *Laa Ilaaha Illallah* (hapana Mwenye kustahiki kuabudiwa kwa haki asiyekuwa Allah) ni imara moyoni mwa Muumini.

وَفَرَعُهَا فِي السَّمَاءِ

**“...na matawi yake yako mbinguni.”**

Anasema Ananyanyua kwa tamko hilo matendo ya muumini kuyapeleka mbinguni.<sup>1</sup> Kama hivi amesema Adh-Dhahhak na Saeed Bin Jubair na Ikrimah na Mujahid, na wengine.<sup>2</sup> Kwa hakika maneno hayo ni msemu unaoelezea matendo ya muumini, maneno yake mazuri na matendo yake mema. Na kwamba muumini ni kama mti wa mtende, haachi kuwa yananyanyuliwa matendo yake mema katika kila asubuhi na jioni.

Al-Bukhari amenukuu kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما amesema, tulikuwa mbele ya Mtume ﷺ akasema:

«أَخْبِرُونِي عَنْ شَجَرَةٍ تُشْبِهُ - أَوْ - كَالرَّجُلِ الْمُسْلِمِ لَا يَتَحَاثُّ وَرَفَهَا صَنِيفًا وَلَا سِنَاءً، وَتُوِي أكلها كُلَّ جِينٍ بِإِذْنِ رَبِّهَا»

<sup>1</sup> At-Tabari 16:557.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:572-573.

*“Nielezeni kuhusu mti ambao unaofanana au alisema kama mtu Muislamu, hayapukutiki majani yake wakati wa kaskazi wala wakati wa kusi na unatoa matunda yake kila wakati kwa amri ya Bwana wake.”*

Ibn Umar رضي الله عنهما amesema: Ikatuka katika nafsi yangu kwamba mti huo ni mtende na niliwaona Abubakri na Umar رضي الله عنهما hawazungumzi nikachukia kuzungumza ilipokuwa hawakusema kitu chochote. Mtume ﷺ alisema,

«هِيَ النَّخْلَةُ»

*“Huo ni mtende.”*

Tuliposimama nilisema kumuambia Umar رضي الله عنه, ‘Ee Baba yangu naapa kwa Allah تعالى ilikuwa imetuka katika nafsi yangu kwamba mti huo ni mtende.’ Akasema: ‘Ni jambo gani ambalo limekuzuia usiseme?’ Nikasema, ‘sikuwaona nyinyi mnazungumza, nikachukia kuzungumza au kusema kitu chochote.’ Umar رضي الله عنه akasema: ‘Kwa hakika lau ungeusema mti huo, ingependeza sana kwangu kuliko kitu kadhaa na kadhaa.’<sup>1</sup>

Na imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ

*“Ni kama mti mzuri.”*

Amesema huo ni mti uko Peponi.<sup>2</sup> Na Kauli Yake.

تُؤْتِي أَكْلَهَا كُلَّ حِينٍ

*“Hutoa matunda yake kila wakati...”*

Pamesemwa asubuhi na jioni. Na lililo wazi katika mtiririko wa maneno ni kwamba muumini mfano wake ni kama mfano wa mti. Hayaachi kuwepo katika mti huo matunda katika kila wakati miongoni mwa wakati wa kaskazi, au wa kusi, usiku au mchana. Ni kama hivyo muumini haachi kuwa yananyanyuliwa kwake matendo mema, nyakati za usiku na ncha za mchana katika nyakati zote.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:228.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:573.

بِإِذْنِ رَبِّهَا<sup>١</sup>

“...*kwa idhini ya Mola wake Mlezi.*” Maana yake: Hali ya kukamilika, hali ya kuwa mazuri hali ya kuwa mengi yaliyo bora yenye kubarikiwa.

وَيَضْرِبُ اللَّهُ الْأَمْثَالَ لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ

**“Na Mwenyezi Mungu Huwapigia watu Mifano Ili Wapate Kukumbuka.”**

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَثَلُ كَلِمَةٍ خَبِيثَةٍ كَشَجَرَةٍ خَبِيثَةٍ

**“Na mfano wa neno ovu ni kama mti muovu...”**

Huu ni mfano wa ukafiri wa mwenye kukufuru, hauna shina na haukuthibiti, umefananishwa na mti wa kitango mwitu na unaitwa mti huo *A-Sharyan*. Amesimulia hilo Shuba kutoka kwa Muawiya bin Qarra kutoka kwa Anasi bin Maliki رحمه الله تعالى kwamba mti huo ni mti wa kitango mwitu:<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

أَجْتَنَّتْ

**“...uliong’olewa...”** Maana yake: Umekatwa mizizi,

مِن فَوْقِ الْأَرْضِ مَا لَهَا مِنْ قَرَارٍ

**“...juu ya ardhi. Hauna imara.”**

Maana yake: Hauna shina wala kuthibiti. Ni kama ukafiri hauna shina wala tawi, na haipandi kwa kafiri amali yeyote na hakikubaliwi kwake kitu chochote.

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ وَيُضِلُّ اللَّهُ  
الظَّالِمِينَ<sup>٢</sup> وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ﴿٢٧﴾

**27. Mwenyezi Mungu Huwatia uimara wenye kuamini kwa kauli imara katika maisha ya dunia na katika Akhera. Na Mwenyezi Mungu Huwaacha kupotea hao wenye kudhulumu. Na Mwenyezi Mungu Hufanya Apendavyo.**

<sup>1</sup> At-Tabari 16:569.

## Allah تعالى Huwaweka Waumini Katika Uimara Duniani na Akhera Katika Kauli Iliyo Imara

Al-Bukhari amepokea kutoka kwa Al-Baraa bin Aazib رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«الْمُسْلِمُ إِذَا سُئِلَ فِي الْقَبْرِ شَهِدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولَ اللَّهِ، فَذَلِكَ قَوْلُهُ:

*“Muislamu atakapoulizwa kaburini atashuhudia kwamba hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.”*

Hayo Ndiyo Maneno Yake.

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ط

*“Mwenyezi Mungu Huwatia Uimara Wenye Kuamini kwa kauli Imara Katika Maisha ya Dunia na Katika Akhera.”<sup>1</sup>*

Muslim ameipokea vilevile na jamaa wote.<sup>2</sup> Na amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Al-Baraa bin Aazib رضي الله عنه amesema: ‘Tulitoka pamoja na Mtume ﷺ katika jeneza la mtu katika Answare, tukakomelea kaburini na maiti ilikuwa haijawekwa katika mwanandani, na hali ya kuwa mkononi mwake Mtume ﷺ pana ujiti, anachokoachokoa kwa ujiti huo katika ardhi, akanyanyua kichwa chake akasema:

«اسْتَعِينُوا بِاللهِ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ»

*“Takeni hifadhi kwa Mwenyezi Mungu na adhabu ya kaburi.”*

Aliyasema hayo mara mbili au mara tatu. Kisha akasema:

«إِنَّ الْعَبْدَ الْمُؤْمِنَ إِذَا كَانَ فِي انْقِطَاعٍ مِنَ الدُّنْيَا وَإِقْبَالٍ مِنَ الْآخِرَةِ، نَزَلَ إِلَيْهِ مَلَائِكَةٌ مِنَ السَّمَاءِ يَبِضُّ أَلْوَجُوهَ، كَأَنَّ وُجُوهَهُمُ السَّمْسُ، مَعَهُمْ كَفَنٌ مِنَ أَكْفَانِ الْجَنَّةِ، وَخَنُوطٌ مِنْ خَنُوطِ الْجَنَّةِ، حَتَّى يَجْلِسُوا مِنْهُ مَدَّ الْبَصْرِ، ثُمَّ يَجِيءُ مَلَكُ الْمَوْتِ حَتَّى يَجْلِسَ عِنْدَ رَأْسِهِ، فَيَقُولُ: أَيَّتَهَا النَّفْسُ الطَّيِّبَةُ أَخْرَجِي إِلَى مَغْفِرَةٍ مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانِ

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:229.

<sup>2</sup> Muslim 4:2201, Abu Dawud 5:112, Tuhat Al-Ahwadhi 8:547, An-Nisai katika As-Sunan Al-Kubra 6:372.

- قَالَ - : فَتَخْرُجُ تَسِيلًا، كَمَا تَسِيلُ الْفَطْرَةُ مِنْ فِي السَّمَاءِ، فَيَأْخُذُهَا، فَإِذَا أَخَذَهَا لَمْ يَدْعُوهَا فِي يَدِهِ طَرْفَةً عَيْنٍ حَتَّى يَأْخُذُوهَا فَيَجْعَلُوهَا فِي ذَلِكَ الْكَفِّ فِي ذَلِكَ الْخُطُوطِ، وَيَخْرُجُ مِنْهَا كَأَطِيبٍ نَفَحَ مِنْكَ وَجِدْتَ عَلَى وَجْهِ الْأَرْضِ، فَيَضَعُونَ بِهَا فَلَا يَمُرُّونَ بِهَا، يَعْنِي عَلَى مَلَأَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ، إِلَّا قَالُوا: مَا هَذِهِ الرُّوحُ الطَّيِّبَةُ؟ فَيَقُولُونَ: فُلَانٌ بَنُ فُلَانٍ بِأَحْسَنِ أَسْمَائِهِ الَّتِي كَانُوا يُسَمُّونَهُ بِهَا فِي الدُّنْيَا حَتَّى يَسْتَهْوَأَ بِهِنَّ إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا فَيَسْتَفْتِحُونَ لَهُ، فَيُنْتَحَ لَهُ فَيَسْبِعُهُ مِنْ كُلِّ سَمَاءٍ مُقَرَّبُوهَا إِلَى السَّمَاءِ الَّتِي تَلِيهَا، حَتَّى يُتَمَّى بِهَا إِلَى السَّمَاءِ السَّابِعَةِ، فَيَقُولُ اللَّهُ: اكْتُبُوا كِتَابَ عَبْدِي فِي عِلِّيِّينَ وَأَعِيدُوهُ إِلَى الْأَرْضِ، فَإِنِّي مِنْهَا خَلَقْتُهُمْ وَفِيهَا أَعِيدُهُمْ، وَمِنْهَا أَخْرَجْتُهُمْ نَارَةَ أُخْرَى، قَالَ: فَتَعَادَ رُوحُهُ فِي جَسَدِهِ، فَيَأْتِيهِ مَلَكَانِ فَيَجْلِسَانِيهِ فَيَقُولَانِ لَهُ: مَنْ رَبُّكَ؟ فَيَقُولُ: رَبِّي اللَّهُ، فَيَقُولَانِ لَهُ: مَا دِينُكَ؟ فَيَقُولُ: دِينِي الْإِسْلَامُ، فَيَقُولَانِ لَهُ: مَا هَذَا الرَّجُلُ الَّذِي بَعَثَ فِيكُمْ؟ فَيَقُولُ: هُوَ رَسُولُ اللَّهِ، فَيَقُولَانِ لَهُ: وَمَا عِلْمُكَ؟ فَيَقُولُ: قَرَأْتُ كِتَابَ اللَّهِ فَأَمَنْتُ بِهِ وَصَدَّقْتُ، فَيَنَادِي مُنَادٍ مِنَ السَّمَاءِ: أَنْ صَدَقَ عَبْدِي فَأَفْرِشُوهُ مِنَ الْجَنَّةِ، وَأَلْبِسُوهُ مِنَ الْجَنَّةِ، وَاقْتَحُوا لَهُ أَبَا إِلَى الْجَنَّةِ - قَالَ - : فَيَأْتِيهِ مِنْ رُوحِهَا وَطِيْبِهَا وَيُنْفَسِحُ لَهُ فِي قَبْرِهِ مَدَّةَ بَصَرِهِ وَيَأْتِيهِ رَجُلٌ حَسَنُ الْوَجْهِ، حَسَنُ الثِّيَابِ، طَيِّبُ الرَّيْحِ، فَيَقُولُ: أَبْيَضُ بِالَّذِي يُسْرُكُ، هَذَا يَوْمُكَ الَّذِي كُنْتَ تُوعَدُ، فَيَقُولُ لَهُ: مَنْ أَنْتَ فَوْجُوكَ الرَّجْمَةُ الَّتِي يَأْتِي بِالْخَيْرِ؟ فَيَقُولُ: أَنَا عَمَلُكَ الصَّالِحِ، فَيَقُولُ: رَبِّ أَوِّمِ السَّاعَةَ رَبِّ أَوِّمِ السَّاعَةَ، حَتَّى أَرْجِعَ إِلَى أَهْلِي وَمَالِي.

*"Hakika mja muumini anapokuwa anaiaga dunia na kuelekea akhera, humshukia malaika kutoka mbinguni, wenye nyuso nyeupe, kana kwamba nyuso zao ni jua. Hali ya kuwa wana sanda katika sanda za peponi, na dalia katika dalia za peponi, mpaka watakaa kwake kiasi cha upeo wa macho. Kisha atakuja malaika wa mauti mpaka atakaa kichwani kwake atasema: 'Ee nafsi njema toka uende kwenye msamaha wa Allah na radhi zake - amesema roho itatoka hali ya kuwa inatirizika kama linavyotirizika tone kutoka katika kiriba, malakulmauti ataichukua, atakapoichukua hataiacha mkononi kwake kiasi cha fumba jicho, mpaka -waichukue na waiweke katika sanda hiyo na katika dalia hiyo. Na utatoka katika nafsi hiyo kama uzuri wa harufu ya miski, iliyopatikana katika uso wa ardhi.*

Watapanda nayo mbinguni, hawatapita nayo juu ya kundi la malaika isipokuwa watasema: 'Ni harufu gani hii nzuri?' Watasema: 'Fulani bin Fulani, kwa jina lililo zuri sana katika majina yake', ambalo walikuwa wanamuita kwayo duniani, mpaka watakomelea naye kwenye mbingu ya dunia, wataomba afunguliwe atafunguliwa watamsindikiza katika kila mbingu, wale wenye kukurubishwa mpaka kwenye mbingu ambayo inafuatia, mpaka atakomelea kwenye mbingu ya saba, Atasema Allah: 'Kiandikeni kitabu cha mja Wangu katika Illiyyin,<sup>1</sup> na mrudisheni ardhini kwani Mimi kutokana na hiyo ardhi Nimewaumba na katika hiyo ardhi Nitawarudisha na katika hiyo ardhi Nitawarudisha mara nyingine.' Amesema: 'Itarudishwa roho yake kwenye mwili wake watamjia malaika wawili watamkalisha watamuuliza: 'Nani Bwana wako?' Atasema, 'Bwana wangu ni Allah.' Watamuuliza, 'Dini yako ni ipi?' Atasema, 'Dini yangu ni Uislamu.' Watamuuliza, 'Ni nani huyo mtu ambaye amepelekwa kwenu?' Atasema, 'huyo ni Mtume wa Allah.' Watamuuliza, 'ni ipi elimu yako?' Atasema, 'nimesoma kitabu cha Allah, nikamuamini na nikamsadiki.' Atanadi mwenye kunadi kutoka mbinguni; kwamba, 'amesema kweli mja wangu mtandikieni na mfungulieni mlango wa peponi.' Amesema, 'utamjia upepo wake na manukato yake na atapanuliwa katika kaburi lake, upeo wa macho yake, na atamjia mtu mzuri wa uso, mzuri wa nguo mzuri wa harufu atamuambia: 'Furahi kwa lile ambalo linakufurahisha, hii ndiyo siku yako ambayo ulikuwa unaahidiwa.' Atamuuliza, 'ni nani wewe kwani uso wako ni uso unaoleta kheri' Atasema: 'Mimi ni amali yako njema.' Atasema: 'Ee Bwana wangu kisimamisha Kiyama, Ee Bwana wangu kisimamisha Kiyama ili nirejee kwa watu wangu na amali zangu."

قَالَ: وَإِنَّ الْعَبْدَ الْكَافِرَ إِذَا كَانَ فِي انْقِطَاعِ مِنَ الدُّنْيَا وَإِقْبَالِ مِنَ الْآخِرَةِ، نَزَلَ إِلَيْهِ مَلَائِكَةٌ مِنَ السَّمَاءِ سُودُ الْوُجُوهِ مَعَهُمُ الْمُسُوحُ، فَجَلَسُوا مِنْهُ مَدَّ الْبَصَرِ، ثُمَّ يَجِيءُ مَلَكُ الْمَوْتِ فَيَجْلِسُ عِنْدَ رَأْسِهِ، فَيَقُولُ: أَيُّهَا النَّفْسُ الْحَيَّةُ، أَخْرِجِي إِلَى سَخَطِ مِنِ اللَّهِ وَعَظْبٍ - قَالَ - : فَتَفْرَقُ فِي جَسَدِهِ فَيَتَرَعُّهَا كَمَا يَتَرَعُّ السَّفُودُ مِنَ الصُّوفِ الْمَبْلُورِ، فَيَأْخُذُهَا فَإِذَا أَخَذَهَا لَمْ يَدْعُوهَا فِي يَدِهِ طَرْفَةَ عَيْنٍ حَتَّى يَجْعَلُوهَا فِي بَلَدِ

<sup>1</sup> Angalia Surat Al-Mutaffifin 83: 18-21.

الْمُسُوحِ، فَيَخْرُجُ مِنْهَا كَأَنَّتِ رِيحٌ جَبِيْفَةٌ وَجِدَتْ عَلَى وَجْهِ الْأَرْضِ، فَيَضَعُدُونَ بِهَا، فَلَا يَمْرُونَ بِهَا عَلَى مَلَأٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِلَّا قَالُوا: مَا هَذِهِ الرُّوحُ الْحَيَّةُ؟ يَقُولُونَ: فُلَانُ بْنُ فُلَانٍ بِأَقْبَحِ أَسْمَائِهِ الَّتِي كَانَ يُسَمِّي بِهَا فِي الدُّنْيَا، حَتَّى بُتِّهِيَ بِهَا إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا، فَيَسْتَفْتَحُ لَهُ فَلَا يَفْتَحُ لَهُ - ثُمَّ قَرَأَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: ﴿لَا تَفْتَحْ لَمْ أُوبُ السَّمَاءَ وَلَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ حَتَّى يَلِجَ الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْلِيْلِيَّةِ﴾ يَقُولُ اللَّهُ: اكْتُبُوا كِتَابَهُ فِي سَجِّينَ فِي الْأَرْضِ السُّفْلَى، فَتَطْرُحُ رُوحَهُ طَرْحًا - ثُمَّ قَرَأَ ﴿وَمَنْ يُنْكِرْ بِاللَّهِ فُكَاَنَّمَآ خَرَّ مِنْ السَّمَاءِ فَتَخْطَفُهُ الطَّيْرُ أَوْ تَهْوِي بِهِ الرِّيحُ فِي مَكَانٍ سَجِيْنٍ﴾ فَتَعَادُ رُوحَهُ فِي حَسْبِيهِ، وَيَأْتِيهِ مَلَكَانِ فَيُجْلِسَانِيهِ وَيَقُولَانِ لَهُ: مَنْ رُبُّكَ؟ يَقُولُ: هَاهُ هَاهُ لَا أَدْرِي، يَقُولَانِ لَهُ: مَا دِيْنُكَ؟ يَقُولُ: هَاهُ هَاهُ لَا أَدْرِي، يَقُولَانِ لَهُ: مَا هَذَا الرَّجُلُ الَّذِي بُعِثَ فِيكُمْ؟ يَقُولُ: هَاهُ هَاهُ لَا أَدْرِي، فَيُنَادِي مُنَادٍ مِنَ السَّمَاءِ: أَنْ كَذَبَ عَبْدِي فَأَفْرِشُوهُ مِنَ النَّارِ، وَافْتَحُوا لَهُ بَابًا إِلَى النَّارِ، فَيَأْتِيهِ مِنْ حَرِّهَا وَسُمُومِهَا، وَيَضِيْقُ عَلَيْهِ قَبْرُهُ حَتَّى تَخْتَلِفَ فِيهِ أَضْلَاعُهُ، وَيَأْتِيهِ رَجُلٌ قَبِيْحُ الْوَجْهِ، قَبِيْحُ الثِّيَابِ، مُنِينُ الرِّيحِ، يَقُولُ: أَبَشِرْ بِالَّذِي يَسُوْؤُكَ، هَذَا يَوْمُكَ الَّذِي كُنْتَ تُوعَدُ، يَقُولُ: وَمَنْ أَنْتَ، فَوَجْهُكَ الْوَجْهُ يَجِيءُ بِالشَّرِّ؟ يَقُولُ: أَنَا عَمَلُكَ الْحَيِّثُ، يَقُولُ: رَبُّ لَا يُقِيْمُ السَّاعَةَ

*"Amesema: na kwa hakika mja kafiri pindi atakapoiaga dunia na kuelekea akhera, watamshukia malaika kutoka mbinguni wenye nyuso nyeusi wakiwa na musuh<sup>1</sup> watakaa kwake kiasi cha upeo wa macho, kisha atakuja malaika wa mauti atakaa kichwani kwake atasema: 'Ee, nafsi mbaya: toka uelekee kwenye Machukivu ya Allah na Ghadhabu Yake.' Amesema: 'Itatawanywa nafsi yake katika mwili wake wote. Ataivuta kama kinavyovutwa chuma cha kuchomea nyama kutoka katika sufi iliyorowanishwa katika maji. Ataichukua, atakapoichukua hawataiacha mkononi mwake kiasi cha kufumba macho, mpaka wataiweka katika yale maguo. Itatoka kutokana na nafsi hiyo, harufu mbaya ya mzoga, uliyopatikana katika uso wa ardhi. Watapanda nayo, hawatapita nayo juu ya kundi la malaika isipokuwa watasema: 'ni roho gani hii mbaya?' Watasema: 'Fulani bin Fulani kwa jina lilo baya sana katika majina yake ambayo alikuwa*

<sup>1</sup> Kipande kigumu na kinene cha nguo kilichotengenezwa kwa ngozi.



anaitwa kwayo huko duniani, mpaka patakomelewa nayo kwenye mbingu ya dunia, pataombwa ifunguliwe haitafunguliwa. Kisha akasoma Mtume ﷺ "...hawatafunguliwa milango ya mbingu, wala hawataingia Peponi mpaka apite ngamia katika tundu ya sindano." (7:40) Atasema Allah: 'Yaandikeni maandishi yake katika Sijjin.'<sup>1</sup> Katika ardhi ya chini itatupwa roho yake kwa nguvu, kisha akasoma: "Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukamtupa pahala mbali." (22:31) itarudishwa roho yake mwilini mwake watamuendea, malaika wawili watamkalisha na watamuuliza, 'ni nani Bwana wako?' Atajibu: 'Aah Hah sielewi.' Watamuuliza: 'ni ipi Dini yako?' Atasema, 'Hah Hah, sielewi.' Watamuuliza: 'Ni yupi huyu mtu ambaye amepelekwa kwenu?' Atasema, 'Hah Hah sielewi.' Atanadi mwenye kunadi kutoka mbinguni, kwamba, 'amesema urongo mja wangu mtandikieni huko motoni na mfungulieni mlango wenye kuelekea motoni.' Kwa hiyo litamjia joto lake, na hewa yake ya moto, yenye kuingia katika kaburi yake. Na litakuwa finyu kaburi lake mpaka zitapishana kwake mbavu zake. Na atamuendea mtu mbaya wa uso, mbaya wa mavazi, mwenye harufu ya uvundo, atasema, 'lia kwa lile ambalo linakuudhi, hii ndiyo siku yako ambayo ulikuwa unaahidiwa.' Atauliza, 'ni nani wewe? Kwani uso wako ni uso ambao inakuja shari.' Atajibu, 'mimi ni amali yako mbaya.' Atasema: 'Ee Bwana wangu usikisimamishe Kiyama.'" Ameipokea Hadithi hii Abu Dawud na Ibn Maja.<sup>2</sup>

Ameipokea Imam Abdu Bin Humaid رحمه الله تعالى, katika kitabu chake cha Musnad kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه amesema. Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ الْعَبْدَ إِذَا وُضِعَ فِي قَبْرِهِ، وَتَوَلَّى عَنْهُ أَصْحَابُهُ، وَإِنَّهُ لَيَسْمَعُ قَرْعَ نِعَالِهِمْ، فَيَأْتِيهِ مَلَكَانِ فَيَقْعِدَانِهِ فَيَقُولَانِ لَهُ: مَا كُنْتَ تَقُولُ فِي هَذَا الرَّجُلِ؟ قَالَ: فَأَمَّا الْمُؤْمِنُ فَيَقُولُ: أَشْهَدُ أَنَّهُ عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ، قَالَ: فَيَقَالُ لَهُ: انظُرْ إِلَى مَقْعِدِكَ مِنَ النَّارِ قَدْ أَبْدَلَكَ اللَّهُ بِمَقْعِدًا مِنَ الْجَنَّةِ»

<sup>1</sup> Angalia Surat Al-Mutaffifin 83: 8.

<sup>2</sup> Ahmad 4:287, Sunan Abu Dawud 3:546, An-Nasai 4:78, Ibn Majah 1:494

“Kwa hakika mja atakapowekwa katika kaburi lake na wakamuondokea watu wake. Huku yeye akisikia vishindo vya viatu vyao. Watamjia malaika wawili, watamkalisha watamuuliza, ‘ni kitu gani ulichokuwa unakisema kwa mtu huyu?’ Amesema: ‘Ama muumini atasema: ‘Ninashuhudia kwamba yeye ni mja wa Allah na Mjumbe wake.’ Amesema, ‘Ataambiwa yatazame makazi yako motoni kwa hakika amekubadilishia Mwenyezi Mungu kwa makazi hayo, makazi mengine peponi.”

Mtume ﷺ amesema ,

«فَيَرَاهُمَا جَمِيعًا»

“Atayaona makazi yake mawili.”

Qatada amesema : Na tumetajiwa kwamba yeye atapanuliwa katika kaburi lake dhira sabini na itajazwa kwake mimea ya kijani mpaka siku ya Kiyama.<sup>1</sup> Muslim ameipokea kutoka kwa Abdi bin Humaid na ameithibitisha Al-Nasai kutokana na hadithi ya Yunus bin Muhammad Al-Muaddab.<sup>2</sup>

Na Al\_Hafidhi Abu Issa Al-Tirmidhy رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه amesema. Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا فُيِّرَ الْمَيِّتُ - أَوْ قَالَ: أَحَدُكُمْ - أَنَاهُ مَلَكَانِ أَسْوَدَانِ أَرْزَقَانِ، يُقَالُ لِأَحَدِهِمَا مُنْكَرٌ وَالْآخِرُ نَكِيرٌ، فَيَقُولَانِ: مَا كُنْتَ تَقُولُ فِي هَذَا الرَّجُلِ؟ فَيَقُولُ: مَا كَانَ يَقُولُ هُوَ عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ، أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، فَيَقُولَانِ: قَدْ كُنَّا نَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُولُ هَذَا، ثُمَّ يُفْسَخُ لَهُ فِي قَبْرِهِ سَبْعُونَ ذِرَاعًا فِي سَبْعِينَ، وَيُتَوَرَّ لَهُ فِيهِ، ثُمَّ يُقَالُ لَهُ: نَمْ، فَيَقُولُ: أَرْجِعْ إِلَى أَهْلِي فَأَخْبِرْهُمْ، فَيَقُولَانِ: نَمْ نَوْمَةَ الْأَعْرُوسِ الَّذِي لَا يُوقِظُهُ إِلَّا أَحَبُّ أَهْلِهِ إِلَيْهِ حَتَّى يَبْعَثَهُ اللَّهُ مِنْ مَضْجَعِهِ ذَلِكَ، وَإِنْ كَانَ مُتَأَيِّفًا قَالَ: سَمِعْتُ النَّاسَ يَقُولُونَ: نَقَلْتُ مِنْهُمْ لَا أُدْرِي، فَيَقُولَانِ: قَدْ كُنَّا نَعْلَمُ أَنَّكَ تَقُولُ هَذَا، فَيُقَالُ لِلْأَرْضِ: الْتَبِيحِي عَلَيْهِ فَتَلْتَبِي عَلَيْهِ حَتَّى تَخْتَلِفَ أَضْلَاعُهُ، فَلَا يَرَأَى فِيهَا مُعَذَّبًا حَتَّى يَبْعَثَهُ اللَّهُ مِنْ مَضْجَعِهِ ذَلِكَ»

“Atakapozikwa maiti au alisema: Mmoja wenu – watamuendea Malaika wawili weusi, anaitwa mmoja wao Munkar na mwingine

<sup>1</sup> Al-Muntakhab cha 'Abd bin Humayd, na. 1178.

<sup>2</sup> Muslim na. 2670, An-Nasai, 4:97.

*anaitwa Nakir, watamuuliza, 'ni kitu gani ambacho ulikuwa unasema kwa mtu huyu?' Anayasema yale aliyokuwa akiyasema yeye kuwa, 'ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, na nakiri kwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ni nakiri kwamba Muhammad ni mja Wake na Mjumbe Wake.' Watasema: 'Kwa hakika tulikuwa tunajua kwamba wewe ulikuwa unasema hivyo.' Kisha atapanuliwa katika kaburi lake kiasi cha dhira sabiini kwa sabiini, na atatiliwa taa kisha ataambiwa: 'Lala.' Atasema: 'Nitarejea kwa watu wangu niwaeleze watuambia lala kulala kwa arusi ambaye hamuamshi isipokuwa yule anayempenda sana katika watu wake mpaka atakapomfufua Mwenyezi Mungu katika malazi yake hayo.' Na akiwa ni mtu mnafiki atasema: 'Niliwasikia watu wakisema nami nikasema wao sielewi.' Watasema: 'kwa hakika tulikuwa tunajua kwamba wewe unasema hivyo.' Itaambiwa ardhi, 'ungana juu yake', itaungana juu yake mpaka zipishane mbavu zake. Hataacha kuwa katika hali hiyo ya kuadhibiwa mpaka atakapomfufua Mwenyezi Mungu kutoka katika malazi yake hayo."*

Kisha A-Tirmidhy amesema: hii ni hadithi Hassan Ghareeb.<sup>1</sup>

Imepokewa kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kuwa amesema, Mtume ﷺ amesema;

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ط

**"Mwenyezi Mungu Huwatia uimara wenye kuamini kwa kauli imara katika maisha ya dunia na katika Akhera."**

ذٰلِكَ اِذَا قِيْلَ لَهُ فِى الْقَبْرِ مَنْ رَبُّكَ، وَمَا دِيْنُكَ، وَمَنْ نَّبِيُّكَ؟ فَيَقُوْلُ: رَبِّيَ اللهُ، وَدِيْنِي الْاِسْلَامُ، وَنَبِيِّ مُحَمَّدٌ جَاءَنَا بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ عِنْدِ اللهِ، فَاَمَنْتُ بِهِ وَصَدَّقْتُ، فَيَقَالُ لَهُ: صَدَقْتَ، عَلٰى هٰذَا عِشْتَ، وَعَلَيْهِ مِتَّ، وَعَلَيْهِ تُبْعَثُ

Amesema: hilo ni pale atakapoulizwa katika kaburi, 'ni nani Bwana wako? Na ni ipi Dini yako? Na ni nani Mtume wako?' Atasema,

<sup>1</sup> At-Tirmidhi 10:71.

'Bwana wangu ni Allah na Dini yangu ni Uislamu na Mtume wangu ni Muhammad ﷺ, ametujia na ishara zilizo wazi kutoka kwa Mwenyezi Mungu nikamuamini na nikamsadikisha.' Ataambiwa, 'Umeseema kweli, juu ya haya uliishi, na juu ya haya umekufa na juu ya haya utafufuliwa.'<sup>1</sup>

Ibn Jariri رحمه الله تعالى amemnuuu Abu Huraira رضي الله عنه kuwa, Mtume ﷺ amesema:

«وَأَلَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، إِنَّ الْمَيِّتَ لَيَسْمَعُ حَقْفَ نِعَالِكُمْ حِينَ تُوَلُّونَ عَنْهُ مُذِيرِينَ، فَإِنْ كَانَ مُؤْمِنًا كَانَتِ الصَّلَاةُ عِنْدَ رَأْسِهِ وَالرَّكَاةُ عَنْ يَمِينِهِ وَالصُّوْمُ عَنْ بَسَارِهِ وَكَانَ فِعْلُ الْخَيْرَاتِ مِنَ الصَّدَقَةِ وَالصَّلَاةِ وَالْمَعْرُوفِ وَالْإِحْسَانِ إِلَى النَّاسِ عِنْدَ رِجْلَيْهِ، فَيُؤْتَى مِنْ قِبَلِ رَأْسِهِ، فَتَقُولُ الصَّلَاةُ: مَا قَبْلِي مَدْخَلٌ، فَيُؤْتَى عَنْ يَمِينِهِ فَتَقُولُ الرَّكَاةُ: مَا قَبْلِي مَدْخَلٌ، فَيُؤْتَى عَنْ بَسَارِهِ فَتَقُولُ الصِّيَامُ: مَا قَبْلِي مَدْخَلٌ، فَيُؤْتَى عِنْدَ رِجْلَيْهِ فَتَقُولُ فِعْلُ الْخَيْرَاتِ: مَا قَبْلِي مَدْخَلٌ، فَيَقَالُ لَهُ: اجْلِسْ، فَيَجْلِسُ قَدْ مَثَلَتْ لَهُ الشَّمْسُ قَدْ دَنَتْ لِلْمَعْرُوبِ، فَيَقَالُ لَهُ: أَخْبِرْنَا عَمَّا نَسَأَلُكَ، فَيَقُولُ: دَعْنِي حَتَّى أَصَلِّيَ، فَيَقَالُ لَهُ: إِنَّكَ سَتَفْعَلُ، فَأَخْبِرْنَا عَمَّا نَسَأَلُكَ، فَيَقُولُ: وَعَمَّ نَسَأَلُونِي؟ فَيَقَالُ: أَرَأَيْتَ هَذَا الرَّجُلَ الَّذِي كَانَ فِيكُمْ مَاذَا تَقُولُ بِهِ، وَمَاذَا تَشْهَدُ بِهِ عَلَيْهِ؟ فَيَقُولُ: أُمَحَمَّدٌ؟ فَيَقَالُ لَهُ: نَعَمْ، فَيَقُولُ: أَشْهَدُ أَنَّهُ رَسُولُ اللَّهِ، وَأَنَّهُ جَاءَنَا بِالْبَيِّنَاتِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ فَصَدَّقْتَاهُ، فَيَقَالُ لَهُ: عَلَى ذَلِكَ حَيِّتَ وَعَلَى ذَلِكَ مِتَّ، وَعَلَيْهِ بُعِثَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ، ثُمَّ يُنْسَخُ لَهُ فِي قَبْرِهِ سَبْعُونَ ذِرَاعًا وَيَتَوَرَّ لَهُ فِيهِ، وَيُفْتَحُ لَهُ بَابٌ إِلَى الْجَنَّةِ فَيَقَالُ لَهُ: انظُرْ إِلَى مَا أَعَدَّ اللَّهُ لَكَ فِيهَا، فَيَزِدَادُ عِنِطَةً وَسُرُورًا، ثُمَّ تُجْعَلُ نَسَمَتُهُ فِي النَّسَمِ الطَّيِّبِ، وَهِيَ طَيْرٌ خُضِرَ تَعْلُقُ بِشَجَرِ الْجَنَّةِ، وَيُعَادُ الْجَسَدُ إِلَى مَا بَدَى مِنْ التُّرَابِ»

"Naapa kwa Allah Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, kwa hakika maiti anasikia viatu vyenu wakati mnapoondoka na kumuacha kaburini hali akiwa ni muumini. Sala itakuwa mbele ya kichwa chake, na Zaka itakuwa kuliani kwake, na Saumu itakuwa kushotoni mwake. Na yatakuwa matendo ya kheri miongoni mwa sadaka na kuunga udugu na kufanya wema kwa watu miguuni kwake. Malaika atakwenda kwa upande wa kichwa chake, Sala

<sup>1</sup> At-Tabari 16:596.

itasema, 'hapana kwangu maingilio'. Ataendewa kwa upande wa kulia kwake, Zaka itasema, 'hapana kwangu maingilio.' Ataendewa upande wa kushotoni kwake Funga itasema, 'hapana upande wangu maingilio.' Ataendewa kwa upande wa miguu yake, matendo mema yatasema: 'hapana upande wangu maingilio.' Ataambiwa, 'kaa.' atakaa na hali ya kuwa limefananizwa kwake jua limekaribia kuzama, ataambiwa jibu kuhusu yale tutakayokuuliza, atasema: 'Niache hadi nisali.' Ataambiwa: 'kwa hakika utasali.' Bali kuhusu ambayo tutakuuliza, atasema, 'mtaniuliza kuhusu jambo gani?' Patasemwa: 'Je unamuonaje mtu huyu ambaye alikuwa kwenu, mlisema nini kuhusiana na yeye? Ni jambo gani unashuhudia kwalo juu yake.' Atajibu, 'mnauliza kuhusu Muhammad?' Patasemwa, 'ndiyo.' Atajibu: 'Ninashuhudia kwamba yeye ni Mjumbe wa Allah, na kwamba ametujia na ishara zilizo wazi kutoka kwa Allah, tukamsadiki.' Ataambiwa, 'juu ya hayo umeishi, na juu ya hayo umekufa, na juu ya hayo utafufuliwa apendapo Allah.' Kisha patapanuliwa kwa ajili yake kaburi lake, kiasi cha dhiraab sabini na atawekewa taa, katika kaburi lake; na utafunguliwa mlango wa kuelekea Peponi, ataambiwa: 'Angalia Aliyokuandalia Allah." Na humo atazidi kuvutiwa na kufurahi. Kisha itawekwa roho yake katika kundi la roho njema nao ni ndege wa kijani watakaoishi katika miti ya Peponi. Na utarudishwa mwili kwenye ile hali ambayo ulianza kwayo miongoni mwa udongo."

Na Hiyo Ndiyo Kauli Yake Allah تعالی:

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ط

**"Mwenyezi Mungu Huwatia uimara wenye kuamini kwa kauli imara katika maisha ya dunia na katika Akhera."**<sup>1</sup>

Ameyapokea hayo Ibn Hibban رحمه الله تعالى. Hivyo anayataja majibu ya kafiri na adhabu yake.<sup>2</sup> Na amepokea Abdurrazzaq رحمه الله تعالى kutoka kwa Twawusi.

<sup>1</sup> At-Tabari 16:596.

<sup>2</sup> Ibn Hibban 5:45.

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۗ

**“Mwenyezi Mungu Huwatia uimara wenye kuamini kwa kauli imara katika maisha ya dunia na katika Akhera.”**

Amesema: Hapana wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى.

وَفِي الْآخِرَةِ ۗ

**“...na katika Akhera...”**

Kuulizwa kaburini.<sup>1</sup> Qatadah amesema Ama duniani, Allah تعالى Atawawathibitisha kwa kheri na matendo mema.

وَفِي الْآخِرَةِ ۗ

**“...na katika Akhera...”**

Kaburini.<sup>2</sup> Na kama hivi wamesema wanawazuoni wengi waliotangulia.<sup>3</sup>

۞ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ۗ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا وَيَبْسُ الْقَرَارُ ۗ وَجَعَلُوا لِلَّهِ أُنْدَادًا لِيُضِلُّوا عَنْ سَبِيلِهِ ۗ قُلْ تَمَتَّعُوا فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ ۗ

**28. Hebu hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo?**

**29. Nayo ni Jahannamu! Maovu yaliyoje makaazi hayo!**

**30. Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili wapoteze watu kwenye njia yake. Sema: Stareheni! Kwani marejeo yenu ni Motoni!**

<sup>1</sup> Abdur-Razzaq 2:342.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:602.

<sup>3</sup> At-Tabari 16:602.

**Hatima ya Mwenye Kubadilisha Neema ya Allah تعالى kwa Kufuru**

Al-Bukhari Amesema Kauli Yake:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا

***“Hebu hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru...”***

Maana yake: ‘Je unayo Elimu juu ya hayo, hivyo hukujua.’ Kama Ilivyo Kauli Yake Allah تعالى

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ

***“Hebu hukuwaona...”***

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ خَرَجُوا

***“Hukuwaona wale waliotoka...”***

قَوْمًا بُورًا

***“...watu walioangamia.” (25:18)*** Al-Bawar maana yake ni maangamizi. Asili ya neno hili katika muktadha wa lugha ya kiarabu ni *Bara-Yabour-Bawran*. ‘Wenye kuangamia’ ametuzungumzia Ali bin Abdillahi, ametuzungumzia Sufyan kutoka kwa Amri bin Atwaa alimsikia Ibn Abbas رضي الله عنهما

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا

***“Hebu hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru...”<sup>1</sup>***

Amesema hao ni makafiri wa Makkah. Amepokea Ibn Aby Hatim kutoka kwa Abu Tufaili kwamba Ibn Al-Kawwaa alimuuliza Ali رضي الله عنه kuhusu,

الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ

***“...wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo.”***

Amesema hao ni makafiri wa Kikuraishi siku ya vita vya Badr.<sup>2</sup> Na amesema: hao ni washirikina wa Kikuraishi ili wajia neema ya Allah تعالى ambayo ni imani

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:229.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:6.

wakaibadili neema ya Allah تعالى kwa kuikufuru na wakawatumbukiza watu wao katika nyumba ya maangamizi.<sup>1</sup> Na maana ya aya hii, inajumuisha Makafiri wote, kwani Allah تعالى Amemtuma Muhammad ﷺ hali ya kuwa rehma kwa viumbe wote. Na ni neema kwa watu wote atakayeikubali na akasimama kwa kuishukuru ataingia Peponi, na mwenye kuipinga na akaikufuru ataingia Motoni. Na Kauli Yake:

وَجَعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا لِّيُضِلُّوا عَنْ سَبِيلِهِ<sup>١</sup>

**“Na walimfanyia Mwenyezi Mungu washirika ili wapoteze watu kwenye njia yake.”**

Maana: Wamemshirikisha Allah تعالى na kuwaita watu kwenye hilo kisha Allah تعالى Akasema kwa Kuwatisha na Kuwakemea kupitia ulimi wa Mtume wake ﷺ,

قُلْ تَمَتُّعُوا فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ

**“Sema: Stareheni! Kwani marejeo yenu ni Motoni!”**

Maana lolote mtakaloliweza hapa duniani lifanyeni kwa hiyo lolote litakalokuwa miongoni mwa jambo,

فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ

**“Kwani marejeo yenu ni Motoni!”**

Maana: marejeo yenu na hatima yenu ni Kwetu tu kama Alivyosema Allah تعالى:

تُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ۝١٤

**“Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24) na,**

مَتَّعْ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ۝٧٠

**“Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.” (10:70)**

قُلْ لِعِبَادِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُنْفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً مِّن قَبْلِ أَنْ

يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خِلَالَ ۝١٤

<sup>1</sup> Ibn Hibban 12273.



**31. Waambie waja wangu walioamini, washike Sala, na watoe katika Tulivyowaruzuku, kwa siri na dhaahiri, kabla haijafika Siku isiyokuwa na biashara wala urafiki.**

### Amri ya Kusali na Kutoa Sadaka

Allah تعالی Anasema hali ya Kuwaamrisha waja wake kumtii na kusimama na haki Yake na Kuwatendea wema viumbe Wake kwa kusimamisha Sala, nako ni kumuabudu Allah تعالی hali ya kuwa Peke Yake Hana mshirika, na watoe katika vile ambavyo Allah تعالی Amewaruzuku wao kwa kutekeleza kutoa Zaka pamoja na matumizi juu ya jamaa na Kuwafanyia wema watu kando. Na makusudio ya kuisimamisha Sala, ni kuhifadhi juu ya wakati wake na mipaka yake, rukuu zake, unyenyekevu wake na kusujudu kwake. Na Ameamrisha Allah تعالی Kutoa katika vile Alivyoruzuku kwa njia ya siri na kwa wazi na kwamba wafanye haraka kutekeleza hayo na waziokoe nafsi zao.

مِّن قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ

“...**kabla haijafika Siku...**” nayo ni Siku ya Kiyama.

لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خِلَالَ

“...**isiyokuwa na biashara wala urafiki.**”

Maana yake: Haikubaliwi kwa mtu yeyote fidia kwa kuuzwa nafsi yake kama Alivyosema Allah تعالی:

فَالْيَوْمَ لَا يُؤْخَذُ مِنْكُمْ فِدْيَةٌ وَلَا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا

“**Basi leo haitapokelewa kwenu fidia, wala kwa wale waliokufuru.**”  
(57:15).

Na Kauli Yake:

وَلَا خِلَالَ

“...**wala urafiki.**”

Amesema Ibn Jarir رحمه الله تعالی hakuna huko kufanyiana urafiki. Kwa hiyo mtu akamsamehe rafiki yake ambaye amewajibikiwa na adhabu, kwa sababu ya kwenda kinyume na yeye. Bali huko kuna uadilifu na kufanya haki.<sup>1</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 17:12.

Na Qatada amesema: Kwa hakika Allah تعالى Amejua kwamba duniani kuna kuuziana na urafiki. Watu wanafanyiana urafiki hapa duniani, kwa hiyo anatazama mtu yule ambaye anamfanyia urafiki, na ni juu ya jambo gani anafanya urafiki. Ukiwa urafiki huo ni kwa sababu ya Allah تعالى na audumishe, na ukiwa kwa asiyekuwa Allah na auvunje.<sup>1</sup> Ninasema: makusudiwa ya maneno haya ni kwamba Anaeleza Allah تعالى kuwa hakutamfaa mtu yeyote kuuza wala kutoa fidia. Atapojikomboa kwa dhahabu kwa ujazo wa ardhi, lau angeupata ujazo huo. Na hautamfaa urafiki wa mali yoyote, wala maombezi ya mtu yeyote atakapokutana na Allah تعالى hali ya kuwa ni kafiri. Allah تعالى Amesema:

وَأَنْقُوا يَوْمًا لَا تَجْزِي نَفْسٌ عَنْ نَفْسٍ شَيْئًا وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا تَنْفَعُهَا شَفَعَةٌ وَلَا  
هُمْ يُنصَرُونَ ﴿١٢٣﴾

***“Na iogopeni siku ambayo hatamfaa mtu mwenziwa kwa lolote, wala hakitakubaliwa kwake kikomboleo, wala maombezi hayatamfaa, wala hawatanusuriwa.” (2:123) na,***

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْفِقُوا مِمَّا رَزَقْنَاكُمْ مِّن قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ يَوْمٌ لَا بَيْعَ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا  
شَفَعَةٌ ۗ وَالْكَافِرُونَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٥٤﴾

***“Enyi mlioamini! Toeni katika Tulivyokupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwapo biashara, wala urafiki, wala uombezi. Na makafiri ndio madhaalimu.” (2:254)***

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ  
رِزْقًا لَّكُمْ ۗ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْفَلَكَ لِتَجْرِيَ فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ ۗ وَسَخَّرَ لَكُمُ الْأَنْهَارَ ﴿٢٥٥﴾  
وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَآبِّينَ ۗ وَسَخَّرَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ ﴿٢٥٦﴾ ۗ وَءَاتَاكُمْ مِّن كُلِّ  
مَا سَأَلْتُمُوهُ ۗ وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا ۗ إِنَّ الْإِنسَانَ لَظَلُومٌ كَفَّارٌ ﴿٢٥٧﴾

***32. Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyeziumba Mbingu na Ardhi, na Akateremsha maji kutoka mbinguni. Na kwa hayo Akatoa matunda kuwa ni riziki yenu. Na Akafanya yakutumikieni majahazi yanayo pita baharini kwa Amri Yake, na Akaifanya mito ikutumikieni.***

<sup>1</sup> At-Tabari 17:12.

**33. Na Akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu, na Akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu.**

**34. Na Akakupeni kila mlichomuomba. Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu Hamuezi kuzidhibiti. Hakika mwanaadamu ni dhaalimu mkubwa, mwenye kuzikufuru neema.**

### Ubainifu wa Neema Nyingi za Allah تعالى

Allah تعالى Anazihesabu neema Zake juu ya viumbe Wake, kwa Kuwaambia mbingu zikiwa ni sakafu iliyohifadhiwa, na ardhi ikiwa ni tandiko, na Ameteremsha maji kutoka mawinguni, Akaotesha kutokana na maji hayo namna mbalimbali za mimea kuanzia matunda na mimea yenye kutofautiana rangi, maumbile, ladha, harufu na manufaa yake. Na Ameyadhalilisha majahazi kwa Kuyafanya yanaelea juu ya mawimbi ya maji ya bahari yanapita juu yake kwa Amri ya Allah تعالى. Na Ameidhalilisha bahari kwa kuyabeba majahazi hayo, ili wapate wasafiri kwa hayo majahazi, kutoka jimbo kwenda jimbo jingine, kwa kuyachukua ya huku kuyapeleka kule na vilivyo hapa kuvipeleka pale. Na Ameidhalilisha mito inayojiri katika ardhi kutoka jimbo kwenda jimbo jingine kwa Kuwaruzuku waja miongoni mwa kuinywa na kunyesheliza. Na yasiyokuwa hayo miongoni mwa manufaa mbalimbali.

وَسَخَّرَ لَكُمُ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ دَائِبَيْنِ ط

**“Na Akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu.”**

Vikizunguka usiku na mchana

لَا الشَّمْسُ يَدْبِغِي هَآءَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ ؕ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٤٠﴾

**“Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao.” (36:40) na,**

يُغْشَى اللَّيْلُ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَيْثُهَا وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهٖ ؕ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ؕ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazotumika kwa Amri Yake. Fahamuni! Kuumba**

**na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (7:54)**

Kwa hiyo jua na mwezi vinapishana, na usiku na mchana vinapingana, mara kinachukua hiki kutoka kwa hiki kwa hiyo kinakuwa kirefu na huchukua chengine katika hiki kinakuwa kifupi.

يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ

**“Anauingiza usiku katika mchana, na Anauingiza mchana katika usiku.” (35:13) na,**

وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَمًّى ۗ أَلَا هُوَ الْعَزِيزُ الْغَفَّورُ ﴿٣٩﴾

**“Na Amefanya jua na mwezi vitumike. Kila kimoja wapo kinakwenda kwa kipindi kilichowekewa. Jueni mtanabahi! Yeye Ndiye Mwenye Nguvu, Mwenye Kusamehe!” (39:5)**

Allah تعالى Akasema,

وَأَتَّكُم مِّن كُلِّ مَا سَأَلْتُمُوهُ

**“Na Akakupeni kila mlichomuomba.”**

Anasema Amewaandalieni mahitaji yenu katika hali zenu zote katika vile ambavyo mnamuomba kufuatana na hali zenu. Na Kauli Yake:

وَإِن تَعُدُّوا نِعْمَتَ اللَّهِ لَا تَحْصُوهَا

**“Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamuezi kuzidhibiti.”**

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Kushindwa waja kuzihesabu neema seuze kusimama kwa kuzishukuru. Na imekuja katika sahihi ya Al-Bukhari kwamba Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«اللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ غَيْرَ مَكْفِيٍّ وَلَا مُوَدَّعٍ وَلَا مُسْتَعْنَى عَنْهُ رَبَّنَا»

**“Ee Mola wangu wa haki ni Zako Wewe tu Sifa Njema hali ya kuwa si Mwenye Kutoshewa wala Mwenye Kuachwa na wala hajitoshelezi mtu yeyote na Wewe Bwana Wetu.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 9:493.

Na pamepokelewa katika *Athar*, kwamba Mtume Dawud عليه السلام amesema: 'Ee Bwana vipi nitakushukuru na shukurani zangu Kwako ni neema kutoka Kwako juu yangu?' Allah تعالى Akasema: 'Hivi sasa umenishukuru Ee Daud.' Maana yake: wakati ulipokiri kushindwa kwako kutekeleza kumshukuru Mwenye Kuneemesha."



وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي  
 وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ الْأَصْنَامَ ﴿٣٥﴾ رَبِّ إِنَّهُنَّ أَضْلَلْنَ كَثِيرًا مِّنَ  
 النَّاسِ ۗ فَمَنْ تَبِعَنِ فَإِنَّهُ مِنِّي ۗ وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿٣٦﴾ رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بُوَادٍ غَيْرِ ذِي  
 زَرْعٍ عِندَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ فَاجْعَلْ  
 أَفْعَادَهُمْ مِنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ وَارْزُقْهُمْ مِنَ الثَّمَرَاتِ  
 لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾ رَبَّنَا إِنَّكَ تَعَلَّمُ مَا تُخْفِي وَمَا تُعْلِنُ ۗ  
 وَمَا يَخْفَى عَلَى اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ  
 ﴿٣٨﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ  
 وَإِسْحَاقَ ۗ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٩﴾ رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ  
 الصَّلَاةِ وَمِن ذُرِّيَّتِي ۗ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ ﴿٤٠﴾ رَبَّنَا اغْفِرْ لِي  
 وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ ﴿٤١﴾ وَلَا  
 تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفِيلاً ۗ عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ۗ إِنَّمَا  
 يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ ﴿٤٢﴾ مُهْطِعِينَ  
 مُقْبِعِي رُءُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ ۗ وَأَفْعِدُكُمْ هَوَاءَ ﴿٤٣﴾

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا  
 الْبَلَدَ آمِنًا وَاجْنُبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ  
 الْأَصْنَامَ ﴿٣٥﴾ رَبِّ إِنَّهُنَّ أَضْلَلْنَ  
 كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ ۗ فَمَنْ تَبِعَنِ فَإِنَّهُ  
 مِنِّي ۗ وَمَنْ عَصَانِي فَإِنَّكَ غَفُورٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿٣٦﴾

35. Na Ibrahim aliposema: Ewe Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani, na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu.

36. Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi. Basi aliyenifuata mimi huyo ni wangu, na aliyeniasi, hakika Wewe ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.

**Maombi ya Ibrahim عليه السلام Wakati Alipomuweka Ismail عليه السلام Makkah**

Hapa Allah تعالی Anabainisha Hoja juu ya washirikina wa kiarabu kwamba mji Mtukufu wa Makkah hapo awali kabisa uliwekwa kwa ajili ya kumuabudu Allah تعالی Peke Yake bila ya uwepo ushirikina, na kwamba Ibrahim عليه السلام ambaye mji wa Makkah uliimarika kwa sababu yake, pamoja na watu wanaoishi hapo walijiepusha kuabudu asiyekuwa Allah تعالی, na kwamba aliuomba mji wa Makkah uwe wa amani amesema:

رَبِّ أَجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا

**“Ewe Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani.”** Na kwa hakika Alimuitikia Allah تعالى kwa Kusema:

أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا آمِنًا

**“Je! Hawaoni ya kwamba Tumeifanya nchi takatifu ina amani,...”**  
(29:67) na,

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي لَبَّيْكَ مَبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿٦٧﴾ فِيهِ ءَايَاتٌ بَيِّنَاتٌ مِّمَّا مَقَامُ إِبْرَاهِيمَ ۖ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا ۗ

**“Hakika Nyumba ya kwanza waliowekewa watu kwa ibada ni ile iliyoko Bakka, iliyobarikiwa na yenye uwongofu kwa walimwengu wote. Ndani yake zipo Ishara zilizowazi - masimamio ya Ibrahim, na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani.”** (3:96)

Na Amesema Allah تعالى kuwa Ibrahim عليه السلام aliomba dua ifuatayo,

رَبِّ أَجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا

**“Ewe Mola wangu Mlezi! Ujaalie mji huu uwe wa amani.”** Ameuarifisha –mji hapa kwa sababu aliyafanya maombi ya mji huo baada ya kuijenga Al-Kaabah na kwa sababu hiyo Amesema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ

**“Alhamdulillah! Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq.”** (14:39)

Ni jambo lenye kujulikana kwamba Ismail عليه السلام ni mkubwa kuliko Is’haq عليه السلام kwa miaka kumi na mitatu, ama wakati alipokwenda na Ismail عليه السلام, na mama yake na hali ya kuwa ananyonya – alipokwenda nao – Makkah aliomba vilevile kwa kusema:

رَبِّ أَجْعَلْ هَذَا الْبَلَدَ آمِنًا

**“Ee Mola wangu Mlezi! Ufanye huu uwe mji wa amani...”** (2:126)

Kama tulivyotaja katika Surat- Al-Baqarah kwa urefu na ufafanuzi zaidi. Na Kauli Yake:

وَأَجْنِبْنِي وَبَنِيَّ أَنْ نَعْبُدَ إِلَّا صَنَامَ

**“...na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu.”**

Kunatakikana kwa kila muhubiri kuiombea nafsi yake, wazazi wake na watoto wake. Kisha ametaja kwamba wamefitinika na masanamu viumbe wengi katika watu. Na kwamba yeye amejiepusha na wale wenye kuyaabudu masanamu na amelirudisha jambo lao kwa Allah تعالى. Akitaka Atawadhibu na Akitaka Atawasamehe kama kauli ya Issa عليه السلام،

إِنْ تُعَذِّبِهِمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ<sup>ط</sup> وَإِنْ تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾

**“Ukiwadhibu basi hao ni waja Wako. Na Ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.” (5:118)**

Na hapana katika hilo zaidi ya kulirejesha kwenye matakwa ya Mwenyezi Mungu تعالى siyo kujuzisha kutuka kwa hilo. Imepokewa kutoka kwa Abdillah bin Amri رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ aliisoma kauli ya Nabii Ibrahim عليه السلام،

رَبِّ إِيَّاهُنَّ أَضَلَّلَنَّا كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ<sup>ط</sup>

**“Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi.”**

Na Kauli ya Issa عليه السلام،

إِنْ تُعَذِّبِهِمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ<sup>ط</sup>

**“Ukiwadhibu basi hao ni waja Wako.” (5:118)**

Kisha Akanyanyua mikono yake kisha akasema:

«اللَّهُمَّ أُمَّتِي، اللَّهُمَّ أُمَّتِي، اللَّهُمَّ أُمَّتِي»

**“Ee Mola wangu wa haki, Umati wangu, Ee Mola wangu wa haki Umati wangu, Ee Mola wangu wa haki, Umati wangu.”**

Na akalia, Akasema Allah تعالى: ‘Ee Jibril nenda kwa Muhammad na, Bwana Wako Anajua sana na muulize, ‘ni jambo gani linalokuliza?’ Akamuendea Jibril عليه السلام akamuuliza, akamueleza Mtume ﷺ yale aliyoyasema Akasema Allah تعالى: ‘Nenda kwa Muhammad! muambie kwa hakika Sisi Tutakuridhisha kwa umati wako na hatutakuhuzunisha.’<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Muslim 1:191.



رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ ذُرِّيَّتِي بُوَادٍ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ  
فَأَجْعَلْ أَفْئِدَةً مِنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ وَأَرْزُقْهُمْ مِنْ الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾

**37. Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya wangu katika bonde lisilokuwa na mimea, kwenye Nyumba yako Takatifu, ewe Mola wetu Mlezi, ili washike Sala. Basi zijaalie nyoyo za miongoni mwa watu zielekee kwako, na waruzuku matunda, ili wapate kushukuru.**

Haya yanafahamisha juu ya dua ya pili baada ya ile ya kwanza, pindi alipoenda kumuacha Hajra na mwanaye, na hilo ni kabla ya kujenga nyumba ya Allah تعالی Al-Kaabah<sup>1</sup> – na dua hii ilikuwa baada ya kujengwa kwa kutilia mkazo, na kwa kujipendekeza kwa Allah تعالی na kwa sababu hiyo amesema,

عِنْدَ بَيْتِكَ الْمُحَرَّمِ

**“...kwenye Nyumba yako Takatifu,...”** Na Kauli Yake,

رَبَّنَا لِيُقِيمُوا الصَّلَاةَ

**“...ewe Mola wetu Mlezi, ili washike Sala.”**

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: Maneno hayo yanafungamana na,

الْمُحَرَّمِ

**“Takatifu.”**

Maana yake: Hakika hapana jambo jengine umeifanya yenye kutukuzwa ili waweze watu wake kusimamisha Sala mbele yake,

فَأَجْعَلْ أَفْئِدَةً مِنَ النَّاسِ تَهْوِي إِلَيْهِمْ

**“Basi zijaalie nyoyo za miongoni mwa watu zielekee kwao.”**

Amesema Ibn Abbas na Mujahidi na Sa'id bin Jubair na wengine رضي الله عنهم lau angesema: Nyoyo za watu, wangesongamana juu yake na wafarsi na Warumi na Mayahudi na Manaswara na watu wote.<sup>2</sup> Isipokuwa amesema

<sup>1</sup> Angalia Al-Bukhari na. 3364. ambapo kumedhihirisha kuwa Ibrahim aliisoma dua hii alipowasili Makkah kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kumuacha hapo mkewe na Ismail.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:25-26.

## مِنَ النَّاسِ

"... *za watu...*" wakahusika na hilo Waislamu tu. Na Kauli Yake:

## وَأَرْزُقُهُمْ مِّنَ الثَّمَرَاتِ

"...*na waruzuku matunda.*" Ili wasaidiwe katika kukutii na kwa kuwa hili ni jangwa lisilomea mimea, walettee matunda ili wayale. Allah تعالى Aliijibu dua ya Ibrahim عليه السلام:

أَوْلَمْ نُمَكِّنْ لَهُمْ حَرَمًا ءَامِنًا يُحْيِي إِلَيْهِ ثَمَرَاتُ كُلِّ شَيْءٍ رَّزَقًا مِّن لَّدُنَّا

***"Je! Kwani Sisi hatukuwaweka imara katika pahala patakatifu, penye amani, ambapo huletewa matunda ya kila aina kuwa ni riziki itokayo Kwetu?" (28:57)***

Hayo ni katika Upole Wake Allah تعالى na Ukarimu Wake, Huruma Zake na Baraka Zake, kwamba hapana katika mji wa Makkah mti wenye kuzaa matunda na bali hukusanywa na kupelekwa huko matunda ya miti iliyo pembizoni mwake, kwa kuyaitikia maombi ya mwandani wa Allah تعالى, Ibrahim عليه السلام.

رَبَّنَا إِنَّكَ تَعَلَّمْ مَا نَخْفِي وَمَا نُعَلِّمُ وَمَا نَحْفِي عَلَى اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ  
 ﴿٣٥﴾ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ  
 ﴿٣٦﴾ رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ الصَّلَاةِ وَمِن ذُرِّيَّتِي رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ ﴿٣٧﴾ رَبَّنَا اغْفِرْ لِي  
 وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ ﴿٣٨﴾

**38. Ewe Mola Wetu Mlezi! Hakika Wewe Unajua tunayo yaficha na tunayoyatangaza. Na hapana kitu kinachofichikana kwa Mwenyezi Mungu katika Ardhi wala katika Mbingu.**

**39. Alhamdulillah! Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye Kusikia maombi.**

**40. Mola Wangu Mlezi! Nijaalie niwe mwenye kushika Sala, na katika dhuriya wangu pia. Ewe Mola Wetu Mlezi, na ipokee dua yangu.**

**41. Mola Wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili, na Waumini, siku ya kusimama hisabu.**

Ibn Jariri عليه السلام Amesema: Allah تعالى Anasema Akimuelezea Ibrahim عليه السلام mwandani Wake kwamba yeye amesema:

رَبَّنَا إِنَّكَ تَعَلَّمُ مَا نُخْفِي وَمَا تُعَلِّمُنَا

**“Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe Unajua tunayoyaficha...”**

Maana yake: Wewe unayajua makusudio yangu katika maombi yangu na yale niliyoyataka kwa maombi yangu kwa watu wa mji huu. Hakika hapana jambo jengine ni kukusudia radhi zako na kukutakasia kwao Wewe, Unayajua mambo yote nje yake na ndani yake, hakijifichi juu Yako katika mambo hayo kitu chochote katika ardhi wala mbinguni. Kisha amemsifu Bwana Wake,

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي وَهَبَ لِي عَلَى الْكِبَرِ إِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ إِنَّ رَبِّي لَسَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿١٢٦﴾

**“Alhamdulillah! Himdi zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyenipa juu ya uzee wangu Ismail na Is-haq. Hakika Mola Wangu Mlezi ni Mwenye Kusikia Maombi.”**

Maana: hakika Yeye Humuitikia mwenye kumuomba na kwa hakika Ameniitikia mimi katika lile ambalo nimemuomba mtoto. Kisha amesema:

رَبِّ اجْعَلْنِي مُقِيمَ الصَّلَاةِ

**“Mola wangu Mlezi! Nijaalie niwe mwenye kushika Sala.”** Maana yake: Mwenye kuhifadhi juu yake, mwenye kuisimamisha mipaka yake.

وَمِنْ ذُرِّيَّتِي

**“...na katika dhuriya zangu pia.”** Maana yake: Wafanye wao kama hivyo wenye kudumu juu yake katika kuisimamisha.

رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَاءِ

**“Ewe Mola wetu Mlezi, na ipokee dua yangu.”** Katika yale niliyokuomba katika hayo yote,

رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ

**“Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili.”**

Maombi haya yalikuwa kabla hajatengana na baba yake mzazi wakati ulipomdhihirikia uadui wake kwa Allah تعالى.

وَلِلْمُؤْمِنِينَ

“...na Waumini.” Maana yake: Wote.

يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ

“Siku ya kusimama hisabu.” Maana yake: Siku ambayo utawahesabu waja Wako, matokeo yake Utawalipa kufuatana na matendo yao. Yakiwa ni kheri Utawalipa kheri na yakiwa ni shari basi Utawalipa shari.

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفِيلاً عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ۚ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ  
الْأَبْصَارُ ۚ مُهْطِعِينَ مُقْنِعِي رُءُوسِهِمْ لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ وَأَفْعِدْتُمْ هَوَاءَ ۝

42. Wala usidhani Mwenyezi Mungu Ameghafilika na wanayo yafanya madhaalimu. Hakika Yeye Anawaakhirisha tu mpaka siku yatapokodoka macho yao.

43. Nao wako mbioni, vichwa juu, na macho hayapepesi, na nyoyo zao tupu.

Allah تعالیٰ Kuwapa Muda Makafiri Hakutokani na Kughafilika na Wanayoyafanya

Allah تعالیٰ Anasema : Na usimdhania kabisa Allah تعالیٰ Ee Muhammad ﷺ kuwa ni mwenye kughafilika na matendo ya madhalimu. Maana: Usimdhania pale Anapowapa muda na Akawachelewesha kwamba Yeye Ameghafilika na wao. Amewapuuza Hatawaadhibu juu ya matendo yao, bali Yeye Anayadhibiti hayo na Anayahesabu kwa undani sana.

إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ الْأَبْصَارُ

“Hakika Yeye Anawaakhirisha tu mpaka siku yatapokodoka macho yao.”

Maana yake: Kutokana na ukubwa wa vituko vya siku ya Kiyama. Kisha Ametaja Allah تعالیٰ namna ya kusimama kwao kutoka makaburini na kwenda haraka kwenye uwanja wa mkusanyiko. Amesema,

مُهْطِعِينَ

“Nao wako mbioni.” Maana hali ya kwenda haraka. Kama Allah تعالیٰ Alivyosema:

مُهَطِّعِينَ إِلَى الدَّاعِ ط

“Wanamkimbilia mwitaji,...” (54:8)

يَوْمَئِذٍ يَتَّبِعُونَ الدَّاعِيَ لَا عِوَجَ لَهُ ط

“Siku hiyo watamfuata mwitaji asiye na upotofu.” (20:108) Mpaka,

وَعَنَتِ اللُّجُوهُ لِلْحَيِّ الْقَيُّومِ ط

“Na zitadhalilika nyuso mbele ya Aliye Hai Milele.” (20:111)

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

يَوْمَ تَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا

“Siku watakapotoka makaburini kwa upesi ...” (70:43)

Na Kauli Yake,

مُقْنِعِي رُءُوسِهِمْ

“...vichwa juu,..”

Ibn Abbas na Mujahid na wengine wamesema رضي الله عنهم hali ya kunyanyua vichwa vyao.<sup>1</sup>

لَا يَرْتَدُّ إِلَيْهِمْ طَرْفُهُمْ ط

“...na macho hayapepesi,...” Maana yake: Macho yao ni yenye kuruka, yamekodoka wanadumu kutazama, hawafumbi hata kidogo, kutokana na wingi wa yale ambayo wao wamo katika hayo, miongoni mwa vituko na kufikiri na kuogopa lile litalowashukia. Tunaomba Kuhifadhiwa na Allah تعالى. Kwa sababu hiyo Amesema:

وَأَقْفِدُهُمْ هَوَاءً

“...na nyoyo zao tupu.” Maana yake: Na nyoyo zao zimekuwa tupu hazina kitu ndani kutokana na hofu kubwa. Na kwa sababu hiyo amesema Oatada na wengine wengi: Kwa hakika nyoyo zao zitakuwa tupu kwa sababu nyoyo zitakuwa makooni, zitakuwa zimeondoka katika sehemu zake kutokana na ukubwa wa hofu.<sup>2</sup>

Kisha Allah تعالى Akamuambia Mtume wake ﷺ,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:31-32.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:34.

وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا  
 أَخْرَجْنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ نُبِغِبْ دَعْوَتَكَ وَنَتَّبِعِ الرَّسُولَ ۗ أَوْلَمْ  
 تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِّن قَبْلُ مَا لَكُم مِّن زَوَالٍ ﴿٤٤﴾  
 وَسَكَنتُمْ فِي مَسْكِينَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ وَتَبَيَّنَ  
 لَكُم كَيْفَ فَعَلْنَا بِهِمْ وَضَرَبْنَا لَكُمُ الْأَمْثَالَ ﴿٤٥﴾ وَقَدْ  
 مَكَرُوا مَكَرَهُمْ وَعِندَ اللَّهِ مَكَرُهُمْ وَإِن كَانَ  
 مَكَرُهُمْ لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ ﴿٤٦﴾ فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ مُخْلِفًا  
 وَعْدِيهِ ۗ رُسُلَهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ ذُو انْتِقَامٍ ﴿٤٧﴾ يَوْمَ تُبَدَّلُ  
 الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ ۗ وَبَرَزُوا لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ  
 ﴿٤٨﴾ وَتَرَى الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ مُّقْرَنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٤٩﴾  
 سَرَابِيلُهُمْ مِّن قَطِرَانٍ وَتَغْشَىٰ وُجُوهَهُمُ النَّارُ ﴿٥٠﴾  
 لِيَجْزِيَ اللَّهُ كُلَّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ  
 ﴿٥١﴾ هَذَا بَلَاغٌ لِلنَّاسِ وَلِيُنذِرُوا بِهِ ۗ وَلِيَعْلَمُوا أَنَّمَا هُوَ  
 إِلَهُهُ وَاحِدٌ ۗ وَلِيَذَّكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٥٢﴾

وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ  
 فَيَقُولُ الَّذِينَ ظَلَمُوا رَبَّنَا أَخْرَجْنَا إِلَىٰ  
 أَجَلٍ قَرِيبٍ نُبِغِبْ دَعْوَتَكَ وَنَتَّبِعِ  
 الرَّسُولَ ۗ أَوْلَمْ تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِّن  
 قَبْلُ مَا لَكُم مِّن زَوَالٍ ﴿٤٤﴾  
 وَسَكَنتُمْ فِي مَسْكِينَ الَّذِينَ ظَلَمُوا  
 أَنفُسَهُمْ وَتَبَيَّنَ لَكُم كَيْفَ فَعَلْنَا  
 بِهِمْ وَضَرَبْنَا لَكُمُ الْأَمْثَالَ ﴿٤٥﴾  
 وَقَدْ مَكَرُوا مَكَرَهُمْ وَعِندَ اللَّهِ  
 مَكَرُهُمْ وَإِن كَانَ مَكَرُهُمْ  
 لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ ﴿٤٦﴾

44. Na waonye watu siku itapowajia adhabu, na waliodhulumu waseme: Ewe Mola wetu Mlezi! Tuakhirishie muda kidogo

tuitikie wito wako na tuwafuate Mitume. Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondokewa?

45. Na mkakaa katika maskani zile zile za waliozidhulumu nafsi zao. Na ikakudhihirikieni jinsi Tulivyowatendea. Nasi Tukakupigieni mifano mingi.

46. Na kwa hakika walifanya vitimbi vyao, na vitimbi vyao Anavijua Mwenyezi Mungu. Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima.

## Hapana Kuongezewa Muda Baada ya Ujio wa Adhabu

Allah تعالى Anasema Ameyaelezea maneno ya wale ambao wamezidhulumu nafsi zao wakati watakapoiona adhabu:

رَبَّنَا أَخْرِنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ نُّحِبُّ دَعْوَتَكَ وَنَتَّبِعُ الرَّسُولَ

**“Ewe Mola Wetu Mlezi! Tuakhirishie muda kidogo tuitikie wito wako na tuwafuate Mitume.”**

Kama Alivyosema:

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ ﴿٩٩﴾

**“Mpaka yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola wangu Mlezi! Nirudishe.” (23:99) na,**

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ أَمْوَالُكُمْ

**“Enyi mlioamini! Yasikusahaulisheni mali yenu.” (63:9)**

Na Amesema Allah تعالى: Akibainisha hali ya kukusanywa kwao:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ

**“Na ungelibaona wakosefu wanavyoinamisha vichwa vyao...” (32:12)**

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ وَقَفُوا عَلَىٰ النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتَنَا نُرَدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِآيَاتِ رَبِّنَا

**“Na ungeona watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungelirudishwa, wala hatutakanusha tena Ishara za Mola Wetu Mlezi...” (6:27) na,**

وَهُمْ يَصْطَرِّخُونَ فِيهَا

**“Na humo watapiga makelele...” (35:27)**

Amesema Allah تعالى Akiwajibu katika maneno yao haya:

أَوَلَمْ تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِّن قَبْلُ مَا لَكُمْ مِّن زَوَالٍ ﴿٤٤﴾

**“Kwani nyinyi si mliapa zamani kwamba hamtaondokewa?”**

Maana yake: Hivi hamkuapa huko nyuma kabla kuwa hali yenu ya nyuma isingebadilika, kuwa hakuna ufufuo wala kuhesabiwa? Kwa hiyo ionjeni adhabu hii kutokana na hayo. Mujahid na wengine wamesema,

مَا لَكُمْ مِّن زَوَالٍ

**“...kwamba hamtaondokewa?”**

Maana yake: Kuondoka duniani na kwenda akhera. Allah تعالى Amesema pia,

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ<sup>٣</sup> لَا يَتَّبِعُ اللَّهُ مَن يَمُوتُ<sup>٤</sup>

**“Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa viapo vyao kwamba Mwenyezi Mungu Hatomfufua aliyekufa.” (16:38)**

وَسَكَنتُمْ فِي مَسْكِينَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ وَتَبَيَّنَ لَكُمْ كَيْفَ فَعَلْنَا بِهِمْ وَضَرَبْنَا لَكُمْ<sup>٥</sup> الْأَمْثَالَ ﴿١٦﴾

**“Na mkakaa katika maskani zile zile za waliozidhulumu nafsi zao. Na ikakudhihirikieni jinsi Tulivyowatendea. Nasi Tukakupigieni mifano mingi.”**

Maana yake: Kwa hakika mmeona, na yamewafikia yale Tuliyouwashushia umati uliyokadhibisha kabla yenu na pamoja na hayo hamkupata kutokana na hayo mazingatio yoyote; na hamkupata katika yale ambayo Tumeyatusha kwao makameo yoyote.

حِكْمَةٌ بَلِغَةٌ<sup>٦</sup> فَمَا تُغْنِ الْنُذُرُ ﴿١٧﴾

**“Hikima kaamili; lakini maonyo hayafai kitu!” (54:5)**

Na amepokea Shuuba kutoka kwa Abii Is’haqa, kutoka kwa Abdirrahman bin Daabil kwamba Ali رضي الله عنه amesema katika aya hii,

وَإِن كَانَتْ مَكْرُهُمْ لِيَرْوَلَ مِنْهُ الْجِبَالُ

**“Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:36.



Amesema: Huyu ni yule aliyejadiliana na Ibrahim عليه السلام kuhusu Bwana Wake, alichukua Tai wadogo wawili akawalea mpaka wakawa wanene, na wakawa wakubwa na wakakua akasema: 'Ufungu mguu wa kila mmoja wao katika kigingi kuelekea kwenye sanduku, na waacheni na njaa.' Na akakaa yeye na mtu mwingine katika sanduku. Amesema: akanyanyua katika lile sanduku fimbo ambayo kulikuwa chini yake kuna nyama, wakaruka Tai hao akawa anamuambia mwenzake: 'Tazama unaona nini?' Akasema, 'ninaona hivi na vile, mpaka akasema ninaona dunia yote kana kwamba ni nzi.' Akasema: 'isimamisha fimbo.' Akaisimamisha wakashuka wote amesema hiyo ndiyo Kauli Yake Allah تعالى:

(وَإِنْ كَادَ مَكْرُهُمْ لَيَتْرُونَ مِنْهُ الْجِبَالَ)

"Ingawa vitimbi vyao havikuweza kuondosha milima."<sup>1</sup>

Na kwa hakika vitimbi vinakaribia, kuondosha majabali. Amesema Abuu Is'haqa na aya hii imesomwa kama hivyo katika kisomo cha Abdillah,

وَإِنْ كَانَتْ مَكْرُهُمْ لَيَتْرُونَ مِنْهُ الْجِبَالَ

**"Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima."**

Na amekitaja Mujahid kisa hiki akimuelezea Bukhtunasasar na kwamba yeye alipokuwa hana tena uwezo wa kuona watu na vitu vya ardhini, (pakalinganwa kwa kusemwa) 'Ee muovu mkubwa unakwenda wapi?' Akaogopa kisha akasikia sauti juu yake, akatega mikuki na tai nao wakatega makucha yao, yakafazaika majabali kutokana na kishindo chake, na yakakaribia majabali kuondoka kutokana na hisia ya jambo hilo. Kwa hiyo jambo hilo Ndiyo Kauli Yake:

وَإِنْ كَانَتْ مَكْرُهُمْ لَيَتْرُونَ مِنْهُ الْجِبَالَ

**"Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima."<sup>2</sup>**

Na amenakili Ibn Juray kutoka kwa Mujahid kwamba yeye aliisoma *Litazalu minhul -Jibal* – kwa *fataha za lamu* ya kwanza - *Lataza* - na *dhumma za Lamu* ya pili - *Lu - Minhul - jibal*. Na Amepokea Al Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:39.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:39.

وَإِنْ كَانَتْ مَكْرَهُمْ لِقَوْلٍ مِنْهُ أَلِجَابًا

**“Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima.”**

Anasema hivi: Kuwa vituko vyao haviwezi kuondosha majabali na kama hivyo amesema Al-Hassan Al Basri, na ametoa ufafanuzi Ibnu Jariri رحمه الله تعالى kwamba haya ambayo wameyafanya kuzifanyia nafsi zao, miongoni mwa kumshirikisha kwao Allah تعالى na kumkufuru, hayo hayakuyadhuru chochote majabali na hayakuyageuza. Hakika hapana jambo jengine limerudi balaa la mambo hayo juu yao wenyewe ninasema: Yanafanana haya na Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾

**“Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima.” (17:37)**

Kauli ya pili inayofasiri aya hiyo ni ya Ali bin Abii Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.

وَإِنْ كَانَتْ مَكْرَهُمْ لِقَوْلٍ مِنْهُ أَلِجَابًا

**“Wala vitimbi vyao si vya kuondosha milima.”**

Anasema: Ni ushirikina wao, kama ilivyo Kauli Yake:

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ

**“Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo,” (19:90)<sup>1</sup>**

Kusema kwao Allah تعالى Amefanya mtoto. Na kama hivyo amesema Adh-Dhahak na Qatada.<sup>2</sup>

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ مُخَلَّفَ وَعَدِيدِهِ ۗ رُسُلَهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ﴿٤٧﴾ يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ ۗ وَبَرَزُوا لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿٤٨﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 17:41.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:41.

**47. Basi usimdhania Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye Kuwavunjia Ahadi Yake Mitume wake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushinda, na ni Mwenye Kulipiza.**

**48. Siku itapogeuzwa Ardhi iwe Ardhi nyengine, na Mbingu pia. Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye Nguvu.**

**Allah تعالی Havunji Ahadi**

Allah تعالی Anasema hali ya Kuithibitisha Ahadi Yake na hali ya Kuitilia mkazo:

فَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ مُخَلِّفًا وَعْدِهِ رُسُلَهُ

**“Basi usimdhania Mwenyezi Mungu kuwa ni Mwenye Kuwavunjia ahadi Yake Mitume wake.”**

Maana yake: miongoni mwa kuwanusuru katika maisha ya dunia na siku ambayo watasimama mashahidi. Kisha Allah تعالی Ameelezea kwamba Yeye ni Mwenye Kushinda hakizuiliki Juu Yake kitu chochote ambacho Amekitaka, na ni Mwenye Mateso kwa wale watakaomkufuru na Wakamkanusha.

وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ

**“Ole wao, siku hiyo hao wanaokanusha!” (77:15)**

Na kwa sababu hiyo Amesema:

يَوْمَ تَبْدَلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ

**“Siku itapogeuzwa ardhi iwe ardhi nyengine, na mbingu pia.”**

Maana yake: Makemeo Yake haya yatapatikana katika siku ambayo itabadilishwa ardhi ikawa siyo ardhi hii. Nayo ni ardhi hii lakini itakuwa haina sifa iliyozeleka na yenye kujulikana. Kama ilivyokuja katika Sahihi ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Sahli Bin Saad amesema, Mtume ﷺ amesema,

«يُحْشَرُ النَّاسُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَى أَرْضٍ بَيْضَاءَ عَفْرَاءَ كَقَرْصَةِ النَّيِّ لَيْسَ فِيهَا مَعْلَمٌ لِأَحَدٍ»

**“Watakusanywa watu juu ya ardhi nyeupe, weupe usiyokuwa safi,**

*kama kipande cha kitu kilicho safi, hapana ndani yake alama kwa yeyote.*<sup>1</sup>

Na Imam Ahmad amepoke kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kwamba yeye amesema: Mimi ni wa kwanza wa watu wote ambaye alimuuliza Mjumbe wa Allah تعالى kuhusu aya hii,

يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ<sup>ط</sup>

**“Siku itapogeuzwa ardhi iwe ardhi nyengine, na mbingu pia.”**

Amesema, ‘Nilisema watakuwa wapi watu siku hiyo Ee Mjumbe wa Allah?’ Akanijibu:

«عَلَى الصِّرَاطِ»

*“Watakuwa juu ya Swirati (njia).”*<sup>2</sup>

Imepokewa na Muslim peke yake, kinyume cha Bukhari, Tirmidhy na Ibn Maja. Na amesema Tirmidhy kwamba hadithi hii ina daraja la *Hasan Sahih*.<sup>3</sup>

Na Imam Muslim bin Al-Hajjaji amepokea katika sahihi yake kwamba Thauban mwacha huru wa Mtume ﷺ amesema: ‘Nilikuwa nimesimama mbele ya Mtume ﷺ akamjia mwanachuoni wa Kiyahudi akasema: ‘Amani Iwe juu yako Ee Muhammad.’ Nikamsukuma usukumaji ambao alikaribia kuanguka kutokana nao, akasema, ‘kwani unanisukuma?’ Nikasema, ‘Hivi husemi Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?’ Akasema Myahudi: ‘Hakika hapana jambo jengine tunamuita kwa jina lake ambalo walimuita kwalo watu wake.’ Akasema Mtume ﷺ,

«إِنَّ اسْمِي مُحَمَّدٌ الَّذِي سَمَّيْتَنِي بِهِ أَهْلِي»

*“Hakika Muhammad ni jina langu nililopewa na familia yangu.”*

Myahudi huyo akasema, “Nimekuja kukuuliza jambo.”

<sup>1</sup> *Fat’hul Al-Bari* 11:379, *Muslim* 4:2150.

<sup>2</sup> Ahmad 6:35. *Sirat* kiasili inamaanisha ‘njia’; pia inamaanisha daraja litakalowekwa kukatisha Jahanamu ili watu wapite juu yake Siku ya Kiama. Limeelezwa kuwa ni kali kuliko panga na jembamba kuliko nywele. Litakuwa na ndoano juu yake zitakazonyakua watu.

<sup>3</sup> *Muslim* 4:2150, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:548, *Ibn Hibban* 2:1430.

## «أَتَيْتُكُمْ شَيْئًا إِنْ حَدَّثْتُكُمْ؟»

“Jee kutakufaa jambo lolote iwapo nitakueleza?”

Akasema, ‘nitasikia kwa sikio langu.’ Mtume ﷺ akachimbachimba chini kwa ujiti alikuwa nao, akasema:

«سَلْ»

“Uliza.”

Myahudi akasema, ‘Watu watakuwa wapi siku ambayo itabadilishwa ardhi isiyokuwa ardhi na mbingu?’ Mtume ﷺ akasema:

«هُمْ فِي الظَّلْمَةِ دُونَ النَّجْرِ» قال: فمن أول الناس إجازة؟ فقال: «فَقَرَاءَةُ  
المُهَاجِرِينَ»، فقال اليهودي: فما تحفتهم حين يدخلون الجنة؟ قال: «زِيَادَةُ كَيْدِ  
التُّونِ» قال: فما غذاؤهم في إثرها؟ قال: «يُنْتَحَرُّ لَهُمْ تَوْرُ الأَنْجَبِ الَّذِي كَانَ يَأْكُلُ  
مِنْ أَطْرَافِهَا» قال: فما شرابهم عليه؟ قال: «مِنْ عَيْنٍ فِيهَا تُسَمَّى سَلْسِيلاً». قال:  
صدقت، قال: وجئت أسألك عن شيء لا يعلمه أحد من أهل الأرض إلا نبي أو  
رجل أو رجلان. قال: «أَتَيْتُكُمْ إِنْ حَدَّثْتُكُمْ؟» قال: أسمع بأذني. قال: جئت  
أسألك عن الولد، قال: «مَاءُ الرَّجُلِ أَيْضُ، وَمَاءُ الْمَرْأَةِ أَصْفَرُ، فَإِذَا اجْتَمَعَا فَعَلَا  
مِنْهُ الرَّجُلُ مِثْلُ الْمَرْأَةِ، أَذْكَرًا بِأَذْنِ اللهِ تَعَالَى، وَإِذَا عَلَا مِثْلُ الْمَرْأَةِ مِثْلَ الرَّجُلِ،  
أُنْثَى بِأَذْنِ اللهِ» قال اليهودي: لقد صدقت وإنك لنبي ثم انصرف، فقال رسول  
الله ﷺ: «لَقَدْ سَأَلْتَنِي هَذَا عَنِ الَّذِي سَأَلْتَنِي عَنْهُ، وَمَا لِي عِلْمٌ بِشَيْءٍ مِنْهُ حَتَّى أَتَانِي  
اللهُ بِهِ»

“Wao watakuwa katika kiza nyuma ya daraja.” Akasema, ‘ni watu gani wa kwanza kuvuka?’ Akajibu, “Mafukara na wale waliohama.” Akauliza Yahudi, ‘Nini tunda lao wakati watakapokuwa wanaingia Peponi?’ Akamjibu: “Nyongeza ya ini la chewa.” Akauliza, ‘Nini chakula chao baada yake?’ Akamjibu: “Watachinjiwa ng’ombe dume wa Peponi ambaye alikuwa anakula katika pembezoni mwake.” Akauliza, ‘ni kipi kinywaji chao?’ akamjibu, “Watakunywa katika chemchem iliyo humo inayoitwa Salsabil.” Akasema: ‘Umesema kweli.’ Na akasema: ‘Nimekuja nina kuuliza jambo ambalo hajui mtu yeyote katika watu wa ardhi isipokuwa Nabii au mtu mmoja au

wawili.' Akamuambia: "Kitakufaa iwapo nitakuzungumzia?" Akasema, 'nitasikia kwa sikio langu.' Akasema, 'nimekujia ninakuuliza kuhusu mtoto.' Akasema, "Maji ya mwanamume meupe na maji ya mwanamke ya manjano yatakapokutana, na yakawa manii ya mwanamume kuyakalia juu (yai la) ya mwanamke, huzaliwa mtoto mwanamume, kwa amri ya Allah; na yatapokuwa (yai la) ya mwanamke yakayakalia juu manii ya mwanamume atazaliwa mtoto mwanamke, kwa amri ya Allah." Akasema Yahudi, 'umesema kweli na hakika wewe ni Mtume.' Kisha akaondoka, Mtume ﷺ akasema, "Kwa hakika ameniuliza haya aliyoniuliza hali yakuwa sina mimi ujuzi wa kitu chochote katika hayo mpaka aliponiletea Allah."<sup>1</sup>

Na Kauli Yake,

وَبَرِّوْا لِلّٰهِ

**"Naowatahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu ..."**

Maana yake: Watatoka viumbe wote katika makaburi yao kwenda kwa Allah تعالى.

الْوَّاحِدِ الْقَهَّارِ

**"Mmoja, Mwenye nguvu."**

Maana yake: Aliyetenza Nguvu kila Kitu na Amekishinda na zimenyenyekea Kwake shingo na zimedhalilika Kwake akili za watu.

وَتَرَى الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ مُّقْرَّبِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٤٩﴾ سَرَابِيلُهُمْ مِنْ قَطْرَانٍ وَتَغْشَىٰ

وُجُوهُهُمْ النَّارُ ﴿٥٠﴾ لِيَجْزِيَ اللَّهُ كُلَّ نَفْسٍ مَا كَسَبَتْ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٥١﴾

**49. Na utaona wakhalifu siku hiyo wamefungwa katika minyororo;**

**50 Nguo zao zitakuwa za lami, na Moto utazigubika nyuso zao.**

**51. Ili Mwenyezi Mungu Ailipe kila nafsi kwa yale iliyoyachuma. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.**

<sup>1</sup> Muslim 315.

## Hali za Waovu Siku ya Kiama

Allah تعالى Anasema:

يَوْمَ تُبَدَّلُ الْأَرْضُ غَيْرَ الْأَرْضِ وَالسَّمَوَاتُ<sup>ط</sup>

**“Siku itapogeuzwa ardhi iwe ardhi nyengine, na mbingu pia.”**

Na wakadhihiri viumbe mbele ya Allah تعالى Atakayewapa malipo juu ya matendo yao. Allah تعالى Anasema, ‘Utawaona Ee Muhammad! Siku hiyo watu nao ni wale ambao wamefanya maovu kwa sababu ya ukafiri wao na ufigadi wao.’

مُؤْمِرِينَ

**“...wamefungwa katika minyororo;...”**

Kwa pamoja, kila mmoja pamoja na anayelingana naye au kufanana. Kama Alivyosema Allah تعالى:

أَحْشَرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

**“Wakusanyeni waliodhulumu, na wake zao,...” (37:22)**

وَإِذَا النُّفُوسُ رُوِّجَتْ ﴿٧﴾

**“Na nafsi zikaunganishwa,...” (81:7)**

وَإِذَا أُلْقُوا مِنْهَا مَكَانًا ضَبِيحًا مُقِرِّينَ دَعَوْا هُنَالِكَ ثُبُورًا ﴿١٣﴾

**“Na watakapotupwa humo mahali dhiki, hali wamefungwa, wataomba wafe.” (25:13) na,**

وَالشَّيْطِينَ كُلَّ بَنَّاءٍ وَغَوَّاصٍ ﴿٣٧﴾ وَأَخْرَيْنَ مُقِرِّينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٣٨﴾

**“Na Tukayafanya mashetani yamtumikie, wote wajenzi na wapiga mbizi. Na wengine wafungwao kwa minyororo.” (38:37-38)**

Kisha Allah تعالى Akasema: neno “Al-Asfad” ni pingu, ameyasema hayo Ibn Abbas na Saeed bin Jubair na Al-Aamashi na Abdur-Rahmani bin Zaid رضي الله عنهم na maana hiyo ni mashuhuri katika lugha. Na Kauli Yake:

سَرَابِيلُهُمْ مِّن قَطِرَانٍ

**“Nguo zao zitakuwa za lami,...”**

Maana yake: Nguo zao ambazo watazivaa ni za lami, ni ile ambayo hupakwa kwayo Ngamia. Amesema Qatada: ‘Na hiyo lami ni kitu kinachogandana sana na moto.’ Na alikuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما anasema:

(سَرَابِيلُهُمْ مِّن قَطِرَانٍ)

‘Qatwirani’ hapo ni shaba iliyoyayushwa.<sup>1</sup> Na huenda akiisoma aya hiyo hivi.

Maana yake: Ni za shaba iliyo na moto na umefikia ukomo wa umoto wake. Na kama hivyo imepokewa kutoka kwa Mujahid na Ikrima na Saeed bin Jubair na Al-Hassan na Qatadah.<sup>2</sup> Na Kauli Yake,

وَتَغَشَّىٰ وُجُوهُهُمُ النَّارُ

**“...na Moto utazigubika nyuso zao.”**

Ambayo ni kama Kauli Yake,

تَلَفَحُ وُجُوهُهُمُ النَّارُ وَهُمْ فِيهَا كَالِحُونَ ﴿١٠٤﴾

**“Moto utababua nyuso zao, nao watakuwa na nyuso zilizokunjana.”**  
(23:104).

Na Imam Ahmad رحمه الله تعالى amesema: ametuzungumzia Yahya Bin Ishaqa, ametupa khabari Abbanu bin Zaid kutoka kwa Yahya bin Abu Kathir kutokana na Zaidi kutoka kwa Abu Salama kutokana na Abu Maliki Al-Ashari رضي الله عنهم amesema, Mtume ﷺ amesema,

«أَزْبَعُ فِي أُمَّتِي مِنْ أَمْرِ الْجَاهِلِيَّةِ لَا يَتْرُكُونَهُنَّ: الْفَخْرُ بِالْأَحْسَابِ، وَالطَّعْنُ فِي الْأَنْسَابِ، وَالْأَسْتِسْقَاءُ بِالنُّجُومِ، وَالنِّيَاحَةُ عَلَى الْمَيِّتِ، وَالنَّائِبَةُ إِذَا لَمْ تَكُنْ قَبْلَ مَوْتِهَا، تَقَامُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَعَلَيْهَا سِرْبَالٌ مِنْ قَطِرَانٍ وَدِرْعٌ مِنْ جَرَبٍ»

<sup>1</sup> At-Tabari 17:56.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:55-56.



*“Mambo manne katika umati wangu ni katika mambo ya Jahiliya, umma wangu hawatayaacha: Kujifakharisha na ukoo na kutia dosari katika ukoo, na kuomba mvua kwa nyota, na kuomboleza juu ya maiti. Na mwanamke mwenye kuomboleza, pindi akiwa hakutubia kabla ya kufa kwake atasimamishwa Siku ya Kiyama na hali pana juu yake kanzu ya lami na kanzu ya chuma ya ukurutu.”<sup>1</sup>*

Imethibitishwa na Muslim peke yake.<sup>2</sup>

Na Kauli Yake:

لِيَجْزِيََ اللَّهُ كُلَّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ<sup>٢</sup>

***“Ili Mwenyezi Mungu Ailipe kila nafsi kwa yale iliyo yachuma.”***

Katika Siku ya Kiama. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

لِيَجْزِيََ الَّذِينَ أَسْتَوُوا بِمَا عملُوا

***“...ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda.” (53:31).***

Allah تعالى Amesema hapa.

إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ

***“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhesabu.”***

Maana: Katika hali ya Kumhisabu Kwake mja Wake ni mharaka wa Kutekeleza, kwa sababu Yeye Anajua kila kitu na hakijifichi juu Yake kitu chochote chenye kujificha. Na kwa hakika viumbe Wake wote wakilinganishwa na uwezo Wake ni kama mtu mmoja miongoni mwao. Kama ilivyo Kauli Yake Allah تعالى:

مَّا خَلَقْتُمْ وَلَا بَعَثْتُمْ إِلَّا كَتَفْسٍ وَاحِدَةً<sup>٤</sup>

***“Hakukuwa Kuumbwa Kwenu, wala Kufufuliwa kwenu ila ni Kama Nafsi Moja tu.” (31:28)***

Na haya ndiyo maana ya maneno ya Mujahid,

<sup>1</sup> Ahmad 5:342.

<sup>2</sup> Muslim 2:644.

## سَرِيعُ الْحِسَابِ

“...Mwepesi wa Kuhisabu.” Kudhibiti.

هَذَا بَلَّغٌ لِلنَّاسِ وَلِيُنذَرُوا بِهِ وَيَعْلَمُوا أَنَّمَا هُوَ إِلَهُ وَاحِدٌ وَلِيَذَّكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٥٢﴾

**52. Hili ni Tangazo liwafikie watu, liwaonye, na wapate kujua kuwa hakika Yeye ni Mungu Mmoja, na wapate kukumbuka wenye akili.**

Allah تعالی Anasema hii Qur’ani ni tangazo kwa watu;

لَأُنذِرَكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

“...ili kwayo Nikuonyeni nyinyi na kila inayomfikia.” (6:19)

Maana yake: Qur’ani hii ni tangazo kwa viumbe wote miongoni mwa majini na watu. Kama Alivyosema mwanzoni mwa Sura hii

الرَّ كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ إِلَيْكَ لِتُخْرِجَ النَّاسَ مِنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ

**“Alif Lam Ra. Hiki ni Kitabu Tulichokiteremsha kwako ili uwatoe watu kwenye Giza uwapeleke kwenye Muangaza,...” (14:1)**

وَلِيُنذَرُوا بِهِ

“...liwaonye,...” Maana yake: Waonyeke kwa hiyo Qur’ani

وَلِيَعْلَمُوا أَنَّمَا هُوَ إِلَهُ وَاحِدٌ

“...na wapate kujua kuwa hakika Yeye ni Mungu Mmoja,...” Maana: Wachukue dalili kwa yaliyo ndani yake miongoni mwa hoja mbalimbali na dalili za utii juu ya kwamba hapana anayestahiki kuabudiwa kwa haki asiyekuwa Yeye.

وَلِيَذَّكَّرَ أُولُو الْأَلْبَابِ

“...na wapate kukumbuka wenye akili.”

Maana yake: Wenye akili ya kufahamu.

Mwisho wa Surat Ibrahim عليه السلام na Sifa Njema zinamstahiki Allah تعالی, Bwana wa viumbe wote.



## Tafsiri ya Suratu Hijr Sura ya 15 Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

سُورَةُ الْحَجَرِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّ ۚ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ وَقُرَّانٍ ۝ مُبِينٍ ۝  
 رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ۝  
 ذَرَهُمْ ۝ وَيَتَمَتَّعُوا وَيُلْهِمُ الْأَمَلُ ۝  
 فَسَوْفَ يَعْمَلُونَ ۝

الرَّ ۚ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ وَقُرَّانٍ ۝ مُبِينٍ ۝ رُبَّمَا يَوَدُّ  
 الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ۝ ذَرَهُمْ يَأْكُلُوا  
 وَيَتَمَتَّعُوا وَيُلْهِمُ الْأَمَلُ ۝ فَسَوْفَ يَعْمَلُونَ ۝ وَمَا  
 أَهْلَكْنَا مِنْ قَرْنٍ إِلَّا وَهَذَا كِتَابٌ مَعْلُومٌ ۝ مَا تَسْبِقُ مِنْ أُمَّةٍ  
 أَجَلَهَا وَمَا يَسْتَفْخِرُونَ ۝ وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ  
 الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ ۝ لَوْ مَا تَأْتِينَا بِالْمَلَكِ إِنْ كُنْتَ  
 مِنَ الصَّادِقِينَ ۝ مَا نُزِّلَ الْمَلَكُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَا كَانُوا  
 إِذَا مُنْظَرِينَ ۝ إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ  
 ۝ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِي شَيْعِ الْأَوَّلِينَ ۝ وَمَا  
 يَأْتِيهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ۝ كَذَلِكَ  
 نَسَلُّكَ فِي قُلُوبِ الْمُجْرِمِينَ ۝ لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ ۝ وَقَدْ  
 خَلَتْ سُنَّةُ الْأَوَّلِينَ ۝ وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِنَ السَّمَاءِ  
 فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ۝ لَقَالُوا إِنَّمَا سُكَّرَتْ أَبْصَارُنَا بَلْ  
 نَحْنُ قَوْمٌ مَسْحُورُونَ ۝

الرَّ ۚ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ وَقُرَّانٍ ۝  
 مُبِينٍ ۝ رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا  
 لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ۝ ذَرَهُمْ  
 يَأْكُلُوا وَيَتَمَتَّعُوا وَيُلْهِمُ الْأَمَلُ ۝  
 فَسَوْفَ يَعْمَلُونَ ۝

1. Alif Lam Ra. Hizi ni Aya za Kitabu na Qur'ani inayobainisha.

2. Huenda ikawa walio-kufuru wakatamani wangekuwa Waislamu.

3. Waache wale, na wasta-rehe, na iwazuge tamaa. Watakuja jua.

Wasioamini Huenda Kuna Siku Watatamani Kuwa Waislamu

Yametangulia maneno juu ya herufi zenye kukatwa mwanzoni mwa Sura. Allah تعالى Amesema:

رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Huenda ikawa waliokufuru wakatamani...”**

Huko ni kuwaelezea kwamba wao watajuta juu ya yale ambayo walikuwa juu yake miongoni mwa ukafiri na wakatamani lau wangukuwa duniani ni Waislamu.

Ama kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿١٧﴾

**“Huenda ikawa waliokufuru wakatamani wangukuwa Waislamu.”**

Na amesema Sufyani Atthauri kutoka kwa Salamata bin Kuhail kutoka kwa Abuu Al-Zaarai kutoka kwa Abdillahi, katika Kauli Yake,

رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿١٧﴾

**“Huenda ikawa waliokufuru wakatamani wangukuwa Waislamu.”**

Watayasema hayo watu wa motoni pindi watakapowaona wanatoka motoni. Amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kwamba Ibn Abbas na Anas bin Maliki رضي الله عنهما walikuwa wanaitolea maelezo aya hii.<sup>1</sup> Walikuwa wanaitolea maelezo kwamba siku Atakapowafunga Allah تعالى watu wa makosa katika Waislamu pamoja na washirikina katika moto. Washirikina watawaambia hakikikusaidieni nyinyi ambacho mkikiabudu kule duniani, kwa hiyo Ataghadhibika Allah تعالى kwa kauli yao hii. Kwa Fadhila Yake na Rehma Yake Atawatoa Waislamu wenye makosa hapo wakati huo watakaposema,

رُبَّمَا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ كَانُوا مُسْلِمِينَ ﴿١٧﴾

**“Huenda ikawa waliokufuru wakatamani wangukuwa Waislamu.”<sup>2</sup>**

Na Kauli Yake تعالى:

ذَرَهُمْ يَأْكُلُوا وَيَتَمَتَّعُوا

**“Waache wale, na wastarehe,..”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:62.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:62.

Na Kauli Yake:

قُلْ تَمَتُّعُوا فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَى النَّارِ

**“Sema: Stareheni! Kwani marejeo yenu ni Motoni! ” (14:30)**

كُلُّوا وَتَمَتُّعُوا قَلِيلًا إِنَّكُمْ عُجْرُمُونَ ﴿٤٦﴾

**“Kuleni na mjifurahishe kidogo tu. Hakika nyinyi ni wakosefu!  
(77:46)**

Allah تعالى Anasema,

وَيُلَهُمْ الْآمَلُ

**“...na iwazuge tamaa.”**

Maana yake: Ya kutubia na kurejea.

فَسَوْفَ يَعْمَلُونَ

**“Watakuja jua.”**

Maana yake: Mwisho wa jambo lao.

وَمَا أَهْلَكْنَا مِنْ قَرْيَةٍ إِلَّا وَهِيَ كِتَابٌ مَعْلُومٌ ﴿٤٧﴾ مَا تَسْبِقُ مِنْ أُمَّةٍ أَجَلَهَا وَمَا يَسْتَفْخِرُونَ ﴿٤٨﴾

**4. Na Hatukuuangamiza mji wowote ule ila ulikuwa na muda wake maalumu.**

**5. Hawawezi watu wowote kuitangulia ajali yao, wala kuchelewa.**

### **Kila Mji Una Muda Wake Maalumu**

Allah تعالى Anaeleza: kwamba Yeye Hakuuang'amiza mji wowote isipokuwa baada ya kusimama hoja juu ya mji huo na kukoma.

Haucheleweshi umma wowote ambao umefika muda wake wa kuangamia, hawautangulizi muda wao.

Na huu ni uzinduzi kwa watu wa Makkah na maelekezo kwao, kwenye kuwataka waachilie mbali yale waliyo nayo, miongoni mwa kushirikisha, kupinga na kukengeuka, mambo ambayo wanastahiki kutokana nayo kuangamizwa.

وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ ﴿٦﴾ لَوْ مَا تَأْتِينَا بِالْمَلَكَةِ إِن كُنْتَ  
 مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٧﴾ مَا نُنزِّلُ الْمَلَكَةَ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَا كَانُوا إِذًا مُنظَرِينَ ﴿٨﴾ إِنَّا نَحْنُ  
 نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴿٩﴾

**6. Na walisema: Ewe (Muhammad) uliyeteremshiwa Ukumbusho! Hakika wewe ni mwendawazimu.**

**7. Mbona hutuletei Malaika ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli?**

**8. Sisi Hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya haki, na hapo hawatapewa muhula.**

**9. Hakika Sisi Ndio Tulioteremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi Ndio Tutaoulinda.**

**Kumsingizia Mtume Kwamba ni Mwendawazimu na Kutaka Malaika Wateremke Kwao na Majibu Yao**

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu ukafiri wao na kuvuka kwao mipaka na upingaji wao katika kauli yao,

يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ

**“Ewe uliyeteremshiwa Ukumbusho!”**

Maana yake: Yule ambaye analidai hilo.

إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ

**“Hakika wewe ni mwendawazimu.”**

Maana yake: Katika kutuita kwako sisi kwenye kukufuata na kuyaacha yale ambayo tumewakuta nayo wazazi wetu.

لَوْ مَا تَأْتِينَا بِالْمَلَكَةِ

**“Mbona hutuletei Malaika?”**

Maana yake: washuhudie kwako usahihi wa lile ambalo umekuja nalo ukiwa ni mkweli. Kama alivyosema Firauni,

فَلَوْلَا أُلْقِيَ عَلَيْهِ أَسْوِرَةٌ مِّنْ ذَهَبٍ أَوْ جَاءَ مَعَهُ الْمَلَأِكَةُ مُقْتَرِنِينَ ﴿٤٣﴾

**“Basi mbona hakuvikwa vikuku vya dhahabu, au hawakuja Malaika pamoja naye wakamwandama?” (43:53) na,**

وَقَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْنَا الْمَلَأِكَةُ أَوْ نَرَى رَبَّنَا لَقَدِ اسْتَكْبَرُوا فِي أَنفُسِهِمْ وَعَتَوْا عُتُوًّا كَبِيرًا ﴿٢١﴾ يَوْمَ يَرَوْنَ الْمَلَأِكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُجْرِمِينَ وَيَقُولُونَ حِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٢٢﴾

**“Na walisema wale wasiotaraji kukutana nasi: Mbona sisi hatuteremshiwi Malaika au hatumuoni Mola wetu Mlezi? Kwa yakini hawa wamejiona bora nafsi zao, na wamepanda kichwa vikubwa mno! Siku watakyowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wakosefu. Na watasema: Mungu Apishe mbali!” (25:21-22)**

Kwa hivyo, Allah تعالى Akasema,

مَا نُزِّلُ الْمَلَأِكَةَ إِلَّا بِالْحَقِّ وَمَا كَانُوا إِذًا مُنظَرِينَ ﴿٢١﴾

**“Sisi Hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya Haki, na hapo hawatapewa Muhula.”**

Na amesema Mujahid katika Kauli Yake:

مَا نُزِّلُ الْمَلَأِكَةَ إِلَّا بِالْحَقِّ

**“Sisi Hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya haki...”**

Kwa ujumbe na adhabu.<sup>1</sup> Kisha Akathibitisha Allah تعالى kwamba Yeye Ndiye Aliyemteremshia Qur’ani na Ndiye Atakayehifadhi dhidi ya kugeuzwa na kubadilishwa.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِي شَيْعِ الْأَوَّلِينَ ﴿١٠﴾ وَمَا يَأْتِيهِمْ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿١١﴾ كَذَلِكَ نَسْلُكُهُمْ فِي قُلُوبِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٢﴾ لَا يُؤْمِنُونَ بِهِ ۗ وَقَدْ خَلَتْ سُنَّةُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٣﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 17:68.



**10. Na hakika Tulikwishawatumia Mitume kabla yako mataifa ya mwanzo.**

**11. Na hakuwafikia Mtume ila walimkejeli.**

**12. Na kama hivi ndivyo Tunavyoingiza katika nyoyo za wakosefu.**

**13. Hawayaamini haya, na hali ya kuwa umekwishawapitia mfano wa watu wa kale.**

### Washirikina wa Kila Umma Waliwakejeli Mitume Wao

Allah تعالی Anamliwaza Mtume wake ﷺ kutokana na Alivyokadhibishwa na makafiri wa Kikureishi. Kwamba Yeye Aliwapeleka kabla yake Mitume katika umma uliopita, na kwamba hakuuendea umma wowote Mtume yoyote isipokuwa walimpinga Mtume huyo na kumkejeli. Kisha Akaeleza kwamba Yeye Anatia ukadhibishaji katika nyoyo za waovu wanaopinga na wanaotakabari katika kuufuata uongofu. Amesema Anas na Al-Hasan Al-Basri,

كَذَلِكَ نَسَلُكُمْ فِي قُلُوبِ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٥﴾

**“Na kama hivi ndivyo Tunavyoingiza katika nyoyo za wakosefu.**

Anakusudia shirki.<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

وَقَدْ خَلَّتْ سُنَّةُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٦﴾

**“...na hali ya kuwa umekwishawapitia mfano wa watu wa kale.”**

Maana yake: Kwa hakika yamejulikana Aliyoyafanya Allah تعالی kwa wale waliokadhibisha Mitume wake, miongoni mwa kuhiliki na kuangamia na namna Alivyowaokoa Mitume na wafuasi wao katika dunia na akhera.

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ﴿١٧﴾ لَقَالُوا إِنَّمَا سُكَّرَتْ أَبْصَارُنَا

بَلْ نَحْنُ قَوْمٌ مَّسْحُورُونَ ﴿١٨﴾

**14. Na lau Tungeliwafungulia mlango wa mbingu, wakawa wanapanda,**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:70.

**15. Basi wangelisema: Macho yetu yamelevywa, bali sisi wenyewe tumerogwa.**

### **Makafiri Sugu, Hawatoamini Hata na Miujiiza na Maajabu Watakayoyaiona**

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu nguvu za ukafiri wao na upingaji wao na kutakabari kwao juu ya haki kwamba Yeye lau Angewafungulia mlango mbinguni wakawa wanapanda kupitia mlango huo wasingelisadikisha hilo bali wangesema:

إِنَّمَا سُكِّرَتْ أَبْصَارُنَا

**“Macho yetu yamelevywa,”**

Amesema Mujahidi, Ibn Kathiri na Adh-Dhahak, ‘yamezibwa macho yetu.’<sup>1</sup> Na amesema Qatada kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: Tumbababishwa na hakika hapana jambo lolote tumerogwa.<sup>2</sup>

سُكِّرَتْ أَبْصَارُنَا

**“Macho yetu yamelevywa.”**

Na amesema Ibn Zaid, Mlevi ni yule ambaye haelewi.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 17:74.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:75.

وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَزَيَّنَّاهَا لِلنَّاظِرِينَ ﴿١٦﴾  
 وَحَفِظْنَاهَا مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿١٧﴾ إِلَّا مَنْ أَسْرَقَ  
 السَّمْعَ فَاتَّبَعَهُ شَهَابٌ مُبِينٌ ﴿١٨﴾ وَالْأَرْضَ مَدَدْنَاهَا  
 وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ شَيْءٍ مَوْزُونٍ ﴿١٩﴾  
 وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا مَعْيِشَ وَمَنْ لَسْتُمْ لَهُ بِرَازِقِينَ ﴿٢٠﴾ وَإِنْ  
 مِنْ شَيْءٍ إِلَّا عِنْدَنَا خَزَائِنُهُ وَمَا نُنزِّلُهُ إِلَّا بِقَدَرٍ مَعْلُومٍ  
 ﴿٢١﴾ وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَاحٍ لَنْفَسٍ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً  
 فَاسْقَيْنَاكُمُوهُ وَمَا أَنْتُمْ لَهُ بِخَازِنِينَ ﴿٢٢﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ مُجِبُّوهُ  
 وَنُصِيتُ وَنَحْنُ الْوَارِثُونَ ﴿٢٣﴾ وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَقْدِمِينَ  
 مِنْكُمْ وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَفْخِرِينَ ﴿٢٤﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ  
 يَخْشُرُهُمْ إِنَّهُ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥﴾ وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ  
 صَلْصَلٍ مِنْ حَمَلٍ مَسْنُونٍ ﴿٢٦﴾ وَالْجَانَ خَلَقْنَاهُ مِنْ قَبْلُ  
 مِنْ نَارِ السَّمُومِ ﴿٢٧﴾ وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَأِكَةِ إِنِّي خَلَقْتُ  
 بَشَرًا مِنْ صَلْصَلٍ مِنْ حَمَلٍ مَسْنُونٍ ﴿٢٨﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُ  
 وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ ﴿٢٩﴾ فَسَجَدَ  
 الْمَلَأِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ ﴿٣٠﴾ إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَى أَنْ يَكُونَ  
 مَعَ السَّاجِدِينَ ﴿٣١﴾ قَالَ يَا إِبْلِيسُ مَا لَكَ أَلَّا تَكُونَ  
 مَعَ السَّاجِدِينَ ﴿٣٢﴾ قَالَ لَمْ أَكُنْ لِأَسْجُدَ لِبَشَرٍ خَلَقْتَهُ  
 مِنْ صَلْصَلٍ مِنْ حَمَلٍ مَسْنُونٍ ﴿٣٣﴾

وَلَقَدْ جَعَلْنَا فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا  
 وَزَيَّنَّاهَا لِلنَّاظِرِينَ ﴿١٦﴾ وَحَفِظْنَاهَا  
 مِنْ كُلِّ شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ ﴿١٧﴾ إِلَّا مَنْ  
 أَسْرَقَ السَّمْعَ فَاتَّبَعَهُ شَهَابٌ مُبِينٌ  
 ﴿١٨﴾ وَالْأَرْضَ مَدَدْنَاهَا وَأَلْقَيْنَا فِيهَا  
 رَوَاسِيَ وَأَنْبَتْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ شَيْءٍ  
 مَوْزُونٍ ﴿١٩﴾ وَجَعَلْنَا لَكُمْ فِيهَا  
 مَعْيِشَ وَمَنْ لَسْتُمْ لَهُ بِرَازِقِينَ ﴿٢٠﴾

16. Na hakika Tumeweka katika mbingu vituo vya sayari, na Tumezipamba kwa wenye kuangalia.

17. Na Tumezilinda na kila shetani afukuzwaye.

18. Isipokuwa mwenye kusikiliza kwa kuibia, naye hufuatwa na kijinga cha moto kinachoonekana.

19. Na ardhi Tumeitandaza na humo Tumeweka milima, na Tumeotesha kila kitu kwa kiasi chake.

20. Na Tumekujaalieni humo vitu vya maisha yenu, na ya hao ambao nyinyi sio wenye kuwaruzuku.

## Uwezo wa Allah na Miujiza Yake Mbinguni na Ardhini

Allah تعالى Anataja Kuumba Kwake mbingu kwa kunyanyuka, na yale ambayo ameipamba nayo mbingu kwayo, miongoni mwa nyota zenye kuthibiti, na sayari mbalimbali kwa mwenye kuchunguza. Na akakariri kuchunguza katika yale ambayo anayaona miongoni mwa maajabu na ishara mbali mbali zenye kushangaza mtazamo wake na uchunguzi wake. Kwa sababu hiyo amesema Mujahid na Qatada: neno “*Al Buruuj*” hapa ni sayari.<sup>1</sup> (Ninasema), na haya ni kama Kauli Yake Allah تعالى:

تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا

**“Ametukuka Aliyezijaalia nyota mbinguni,...” (25:61)**

Na amesema Atiyaah Al-Awfi: *Al-Buruuj* hapa ni majumba marefu ya walinzi.<sup>2</sup> Na Amevifanya vimondo kuwa ni walinzi wa hizo mbingu, mashetani ili wasije wakawasikiliza viumbe wa juu. Kwa hiyo, yule ambaye ataasi katika wao kwa ajili ya kuiba usikivu kitamjia Kimondo kilichowazi kitamuangamiza. Na huenda akawa ameyatupa maneno ambayo ameyasikia, kabla ya kupatwa na kimondo hicho, kwa mwenzake ambaye yuko chini yake. Naye huyachukuwa maneno hayo kwa mwingine, anakuja nayo kwa kiongozi wake, kama yalivyobainishwa hayo katika Hadithi Sahihi.

Kama alivyopokea Al-Bukhari katika tafsiri ya aya hii kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه hali ya kuwa anaifikisha Hadithii hiyo kwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا قَضَى اللَّهُ الْأَمْرَ فِي السَّمَاءِ صَرَبَتْ الْمَلَائِكَةُ بِأَجْنِحَتِهَا خُضَعَانًا يَقُولُهُ كَأَنَّهُ سَلِيلَةٌ عَلَى صَفْرَانٍ»

*“Pindi Allah Anapolihukumu jambo huko mbinguni hupiga malaika mbawa zao, hali ya kuwa wanyenyekavu, kwa sababu ya Maneno Yake, kana kwamba ni mnyororo uliyo juu ya jiwe lenye kuteleza.”*

Amesema Ali رضي الله عنه na wengine: Juu ya jiwe Allah تعالى Hupitisha jambo hilo kwa malaika, na pindi zitakapofadhaika nyoyo zao, watasema: ‘Amesema

<sup>1</sup> At-Tabari 17:77.

<sup>2</sup> Al-Baghawi 3:45.

nini Bwana wenu?’ Watasema: ‘Kwa hakika yale ambayo Ameyasema ni kweli na Yeye Ndiye **تعالى** Aliye Mkubwa sana.’ Huyasikia hayo wale wenye kuiba usikivu na huwapa wenzao wengine. Hali inaenda hivyo mmoja baada ya mwingine. Na amesifia Sufyani kwa mkono wake, akatenganisha vidole na akafanya nafasi kati ya vidole vya mkono wake wa kuume, alivisimamisha baadhi yake juu ya vingine, huenda kikampata kimondo mwenye kusikiliza kabla hajamueleza na hakijatupwa kwa mwenzake, hivyo kikamuunguza. Na huenda akafanikiwa kumuhabarisha mwenzake, hali ikawa hivyo hadi habari ikafika chini ya Ardhi. Na huenda alisema Sufyani mpaka yakomelee kwenye ardhi, kutupwa maneno hayo mdomoni mwa mchawi au kuhani. Huongopa pamoja na maneno hayo urongo mia moja na ukweli mchache. Wanasema: ‘Hivi hakutueleza siku kadha na kadha kwamba litakuwa jambo kadha na kadha tukayakuta kuwa ni kweli kutokana na jambo ambalo limesikiwa kutoka mbinguni.’<sup>1</sup> Kisha Ametaja Allah **تعالى** Kuumba Kwake ardhi na Kuitandika Kwake na Kuipanua na Kuikunjua na yale ambayo Ameyafanya ndani ya hiyo ardhi, miongoni mwa majabali yenye kuthibiti majangwa, udongo na michanga. Na Ameotesha humo mimea na matunda yenye kulingana. Na amesema Ibn Abbas **رضي الله عنهما**,

مِنْ كُلِّ شَيْءٍ مَّوْزُونٍ

**“...na Tumeotesha kila kitu kwa kiasi chake.”**

Maana yake: chenye kujulikana. Na kama hivyo amesema Saeed bin Jubair na Ikrima na Abu Malik na Mujahid na Al-Hakam bin Utaibah na Al-Hassan bin Muhammad na Abu Swaleh na Qatada.<sup>2</sup> Na Kauli Yake Allah **تعالى**:

وَجَعَلْنَا لِكُلِّ فِيهَا مَعْيِشَ

**“Na Tumekujaalieni humo vitu vya maisha yenu,”**

Allah **تعالى** Anataja kwamba Yeye Amewatawanya katika ardhi pamoja na sababu za maisha. Na Kauli Yake Allah **تعالى**:

وَمَنْ لَّسْتُمْ لَهُدٍ بَرَّازِقِينَ

**“...na ya hao ambao nyinyi sio wenye kuwaruzuku.”**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:231.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:79-81.

Mujahid amesema ni wanyama kwa ujumla na wale wanaofugwa.<sup>3</sup> Na amesema Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, hao ni watumwa na wajakazi na wanyama wasiofugwa na wenye kufugwa. Na makusudiwa ni kwamba Yeye Allah تَعَالَى Anaonesha Neema Zake juu yao, kwa yale ambayo Ameyarahisisha kwao miongoni mwa sababu za chumo na njia za sababu hizo. Na namna za maisha na kwa vile ambavyo Amevidhalilisha kwao miongoni mwa wanyama ambao wanawapanda na wanyama ambao wanawala na watumwa na wajakazi ambao wanawatumikisha, riziki ya hao wote iko juu ya Muumba wao, haiko juu yao. Wao ni yao manufaa tu na riziki ni juu ya Allah تَعَالَى.<sup>1</sup>

وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا عِنْدَنَا خَزَائِنُهُ وَمَا نُنزِلُهُ إِلَّا بِقَدَرٍ مَعْلُومٍ ﴿٢١﴾ وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَاحٍ  
فَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَسْقَيْنَاكُمُوهُ وَمَا أَنْتُمْ لَهُ بِخَازِنِينَ ﴿٢٢﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ نُحْيِيهِ  
وَنُمِيتُهُ وَنَحْنُ الْوَارِثُونَ ﴿٢٣﴾ وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنْكُمْ وَلَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَخْرِينَ  
﴿٢٤﴾ وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَحْشُرُهُمْ إِنَّهُ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٢٥﴾

**21. Na hakuna chochote ila asili yake inatokana na Sisi; wala Hatukiteremshi ila kwa kipimo maalumu.**

**22. Na Tunazipeleka pepo za kupandishia, na Tunateremsha kutoka mbinguni maji, kisha Tukakunywesheni maji hayo. Wala si nyinyi mnayoyaweka.**

**23. Na Sisi Ndio Tunaohuisha na Tunaofisha. Na Sisi Ndio Warithi.**

**24. Na Tunawajua waliotangulia katika nyinyi, na Tunawajua waliotaakhari.**

**25. Na hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Atakayewakusanya. Hakika Yeye ni Mwenye Hikima na Mjuzi.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:82.

### Mtoaji Pekee wa Kila Kitu ni Allah تعالى

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye ni Mmiliki wa kila kitu na kwamba kila kitu ni chepesi Kwake na ni rahisi Kwake. Na kwamba ni za Kwake hazina za kila kitu katika namna zote,

وَمَا نُزِّلَهُ إِلَّا بِقَدَرٍ مَّعْلُومٍ

**“...wala hatukiteremshi ila kwa kipimo maalumu.”**

Kama Anavyotaka na kama Anavyokusudia, na lile ambalo Ana Yeye katika hayo miongoni mwa hekima kubwa na kuwahurumia waja Wake. Siyo kwa njia ya kupasa bali ni kwamba Yeye Amejiwajibishia juu ya nafsi Yake Kuwahurumia waja Wake. Amesema Yazid bin Abu Ziad kutoka kwa Abuu Juhaifa kutoka kwa Abdillahi رضي الله عنهم haukuwa mwaka una mvua nyingi kuliko mwaka mwingine, isipokuwa Allah تعالى Anaigawa mvua kati yao, kwa namna Anayoitaka, mwaka Ananyesha hapa na mwaka mwingine Ananyesha pale kisha akasoma:

وَأَنَّ مِّن شَيْءٍ إِلَّا عِنْدَنَا خَزَائِنُهُ

**“Na hakuna chochote ila asili yake inatokana na Sisi...”**

Ameyapokea hayo Ibn Jarir رحمه الله تعالى<sup>1</sup>

### Manufaa ya Upepo

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَاقِحَ

**“Na Tunazipeleka pepo za kupandishia.”**

Maana yake: Zinayabeba mawingu, matokeo yake yanatoa maji, na yanateremsha maji juu ya miti. Matokeo yake hufungua majani yake na mafumba yake. Na Amezitaja pepo kwa kutumia tamko la wingi ili kupatikane kutokana na hayo kuzalisha mazao. Tofauti zinapotajwa Pepo kwa tamko la umoja kwa kusema: (Arrihu Al-Aqim) Pepo zisizokuwa na kheri yoyote. Kwani Allah تعالى Amezitaja kwa tamko la umoja na akazisifu kwa Utasa – kutokuwa

<sup>1</sup> At-Tabari 17:82.

na kheri yoyote na huko ni kutotoa mazao kwa sababu kuzalisha hakuwi isipokuwa kutokana na vitu viwili na zaidi. Na imepokewa kutokana na Abdillah bin Masoud رضي الله عنه Katika Kauli Yake:

وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَّاحٍ

***“Na Tunazipeleka pepo za kupandishia.”***

Amesema: Unapelekwa upepo unabeba maji kutoka mbinguni, kisha Huyakamua mawingu mpaka yatoe maji, kama anavyotoa maziwa mwanamke mwenye kunyonyesha.<sup>1</sup> Na kama hivyo amesema Ibn Abbas na Ibrahim Al-Nakha'i na Qatada رضي الله عنهم.<sup>2</sup> Na amesema Adh-Dhahaak, anazipeleka Allah تعالى hizo pepo juu ya mawingu, huyabeba, kwa hiyo yanajaa maji.<sup>3</sup> Na amesema Ubayd bin Umair Al-Laythi, Anapeleka Allah تعالى Pepo zenye kutimua, zinayatimua mawingu, kisha Hupeleka Allah تعالى Pepo zenye kuyakamua mawingu, huyakamua, kisha maji yakaanguka juu ya miti.

Kisha akasoma:

وَأَرْسَلْنَا الرِّيحَ لَوَّاحٍ

***“Na Tunazipeleka pepo za kupandishia.”<sup>4</sup>***

**Maji Matamu ni Neema za Mwenyezi Mungu Mtukufu.**

فَأَسْقَيْنَكُمُوهُ

***“...kisha Tukakunywesheni maji hayo.”***

Maana yake: Tumewateremshieni hali ya kuwa matamu kunawazekana kuyanywa. Lau tunataka tungeyafanya kuwa ya chumvi, kama Alivyotuzindua juu ya hilo katika aya nyingine katika Surat Al-Waqia.

Nayo ni Kauli Yake Allah تعالى:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:84.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:86.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:87-88.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:88.



أَفَرَأَيْتُمُ الْمَاءَ الَّذِي تَشْرَبُونَ ﴿٦٨﴾ ءَأَنْتُمْ أَنْزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ ﴿٦٩﴾ لَوْ  
 دَشَاءُ جَعَلْنَاهُ أُجَاجًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ ﴿٧٠﴾

*“Je! Mnayaona maji mnayoyanywa? Je! Ni nyinyi mnayoyateremsha kutoka mawinguni au ni Sisi Ndio Wenye Kuyateremsha? Tungelipenda Tungeliyafanya ya chumvi. Basi mbona hamshukuru?” (56:68-70)*

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لَكُمْ مِنْهُ شَرَابٌ وَمِنْهُ شَجْرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ ﴿١٠﴾

*“Yeye Ndiye Anayekuteremshieni maji kutoka mbinguni. Katika hayo Nyinyi Mnapata ya Kunywa, na Miti ya kulishia.” (16:10)*

وَمَا أَنْتُمْ لَهُ بِخَازِنِينَ

*“Wala si nyinyi mnayoyaweka.”*

Maana yake: Hamkuwa nyinyi hayo maji mnayahifadhi bali Sisi ndiyo Tunaoyateremsha na Tunayahifadhi juu yenu na Tunayafanya yenye kuonekana. Na lau Angetaka Allah تعالى Angeyazamisha na Akayaondosha, isipokuwa kutokana na Rehma Yake, Ameyateremsha na Ameyafanya kuwa matamu na Ameyahifadhi katika chemuchemu, visima na mito na yasiyokuwa hayo. Amefanya hivyo ili yabakie katika mwaka wote wanakunywa na kunywesha wanyama pamoja na kumwagilia mimea yao na matunda yao.

**Nguvu na Uwezo wa Allah تعالى wa Kuanza Uumbaji na Kuurudia**

وَإِنَّا لَنَحْنُ نُحْيِيهِمْ وَنُمِيتُهُمْ

*“Na Sisi ndio Tunaohuisha na Tunaofisha.”*

Ni maelezo kuhusu Nguvu na Uwezo wa Allah تعالى wa Kuanza Kuumba na Kurejesha umbo kama mwanzo na kwamba Yeye Ndiye Aliyeviumba viumbe ambavyo havikuwepo. Kisha Atawaua watu wote siku ya kukusanywa, na Ameeleza kwamba Allah تعالى Atairithi Ardhi na vilivyo juu yake, na Kwake tu watarudishwa. Kisha Allah تعالى Ameeleza kuhusu Ukamilifu wa Elimu Yake kwao kuanzia wa mwanzo wao hadi wa mwisho wao. Amesema;

وَلَقَدْ عَلَّمْنَا الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنْكُمْ

**“Na Tunawajua waliotangulia katika nyinyi.”**

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema waliotangulia ni kila walioishi tokea Adamu عليه السلام; na waliochelewa, ni walio hai na watakaokuja mpaka siku ya Kiyama.<sup>1</sup>

Na yamepokelewa maneno mfano wake kutoka kwa Ikrima na Mujahid na Adh-dhahaak na Qatada na Muhammad bin Kaab na Al-Shaaby na wengine.<sup>2</sup>

Na amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Muhammad bin Abii Maashar kutoka kwa baba yake kwamba yeye amemsikia Auni bin Abdillah akikumbushana na Muhammad bin Kaab katika Kauli Yake:

وَلَقَدْ عَلَّمْنَا الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنْكُمْ وَلَقَدْ عَلَّمْنَا الْأَسْتَخْرِينَ ﴿١٦﴾

**“Na Tunawajua waliotangulia katika nyinyi, na Tunawajua waliotaakhari.”**

Kwamba aya hiyo inaelezea wakati wanapokuwa watu katika safu za Sala. Muhammad bin Kaab akasema maana siyo hayo.

وَلَقَدْ عَلَّمْنَا الْمُسْتَقْدِمِينَ مِنْكُمْ

**“Na Tunawajua waliotangulia katika nyinyi.”**

Aliyekufa na aliyeuliwa.

الْأَسْتَخْرِينَ

**“...na Tunawajua waliotaakhari.”**

Watakaoumbwa baada ya hapo.

وَإِنَّ رَبَّكَ هُوَ يَحْشُرُهُمْ إِنَّهُ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿١٧﴾

**“Na hakika Mola wako Mlezi Ndiye Atakayewakusanya. Hakika Yeye ni Mwenye Hikima na Mjuzi.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:91.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:90-92.

Akasema Aun Bin Abdillahi: Akuwezeshe Allah تعالى na Akulipe kheri.<sup>1</sup>

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ صَلْصَلٍ مِنْ حَمَلٍ مَسْنُونٍ ﴿١٦﴾ وَالْجَانَّ خَلَقْنَاهُ مِنْ قَبْلُ مِنْ نَارِ  
السَّمُورِ ﴿١٧﴾

**26. Na Tulimuumba mtu kwa udongo unaotoa sauti, unaotokana na matope yaliyotiwa sura.**

**27. Na Majini Tuliwaumba kabla kwa moto wa upepo umoto.**

### Asili Aliyoubiwa Mwanadamu na Jini

Ibn Abbas, Mujahid na Qatadah رضي الله عنهم wamesema, 'Makusudio ya neno Swalswal hapa ni udongo mkavu.'<sup>2</sup> Na lililowazi katika Kauli Yake Allah تعالى:

خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ صَلْصَلٍ كَالْفَخَّارِ ﴿١٤﴾ وَخَلَقَ الْجَانَّ مِنْ مَارِجٍ مِنْ نَارٍ ﴿١٥﴾

**"Amemuumba mtu kwa udongo wa kinamo. Na Akawaumba majini kwa ulimi wa moto." (55:14:15)**

Na imepokewa kutoka kwa Mujahid vilevile

صَلْصَلٍ

**"Unaotoa sauti,"**

Ni udongo uliovunda<sup>3</sup> na kuifasiri aya kwa aya ni bora,

مِنْ حَمَلٍ مَسْنُونٍ

**"...unaotokana na matope yaliyotiwa sura."**

Maana yake: Swalswal ni katika Hamai, nayo ni udongo na Al-Masnun ni uliyo laini. Na Kauli Yake:

وَالْجَانَّ خَلَقْنَاهُ مِنْ قَبْلُ

**"Na majini Tuliwaumba kabla..."** Kabla ya watu.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:90.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:96.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:97.

مِن نَّارِ السَّمُومِ

**“...kwa moto wa upepo umoto.”**

Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما: Ni “Mum” ambayo huu. <sup>1</sup> Na amesema Abu Dawud Al-Twayalisi: Ametuambia Shuuba kuwa Abuu Ishaq amesema: nilimzuru Umar Al-Aswamm juu ya maradhi yake, akasema hivi, ‘nikuambie niliyoyasikia kutoka kwa Abdillahi bin Masoud رضي الله عنهما? Hii “Ssamum” ni sehemu moja kati ya sabiini ya aliyoubwa kwayo jini, kisha akasoma:

وَالْجَانَّ خَلَقْتَهُ مِنْ قَبْلُ مِنْ نَّارِ السَّمُومِ ﴿١٦﴾

**“Na majini Tuliwaumba kabla kwa moto wa upepo umoto.”<sup>2</sup>**

Na kwa hakika imekuja katika hadithi sahihi.

«خُلِقَتِ الْمَلَائِكَةُ مِنْ نُورٍ، وَخُلِفَتِ الْجَانُّ مِنْ مَارِجٍ مِنْ نَارٍ، وَخُلِقَ آدَمُ مِنْ مِمَّا وَصِفَ لَكُمْ»

*“Wameumbwa Malaika kutokana na nuru na wameumbwa majini kutokana na ulimi wa moto na Ameumbwa Adamu kutokana na kile ambacho mumeelezwa.”<sup>3</sup>*

Na makusudio ya aya ni kuzindua juu ya utukufu wa Adamu عليه السلام na uzuri wa asili yake na usafi wa shina lake.

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي خَلِيقٌ بَشَرًا مِّنْ صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ ﴿١٧﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُ  
وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ ﴿١٨﴾ فَسَجَدَ الْمَلَائِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ ﴿١٩﴾  
إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ أَن يَكُونَ مَعَ السَّاجِدِينَ ﴿٢٠﴾ قَالَ يَا آدَمُ اسْكُنْ أَهْلَكَ وَالْجَنَّةَ مَعَ الْوَالِدَيْنِ  
السَّاجِدِينَ ﴿٢١﴾ قَالَ لَمْ أَكُنْ لَأَسْجُدَ لِبَشَرٍ خَلَقْتَهُ مِنْ صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٢﴾

**28. Na Mola wako Mlezi Alipowaambia Malaika: Hakika Mimi Nitamuumba mtu kwa udongo unaotoa sauti, unaotokana na matope yaliyotiwa sura.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:99.

<sup>2</sup> At-Tabari 16:21.

<sup>3</sup> Muslim 4:2294.

**29. Basi Nitakapomkamilisha na Nikampulizia roho Yangu, basi mumuangukie kumsujudia.**

**30. Basi Malaika wote pamoja walimsujudia,**

**31. Isipokuwa Iblisi. Yeye alikataa kuwa pamoja na waliosujudu.**

**32. (Mwenyezi Mungu) Akasema: Ewe Iblisi! Una nini hata hukuwa pamoja na waliosujudu?**

**33. Akasema: Haiwi mimi nimsujudie mtu Uliyemuumba kwa udongo unao toa sauti, unaotokana na matope yenye sura.**

**Kuumbwa kwa Adamu عليه السلام na Kuamrisha kwa Malaika Kumsujudia na Uasi kwa Kukataa kwa Iblisi**

Allah تعالى Anatujulisha kuwa Alimtaja Adam عليه السلام kwa Malaika Wake kabla hajamuumba, na jinsi Alivyompa utukufu kwa Kuwaamuru malaika wamsujudie. Anaeleza namna adui Yake, Iblis akiwa katika kundi la Malaika, alivyokataa kumsujudia kwa sababu ya husuda, ukafiri, ukaidi na kiburi. Ndiyo sababu Iblis alisema,

لَمْ أَكُنْ لَأَسْجُدَ لِبَشَرٍ خَلَقْتَهُ مِنْ صَلْصَلٍ مِنْ حَمَلٍ مَسْنُونٍ

**“Haiwi mimi nimsujudie mtu Uliyemuumba kwa udongo unaotoa sauti.”**

Hayo ni sawa na Kauli Yake Nyingine,

أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ

**“Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, naye Umemuumba kwa udongo.” (7:12) na,**

أَرْءَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْتَ عَلَيَّ

**“Hebu nambie khabari ya huyu Uliyemtukuza juu yangu.” (17:62)**



قَالَ فَأَخْرِجْ مِنْهَا فَإِنَّكَ رَاجِعٌ ﴿٣٤﴾ وَإِنَّ عَلَيْكَ اللَّعْنَةَ  
 إِلَى يَوْمِ الدِّينِ ﴿٣٥﴾ قَالَ رَبِّ فَأَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ  
 ﴿٣٦﴾ قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِينَ ﴿٣٧﴾ إِلَى يَوْمِ الْوَقْتِ  
 الْمَعْلُومِ ﴿٣٨﴾ قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأُزَيِّنَنَّ لَهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ وَلَأُغْوِيَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ  
 الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٠﴾ قَالَ هَذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿٤١﴾  
 إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ إِلَّا مَنْ اتَّبَعَكَ مِنَ  
 الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٣﴾ هَا  
 سَعَةَ أَبْوَابِ لَيْلٍ لِكُلِّ بَابٍ مِنْهُمْ جُزْءٌ مَقْسُومٌ ﴿٤٤﴾ إِنَّ  
 الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٤٥﴾ أَدْخُلُوهَا بِسَلَامٍ ءَامِينَ ﴿٤٦﴾  
 وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِنْ غَلٍّ إِخْوَانًا عَلَى سُرُرٍ  
 مُتَقَابِلِينَ ﴿٤٧﴾ لَا يُمَسُّهُمْ فِيهَا نَصَبٌ وَمَا هُمْ مِنْهَا  
 بِمُخْرَجِينَ ﴿٤٨﴾ \* نِعْمَ عِبَادِي أَنتَ أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ  
 ﴿٤٩﴾ وَأَنَّ عَدْلِي هُوَ الْعَدَابُ الْأَلِيمُ ﴿٥٠﴾

قَالَ فَأَخْرِجْ مِنْهَا فَإِنَّكَ رَاجِعٌ ﴿٣٤﴾  
 وَإِنَّ عَلَيْكَ اللَّعْنَةَ إِلَى يَوْمِ الدِّينِ  
 ﴿٣٥﴾ قَالَ رَبِّ فَأَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ  
 يُبْعَثُونَ ﴿٣٦﴾ قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ  
 الْمُنْظَرِينَ ﴿٣٧﴾ إِلَى يَوْمِ الْوَقْتِ  
 الْمَعْلُومِ ﴿٣٨﴾

**34. (Mwenyezi Mungu)**  
**Akasema: Basi toka humo,**  
**kwani hakika wewe ni**  
**maluuni!**

**35. Na hakika juu yako ipo**  
**laana mpaka Siku ya Malipo.**

**36. Akasema (Iblisi): Mola**  
**wangu Mlezi! Nipe muhula**  
**mpaka siku watapofu-**  
**fuliwa.**

**37. (Mwenyezi Mungu)**  
**Akasema: Hakika wewe ni**  
**katika waliopewa muhula**

**38. Mpaka siku ya wakati maalumu.**

**Iblisi Anaondoshewa Hadhi ya Utukufu, na Anafukuzwa, na Kuahirishiwa Adhabu mpaka Siku ya kياما**

Allah تعالى Anataja kwamba Yeye Alimuamrisha Iblisi amri ya kiulimwengu isiyopingwa na isiyozuilika na kutoka katika daraja ambalo alikuwemo ndani yake katika ulimwengu wa juu. Na kwamba Iblisi amewekwa mbali na Rehma ya Allah تعالى na kwamba Yeye Amempa iblisi laana, ambayo haitaacha kuwa ni yenye kumwandama na kumiminika juu yake mpaka Siku ya Kiyama.

Imepokewa kutoka kwa Saeed bin Jubair kwamba yeye amesema: Wakati Allah تعالى Alipomlaani Iblisi, Iblisi alibadilika sura yake, ikatofautiana na sura ya malaika, na akatoa mlio. Kwa hiyo kila mlio hapa duniani unatokana na mlio huo mpaka Siku ya Kiyama. Ameipokea Ibn Abii Hatima.

قَالَ رَبِّ يَا أُغْوَيْتَنِي لِأُرِيَنَّ لَهُمْ فِي الْأَرْضِ وَلَا أُغْوَيْتَهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٩﴾ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ  
 الْمُخْلِصِينَ ﴿٤٠﴾ قَالَ هَذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿٤١﴾ إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ  
 سُلْطَانٌ إِلَّا مَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿٤٢﴾ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٤٣﴾ هَا سَبْعَةُ  
 أَبْوَابٍ لِكُلِّ بَابٍ مِنْهُمْ جُزْءٌ مَّقْسُومٌ ﴿٤٤﴾

**39. Akasema: Mola wangu Mlezi! Ilivyo kuwa Umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote,**

**40. Ila waja wako waliosafika.**

**41. Akasema: Hii njia ya kujia Kwangu Iliyonyooka.**

**42. Hakika waja Wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao, isipokuwa wale wapotofu Waliokufuata.**

**43. Na bila shaka Jahannamu ndipo pahali pao walipoahidiwa wote.**

**44. Ina milango saba; na kwa kila mlango iko sehemu waliotengewa.**

**Tishio la Ibilisi la Kujigamba Kupoteza Watu na Allah تعالى Anamuahidi Jahannamu**

Allah تعالى Anaeleza Akimuelezea Iblisi na kuasi kwake na kutakabari kwake kwamba yeye alimuambia Bwana:

يَا أُغْوَيْتَنِي

**“Ilivyokuwa Umenitia makosani.”**

Maana yake: Kwa sababu ya kunipoteza.

لَأُرِيَنَّ لَهُمْ

**“...basi nahakikisha nitawazaini...”**Maana yake: Watoto wa Adamu عليه السلام,

فِي الْأَرْضِ

“...duniani...”

Maana: Nitayapendekeza kwao maasia na nitawavutia katika hayo maasi. Nitawasukuma kwenye hayo maasi nitawashawishi kukubwa.

وَلَا غُوبِيَهُمْ أَجْمَعِينَ

“...na nitawapoteza wote,”

Kwa sababu Umenipoteza,

إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلِصِينَ ﴿٦٦﴾

“...Ila waja wako waliosafika.”

Kama ilivyo kauli yake:

قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْت عَلَيَّ لَئِنِ أَخَّرْتَنِي إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَأُحْتَنِكَنَّ بِذُرِّيَّتِهِ

إِلَّا قَلِيلًا ﴿٦٧﴾

“Hebu nambie khabari ya huyu uliyemtukuza juu yangu. Ukiniakhirisha mpaka Siku ya Kiyama, hapana shaka nitawaangamiza dhuriya wake wasipokuwa wachache tu.”(17:62)

قَالَ

“Akasema...” Akimtisha na Akimkemea,

هَذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ

“Hii njia ya kujia Kwangu iliyonyooka.”

Maana yake: Marejeo yenu nyote ni Kwangu Nitawalipeni kufuatana na matendo yenu, yakiwa mema, basi malipo nayo yatakuwa mema; na yakiwa matendo ni shari, basi na malipo nayo yatakuwa shari. Kama Ilivyo Kauli Yake Allah تعالى.

إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ﴿٦٨﴾

“Hakika Mola wako Mlezi Yupo kwenye mavizio Anawavizia.” (89:14)



وَعَلَى اللَّهِ قَصْدُ السَّبِيلِ

**“Na ni juu ya Mwenyezi Mungu Kuelekeza Njia.” (16:9)**

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَنٌ

**“Hakika waja Wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao,”**

Maana yake: Hutakuwa na fursa ya kuwafikia wale niliowakadiria uongofu.

إِلَّا مَنْ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ

**“...isipokuwa wale wapotofu waliokufuata.”**

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema kuwa Yazid bin Qusait amesema: Mitume walikuwa na misikiti nje ya vijiji vyao, na Mtume yeyote alipotaka kumuuliza habari Bwana Wake, alikuwa akienda katika sehemu yake ya kufanyia ibada na kusali kiasi Alichomuandikia Allah تعالى, kisha aliomba jambo lilomdhihirikia. Wakati Mtume fulani akiwa katika Msikiti wake, ghafla alimjia adui wa Allah تعالى Iblisi – mpaka akakaa kati yake na kibla. Na akasema Mtume, ‘Nataka hifadhi kwa Allah تعالى na shetani aliyewekwa mbali na Rehma ya Allah تعالى,’ akasema: ‘Je umemjua unayemuomba hifadhi? Ndio huyu.’ Akasema Mtume: ‘Nataka hifadhi kwa Allah تعالى dhidi ya Shetani aliyewekwa mbali na Rehma ya Allah تعالى.’ Alikariri hayo mara tatu. Akasema adui wa Allah تعالى, ‘utaokolewa na nini dhidi yangu?’ Akasema mara mbili Mtume: ‘Bali wewe niambie kuwa utamshinda mwanadamu kwa lipi?’ Kila mmoja alimsisitiza mwenzake amjibu kwanza. Kisha Akajibu Allah تعالى;

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَنٌ إِلَّا مَنْ اتَّبَعَكَ مِنَ الْغَاوِينَ ﴿١٦﴾

**“Hakika waja Wangu, wewe hutakuwa na mamlaka juu yao, isipokuwa wale wapotofu waliokufuata.”**

Akasema adui wa Allah تعالى, ‘nimesikia haya kabla hujazaliwa.’ Mtume ﷻ akasema, Amesema Allah تعالى:

وَأَمَّا يَتَرَعَّنَكَ مِنَ الشَّيْطَانِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٧﴾

**“Na uchochezi wa Shet’ani ukikuchochea basi omba ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye ni Msikizi, Mjuzi.” (7:200).**

‘Wallahi! Sijakuhisi wewe kabisa isipokuwa nataka hifadhi kwa Allah تعالى dhidi yako.’ Akasema adui wa Allah تعالى: ‘Umesema kweli kwa kufanya hivi utaokoka na mimi.’ Mtume akasema, ‘nielezeni kwa kitu gani mnamshinda mwanadamu?’ Akasema, ‘ninampata wakati wa kughadhibika na wakati wa matamanio.’<sup>1</sup> Na Kauli Yake;

وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمَوْعِدُهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٧﴾

**“Na bila shaka Jahannamu ndipo pahali pao walipoahidiwa wote.”**

Maana yake: Jahanamu ni makazi ya wanaomfuata Iblisi. Allah تعالى Anasema katika Qur’ani,

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنْ آلِ حَرْابٍ فَأَلْتَنَارُ مَوْعِدُهُ<sup>٤</sup>

**“...na anayemkataa katika makundi, basi Moto ndio pahala pa miadi yao” (11:17).**

### Milango ya Jahanam ni Saba

Kisha Allah تعالى Ameeleza kwamba moto wa Jahanam una milango saba,

لِكُلِّ بَابٍ مِنْهُمْ جُزْءٌ مَّقْسُومٌ

**“...na kwa kila mlango iko sehemu waliotengewa.”**

Maana yake: Kwa hakika milango hiyo yote imeandikwa fungu katika wafuasi wa Iblisi, wataliingia fungu hilo hapa wa kukengeuka na fungu hilo. Atunusuru Allah تعالى dhidi ya moto. Na kila mmoja ataingia katika mlango kulingana na matendo yake, na atatulizana katika kidato cha chini kwa kiasi cha matendo yake na mashukio yao yataenda na matendo yao.

Ibn Abuu Hatim رحمه الله تعالى amesimulia kutoka kwa Samurah bin Jundub عنه رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema kuhusu,

«إِنَّ مِنْ أَهْلِ النَّارِ مَنْ تَأْخُذُهُ النَّارُ إِلَى كَعْبِيهِ، وَإِنَّ مِنْهُمْ مَنْ تَأْخُذُهُ النَّارُ إِلَى حُجْرَتِهِ، وَمِنْهُمْ مَنْ تَأْخُذُهُ النَّارُ إِلَى تَرَاقِيهِ»

<sup>1</sup> At-Tabari 17:105.

*"Hakika kwa watu wa Motoni, wapo ambao utawafikia katika fundo mbili za miguu, wengine moto utawafikia kifuani, na wengine moto utawafikia mpaka katika mitulinga."*

Kiwango kitachotegemea amali zao. Hii ni sawa na Aya ifuatayo:

لِكُلِّ بَابٍ مِّنْهُمْ جُزْءٌ مَّقْسُومٌ

**"...na kwa kila mlango iko sehemu waliotengewa."**

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٣٤﴾ أَدْخُلُوهَا بِسَلَامٍ ءَأَمِينٍ ﴿٣٥﴾ وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِّنْ غَلٍّٰ إِخْوَانًا عَلَىٰ سُرُرٍ مُّتَقَابِلِينَ ﴿٣٦﴾ لَا يَمَسُّهُمْ فِيهَا نَصَبٌ وَمَا هُمْ مِنْهَا بِمُخْرَجِينَ ﴿٣٧﴾ \* نَبِيُّ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٣٨﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ ﴿٣٩﴾

**45. Hakika wachamungu watakuwa katika bustani na chemchem.**

**46. (Wataambiwa:) Ingieni kwa salama na amani.**

**47. Na Tutaondoa chuki iliyokuwamo vifuani mwao, wawe ndugu juu ya viti vya enzi wameelekeana.**

**48. Humo hayatawagusa machofu, wala hawatatolewa humo.**

**49. Waambie waja Wangu ya kwamba Mimi Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.**

**50. Na kwamba Adhabu Yangu ndio adhabu iliyochungu!**

### Ubainifu wa Watu wa Peponi na Hali Zao

Alipotaja Allah تعالى hali ya watu wa motoni, Amefuatishia Kueleza hali ya watu wa Peponi, kwamba watakuwa katika bustani na chemchem. Kauli Yake Allah تعالى,

أَدْخُلُوهَا بِسَلَامٍ

**"Ingieni kwa salama."**

Maana yake: Bila ya matatizo yoyote,

ءَامِينَ

“...na amani.”

Maana yake: Bila ya khofu na fazaa yoyote. Hawatahofia kutolewa au kukatika na kumalizika. Na Kauli Yake:

وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِّنْ غَلٍّٰٓٔٓ إِخْوَانًا عَلَىٰ سُرُرٍّٔ مُّتَقَبِلِينَ ﴿٤٧﴾

**“Na Tutaondoa chuki iliyokuwamo vifuani mwao, wawe ndugu juu ya viti vya enzi wameelekeana.”**

Amepokea Al-Qasim kuwa Abuu Umama amesema: Watu wa Peponi wataingia huku vifuani wakiwa na uadui na mifundo ya duniani mpaka watakapokutana. Allah تعالى Ataondosha hayo toka nyoyoni mwao.<sup>1</sup> Kisha Akasoma:

وَنَزَعْنَا مَا فِي صُدُورِهِمْ مِّنْ غَلٍّٰٓٔٓ

**“Na Tutaondoa chuki iliyokuwamo vifuani mwao.”**

Ndivyo ilivyosimuliwa hapa, lakini Al-Qasim bin Abdurrahmani katika riwaya zake kutoka kwa Abuu Umama ni dhaifu. Hata hivyo riwaya hii inakubaliana na iliyo katika Hadithi Sahihi ambapo Qatada anasema, ‘Abu Al-Mutawakil Al-Naji ametuambia kuwa Abu Saeed Al- Khudiry رضي الله عنه aliwaambia kwamba Mtume ﷺ amesema:

«يَخْلَصُ الْمُؤْمِنُونَ مِنَ النَّارِ، فَيُحْبَسُونَ عَلَىٰ فَنطَرَةٍ بَيْنَ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ. فَيَقْتَصِرُ لِبَعْضِهِمْ مِنْ بَعْضِ مَطَالِمٍ كَانَتْ بَيْنَهُمْ فِي الدُّنْيَا حَتَّىٰ إِذَا هُدُّبُوا وَنُقُوا، أُذِنَ لَهُمْ فِي دُخُولِ الْجَنَّةِ»

*“Watatoka waumini motoni watazuiwa katika daraja lililo kati ya Pepo na moto, patachukuliwa kisasi kwa baadhi yao kutokana na baadhi ya mambo ya dhulma yaliyokuwa kati yao huko duniani, mpaka watakapokuwa wamesafishwa na wakatakaswa wataruhusiwa kuingia Peponi.”<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:107.

لَا يَمَسُّهُمْ فِيهَا نَصَبٌ

**“Humo hayatawagusa machofu.”**

Maana yake: taabu na maudhi kama ilivyokuja katika Sahihi ya Bukhari na Muslim.

«أَنَّ اللَّهَ أَمَرَنِي أَنْ أُبَشِّرَ خَدِيجَةَ بِنْتِ أَبِي الْجَنَّةِ مِنْ فَصَبٍ لَا صَحَبَ فِيهِ وَلَا نَصَبٍ»

*“Kwa hakika Allah Ameniamrisha nimpe habari njema Khadija kwa kupata nyumba huko Peponi ya dhahabu, hamna makelele ndani yake na hamna taabu.”<sup>2</sup>*

وَمَا هُمْ مِنْهَا بِمُخْرَجِينَ

**“...wala hawatatolewa humo.”**

Kama ilivyokuja katika hadithi:

«يُقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ! إِنَّ لَكُمْ أَنْ تَصِحُّوا فَلَا تَمْرُضُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تَعِشُوا فَلَا تَمُوتُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تَشَبُّوا فَلَا تَهْرَمُوا أَبَدًا، وَإِنَّ لَكُمْ أَنْ تُقِيمُوا فَلَا تَطْعَمُوا أَبَدًا»

*“Patasemwa, ‘Enyi watu wa Peponi! Mna haki ya kuwa na afya njema, msiugue milele, mna haki ya kuishi, msife milele, mna haki ya kuwa vijana, msizeeke milele, na mna haki ya kuishi Peponi milele bila ya kuondoka.”<sup>3</sup> Na Amesema Allah تعالى,*

خَلْدِينَ فِيهَا لَا يَبْتَغُونَ عَنْهَا حَوْلًا ﴿١٥٠﴾

**“Watadumu humo; hawatataka kuondoka.” (18:108)**

\* نَبِيٌّ عِبَادِي أَنِّي أَنَا الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٥١﴾ وَأَنَّ عَذَابِي هُوَ الْعَذَابُ الْأَلِيمُ ﴿١٥٢﴾

**“Waambie waja Wangu ya kwamba Mimi Ndiye Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu. Na kwamba Adhabu Yangu ndio Adhabu iliyochungu! ”**

<sup>1</sup> Al-Bukhari na. 6535.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 7:166, Muslim 4:1887.

<sup>3</sup> Muslim 4:2182.

Maana: 'Ee Muhammad! Waeleze waja Wangu kwamba Mimi ni Mwenye Huruma na Mwenye Kuadhibu.'

Aya zenye kufanana na hiyo zimeshataja kuwa mara zote tuwe katika hali ya kutumaini (Rehema ya Allah تعالی) au kuhofia (Adhabu ya Allah تعالی).



وَنَبِّئَهُمْ عَن صَيْفِ إِبْرَاهِيمَ ﴿٥١﴾ إِذْ دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا  
 سَلِّمًا قَالَ إِنَّا مِنكُمْ وَجِلُونَ ﴿٥٢﴾ قَالُوا لَا تَوْجَلْ إِنَّا  
 نُبَيِّرُكَ بِغُلْمِ عَلِيمٍ ﴿٥٣﴾ قَالَ أَبَشْرْتُمُونِي عَلَىٰ أَن مَّسِّنِي  
 الْكِبْرَ فِيمَ تُبَشِّرُونَ ﴿٥٤﴾ قَالُوا بِشْرَتِكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُن  
 مِنَ الْقٰٓئِبِطِينَ ﴿٥٥﴾ قَالَ وَمَن يَقْنَطُ مِن رَّحْمَةِ رَبِّهِ  
 إِلَّا الضَّالُّونَ ﴿٥٦﴾ قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ  
 ﴿٥٧﴾ قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٥٨﴾ إِلَّا ءَالَ  
 لُوطٍ إِنَّا لَمُنَجُّوهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٩﴾ إِلَّا أَمْرًا تَهُ قَدَرْنَا  
 إِنَّا لَمِنَ الْغٰٓئِبِينَ ﴿٦٠﴾ فَلَمَّا جَاءَ ءَالَ لُوطٍ الْمُرْسَلُونَ  
 ﴿٦١﴾ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ مُّسْكِرُونَ ﴿٦٢﴾ قَالُوا بَلْ جِئْنَاكَ  
 بِمَا كَانُوا فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٦٣﴾ وَأَتَيْنَاكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّا  
 لَصٰٓدِقُونَ ﴿٦٤﴾ فَأَسْرِ بِأَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ اللَّيْلِ وَاتَّبِعْ  
 أَدْبَارَهُمْ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنكُمْ أَحَدٌ وَامْضُ حَيْثُ تُؤْمَرُونَ  
 ﴿٦٥﴾ وَقَضَيْنَا إِلَيْهِ ذَٰلِكَ الْأَمْرَ أَنَّ دَابِرَ هٰٓؤُلَاءِ مَقْطُوعٌ  
 مُّصْبِحِينَ ﴿٦٦﴾ وَجَاءَ أَهْلَ الْمَدِينَةِ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٦٧﴾ قَالَ  
 إِنَّ هٰٓؤُلَاءِ صٰٓئِفِي فَلَا تَفْضَحُونِ ﴿٦٨﴾ وَاتَّقُوا اللَّهَ وَلَا  
 تُخۡزَوۡنَ ﴿٦٩﴾ قَالُوا أَوَلَمْ نُنهَك عَنِ الْعٰلَمِينَ ﴿٧٠﴾ قَالَ  
 هٰٓؤُلَاءِ بَنَاتِي إِن كُنتُمْ فٰٓئِلِينَ ﴿٧١﴾ لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي  
 سَكْرَتِهِمۡ يَعۡمَهُونَ ﴿٧٢﴾

وَنَبِّئَهُمْ عَن صَيْفِ إِبْرَاهِيمَ ﴿٥١﴾ إِذْ  
 دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا سَلِّمًا قَالَ إِنَّا  
 مِنكُمْ وَجِلُونَ ﴿٥٢﴾ قَالُوا لَا تَوْجَلْ  
 إِنَّا نُبَيِّرُكَ بِغُلْمِ عَلِيمٍ ﴿٥٣﴾ قَالَ  
 أَبَشْرْتُمُونِي عَلَىٰ أَن مَّسِّنِي الْكِبْرَ  
 فِيمَ تُبَشِّرُونَ ﴿٥٤﴾ قَالُوا بِشْرَتِكَ  
 بِالْحَقِّ فَلَا تَكُن مِنَ الْقٰٓئِبِطِينَ  
 ﴿٥٥﴾ قَالَ وَمَن يَقْنَطُ مِن رَّحْمَةِ  
 رَبِّهِ إِلَّا الضَّالُّونَ ﴿٥٦﴾

51. Na uwape khabari za wageni wa Ibrahim.

52. Walipoingia kwake na wakasema: Salama! Yeye akasema: Hakika sisi tunakuogopeni.

53. Wakasema: Usiogope. Sisi tunakubashiria kijana mwenye ujuzi.

54. Akasema: Mnani-bashiria nami uzee umeni-shika! Basi kwa njia gani mnanibashiria?

55. Wakasema: Tunakubashiria kwa haki; basi usiwe miongoni mwa wanaokata tamaa.

56. Akasema: Na nani anayekata tamaa na rehema ya Mola wake Mlezi ila wale waliopotea?

**Wageni wa Ibrahim عليه السلام na Kumbashiria Kupata Mtoto**

Allah تعالى Anasema: Na waeleze Ee Muhammad, kuhusu kisa cha,

ضَيْفٍ إِبْرَاهِيمَ

*“...wageni wa Ibrahim.”*

Neno “Dhayf” hutumiwa kwa mgeni mmoja na wengi. Ameeleza,

دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا سَلَمًا قَالَ إِنَّا مِنْكُمْ وَجِلُونَ

***“Walipoingia kwake na wakasema: Salama! Yeye akasema: Hakika sisi tunakuogopeni.”***

Maana yake: Ni wenye kuogopa na ametaja sababu ya kuogopa kwake wakati alipoona kuwa mikono yao haifikii kwenye chakula alichowakaribisha. Naye ni ndama aliyenona.

قَالُوا لَا تَوْجَلْ

***“Wakasema: Usiogope.”*** Maana yake: Usihofu.

وَدَشَرُوهُ بِغُلْمٍ عَلَيْهِ

***“Na Wakambashiria kijana mwenye ujuzi.”***

Maana yake: Is’haqa عليه السلام kama ilivyotangulia katika Surat Hud عليه السلام. Kisha,

قَالَ

***“Akasema...”***

Hali ya kustaajabu kutokana na utu uzima wake na utu uzima wa mke wake hali ya kuithibitisha ahadi:

أَدْبَرْتُ مَوْنِي عَلَىٰ أَنْ مَسَّنِيَ الْكِبَرُ فَبِمَ تَبْشُرُونَ

***“Mnanibashiria nami uzee umenishika! Basi kwa njia gani mnanibashiria?”***

Walimjibu kwa kusisitiza walilombashiria. Walileta na bishara baada ya bishara.



قَالُوا بِشَرِّنَكَ بِالْحَقِّ فَلَا تَكُن مِّنَ الْقَانِطِينَ ﴿٥٦﴾

**“Wakasema: Tunakubashiria kwa haki; basi usiwe miongoni mwa wanaokata tamaa.”**

قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٥٧﴾ قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٥٨﴾ إِلَّا ءَالَ لُوطٍ إِنَّا لَمُنَجُّوهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٩﴾ إِلَّا أَمْرًا تَدْرَأُوهُ إِنَّا لَمِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٦٠﴾

**57. Akasema: Hebu nini amri yenu, enyi wajumbe?**

**58. Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa kaumu ya wakosefu!**

**59. Isipo kuwa waliomfuata Luut'i. Bila ya shaka sisi tutawaokoa hao wote.**

**60. Ila mkewe. Tunakadiria<sup>1</sup> huyo atakuwa miongoni wataobakia nyuma.**

### Sababu ya Kuja kwa Malaika

Allah تعالی Anaeleza hali ya Kumuelezea Ibrahim عليه السلام wakati ilipomuondokea khofu na ikamjia habari njema kwamba yeye alianza kuwauliza kuhusu sababu ya kuja kwao, wakasema,

إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ

**“Hakika sisi Tumetumwa kwa kaumu ya wakosefu!”**

Wanawakusudia watu wa Mtume Lut عليه السلام na wakawaeleza kwamba wao watawaokoa watu wa Lut عليه السلام, isipokuwa mke wake kwani yeye ni miongoni mwa watakaoangamia. Na kwa sababu hiyo wamesema:

إِلَّا أَمْرًا تَدْرَأُوهُ إِنَّا لَمِنَ الْغَابِرِينَ ﴿٦٠﴾

**“Ila mkewe. Tunakadiria huyo atakuwa miongoni wataobakia nyuma.”**

<sup>1</sup> Neno “Qaddama” linamaanisha, “tumeazimia” linafasiriwa na wasomi wa Tafsiri kama lilivyotafsiriwa. Wanasema kuwa malaika huzungumza kwa namna hiyo kwa sababu ya ukaribu wao kwa Allah تعالی, daraja ambalo viumbe wengine hawajabahatika kulifikia. Angalia Tafsiri ya At-Tabari.

Maana yake: Watakaobaki wenye kuangamizwa.

فَلَمَّا جَاءَ آلَ لُوطٍ الْمُرْسَلُونَ ﴿٦١﴾ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ مُنْكَرُونَ ﴿٦٢﴾ قَالُوا بَلْ جَعَلْنَاكَ  
بِمَا كَانُوا فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٦٣﴾ وَأَتَيْنَاكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٦٤﴾

**61. Basi wale wajumbe walipofika kwa Luut'i,**

**62. Alisema (Luut'i): Hakika nyinyi ni watu msiojulikana.**

**63. Wakasema: Bali sisi tumekuletea yale waliyokuwa wakiyafanyia shaka.**

**64. Na tumefika kwako kwa Haki, na hakika sisi tunasema kweli.**

**Ujio wa Malaika kwa Lut عليه السلام**

Allah تعالى Anasema Akimuelezea Lut عليه السلام wakati walipomuendea malaika. Katika sura ya vijana wazuri wa sura. Wakaingia nyumbani kwake, akasema,

إِنَّكُمْ قَوْمٌ مُنْكَرُونَ ﴿٦١﴾ قَالُوا بَلْ جَعَلْنَاكَ بِمَا كَانُوا فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٦٢﴾

**“Hakika nyinyi ni watu msiojulikana. Wakasema: Bali sisi tumekuletea yale waliyokuwa wakiyafanyia shaka.”**

Wanakusudia adhabu yao na kuangamia kwao, ambako walikuwa wanatilia shaka katika kutuka kwake, kuwatukia wao na kushuka mahala pao.

وَأَتَيْنَاكَ بِالْحَقِّ

**“Na tumefika kwako kwa Haki,..”**

Kama Ilivyo Kauli Yake Allah تعالى:

مَا نُنزِلُ الْمَلٰٓئِكَةَ اِلَّا بِالْحَقِّ

**“Sisi Hatuwateremshi Malaika ila kwa sababu ya haki,..” (15:8) na,**

وَإِنَّا لَصَادِقُونَ

**“...na hakika sisi tunasema kweli.”**

Maneno haya ni kutilia mkazo habari yao kwake, kwa lile ambalo walimueleza kwalo miongoni mwa kuokoka kwake na kuangamizwa kwa watu wake.

فَأَسِرْ بِأَهْلِكَ بِقِطْعٍ مِّنَ اللَّيْلِ وَاتَّبِعْ أَدْبَارَهُمْ وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ أَحَدٌ وَامْضُوا  
حَيْثُ تُؤْمَرُونَ ﴿٦٥﴾ وَقَضَيْنَا إِلَيْهِ ذَلِكَ الْأَمْرَ أَنَّ دَابِرَ هَتُولَاءِ مَقْطُوعٌ مُّصْبِحِينَ ﴿٦٦﴾

**65. Basi ondoka na ahli zako usiku ungalipo, nawe ufuata nyuma yao, wala yeyote kati yenu asigeuke nyuma. Na mwende mnapoamrisha.**

**66. Na Tukamfunulia hukumu hiyo, ya kwamba hata wa mwisho wao hao ikifika asubuhi atakuwa keshakatiliwa mbali.**

### Kuamrisha Lut عليه السلام Kutoka Pamoja na Familia Yake Usiku

Anataja Allah تعالى kuhusu malaika kwamba walimuamrisha Lut عليه السلام aende na watu wake wa nyumbani kwake, baada ya kupita sehemu za usiku, na kuwa Lut عليه السلام awe nyuma yao ili awe ni mwenye kuwahifadhi zaidi. Na pia Mtume ﷺ alipokwenda vitani alikuwa anakwenda nyuma kwa madhumuni ya kumhimiza mnyonge na kumchukua aliye katika wao. Na Kauli Yake:

وَلَا يَلْتَفِتْ مِنْكُمْ أَحَدٌ

**“...wala yeyote kati yenu asigeuke nyuma.”**

Maana yake: Mtakapousikia ukelele kwa wale watu msigeuke na waacheni katika lile ambalo limewashuka miongoni mwa adhabu na mateso.

وَامْضُوا حَيْثُ تُؤْمَرُونَ

**“Na mwende mnapoamrisha.”**

Kana kwamba walikuwa na anayewaongoza katika njia.

وَقَضَيْنَا إِلَيْهِ ذَلِكَ الْأَمْرَ

**“Na Tukamfunulia hukumu hiyo.”**

Maana yake: Tayari Tulishampelekea jambo hilo.

أَنْ دَابِرَ هَتُولَاءِ مَقْطُوعٍ مُّصْبِحِينَ

**“...ya kwamba hata wa mwisho wao hao ikifika asubuhi atakuwa kesho katiliwa mbali.”**

Maana yake: Wakati wa asubuhi. Kama Kauli Yake katika aya nyingine,

إِنَّ مَوْعِدَهُمُ الصُّبْحُ أَأَيْسَ الصُّبْحِ بِقَرِيبٍ ﴿٦٨﴾

**“Hakika miadi yao ni asubuhi. Je, asubuhi si karibu?” (11:81)**

وَجَاءَ أَهْلَ الْمَدِينَةِ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٦٧﴾ قَالَ إِنَّ هَتُولَاءِ صِيفِي فَلَا تَفْضَحُونَ ﴿٦٨﴾ وَأَنْتَقُوا  
 اللَّهُ وَلَا تَخْزُونَ ﴿٦٩﴾ قَالُوا أَوْلَمْ نَنْهَكَ عَنِ الْعَلَمِينَ ﴿٧٠﴾ قَالَ هَتُولَاءِ بَنَاتِي إِنْ كُنْتُمْ  
 فَعَلِينَ ﴿٧١﴾ لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٢﴾

**67. Na wakaja watu wa mji ule nao furahani.**

**68. Akasema: Hakika hawa wageni wangu, basi msinifedheheshe.**

**69. Na mcheni Mwenyezi Mungu, wala msinihizi.**

**70. Wakasema: Sisi hatukukukataza usimkaribishe yeyote?**

**71. Akasema: Hawa binti zangu, ikiwa nyinyi ni watendaji.**

**72. Naapa kwa umri wako! Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakihangaika ovyo.**

**Wakazi wa Mji Wanawaendea Malaika Wakidhania ni Wanaume**

Allah تعالیٰ Anaeleza kuhusu ujio wa watu wa Lut عليه السلام, pindi walipojua habari ya wageni wake na kung'ara kwa sura zao. Na kwamba ujio uliwafurahisha na kushangilia.

قَالَ إِنَّ هَتُولَاءِ صِيفِي فَلَا تَفْضَحُونَ ﴿٦٨﴾ وَأَنْتَقُوا اللَّهَ وَلَا تَخْزُونَ ﴿٦٩﴾

**“Akasema: Hakika hawa wageni wangu, basi msinifedheheshe. Na mcheni Mwenyezi Mungu, wala msinihizi.”**

Hayo ndiyo aliyowaambia Lut عليه السلام kabla hajajua kwamba walikuwa

Wajumbe wa Allah تعالى kama alivyosema katika Surat Hud, ama hapa tumeshaambiwa kuwa ni wajumbe wa Allah تعالى, na kufuatia kuja kwa watu wa Lut عليه السلام na kuhojiana nao. Hata hivyo, kiunganishi (wa, yaani na) hakiashirii mtiririko wa matukio, hususani kwa kuwa kuna jambo la kuashiria kuwa haikuwa hivyo. Wakamjibu:

أَوَلَمْ تَنْهَكَ عَنِ الْعَالَمِينَ

**“Sisi hatukukukataza usimkaribishe yeyote?”**

Akawaelekeza kuelekea kwa wake zao, na kile ambacho Amewaambia wao Allah تعالى kwa hao wake, miongoni mwa tupu zilizoruhusiwa. Jambo hili lilishaelezwa na hakuna haja ya kulikariri hapa.<sup>1</sup> Haya yote na hali ya kuwa wao wameghafilika na lile linalotakiwa kwao, na lile ambalo limewazunguka miongoni mwa balaa, na lipi litakalowapata miongoni mwa adhabu yenye kutulizana. Na kwa sababu hiyo Allah تعالى Alimuambia Muhammad ﷺ,

لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٦﴾

**“Naapa kwa umri wako! Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakihangaika ovyo.”**

Allah تعالى Ameapa kwa uhai wa Mtume wake Rehma za Allah na Amani yake ziwe juu yake na katika hili pana kumtukuzwa kukubwa na daraja ya juu na cheo kikubwa sana. Amesema Amri bin Maliki Al-Nakri kutoka kwa Abii Al-Jawazai kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwamba yeye amesema: Hakuumba Allah تعالى nafsi iliyotukufu sana kwake kuliko Muhammad ﷺ na sikumsikia Allah تعالى Ameuapia uhai wa mtu yeyote asiyekuwa yeye.

Allah تعالى Amesema:

لَعَمْرُكَ إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿٧٦﴾

**“Naapa umri wako! Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakihangaika ovyo.”**

Anasema: Ninaapa kwa uhai wake na umri wako na kubaki kwako duniani:

<sup>1</sup> Angalia Tafsiri ya Surat Hud.

إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ

***“Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakhangaika ovyo.”***<sup>1</sup>

Ameyapokea hayo Ibn Jarir رحمه الله تعالى na amesema Qatada.

لَفِي سَكْرَتِهِمْ

***“Hakika hao walikuwa katika ulevi wao.”***

Maana yake: Katika upotevu wao.

يَعْمَهُونَ

***“...wakhangaika ovyo.”***

Maana yake: Wanacheza.<sup>2</sup>

Na amesema Ali bin Abii Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما:

لَعَمْرُكَ

***“Naapa kwa umri wako!”***

Naapa kwa maisha yako.

إِنَّهُمْ لَفِي سَكْرَتِهِمْ يَعْمَهُونَ

***“Hakika hao walikuwa katika ulevi wao, wakhangaika ovyo.”***

Amesema wanababaika.<sup>3</sup>

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:118.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:118.

<sup>3</sup> Sawa na hayo yameandikwa na At-Tabari.

فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ مُشْرِقِينَ ﴿٧٣﴾ فَجَعَلْنَا عَلَيَّهَا سَافِلَهَا  
 وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ ﴿٧٤﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ  
 لَآيَاتٍ لِّمُتَوَشِّئِينَ ﴿٧٥﴾ وَإِنَّا لَبِيسِيلٍ مُّقِيمٍ ﴿٧٦﴾ إِنَّ فِي  
 ذَلِكَ لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٧﴾ وَإِن كَانَ أَصْحَابُ الْأَيْكَةِ  
 لَطَّالِمِينَ ﴿٧٨﴾ فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ وَإِنَّا لَبِإِمَامٍ مُّبِينٍ ﴿٧٩﴾  
 وَلَقَدْ كَذَّبَ أَصْحَابُ الْحِجْرِ الْمُرْسِلِينَ ﴿٨٠﴾ وَعَآتَيْنَهُمْ  
 ءآيَاتِنَا فَكَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٨١﴾ وَكَانُوا يَنْحِتُونَ مِّن  
 الْجِبَالِ بُيُوتًا ءَامِينِينَ ﴿٨٢﴾ فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ مُضْحِكِينَ  
 ﴿٨٣﴾ فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٤﴾ وَمَا خَلَقْنَا  
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَإِنَّ السَّاعَةَ  
 لَآتِيَةٌ ۖ فَاصْفَحِ الصَّفْحَ الْجَمِيلَ ﴿٨٥﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ  
 الَّذِي خَلَقَ الْعَلِيمَ ﴿٨٦﴾

فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ مُشْرِقِينَ ﴿٧٣﴾  
 فَجَعَلْنَا عَلَيَّهَا سَافِلَهَا وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ  
 حِجَارَةً مِّن سِجِّيلٍ ﴿٧٤﴾ إِنَّ فِي  
 ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّمُتَوَشِّئِينَ ﴿٧٥﴾ وَإِنَّا  
 لَبِيسِيلٍ مُّقِيمٍ ﴿٧٦﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ  
 لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٧﴾

73. Ukelele ukawatwaa wakipambaukiwa.

74. Na Tukaigeuza nchi juu chini, na Tukawanyeshea mvua ya mawe ya udongo wa Motoni.

75. Hakika katika hayo zipo ishara kwa wachunguzi.

76. Na miji hii ipo kwenye njia inayopitiwa.

77. Hakika katika hayo ipo ishara kwa Waumini.

Kuangamizwa kwa Watu wa Lut عليه السلام

Allah تعالى Anasema:

فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ

“Ukelele ukawatwaa...”

Ni sauti kali iliyowajia wakati wa kuchomoza jua, ikiwa ni pamoja na kuipindua miji yao, juu chini, na kuwapelekea mawe ya udongo mkavu juu yao, na maelezo kuhusu neno – *Sijjin* – katika Surat Hud yanatosha.

Na Kauli Yake:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّمَتَّوِّبِينَ ﴿٧٥﴾

**“Hakika katika hayo zipo ishara kwa wachunguzi.”**

Maana yake: Hakika athari za haya mateso yaliyo wazi juu ya miji hiyo ni kwa mwenye kulichunguza hilo na akalitazama kwa jicho lake la dhahiri au uoni wake kiakili na wa kiroho.

Kama alivyosema Mujahid katika Kauli Yake:

لِّمَتَّوِّبِينَ

**“...kwa wachunguzi.”**

Amesema, ‘kwa wenye kufanya uhakiki na kuchunguza.’<sup>1</sup> Na Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na Adh-dhahaak, ‘kwa wenye kuzingatia.’<sup>2</sup>

Na amesema Qatada, ‘kwa wenye kuzingatia.’<sup>3</sup>

لِّمَتَّوِّبِينَ

**“...kwa wachunguzi.”**

Wenye kuangalia kwa undani.

### **Mji wa Sodoma Upo Njiani**

وَأَنَّهَا لَبِسَبِيلٍ مُّقِيمٍ ﴿٧٦﴾

**“Na miji hii ipo kwenye njia inayopitiwa.”**

Maana yake: Kwa hakika mji wa Sodoma ambao ulipata gharika miongoni mwa kupinduliwa muonekano wake wa kihisia na kimaana, na kupopolewa kwa mawe, mpaka ukawa ni ziwa lenye kunuka uvundo, likiwa baya. Mji huo uko katika njia ambayo mapito yake yanaendelea mpaka leo.

Kama Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:120.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:121.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:121.



وَأَنْتُمْ تَتَمُرُونَ عَلَيْهِمْ مُصْبِحِينَ ﴿١٣٧﴾ وَبِالْيَلِّ أَلَّا تَعْقِلُونَ ﴿١٣٨﴾

**“Na hakika nyinyi mnawapitia wakati wa asubuhi, na usiku. Basi je! Hamyatii akilini?” (37:137-138)**

Na Kauli Yake:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٣٧﴾

**“Hakika katika hayo ipo ishara kwa Waumini.”**

Maana yake: Lile ambalo Tumefanya kwa watu wa Lut عليه السلام, miongoni mwa kuangamia na kuteketea na kumuokoa Kwetu Lut عليه السلام na watu wake wa nyumbani ni dalili ya wazi kwa waumini juu ya kuwepo kwa Allah تعالى na ukweli wa Mitume Wake.

وَإِنْ كَانَ أَصْحَابُ الْأَيْكَةِ لَظَالِمِينَ ﴿١٣٨﴾ فَآتَقَمْنَا مِنْهُمْ وَإِنَّهُمَا لَبِإِمَامٍ مُّبِينٍ ﴿١٣٩﴾

**78. Na hakika watu wa Kichakani walikuwa wenye kudhulumu.**

**79. Kwa hivyo Tukawaadhibu. Na nchi mbili hizi ziko kwenye njia ilio wazi.**

**Kuangamizwa Watu wa Msitu, Watu wa Shu'aib عليه السلام**

Watu wa msitu ni watu wa Shu'aib عليه السلام. Wamesema hivyo Adh-dhahak, Qatada na wengineo. *Al-Aykah* – ni miti yenye kusongamana<sup>1</sup> na ilikuwa dhulma yao ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kufanya uvamizi njiani, na kupunguza kwao pishi na mizani. Allah تعالى Akawaadhibu wao, kwa ukelele na tetemeko na adhabu ya siku ya kiwingu.<sup>2</sup> Na walikuwa karibu na watu wa Lut عليه السلام, baada yao, katika zama, na majirani zao katika makazi, na kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema:

وَإِنَّهُمَا لَبِإِمَامٍ مُّبِينٍ

**“Na nchi mbili hizi ziko kwenye njia ilio wazi.”**

Maana yake: Katika njia zilizo dhahiri.<sup>3</sup> Amesema hivyo Ibn Abbas, Mujahid, Addhahak na wengine رضي الله عنهم, njia iliyo wazi. Na kwa sababu hiyo wakati alipowakhofisha Shu'aib عليه السلام watu wake alisema katika kuwaonya huko:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:125.

<sup>2</sup> Ibn Kathir analieleza hilo baadaye katika Tafsiri ya Surat Ash-Shu'araa.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:125.

وَمَا قَوْمٌ لُوطٍ مِّنكُمْ بِبَعِيدٍ

**“Na watu wa Lut’ si mbali nanyi.” (11:89)**

وَلَقَدْ كَذَّبَ أَصْحَابُ الْحِجْرِ الْمُرْسَلِينَ ﴿٨٩﴾ وَأَتَيْنَهُمْ آيَاتِنَا فَكَانُوا عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٩٠﴾  
وَكَانُوا يَنْحِتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا ءَامِنِينَ ﴿٩١﴾ فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةُ مُصْبِحِينَ ﴿٩٢﴾ فَمَا  
أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٣﴾

**80. Na bila ya shaka wakaazi wa Hijr waliwakanusha Mitume.**

**81. Na Tuliwapa ishara Zetu, nao wakazipuuzwa.**

**82. Nao walikuwa wakichonga majumba katika milima kwa amani.**

**83. Basi ukelele ukawatwaa asubuhi.**

**84. Hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.**

### Kuangamizwa kwa Watu wa Al-Hijri, Nao ni Thamud

Watu wa Hijri ni Thamud, ambao walimkadhibisha Mtume Swaleh عليه السلام Mtume wao, na mwenye kumkadhibisha Mtume mmoja kwa hakika amewakadhibisha Mitume wote. Na Ametaja Allah تعالى kwamba Aliwajia Saleh عليه السلام na Ishara za kweli kwa kile alichowaletea Saleh عليه السلام, kama vile ngamia ambaye Alimtoa Allah تعالى kwao kwa maombi ya Saleh عليه السلام kutoka katika jiwe gumu. Na alikuwa anakula nyasi katika nchi yao, ana siku ya kunywa maji na wao wana siku yao ya kuchota maji, katika siku yenye kujulikana. Walipotakabari, na wakamkata miguu yake aliwaambia:

تَمَتُّعُوا فِي دَارِكُمْ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ ۖ ذَٰلِكَ وَعَدُّ غَيْرٍ مُّكَذِّبٍ

**“Stareheni katika mji wenu muda wa siku tatu. Hiyo ni ahadi isiyo kuwa ya uwongo.” (11:65)**

Na Allah تعالى Amesema:

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ فَاسْتَحَبُّوا الْعَمَىٰ عَلَىٰ الْهُدَىٰ

**“Na ama Thamudi Tuliwaongoza, lakini walipenda upofu kuliko uwongofu.” (41:17)** Allah تعالى Anasema,

وَكَانُوا يَنْحِتُونَ مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا ءَامِنِينَ ﴿٧٣﴾

**“Na walikuwa wakichonga majumba katika milima kwa amani.”**

Maana yake: Pasi na khofu na wala kuyahitajia. Bali ni kwa kiburi na majivuno tu na kwa kucheza kama ambavyo hilo linashuhudiwa katika kutengeza kwao katika majumba yao katika jangwa la Hijri. Jangwa ambalo alilipitia Mtume ﷺ na hali ya kuwa yeye anakwenda Tabuk, akakiinamisha kichwa chake na akampeleka haraka mnyama wake. Na akawaambia Sahaba wake:

«لَا تَدْخُلُوا بُيُوتَ الْمُعَذِّبِينَ إِلَّا أَنْ تَكُونُوا بِأَيِّنَّ، فَإِنْ لَمْ تَبْكُوا فَبَاكُوا خَشْيَةً أَنْ يُصِيبَكُمْ مَا أَصَابَهُمْ»

*“Msiingie majumba ya watu wenye kuadhibiwa isipokuwa hali ya kuwa mnalia, msipolia, basi jilizeni kwa kuogopea kuwapata nyinyi yaliyo wapata wao.”<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake:

فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ مُصْبِحِينَ ﴿٧٤﴾

**“Basi ukelele ukawatwaa asubuhi.”** Maana yake: Wakati wa asubuhi ya siku ya nne.

فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٧٥﴾

**“Hayakuwafaa waliyokuwa wakiyachuma.”**

Maana: Waliyokuwa wanazalisha kutokana na mimea yao na matunda yao waliyoyafanyia ubakhili maji yake, wakamnyima ngamia, mpaka wakamkata miguu, ili asife, akawafanyia ufinyu katika maji. Kwa hiyo hazikuwaondolea wao mali hizo na wala hazikuwafaa wakati ilipokuja amri ya Bwana Wako.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَإِنَّ السَّاعَةَ لَأَتِيَةٌ فَاصْفَحِ  
الصَّفْحَ الْجَمِيلَ ﴿٧٦﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْخَلَّاقُ الْعَلِيمُ ﴿٧٧﴾

**85. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa ajili ya Haki. Na hakika Kiyama kitafika. Basi samehe msamaha mzuri.**

**86. Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Muumbaji Mjuzi.**

<sup>1</sup> Ahmad 2:91.

## Imeumbwa Dunia kwa Madhumuni Maalumu Kisha Kitasimama Kiama

Allah تعالى Anasema:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَإِنَّ السَّاعَةَ لَأْتِيَةٌ

**“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa ajili ya Haki. Na hakika Kiyama kitafika.”**

Kwa Kufanya Uadilifu:

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَوُوا بِمَا عَمِلُوا

**“ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda.” (53:31)**

Na Allah تعالى Amesema:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطْلًا ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ

كَفَرُوا مِنَ النَّارِ ﴿٣٧﴾

**“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya waliokufuru. Ole wao waliokufuru kwa Moto utaowapata.” (38:27)**

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٨﴾ فَتَعَلَىٰ اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿٣٩﴾

**“Je! Mlidhani ya kwamba Tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi Kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mola ila Yeye, Mola Mlezi wa Arshi Tukufu.” (23:115-116)**

Kisha Amemueleza Mtume wake ﷺ kuhusu Kiama na kwamba itakuwa makosa kwa washirikina watakapomtukana na kuyakadhibisha kwao yale ambayo amewajia nayo. Kama ilivyo Kauli Yake:

فَأَصْفَحْ عَنْهُمْ وَقُلْ سَلَامٌ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٤٠﴾

**“Basi wasamehe, na uwambie maneno ya salama. Watakuja jua.” (43:89)**

Na Mujahid, Qatada na wengine wamesema yalikuwa hayo kabla ya

kuamrisha kupigana na maadui. Na hayo ni kama, walivyosema kwani sura hii imeshuka Makkah na kupigana kumekuwa sheria baada ya kuhama.

إِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْخَلْقُ الْعَلِيمُ ﴿٨٦﴾

**“Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Muumbaji Mjuzi.” (15:86)**

Huko ni kuthibitisha juu ya kuwepo kurejea akhera na kwamba Yeye Allah تعالى Anaweza Kukisimamisha Kiyama kwani Yeye Ndiye Muumbaji Ambaye Hashindwi Kuumba kitu chochote, Mwenye Kuvijua sana vile vilivyochakaa katika viwiliwili na vikatawanyika katika maeneo yote ya Ardhi.

Kama ilivyo Kauli Yake:

أُولَئِكَ الَّذِينَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدْرٍ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلْقُ  
 الْعَلِيمُ ﴿٨٦﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٧﴾ فَسُبْحَانَ الَّذِي  
 بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٨٨﴾

**“Kwani Aliyeziumba mbingu na ardhi hawezi Kuwaumba mfano wao? Kwani! Naye Ndiye Muumbaji Mkuu, Mjuzi. Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni Kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa. Basi Ametakasika Yule Ambaye Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu; na Kwake Yeye mtarejeshwa.” (36:81-83)**

\* \* \*

وَلَقَدْ آتَيْنَاكَ سَبْعًا مِنَ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنَ الْعَظِيمَ ﴿٨٧﴾ لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَآخِضْ بِجَنَاحِكِ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾ وَقُلْ إِنِّي أَنَا النَّذِيرُ الْمُبِينُ ﴿٨٩﴾ كَمَا أَنْزَلْنَا عَلَى الْمُقْتَسِمِينَ ﴿٩٠﴾ الَّذِينَ جَعَلُوا الْقُرْآنَ عِضِينَ ﴿٩١﴾ فَوَرَّيْنَاكَ لَئْسَ لَكَ مِنَ الْأَعْيُنِ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٢﴾ فَاصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٣﴾ إِنَّا كَفَيْنَاكَ الْمُسْتَهْزِئِينَ ﴿٩٤﴾ الَّذِينَ يَحْتَفِلُونَ فِي اللَّهِ لَهَا آخَرٌ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٩٥﴾ وَلَقَدْ نَعَلْنَاكَ أَنْتَ يَضِيقُ صَدْرُكَ بِمَا يَقُولُونَ ﴿٩٦﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُن مِّنَ السَّجْدِينَ ﴿٩٧﴾ وَاعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿٩٨﴾

وَلَقَدْ آتَيْنَاكَ سَبْعًا مِنَ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنَ الْعَظِيمَ ﴿٨٧﴾ لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَآخِضْ بِجَنَاحِكِ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾

87. Na Tumekupa Aya saba zinazo somwa mara kwa mara, na Qur’ani Tukufu.<sup>1</sup>

88. Usiviangalie kwa macho yako vitu Tulivyowa-neemesha makundi fulani kati yao, wala usiwahuzunikie. Na wainamishie bawa lako (la huruma) Waumini.

**Ukumbusho wa Neema za Qur’an na Amri ya Kuzingatia Ujumbe Wake.**

Allah تعالی Anasema kwa Mtume Wake ﷺ kama Tulivyokupa Qur’ani tukufu, basi usiitazame dunia na pambo lake na kile ambacho Tumewastarehesha kwacho watu wake miongoni mwa starehe zake zenye kwisha. Tumefanya hivyo kuwajaribu ndani yake. Kwa hiyo usionee gere kwa lile ambalo wao wamo ndani yake. Na kwa nafsi yako juu yao isiwe na masikitiko kwa kuwahuzunikia kutokana na kuipinga kwao dini yako.

﴿٨٨﴾ وَآخِضْ بِجَنَاحِكِ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

**“Na watwae kwa upole wanaokufuata miongoni mwa waumini.”**  
(26:215)

<sup>1</sup> Maana ya neno Mathani ni “yenye kusomwa mara kwa mara.”

Maana yake: Walainishie upande wako. Kama ilivyo Kauli Yake:

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ

بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**“Hakika Amekwishakujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayokutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.” (9:128)**

Kwa hakika wametofautiana wafasiri wa Qur’ani kuhusu sura saba zinazoitwa “*Sab’u ul - Mathani*” ni zipi sura hizo? Ibn Masud, Ibn Umar na Ibn Abbas, Mujahid, Saeed bin Jubair, Adh-dhahak na wengine رضي الله عنهم, wamesema hizo ni zile sura saba ndefu, wanazikusudia sura zifuatazo: *Al-Baqarah. Al-Imran, A-Nisaa, Al-Maida, Al-Anaam, Al-Aaraf, na Yunus*. Ametoa maelezo ya wazi juu ya hilo Ibn Abbas na Saeed bin Jubair رضي الله عنهما; na amesema Saeed رضي الله عنه, Ameweka wazi katika sura hizo mambo ya faradhi na adhabu kwa wenye makosa na visa na hukumu. Na Ibn Abbas رضي الله عنه amesema, Ameweka wazi upigaji mifano habari na mazingatio.<sup>1</sup> (Na kauli ya pili) “*Sab’u ul Mathani*” ni *Surat Al-Fatiha* nayo ni aya saba. Na yamepokewa hayo kutoka kwa Ali, Umar na Ibn Masoud رضي الله عنهم, amesema Ibn Abbas رضي الله عنه na *Bismillah*<sup>2</sup> ndiyo aya ya saba. Na kwa hakika Allah<sup>3</sup> Amewahusisheni nyie, kwa aya saba hizo. Na kwa kauli hiyo amesema Ibrahim Al-Nnakhai na Abdillah bin Ubayd bin Umar, Ibn Abii Mulayka, Shahr bin Hawshab, Al-Hassan Al-Basry na Mujahid.<sup>4</sup>

Al-Bukhari رحمه الله تعالى ameleta hapa Hadithi mbili, moja yao: Kutoka kwa Abu Saeed bin Al-Mualla رضي الله عنه amesema: Alipita Mtume ﷺ na hali ya kuwa mimi ninasali akaniita, si kumuendea, mpaka nilipomaliza kusali nikamuendea akasema:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:130-132.

<sup>2</sup> Hiyo ni kusema, *Bismillahir Rahmanir Rahim*,” na tarjama yake ni “Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Kadhalika, *Fatihah* ina Aya saba.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:133.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:133.

«مَا مَنَعَكَ أَنْ تَأْتِيَنِي؟»

“Ni jambo gani lililokuzuia kuniitikia?”

Nikasema, ‘nilikuwa ninasali’, akasema:

«أَلَمْ يَقُلِ اللَّهُ

“Hivi hakusema Mwenyezi Mungu,”

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ

**“Enyi mlioamini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume pindi wanapowaiteni...” (8:24)**

أَلَا أَعْلَمُكَ أَعْظَمَ سُورَةٍ فِي الْقُرْآنِ قَبْلَ أَنْ أُخْرَجَ مِنَ الْمَسْجِدِ»

“Je nikufundishe sura kubwa sana katika Qur’ani kabla sijatoka msikitini?”

Akaenda Mtume ﷺ ili atoke, nikamkumbusha. Akasema:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

**“Sifa njema zote ni za Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (1:2)**

هِيَ السَّبْعُ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنُ الَّذِي أُوتِيَتْهُ»

“Hizo ndiyo aya saba zenye kukaririwa, na Qur’ani ambayo nimepewa.”

Ya pili, Abu Huraira رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema,

«أُمُّ الْقُرْآنِ هِيَ السَّبْعُ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنُ الْعَظِيمُ»

“Mama wa Qur’ani ndiyo aya saba zenye kukaririwa, na Qur’ani tukufu ambayo nimepewa.”<sup>1</sup>

Hili ni andiko la wazi lililothibitisha kuwa *Al-Fatiha*, ndiyo aya saba zinazoitwa “*Sab’u ul Mathani*” na Qur’ani tukufu, isipokuwa ni kwamba hilo halipingani

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:232.



na kuzisifu sura nyingine isiyokuwa hiyo katika sura saba ndefu. Kwa kuwa ndani yake kuna wasifu kama huu, kama ambavyo vilevile hakupingani na kuisifu Qur'ani yote kwa sifa hiyo. Kama Alivyosema Allah تعالى:

اللَّهُ نَزَلَ أَحْسَنَ الْحَدِيثِ كِتَابًا مُتَشَابِهًا مَثَانٍ

**“Mwenyezi Mungu Ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa;...” (39:23)**

Kwa hiyo kitabu hicho kinakaririka kwa njia na kinafanana kwa njia nyengine nayo ni Qur'ani Tukufu, vilevile. Na Kauli Yake:

وَلَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ

**“Wala usivikodolee macho Tulivyowastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao;...” (20:131)**

Maana yake: Tosheka na kile ambacho Amekupa Allah تعالى miongoni mwa Qur'ani Tukufu, na wala usijali yale ambayo wao wamo ndani yake, miongoni mwa starehe na anasa zenye kumalizika. Amesema Al-Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ

**“Usivitumbulie macho yako...”** Amesema: “Ni kumkataza mtu kuyatamani yale ambayo yanamilikiwa na mwenzake.”<sup>1</sup> Na amesema Mujahid:

إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ

**“...vitu Tulivyowaneemesha makundi fulani kati yao,”** Hao ni matajiri.<sup>2</sup>

وَقُلْ إِنِّي - أَنَا النَّذِيرُ الْمُبِينُ ﴿٨١﴾ كَمَا أَنْزَلْنَا عَلَى الْمُقْتَسِمِينَ ﴿٨٢﴾ الَّذِينَ جَعَلُوا

الْقُرْآنَ عِضِينَ ﴿٨٣﴾ فَوَرَبِّكَ لَنَسَعَنَّاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٨٤﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٥﴾

**89. Na sema: Hakika mimi ni mwonyaji mwenye kubainisha.**

**90. Kama hivyo Tuliwateremshia walioapizana.**

**91. Ambao wakaifanya Qur'ani vipande vipande.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:141.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:141.

92. *Basi Naapa kwa Mola wako Mlezi! Tutawahoji wote,*

93. *Kwa waliyokuwa wakiyatenda.*

### Mtume ﷺ ni Mhofishaji Aliye Wazi Uhofishaji Wake

Allah تعالیٰ Anamuamuru Mtume wake ﷺ aseme kuwaambia watu:

إِنِّي أَنَا النَّذِيرُ الْمُبِينُ

***“Hakika mimi ni mwonyaji mwenye kubainisha.”***

Niliye wazi katika ukhofishaji, ni mwonyaji watu na adhabu yenye kuumiza, kuwashukia wao kutokana na kumkadhibisha Mtume. Kama ilivyowashukia wale wa kabla yao, miongoni mwa umma, uliokadhibisha Mitume wao, na namna ya adhabu ya mateso Aliyowapa watu hao. Na imekuja katika sahihi ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنهما kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّمَا مَنَّلِي وَمَثَلُ مَا بَعَنِّي اللهُ بِهِ كَمَثَلِ رَجُلٍ أَتَى قَوْمَهُ فَقَالَ: يَا قَوْمُ! إِنِّي رَأَيْتُ الْجَيْشَ بِعَيْنِي، وَإِنِّي أَنَا النَّذِيرُ الْعُرْنَانُ فَالْتَّجَاءَ النَّجَاءَ، فَأَطَاعَهُ طَائِفَةٌ مِنْ قَوْمِهِ فَأَذْلَجُوا وَأَنْطَلَقُوا عَلَى مُهْلِهِمْ فَتَجَّوْا، وَكَذَّبَهُ طَائِفَةٌ مِنْهُمْ فَأَضْحَوْا مَكَانَهُمْ، فَصَبَّحَهُمُ الْجَيْشُ فَأَهْلَكَهُمْ وَاجْتَاَحَهُمْ، فَذَلِكَ مَثَلُ مَنْ أَطَاعَنِي وَاتَّبَعَ مَا جِئْتُ بِهِ وَمَثَلُ مَنْ عَصَانِي وَكَذَّبَ مَا جِئْتُ بِهِ مِنَ الْحَقِّ»

*“Hakika si vingine mfano wangu na mfano wa kile ambacho amenipeleka kwacho Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa mtu aliyewaendea watu wake akasema, ‘Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi nimeliona jeshi kwa macho yangu na kwa hakika mimi ni mkhofishaji wa wazi kwa hiyo jiokoeni, likamtii kundi katika watu wake, wakaondoka mapema na wakaondoka kidogo kidogo wakaokoka; na likamkadhibisha kundi katika wao, wakapambazukiwa wakiwa mahali pao, likawaendea asubuhi jeshi na likawaangamiza na kuwateketeza. Kwa hiyo, huo ni mfano wa wale ambao wamenitii na wakayafuata yale ambayo nimekuja nayo, na mfano wa wale ambao wameniasi na wakayakadhibisha yale ambayo nimekuja nayo miongoni mwa haki.”<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 13:264, Muslim 4:1788.

Tafsiri ya Tamko *Al-Muqtasimin*

الْمُقْتَسِمِينَ

“...*walioapiziana*,” Inamaanisha walioapiana juu ya kuwapinga Mitume na Kuwaadhibu kama ilivyo Kauli ya Allah عليه السلام kuhusu watu wa Saleh ,

قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ

**“Wakasema: Apishaneni kwa Mwenyezi Mungu tutamshambulia usiku yeye na ahali wake;...” (27:49)**

Maana: Tutawaua usiku. Amesema Mujahid رضي الله عنه waliapiana,

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَا يَبْعَثُ اللَّهُ مَنْ يَمُوتُ

**“Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa viapo vyao kwamba Mwenyezi Mungu Hatomfufua aliyekufa.” (16:38)**

أَوْلَمْ تَكُونُوا أَقْسَمْتُمْ مِّن قَبْلُ

**“Kwani nyinyi si mliapa zamani...” (14:44)**

أَهْتَوَلَاءِ الَّذِينَ أَقْسَمْتُمْ لَا يَنَالُهُمُ اللَّهُ بِرَحْمَةٍ

**“Je, hawa sio wale mliokuwa mkiwaapia kuwa Mwenyezi Mungu hatawafikishia rehema.” (7:49)**

Kama kwamba wao walikuwa hawalikadhibishi jambo lolote hapa duniani isipokuwa wanaapa juu yake. Hivyo “*muktasimini*” kwa maana wakaitwa waapaji. Na Kauli Yake,

الَّذِينَ جَعَلُوا الْقُرْآنَ عِضِينَ ﴿٧٩﴾

**“Ambao wakaifanya Qur’ani vipande vipande.”** Maana yake: Wamevigawa vitabu vyao vilivyoteremshwa juu yao, wakaamini baadhi na wakakufuru baadhi. Amepokea Bukhari kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما ,

جَعَلُوا الْقُرْآنَ عِضِينَ

**“...wakaifanya Qur’ani vipande vipande.”** Amesema hao ni watu wa kitabu wamevigawanya vitabu mafungu tofauti wakaamini baadhi na wakakufuru<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:233.

baadhi na pamesemwa: Makusudio ya *Al-Muqtasimin* ni Makuraishi, na makusudio ya tamko Qur'ani katika Aya hii ni Qur'ani hii. Na maana ya kuifanya mafungu ni kama alivyosema Atwaa kuwa wengine wamesema Muhammad ni mchawi, wengine mwenda wazimu na wengine wakasema kuhani. Hayo ni makundi mbalimbali kama ilivyosimuliwa na Addhahak na wengine.

Amepokea Muhammad bin Ishaq kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwamba Al-Walid bin Ali Mughira alikutana na kundi la Makuraishi, na alikuwa ni mwenye utukufu kwao, na alikuwa amehudhuria msimu wa Hijjah akawaambia: 'Enyi Maquraishi, wamehudhuria msimu huu watu mbalimbali, na kwa hakika makundi ya Waarabu yatakujieni katika msimu huu, na kwa hakika wamelisikia jambo la mwenzenu huyu. Kwa hiyo, afikianeni katika rai moja tu, msitofautiane, wala kupingana kauli zenu nyinyi wenyewe kwa wenyewe.' Wakasema, "Na wewe Ee Aba Abdi Shamsi, tupe rai ambayo tutaisema.' Akasema: 'Bali nyinyi semeni nitasikiliza.' Wakasema: 'Tutasema kwamba ni kuhani.' Akasema, 'hakuwa kuhani.' Wakasema tutasema, 'mwendawazimu.' Akasema, 'hakuwa mwendawazimu.' Wakasema, 'tutasema mshairi.' Akasema, 'hakuwa mshairi.' Wakasema, 'tutasema mchawi.' Akasema, 'hakuwa mchawi.' Wakasema, 'tutasema nini?' Akasema, 'naapa kwa Allah تعالى, maneno yake yana utamu, hamtakuwa wenye kusema chochote isipokuwa mtu atajua kuwa ni maneno batili, na hakika kauli nzuri ni kusema yeye ni mchawi.' Wakaondoka wakiwa na kauli mbiu hiyo. Akateremsha Allah تعالى juu yao:

الَّذِينَ جَعَلُوا الْقُرْآنَ عِضِينَ ﴿١٦﴾

***"Ambao wakaifanya Qur'ani vipande vipande."*** Namna, mbalimbali,

فَوَرَبِّكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٧﴾

***"Basi Naapa kwa Mola wako Mlezi! Tutawahoji wote."***

Hao watu ambao wameyasema hayo kwa Mtume ﷺ,<sup>1</sup>

فَوَرَبِّكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٧﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾

***"Basi Naapa kwa Mola wako Mlezi! Tutawahoji wote, kwa waliyo kuwa wakiyatenda."***

<sup>1</sup> Sirah Ibn Hisham 1:288. Riwaya hii si sahihi kwa kuwa mmojawapo katika wapokezi wake hajulikani.

Amesema Abu Jaafar kutoka kwa Arabii kutoka kwa Abuu Al-Alia kuhusu kauli yake hii akasema, "Watu wote wataulizwa juu ya mambo mawili Siku ya Kiama: Walikuwa wanaabudu nini na waliwajibu nini Mitume."<sup>1</sup> Ali bin Abi Talhah amesimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema,

﴿فَوَزِيكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ﴾ ﴿عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾

***"Basi Naapa kwa Mola wako Mlezi! Tutawahoji wote, Kwa waliyokuwa wakiyatenda."***

Kisha Akasema,

﴿فَيَوْمَئِذٍ لَا يُسْأَلُ عَنْ ذَنْبِهِ إِنْسٌ وَلَا جَانٌّ﴾

***"Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jini."*** (55:39)

Amesema, 'hataauliza Je mmefanya kadha?' Kwa sababu Anajua zaidi hali yao, isipokuwa Atasema, 'kwa nini mmefanya hivi na hivi?'<sup>2</sup>

﴿فَأَصْدَعُ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضُ عَنِ الْمُشْرِكِينَ﴾ ﴿إِنَّا كَفَيْنَاكَ الْمُسْتَهْزِئِينَ﴾  
 ﴿الَّذِينَ يَجْعَلُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ﴾ ﴿وَلَقَدْ نَعَلْنَاكَ أَنْكَ يَضْبِقُ﴾  
 ﴿صَدْرَكَ بِمَا يَقُولُونَ﴾ ﴿فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُن مِّنَ السَّاجِدِينَ﴾ ﴿وَأَعْبُدْ رَبَّكَ﴾  
 ﴿حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ﴾

**94. Basi wewe yatangaze uliyoamrishwa, na jitenge na washirikina.**

**95. Hakika Sisi Tunatosha kukuinga na wanaokejeli.**

**96. Hao wanaofanya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Yupo mola mwingine. Basi, watakuja jua!**

**97. Na Sisi Tunajua kwa hakika kuwa wewe kifua chako kinaona dhiki kwa hayo wayasemayo.**

**98. Basi mtakase Mola Wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanaomsujudia.**

**99. Na muabudu Mola Wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:150.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:150.

### Amri ya Kudhihirisha Ukweli kwa Uwazi

Allah تعالى Alimuamrisha Mjumbe wake ﷺ kufikisha aliyotumwa, kutangaza na kueneza ujumbe ambao ni kukabiliana na washirikina. Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema kuwa Kauli Yake:

فَأَصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ

**“Basi wewe yatangaze uliyoamrisha.”**

Maana: litekeleze.<sup>1</sup> Na katika upokezi mwingine:

(افْعَلْ مَا تُؤْمَرُ)

(Fanya lile unaloamrisha.)

Na amesema Mujahid huko ni kuidhihirisha Qur'an katika Sala.<sup>2</sup> Na amesema Abu Ubaida kutoka kwa Abdillah bin Masu'd رضي الله عنهما hakuacha kuwa Mtume ﷺ ni mwenye kujificha mpaka iliposhuka aya hii,

فَأَصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ

**“Basi wewe yatangaze uliyoamrisha,...”**

Akatoka yeye na Masahaba zake.<sup>3</sup>

### Amri ya Kuwapuuzwa Washirikina na Allah تعالى Kuchukua Dhamana ya Kumkinga dhidi ya Wanaokejeli

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٥١﴾ إِنَّا كَفَيْنَاكَ الْمُسْتَهْزِئِينَ ﴿١٥٢﴾

**“...na jitenge na washirikina. Hakika Sisi Tunatosha Kukukinga na wanaokejeli.”**

Maana: Fikisha kile ambacho kimeteremshwa kwako kutoka kwa Bwana wako, na usigeuke kwa washirikina ambao wanataka kukuzuia na aya za Allah تعالى,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:151.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:151.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:152.

وَدُّوْا لَوْ تَدَّهِنُ فَيَدَّهِنُوْنَ ﴿٩﴾

**“Wanatamani lau ungelainisha ili nao wakulainishie.” (68:9)**

Na usiogope kwani hakika Allah تعالى Atakuinga na Kukulinda na wao. Kama ilivyo Kauli Yake Allah تعالى:

﴿ يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ۗ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ ۗ ﴾

**“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe Wake. Na Mwenyezi Mungu Atakulinda na watu.” (5:67)**

Muhammad ibn Is’haq رحمه الله تعالى amesema: “Watu watano ndio walioongoza katika kudhihaki, na walikuwa viongozi na waheshimiwa katika watu. Kutoka kwa Bani Asad bin ‘Abd Al-Uzzah bin Qusayy alikuwepo Al-Aswad bin Al-Muttalib Abu Zam’ah. Kwa mujibu wa dua niliyomsikia Mtume ﷺ alikuwa akiwalaani kwa sababu ya machungu na kejeli waliyomfanyia. Mtume ﷺ alisema,

«اللَّهُمَّ أَعِمَّ بَصْرَهُ، وَأَنْكِلُهُ وَلَدَهُ»

**“Ewe Allah, mpe upofu na chukua (uhai wa) mwanaye.”**

Na kwa Banuu Zuhra, Al-Aswad bin Abdi Yaqhouthi bin Wahab bin Abdi Manafi, bin Zuhra. Na kwa Banuu Makhzoum, Al-Walidi bin Al Mukhira bin Abdillah bin Umar Bin Makhzoum. Na kwa Banuu Sahn Ibn Amri bin Huswai Sui bin Kaaba bin Luayy ni Al-Aswi bin Waili bin Itisham bin Said Bin Saad. Na katika Khuzaa Al-Harithi bin Al-Twala, ni Twala bin Amri Ibin Al-Harith, bin Abdi Amri bin Malkan. Walipozidisha shari kwa Mtume ﷺ kumcheza shere, Aliteremsha Allah تعالى:

﴿ فَاصْدَعْ بِمَا تُؤْمَرُ وَأَعْرِضْ عَنِ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠﴾ إِنَّا كَفَيْنَاكَ الْمُسْتَهْزِئِينَ ﴿١١﴾ الَّذِينَ سَجَعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ ۗ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿١٢﴾ ﴾

**“Basi wewe yatangaze uliyoamrishwa, na jitenge na washirikina. Hakika Sisi Tunatosha kukuinga na wanaokejeli. Hao wanaofanya**

***kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu yupo mola mwingine. Basi, watakuja jua! "***

Amesema Ibn Is'haqa رحمه الله تعالى amenizungumzia Yazid bin Ruman kutoka kwa Urwa bin Azzubair au wengine katika wanawazuoni kwamba Jibril عليه السلام alimuendea Mtume ﷺ na hali ya kuwa anatufu Al-Kaaba, na akasimama pamoja na Mtume ﷺ ubavuni mwake, akampitia Al-Aswad bin Al-Muttalib akamtupia usoni mwake jani bichi akapofuka. Na akampitia Al-Aswad bin Abd Yaghauthi akaashiri tumboni kwake, tumbo lake likapata ugonjwa, wa kuharisha akafa, kwa Amri ya Allah تعالى, kwa sababu ya kuvimba tumbo. Na akampitia Al-Walid bin Al-Mughira, akaashiria kwenye jeraha, lililokuwa chini ya mguu – fundo la mguu wake na lilikuwa limempata kabla ya hapo kwa miaka miwili, huku akiishikilia shuka yake. Na sababu ya jeraha hilo, kwamba yeye alimpitia mtu mmoja katika Khuzaa akiwa anagandisha nyoya katika chembe cha mshale wake, kikanasa chembe hicho shuka yake, kikamparua mguu wake, ikawa hiyo ni sababu ya kufa kwake. Na alimpitia Al-Asi bin Waili akaashiria kwenye unyayo wa mguu wake, akatoka hali ya kuwa juu ya punda wake akiwa anakusudia kwenda Twaif, akapiga magoti, kipande cha nguo kikaingia katika unyayo wa mguu wake kikamuua. Na akampitia Al-Harithi bin Al Twula Twala akaashiria kichwani kwake akamuweka usaha, hivyo ukamuua.<sup>1</sup>

الَّذِينَ يَجْعَلُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿١٦﴾

***"Hao wanaofanya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu yupo mola mwingine. Basi, watakuja jua!"***

Hayo ni matisho makubwa sana na makemeo yenye mkazo kwa yule aliyefanya pamoja na Mwenyezi Mungu mola mwingine mwenye kuabudiwa.

<sup>1</sup> Sirah Ibn Hisham 1:409, 410. Riwaya hii si sahihi. Licha ya kutokuwa sahihi, 'Urwah alizaliwa miaka kumi na tisa baada ya Hijrah kwa ukokotoaji hisabati hizo wa awali kwa mujibu wa Adh-Dhahabi (Angalia As-Siyar).



## Uhamasishaji Katika Kuyavumilia Matatizo na Kuamrisha Kushikamana na Tasbihi na Kumuabudu Allah تعالى Mpaka Kufa

وَلَقَدْ نَعَلْنَا أُنُوكَ يَضِيقُ صَدْرُكَ بِمَا يَقُولُونَ ﴿٧٧﴾ فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُنْ مِنَ  
السَّاجِدِينَ ﴿٧٨﴾

***“Na Sisi Tunajua kwa hakika kuwa wewe kifua chako kinaona dhiki kwa hayo wayasemayo. Basi mtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanaomsujudia.”***

Maana yake: Sisi kwa hakika tunajua Ee Muhammad kwamba unanyongeka na kujikunja kutokana na Maudhi yao kwako, basi yasikufazaishe hayo na kukuvunja moyo na ukaacha kuufikisha ujumbe wa Allah تعالى, mtegemee Yeye, kwani Anakutosha na Atakunusuru juu yao. Hivyo shughulikia Kumtaja Allah تعالى, Kumsifu na Kumtakasa na Kumuabudu (Sala) na kwa sababu hiyo Amesema:

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُنْ مِنَ السَّاجِدِينَ ﴿٧٧﴾

***“Basi mtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanaomsujudia.”***

Kama ilivyokuja katika hadithi aliyopokea Imam Ahmad: kutoka kwa Nuaim bin Hammar kwamba yeye amemsikia Mtume ﷺ akiwa anasema:

«قَالَ اللَّهُ تَعَالَى يَا ابْنَ آدَمَ! لَا تَعْبُزُ عَنْ أَرْبَعِ رَكَعَاتٍ مِنْ أَوَّلِ النَّهَارِ أَكْفِكَ آخِرَهُ»

*“Amesema Allah تعالى: Ee Mwanadamu usishindwe na raka'a nne mwanzoni mwa mchana, nitakutoshea mwisho wake.”<sup>1</sup>*

وَأَعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿٧٩﴾

***“Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini.” (15:99)***

Amesema Al-Bukhary: Amesema Salim Yakini ni kifo<sup>2</sup> na Salim huyu ni Salim bin Abdillah bin 'Umar kama alivyopokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa Salim Bin Abdillah.

<sup>1</sup> Ahmad 5:286.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:235.

وَأَعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿١١﴾

**“Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini.”**

Amesema mauti.<sup>1</sup> Hadithi Sahihi kutoka kwa Ummu Al-Alaa, mwanamke wa Kianswari kwamba Mtume ﷺ alipoingia kwa Uthumani bin Madhoum akiwa amekwishakufa, alisema Ummu Al-Alaa, Rehema ya Allah تعالى iwe juu yako Abuu Assaib Ushahidi wangu juu yako, Amekutukuza Allah تعالى, Mtume ﷺ akamuuliza,

«وَمَا يُدْرِيكَ أَنَّ اللَّهَ أَكْرَمُهُ؟»

*“Na ni jambo gani lililokufahamisha kwamba Allah Amemtukuza?”*

Akasema: ‘Ninakukomboa kwa baba na mama yangu Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwani amekuwaaje?’ Akasema:

«أَمَّا هُوَ فَقَدْ جَاءَهُ الْيَقِينُ، وَإِنِّي لَأَرْجُو لَهُ الْخَيْرَ»

*“Ama yeye, kwa hakika yamemjia mauti na kwa hakika mimi ninamtarajia kheri.”<sup>2</sup>*

Na panachukuliwa dalili kwa aya hii tukufu, nayo ni Kauli Yake

وَأَعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿١١﴾

**“Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini.”**

Kwamba ibada kama vile Sala na mfano wake, inapasa kwa mtu muda wa kuwa akili yake imethibiti, kwa hiyo atasali kufuatana na hali yake.

Kama ilivyothibiti katika Sahih ya Al-Bukhari kutoka kwa Imran bin Huswain رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema:

«صَلِّ قَابِلًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَقَاعِدًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَعَلَىٰ جَنْبٍ»

*“Sali hali ya kuwa umesimama, ikiwa hukuweza basi hali ya kukaa; ikiwa hukuweza basi ni juu ya ubavu.”<sup>3</sup>*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:1.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 3:137.

<sup>3</sup> Fat’hul Al-Bari 2:684

Na panachukuliwa dalili kwa aya hiyo juu ya kukosoa mtazamo wa kundi la wapingaji. Kundi hilo wametafsiri neno “*Yaqini*” ni maarifa, kwa hiyo wakati wowote atakapofikia mmoja wao kwenye maarifa, huacha kufanya hukumu zote za kisharia. Na huu ni ukafiri upotevu na ujinga. Kwani Mitume walikuwa pamoja na Maswahaba wao ni wajuzi sana kuliko watu wote kwa Allah تعالی, katika kujua sana Haki Zake na Sifa Zake na yale anayoyastahiki miongoni mwa kutukuzwa. Na walikuwa pamoja na hayo wanaabudu na kudumu juu ya kufanya kheri mpaka wakati wa kufa. Na hakika hapana jambo jengine, makusudio ya neno *Yaqin* hapa ni kifo kama tulivyotanguliza.

Na Sifa Njema zinamstahiki Allah تعالی tu na neema. Na Sifa Njema ni za Allah تعالی tu juu ya Kutuongoza na ni juu Yake tu Kuombwa msaada na Kutegemewa. Na Yeye Ndiye Mwenye Kuombwa, Kutufisha juu ya hali timilifu na nzuri. Na Sifa Njema tena zinamstahiki Mwenyezi Mungu Bwana wa viumbe wote.



## Tafsiri ya Suratu An-Nahl

### Sura ya 16

#### Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

#### سُورَةُ النَّحْلِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَتَىٰ أَمْرٌ لِلَّهِ فَلَا تَشْتَعِلْهُ ۚ سُبْحٰنَهُ ۚ وَتَعَلَّىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١﴾ يُنزِلُ الْمَلٰٓئِكَةَ بِالرُّوحِ مِنْ أَمْرِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ أَنْ أَنْذِرُوا أَنَّهُ لَا إِلٰهَ إِلَّا أَنَا فَاتَّقُونِ ﴿٢﴾ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ ۚ تَعَلَّىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣﴾ خَلَقَ الْإِنسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ ۖ إِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴿٤﴾ وَالْأَنْعَامَ خَلَقَهَا ۗ لَكُمْ فِيهَا دِفْءٌ وَمَنْفَعٌ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٥﴾ وَلَكُمْ فِيهَا جَمَالٌ حِينَ تُرْبِحُونَ وَحِينَ تَسْرَحُونَ ﴿٦﴾ وَتَحْمِلُ أُنْفُسَكُمْ إِلَىٰٓ أَهْلِكُمْ إِلَىٰ بَلَدٍ لَّمْ تَكُونُوا بَلِغِيهِ إِلَّا بِشِقِّ الْأُنْفُسِ ۚ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٧﴾ وَالْحَيْلَ وَالْبِغَالَ وَالْحَمِيرَ لِتَرْكَبُوهَا وَزِينَةً ۚ وَخَلَقَ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨﴾ وَعَلَى اللَّهِ قَصْدُ السَّبِيلِ وَمِنْهَا جَائِرٌ وَلَوْ شَاءَ لَهَدَلَكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٩﴾

أَتَىٰ أَمْرٌ لِلَّهِ فَلَا تَشْتَعِلْهُ ۚ سُبْحٰنَهُ ۚ

وَتَعَلَّىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١﴾

1. Amri ya Mwenyezi Mungu itafika tu. Basi msiihimize. Ametakasika na Ametukuka na wanayo mshirikisha nayo.

#### Onyo la Kukaribia Kiyama

Allah تعالیٰ Anaelezea kukaribia Kiyama kwa tamko la kitendo kilichofanyika kinachojulisha uhakika wa kutokea kwake.

Kama Alivyosema:

أَقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي

غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿١٠﴾

“Imekaribia kwa watu hisabu yao nao wameghafilika mno wamepuuza.” (21:1) na,

أَقْرَبَتْ السَّاعَةَ وَأَنْشَقَّ الْقَمَرَ ﴿١٦﴾

“...kimekaribia kiama na mwezi umepasuka.” (54:1)

Kauli Yake Allah تعالى،

فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ

“Basi msiihimize.”

Anakusudia: kilicho mbali kimekaribia kwa hiyo msikiharakishe. Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَلَوْلَا أَجَلٌ مُّسَمًّى لَجَاءَهُمُ الْعَذَابُ وَلَيَأْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا

يَشْعُرُونَ ﴿١٦﴾ يَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿١٧﴾

“Na wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka. Na lau kuwa hapana wakati maalumu ulio wekwa, basi adhabu ingeli wajia, na ingeli watokea kwa ghafla, na hali wao hawana khabari. Wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka, na hali Jahannamu kwa hakika imewazunguka makafiri!” (29:53-54)

Amepokea Ibni Abi Haatim kutoka kwa Uqba Ibn Amir رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

«تَطَّلِعُ عَلَيْكُمْ عِنْدَ السَّاعَةِ سَحَابَةٌ سَوْدَاءٌ مِنَ الْمَغْرِبِ مِثْلَ الثُّرَيْسِ، فَمَا تَرَآل تَرْتَفِعُ فِي السَّمَاءِ ثُمَّ يُنَادِي مُنَادٍ فِيهَا: يَا أَيُّهَا النَّاسُ! فَيَقْبِلُ النَّاسُ بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ: هَلْ سَمِعْتُمْ، فَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ: نَعَمْ، وَمِنْهُمْ مَنْ يَشْكُ، ثُمَّ يُنَادِي الثَّانِيَةَ: يَا أَيُّهَا النَّاسُ! فَيَقُولُ النَّاسُ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ: هَلْ سَمِعْتُمْ، فَيَقُولُونَ: نَعَمْ، ثُمَّ يُنَادِي الثَّالِثَةَ: يَا أَيُّهَا النَّاسُ! أَتَى أَمْرُ اللَّهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ»

“Wakati wa kiyama yatawajia mawingu meusi kutokea Magharibi kama vile ngao, itaendelea kupaa mbinguni. Kisha atatoa wito muitaji ndani ya wingu hilo, ‘Enyi watu!’ Na hapo watu wataelekeana wao kwa wao na kuulizana: ‘Je mmesikia?’ Baadhi yao watasema: ‘Ndiyo’. Na wengine watakuwa na shaka, kisha atatoa wito wa pili: ‘Enyi watu!’ Wao kwa wao wataulizana: ‘Je mmesikia?’ Watasema: ‘Ndiyo.’ Kisha ataita kwa mara ya tatu: ‘Enyi watu! Amri ya Allah imeshafika msiihimize.”

Mtume ﷻ amesema,

«فَوَ الَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، إِنَّ الرَّجُلَيْنِ لَيَنْشُرَانِ الثَّوْبَ فَمَا يَطْوِيَانِهِ أَبَدًا، وَإِنَّ الرَّجُلَ  
لَيَمُدُّنَّ حَوْضَهُ فَمَا يَسْقِي فِيهِ شَيْئًا أَبَدًا، وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَخْلُبُ نَافَتَهُ فَمَا يَشْرِبُهُ أَبَدًا -  
فَالَ - وَيَسْتَغِيلُ النَّاسُ»

*“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake! Hakika ya watu wawili watakunjua nguo, kamwe hawatawahi kuzikunja, na hakika mtu atatayarisha hodhi (birika ya maji) yake, lakini hatowahi kuwanywesha wanyama wake, na hakika mtu atamkama ngamia wake lakini hatowahi kuyanywa – amesema – na watu watashughulika.”<sup>1</sup>*

Kisha Allah تعالى Akaitakasa Nafsi Yake na kumshirikisha kwao na kitu kingine, na kuabudu kwao pamoja Naye kitu kingine kisichokuwa Yeye, katika masanamu na washindani. Ametukuka na Kutakasika, Sifa na Utukufu Mkubwa, na hao ndio wenye kukadhibisha kiyama, Akasema:

سُبْحٰنَهُ وَتَعَالٰى عَمَّا يُشْرِكُوْنَ

**“Ametakasika na Ametukuka na wanayo mshirikisha nayo.”**

يُنزِلُ الْمَلٰٓئِكَةَ بِالرُّوحِ مِنْ أَمْرِهِ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِۦ أَنْ أَنْذِرُوْا أَنَّهُ لَا إِلٰهَ إِلَّا أَنَا  
فَآتِقُوْنَ ﴿٦﴾

**2. Huwateremsha Malaika na Roho kwa Amri Yake juu ya amtakaye katika waja Wake ili nyinyi muone kwamba hapana mola ila Mimi, basi nicheni Mimi.**

Allah تعالى Anamtuma Amtakae na Ujumbe wa Tawhidi

Allah تعالى Anasema:

يُنزِلُ الْمَلٰٓئِكَةَ بِالرُّوحِ

**“Huwateremsha Malaika na Roho.”**

Maana yake: Wahyi. Kama Kauli Yake:

<sup>1</sup> Al-Hakim 4:539.

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا ۗ مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ وَلَا الْإِيمَانُ وَلَٰكِن جَعَلْنَاهُ نُورًا نَّهْدِي بِهِ مَن نَّشَاءُ مِّنْ عِبَادِنَا ۗ

**“Na namna hivi? Tumekufunulia Qur’ani kwa Amri Yetu. Ulikuwa hujui Kitabu ni nini, wala Imani. Lakini Tumekifanya kuwa ni Nuru ambayo kwayo Tunamuongoa Tumtakaye katika waja Wetu.”**  
(42:52)

Na Kauli Yake:

عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِّنْ عِبَادِهِ ۗ

**“...juu ya Amtakaye katika waja Wake.”**

Nao ni Mitume. Kama Alivyosema Allah تعالى:

اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ

**“...Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi Anaweka ujumbe Wake...”** (6:124)

اللَّهُ يَصْطَفِي مَنِ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِنَ النَّاسِ ۗ

**“Mwenyezi Mungu Huteua Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu.”** (22:75)

يُلْقِي الرُّوحَ مِنْ أَمْرِهِ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ لِيُنذِرَ يَوْمَ التَّلَاقِ ﴿١٥﴾ يَوْمَ هُمْ بَبْرُونَ  
لَا يَخْفَىٰ عَلَى اللَّهِ مِنْهُمْ شَيْءٌ ﴿١٦﴾ لِمَنِ الْمُلْكُ الْيَوْمَ ۗ لِلَّهِ الْوَاحِدِ الْقَهَّارِ ﴿١٧﴾

**“Hupeleka Roho kwa Amri Yake juu ya Amtakaye katika waja Wake, ili kuonya kwa Siku ya Mkutano. Siku watakatodhihiri wao. Hapana kitachofichikana chochote kwa Mwenyezi Mungu. Ufalme ni wa nani leo? Ni wa Mwenyezi Mungu Mmoja Mtenda nguvu.”**  
(40:15-16)

أَن نُّنذِرُوا

**“...waonyeni...”**

Maana yake: Ili uwakataze.

أَنْتُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاتَّقُونِ

**“...kwamba hapana mola ila Mimi, basi nicheni Mimi.”**

Maana yake: Ogopeni Adhabu Yangu ambayo ipo kwa ajili ya mwenye kukhalifu Amri Yangu na kumuabudu asiye kuwa Mimi.

خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ تَعَالَى عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٦﴾ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُبِينٌ ﴿١٧﴾

**3. Ameziumba mbingu na ardhi kwa Haki. Ametukuka na wanayoshirikisha.**

**4. Amemuumba mtu kwa tone la manii. Naye mara amekuwa mshindani dhaahiri.**

**Allah تعالی Ndiye Ambae Ameumba Mbingu, Ardhi na Mwanadamu**

Allah تعالی Anaelezea Kuumba Kwake Ulimwengu wa juu, nayo ni mbingu, na ulimwengu wa chini, nayo ni ardhi na vilivyo humo, na kwamba hivyo vimeumbwa kwa haki si kwa upuuzi, bali,

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَفُؤْ بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحَسَنَى ﴿١٦﴾

**“...ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema Awalipe mema.” (53:31)**

Kisha Akatakasa Nafsi Yake dhidi ya ushirikina wa aliyeabudu pamoja Naye kitu kingine. Wakati Yeye Ndiye Pekee katika Kuumba Hana mshirika. Na kwa hili Anastahiki Kuabudiwa Peke Yake bila mshirika. Kisha Akakumbusha kuwa Ameumba jinsi ya mwanadamu kutokana na tone la manii. Yaani: duni dhaifu. Na alipofikia hatua ya kujitegemea, ghafla anampinga Mola Wake تعالی, na anamkadhibisha na anawapiga vita Mitume Wake, wakati yeye ameumbwa awe mtumwa, si mpinzani. Kama inavyosema Kauli Yake تعالی:

خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِالْحَقِّ تَعَالَى عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٦﴾

**“Ameziumba mbingu na ardhi kwa Haki. Ametukuka na wanayoshirikisha.”**



وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ مِنَ الْمَاءِ بَشَرًا فَجَعَلَهُ نَسَبًا وَصِهْرًا ۗ وَكَانَ رَبُّكَ قَدِيرًا ﴿٥٤﴾ وَيَعْبُدُونَ  
 مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُهُمْ وَلَا يَضُرُّهُمْ ۗ وَكَانَ الْكَافِرُ عَلَىٰ رَبِّهِ ظَهِيرًا ﴿٥٥﴾

**“Naye Ndiye Aliyemuumba mwanaadamu kutokana na maji, Akamjaalia kuwa na nasaba na ushemeji. Na Mola wako Mlezi ni Muweza. Na wanayaabudu badala ya Mwenyezi Mungu yasiyo wafaa wala yasiyo wadhuru. Na kafiri daima ni msaidizi wa kumpinga Mola wake Mlezi.” (25:54-55)**

Na Kauli Yake:

أَوَلَمْ يَرَ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُبِينٌ ﴿٧٦﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا  
 وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۗ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٧﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۗ  
 وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٨﴾

**“Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi Tumemuumba yeye kutokana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri! Na akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake, akasema: Ni nani huyo atakayeihisha mifupa nayo imekwisha mung’unyika? Sema: Ataihuisha huyo huyo Aliyeiumba hapo mara ya mwanzo. Na Yeye ni Mjuzi wa kila aina ya Kuumba.”**

Na imekuja katika Hadithi aliyoipokea Imam Ahmad na Ibn Majah kutoka kwa Busra Ibn Jahsh amesema: Mtume ﷺ alitema katika kitanga chake cha mkono kisha akasema:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: ابْنِ آدَمَ أَنِّي تُعْجِزُنِي وَقَدْ خَلَقْتُكَ مِنْ مِثْلِ هَذِهِ، حَتَّى  
 مَشَيْتَ بَيْنَ بُرْدَيْكَ وَلِلْأَرْضِ مِنْكَ وَنَيْدٌ، فَجَمَعْتَ وَمَنْعْتَ حَتَّى إِذَا  
 بَلَغْتَ الْحُلُقُومَ قُلْتَ: أَتَصَدَّقُ، وَأَنَّى أَوَانُ الصَّدَقَةَ»

**“Allah تعالى Anasema; ‘Ewe mwanadamu utanishinda vipi na hali Nimekuumba kwa kitu kama hiki? Mpaka pale Nilipo kukamilisha ukawa sawa, ukatembea kati ya nguo zako na ardhi inahisi uzito wako. Ukakusanya na ukazuia mpaka pale roho ilipofika kwenye koo**

ukasema: 'Nitatoa sadaka na uko wapi wakati wa kutoa sadaka sasa?'<sup>1</sup> (Al-Hakim).

وَالْأَنْعَمَ خَلَقَهَا لَكُمْ فِيهَا دِفْءٌ وَمَنْفَعٌ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿٥﴾ وَلَكُمْ فِيهَا جَمَالٌ  
حِينَ تَرْحَمُونَ وَحِينَ تَسْرَحُونَ ﴿٦﴾ وَتَحْمِلُ أَوْقَالَكُمْ إِلَىٰ بَلَدٍ لَّمْ تَكُونُوا بِلَاغِهِ إِلَّا  
بِشِقِّ الْأَنْفُسِ ۗ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرؤُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٧﴾

**5. Na wanyama hao Amekuumbieni. Katika hao mna vifaa vya kutia joto, na manufaa mengineyo, na baadhi yao mnawala.**

**6. Na wanakupeni furaha pale mnapowarudisha jioni na mnapowapeleka malishoni asubuhi.**

**7. Na hubeba mizigo yenu kupeleka kwenye miji msiyoweza kuifikia ila kwa mashaka ya nafsi. Hakika Mola wenu Mlezi ni Mpole na Mwenye Kurehemu."**

**Wanyama ni Miongoni mwa Alivyoviumba Allah تعالى na ni Neema Kutoka Kwake.**

Allah تعالى Anajisifu juu ya waja Wake kwa Alichowaumbia katika wanyama, ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kama Alivyowachanganua katika *Suratil-Al-An-'aam* wakafikia jozi nane,<sup>1</sup> na kwa Alichowaumbia ndani ya wanyama miongoni mwa maslahi na manufaa yatokanayo na sufu, manyoya yao na nywele zao. Kwayo wanavaa na wanatandika, na maziwa yao wanakunywa na walichokizaa wanakula na wanafaidika na mazuri walionayo. Maana yake: Pambo. Na kwa sababu hii Akasema:

وَلَكُمْ فِيهَا جَمَالٌ حِينَ تَرْحَمُونَ

**"...Na wanakupeni furaha pale mnapowarudisha jioni."**

Na huo ni wakati wa kuwarejesha kutoka malishoni jioni. Kwani wakati huo matumbo yao yamejaa, na zimejaa chuchu zao, na ziko juu nundu zao.

<sup>1</sup> Ahmad 2:410, Ibn Majah 2:903.

وَحِينَ نَسْرَحُونَ

**"...na mnapowapeleka malishoni asubuhi."**

Asubuhi pale mnapowatoa na kuwapeleka machungani.

وَتَحْمِلُ أَنْفَالَكُمْ

**"Na hubeba mizigo yenu,"**

Na hiyo ni mizigo mizito ambayo hamuwezi kuichukua na kuibeba.

إِلَىٰ بَلَدٍ لَّمْ تَكُونُوا بَلِّغِيهِ إِلَّا بِشِقِّ الْأَنْفُسِ

**"...kupeleka kwenye miji msiyoweza kuifikia ila kwa mashaka ya nafsi."**

Hayo ni katika Hijjah, Umrah, vita na biashara na yaliyo kama hayo. Pia mnawatumia katika aina za matumizi ya kupanda na kubebesha kama Alivyosema:

وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۖ نُسْقِيكُمْ مِمَّا فِي بُطُونِهَا وَلَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ كَثِيرَةٌ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿١٦﴾  
وَعَلَيْهَا وَعَلَىٰ الْفُلْكِ تُحْمَلُونَ ﴿١٧﴾

**"Na hakika mnayo mazingatio makubwa katika wanyama hao - Tunakunywesheni katika vile viliomo matumboni mwao, na nyinyi mnapata katika hao manufaa mengi, na pia mnawala. Na juu yao na juu ya marikebu mnabebwa." (23:21-22)**

Na Akasema:

اللَّهُ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَنْعَامَ لِتَرْكَبُوا مِنْهَا وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿١٦﴾ وَلَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ  
وَلِتَبْلُغُوا عَلَيْهَا حَاجَةً فِي صُدُورِكُمْ وَعَلَيْهَا وَعَلَىٰ الْفُلْكِ تُحْمَلُونَ ﴿١٧﴾ وَرِيكُم  
ءَايَاتِهِ فَأَيُّ آيَاتِ اللَّهِ تُنْكِرُونَ ﴿١٨﴾

**"Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekujaalieni nyama hao, mifugo, ili muwapande baadhi yao, na muwale baadhi yao. Na katika hao**

<sup>1</sup> Angalia Tafsiri ya Surat Al-An'am (6:143-144).

***mnayo manufaa kadhaa wa kadhaa, na mnapata kwao haja ziliomo vifuani mwenu; na mnachukuliwa juu yao, na juu ya marikebu. Naye Anakuonesheni Ishara zake. Basi Ishara gani za Mwenyezi Mungu mnazozikataa?”(40:79-81)***

Hivyo, hapa Akasema baada ya kuzihesabu neema hizi.

إِنَّ رَبَّكُمْ لَرءُوفٌ رَّحِيمٌ

***“Hakika Mola wenu Mlezi ni Mpole na Mwenye Kurehemu.”***

Maana: Mola Wenu Aliyewadhililishia wanyama hawa. Kama Alivyosema,

أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّا خَلَقْنَا لَهُمْ مِمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَمًا فَهُمْ لَهَا مَلَائِكُونَ ﴿٧١﴾ وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ فَمِنْهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ ﴿٧٢﴾

***“Je! Hawaoni kwamba Tumewaumbia kutokana na iliyofanya Mikono Yetu wanyama wa mifugo, na wao wakawa wenye kuwamiliki. Na Sisi Tukawadhililishia. Basi baadhi yao wako wanao wapanda, na baadhi yao wanawala.”(36:71-72).***

Na Akasema:

وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلْكِ وَالْأَنْعَامِ مَا تَرْكَبُونَ ﴿٧٣﴾ لِتَسْتَوُوا عَلَى ظُهُورِهِمْ تَدْكُرُوا نِعْمَةَ رَبِّكُمْ إِذَا اسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ وَتَقُولُوا سُبْحٰنَ الَّذِي سَخَّرَ لَنَا هٰذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ ﴿٧٤﴾ وَإِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴿٧٥﴾

***“Na Akakufanyieni marikebu na wanyama mnaowapanda. Ili mkae vizuri migongoni mwao, kisha mkumbuke neema za Mola wenu Mlezi mnapokaa sawa sawa juu yao na msemi: Ametakasika Aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe. Na hakika sisi tutarudi kwa Mola wetu Mlezi.” (43:12-14).***

Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema:

لَكُمْ فِيهَا دِفءٌ

***“Katika hao mna vifaa vya kutia joto.”*** Anakusudia nguo,

وَمَنْفَعُ

“...na manufaa mengineyo.”

Anakusudia manufaa wanayoyapata ya chakula na vinywaji kutoka kwa wanyama hao.<sup>1</sup>

وَالْحَيْلَ وَالْبِغَالَ وَالْحَمِيرَ لِتَرْكَبُوهَا وَزِينَةً وَيَخْلُقُ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿١٦﴾

**8. Na farasi, nyumbu na punda ili muwapande, na kuwa ni pambo. Na Ataumba msivyovijua.**

Hii ni aina nyingine miongoni mwa Alivyowaambia waja Wake, Mwenyezi Mungu Mwenye Kutukuka Utukufu ni Wake, Anajifakharisha nao juu yao, nao ni farasi, nyumbu na punda ambao Amewafanya kwa ajili ya kupanda na mapambo na hayo ndiyo makusudio makubwa kwao. Imethibiti katika Bukhari na Muslim, Hadithi kutoka kwa Jabir bin Abdillah رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ amekataza kula nyama ya punda wafugwao, ameruhusu nyama ya farasi.<sup>2</sup>

Na amepokea Imam Ahmad na Abu Daud kwa isnadi mbili kila moja kwa masharti ya Muslim kutoka kwa Jabir رضي الله عنه amesema: ‘Siku ya Khaibar tulichinja farasi, nyumbu na punda, Mtume ﷺ akatukataza kula nyumbu na punda na hakutukataza kula farasi.’<sup>3</sup>

Na katika Muslim imethibiti Hadithi kutoka kwa Asmaa bint Abubakri رضي الله عنها amesema: “Tulichinja farasi wakati wa Mtume ﷺ tukamla wakati sisi tuko Madinah.”<sup>1</sup>

وَعَلَى اللَّهِ فَصْدُ السَّبِيلِ وَمِنْهَا جَائِرٌ وَلَوْ شَاءَ لَهَدْنَاكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٧﴾

**9. Na ni juu ya Mwenyezi Mungu Kuelekeza njia. Na zipo njia za upotovu. Na angelipenda angelikuongoeni nyote.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:168.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 9:570, Muslim 3:1541.

<sup>3</sup> Ahmad 3:356, 362, Abu Dawud 4:149, 151.

## Ufafanuzi wa Njia za Tafauti za Dini

Allah تعالى Alipoelezea wanyama wanaoweza kutumiwa kusafiri kimwili, pia Ametaja njia za kimaadili na kidini ambazo watu wanaweza kupita. Na mara nyingi inatokea katika Qur'ani uelezeaji wa mambo yanayofahamika kupitia njia za fahamu hadi kwenye mambo ya kimaana yenye manufaa kidini. Kama vile Kauli Yake Allah تعالى:

وَتَزَوَّدُوا فَإِنَّ خَيْرَ الزَّادِ التَّقْوَىٰ<sup>ع</sup>

***“Na jitengezeeni zawadi. Na hakika bora ya zawadi ni uchamungu...”, (2:297)***

يَبْنَئِي ۖ أَدَمَ قَدْ أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ لِبَاسًا يُورِي سَوَاءَ تَكْمٌ وَرِدِشًا<sup>ط</sup> وَلِبَاسٌ التَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ<sup>ع</sup>

***“Enyi wanaadamu! Tumekuteremshieni nguo za kuficha tupu zenu, na nguo za pambo. Na nguo za uchamungu ndio bora.” (7:26)***

Allah تعالى Alipotaja katika Sura hii wanyama miongoni mwa ngamia, ng'ombe, mbuzi na wengine ambao wanawapanda na wanawatimizia mahitaji yao wanayoyalenga na kuwabebea mizigo yao kwenda kwenye nchi na sehemu za mbali na safari ngumu, Akaingia kuelezea njia ambazo watu wanazozipita kufikia Kwake. Kwa hiyo Akaeleza kuwa njia ya haki katika hizo ni ile itakayomfikisha mtu Kwake. Akasema:

وَعَلَىٰ اللَّهِ فَصَدُّ السَّبِيلِ

***“Na ni juu ya Mwenyezi Mungu Kuelekeza njia.”***

Kama Alivyosema Allah تعالى:

وَأَنَّ هَذَا صِرَاطِي مُسْتَقِيمًا فَاتَّبِعُوهُ<sup>ط</sup> وَلَا تَتَّبِعُوا السُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمْ عَن سَبِيلِهِ<sup>ع</sup>

***“Na kwa hakika hii ndiyo njia Yangu Iliyonyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia Yake.” (6:153).***

<sup>1</sup> Muslim 3:1541

Amesema:

قَالَ هَذَا صِرَاطٌ عَلَيَّ مُسْتَقِيمٌ ﴿١٦﴾

**“Akasema: Hii njia ya kujia Kwangu iliyonyooka.” (15:41)**

Mujaahidi amesema: Ni njia ya haki kwa Allah تعالى.<sup>1</sup> Na Al-Awfi amesema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake:

وَعَلَى اللَّهِ قَصْدُ السَّبِيلِ

**“Na ni juu ya Mwenyezi Mungu Kuelekeza njia...”**

Anasema: Na ni juu ya Allah تعالى Kubainisha. Yaani: Anabainisha uongofu na upotofu. Kama hivi amepokea Ali Ibn Abi Twalha kutoka kwake. Na hivyo hivyo amesema Qatadah na Adh- Dhahaak kwa sababu hii amesema Allah تعالى,

وَمِنْهَا جَائِرٌ

**“Na zipo njia za upotovu...”**

Maana yake: Zimepondoka kinyume cha haki. Amesema Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine: Hizo ni njia mbali mbali<sup>2</sup>, maoni na matamania tofauti, kama vile Uyahudi, Unaswara na Umajusi. Ibn Mas`ud رضي الله عنه alikuwa akisoma,

(وَمِنْكُمْ جَائِرٌ)

(Na miongoni mwenu wamepotoka,)<sup>3</sup>

Kisha Allah تعالى Anaeleza kuwa yote yanatokana na uwezo Wake na Matakwa Yake. Kisha Allah تعالى Akasema:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلَّهُمْ جَمِيعًا

**“Na Angelipenda Angelikuongoeni nyote...”**

Na Amesema,

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلَّهُمْ جَمِيعًا

**“Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:175.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:176.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:176.

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٨﴾ إِلَّا مَنْ رَّحِمَ رَبُّكَ ۗ  
وَلِذَلِكَ خَلَقَهُمْ ۗ وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لِأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٩﴾

***“Na Mola wako Mlezi Angelipenda Angewafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu; na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu Amewaumba. Na litatimia Neno la Mola wako Mlezi: Kweli kweli Nitaijaza Jahannam kwa majini na watu pamoja.” (11:118-119).***

\* \* \*



هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لَكُمْ مِنْهُ شَرَابٌ وَمِنْهُ شَجَرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ ﴿١٠﴾ يُنْبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُونَ وَالنَّخِيلَ وَالْأَعْنَبَ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١١﴾ وَسَخَّرَ لَكُمْ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٢﴾ وَمَا ذَرَأَ لَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِقَوْمٍ يَذَكَّرُونَ ﴿١٣﴾ وَهُوَ الَّذِي سَخَّرَ الْبَحْرَ لِتَأْكُلُوا مِنْهُ لَحْمًا طَرِيًّا وَتَسْتَخْرِجُوا مِنْهُ حَبْلَ قَنَطَرٍ وَتَرَى الْفُلَّكَ مَوَازِرَ فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٤﴾ وَالْقَلَى فِي الْأَرْضِ رَوَّاسٍ أَنْ تَعِيدَ بِكُمْ وَأَنْهَرَ وَصُبُلًا لِعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥﴾ وَعَلَّمَتِ السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَالنَّجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ ﴿١٦﴾ أَفَمَنْ يَخْلُقُ كَمَنْ لَا يَخْلُقُ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١٧﴾ وَإِنْ تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا إِنَّ اللَّهَ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨﴾

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لَكُمْ مِنْهُ شَرَابٌ وَمِنْهُ شَجَرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ ﴿١٠﴾ يُنْبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُونَ وَالنَّخِيلَ وَالْأَعْنَبَ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿١١﴾

10. Yeye ndiye Anaye-kuteremshieni maji kutoka mbinguni. Katika hayo nyinyi mnapata ya kunywa, na miti ya kulishia.

11. Kwa hayo Yeye Anai-zalisha kwa ajili yenu mimea, na mizaituni, na mitende, na mizabibu, na kila namna ya matunda. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanao-fikiri.

### Rehema za Mvua na Faida Zake na Mvua ni katika Alama Zake

Allah تعالی Alipoelezea neema ya mifugo na wanyama wengine kwa wanadamu, kisha Ameerleza neema Aliyowaneemesha ya Kuteremsha mvua kutoka mawinguni. Hiyo ilikuwa inatimiza haja zao na wanyama wao. Akasema:

لَكُمْ مِنْهُ شَرَابٌ

“Kwa hayo mnapata kinywaji...” Maana yake: Ameyafanya maji kuwa matamu ili waweze kunywa na hakuyafanya yenye chumvi kali,

وَمِنْهُ شَجَرٌ فِيهِ تُسِيمُونَ

**"....na miti ya kulishia..."**

Maana yake: Akawatolea kutokana nayo miti mnayowalisha wanyama wenu. Kama alivyosema Ibn Abbas, Ikrima, Adh-Dhahaak, Qatada na Ibn Zaid رضي الله عنهم. Katika Kauli Yake, **"Na miti ya kulishia"**, mnawachungia<sup>1</sup>, miongoni mwao ni ngamia walishwao, na kuchungwa. Na Neno Lake:

يُنْبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُونَ وَالنَّخِيلَ وَالْأَعْنَابَ وَمِنْ كُلِّ الثَّمَرَاتِ

**"Kwa hayo Yeye Anaizalisha kwa ajili yenu mimea, na mizaituni, na mitende, na mizabibu, na kila namna ya matunda..."**

Maana yake: Anayatoa matunda hayo ardhini kwa maji ya aina moja, huku matunda yao yakitafautiana aina zake, ladha zake, rangi zake, harufu zake na maumbo yake, na kwa ajili hiyo Akasema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

**"Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanao fikiri."**

Maana yake: Dalili na hoja kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى. Kama Alivyosema:

أَمَّنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَأَنْزَلَ لَكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَنْبَتْنَا بِهِ حَدَائِقَ ذَاتَ بَهْجَةٍ مَا كَانَ لَكُمْ أَنْ تُنْبِتُوا شَجَرَهَا ؕ أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَعْلَمَ بِقَوْمٍ يَعْدِلُونَ ﴿٦٠﴾

**"Au Nani Yule Aliyeziumba mbingu na ardhi, na Akakuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwayo Tukaziotesha bustani zenye kupendeza? Nyinyi hamna uwezo wa kuiotesha miti yake. Je! Yupo mola pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali hao ni watu waliopotoka." (27:60)**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:178.

وَسَخَّرَ لَكُمْ الَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهٖ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿١٠﴾ وَمَا ذَرَأَ لَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ ﴿١١﴾

**12. Na Amefanya ukutumikieni usiku na mchana, na jua na mwezi, na nyota zikutumikieni kwa Amri Yake. Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wenye akili.**

**13. Na hivi Alivyovieneza katika ardhi vya rangi mbalimbali. Hakika katika hayo ipo ishara kwa watu wanaowaidhika.**

### Ishara Zilizotulizwa Ndani ya Kuudhalilisha Usiku na Mchana, Jua na Mwezi na Kinachoota Katika Ardhi

Allah تعالى Anawakumbusha waja Wake juu ya ishara Zake kubwa, zikiwemo neema kubwa katika Kuudhalilisha Kwake usiku na mchana hali ukipishana. Jua na mwezi vikizunguka, na nyota zilizotulia na zinazotembea katika pande za mbingu, ni nuru na mwangaza, ili zitumiwe kuongoza katika kiza. Na kila kimoja ya hivyo kinatembea katika muhimili wake ambao Allah تعالى Ameuwekea ndani yake, kinatembea kwa kasi iliyokadiriwa haizidi wala haipungui. Na vyote viko chini ya Nguvu na Utawala Wake, Udhalilisho Wake, Makadirio Yake na Usahilisho Wake. Kama Alivyosema:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهٖ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿١٢﴾

**“Hakika Mola Mlezi wenu ni Mwenyezi Mungu Aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha Akatawala juu ya Kiti cha Enzi. Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazotumika kwa Amri Yake. Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote”. (7:54).**

Na kwa sababu hii Amesema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ

**"Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wenye akili."**

Maana: Ishara za Uwezo Wake na Utawala Wake mkubwa kwa watu wanaomfahamu Allah تعالى na wanazifahamu hoja Zake.

Na Kauli Yake,

وَمَا ذَرَأَّا لَكُمْ فِي الْأَرْضِ مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ

**"Na hivi Alivyovieneza katika ardhi vya rangi mbalimbali."**

Allah تعالى Alipokumbusha ishara za mbinguni, Akakumbusha Alivyoviumba ardhini miongoni mwa maajabu, na vitu mbalimbali kama vile wanyama, madini, mimea na visivyo na uhai pamoja na tofauti za rangi zake, maumbo yake, na manufaa yaliyomo humo na sifa Zake,

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَذَّكَّرُونَ

**"Hakika katika hayo ipo ishara kwa watu wanaowaidhika."**

Maana: Neema za Allah تعالى wanazishukuru.

وَهُوَ الَّذِي سَخَّرَ الْبَحْرَ لِتَأْكُلُوا مِنْهُ لَحْمًا طَرِيًّا وَتَسْتَخْرِجُوا مِنْهُ حِلْيَةً تَلْبَسُونَهَا وَتَرَى الْفُلْكَ مَوَاحِرَ فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِنْ فَضْلِهِ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٤﴾ وَالْقَلْبُ فِي الْأَرْضِ رَوَاسِي أَنْ تَمِيدَ بِكُمْ وَأَنْهَارًا وَسُبُلًا لِّعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥﴾ وَعَلَّمَنَّا وَعَلَّمْنَاهُ وَإِلَّا نَجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ ﴿١٦﴾ أَفَمَنْ يَخْلُقُ كَمَنْ لَا يَخْلُقُ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١٧﴾ وَإِنْ تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا إِنَّ اللَّهَ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨﴾

**14. Yeye Ndiye Aliyeifanya bahari ikutumikieni, ili kutokana na humo mpate kula nyama laini, na mtoe humo mapambo mnayoyavaa. Na unaona marikebu zikikata maji humo, ili mtafute fadhila Yake, na mpate kushukuru.**

**15. Na Kaweka katika ardhi milima ili ardhi isiyumbe yumbe nanyi. Na mito, na njia ili mpate kuongoka.**

**16. Na alama nyengine. Na kwa nyota wao wanajiongoza.**

**17. Ati Anaye umba ni kama asiye umba? Basi hebu, hamkumbuki?**

**18. Na mkizihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamuezi kuzidhibiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira, Mwenye Kurehemu.**

### **Ishara za Uwezo wa Allah تعالی Ndani ya Bahari, Milima, Mito, Njia na Nyota**

Allah تعالی Anaelezea Kudhalilisha Kwake bahari inayopiga mawimbi, na Anajisifu kwa waja Wake kwa Kuwadhalilishia na Kuwarahisishia kupanda ndani yake, kuweka humo samaki wadogo na wakubwa, na Kuwahalalishia nyama ya samaki hao wawe hai au wamekufa, ndani ya kipindi cha Hijjah na Umrah. Kadhalika, Amewahalalishia vingine Alivyoviumba humo, kama vile lulu na johari zingine za thamani. Kurahisisha Kwake Allah تعالی Kuzitoa kwao kutoka ndani ya mkondo wa bahari, likiwa ndio pambo wanalolivaa, na Kuidhalilisha Kwake bahari. Kubeba mashua ambazo zinapasua bahari, na yasemekana zinapasua upepo na maana zote mbili ni sahihi. Na kwa maana nyingine ni kuwa inasemekana zinapasua bahari kwa omo zake ambazo Allah تعالی Amewaelekeza waja Kuzitengeneza, Amewaelekeza hilo ikiwa ni urithi kutoka kwa baba yao Nuhu, amani iwe juu yake, kwani yeye ndiye wa kwanza kupanda mashua, na ufundi wa mashua umeanzia kwake. Kisha watu wengine nao wakauchukua kutoka kwake, karne baada ya karne, na kizazi hadi kizazi, wanaenda mji hata mji, na nchi hata nchi na kitongoji hata kitongoji, ili kukichukua kilicho huko mbali na kukileta hapa, na kilicho hapa kukipeleka huko mbali. Na kwa sababu hii Akasema Allah تعالی:

وَلْتَبْتَغُوا مِن فَضْلِهِ وَلِعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

**"...ili mtafute Fadhila Yake, na mpate kushukuru..."**

Kwa neema na hisani Zake. Kisha Allah تعالی Akaelezea ardhi na Alichokiweka humo kama vile milima mirefu na milima iliyodidimia sana ardhini, ili ardhi itulie na isiende mrama na kilicho juu yake katika wanyama wakakosa maisha mazuri.

Kwa sababu hii Akasema:

وَالْجِبَالَ أَرْسَنَهَا ﴿١٧﴾

**“Na milima Akaisimamisha.”**

وَأَنْهَرَهَا وَسُبُلًا

**“Na mito, na njia.”**

Maana yake: Ameweka humo mito inayotiririka kutoka mahala na kwenda kwingine ikiwa ni riziki kwa waja. Huchimbuka mahala fulani, nayo ni riziki kwa watu wa mahala pengine. Inakata maeneo, bara na majangwa, inatoboa milima mikubwa na midogo mpaka inafika ardhi ya waliokusudiwa neema hiyo. Ikitembea ardhini kulia na kushoto, kusini na kaskazini, mashariki na magharibi. Kati ya mito mikubwa na midogo na vijito vya msimu. Kadhalika baina ya chemchem inayotiririsha na inayokusanya, inayotiririka kwa kasi na taratibu kulingana na Alivyotaka, Akakadiria, Akadhaliisha na Kurahisisha, basi hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye tu, na hakuna mola asiyekuwa Yeye. Na kama hivyo Ameweka humo njia. Yaani: Njia zinazopitwa kutoka nchi kwenda nyingine. Mara nyingine Allah تعالی Anapasua mlima ili baina yake yawe ni mapito na njia. Kama Alivyosema Allah تعالی:

وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا

**“...na Tukaweka humo njia pana ili wapate kuongoka.” (21:31).**

Na Kauli Yake,

وَعَلَّمْنَاهُ

**“Na alama nyengine.”**

Maana yake: Vitambulisho kama vile milima mikubwa na midogo, na mfano wa hayo, wanayoitumia wasafiri wa bara na baharini wanapopotea njia.

Na Kauli Yake:

وَيَا النِّجْمِ هُمْ يَهْتَدُونَ

**“Na kwa nyota wao wanajiongoza.”**

Maana yake: Katika kiza cha usiku. Haya ameyasema Ibn Abbas رضي الله عنهما<sup>1</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 17:187.

**Ibada ni Haki ya Allah** تعالیٰ

Kisha Akakumbusha juu ya Utukufu Wake, na kwamba ibada haistahiki isipokuwa Kwake tu, si mwingine asiye kuwa Yeye kama vile masanamu ambayo hayaumbi chochote bali hayo yanaumbwa. Na kwa sababu hiyo Akasema:

أَفَمَنْ يَخْلُقُ كَمَنْ لَا يَخْلُقُ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿١٧﴾

***"Ati Anayeumba ni kama asiyeumba? Basi hebu, hamkumbuki?"***

Kisha Akawakumbusha wingi wa neema Zake kwao na hisani Zake kwao Akasema:

وَإِنْ تَعُدُّوا نِعْمَةَ اللَّهِ لَا تُحْصُوهَا إِنَّ اللَّهَ لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨﴾

***"Na mkizihisabu neema za Mwenyezi Mungu, hamuezi kuzidhibiti. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghfira, Mwenye Kurehemu". (16:18)***

Maana yake: Anawaachia na kama Angewataka mumshukuru kwa Neema Zake zote mngalishindwa kufanya hivyo na kama Angewaamuru hilo mngeshindwa na mngeacha. Na kama Angewaadhibu, Angaliwaadhibu si kwa kuwa Mwenye Kuwadhulumu lakini Yeye ni Mwingi wa Msamaha, Mwingi wa Huruma, Anasamehe sana na Analipa hata kwa kidogo.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema: Hakika ya Allah تعالیٰ ni Mwingi wa msamaha kwa uzembe mliyo nao, katika kushukuru baadhi ya hayo, mtakapotubu na mkarejea kwenye kumtii Yeye na kuifuata Ridhaa Yake. Naye ni Mwenye Huruma hatakuadhibuni baada ya kurejea na kutubu<sup>1</sup>.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:187.

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُسِرُّونَ وَمَا تُعْلِنُونَ ﴿١٩﴾ وَالَّذِينَ  
 يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَخْلُقُونَ شَيْئًا وَهُمْ يُخْلَقُونَ ﴿٢٠﴾  
 أَمْوَاتٌ غَيْرُ أَحْيَاءٍ ۗ وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٢١﴾  
 إِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ ۖ فَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ قُلُوبُهُمْ  
 مُنْكَرَةٌ وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ ﴿٢٢﴾ لَا جَرَمَ أَنْ اللَّهُ يَعْلَمَ مَا  
 يُسِرُّونَ وَمَا يُعْلِنُونَ ۗ إِنَّهُمْ لَا يُحِبُّونَ الْمُسْتَكْبِرِينَ ﴿٢٣﴾  
 وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ مَآذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ ۗ قَالُوا أَسْطِطِيرُ  
 الْأَوَّلِينَ ﴿٢٤﴾ لِيُخْلِعُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ  
 وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ أَلَا سَاءَ مَا  
 يَزُرُونَ ﴿٢٥﴾ قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَاتَى اللَّهُ  
 بُيُوتَهُمْ مِنَ الْفَوَاحِشِ فَخَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ مِنْ فَوْقِهِمْ  
 وَأَتَنَّهُمْ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٦﴾ ثُمَّ يَوْمَ  
 الْقِيَامَةِ يُخْزِبُهُمْ وَيَقُولُ بَيْنَ يَدَيْهِ الَّذِينَ كُنْتُمْ  
 تُشْتَفِقُونَ فِيهِمْ ۗ قَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ إِنَّ الْخِزْيَ  
 الْيَوْمَ وَالسُّوءَ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٢٧﴾ الَّذِينَ تَتَوَفَّاهُمْ  
 الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ ۗ فَأَلْفَوْا السَّلَامَ ۗ مَا كُنَّا نَعْمَلُ  
 مِنْ سُوءٍ ۗ بَلَىٰ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٨﴾  
 فَادْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ فَلَيْسَ مَثْوًى  
 الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٢٩﴾

وَاللَّهُ يَعْلَمُ مَا تُسِرُّونَ وَمَا  
 تُعْلِنُونَ ﴿١٩﴾ وَالَّذِينَ يَدْعُونَ  
 مِنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَخْلُقُونَ شَيْئًا وَهُمْ  
 يُخْلَقُونَ ﴿٢٠﴾ أَمْوَاتٌ غَيْرُ أَحْيَاءٍ ۗ  
 وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ ﴿٢١﴾

19. Na Mwenyezi Mungu Anayajua mnayoyaficha na mnayoyatangaza.

20. Na wale wanaowaomba wasiokuwa Mwenyezi Mungu hawaumbi kitu, bali wao wameumbwa.

21. Ni wafu si wahai, na wala hawajui watafufuliwa lini.

Miungu ya Washirikina Imeumbwa Haiumbi

Kisha Allah تعالی Akaeleza kuwa masanamu wanayo-yaomba badala ya Allah تعالی hayaumbi kitu na hayo yanaumbwa kama alivyo-sema Khalilii Ibrahim عليه السلام:

قَالَ أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْحِتُونَ ﴿٢٥﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٢٦﴾

“Hivyo mnaviabudu vitu mnavyovichonga wenyewe? Na hali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na hivyo mnavyovifanya!” (37:95-96).



أَمْوَاتٌ غَيْرُ أَحْيَاءٍ ۗ

“...Ni wafu si wahai...”

Maana yake: Ni viumbe visivyo na uhai, havina roho, kwa hiyo havisikii havioni na wala havina akili,

وَمَا يَشْعُرُونَ أَيَّانَ يُبْعَثُونَ

“...na wala hawajui watafufuliwa lini...”

Maana yake: Hawajui Kiama kitakuwa lini, basi vipi yanatarajiwa manufaa kutoka kwao au thawabu au malipo? Bila shaka hayo yanatarajiwa kutoka kwa Ambaye Anajua kila kitu naye ni Muumba wa kila kitu.

إِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ ۖ فَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ قُلُوبُهُمْ مُنْكَرَةٌ وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ ﴿٢٢﴾ لَا جَرَمَ أَنِ اللَّهُ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ ۗ وَمَا يُعْلِنُونَ ۗ إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْتَكْبِرِينَ ﴿٢٣﴾

**22. Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Lakini wasioiamini Akhera nyoyo zao zinakataa, nao wanajivuna.**

**23. Hapana shaka kuwa hakika Mwenyezi Mungu Anayajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza. Kwa hakika Yeye Hawapendi wanaojivuna.**

**Hakuna wa Kuabudiwa Isipokuwa Allah تعالى Tu**

Allah تعالى Anaeleza kuwa hakuna mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye Mmoja Peke Yake, Mwenye kukusudiwa, na Akaeleza kuwa makafiri nyoyo zao zinayakataa hayo. Kama Alivyoelezea kuhusu wao wakishangazwa na hilo,

أَجْعَلِ الْآلِهَةَ إِلَهًا وَاحِدًا ۗ إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ عَجَابٌ ﴿٢٤﴾

**“Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu.” (38:5).**

وَإِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَحْدَهُ اشْمَأَزَّتْ قُلُوبُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ ۗ وَإِذَا ذُكِرَ الَّذِينَ مِنْ

دُونِهِ إِذَا هُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٢٥﴾

**“Na Anapotajwa Mwenyezi Mungu Peke Yake nyoyo za wasioiamini Akhera huchafuka. Na wanapotajwa wenginewe asiye kuwa Yeye basi wao hufurahi.” (39:45)**

وَهُمْ مُسْتَكْبِرُونَ

**“...nao wanajivuna...”**

Maana yake: Katika kufanya ibada ya Allah تعالى pamoja na kupinga nyoyo zao tawhidi Yake. Kama Alivyoosema:

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ

**“ ...Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.” (40:60)**

Na kwa sababu hii Akasema:

لَا جَرَمَ

**“Hapana shaka.”** Maana: Ni haki,

أَنْ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُسْرُونَ وَمَا يُعْلِنُونَ

**“...kuwa hakika Mwenyezi Mungu Anayajua wanayoyaficha na wanayoyatangaza...”**

إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْتَكْبِرِينَ

**“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wanaotakabari...”**

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ مَاذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ قَالُوا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٦﴾ لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَزُرُونَ ﴿١٧﴾

**24 Na wanapoambiwa: Kateremsha nini Mola wenu Mlezi? Husema: Hadithi za kubuni za watu wa kale!**

**25. Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kujua. Angalia, ni maovu mno hayo wanayoyabeba!”**

## Kuangamizwa Makafiri na Kuongezwa Ukali wa Adhabu kwa Kukataa Kwao Uteremsho Kutoka kwa Mola Wao

Allah تعالى Anasema: Na kama wataulizwa wapingaji hawa:

مَاذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ

**“Kateremsha nini Mola wenu Mlezi?”** Wakiwa wamelitupilia mbali jibu, la swali waliloulizwa.

قَالُوا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ

**“Wanasema, Hadithi za kubuni za watu wa kale!”**

Hakuna alichoteremsha, na hiki anachotusomea ni Hadithi za waliotangulia, maana: Yametoka katika vitabu vya watu wa kale. Kama Alivyosema Allah

تعالى:

وَقَالُوا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٥﴾

**“Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni.” (25:5)**

Maana yake: Wanamzulia Mtume na wanayasema maneno yanayopingana na yanayotofautiana, na yote ni batili. Kama Alivyosema:

أَنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٤٨﴾

**“Tazama vipi wanavyokupigia mifano. Basi wamepotea. Kwa hivyo hawawezi kuipata njia.” (17:48).**

Na hayo ni kwamba kila anayetoka katika haki basi kwa vyovyote atavyosema atakosea tu. Na walikuwa wanasema: ‘ni mchawi, malenga, kuhani na kichaa.’ Kisha wakabaki katika uongo wao aliowaongopea Sheikh wao wa pekee anayeitwa Waliid Ibn Mughaira Makhzuumiy.

إِنَّهُ فَكَّرَ وَقَدَّرَ ﴿١٩﴾ فَقَتَلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٢٠﴾ ثُمَّ قَتَلَ كَيْفَ قَدَّرَ ﴿٢١﴾ ثُمَّ نَظَرَ ﴿٢٢﴾

ثُمَّ عَبَسَ وَبَسَرَ ﴿٢٣﴾ ثُمَّ أَدْبَرَ وَاسْتَكْبَرَ ﴿٢٤﴾ فَقَالَ إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ يُؤْتَرُ ﴿٢٥﴾

**“Kwani hakika yeye alifikiri na akapima. Basi ameangamia! Vipii alivyopima! Tena ameangamia! Vipii alivyopima! Kisha akatazama, Kisha kakunja uso, na akanuna. Kisha akaipa kisogo haki, na akatakabari. Na akasema: Haya si chochote ila ni uchawi ulionukuliwa.” (74:19-24)**

Maana yake: Ananakili na anasimulia, kwa hiyo wakatofautiana kuhusu kauli yake na maoni yake. Allah تعالى: Awaangamize. Allah تعالى Amesema:

لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ

***“Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kujua.”***

Maana yake: Tulikadiria kuwa waseme hivi ili wapate kubeba mizigo yao na sehemu ya mizigo ya ambao wanawafuata na wanawaafiki. Yaani: Watachukua dhambi za kupotea kwao wenyewe na dhambi za kuwapoteza wengine pamoja na dhambi za hao wanaowafuata wao. Kama ilivyokuja katika Hadithi:

«مَنْ دَعَا إِلَى هُدًى كَانَ لَهُ مِنَ الْأَجْرِ مِثْلُ أُجُورِ مَنْ اتَّبَعَهُ، لَا يَنْقُصُ ذَلِكَ مِنْ أُجُورِهِمْ شَيْئًا، وَمَنْ دَعَا إِلَى ضَلَالَةٍ كَانَ عَلَيْهِ مِنَ الْإِثْمِ مِثْلُ آثَامِ مَنْ اتَّبَعَهُ، لَا يَنْقُصُ ذَلِكَ مِنْ آثَامِهِمْ شَيْئًا»

*“Mwenye kuitia kwenye muongozo atapata malipo kama malipo ya wenye kumfuata, na hilo halipunguzi kitu katika malipo ya wenye kufuata; na mwenye kuitia kwenye upotevu atapata dhambi kama wanayoipata wenye kufuata na kupata kwake hakupunguzi kitu katika dhambi za wanaofuata.”<sup>1</sup> Na Amesema تعالى:*

وَلِيَحْمِلُوا أَثْقَاهُمْ وَأَثْقَالًا مَعَ أَثْقَالِهِمْ وَلَيَسَّعُنَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَمَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿١٧﴾

***“Na hapana shaka wataibeba mizigo yao na mizigo mingine pamoja na mizigo yao. Na kwa yakini wataulizwa Siku ya Kiyama juu ya waliyokuwa wakiyazua.” (29:13).***

Mujahid amesema:

لِيَحْمِلُوا أَوْزَارَهُمْ كَامِلَةً يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَمِنْ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ

***“Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanaowapoteza bila ya kujua...”***

Kama hivi amepokea Awfy toka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika aya hii: Na kuwa hio ni kama Kauli Yake:

<sup>1</sup> Muslim 4:2060.

وَلِيَحْمِلُوا أُنْقَاهُمْ وَأُنْقَالًا مَّعَ أُنْقَاهِمُ<sup>ط</sup>

“...ili wabebe mizigo yao na mizigo ya waliowatii wao...” (29:13)<sup>1</sup>

Mujahidi amesema: wanabeba mizigo yao, dhambi zao na dhambi za walio watii, wala wale waliowatii hawapunguziwi katika adhabu yao chochote,<sup>2</sup>

قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَأَتَى اللَّهَ بُنْيَانُهُمْ مِنَ الْقَوَاعِدِ فَحَرَّ عَلَيْهِمُ السَّقْفُ  
مِنْ فَوْقِهِمْ وَأَتَاهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٦﴾ ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يُخْزِبُهُمْ وَيَقُولُ  
اَيْنَ شُرَكَآئِكُمُ الَّذِينَ كُنْتُمْ تُشْتَقُونَ فِيهِمْ ؕ قَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ إِنَّ الْخِزْيَ  
الْيَوْمَ وَالسُّوءَ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٦٧﴾

**26. Walipanga vitimbi waliokuwa kabla yao, Mwenyezi Mungu Akayasukua majengo yao kwenye misingi, dari zikawaporomokea juu yao, na adhabu ikawajia kutoka wasipokujua.**

**27. Kisha Siku ya Kiyama Atawahizi na Atasema: Wako wapi hao washirika Wangu ambao kwao mkiwakutisha (Manabii) mashaka? Watasema waliopewa ilimu: Hakika leo ndiyo hizaya na adhabu itawashukia makafiri.**

### Majadiliano ya Walichokifanya Waliotangulia na Walichofanyiwa

Amesema Al-Aufi, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika Kauli Yake:

قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

“Walipanga vitimbi waliokuwa kabla yao.”

Akasema: Huyu ni Namrud ambaye alijenga ngome.<sup>3</sup> Na wengine wamesema ni Bakh'tanaswar. Na sahihi ni kuwa: hii ni katika mlango wa kupiga mfano kwa ajili ya kubatilisha walichokifanya hawa waliompinga Allah تعالى na wakamshirikisha na mwingine katika ibada Yake. Kama alivyosema Nuhu عليه السلام:

وَمَكْرُوا مَكْرًا كُبَارًا ﴿٦٦﴾

“Na wakapanga vitimbi vikubwa.” (71:22)

<sup>1</sup> At-Tabari 17:191.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:192.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:193.

Maana yake: Wamefanya kila hila katika kuwapoteza watu na wamewavutia kwenye ushirikina wao kwa kila njia. Kama watavyokuja waambia wafuasi wao Siku ya Kiama:

بَلْ مَكْرُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ إِذْ تَأْمُرُونَنَا أَنْ نَكْفُرَ بِاللَّهِ وَنَجْعَلَ لَهُ أَنْدَادًا

**“Bali ni vitimbi vyenu vya usiku na mchana, mlipokuwa mkituamrisha tumkufuru Mwenyezi Mungu, na tumfanyie washirika.” (34:33)**

فَأْتَى اللَّهَ بُنَيْنُهُمْ مِنَ الْقَوَاعِدِ

**“Mwenyezi Mungu Akayasukua majengo yao kwenye misingi...”**

Maana yake: Aliyang’oa kutoka kwenye misingi yake na Kubatilisha matendo yao. Kama Alivyosema Allah تعالى:

كُلَّمَا أَوْقَدُوا نَارًا لِلْحَرْبِ أَطْفَأَهَا اللَّهُ

**“Kila Mara Wanapowasha Moto wa Vita Mwenyezi Mungu Anauzima.” (5:64). Na Kauli Yake:**

فَأْتَنَّهُمُ اللَّهُ مِنْ حَيْثُ لَمْ يَحْتَسِبُوا وَقَذَفَ فِي قُلُوبِهِمُ الرُّعْبَ يُخْرِبُونَ بُيُوتَهُمْ بِأَيْدِيهِمْ وَأَيْدِي الْمُؤْمِنِينَ فَاعْتَبِرُوا يَا أُولِيَ الْأَبْصَارِ

**“Lakini Mwenyezi Mungu Aliwajia kwa mahali wasipopatazamia na Akatia woga katika nyoyo zao (wasiweze kupigana na Waislamu walipokuja kupigana nao). Wakawa wanazivunja nyumba zao kwa mikono yao na kwa mikono ya Waislamu basi Enyi wenye macho (maoni)! Zingatieni.” (59:2)**

Na Allah تعالى hapa Akasema:

قَدْ مَكَرَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ فَأَتَى اللَّهَ بُنَيْنُهُمْ مِنَ الْقَوَاعِدِ فَحَرَّ عَلَيْهِمُ  
السَّقْفُ مِنْ فَوْقِهِمْ وَأَتَنَّهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٤﴾ ثُمَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ يُخْزِبُهُمْ

**“Walipanga vitimbi waliokuwa kabla yao, Mwenyezi Mungu Akayasukua majengo yao kwenye misingi, dari zikawaporomokea juu yao, na adhabu ikawajia kutoka wasipokujua. Kisha Siku ya Kiyama Atawahizi.”**

Maana yake: Atazionesha fedheha zao na kilichokuwa kinafichwa na dhamira zao Atakiweka hadharani. Kama Alivyosema Allah تعالى،

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿٩﴾

**“Siku zitakapodhihirishwa siri.” (86:9)**

Maana: Zitadhihirishwa na kufahamishwa, kama ilivyonukuliwa katika Bukhari na Muslim kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ amesema.

يُنْصَبُ لِكُلِّ عَادِرٍ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ عِنْدَ اسْتِئْذَانِ عَدْرَتِهِ، قِيَالُ: هَذِهِ عَدْرَةُ فُلَانِ  
ابْنِ فُلَانٍ

*“Kila mfanya khiyana atasimamishiwa bendera Siku ya Kiama kwenye matako yake kwa kadiri ya khiyana yake, na itaelezwa: kuwa hii ni khiyana ya fulani Ibn fulani”.*<sup>1</sup>

Kama hivi zitawabainikia watu zile hila walizokuwa wanazificha, na Allah تعالى Atawafedhehesha hadharani, na Atawaambia kwa Kuwakemea na Kuwafedhehesha:

أَيْنَ شُرَكَاءِكَ الَّذِينَ كُنْتُمْ تُشْتَقُونَ فِيهِمْ

**“Wako wapi hao washirika wangu ambao kwao mkiwakutisha (Manabii) mashaka?”**

Maana: Mkipigana na mkiyombana kwa ajili yao, wako wapi hao wawasaidie na wawakombowe hapa?

هَلْ يَنْصُرُونَكُمْ أَوْ يَنْتَصِرُونَ

**“Badala ya Mwenyezi Mungu? Je! Wanakusaidieni, au wanajisaidia wenyewe?” (26:93)**

فَمَا لَهُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَلَا نَاصِرٍ ﴿١٠﴾

**“Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi.” (86:10)**

Na hoja inapoelekezwa kwao na dalili kwao zikasimama na juu yao tamko likathibitika, na wakashindwa kujitetea wakati hakuna kukimbia,

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 10:578, Muslim 3:1360.





وَاللَّهُ رَبَّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ

**"Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina." (6:23)**

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ كَمَا سَحَلِفُونَ لَكُمْ<sup>ط</sup>

**"...Siku atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuwapie kama wanavyo kuwapieni nyinyi." (58:18)**

Allah تعالی Akasema kwa Kuwakadhibisha katika kauli yao:

بَلَىٰ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٦﴾ فَادْخُلُوا أَبْوَابَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا فَلَبِئْسَ

مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٣٧﴾

**"Kwani! Hakika Mwenyezi Mungu Anajua sana mliyokuwa mkiyatenda, Basi ingieni milango ya Jahannamu, humo mdumu. Ni maovu mno makaazi ya wafanyao kiburi!"**

Maana yake: Ubaya wa mapumziko. Makazi na mahala ni nyumba hiyo ya udhalili kwa mwenye kuzifanyia kiburi Aya za Allah تعالی na kukataa kuwafuata Mitume wake, na hao wataingia Jahannamu tokea siku ya kufa kwao wao pamoja na roho zao. Na miili yao ikiwa ndani ya makaburi yake itapata joto na upepo wa moto samuumi wa Jahannamu na inapofika siku ya Kiyama roho zao zitaingia katika miili yake na kubaki katika moto wa Jahannamu milele,

لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فِيمَوتُوا وَلَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِنْ عَذَابِهَا

**"...hawahukumiwi wakafa, wala hawatapunguziwa adhabu yake." (35:36)**

Kama Alivyosema Allah تعالی:

النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا<sup>ط</sup> وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ

الْعَذَابِ ﴿٤٦﴾

**"Wanaoneshwa Moto asubuhi na jioni. Na itapofika Saa ya Kiyama patasemwa: Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali kabisa!" (40:46)**

\* وَقِيلَ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا مَاذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ <sup>٤</sup> قَالُوا خَيْرًا <sup>٥</sup>  
 لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ <sup>٦</sup> وَلَدَارُ الْآخِرَةِ  
 خَيْرٌ <sup>٧</sup> وَلَنِعَمَ دَارَ الْمُتَّقِينَ <sup>٨</sup> جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا  
 يُجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ <sup>٩</sup> لَهُمْ فِيهَا مَا يَشَاءُونَ <sup>١٠</sup> كَذَلِكَ  
 يُجْزَى اللَّهُ الْمُتَّقِينَ <sup>١١</sup> الَّذِينَ تَتَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ  
 طَيِّبِينَ <sup>١٢</sup> يَقُولُونَ سَلِّمْ عَلَيْنَا أَدْخُلُوا الْجَنَّةَ بِمَا كُنْتُمْ  
 تَعْمَلُونَ <sup>١٣</sup> هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ  
 يَأْتِي أَمْرٌ رَبِّكَ <sup>١٤</sup> كَذَلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ <sup>١٥</sup> وَمَا ظَلَمَهُمُ  
 اللَّهُ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ <sup>١٦</sup> فَأَصَابَهُمْ  
 سَيِّئَاتٌ مَا عَمِلُوا وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِمِيسِرٍ فِيهَا <sup>١٧</sup>  
 وَقَالَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا عَبَدْنَا مِنْ  
 دُونِهِ مِنْ شَيْءٍ نَحْنُ وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِنْ دُونِهِ  
 مِنْ شَيْءٍ <sup>١٨</sup> كَذَلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ <sup>١٩</sup> فَهَلْ عَلَى  
 الرُّسُلِ إِلَّا الْبَلَاغُ الْمُبِينُ <sup>٢٠</sup> وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ  
 رُسُلًا أَنْ أَعْبُدُوا اللَّهَ وَأَجْتَنِبُوا الصُّلُوعَ <sup>٢١</sup> فَمِنْهُمْ مَنْ  
 هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَنْ حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ <sup>٢٢</sup> فَسِيرُوا فِي  
 الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكذِبِينَ <sup>٢٣</sup>  
 إِنْ تَحَرَّصَ عَلَى هُدَاهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ يُضِلُّ <sup>٢٤</sup> وَمَا  
 لَهُمْ مِنْ ناصِرِينَ <sup>٢٥</sup>

\* وَقِيلَ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا مَاذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ <sup>٤</sup>  
 قَالُوا خَيْرًا <sup>٥</sup> لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي  
 هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ <sup>٦</sup> وَلَدَارُ الْآخِرَةِ  
 خَيْرٌ <sup>٧</sup> وَلَنِعَمَ دَارَ الْمُتَّقِينَ <sup>٨</sup>  
 جَنَّاتُ عَدْنٍ يَدْخُلُونَهَا يُجْرَى مِنْ  
 تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ <sup>٩</sup> لَهُمْ فِيهَا مَا يَشَاءُونَ <sup>١٠</sup>  
 كَذَلِكَ يُجْزَى اللَّهُ الْمُتَّقِينَ <sup>١١</sup>  
 الَّذِينَ تَتَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ طَيِّبِينَ <sup>١٢</sup>  
 يَقُولُونَ سَلِّمْ عَلَيْنَا أَدْخُلُوا  
 الْجَنَّةَ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ <sup>١٣</sup>

30. Na wataambiwa waliomcha Mungu: Mola wenu Mlezi kateremsha nini? Watasema: Kheri. Waliofanya wema katika dunia hii watapata wema. Na nyumba ya Akhera ni bora zaidi, na njema mno nyumba ya wachamungu.

31. Bustani za milele wataziingia; iwe inapita kati yake mito. Humo watapata watakacho. Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Awali-pavyo wenye kumcha.

**32. Wale ambao Malaika Huwafisha katika hali njema, wanawaambia: Amani iwe juu yenu! Ingeni Peponi kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyatenda.**

**Kauli ya Wachamungu Kuhusu Wahyi, Malipo Yao na Hali Zao Wakati wa Kufa na Baada Yake**

Hii ni taarifa ya watu wema, tofauti na Aliyoyaeleza Allah تعالى kwa watu waovu, kwani hao walipoelezwa,

مَاذَا أَنْزَلَ رَبُّكُمْ

**“Mola wenu Mlezi kateremsha nini?”**

Wakasema wakiwa wamelipuuza jibu: Hakuteremsha kitu bali hizi ni hadithi za watu wa kale, wachamungu hawa wamesema: Ametuteremshia kheri. Maana: Rehema na Baraka kwa mwenye kumfuata na akamuamini. Kisha akakieleza kile Allah تعالى Alichowaahidi katika Alichokiteremsha juu ya Mitume Wake Akasema:

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةٌ

**“Waliofanya wema katika dunia hii watapata wema.”**

Sawa na Kauli Yake Allah تعالى:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهٗ حَيٰوةً طَيِّبَةً ۖ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧٧﴾

**“Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, Tutamhuisha maisha mema; na Tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyokuwa wakiyatenda.” (16:97).**

Maana: Atakayefanya mema duniani, basi Allah تعالى Atampa mema duniani na akhera. Kisha Akaeleza kuwa nyumba ya akhera ni bora kuliko maisha ya duniani na malipo ya akhera ndiyo kamili kuliko ya duniani. Kama Alivyosema:

وَقَالَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ وَيَلَكُمْ ثَوَابُ اللَّهِ خَيْرٌ

**“Na wakasema wale waliopewa ilimu: Ole wenu! Malipo ya Mwenyezi Mungu ni bora...” (28:80)**

Na Amesema تعالى:

وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ لِلْأَبْرَارِ

**“Na vilioko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.”**

**(3:198) Na,**

وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ وَأَبْقَى ﴿١٦﴾

**“Na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.” (87:17)**

Na Akamuambia Mtume wake ﷺ,

وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ الْأُولَى ﴿١٧﴾

**“Na bila ya shaka wakati ujao utakuwa bora kwako kuliko uliotangulia.” (93:4)**

Kisha, Akaijeleza nyumba ya akhera. Akasema:

وَلْيَعْمَ دَارُ الْمُتَّقِينَ

**“...Na nyumba ya Akhera ni bora zaidi.”**

Na Kauli Yake:

جَنَّتُ عَدْنٍ

**“...Pepo za milele...”**

Mbadala wa nyumba ya wachamungu. Maana: Akhera wana bustani za milele.

Maana yake: Za kudumu wataziingia,

تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ﴿١٨﴾

**“...ziwe zinapita kati yake mito...”** Maana yake: Kati ya miti yake na maghorofa yake,

هُمْ فِيهَا مَا يَشَاءُونَ ﴿١٩﴾

**“...Humo watapata watakacho...”** Sawa na Kauli Yake:

وَفِيهَا مَا تَشْتَهِيهِ الْأَنْفُسُ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ ﴿٢٠﴾ وَأَنْتُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢١﴾

**“...na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanavifurahia, na nyinyi mtakaa humo milele.”**

كَذَلِكَ يَجْزِي اللَّهُ الْمُتَّقِينَ

**“Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Awalipavyo wenye kumcha.”**

Maana yake: Hivi ndivyo Allah تعالى Anavyomlipa kila anayemuamini na akamcha na akayafanya matendo mazuri. Kisha Allah تعالى Akaiieleza hali yao wakati wa kufikwa na kifo kuwa ni wazuri: Yaani, hawana ushirikina, uchafu, na kila ovu wamesalimika nalo, na kwamba malaika wanawasalimia na kuwabashiria pepo.

Sawa na Kauli Yake تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا  
وَأَبْشُرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾ نَحْنُ أَوْلِيَاؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ  
وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَشْتَهَى أَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ﴿٣١﴾ نُزُلًا مِّنْ غَفُورٍ رَّحِيمٍ ﴿٣٢﴾

**“Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinachotamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka. Ni takrima itokayo kwa Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu.” (41:30-32)**

Na tulishazitanguliza Hadithi zilizokuja katika kupokelewa roho za waumini na roho za makafiri tulipoifasiri Kauli Yake,

يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ وَيُضِلُّ اللَّهُ  
الظَّالِمِينَ ۗ وَيَفْعَلُ اللَّهُ مَا يَشَاءُ ﴿١٧﴾

**“Mwenyezi Mungu Huwatia uimara wenye kuamini kwa kauli imara katika maisha ya dunia na katika Akhera. Na Mwenyezi Mungu Huwaacha kupotea hao wenye kudhulumu. Na Mwenyezi Mungu Hufanya Apendavyo.” (14:27)**

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمُ الْمَلَائِكَةُ أَوْ يَأْتِيَ أَمْرٌ رَبِّكَ ۚ كَذَلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ  
 وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٣٣﴾ فَأَصَابَهُمْ سَيِّئَاتُ مَا عَمِلُوا  
 وَحَاقَ بِهِمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٣٤﴾

**33. Wanangojea jengine hawa ila Malaika wawafikie, au iwafikie Amri ya Mola wako Mlezi? Na kama hivi wamefanya ambao waliokuwa kabla yao. Na Mwenyezi Mungu Hakuwadhulumu, lakini walijidhulumu wenyewe.**

**34. Basi ukawafikia uovu wa waliyoyatenda, na waliyokuwa wakiyakejeli yakawazunguka."**

### Maana ya Makafiri Kuchelewa Kuamini Ili Wangojee Adhabu

Allah تعالیٰ Anasema Akiwakemea washirikina kuendelea kwao katika batili na kuhadaika kwao na dunia. Hivi kuna wanachokisubiri hawa kisichokuwa malaika kuwajia ili kuchukua roho zao?. Hayo ameyaeleza Qatada.<sup>1</sup>

أَوْ يَأْتِيَ أَمْرٌ رَبِّكَ ۚ

**"...au iwafikie amri ya Mola wako Mlezi?..."**

Maana yake: Siku ya Kiama na misukosuko wanayoiona. Na Kauli Yake:

كَذَلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ

**"Na kama hivi wamefanya ambao waliokuwa kabla yao."**

Maana yake: Walizidi katika ushirikina watangulizi wao na mfano wao miongoni mwa washirikina, mpaka wakaonja adhabu ya Allah تعالیٰ, na kikawafika hicho walicho nacho. Maana: Adhabu na mateso.

وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ

**"...Na Mwenyezi Mungu Hakuwadhulumu..."**

Kwa sababu Allah تعالیٰ tayari Amewahadharisha na Amewasimamishia hoja kwa Kuwaleta Mitume Wake na Kuteremsha Vitabu Vyake,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:199.

وَلَيْكِن كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ

*"Lakini walijidhulumu wenyewe."*

Kwa kuwakhaliifu Mitume na kupinga waliyoyaleta, na kwa sababu hii adhabu ya Allah تعالى iliwapata kwa hilo,

وَحَاقَ بِهِم

*"...na yakawazunguka..."*

Maana yake: Adhabu kali ikawazunguka,

مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ

*"...waliyokuwa wakiyakejeli..."*

Wakiwafanyia mzaha Mitume wanapowaahidi adhabu ya Allah تعالى, na kwa sababu hii wataambiwa siku ya Kiama,

هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿١٤﴾

*"(Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha!" (52:14)*

وَقَالَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا عَبَدْنَا مِن دُونِهِ مِن شَيْءٍ نَّحْنُ وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِن دُونِهِ مِن شَيْءٍ كَذَلِكَ فَعَلَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَهَلْ عَلَى الرَّسُولِ إِلَّا أَلْبَلَاغُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾ وَلَقَدْ بَعَدْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ فَمِنْتُم مَّن هَدَى اللَّهُ وَمِنْتُم مَّن حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكْذِبِينَ ﴿١٦﴾ إِنَّ تَحْرِيصَ عَلَيَّ هَدَيْتُهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَن يُضِلُّ وَمَا لَهُم مِّن نَّاصِرِينَ ﴿١٧﴾

**35. Na washirikina wanasema: Mwenyezi Mungu Angelitaka tusingeliabudu chochote badala Yake, sisi wala baba zetu, wala tusingeliharimisha chochote bila ya Yeye. Kama hivyo walifanya waliokuwa kabla yao. Basi lipo lolote juu ya Mitume isipokuwa kubalighisha kwa uwazi?"**

**36. Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na Muepukeni Shetani. Basi kati yao wapo Aliowaongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao uliowathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanaokanusha.**

**37. Hata ukiwa na pupa ya kutaka kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Hamuongoi yule anayeshikilia kupotea. Wala hawatapata wa kuwanusuru.”**

### **Hoja ya Washirikina Juu ya Ushirikina Wao Kuwa Unatokana na Kudura na Jibu la Hoja Yao Hiyo**

Allah تعالی Anaelezea kuhusu washirikina kuhadaika na vitendo vyao vya ushirikina na kutoa kwao udhuru juu ya hilo. Huku wakitoa hoja ya kuwa wasingefanya hivyo, ila ni kudura ya Allah تعالی. Wanasema:

لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا عَبَدْنَا مِنْ دُونِهِ مِنْ شَيْءٍ نَحْنُ وَلَا آبَاؤُنَا وَلَا حَرَمْنَا مِنْ  
دُونِهِ مِنْ شَيْءٍ<sup>ع</sup>

**“Mwenyezi Mungu Angelitaka tusingeliabudu chochote badala Yake, sisi wala baba zetu, wala tusingeliharamisha chochote bila ya Yeye.”**

Maana yake: Kama vile *Baha-ir*,<sup>1</sup> *Sawa-ib*, *Waswa-i*, na vingine walivyovibuni na kuvizua wao wenyewe, ambavyo Allah تعالی Hakuviletea hoja. Na madhumuni ya maneno yao ni kuwa kama Allah تعالی Asingependa basi tusingefanya. Angetukataza kwa mateso, wala Asingalituwezesha hilo. Allah تعالی Akawajibu kutatanisha kwao:

فَهَلْ عَلَى الرُّسُلِ إِلَّا الْبَلَاغُ

**“Basi lipo lolote juu ya Mitume isipokuwa kubalighisha kwa uwazi?”**

Maana yake: Si kama mnavyodai kuwa Allah تعالی Hakuwakataza, bali Amewakataza katazo kali mno, na Akapeleka Mtume katika kila umma wa

<sup>1</sup> Angalia: Tafsiri ya *Surat Yunus* na. 59-60.



kila karne na kila taifa la watu, na wote walitoa wito wa kumuabudu Allah تعالى na walikataza kumuabudu asiyekuwa Yeye.

أَبِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ<sup>ط</sup>

***“Mumuabudu Mwenyezi Mungu na muepukeni Shetani.”***

Allah تعالى Hakuacha Kupeleka Mitume kwa watu kwa madhumuni hayo tokea ushirikina ulipoanza, kwa Wanadamu. Katika watu wa Nuhu عليه السلام ambao Allah تعالى Amewapelekea Nuh عليه السلام, na akawa ndiye wa kwanza katika Mitume Aliyepolekwa na Allah تعالى kwa watu wa Ardhini, mpaka Akawakhitimisha na Muhammad ﷺ, ambaye wito wake ulifungwa kwa wote wanadamu na majini, Mashariki na Magharibi. Na wote hao kama Alivyosema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

***“Na Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mola isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu...”***  
(21:25)

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَسْأَلَنَّ مَنْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ إِلَهًا يُعْبَدُونَ ﴿٤٥﴾

***“Na waulize Mitume wetu Tuliowatuma kabla yako: Je! Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Rah’mani?”*** (43:45)

Na Allah تعالى katika Aya hii Tukufu Amesema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ<sup>ط</sup>

***“...na bila shaka Tulipeleka Mtume katika kila umma ya kwamba muabuduni Mwenyezi Mungu na muepukeni ibilisi...”***

Vipi tena iwe halali kwa mshirikina yeyote baada ya haya aseme:

لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا عَبَدْنَا مِنْ دُونِهِ مِنْ شَيْءٍ

***“Kama Angalipenda Mwenyezi Mungu tusingaliabudu chochote badala Yake.”***

Kwa hiyo Utakaji wa Allah تعالى ni wa kisheria, Ameshawakataza kupitia ndimi za Mitume Wake, ama Kutaka Kwake kimaumbile nako ni kule Kuwawezesha kwao kufanya hivyo, hakuna hoja kwao. Kwani Allah تعالى Ameumba moto na watu wake miongoni mwa shetani na makafiri. Naye Haridhii ukafiri kwa waja Wake, na Allah تعالى katika hilo Ana Hoja kubwa na Hekima yenye nguvu. Kisha Allah تعالى Akaeleza kuwa Amewakemea kwa Kuwaletea adhabu baada ya hadharisho la Mitume Wake. Na kwa sababu hii Akasema:

فَمِنْهُمْ مَنْ هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَنْ حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ ۚ فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا  
كَيْفَ كَانَ عِقَابُ الْمُكذِّبِينَ ۚ

**“Basi kati yao wapo Aliowaongoa Mwenyezi Mungu. Na kati yao wapo ambao uliowathibitikia upotovu. Basi tembeeni katika ardhi, muangalie ulikuwaje mwisho wa wanaokanusha.”**

Maana yake: Ulizeni hatima ya wale walioenda kinyume na Mitume na wakapinga haki, namna gani Allah تعالى Alivyowafanya,

دَمَّرَ اللَّهُ عَلَيْهِمُ ۖ وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَلُهَا ﴿١٠﴾

**“...Mwenyezi Mungu Aliwaangamiza, na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo.” (47:10)**

Akasema:

وَلَقَدْ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ فَكَيفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿١٨﴾

**“...Na bila ya shaka walikwishakanusha waliokuwa kabla yao; basi kulikuwaje Kukasirika Kwangu?” (67:18)**

Kisha Allah تعالى Akamueleza Mtume wake ﷺ kuwa pupa yake ya kutaka awaongoe haitawafaa kama Allah تعالى Ametaka Kuwapoteza.

Sawa na Kauli Yake,

وَمَن يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَن تَمْلِكَ لَهُ مِن آلِهِ شَيْئًا ۗ

**“Na mtu ambaye Mwenyezi Mungu Anataka kumfitini huwezi kuwa na madaraka naye mbele ya Mwenyezi Mungu.” (5:41)**

Na Nuhu عليه السلام aliwaambia watu wake:

وَلَا يَنْفَعُكُمْ نُصْحِي إِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ أَنْصَحَ لَكُمْ إِنْ كَانَ اللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يُغْوِيَكُمْ

**“Wala nasaha yangu haikufaeni kitu nikitaka kukunasihini, ikiwa Mwenyezi Mungu Anataka Kukuachieni mptotee.” (11:34)**

Na katika Aya hii Tukufu Akasema,

إِنْ تَحَرَّصَ عَلَىٰ هُدًىٰ لَهُمُ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ يُضِلُّ

**“Ukiwa na hima kubwa ya kutaka kuwaongoza, lakini Mwenyezi Mungu Hamuongozi yule anaewapoteza wengine.”**

Kama Alivyosema Allah تعالى،

مَنْ يُضِلِّ اللَّهُ فَلَا هَادِيَ لَهُ وَيَذَرُهُمْ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٨٦﴾

**“Aliyemuacha Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumuongoa. Atawaacha hao wakitangatanga katika upotofu wao.” (7:186)**

Kama Alivyosema Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠٦﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿١٠٧﴾

**“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa itawajia kila Ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.” (10:96-97)**

فَإِنَّ اللَّهَ

**“...lakini Mwenyezi Mungu...”**

Maana yake: Shani na Amri Yake, Anachotaka kina kuwa na Asichokitaka hakiwi, na kwa sababu hii Akasema:

لَا يَهْدِي مَنْ يُضِلُّ

**“lakini Mwenyezi Mungu Hamuongoi yule anayeshikilia kupotea.”**

Maana: Aliyempoteza, nani ambaye atamuongoza baada ya Allah تعالى? Maana: Hakuna,

وَمَا لَهُمْ مِّنْ نَّاصِرِينَ

**“...Wala hawatapata wa kuwanusuru...”**

Maana yake: Watakaowaokoa kutoka kwenye adhabu, na kifungo chake,

أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴿٥٤﴾

**“...Fahamuni! Kuumba na Amri ni Zake. Ametukuka kabisa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote.” (7:54)**

\* \* \*

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ ۗ لَا يَبْعَثُ اللَّهُ مَن يَمُوتُ ۚ  
 بَلَىٰ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ۚ  
 ۞ لِيُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي سُخِّتُوا فِيهِ وَيَعْلَمَ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا أَنَّهُمْ كَانُوا كَذِبِينَ ۞ إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا  
 أَرَدْنَاهُ أَن نَّقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ۞ وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي  
 اللَّهِ مِن بَعْدِ مَا ظَلَمُوا لَنُبَوِّئَنَّهُمْ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَلَا جُزْ  
 ۞ الْأَخْرَةَ أَكْبَرَ ۚ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ۞ الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ  
 رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ۞ وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا  
 نُّوحِي إِلَيْهِمْ ۚ فَسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِن كُنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ۞  
 بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ ۗ وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا  
 نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ۞ أَفَأَمِنَ الَّذِينَ مَكَرُوا  
 السَّيِّئَاتِ أَن يَخْسِفَ اللَّهُ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ  
 مِن حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ۞ أَوْ يَأْخُذَهُمْ فِي تَقْلِبِهِمْ فَمَا  
 هُمْ بِمُعْجِزِينَ ۞ أَوْ يَأْخُذَهُمْ عَلَى تَخَوُّفٍ فَإِنَّ رَبَّكُمْ  
 لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ۞ أَوْلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ  
 يَتَفَيَّؤُوا ظِلَالُهُ عَنِ الْيَمِينِ وَالشَّمَائِلِ سُجَّدًا لِلَّهِ وَهُمْ  
 دَاخِرُونَ ۞ ۞ وَاللَّهُ يَسْجُدُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي  
 الْأَرْضِ مِن دَابَّةٍ وَالْمَلَائِكَةُ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ۞  
 ۞ خَافُونَ رَبَّهُمْ مِّنْ قُدْرَتِهِمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ۞

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ ۗ لَا  
 يَبْعَثُ اللَّهُ مَن يَمُوتُ ۚ بَلَىٰ وَعْدًا  
 عَلَيْهِ حَقًّا وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا  
 يَعْلَمُونَ ۚ لِيُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي  
 سُخِّتُوا فِيهِ وَيَعْلَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا  
 أَنَّهُمْ كَانُوا كَذِبِينَ ۞ إِنَّمَا  
 قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا أَرَدْنَاهُ أَن نَّقُولَ لَهُ  
 كُنْ فَيَكُونُ ۞

38. Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu ukomo wa viapo vyao kwamba Mwenyezi Mungu Hato-mfufua aliyekufa. Kwani! Ni ahadi iliyo juu Yake kikweli; lakini watu wengi hawajui.

39. Ili Kuwabainishia yale waliyokhitalifiana, na ili wajue waliokufuru kwamba wao walikuwa ni waongo.

40. Kauli Yetu kwa kitu Tunachokitaka kiwe, ni kukiambia: Kuwa! Basi kinakuwa.

## Kufufuliwa Baada ya Kufa ni Kweli, na Ndani Yake Kuna Hekima Nalo ni Jepesi kwa Allah تعالیٰ

Allah تعالیٰ Anasema Akielezea habari za washirikina kuwa wao wamekula kiapo kwa Allah تعالیٰ, nguvu ya kiapo chao. Maana yake: Wamejitahidi katika kuapa na wakavipa uzito viapo kuwa Allah تعالیٰ Hatamfufua anayekufa. Maana: Wakalifanya hilo kuwa liko mbali, na wakawakadhibisha Mitume katika kuwaelezea kwao hilo. Wakala yamini kwa kinyume chake. Allah تعالیٰ Akasema: Akiwakadhibisha wao na Kuwajibu:

بَلَىٰ

**“Kwani!”** Maana yake: Kwanini! Hilo litakuwa.

وَعَدًّا عَلَيْهِ حَقًّا

**“Ni ahadi iliyo juu Yake kikweli.”**

Maana yake: haina budi kuwa,

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

**“Lakini watu wengi hawajui.”**

Maana yake: Kutokana na ujinga wao wanatofautiana na Mitume na wanaingia katika ukafiri. Kisha Allah تعالیٰ Akaeleza Hekima Yake katika Kufufua na Kusimama miili siku ya wito. Akasema:

لِيُبَيِّنَ لَهُمُ

**“Ili kuwabainishia.”** Maana yake: Watu,

الَّذِي يَخْتَلِفُونَ فِيهِ

**“...yale waliyokhitalifiana...”** Maana yake: Katika kila kitu.

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَفُؤْ بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى ﴿٣١﴾

**“Ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, ili Awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema Awalipe mema.” (53:31)**

وَلْيَعْلَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّهُمْ كَانُوا كَذِبِينَ

**“...na ili wajue waliokufuru kwamba wao walikuwa ni waongo.”**

Maana yake: Katika viapo vyao na yamini zao kuwa Allah تعالى Hamfufui anayekufa. Na kwa sababu hii kesho Siku ya Kiama watasukumiwa motoni kwa nguvu. Na mazabania (malaika wa moto) watawaambia:

هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٥٠﴾ أَفَسِحْرٌ هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿٤٩﴾  
أَصْلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ إِنَّمَا تُجْرُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٥١﴾

**“(Waambiwe): Huu ndio ule Moto mlio kuwa mkiukanusha! Je! Huu ni uchawi, au hamuoni tu? Uingieni, mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu. Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda.” (52:14-16)**

Kisha Allah تعالى Akaelezea Uwezo Wake kwa Anachotaka na kwamba Yeye hakuna kinachomshinda ardhini wala mbinguni, na kwa hakika Anachotaka ni kukiambia tu “Kuwa” basi kinakuwa. Na, kufufua ni miongoni mwa hayo Anapotaka iwe Anaiamuru mara moja tu inakuwa, kama Anavyotaka. Sawa na Kauli Yake:

وَمَا أَمْرًا إِلَّا وَاحِدَةً كَلِمَةً بِلَبْسٍ ﴿٥٠﴾

**“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50) Na Kauli Yake,**

مَا خَلَقْنَاكُمْ وَلَا بَعَثْنَاكُمْ إِلَّا كَفْتَسٍ وَاحِدَةً إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٥١﴾

**“Hakukuwa Kuumbwa kwenu, wala Kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.” (31:28)**

Na Amesema katika aya hii Tukufu:

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا أَرَدْنَاهُ أَنْ نَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٥٢﴾

**“Kauli Yetu kwa kitu Tunachokitaka kiwe, ni kukiambia: Kuwa Basi kinakuwa.”**

Maana yake: Ni kukiamuru mara moja tahamaki kimekuwa. Maana yake: Allah تعالى Hana haja ya Kusisitiza kwa Anachokiamuru kwani Yeye تعالى Hazuiwi na wala Hapingwi, kwa sababu Yeye Ndiye Pekee Mwenye Nguvu, Mkubwa Ambaye Utawala Wake ni Wenye Nguvu; na Ushindi Wake Umeshinda kila kitu, hakuna Mola isipokuwa Yeye tu na hakuna Mola asiyekuwa Yeye.

وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي اللَّهِ مِنْ بَعْدِ مَا ظَلَمُوا لَنَبُوْنَهُمْ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۗ وَلَا جُزْءَ الْآخِرَةِ أَكْبَرَ  
لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾ الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٤٢﴾

**41. Na wale waliohama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu baada ya kudhulumiwa, bila ya shaka Tutawaweka duniani kwa wema; na ujira wa Akhera ni mkubwa zaidi; laiti kuwa wanajua!**

**42. Wale wanao subiri na wakamtegemea Mola wao Mlezi.**

### Malipo ya Muhajirina

Allah تعالى Anaelezea malipo Yake kwa muhajirina katika Dini Yake kwa ajili ya kutaka Radhi Yake, ambao wameiacha miji yao, ndugu zao na marafiki zao wakitaraji kupata thawabu na malipo ya Allah تعالى. Yawezekana kuwa sababu ya kuteremka kwake ni wale waliohamia Habasha ambao walizidiwa na manyanyaso ya ndugu zao kwao kule Makkah mpaka wakaondoka ili waweze kumuabudu Mola wao. Na miongoni mwao ni Uthmani bin Affaan رضي الله عنه, akiwa na mkewe Ruqiya رضي الله عنها, binti wa Mtume ﷺ, na Ja'afar Ibn Abi Twaalib رضي الله عنه, mtoto wa ami yake Mtume ﷺ na Abuu Salamah Ibn Abdil-As-wad رضي الله عنه, wakiwa katika kundi linalokaribia watu thamanini, kati ya wanaume na wanawake. Allah تعالى Awaridhie, na Amekwisha lifanya hilo, Allah تعالى Amewaahidi malipo mazuri duniani na akhera. Akasema:

لَنَبُوْنَهُمْ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۗ

**“...bila shaka Tutawakalisha katika dunia kwa wema...”**

Ibni Abbas, Ash-Sshaabi na Qatadah رضي الله عنهم wamesema: Ni Madina<sup>1</sup>. Na imesemwa maana yake: Ni rizki nzuri. Ameyasema Mujaahid<sup>2</sup>. Na hakuna tofauti

<sup>1</sup> At-Tabari 17:205, 206.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:206.



kati ya kauli mbili hizi, bila shaka hao wameacha nyumba zao na mali zao. Allah تعالی Akawapa badala bora kuliko walivyoviacha duniani, kwani mwenye kuacha kitu kwa ajili ya Allah تعالی, Allah تعالی Atambadilishia kilicho bora zaidi kwake kuliko hicho. Na ndivyo ilivyotokea kwa sababu wao Allah تعالی Amewawezesha katika nchi na Akawafanya ni watawala kwa watu, wakawa viongozi, mahakimu na kila mmoja wao ni kiongozi kwa wacha-Mungu. Na Akaeleza kuwa thawabu Zake kwa Muhaajirina akhera ni kubwa zaidi kuliko Aliyowapa duniani. Akasema:

وَلَا جُزْءَ الْآخِرَةِ أَكْبَرُ

**“...na ujira wa Akhera ni mkubwa zaidi...”**

Maana: Kuliko ule Tuliowapa duniani.

لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ

**“...laiti kuwa wanajua!...”**

Maana yake: Laiti wale walioacha kuhama pamoja nao wangajua Alichoweka Allah تعالی, kwa ajili ya wenye kumtii na kumfuata Mtume Wake.

Kisha Allah تعالی Akawasifu Akasema:

الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٤٤﴾

**“...Wale wanaosubiri na wakamtegemea Mola wao Mlezi.”**

Maana yake: Wamevumilia kero za watu wao, wakiwa wamemtegemea Allah تعالی Ambaye Aliyewatengenezea hatima nzuri duniani na akhera.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ فَسَلُّوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ ۗ وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ

يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٥﴾

**43. Nasi Hatukuwatuma kabla yako ila watu wanaume Tuliowapa Wahyi (Ufunuo). Basi waulizeni wenye ukumbusho kama nyinyi hamjui.**

**44. Kwa Ishara wazi na Vitabu. Nasi Tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao, wapate kufikiri.**

### Hakupelekwa Mtume Yeyote Isipokuwa ni Miongoni mwa Wanadamu

Dhahaak amesema kutokana na Ibn Abbas رضي الله عنهما: Allah تعالى Alipomtuma Muhammad ﷺ kuwa Mtume Waarabu au baadhi yao miongoni mwao walimpinga na wakasema: "Allah تعالى ni Mtukufu zaidi haiwezekani kumtuma mwanadamu kuwa Mtume." Kisha Allah تعالى Akateremsha:

أَكَا نَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَى رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ

**"Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba Tumemfunulia mmoja wao kuwa: Waonye watu..." (10:2)**

Na Akasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ فَسَلُّوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْمُونَ ﴿١٠﴾

**"Nasi Hatukuwatuma kabla yako ila watu wanaume Tuliowapa Wahyi (Ufunuo). Basi waulizeni wenye ukumbusho kama nyinyi hamjui."**

Maana yake: *Ahlul kitaab*, waliopita. Je Mitume waliopelekwa kwao walikuwa wanadamu au malaika? Kama walikuwa malaika basi mtawakataa na kama walikuwa wanadamu basi msipinge Muhammad ﷺ kuwa Mtume. Allah تعالى Amesema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ ۗ

**"Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipo kuwa wanaume Tulio wafunulia wahyi miongoni mwa watu wa mijini..." (12:109)**

Hawakuwa wa mbinguni kama mlivyosema<sup>1</sup>. Hivyo hivyo imepokewa kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa: Madhumuni ya *Ahli Dhikri* ni Ahli kitabu<sup>2</sup>. Na kusudio ni: Ni kwamba aya hii Tukufu imeelezea kuwa

<sup>1</sup> At-Tabari 17:208.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:208.

Mitume wote waliotangulia kabla ya Muhammad ﷺ walikuwa binadamu, kama alivyo yeye Muhammad ﷺ. Na hilo ni sawa na Alivyosema Allah تعالى:

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا ﴿٩٣﴾ وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمْ  
الْهُدَىٰ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَبَعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَسُولًا ﴿٩٤﴾

**“Sema: Subhana Rabbi, Ametakasika Mola wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani isipokuwa ni mwanaadamu na Mtume? Na nini kilichowazuilia watu kuamini ulipowajia uwongofu isipokuwa walisema: Je! Mwenyezi Mungu Humtuma mwanaadamu kuwa ni Mtume?” (17:93-94)**

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ ﴿٢٠﴾  
**“Na Hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakenda masokoni...” (25:20)**

وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوا خَالِدِينَ ﴿٨﴾

**“Wala Hatukuwafanya miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele.” (21:8),**

Na Akasema:

قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَاٍ مِنَ الرُّسُلِ

**“Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume.” (46:9)**

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ

**“Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi.” (18:110)**

Kisha Allah تعالى Akamuelekeza mwenye shaka kuwa Mitume walikuwa wanadamu, waulize wenye vitabu vilivyotangulia kuhusu Mitume ambao wamepita, je Mitume wao walikuwa wanadamu au malaika?

Kisha Allah تعالى Akaeleza kuwa Yeye Amewapeleka,

بِالْبَيِّنَاتِ

“...kwa ubainifu...”

Maana yake: Kwa hoja na dalili na,

وَالزُّبُرِ

“Zaburi”.

Navyo ni vitabu, hayo ameyasema Ibn Abbas, Mujahid, Dhahaak na wengine <sup>1</sup> رضي الله عنهم. Na Amesema:

وَكُلُّ شَيْءٍ فَعَلُوهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٢﴾

“Na kila jambo walilolifanya limo vitabuni.” (54:52)

Na Amesema:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزُّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿١٠٥﴾

“Na hakika Tulikwishaandika katika Zaburi<sup>2</sup> baada ya Kumbukumbu,<sup>3</sup> ya kwamba nchi watairithi waja Wangu waliowema.” (21:105)

Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ

“...Na Tumekuteremshia mawaidha.”

Maana yake: Qur’ani,

لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ

“...ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao...”

<sup>1</sup> At-Tabari 17:211

<sup>2</sup> Maana ya hapa inajumuisha Vitabu Vitakatifu - Taurati, Injili na Zaburi, Qur’an - kama ilivyofasiriwa na wanazuoni wa *Tafsir*. Angalia maelezo ya Surat Al-Anbiyaa aya ya 105 kwa maelezo zaidi.

<sup>3</sup> Katika Aya hii, *Dhikri* imefasiriwa na wanazuoni kwa maana hiyo hiyo ya *Al-Lawh Al-Mahfudh*, Ubao Uliohifadhiwa ambapo hukumu zote za kiungu zimeandikwa humo. Angalia rejea iliyotangulia.

Kutoka kwa Mola wao. Kwa kujua kwako maana ya Alichokuteremshia Allah تعالى na kukielewa na kukifuata kwako, na kuelewa kwetu kuwa wewe ni mbora wa viumbe na Bwana wa wanadamu. Hivyo, utawafanulia kilichoelezwa kwa kifupi, na utawabainishia kilichowatatiza,

وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ

*“...wapate kufikiri.”*

Maana yake: Wataziangalia nafsi zao, kwa hiyo wataongoka watafuzu na kusalimika katika nyumba mbili.

أَفَأَمِنَ الَّذِينَ مَكَرُوا السَّيِّئَاتِ أَنْ يَخْسِفَ اللَّهُ بِهِمُ الْأَرْضَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٤٥﴾ أَوْ يَأْخُذَهُمْ فِي تَقْلُبِهِمْ فَمَا هُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿٤٦﴾ أَوْ يَأْخُذَهُمْ عَلَى تَخَوُّفٍ فَإِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٤٧﴾

**45. Je! Wameaminisha wanaofanya vitimbi vya uovu kwamba Mwenyezi Mungu Hatawadidimiza katika ardhi, na haitawafika adhabu kutoka wasipopajua?**

**46. Au hatawashika katika nyendo zao, na wala hawataponyoka?**

**47. Au Hatawashika kwa kitisho na kuwapunguza kidogo kidogo? Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye Huruma, Mwenye Kurehemu.**

### Ni Kwanini Waovu Wanajiaminisha

Allah تعالى Anaelezea Uvumilivu Wake na Kuwasubiria Kwake waasi wanaofanya maovu na kuyalingania na wanawawekea mikakati watu katika kuwaita kwao na kuwahamasisha pamoja na Uwezo Alionao wa Kuwazamisha ardhini au Kuwaletea adhabu,

مِنْ حَيْثُ لَا يَشْعُرُونَ

*“...kutoka wasipo pajua?”*

Maana yake: Kwa namna wasiojua itakavyowajia.

Sawa na Kauli Yake تعالى:

ءَأَمِنْتُمْ مِّن فِي السَّمَاءِ أَن يَخْسِفَ بِكُمُ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورٌ ﴿١٦﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ مِّن فِي  
السَّمَاءِ أَن يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۗ فَسَتَعْمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ ﴿١٧﴾

***“Mnadhani mko salama kwa Alioko juu kuwa Hatakudidimizeni kwenye ardhi, na tahamaki hiyo inatikisika! Au mnadhani mko salama kwa Alioko juu ya kuwa Yeye Hakupelekeeni kimbunga chenye changarawe? Mtajua vipi maonyo yangu?” (67:16-17)***

أَوْ يَأْخُذَهُمْ فِي تَقْلِبِهِمْ

***“Au Hatawashika katika nyendo zao.”***

Maana yake: Katika kwenda kwao huku na huko katika kujitafutia maisha yao, na kuishughulikia kwao, katika safari zao na mfano wake miongoni mwa shughuli zenye kupumbaza. Oatada na S-Suddiyyi wamesema:

تَقْلِبُهُمْ

***“...nyendo zao.”***

Maana yake: Safari zao<sup>1</sup>. Sawa na Kauli Yake:

أَفَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَن يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا بَيِّنًا وَهُمْ نَائِمُونَ ﴿٧٧﴾ أَوْ أَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَن  
يَأْتِيَهُمْ بَأْسُنَا ضُحًى وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٧٨﴾

***“Je, watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafika usiku, nao wamelala? Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa Adhabu Yetu haitawafika mchana, nao wanacheza?” (7:97-98)***

فَمَا هُمْ بِمُعْجِزِينَ

***“...na wala hawataponyoka?...”***

Maana yake: Hawatamshinda Allah تعالیٰ kwa hali yoyote waliyo nayo. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:213.

أَوْ يَأْخُذْهُمْ عَلَىٰ تَخَوُّفٍ

**“...Au Hatawashika kwa kitisho...”**

Maana: Au Allah تعالى Atawachukua katika hali ya khofu yao kutokana na Kuadhibu Kwake kwao wao, na bila shaka Kufanya huko ni vizuri zaidi. Kwa sababu kutokea kinachotazamiwa kutokea pamoja na kuwa na hofu kunaumiza mno, na kwa sababu hii Al-Aufy amesema: Kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

أَوْ يَأْخُذْهُمْ عَلَىٰ تَخَوُّفٍ

**“Au Hatawashika kwa kitisho.”**

Anasema: Nikitaka nitamchukua kwa athari ya mauti ya mwenzake na kumkhofisha kwake hilo<sup>1</sup>. Na hivyo hivyo imepokewa kutoka kwa Mujahid, Adh-Dhahaak, Qatada na wengine,<sup>2</sup> Kisha Akasema تعالى:

فَإِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**“Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenye Huruma, Mwenye Kurehemu”.**

Maana yake: Kwa kuwa Haharakishi Kuadhibu, kama ilivyoandikwa katika Sahih Mbili,

«لَا أَحَدٌ أَضَبُّ عَلَىٰ أَدَىٰ سَمِيعُهُ مِنَ اللَّهِ، إِنَّهُمْ يَجْعَلُونَ لَهُ وَلَدًا وَهُوَ يُرْزُقُهُمْ وَيُعَافِيهِمْ»

*“Hakuna yeyote mvumilivu zaidi wa maudhi alioyasikia zaidi ya Allah, hakika wao wanamfanya ana mtoto na Yeye Anawaruzuku na Kuwapa afya.”<sup>3</sup>*

Kadhalika imenukuliwa katika Sahih mbili:

«إِنَّ اللَّهَ لَيَمْلِكُ لِلظَّالِمِ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يُفْلِتْهُ»

*“Hakika Allah Anampa muda dhwaliwa mpaka anapokuja mkamata hatatoka.”*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:214.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:215.

<sup>3</sup> Fat’hul Al-Bari 13:372, Muslim 4:2160.

Kisha Mtume ﷺ akasoma:

وَكَذَٰلِكَ أَخَذَ رَبُّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُمْ شَدِيدٌ ﴿١٢٢﴾

**“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi anapoikamata miji inapokuwa imedhulumu. Hakika Mkamoto Wake ni mchungu na mkali.” (11:102)<sup>1</sup>**

Na Kauli ya Allah تعالى،

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَّتْ لَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ نَّمُرُ أَخَذْتَهَا وَإِلَى الْمَصِيرِ ﴿٤٨﴾

**“Na miji mingapi Niliipa muda na hali ilikuwa imedhulumu, na kisha Nikaitia Mkononi? Na Kwangu Mimi ndio marudio yote.” (22:48)**

أُولَٰئِكَ يَرْوُونَ إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِنْ شَيْءٍ يَتَفَيَّؤُا ظِلَالُهُ عَنِ الْيَمِينِ وَالشَّمَائِلِ سُجَّدًا لِلَّهِ وَهُمْ دَاخِرُونَ ﴿٤٩﴾ وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مِن دَابَّةٍ وَالْمَلَائِكَةِ وَهُمْ لَا يُسْتَكْبِرُونَ ﴿٥٠﴾ تَخَافُونَ رَبَّهُم مِّن فَوْقِهِمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٥١﴾

**48. Je! Hawavioni vitu Alivyoviumba Mwenyezi Mungu - vivuli vyao vinaelekea kuliani na kushotoni, kumsujudia Mwenyezi Mungu na vikinyenyekea?**

**49. Na vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi, tangu wanyama mpaka Malaika, vinamsujudia Mwenyezi Mungu, na wala havitakabari.**

**50. Vinamkhofu Mola wao Mlezi Aliye juu yao, na vinafanya vinavyoamrisha.**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:205, Muslim 4:1997.



## Kusujudu kwa Kila Kitu ni kwa Ajili ya Allah

Allah تعالیٰ Anaelezea Utukufu Wake na Kibri Chake ambacho kimetiwa na kila kitu na kudhalilikiwa na vitu vyote na viumbe wote. Wenye uhai na visivyo na uhai na vyenye majukumu kama vile mwanadamu, jini na malaika. Akasema kuwa kila kilicho na kivuli kinachoenda na kurudi kuliani na kushotoni, kwa maana, asubuhi na jioni, basi hicho kinasujudu kwa kivuli chake kwa Allah تعالیٰ.<sup>1</sup>

Mujahid amesema: Jua likishuka kila kitu kinamsujudia Allah تعالیٰ Mwenye Ushindi na Utukufu. Na hivyo hivyo amesema Qatada, Adh-Dhahaak na wengine.<sup>2</sup> Na Kauli Yake:

وَهُمْ دَاخِرُونَ

*“...na vikinyenyekea?...”*

Maana yake: Vimedhalilika. Na pia Mujaahid amesema: Sijida ya kila kitu ni kivuli chake. Na akataja milima kuwa: Sijida yake ni kivuli chake. Na Abuu Ghaalib Shaybany amesema: Mawimbi ya bahari ndiyo Sala yake, na Ameviweka pamoja katika kundi la walio na akili, kwa vile sijida imeegemezwa kwao. Akasema:

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ دَابَّةٍ

***“Na vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi, tangu wanyama vinamsujudia Allah.”***

Kama Alivyosema:

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَظِلَلُهُمْ بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ ﴿١٥﴾

***“Na viliomo mbinguni na katika ardhi vinamsujudia Mwenyezi Mungu tu vikitaka visitake. Na pia vivuli vyao asubuhi na jioni.”***  
(13:15).

<sup>1</sup> At-Tabari 17:217.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:217.

Na Kauli Yake:

وَأَلْمَلَيْكَتُ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ

**“...Na Malaika, na wala hawatakabari...”**

Maana yake: Wanamsujudia Allah تعالى bila ya kutakabari katika ibada Yake.

مَخَافُونَ رَبَّهُمْ مِنْ فَوْقِهِمْ

**“...Wanamkhofu Mola wao Mlezi aliye juu yao...”**

Maana yake: Wanasujudu hali ya kumkhofu Mola wao.

وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ

**“...na wanafanya vinavyoamrisha...”**

Maana yake: Wanadumu juu ya kumtii تعالى na kutekeleza Amri Zake na kuacha Makatazo Yake.

\* \* \*

\* وَقَالَ اللَّهُ لَا تَتَّخِذُوا إِلَهَيْنِ اثْنَيْنِ ۗ إِنَّمَا هُوَ إِلَهُ وَاحِدٌ ۗ  
 فَإِنِّي فَأَرْهَبُونَ ﴿٥١﴾ وَلَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ وَلَهُ  
 الدِّينُ وَاصِيبًا ۗ أَفَغَيَّرَ اللَّهُ تَتَّقُونَ ﴿٥٢﴾ وَمَا بِكُمْ مِّن تَعَمَّرٍ  
 فَمَنَ اللَّهُ ۗ ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمْ الضَّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْرِعُونَ ﴿٥٣﴾ ثُمَّ إِذَا  
 كَشَفَ الضَّرَّ عَنْكُمْ إِذَا فَرِيقٌ مِّنكُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾  
 لِيَكْفُرُوا بِمَا ءَاتَيْنَاهُمْ ۗ فَتَمَتَّعُوا ۗ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾  
 وَيَجْعَلُونَ لِمَا لَا يَعْلَمُونَ نَصِيبًا مِّمَّا رَزَقْنَاهُمْ ۗ تَاللَّهِ  
 لَتَشْتَلُنَّ عَمَّا كُنْتُمْ تَفْتُرُونَ ﴿٥٦﴾ وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ الْبَنَاتِ  
 سُبْحٰنَهُ ۗ وَلَهُمْ مَا يَشْتَهُونَ ﴿٥٧﴾ وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ  
 بِالْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهَهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٥٨﴾ يَتَوَارَىٰ مِّن  
 الْقَوْمِ مِن سُوءِ مَا بُشِّرَ بِهٖ ۗ أَيُّسُّكُهُ عَلَىٰ هٗن ۗ أَم  
 يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٥٩﴾ لِلَّذِينَ لَا  
 يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ مَثَلُ السَّوْءِ ۗ وَلِلَّهِ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ ۗ وَهُوَ  
 الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٠﴾

\* وَقَالَ اللَّهُ لَا تَتَّخِذُوا إِلَهَيْنِ اثْنَيْنِ ۗ  
 إِنَّمَا هُوَ إِلَهُ وَاحِدٌ ۗ فَإِنِّي فَأَرْهَبُونَ  
 ﴿٥١﴾ وَلَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ  
 وَلَهُ الدِّينُ وَاصِيبًا ۗ أَفَغَيَّرَ اللَّهُ تَتَّقُونَ  
 ﴿٥٢﴾ وَمَا بِكُمْ مِّن تَعَمَّرٍ فَمَنَ اللَّهُ ۗ  
 ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمْ الضَّرُّ فَإِلَيْهِ تَجْرِعُونَ  
 ﴿٥٣﴾ ثُمَّ إِذَا كَشَفَ الضَّرَّ عَنْكُمْ إِذَا  
 فَرِيقٌ مِّنكُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾  
 لِيَكْفُرُوا بِمَا ءَاتَيْنَاهُمْ ۗ فَتَمَتَّعُوا ۗ  
 فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾

51. Na Mwenyezi Mungu Amesema: Msiwe na miungu wawili! Hakika Yeye ni Mungu Mmoja. Basi niogopeni Mimi tu!

52. Na ni Vyake Yeye viliomo katika mbingu na

ardhi. Na Dini ni Yake Yeye daima. Je! Mtamcha mwengine asiye kuwa Mwenyezi Mungu?

53. Na neema yoyote mliyonayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara mnamyayatikia Yeye.

54. Na Anapokuondosheeni madhara mara kundi moja miongoni mwenu linamshirikisha Mola wao Mlezi,

55. Wakizikataa neema Tulizowapa. Basi stareheni. Mtakuja jua!

## Ni Allah Peke Yake Anayestahiki Kuabudiwa

Allah تعالٰى Anaeleza kuwa hakuna Mola isipokuwa Yeye tu. Na kwamba hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila Yeye Peke Yake. Hana mshirika, kwa sababu Yeye Ndiye Mmiliki wa kila kitu na Muumba Wake na Mola Wake.

اَلدِّينُ وَاَصْبًا

**“...Na Dini ni Yake Yeye daima..”**

Amesema Ibn Abbas, Mujahid, Ikrima, Maimuna Ibn Mahran, Suddi na Qatada na wengine رضي الله عنهما. Maana: Daima.<sup>1</sup> Imeelezwa kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, ‘Ya lazima.’<sup>2</sup> Na akasema Mujahid: Na ni Yake Yeye tu. Maana yake: Ibada ni Yake Yeye tu Peke Yake mbinguni na ardhini. Kama Kauli Yake Allah:

أَفْغَيْرَ دِينَ اللَّهِ يَبْتَغُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ

يُرْجَعُونَ ﴿٣٨﴾

**“Je, wanataka Dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumt’ii Yeye kikipenda kisipende, na Kwake Yeye watarejeshwa?” (3:83)**

Hii kufuatia kauli ya Ibn Abbas na Ikrima رضي الله عنهما, wao wanaona imekuja katika muundo wa taarifa. Ama kwa kauli ya Mujahid itakuwa katika muundo wa kuamrisha. Maana: Ogopeni kunishirikisha na chochote na mnitii Mimi tu.

Kama Kauli Yake inavyosema.

أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ

**“Hakika Dini Safi ni ya Mwenyezi Mungu tu.” (39:3)**

Kisha Akaeleza kuwa Yeye Ndiye Mmiliki manufaa na madhara na kwamba walichonacho waja kama vile riziki, neema, afya na ushindi ni baadhi ya Fadhila Zake kwao na Hisani Yake kwao.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:222.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:223.

ثُمَّ إِذَا مَسَّكُمْ الضُّرُّ فَالْيَدِ فَجِئْرُونَ

**“Kisha inapokuguseni dhara mara Yeye mnamlilia na mnamlalamikia.”**

Maana yake: Kwa kuelewa kwenu kuwa hakuna anayeweza kuliondoa ila Yeye kwa hiyo nyinyi katika madhara mnakimbilia Kwake na mnamuomba; tena mnapenda mno kumuomba msaada, kama Alivyosema تعالیٰ:

وَإِذَا مَسَّكُمْ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَاهُ ۗ فَأَمَّا جُنُودُكَ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ ۗ وَكَانَ  
الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾

**“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu. Na anapowaokoeni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanaadamu ni mwingi wa kukanusha.”**  
(17:67)

Na hapa Akasema:

ثُمَّ إِذَا كَشَفَ الضُّرُّ عَنْكُمْ إِذَا فَرِيقٌ مِّنْكُمْ بِرَبِّهِمْ يُشْرِكُونَ ﴿٥٥﴾ لِيَكْفُرُوا بِمَا ءَاتَيْنَاهُمْ ۗ

**“Na Anapokuondosheeni madhara mara kundi moja miongoni mwenu linamshirikisha Mola wao Mlezi, Wakizikataa neema Tulizo wapa...”**(16:54-55)

Imesemwa *Laam* hapa ni kwa sababu ya kuonesha matokeo na imesemwa pia ni *Laam* ya kutolea sababu. Kwa maana yake: Tuliwahukumia hilo wao ili wakufuru, wafiche na wapinge, neema za Allah تعالیٰ kwao. Wakati Ndiye Anaye-waondolea mateso, kisha Akawakemea kwa kusema:

فَتَمَتَّعُوا ۗ

**“Basi stareheni.”**

Maana yake: Fanyeni mtakacho na stareheni na mlichu nacho kidogo.

فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ

**“Mtakuja jua!”** Maana yake: Hatima ya hilo,

وَجَعَلُونَ لِمَا لَا يَعْلَمُونَ نَصِيبًا مِّمَّا رَزَقْنَاهُمْ ۗ تَاللَّهِ لَتُسْأَلُنَّ عَمَّا كُنْتُمْ تَفْتَرُونَ ﴿٥٦﴾  
 وَجَعَلُونَ لِلَّهِ الْآبِنَاتِ سُبْحَانَهُ ۗ وَلَهُمْ مَا يَشْتَهُونَ ﴿٥٧﴾ وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِالْأُنثَىٰ ظَلَّ  
 وَجْهَهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿٥٨﴾ يَتَوَارَىٰ مِنَ الْقَوْمِ مِنْ سُوءِ مَا بُشِّرَ بِهِ ۚ أَيُمْسِكُهُ عَلَىٰ  
 هُونٍ أَمْ يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٥٩﴾ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ  
 مَثَلُ الْسَّوءِ ۗ وَلِلَّهِ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ ۗ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٠﴾

**56. Na hao ambao hata hawawajui wanawawekea sehemu ya Tunavyowaruzuku. Wallahi! Bila ya shaka mtasailiwa kwa hayo mliyokuwa mnayazua!**

**57. Na wanamfanyia Mwenyezi Mungu ati ana mabinti, Subhanahu, Aliyetakasika! Na wao wenyewe, ati ndio wawe na hayo wanayoyatamani!**

**58. Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki.**

**59. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyobashiriwa! Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni? Tazama uovu wa wanavyohukumu!**

**60. Hali ya wasioiamini Akhera ni ovu; na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye Sifa Tukufu. Naye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.**

**Miongoni mwa Tabia za Washirikina ni Kuweka Nadhiri kwa Miungu Miongoni mwa Alivyowaruzuku Allah تعالى**

Allah تعالى Anaelezea baadhi ya mabaya ya washirikina ambao wameabudu pamoja na Allah تعالى kitu kingine, kama vile masanamu na viabudiwa vingine, bila ya elimu na wakayapa masanamu fungu kutoka katika kile Alichowapa Allah تعالى wakasema:

فَقَالُوا هَذَا لِلَّهِ بِزَعْمِهِمْ وَهَذَا لِشُرَكَائِنَا ۗ فَمَا كَانَ لِشُرَكَائِهِمْ فَلَا يَصِلُ إِلَى  
 اللَّهِ ۗ وَمَا كَانَ لِلَّهِ فَهُوَ يَصِلُ إِلَىٰ شُرَكَائِهِمْ ۗ سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٦٠﴾

**“...nao husema: Hii ni sehemu ya Mwenyezi Mungu - kwa madai yao - na hii ni ya miungu tunaowashirikisha. Basi vile walivyowakusudia miungu yao havimfikii Mwenyezi Mungu, na vilivyokuwa vya Mwenyezi Mungu huwafikia miungu yao. Ni uovu kabisa hayo wanayoyahukumu.” (6:136)**

Maana yake: Kuipa miungu yao fungu pamoja na Allah تعالى na wakaipendelea kuliko Allah تعالى, kwa hiyo Allah تعالى Akajiapia Mwenyewe kuwa Atawauliza kuhusu uongo walioubuni na Atawapa malipo yao katika moto wa Jahannamu. Akasema:

تَاللّٰهِ لَشَطْرُنَّ عَمَّا كُنْتُمْ تَفْتَرُونَ

**“Wallahi! Bila ya shaka mtasailiwa kwa hayo mliyokuwa mnayazua!”**

Kisha Allah تعالى Akazieleza habari zao kuwa wao wamewafanya malaika ambao ni waja wa Allah تعالى Mwingi wa Rehema, kuwa ni wanawake, na wamewafanya kuwa binti zake Allah تعالى, kwa hiyo wakawaabudu pamoja na Yeye. Hivyo wakakosea kosa kubwa katika kila nafasi katika nafasi hizi tatu, wakamnasibishia mtoto na wala hana mtoto. Kisha wakampa yule aliye daraja la chini katika aina mbili za watoto nayo ni mabinti na hata wao hawakubali kuwa ni watoto wao.

Kama Alivyosema:

أَلَا إِنَّكُمْ أَلذَّكَرُ وَلَهُ الْأُنثَى ﴿٥١﴾ تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَى ﴿٥٢﴾

**“Je! Nyinyi mnao wana wanaume na Yeye ndio awe na wanawake? Huo ni mgawanyo wa dhulma! ” (53:21-22)**

Na Kauli Yake hapa,

وَيَجْعَلُونَ لِلّٰهِ الْبَنَاتِ سُبْحٰنَهُ

**“Na wanamfanyia Mwenyezi Mungu ati ana mabinti, Subhanahu.”**

Maana yake: Kutoka kwenye kauli yao na uzushi wao.

أَلَا إِنَّهُمْ مِّنْ إِفْكِهِمْ لَيَقُولُونَ ﴿٥٣﴾ وَلَدَ اللّٰهُ وَإِنَّمْ لَكٰذِبُونَ ﴿٥٤﴾ أَصْطَفَى الْبَنَاتِ عَلَى الْبَنِينَ ﴿٥٥﴾ مَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٥٦﴾

***“Ati ni kwa uzushi wao ndio wanasema: Mwenyezi Mungu amezaa!  
Ama hakika bila ya shaka hao ni waongo! Ati amekhiari watoto  
wa kike kuliko wanaume? Mna nini? Mnahukumu vipi nyinyi?”  
(37:151-154)***

وَلَهُمْ مَا يَشْتَهُونَ

***“...na hayo wanayo yatamani!...”***

Maana yake: Wao wanajiteulia watoto wa kiume na wanawakataa watoto wa kike. Allah تعالى Ametukuka zaidi na Kuepukana na kauli yao hiyo, Kutukuka Kukubwa.

**Washirikina Wanakataa Kunasibishwa na Mabinti**

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُم بِالْأُنثَىٰ ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا

***“Na mmoja wao akibashiriwa kupata msichana, uso wake  
unasawijika...”***

Maana yake: Simanzi kutokana na huzuni,

وَهُوَ كَظِيمٌ

***“...naye kajaa chuki...”***

Mwenye kuwa kimya kutokana na shida ya aliyokuwa nayo katika huzuni,

يَتَوَارَىٰ مِنَ الْقَوْمِ

***“Anajificha asionekane na watu.”***

Hapendi watu wamuone.

مِنْ سُوءٍ مَا بُشِّرَ بِهَا ۚ أَيْمَسْكُهُمْ عَلَىٰ هُوبٍ ۚ أَمْ يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ

***“...kwa ubaya wa aliyobashiriwa! Je, akae naye juu ya fedheha  
hiyo au amfukie udongoni?”***

Maana yake: Kama akimbakisha atambakisha kwa udhalilifu, hatamrithisha wala hatamjali, na atawapa kipaumbele watoto wake wa kiume kuliko yeye,



أَمْ يَدُسُّهُ فِي التُّرَابِ ۗ

**“Au amfukie udongoni?”**

Maana yake: Atamfukia, nako ni kumzika akiwa hai, kama walivyokuwa wanafanya kabla ya Uislamu, hivi huyu wanayemchukia namna hii, hata wenyewe hawamkubali ndiye wanayemnasibisha na Allah?

أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ

**“Tazama uovu wa wanavyohukumu!”**

Maana yake: Ni mabaya mno waliyosema, na ni mabaya mno walioyagawa. Na kibaya mno walichomnasibisha, kama Anavyosema تعالى:

وَإِذَا بُشِّرَ أَحَدُهُمْ بِمَا ضَرَبَ لِلرَّحْمَنِ مَثَلًا ظَلَّ وَجْهُهُ مُسْوَدًّا وَهُوَ كَظِيمٌ ﴿١٧﴾

**“Na anapobashiriwa mmoja wao kwa yale aliyompigia mfano Mwenyezi Mungu, uso wake husawijika na hujaa hasira.” (43:17)**

Maana yake: Akiambiwa amezaa mtoto mwanamke uso wake huwa mweusi na huhuzunika sana. Na Kauli Yake hapa:

لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ مَثَلُ السَّوِّءِ ۗ

**“Hali ya wasioiamini Akhera ni ovu.”**

Maana yake: Upungufu wote ni wao.

وَلِلَّهِ الْمَثَلُ الْأَعْلَىٰ ۗ

**“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Sifa Tukufu.”**

Maana yake: Aliyekamilika kabisa katika kila upande wa ukamilifu,

وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

**“Naye ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”**

\* \* \*

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِظُلْمِهِمْ مَا  
 تَرَكَ عَلَيْهَا مِنْ دَابَّةٍ وَلَكِنْ يُؤَخِّرُهُمْ  
 إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ  
 يَسْتَخْرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٦١﴾ وَجَعَلُونَ  
 لِلَّهِ مَا يَكْرَهُونَ وَتَصِفُ أَلْسِنَتُهُمُ الْكَذِبَ أَنَّ لَهُمُ  
 الْحُسْنَىٰ ۖ لَا جَرَمَ أَنَّ لَهُمُ النَّارَ وَأَنَّهُمْ مُّفْرَطُونَ ﴿٦٢﴾ تَاللَّهِ  
 لَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَرِئِن لَّهُمُ الشَّيْطَانُ عَمَلُهُمْ  
 فَهَوَّوْا لَهُمْ الْيَوْمَ وَهَمَّ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾ وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ  
 الْكِتَابَ إِلَّا لِتُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي اخْتَلَفُوا فِيهِ ۖ وَهُدًى وَرَحْمَةً  
 لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٦٤﴾ وَاللَّهُ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْبَا  
 بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ  
 ﴿٦٥﴾ وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۚ نَشْفِيكُم بِمَا فِي بُطُونِهِمْ  
 مِنْ بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَّبَنًا خَالِصًا سَائِغًا لِلشَّارِبِينَ ﴿٦٦﴾ وَمِنْ  
 ثَمَرَاتِ النَّخِيلِ وَالْأَعْنَابِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سَكَرًا وَرِزْقًا  
 حَسَنًا ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾ وَأَوْحَىٰ رَبُّكَ  
 إِلَى النَّخْلِ أَنْ اتَّخِذِي مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا وَمِنَ الشَّجَرِ وَمِمَّا  
 يَعْرِشُونَ ﴿٦٨﴾ ثُمَّ كُلِي مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ فَاسْلُكِي سُبُلَ  
 رَبِّكِ ذُلُلًا ۚ يَخْرُجُ مِنْ بُطُونِهَا سَرَابٌ مُّخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ فِيهِ  
 شِفَاءٌ لِلنَّاسِ ۚ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٦٩﴾ وَاللَّهُ  
 خَلَقَكُمْ ثُمَّ يَتَوَفَّاكُمْ ۖ وَمِنْكُمْ مَنْ يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمَرِ لَكُمْ  
 لَا يَعْلَمُ بَعْدَ عِلْمٍ شَيْئًا ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ قَدِيرٌ ﴿٧٠﴾

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ بِظُلْمِهِمْ مَا  
 تَرَكَ عَلَيْهَا مِنْ دَابَّةٍ وَلَكِنْ يُؤَخِّرُهُمْ  
 إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۖ فَإِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ  
 لَا يَسْتَخْرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا  
 يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٦١﴾ وَجَعَلُونَ  
 لِلَّهِ مَا يَكْرَهُونَ وَتَصِفُ  
 أَلْسِنَتُهُمُ الْكَذِبَ أَنَّ لَهُمُ  
 الْحُسْنَىٰ ۖ لَا جَرَمَ  
 أَنَّ لَهُمُ النَّارَ وَأَنَّهُمْ مُّفْرَطُونَ ﴿٦٢﴾

**61. Na lau kuwa Mwenyezi Mungu Angeliwachukulia watu kwa mujibu wa dhulma zao, basi Asingelimuacha hapa hata mnyama mmoja. Lakini Anawaakhirisha mpaka muda uliowekwa. Na unapofika muda wao hawatakawilia hata saa moja wala hawatatangulia.**

**62. Na wanampa Mwenyezi Mungu wanavyovichukia wao, na ndimi zao zinasema uwongo kwamba wao watapata mema. Hapana shaka hakika wamewekewa Moto, nao watachwa humo.**

### Allah تعالیٰ Hana Haraka ya Kuadhibu Waliokaidi

Allah تعالیٰ Anaelezea uvumilivu Wake kwa viumbe Wake pamoja na dhulma yao na kwamba kama Angewachukulia haraka kwa dhambi walizozifanya asingalimuacha mnyama yoyote juu ya mgongo wa ardhi. Maana yake: Angaliwaangamiza wanyama wote kufuatia kuangamizwa kwa wanadamu, lakini Mola تعالیٰ Anavumilia, Anasitiri, na Anasubiri muda ufike. Maana yake ni kuwa: Hawafanyii haraka adhabu, kwani kama Angaliharakisha kwao adhabu Asingalimbakisha yeyote. Amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ kutoka kwa Abi Salama amesema: Abu Hurairah عنه الله رضي amemsikia mtu fulani akisema: 'Hakika dhalimu haidhuru isipokuwa nafsi yake.' Amesema: Akamgeukia, Akasema: "Ni kweli Wallaahi! Hata ndege katika viota vyao wanakufa kwa dhulma ya dhalimu."<sup>1</sup>

### Washirikina Wanamnasibishia Allah تعالیٰ Wanavyovichukia

وَيَجْعَلُونَ لِلَّهِ مَا يَكْرَهُونَ

***"Na wanampa Mwenyezi Mungu wanavyovichukia."***

Maana yake: Mabinti na washirika ambao hao ni watumwa wa Allah تعالیٰ, na wao hawataki mmoja wao kuwa na mshirika yoyote katika mali yake. Na Kauli Yake:

وَتَصِفُ أَلْسِنَتُهُمُ الْكَذِبَ أَنَّ لَهُمُ احْسَنًا

***"Na ndimi zao zinasema uwongo kwamba wao watapata mema."***

Ni kuwakatalia dai lao. Lakini pamoja na hayo eti wanadai kuwa wana mema hapa duniani na ikiwa kuna marejeo basi pia watapata mema na kuelezea kilichosemwa na aliyesema miongoni mwao. Na Kauli Yake:

وَلَيْنَ أَذْقَنَّا إِلَّا نَسْنَمِنَا رَحْمَةً ثُمَّ نَزَعْنَاهَا مِنْهُ إِنَّهُ لَيَكُوسُ كَكُفُورٍ ﴿١١﴾ وَلَيْنَ أَذْقَنَّهُ نَعْمَاءَ بَعْدَ ضَرَاءٍ مَسْتَهُ لَيَقُولَنَّ ذَهَبَ السَّيِّئَاتُ عَنِّي إِنَّهُ لَفَرِحٌ فَخُورٌ ﴿١٢﴾

***"Na Tukimuonjesha mtu rehema inayotoka Kwetu, kisha Tukamuondolea, hukata tamaa akakufuru. Na Tukimuonjesha neema baada ya madhara yaliyompata husema: Taabu zimekwishaniondokea. Hakika yeye hujitapa na kutafakhari." (11:9-10)***

<sup>1</sup> At-Tabari 17:231.

وَلَيْنَ أَذَقْنَهُ رَحْمَةً مِنَّا مِنْ بَعْدِ ضَرَاءٍ مَسَّتَهُ لَيَقُولَنَّ هَذَا لِي وَمَا أَطُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَيْنَ رُجِعْتُ إِلَىٰ رَبِّي إِنَّ لِي عِنْدَهُ لَلْحُسْنَىٰ فَلَنُنَبِّئَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِمَا عَمِلُوا وَلَنُذِيقَنَّهُمْ مِنَ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٥٥﴾

**“Na pindi Tukimuonjeshha rehemu itokayo Kwetu baada ya kumgusa madhara, bila ya shaka husema: Haya nayastahiki mimi, wala sidhani kuwa Kiyama kitakuja. Na hata nikirudishwa kwa Mola Wangu Mlezi bila ya shaka nina mema yangu Kwake! Basi kwa yakini Tutawaelezea waliokufuru hayo waliyoyatenda, na kwa yakini Tutawaonjeshha adhabu ngumu.” (41:50)**

وَدَخَلَ جَنَّتَهُ وَهُوَ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ قَالَ مَا أَظُنُّ أَنْ تَبِيدَ هَذِهِ أَبَدًا ﴿٥٦﴾ وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَيْنَ رُدِدْتُ إِلَىٰ رَبِّي لأَجِدَنَّ خَيْرًا مِنْهَا مُنْقَلَبًا ﴿٥٧﴾

**“Na akaingia kitaluni kwake, naye hali anajidhulumu nafsi yake. Akasema: Sidhani kabisa kuwa haya yataharibika. Wala sidhani kuwa hiyo Saa (ya Kiyama) itatokea. Na ikiwa nitarudishwa kwa Mola wangu Mlezi, bila ya shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya.” (18:35-36)**

Wakakusanya kati ya tendo ovu na matamanio batili kuwa watalipwa mema na hili ni muhali kutokea. Hivyo Allah تعالى Akawajibu katika kutamani kwao huko.

لَا جَرَمَ

**“...Hapana shaka...”** Ni haki isio na budi,

أَنَّ لَهُمُ النَّارَ

**“...hakika wamewekewa Moto...”**

Maana yake: Siku ya Kiyama.

أَفَرَأَيْتَ الَّذِي كَفَرَ بِعَائِبَتِنَا وَقَالَ لَأُوتِينَ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٧٧﴾

**“Je, umemuona aliyezikana Ishara Zetu na akasema: Kwa hakika mimi nitapewa mali na wana!” (19:77)**

Na akasema akielezea kuhusu mmoja wa watu wawili kuwa:

وَأَنْتُمْ مُفْرَطُونَ

*"...nao watachwa humo..."*

Mujahid, Said bin Jubayr, Qatadah na wengine walisema. 'Maana yake: Watasahauliwa na kuachwa hukohuko. Ni sawa na Aya nyingine,

فَالْيَوْمَ نَنْسَهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا

*"Basi leo Sisi Tunawasahau kama waliviousahau mkutano wa Siku yao hii,..." (7:51)*

Qatadah alieleza kuwa,

مُفْرَطُونَ

*"...watachwa..."*

Maana yake: 'Wataharakishwa kuingizwa Motoni.'<sup>1</sup> Rai hizo mbili hazipingani, kwa sababu wataharakishwa kuingia Motoni katika Siku ya Kiyama, halafu watasahauliwa huko huko. Kwa maana wakae humo milele.

تَاللَّهِ لَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ فَهُوَ وَيَوْمَ الْيَوْمِ وَهُمْ

عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٦﴾ وَمَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ إِلَّا لِتُبَيِّنَ لَهُمُ الَّذِي اخْتَلَفُوا فِيهِ وَهُدًى

وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٦٧﴾ وَاللَّهُ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَحْيَا بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٨﴾

**63. Wallahi! Sisi Tulituma Mitume kwa umati uliokuwa kabla yako, lakini Shetani aliwapambia vitendo vyao. Kwa hivyo leo yeye ndiye rafiki yao; nao watapata adhabu chungu.**

**64. Na hatukukuteremshia Kitabu isipokuwa uwabainishie yale ambayo wanakhitalifiana, na kiwe Uwongofu na Rehema kwa watu wanaoamini.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:233.

**65. Na Mwenyezi Mungu Ameteremsha maji kutoka mbinguni na kwa hayo Akaihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Kwa hakika katika hayo imo Ishara kwa watu wanaosikia.**

### **Kutafuta Faraja kwa Waliopita Kabla Yetu**

Allah تعالی Anaeleza kuwa Amepeleka Mitume kwa Umma uliopita nao wakawakadhibisha Mitume kwa uongo. Kwa hiyo ee! Muhammad una kiigizo kwa ndugu zako hao, Mitume, lisikufadhaishe kadhibisho la watu wako kwako. Ama washirikina ambao wamewakadhibisha Mitume, kilichowapelekea kufanya hivyo ni shaitwani kuwapambia uovu kwa walilolifanya,

فَهُوَ وَلِيُّهُمُ الْيَوْمَ

**“Kwa hivyo leo yeye ndiye rafiki yao.”**

Maana yake: Wataadhibiwa huku shetani ni rafiki yao, na hawezi kuwaokoa na hawana wa kuwaitikia wito wao wa kuomba msaada, na wana adhabu yenye maumivu makali sana.

### **Sababu ya Kuteremsha Qur-aan**

Kisha تعالی Akamuambia Mtume Wake: Kuwa Yeye Alimteremshia Qur’ani ili kuwafafanulia watu ambacho wanakhitilafiana ndani yake, kwa hiyo Qur’ani ndio muamuzi kati ya watu katika kila wanachotofautiana, na

وَهَدَىٰ

**“...Uwongofu...”** Maana yake: Wa nyoyo,

وَرَحْمَةً

**“...na ni rehema...”**

Maana yake: Kwa mwenye kushikamana nacho.

لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

**“...kwa watu wanaoamini.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:234.

Na kama Allah تعالى Alivyoifanya Qur'ani ni huisho la nyoyo zilizokufa kwa ukafiri wake, basi vivyo hivyo Anaihuisha ardhi baada ya kufa kwake, na uhai wake – kwa ambacho Anakiteremshia kutoka mbinguni. Maana yake: Maji.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ

**“Kwa hakika katika hayo imo Ishara kwa watu wanaosikia.”**

Kwa maana: Wanaoyafahamu maneno na maana yake.

وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ۗ نُسْقِيكُمْ مِمَّا فِي بُطُونِهِمْ مِنْ بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَبَنًا خَالِصًا سَائِغًا  
لِّلشَّارِبِينَ ﴿٦٦﴾ وَمِنْ ثَمَرَاتِ النَّخِيلِ وَالْأَعْنَابِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سَكَرًا وَرِزْقًا حَسَنًا ۗ إِنَّ  
فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾

**66. Na hakika katika wanyama hao nyinyi mnamazingatio. Tunakunywesheni katika vile viliomo matumboni mwao, vikatoka baina ya mavi na damu, maziwa safi mazuri kwa wanywao.**

**67. Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza ulevi na riziki nzuri. Hakika katika hayo ipo Ishara kwa wanaotumia akili.**

**Mafundisho na Neema Katika Wanyama na Matunda, ya Mitende na Mizabibu**

وَإِنَّ لَكُمْ

**“...na hakika nyinyi mnayo...”** Enyi watu.

فِي الْأَنْعَامِ

**“...katika wanyama...”**

Nao ni ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo.

لَعِبْرَةً

**“...mazingatio...”**

Maana yake: Ni alama na dalili juu na hekima ya Aliyewaumba, na Uwezo Wake, Huruma Yake na Upole Wake:

نُسْقِيكُمْ مِمَّا فِي بُطُونِهِ

**“Tunakunywesheni katika vile vilivyomo matumboni mwao.”**

Ametumia kiwakilishi cha umoja katika neno “Butuunihi” kwa maana huwakilisha neno “Niam” wanyama au hayawani.

Na Kauli ya Allah تعالى:

مِنْ بَيْنِ فَرْثٍ وَدَمٍ لَبْنَا خَالِصًا

**“...vikatoka baina ya kinyesi na damu, maziwa safi...”**

Maana: Inasafika na damu kwa weupe, ladha na utamu wake, iko kati ya choo na damu, ndani ya tumbo la mnyama. Hivyo, kila kitu kinaenda katika nafasi yake kinapopevuka chakula katika matumbo yake. Damu inapelekwa kwenye mishipa yake, maziwa kwenye kiwele chake, mkojo kwenye kibofu chake na choo kwenye njia yake ya kutokea. Kila kimoja kati ya hivyo hakichanganyiki na kingine baada ya kuondoka hapo na wala hakibadilishwi kwa kingine.

لَبْنَا خَالِصًا سَابِغًا لِلشَّرِيبِ

**“...maziwa safi mazuri kwa wanywao...”**

Maana yake: Hayamkwami yeyote.

Allah تعالى Alipotaja maziwa na kwamba Ameyafanya kinywaji kizuri kwa watu, Akataja vinywaji wanavyotengeneza watu kutokana na matunda ya mtende na mzabibu na walichokuwa wanatengeneza. Maana: Mvinyo inaoleweshwa itokanayo na tende kabla haijaharamishwa. Anawakumbusha kwa Kusema:

وَمِنْ ثَمَرَاتِ النَّخِيلِ وَالْأَعْنَابِ تَتَّخِذُونَ مِنْهُ سَكَرًا

**“...Na kutokana na matunda ya mitende na mizabibu mnatengeneza ulevi...”**

Aya imejulisha uhalali wake kisheria kabla ya kuharamishwa, na imejulisha usawa kati ya kilevi kilichotokana na mtende na kilichotengenezwa na mzabibu na pia hukumu ya vileo vilivyotengenezwa kutokana na ngano, shairi, mtama na asali. Kama Sunna ilivyopambanua hayo. Kama alivyosema Ibn Abbas رضي الله عنهما.



سَكْرًا وَرِزْقًا حَسَنًا<sup>١</sup>

*"...ulevi na riziki nzuri."*

Maana yake: Ulevi ni kilichoharamishwa kutokana na matunda haya mawili tende na zabibu. Na katika mapokezi mengine: 'Sakaran' ni kinywewa haramu na 'Rizqi Hasan' ni kinywaji halali<sup>1</sup>. Maana yake: Tende kavu na zabibu kavu. Na kilichotengenezwa kutoka humo kama vile kinywaji cha asali, siki ya zabibu na juisi ya tende ni halali kabla haijachacha. Kama Sunna ilivyoeleza.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ

*"...Hakika katika hayo ipo Ishara kwa wanaotumia akili..."*

Amenasibisha hapa kutaja akili kwa sababu akili ni kitu bora mno kilicho ndani ya mwanadamu. Na kwa sababu hii Allah تعالیٰ Ameuharamishia umma huu vinywaji vinavyoleweshwa ili kuzilinda akili zao. Allah تعالیٰ Amesema:

وَجَعَلْنَا فِيهَا جَنَّاتٍ مِّنْ نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ وَفَجَّرْنَا فِيهَا مِنَ الْعُيُونِ ﴿٣٤﴾ لِيَأْكُلُوا مِنْ ثَمَرِهِ  
وَمَا عَمِلَتْهُ أَيْدِيهِمْ أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٣٥﴾ سُبْحٰنَ الَّذِي خَلَقَ الْأَزْوَاجَ كُلَّهَا مِمَّا تُنْبِتُ  
الْأَرْضُ وَمِنَ أَنْفُسِهِمْ وَمِمَّا لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٦﴾

*"Na Tukafanya ndani yake bustani ya mitende na mizabibu, na Tukatimbia chemchem ndani yake, Ili wale matunda yake, na hayo hayakufanywa na mikono yao! Basi je, hawashukuru? Subhana, Ametakasika, Aliyeumba dume na jike, vyote katika vinavyomea katika ardhi, na katika nafsi zao, na katika wasivyo vijua." (36:34-36)*

وَأَوْحَىٰ رَبُّكَ إِلَى النَّخْلِ أَنْ اتَّخِذِي مِنَ الْجِبَالِ بُيُوتًا وَمِنَ الشَّجَرِ وَمِمَّا يَعْرِشُونَ ﴿٣٦﴾  
ثُمَّ كُلِي مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ فَاسْلُكِي سُبُلَ رَبِّكِ ذُلًّا ۗ تَخْرُجُ مِنْ بُطُونِهَا شَرَابٌ مُّخْتَلِفٌ  
أَلْوَانُهُ فِيهِ شِفَاءٌ لِلنَّاسِ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٣٧﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 17:241.

**68. Na Mola Wako Mlezi Amemfunulia nyuki: Jitengenezee majumba yako katika milima, na katika miti, na katika wanayojenga watu.**

**69. Kisha kula katika kila matunda, na upite katika njia za Mola Wako Mlezi zilizofanywa nyepesi kuzipita. Na kutoka matumbo yao kinatoka kinywaji chenye rangi mbali mbali; ndani yake kina matibabu kwa wanaadamu. Hakika katika haya ipo Ishara kwa watu wanaofikiri”.**

### **Katika Nyuki na Asali Yake Kuna Neema na Mafundisho**

Madhumuni ya Wahyi hapa ni ufahamisho na maelekezo kwa nyuki atengeneze nyumba katika milima atakayoishi humo, na katika miti na katika wanavyovijenga watu. Nyumba hizo ziwe madhubuti na zimetengenezwa kwa ufundi stadi mkubwa, katika umbo la pembe sita, na kuzipanga bila ya kuwa mwanya katika nyumba yake. Kisha Allah تعالی Akampa ruhusa ya kiuwezo na kumdhalilishia kula kila matunda na kupita njia ambazo Allah تعالی Amemdhalilishia.

Maana yake: Zilizorahisishwa kwake kufika atakapo katika anga hili kubwa, na bara lililo pana, mabonde na milima mirefu. Kisha kila mmoja wao anarudi kutoka huko na kwenda nyumbani kwake bila ya kuacha njia kushoto au kulia, bali kuenda kwenye nyumba yake pamoja na vilivyo humo miongoni mwa kizazi chake na asali. Na hapo anatengeneza mshumaa kutoka kwenye mbawa zake na anacheua asali kutoka kinywani mwake na anataga mayai kutoka mkiani mwake, kisha asubuhi ya siku inayofuata anakwenda katika malisho yake.

فَأَسْلِكِي سُبُلَ رَبِّكِ ذُلُلًا

**“...na upite katika njia za Mola wako Mlezi zilizofanywa nyepesi...”**

Qatadah, na AbduRahmaani bin Zaid bin Aslam wamesema:

Maana: Zenye kutii<sup>1</sup>. Ibn Zaid amesema: Na hiyo ni sawa na Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:242.

وَدَلَّلْنَاهَا هُمْ فَمِنهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنهَا يَأْكُلُونَ ﴿٦٧﴾

***“Na Sisi Tukawadhilishia. Basi baadhi yao wako wanaowapanda, na baadhi yao wanawala.” (36:72)<sup>1</sup>***

Amesema: Hivi hauoni kuwa wao wanawahamisha nyuki kutoka mji mmoja kwenda mji mwingine, naye anakuwa pamoja na wao. Na kauli ya kwanza iko wazi zaidi. Ibn Jariri رحمه الله تعالى amesema: Maana mbili zote ni sahihi.<sup>2</sup> Na Kauli Yake تعالى:

مَخْرُجٌ مِنْ بَطُونِهَا شَرَابٌ مُخْتَلِفٌ أَلْوَانُهُ فِيهِ شِفَاءٌ لِلنَّاسِ ۗ

***“...kinatoka kinywaji chenye rangi mbali mbali; ndani yake kina matibabu kwa wanaadamu.”***

Kati ya rangi nyeupe, njano na nyekundu na zisizokuwa hizo miongoni mwa rangi nzuri kulingana na tofauti za malisho yake na chakula chake. Kauli Yake:

فِيهِ شِفَاءٌ لِلنَّاسِ ۗ

***“...ndani yake kina matibabu kwa wanaadamu...”***

Maana yake: Katika asali kuna tiba kwa watu. Maana: Katika maradhi yanayowapata. Wamesema baadhi ya waliozungumzia tiba ya Mtume: Kama angesema: Ndani yake kuna ponyo kwa watu ingekuwa ni ponyo la kila ugonjwa, ‘Ash-Shifaa Linnas’. Lakini amesema: ‘Shifaa Linnas.’ Maana: Bila ya ‘Al’. Maana: Inafaa kwa kila mtu kwa maradhi baridi, kwa sababu asali ina joto na kitu kinatibiwa kwa kinyume chake.

Wamepokea Bukhari na Muslim katika Sahih zao katika mapokezi ya Qatadah kutoka kwa Abiil Mutawakkil Ali Ibin Dawuud An-Nnajy kutoka kwa Abi Said Al-Khudriy رضي الله عنه kuwa: Mtu fulani alikuja kwa Mtume ﷺ akasema: ‘Ndugu yangu anaharisha.’ Akamuambia:

<sup>1</sup> Neno lililofasiriwa hapa kama “imerahisishwa” ni *Dhululan*. Hilo linaweza kufahamika kwa maana ya “imerahisishwa”, ambalo kwa hali hiyo linaashiria njia inayofuatwa na nyuki, au linaweza kufahamika “wametiishwa”, ambalo kwa hali hiyo linarejea kwa nyuki wenyewe. Tafsiri hizi mbili za kisomi ndizo zinazoelezwa hapa.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:249.

«اسْتَقِ عَسَلًا»

“Mnyweshe asali”,

Kisha akaja akasema: ‘Ewe Mtume wa Allah! Nimemnywesha asali, lakini haikumuongezea isipokuwa kuhara.’ Akamuambia:

«أَذْهَبْ فَاسْقِ عَسَلًا»

“Nenda ukamnyweshe Asali.”

Akaenda ukamnywesha asali kisha akaja akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Haikumuongezea isipokuwa kuhara.” Mtume wa Allah ﷺ akasema:

«صَدَقَ اللَّهُ وَكَذَّبَ بَطْنُ أَخِيكَ، أَذْهَبْ فَاسْقِ عَسَلًا»

“Allah Amesema kweli na tumbo la ndugu yako limeongopa nenda kamnyweshe asali.”

Akaondoka ukamnywesha asali na akapona<sup>1</sup>.

Na katika Sahih mbili wamepokea kutoka kwa Aisha رضي الله عنها kuwa Mtume ﷺ alivutiwa na vitu vitamu na asali.<sup>2</sup> Hili ni tamko la al-Bukhari. Na katika sahihi ya Bukhari amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: Mtume ﷺ amesema:

«الشِّفَاءُ فِي ثَلَاثَةٍ: فِي شَرْطَةِ مِخْجَمٍ، أَوْ شَرْبَةِ عَسَلٍ، أَوْ كَيْتِ بِنَارٍ، وَأَنْهَى أُمَّتِي  
عَنِ الْكَيْ»

“Tiba iko katika (vitu) vitatu: Chale ya kuumika, kunywa asali au kuchoma kwa moto, na ninaukataza umma wangu kuchoma kwa moto.”<sup>3</sup>

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَةً لِّقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

“Hakika katika haya ipo Ishara kwa watu wanaofikiri.”

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 10:178, Muslim 4:1732.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 10:81, Muslim 2:1101.

<sup>3</sup> Fat’hul Al-Bari 10:143.

Maana: Allah تعالى Anampa msukumo kiumbe huyu mdogo kupita sehemu muhimu na kula matunda mbalimbali na vitu vingine kisha kuyakusanya kwa ajili ya nta na Asali. Nayo ni miongoni mwa vitu bora zaidi, ni alama kwa watu wanaotafakari katika Uungu wa Aliyewaumba nyuki hao, Kuwawezesha, Kuwadhalilisha, na Kuwarahisisha. Hivyo ikawa ni hoja inayowathibitishia kuwa Allah تعالى Ndiye Mtendaji Muweza, Mwenye Hekima, Mjuzi, Karimu, Mwingi wa Huruma.

وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ ثُمَّ يَتَوَفَّاكُمْ ۗ وَمِنْكُمْ مَنْ يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمُرِ لِكَيْ لَا يَعْلَمَ بَعْدَ عِلْمٍ شَيْئًا ۗ  
 إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ قَدِيرٌ ﴿٧٠﴾

**70. Na Mwenyezi Mungu Amekuumbeni; kisha Anakufisheni. Na miongoni mwenu wapo wanaorudishwa kwenye umri mbaya kabisa, hata akawa asijue kitu baada ya ujuzi aliokuwa nao. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi na Muweza.**

### Katika Vipindi vya Umri wa Mwanadamu Kuna Mazingatio

Allah تعالى Anaelezea kuwa Anadhibiti mambo ya waja Wake. Yeye Ndiye Aliyewaumba kutoka katika kukosekana, kisha Atawafisha na baadhi yao Atawaacha mpaka wazeeke, na uzee ni udhaifu, kimwili.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِنْ بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً

**“Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni kutokana na udhaifu kisha Akajaalia nguvu baada ya unyonge...” (30:54)**

لِكَيْ لَا يَعْلَمَ بَعْدَ عِلْمٍ شَيْئًا

**“...hata akawa asijue kitu baada ya ujuzi...”**

Maana yake: Baada ya kuwa mjuzi akawa hajui kitu kutokana na udhaifu wa akili na kuzingatia.

Na kwa ajili hii Bukhari amepokea katika tafsiri ya aya hii kutoka kwa Anas Ibn Malik رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alikuwa anaomba:

«أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْبُخْلِ وَالْكَسَلِ وَالْهَرَمِ، وَأَزْذِلِ الْعُمُرِ وَعَذَابِ الْقَبْرِ، وَفِتْنَةِ الدَّجَالِ  
وَفِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ»

*“Ninajilinda kwako na ubakhili, uvivu, uzee na umri duni na adhabu  
ya kaburi na Fitina ya Dajjali pamoja na fitina ya uhai na kifo.”<sup>1</sup>*

Zuhair bin Abi Salmaa amesema katika mashairi yake mashuhuri<sup>2</sup>:

سَمِّتُ تَكَالِيفَ الْحَيَاةِ وَمَنْ يَعِشُ  
ثَمَانِينَ عَامًا - لَا أَبَا لَكَ - يَسْأَمُ  
رَأَيْتُ الْمَنَايَا خَبَطَ عَشْوَاءَ مَنْ تُصَبُّ  
تُؤْتُهُ وَمَنْ تُحْطِئُهُ يُعَمَّرُ فِيهِمْ

*Nimetweshwa na majukumu ya maisha  
Afika umri wa miaka themanini  
Kwake kuchoka si Ajabu  
Nimekiona kifo kikibamiza watu  
Mithili ya Ngamia mwenye uoni dhaifu  
Na kila abamizwaye hufa  
Na kitayemkosa huishi mpaka akonge.*

\* \* \*

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:239.

<sup>2</sup> Mu'allaq (kilugha, iliyoangikwa) katika zama za Jahiliyyah, ushairi, kwa namna ya kaswida ilikuwa namna pekee ya kufikisha ujumbe. Kaswida saba zilizokuwa namna yao bora zaidi ziliangikwa katika kuta za Ka'bah. Zinajulikana kwa jina, "Mu'allaqaat Saba."

وَاللَّهُ فَضَّلَ بَعْضَكُمْ عَلَى بَعْضٍ فِي الرِّزْقِ ۗ فَمَا الَّذِينَ  
 فَضَّلُوا بَرَادَىٰ رِزْقِهِمْ عَلَىٰ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَهُمْ فِيهِ  
 سَوَاءٌ ۗ أَفَبِنِعْمَةِ اللَّهِ تَجْحَدُونَ ﴿٧١﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ  
 أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا ۖ وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنْزَالِكُمْ بَيْنَ وَحَفْدَةٍ  
 وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ ۗ أَفَبِالْبِطْلِ يُؤْمِنُونَ وَبِنِعْمَتِ اللَّهِ هُمْ  
 يَكْفُرُونَ ﴿٧٢﴾ وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَهُمْ  
 رِزْقًا مِنَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ شَيْئًا وَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٧٣﴾  
 فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ  
 ﴿٧٤﴾ \* ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا عَبْدًا مَمْلُوكًا لَا يَقْدِرُ عَلَىٰ شَيْءٍ  
 وَمَنْ رَزَقْنَاهُ مِنْآ رِزْقًا حَسَنًا فَهُوَ يُفُوقُ مِنْهُ سِرًّا وَجَهْرًا ۗ  
 هَلْ يَسْتَوُونَ ۗ أَلْحَمْدُ لِلَّهِ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾  
 وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَجُلَيْنِ أَحَدُهُمَا أَبْكَمُ لَا يَقْدِرُ عَلَىٰ  
 شَيْءٍ وَهُوَ كَلٌّ عَلَىٰ مَوْلَاهُ أَيْنَمَا يُوَجِّههُ لَا يَأْتِ بِخَيْرٍ ۗ  
 هَلْ يَسْتَوِي هُوَ وَمَنْ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ ۗ وَهُوَ عَلَىٰ صِرَاطٍ  
 مُسْتَقِيمٍ ﴿٧٦﴾

وَاللَّهُ فَضَّلَ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ فِي  
 الرِّزْقِ ۗ فَمَا الَّذِينَ فَضَّلُوا بَرَادَىٰ  
 رِزْقِهِمْ عَلَىٰ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ  
 فَهُمْ فِيهِ سَوَاءٌ ۗ أَفَبِنِعْمَةِ اللَّهِ  
 تَجْحَدُونَ ﴿٧١﴾

**71. Na Mwenyezi Mungu  
 Amewafadhilisha baadhi  
 yenu kuliko wengine katika  
 riziki. Na wale walio-  
 fadhilishwa hawarudishi  
 riziki zao kwa wale iliowa-  
 miliki mikono yao ya kulia  
 ili wawe sawa katika riziki  
 hiyo. Basi je, wanazikataa  
 neema za Mwenyezi  
 Mungu?**

**Katika Mambo ya Maisha  
 ya Wanadamu Kuna  
 Ishara na Neema**

Allah تعالیٰ Anawafanulia  
 washirikina ujinga wao na

ukafiri wao katika kile walichodai kuwa ni cha Allah تعالیٰ. Miongoni mwa  
 washirika, na huku wao wanakiri kuwa hao ni watumwa wa Allah تعالیٰ kama  
 walivyokuwa wanasema katika kuitikia kwao katika hijjah yao<sup>1</sup>: "Tumeitika  
 Ewe Bwana wetu kisha tumeitika, hauna mshirika isipokuwa huyo mshirika ni  
 wako, unammiliki yeye na alichokimiliki." Allah تعالیٰ Akasema Akiwapinga:  
 Ninyi hamridhii kuwa sawa na watumwa wenu katika kile tulichokuruzukuni,  
 na sasa vipi Allah تعالیٰ Hulinganishwa na watumwa Wake katika Uungu na  
 Utukufu. Kama Alivyosema katika aya nyingine:

ضَرَبَ لَكُمْ مَثَلًا مِّنْ أَنْفُسِكُمْ ۗ هَلْ لَّكُمْ مِّنْ مَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّنْ شُرَكَاءَ فِي مَآ رَزَقْنَكُمْ فَأَنْتُمْ فِيهِ سَوَاءٌ تَخَافُونَهُمْ كَخِيفَتِكُمْ أَنْفُسَكُمْ ۗ

***“Amekupigieni mfano kutokana na nafsi zenu. Je! Katika hao iliyowamiliki mikono yenu ya kulia mnao washirika katika hivyo Tulivyokuruzukuni, mkawa nyinyi katika hivyo ni sawasawa, mnawaogopa kama mnavyoogopana wenyewe kwa wenyewe?” (30:28)***

Al-Awfi amesema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما katika aya hii: Hawawashirikishi watumwa wao katika mali zao na wake zao, vipi basi wanawashirikisha watumwa Wangu katika Utawala Wangu.

Na hiyo ndiyo Kauli Yake:

أَفَبِعِزَّةِ اللَّهِ تَجْحَدُونَ.

***“Basi je, wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?”<sup>1</sup>***

Na amesema katika mapokezi mengine kutoka kwake: Basi kwa vipi mnaridhia Kwangu msichokiridhia wenyewe. Na Kauli Yake :

أَفَبِعِزَّةِ اللَّهِ تَجْحَدُونَ.

***“Basi je, wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu?”***

Maana: Wamempa Allah تعالى sehemu ya baadhi ya Alivyoviumba, mimea na wanyama wakapinga Neema Yake na wakamshirikisha pamoja Naye kitu kingine. Na kutoka kwa Al-Hasan Al-Basry رحمه الله تعالى. Amesema Umar Ibn Khatwaab رضي الله عنه alimuandikia Abi Musa Al Ash`ari رضي الله عنه barua hii:

“Tosheka na upatacho duniani, kwani Allah تعالى Amewaboresha baadhi ya waja wake kuliko wengine katika kipato kwa kuwatahini. Yule aliyepewa nafasi katika riziki, hutahiniwa vipi atamshukuru Allah تعالى na atautekeleza vipi wajibu Wake katika hicho alichompa?” Ameipokea Ibn Abi Hatim.

<sup>1</sup> Dua inayotamkwa zinapoanza ibada za Hajj, “Nimekuitika Ewe Allah...”

<sup>2</sup> At-Tabari 17:252.



وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَزْوَاجًا وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ بَيْنًا وَحَفْدَةً وَرَزَقَكُمْ  
 مِنَ الطَّيِّبَاتِ أَفَبِالْبَاطِلِ يُؤْمِنُونَ وَبِالنِّعْمَةِ اللَّهُ هُمْ يَكْفُرُونَ ﴿٧٦﴾

**72. Na Mwenyezi Mungu Amekuumbieni wake katika jinsi yenu, na Akakujaalieni kutoka kwa wake zenu wana na wajukuu, na Akakuruzukuni vitu vizuri vizuri. Basi je, wanaamini upotovu na wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu.**

### Miongoni mwa Neema na Ishara ni Kuruzukiwa Wake, Watoto na Wajukuu

Allah تعالى Anataja Neema Zake kwa waja Wake kuwa Amewaumbia wake wanaotokana na nafsi zao. Kwa kuwa ni binadamu kama wao na wana umbo kama lao. Na lau kama Angaliwaumba katika jinsi nyingine kusingepatikana kuzoweana, kupendana na kuhurumiana. Lakini kwa Rehema Zake Ameumba katika wanadamu wanaume na wanawake na Akawafanya wanawake ni wake wa wanaume. Kisha Allah تعالى Akaeleza kuwa Ameumba kutoka kwa wake, watoto na wajukuu, nao ni watoto wa watoto. Hayo ameyaeleza Ibn Abbas, Ikrima, Al'Hasan, Dhahaak na Ibn Zaid رضي الله عنهم.<sup>1</sup> Amesema Shu-uba kutoka kwa Abi Bishri kutoka kwa Said Ibn Jubair kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, hao ni mtoto na mjukuu.<sup>2</sup> Na imesemwa kuwa maana yake ni watumishi na wasaidizi, na imesemwa: Wakwe. Nimesema likiwa neno,

وَحَفْدَةً

**"...na wajukuu..."**

linahusiana na wake zenu, basi lazima madhumuni yake itakuwa watoto na watoto wa watoto na wakwe, kwa sababu hao ni watoto wa mke.

Na Kauli Yake:

وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ

**"...na Akakuruzukuni vitu vizuri vizuri..."**

Maana: Katika vinavyoliwa na vinavyonywewa. Kisha Akasema Akimkanusha Aliyemshirikisha katika ibada:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:256, 257.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:257.

أَفَبِالْبَاطِلِ يُؤْمِنُونَ

**“Basi je, wanaamini upotovu nayo.”**

Ni masanamu na wanavyomfananisha navyo.

وَبِنِعْمَتِ اللَّهِ هُمْ يَكْفُرُونَ

**“Na wanazikataa neema za Mwenyezi Mungu.”**

Maana yake: Wanazificha neema za Allah تعالى juu yao na kuzinasibisha kwa mwingine. Na katika Hadithi Sahihi:

«إِنَّ اللَّهَ يَقُولُ لِلْعَبِيدِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مُنْتَأً عَلَيْهِ: أَلَمْ أَرْزُقْكُمْ؟ أَلَمْ أُغْنِكُمْ؟ أَلَمْ أُسَخِّرْ لَكُمْ الْخَيْلَ وَالْإِبِلَ، وَأَذْرَكَ تَرَاسُ وَتَرْبِيعُ؟»

*“Hakika ya Allah Atasema Siku ya Kiama kumuambia mja akimtajia neema Alizomneemesha: Sikukuozesha? Sikukukirimu? Sikuku dhalilishia Farasi na Ngamia, na kukuacha unaongoza na unachukua robo ya ngawira.”<sup>1</sup>*

وَيَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَهُمْ رِزْقًا مِّنَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ شَيْئًا وَلَا يَسْتَطِيعُونَ ﴿٧٦﴾ فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٧٧﴾

**73. Na badala ya Mwenyezi Mungu wanawaabudu wasiowamilikia riziki kutoka mbinguni wala kwenye ardhi, wala hawawezi kitu.**

**74. Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano. Hakika Mwenyezi Mungu Anajua, na nyinyi hamjui.**

**Kupingwa Ibada ya Yoyote Asiyekuwa Allah تعالى**

Allah تعالى Anazieleza habari za washirikina ambao wameabudu pamoja na Allah kitu kingine pamoja na kuwa Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuneemesha, Kufadhili, Kuumba na Kutoa riziki, Peke Yake hana mshirika, pamoja na haya wanaabudu kisichokuwa Allah تعالى . Maana yake: masanamu na vinginevyo.

<sup>1</sup> Muslim 4:2279.

مَا لَا يَمْلِكُ لَهُمْ رِزْقًا مِّنَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ شَيْئًا

**“...wasiowamilikia riziki kutoka mbinguni wala kwenye ardhi wala hawawezi kitu...”**

Maana yake: Hawawezi kuteremsha mvua, kuotesha mimea wala miti, na wala hawamiliki hilo kwa ajili yao wenyewe. Maana yake: Hawana uwezo wa kufanya hivyo na hata kama watataka hawataweza.

Na kwa sababu hii Allah تعالى Akasema;

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ

**“Basi msimpigie Mwenyezi Mungu mifano.”**

Maana: Msimuwekee mifano.

إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Anajua, na nyinyi hamjui.”**

Maana yake: Hakika Yeye Anajua na Anashuhudia kuwa hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye na nyinyi kwa kutokujua kwenu mnamshirikisha na kingine.

\* ضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا عَبْدًا مَّمْلُوكًا لَا يَقْدِرُ عَلَى شَيْءٍ وَمَن رَزَقْنَاهُ مِنَّا رِزْقًا حَسَنًا فَهُوَ

يُنْفِقُ مِنْهُ سِرًّا وَجَهْرًا ۗ هَلْ يَسْتَوُونَ ۗ الْحَمْدُ لِلَّهِ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾

**75. Mwenyezi Mungu Anapiga mfano wa mtumwa aliyemilikiwa, asiyeweza kitu, na mwingine Tuliyemruzuku riziki njema inayotoka Kwetu, naye akawa anatoa katika riziki hiyo kwa siri na dhaahiri. Je, hao watakuwa sawa? Alhamdu Lillahi! Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui.**

## Mfano wa Muumini na Kafiri Au Ushirikina na Mungu wa Kweli

Al-Awfi amesema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: Mfano huu Allah تعالى Amempigia kafiri na muumini.<sup>1</sup> Hii ilikuwa rai ya Qatadah pia,<sup>2</sup> na ameichagua Ibn Jariri رحمه الله تعالى.<sup>3</sup> Kwa hiyo mtumwa aliyemilikiwa ambaye hawezi lolote ni kama Kafiri. Na mwenye kupewa riziki nzuri, naye anatoa kutoka kwenye riziki hiyo, kwa siri na dhahiri, huyo ndiye Muumini. Na Ibn Najihi kutoka kwa Mujahid amesema huo ni mfano uliotolewa kwa sanamu na Haki ambaye ni Allah تعالى. Je, huyu na huyu wanalingana?<sup>4</sup> Na ilipokuwa tofauti kati yao iko wazi hakuna asiyeijua isipokuwa mpumbavu kabisa. Allah تعالى Akasema:

الْحَمْدُ لِلَّهِ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

***“Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu lakini wengi katika wao hawajui”.***

وَصَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا رَجُلَيْنِ أَحَدُهُمَا أَبْكَمُ لَا يَقْدِرُ عَلَى شَيْءٍ وَهُوَ كَلٌّ عَلَى مَوْلَاهُ  
أَيْنَمَا يُوَجِّههُ لَا يَأْتِ بِخَيْرٍ ۗ هَلْ يَسْتَوِي هُوَ وَمَنْ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَهُوَ عَلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٧٦﴾

***76. Na Mwenyezi Mungu Anapiga mfano wa watu wawili. Mmoja wao ni bubu, hawezi chochote, naye ni mzigo kwa bwana wake. Popote anapomuelekeza haleti kheri. Je! Huyu anaweza kuwa sawa na yule anayeamrisha uadilifu, naye yuko juu ya njia lliyonyooka.”***

## Mfano Mwingine

Mujahid amesema: Huu pia madhumuni yake ni: Sanamu na Allah تعالى. Anakusudia kuwa sanamu ni bubu na wala halitamki kheri wala chochote na haliwezi kitu kabisa, si maneno wala matendo, na pamoja na hayo ni tegemezi na mzigo tu juu ya bwana wake (anayeliabudu).

أَيْنَمَا يُوَجِّهُهُ

***“...popote amuelekezapo...”***Maana: Ampelekapo,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:261

<sup>2</sup> At-Tabari 17:261.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:263.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:263.

لَا يَأْتِ بِخَيْرٍ<sup>ط</sup>

**“...haleti kheri.”**

Wala hafanikishi juhudi zake.

هَلْ يَسْتَوِي

**“Je! Huyo anaweza kuwa sawa...”**

Maana yake: Mwenye sifa hizi,

وَمَنْ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ<sup>ص</sup>

**“...na yule anayeamrisha uadilifu.”**

Hivyo maneno yake ni ya haki na matendo yake ya sawa.

وَهُوَ عَلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

**“...Naye yuko juu ya njia iliyonyooka...”**

Na Al-Awfi amesema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: Huo ni mfano wa kafiri na muumini, pia kama tulivyosema awali.

\* \* \*

وَلِلَّهِ غَيْبُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ  
 وَمَا أَمْرُ السَّاعَةِ إِلَّا كَلَمْحِ الْبَصَرِ  
 أَوْ هُوَ أَقْرَبُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ  
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٧٧﴾ وَاللَّهُ  
 أَخْرَجَكُمْ مِنْ بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ لَا  
 تَعْلَمُونَ شَيْئًا وَجَعَلَ لَكُمُ  
 السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ لَعَلَّكُمْ  
 تَشْكُرُونَ ﴿٧٨﴾ أَلَمْ يَرَوْا إِلَى  
 الطَّيْرِ مُسَخَّرَاتٍ فِي جَوْ السَّمَاءِ  
 مَا يُمَسِّكُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ  
 لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٧٩﴾

77. Na siri zote za katika mbingu na ardhi ziko kwa Mwenyezi Mungu. Wala halikuwa jambo la Saa (ya Kiyama) ila kama kupepesa kwa jicho, au akali ya hivyo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

وَلِلَّهِ غَيْبُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَمَا أَمْرُ السَّاعَةِ إِلَّا كَلَمْحِ  
 الْبَصَرِ أَوْ هُوَ أَقْرَبُ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٧٧﴾  
 وَاللَّهُ أَخْرَجَكُمْ مِنْ بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ لَا تَعْلَمُونَ شَيْئًا  
 وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ لَعَلَّكُمْ  
 تَشْكُرُونَ ﴿٧٨﴾ أَلَمْ يَرَوْا إِلَى الطَّيْرِ مُسَخَّرَاتٍ فِي جَوْ  
 السَّمَاءِ مَا يُمَسِّكُهُنَّ إِلَّا اللَّهُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ  
 يُؤْمِنُونَ ﴿٧٩﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ بُيُوتِكُمْ سَكَنًا  
 وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ جُلُودِ الْأَنْعَامِ بُيُوتًا تَسْتَخِفُّونَهَا يَوْمَ  
 ظَعْنِكُمْ وَيَوْمَ إِقَامَتِكُمْ ۗ وَمِنْ أَصْوَابِهَا وَأَوْبَارِهَا  
 وَأَشْعَارِهَا أَثْنَا وَمِئْتًا إِلَىٰ حِينٍ ﴿٨٠﴾ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِمَّا  
 خَلَقَ ظِلَالًا وَجَعَلَ لَكُمْ مِنَ الْجِبَالِ أَكْنَانًا وَجَعَلَ  
 لَكُمْ سَرَابِيلَ تَقِيكُمُ الْحَرَّ وَسَرَابِيلَ تَقِيكُمْ بَأْسَكُمْ ۗ  
 كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تُسْلِمُونَ ﴿٨١﴾  
 فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ الْمَمِينُ ﴿٨٢﴾ يَعْرِفُونَ  
 نِعْمَتَ اللَّهِ ثُمَّ يُنْكِرُونَهَا وَأَكْثَرُهُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٨٣﴾

78. Na Mwenyezi Mungu Amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na Amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.

79. Je! Hawawaoni ndege walivyowat'iifu katika anga la mbingu? Hapana mwenye kuwashika isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanaoamini.

### Ghaibu ni ya Allah تعالیٰ Pekee, na Ndiye Mwenye Elimu ya Kiyama

Allah تعالیٰ Anaelezea ukamilifu wa Elimu na Uwezo Wake juu ya vitu katika Elimu Yake ya ghaibu mbinguni na ardhini. Na kuwa Ujuzi wa ghaibu ni Wake Yeye tu. Hakuna anayeijua ghaibu isipokuwa amjulishe Yeye juu ya Anachokitaka na katika Uwezo Wake uliyokamilika ambao haukosei, wala haupingwi. Na kwamba Anapotaka kitu Hukiambia tu kuwa na kinakuwa, kama Alivyosema:

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾

**“Na amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.”**  
(54:50).

Maana yake: Basi kinakuwa anachokitaka kama kupepesa jicho tu na hivihivi ndivyo Alivyosema hapa:

وَمَا أَمْرُ السَّاعَةِ إِلَّا كَلَمْحِ الْبَصَرِ أَوْ هُوَ أَقْرَبُ ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥١﴾

**“Wala halikuwa jambo la saa ile ya kiama ila ni kama kupepesa jicho au ni karibu zaidi hakika Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”** Kama Alivyosema:

مَا خَلَقْنَاكُمْ وَلَا نَبْعَثُكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ ﴿٢٨﴾

**“Hakukuwa Kuumbwa kwenu, wala Kufufuliwa kwenu ila ni kama nafsi moja tu.”** (31:28)

### Miongoni mwa Neema za Allah تعالیٰ Alizowapa Wanaadamu ni Masikio, Macho na Nyoyo

Kisha Allah تعالیٰ Akazitaja Neema Zake kwa waja Wake katika Kuwatoa wao toka matumboni mwa mama zao wakiwa hawajui kitu, kisha baada ya hali hii Anawapa usikivu ambao kwake wanazielewa sauti, na Anawapa macho ambayo kwayo wanavitambua vinavyoonekana, na nyoyo. Kwa maana ya akili, ambazo chanzo chake ni katika moyo. Wapo waliosema chanzo chake ni katika ubongo, kwa kutumia akili mwanadamu anaweza kutenganisha kati ya vyenye madhara na vyenye manufaa. Na nguvu hizi na ufahamu huu upo kwa mwanadamu taratibu kidogo kidogo. Kila anapokua anaongezeka katika kusikia kwake, kuona kwake na akili yake mpaka anafikia kupevuka kwake.

Allah تعالى Amempa vitu hivi mwanadamu ili aweze kumuabudu Mola Wake hivyo atakitumia kila kiungo na kila nguvu katika kumtii Mola wake. Kama ilivyokuja katika Sahih Bukhari kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

«يَقُولُ تَعَالَى: مَنْ عَادَى لِي وَلِيًّا فَقَدْ بَارَزَنِي بِالْحَرْبِ، وَمَا تَقَرَّبَ إِلَيَّ عَبْدِي بِشَيْءٍ أَحْضَرُ مِنْ أَدَاءٍ مَا افْتَرَضْتُ عَلَيْهِ، وَلَا يَزَالُ عَبْدِي يَتَقَرَّبُ إِلَيَّ بِالتَّوَابِلِ حَتَّىٰ أُجِيبَهُ، فَإِنَّا أَحْبَبْتُهُ كُنْتُ سَمْعَهُ الَّذِي يَسْمَعُ بِهِ، وَبَصَرَهُ الَّذِي يُبْصِرُ بِهِ، وَيَدَهُ الَّتِي يَبْطِشُ بِهَا، وَرِجْلَهُ الَّتِي يَمْشِي بِهَا، وَلَئِن سَأَلَنِي لِأَعْطَيْتَهُ، وَلَئِن دَعَانِي لِأَجِيبْتَهُ، وَلَئِن اسْتَعَاذَ بِي لِأَعِيذَنَّهُ، وَمَا تَرَدَّدْتُ فِي شَيْءٍ أَنَا فَاعِلُهُ تَرَدُّدِي فِي قَبْضِ نَفْسِ عَبْدِي الْمُؤْمِنِ يَكْرَهُ الْمَوْتَ وَأَكْرَهُ مَسَاءَتَهُ وَلَا بُدَّ لَهُ مِنْهُ»

*“Anasema Allah: Atayemfanyia uadui walii Wangu basi huyo Amenitambia kwa vita, na hakujikurubisha Kwangu mja kwa kitu bora zaidi kuliko kutekeleza Niliyomuajibishia, na ataendelea kujikurubisha Kwangu mja Wangu kwa ibada za ziada mpaka Nitampenda na Nikishampenda Nitakuwa ni sikio lake ambalo kwalo anasikia, na jicho lake ambalo kwalo anaona, na mkono wake ambao kwa huo anashika, na mguu wake ambao anatembelea. Na kama ataniomba Nitampa na akinitaka himaya Nitamlinda na sijiulizi katika kitu Nikifanyacho kama Ninavyojiuliza katika kuichukua nafsi ya mja Wangu Muumini. Hapendi kufa Nami Sipendi Nimuudhi lakini lazima Nifanye hivyo.”<sup>1</sup>*

Maana ya Hadithi hii ni kwamba mja anapotii kwa dhati basi matendo yake yote yatakuwa kwa ajili ya Allah تعالى, hasikii isipokuwa kwa ajili ya Allah تعالى, hashiki wala hatembe isipokuwa katika kumtii Allah تعالى, na katika kutekeleza yote hayo anaomba msaada kwa Allah تعالى. Ndiyo maana baadhi ya riwaya za Hadithi hii zina nyongeza baada ya maneno, “mguu wake ambao kutembelea,” kuna nyongeza ya maneno yafuatayo,

«فَبِي سَمْعٍ، وَبِي بَصِيرٍ، وَبِي يَبْطِشُ، وَبِي يَمْشِي»

*“Kwa ajili Yangu tu anasikia, na kwa ajili Yangu tu anaangalia, na kwa ajili Yangu tu anakamata, na kwa sababu Yangu tu anatembea.”<sup>2</sup>*

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 11:348.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 11:352.



Na kwa sababu hii Allah تعالى Amesema:

وَجَعَلَ لَكُمْ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

**“...Na Amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru...”**

Sawa na Kauli Yake Allah تعالى katika aya nyingine

قُلْ هُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمْ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿٦٧﴾ قُلْ هُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ وَإِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٦٨﴾

**“Sema: Yeye Ndiye Aliyekuumbeni tangu mwanzo, na Akakupeni masikio na macho, na nyoyo. Ni kidogo kabisa shukrani zenu, Sema: Yeye Ndiye Aliyekutawanyeni katika ardhi, na Kwake mtakusanywa.” (67:23-24)**

### Katika Kuwadhalilisha Ndege Angani Kuna Alama

Kisha Allah تعالى Akawazindua waja Wake kuangalia ndege walivyodhalilishwa kati ya mbingu na ardhi, huko hakuna anayemzuia asianguke isipokuwa Allah تعالى kwa Uwezo Wake, ambaye Amemuumbia nguvu inayofanya hivyo.

Kama Alivyosema Allah تعالى katika Suratil Mulk,

أُولَئِكَ يَرَوْنَ إِلَى الطَّيْرِ فَوْقَهُمْ صَفَّتْ وَيَقْبِضْنَ ۗ مَا يُمَسِّكُهُنَّ إِلَّا الرَّحْمَنُ ۗ إِنَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ  
بَصِيرٌ ﴿١٩﴾

**“Kwani hawawaoni ndege walioko juu yao namna wanavyozikunjua mbawa zao, na kuzikunja? Hawawashikilii ila Mwingi wa Rehema. Hakika Yeye ni Mwenye Kuona kila kitu.” (67:19)**

Na hapa Akasema:

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ

**“Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanaoamini.”**

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِنْ بُيُوتِكُمْ سَكَنًا وَجَعَلَ لَكُمْ مِنْ جُلُودِ الْأَنْعَامِ بُيُوتًا تَسْتَخِفُّونَهَا  
 يَوْمَ ظَعْنِكُمْ وَيَوْمَ إِقَامَتِكُمْ ۗ وَمِنْ أَصْوَابِهَا وَأَوْبَارِهَا وَأَشْعَارِهَا أَثْنَا وَمِئَةً إِلَىٰ حِينٍ  
 ۝ وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِمَّا خَلَقَ ظِلَالًا وَجَعَلَ لَكُمْ مِنَ الْجِبَالِ أَكْنَانًا وَجَعَلَ لَكُمْ  
 سَرَابِيلَ تَقِيكُمُ الْحَرَّ وَسَرَابِيلَ تَقِيكُم بَأْسَكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ لَعَلَّكُمْ  
 تُسَلِّمُونَ ۝ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ الْمُبِينُ ۝ يَعْرِفُونَ نِعْمَتَ اللَّهِ ثُمَّ  
 يُنْكِرُونَهَا وَأَكْثَرُهُمُ الْكَافِرُونَ ۝

**80. Na Mwenyezi Mungu Amekujaalieni majumba yenu yawe ni maskani yenu, na Amekujaalieni kutokana na ngozi za wanyama nyumba mnazoziona nyepesi wakati wa safari zenu na wakati wa kutua kwenu. Na kutokana na sufi zao na manyoya yao na nywele zao mnafanya matandiko na mapambo ya kutumia kwa muda.**

**81. Na Mwenyezi Mungu Amekufanyieni vivuli katika vitu Alivyo viumba, na Amekufanyieni maskani milimani, na Amekufanyieni nguo za kukukingeni na joto, na nguo za kukukingeni katika vita vyenu. Ndio hivyo Anakutimizieni Neema Zake ili mpate kut'ii.**

**82. Basi wakikengeuka lilio juu yako wewe ni kufikisha ujumbe wazi wazi.**

**83. Wanazijua neema za Mwenyezi Mungu, kisha wanazikanusha; na wengi wao ni makafiri.**

### **Nyumba, Samani na Nguo ni Miongoni mwa Neema za Allah**

Allah تعالى Anaelezea ukamilifu wa Neema Zake kwa waja Wake kwa kile Alichowajaalia. Nacho ni nyumba ambazo ni makazi yao wanakaa humo na wanajistiri kwa nyumba hizo, na matumizi mengine. Pia Amewajaalia kutokana na ngozi za wanyama, kama Ngamia, Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo, Nyumba wanaziona nyepesi kuzibeba katika misafara yao ili wazisimike wanapoweka kambi safarini na nyumbani.

Na kwa sababu hii Akasema:

تَسْتَخِفُّونَهَا يَوْمَ ظَعْنِكُمْ وَيَوْمَ إِقَامَتِكُمْ

**“...mnazoziona nyepesi wakati wa safari zenu na wakati wa kutua kwenu.”**

وَمِنْ أَصْوَابِهَا وَأَوْبَارِهَا وَأَشْعَارِهَا

**“Na kutokana na sufi zao na manyoya yao na nywele zao.”**

Maana: Kondoo na manyoya yao, ngamia na nywele zao,

أُنثَىٰ

**“...matandiko na mapambo...”**

Mnatengeneza vyombo na vifaa vya kutumia kwa muda mrefu navyo ni mali. Na imesemwa kuwa ni vyombo vya kutumia kwa muda mfupi. Kadhalika imetajwa kuwa ni nguo. Lakini iliyo sahihi ni kuwa maana yake ni pana kuliko hivi ilivyotajwa.

Mbali na hivyo hutengenezwa kutoka humo mabusati, nguo na vinginevyo, na yafanywa mali na biashara. Na Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema: *Al-Thath* ni vyombo.<sup>1</sup> Pia Mujahid, Ikrima, Said Ibn Jubair, Al Hasan, Atwiya Al-Awfi, Atwaa-Al-Khurrasaani, Adh-Dhahaak na Qatadah wamesema hivyo hivyo. Na Kauli Yake:

إِلَىٰ حِينٍ

**“...kwa muda...”**

Maana yake: Muda uliyotajwa na wakati maluum.

**Kivuli, Milima, Kanzu za Nguo na Chuma Pia ni katika Neema za Allah**

وَاللَّهُ جَعَلَ لَكُمْ مِمَّا خَلَقَ ظِلَالًا

**“Na Mwenyezi Mungu Amekufanyieni vivuli katika vitu Alivyoviumba.”**

Qatadah amesema: Anakusudia miti<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:268.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:269.

وَجَعَلَ لَكُمْ مِّنَ الْجِبَالِ أَكْنَانًا

*"...na Amekufanyieni maskani milimani..."*

Maana yake: Ngome.

جَعَلَ لَكُمْ سَرَائِلَ تَقِيكُمْ الْحَرَّ

*"Amekufanyieni nguo za Kukukingeni na joto."*

Nazo ni nguo kutokana na pamba na katani na sufu.

وَسَرَائِلَ تَقِيكُمْ بِأَسْكُمُ

*"...na nguo za Kukingeni katika vita vyenu..."*

Kama dereya za chuma na suweta zenye kowa, na zingine.

كَذَلِكَ يُتِمُّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ

*"Ndio hivyo Anakutimizieni Neema Zake."*

Hivyo, Anakutimizieni haja zenu ili yawasaidie katika mambo yenu, na ili muweze kumtii na kumuabudu.

لَعَلَّكُمْ تُسَلِّمُونَ

*"...Ili Mnyenyekee Kwake..."*

Hivi hivi ndivyo walivyoifasiri Jamhuri na wakaisoma kwa kutia *kasiri laam* 'Tuslimuun' maana, inatokana na *Al-Islaam* (Uislamu).

**Hakuna Wajibu kwa Mtume Isipokuwa Kufikisha Ujumbe**

Na Kauli Yake:

فَإِنْ تَوَلَّوْا

*"...Basi wakikengeuka..."*

Maana: Baada ya ubainifu huu na neema hii,

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ الْأَمِينُ

*"...lilio juu yako wewe ni kufikisha ujumbe wazi wazi...."*

Na umeshawatekelezea.

يَعْرِفُونَ نِعْمَتَ اللَّهِ ثُمَّ يُنْكِرُونَهَا

**“...Wanazijua neema za Mwenyezi Mungu, kisha wanazikanusha...”**

Maana yake: Wanaelewa kuwa Allah تعالى Ndiye Aliyewapa hivyo. Naye Ndiye Aliyewafadhili hayo, pamoja na haya wanamkanusha huyo na wanaabudu pamoja na Yeye kitu kingine, na wanasibisha nusra na riziki kwa wengine.

وَأَكْثَرُهُمُ الْكَافِرُونَ

**“...na wengi wao ni makafiri...”**

\* \* \*

وَيَوْمَ نَبْعَثُ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا ثُمَّ لَا يُؤَدَّبُ لِلَّذِينَ  
 كَفَرُوا وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٨٤﴾ وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ ظَلَمُوا  
 الْعَذَابَ فَلَا تُخَفِّفْ عَنْهُمْ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٨٥﴾ وَإِذَا  
 رَأَى الَّذِينَ أَشْرَكُوا شُرَكَاءَهُمْ قَالُوا رَبَّنَا هَؤُلَاءِ  
 شُرَكَائُونَا الَّذِينَ كُنَّا نَدْعُوا مِنْ دُونِكَ ۗ فَأَلْقَوْا إِلَيْهِمُ  
 الْقَوْلَ إِنَّكُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٨٦﴾ وَالْقَوْلَ إِلَى اللَّهِ يَوْمَئِذٍ  
 أَسْلَمَ ۗ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٨٧﴾ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ  
 بِمَا كَانُوا يُفْسِدُونَ ﴿٨٨﴾ وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ  
 شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِنْ أَنْفُسِهِمْ ۗ وَجَعَلْنَا بِلِكِّ شَهِيدًا عَلَى  
 هَؤُلَاءِ ۗ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تَبْيِينًا لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى  
 وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ ﴿٨٩﴾ \* إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ  
 وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَايِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ  
 وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ ۗ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٩٠﴾

وَيَوْمَ نَبْعَثُ مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا ثُمَّ  
 لَا يُؤَدَّبُ لِلَّذِينَ كَفَرُوا وَلَا هُمْ  
 يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٨٤﴾ وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ  
 ظَلَمُوا الْعَذَابَ فَلَا تُخَفِّفْ عَنْهُمْ وَلَا  
 هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٨٥﴾ وَإِذَا رَأَى  
 الَّذِينَ أَشْرَكُوا شُرَكَاءَهُمْ قَالُوا  
 رَبَّنَا هَؤُلَاءِ شُرَكَائُونَا الَّذِينَ كُنَّا  
 نَدْعُوا مِنْ دُونِكَ ۗ فَأَلْقَوْا إِلَيْهِمُ  
 الْقَوْلَ إِنَّكُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٨٦﴾ وَالْقَوْلَ  
 إِلَى اللَّهِ يَوْمَئِذٍ أَسْلَمَ ۗ وَضَلَّ  
 عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٨٧﴾  
 الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ  
 اللَّهِ زِدْنَهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ بِمَا  
 كَانُوا يُفْسِدُونَ ﴿٨٨﴾

84. Na siku Tutakapowainua kutokana na kila umma shahidi, kisha hawataruhusiwa waliokufuru wala hawataachiliwa kutaka radhi.

85. Na waliodhulumu watakapoiona adhabu hawatapunguziwa hiyo adhabu, wala hawatapewa muhula.

86. Na walioshirikisha watakapowaona hao waliowashirikisha na Mwenyezi Mungu, watasema: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio washirikishwa wetu ambao tulikuwa tukiwaabudu badala Yako. Ndipo wale watakapowatupia kauli: Hakika nyinyi ni waongo!

**87. Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya Mwenyezi Mungu, na yatapotea waliyokuwa wakiyazua.**

**88. Wale waliokufuru na kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu Tutawazidishia adhabu juu ya adhabu, kwa walivyokuwa wakifisidi.**

### Hali ya Washirikina Siku ya Kukusanywa Siku ya Hesabu

Allah تعالى Anaeleza hali ya washirikina siku ya kurejea kwao Akhera – na kuwa Atamuinua shahidi katika, kila umma. Maana: Mtume wao atoe ushahidi kuhusu walivyoitikia ujumbe waliofikishiwa kutoka kwa Allah تعالى.

ثُمَّ لَا يُؤَدِّنُ لِلَّذِينَ كَفَرُوا

**“...kisha hawataruhusiwa waliokufuru...”**

Maana: Hawataruhusiwa kutoa udhuru wowote. Kama ilivyo katika Kauli Yake:

هَذَا يَوْمٌ لَا يَنْطِقُونَ ﴿٣٦﴾ وَلَا يُؤَدِّنُ لَهُمْ فَيَعْتَدِرُونَ ﴿٣٧﴾

**“...Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu. Wala hawataruhusiwa kutoa udhuru...”. (77:35-36)**

Na kwa sababu hii Akasema:

وَلَا هُمْ يُسْتَعْتَبُونَ ﴿٤١﴾ وَإِذَا رَأَوْا الَّذِينَ ظَلَمُوا

**“...wala hawataachiliwa kutaka radhi. Na waliodhulumu watakapoiona...”**

Maana yake: Waliomshirikisha.

الْعَذَابِ فَلَا تُخَفِّفُ عَنْهُمْ

**“...adhabu hawatapunguziwa...”**

Maana: Haitacheleweshwa hata saa moja.

وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ

**“...wala hawatapewa muhula...”**

Maana yake: Hawatacheleweshewa bali watachukuliwa haraka kutoka mahali pa mkusanyiko bila ya hisabu. Kisha italetwa Jahanamu ikiongozwa kwa hatamu sabini elfu, huku kila hatamu ikiwa na malaika sabini elfu, itatokeza kwa watu kutoka katika Jahanamu na itatoa pumzi hatabaki mtu ila atapiga magoti, na hapo Jahanamu itasema: ‘Mimi nimewakilishwa kwa kila jabari mkaidi, aliyemshirikisha Allah تعالى.’ Na kwa kadha wa kadha, na utazitaja aina za watu kama ilivyokuja katika Hadithi kisha utawazoa na utawaokota hapo katika kisimamo kama ndege anavyookota nafaka.

Amesema Allah تعالى:

إِذَا رَأَتْهُمْ مِّن مَّكَانٍ بَعِيدٍ سَمِعُوا لَهَا تَغِيْظًا وَزَفِيرًا ﴿١٤﴾ وَإِذَا أَلْقَا مِنْهَا مَكَانًا صَبِيحًا  
مُّقْرِنِينَ دَعَوْا هُنَالِكَ ثُبُورًا ﴿١٥﴾ لَا تَدْعُوا الْيَوْمَ ثُبُورًا وَجِدًّا وَادْعُوا ثُبُورًا كَثِيرًا ﴿١٦﴾

**“Ule Moto ukiwaona tangu mahali mbali wao watasikia hasira yake na mngurumo wake. Na watakapotupwa humo mahali dhiki, hali wamefungwa, wataomba wafe. Msiombe kufa mara moja bali mfe mara nyingi!” (25:12-14)**

وَرَاءَ الْمَجْرُمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُّوَافِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿١٧﴾

**“Na wakhalifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.”**

لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا يَكْفُونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ وَلَا هُمْ  
يُنصَرُونَ ﴿١٨﴾ بَلْ تَأْتِيهِمْ بَغْتَةً فَتَبْهَتُهُمْ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ رَدَّهَا وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿١٩﴾

**“Lau wangelijua wale waliokufuru wakati ambao hawatauziua Moto kwenye nyuso zao wala migongo yao, na wala hawatanusuriwa! Bali utawafikia kwa ghafla, na utawashitua na wala hawataweza kuurudisha, wala hawatapewa muhula!”**



## Miungu ya Washirikina Itawakataa Katika Kipindi Wanapowahitaji Mno

Kisha Allah تعالى Akaelezea kuhusu miungu ya washirikina itavyowakataa washirikina kipindi ambacho washirikina wataihitaji mno miungu yao hiyo, Akasema

وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ أَشْرَكُوا شُرَكَاءَهُمْ

**“...Na walioshirikisha watakapowaona hao waliowashirikisha...”**

Maana yake: Ambao walikuwa wanawaabudu duniani,

قَالُوا رَبَّنَا هَؤُلَاءِ شُرَكَائُنَا الَّذِينَ كُنَّا نَدْعُوا مِنْ دُونِكَ ۗ فَأَلْقَوْا إِلَيْهِمُ الْقَوْلَ إِنَّكُمْ لَكَاذِبُونَ

**“...watasema: Mola wetu Mlezi! Hawa ndio washirikishwa wetu ambao tulikuwa tukiwaabudu badala Yako. Ndipo wale watakapo watupia kauli: Hakika nyinyi ni waongo!”**

Maana yake: Miungu itawaambia: “Nyinyi ni waongo sisi hatukuwaamuru kutuabudu.” Kama Alivyosema تعالى:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَنِ دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ﴿٥٥﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٥٦﴾

**“Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao. Na ambao watu watakapokusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.” (46:5-6)** Na Amesema Allah تعالى:

وَاتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ ءَالِهَةً لَّيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٨١﴾ كَلَّا ۗ سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٨٢﴾

**“Na wamechukua miungu mingine badala ya Mwenyezi Mungu ili ati iwape nguvu. Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao.” (19:81-82)**

Na Amesema Al-Khalili عليه السلام:

نُورَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ يَكْفُرُ بَعْضُكُمْ بِبَعْضٍ

**“Kisha Siku ya Kiyama mtakataana nyinyi kwa nyinyi, na mtalaaniana nyinyi kwa nyinyi.” (29:25)**

وَقِيلَ ادْعُوا شُرَكَاءَكُمْ

**“Na itasemwa: Waiteni hao miungu wa kishirikina wenu!” (28:64)**

Na Aya katika maudhui haya ziko nyingi

**Kila Kitu Siku ya Kiyama Kitajisalimisha kwa Allah تعالى**

وَأَلْقُوا إِلَى اللَّهِ يَوْمَئِذٍ أَلْسَلَمًا

**“Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya Mwenyezi Mungu.”**

Qatada na Ikrima wamesema: Wamedhalilika na watajisalimisha siku hiyo.<sup>1</sup>

Wote watajisalimisha kwa Allah تعالى kwani kila mmoja atasikia na kutii. Ni kama Kauli Yake:

أَسْمِعْ بِهِمْ وَأَبْصِرْ يَوْمَ يَأْتُونَنَا

**“Watasikia na wataona vizuri vilioje Siku watakayotufikia!” (19:38)**

Maana yake: Ni kusikia kulioje kwa wao na kuona kulioje kwao siku hiyo.

Na Amesema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا

**“Na ungesi waona wakosefu wanavyoinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao Mlezi, (wakisema): Mola wetu Mlezi! Tumeshona, na tumeshasikia.” (32:12)**

وَعَسَتْ أَلْوَجُوهُ لِحَيِّ الْقِيَوْمِ<sup>ط</sup> \*

***“Na zitadhalilika nyuso mbele ya Aliye Hai Milele.” (20:111).***

Maana yake: Zitanyenyekea na zitadhalilika, zitatulizana na zitajisalimisha. Na Kauli Yake:

وَأَلْقُوا إِلَى اللَّهِ يَوْمَئِذٍ أَسْلَمًا<sup>ط</sup> وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ

***“Na siku hiyo watasalimu amri mbele ya Mwenyezi Mungu, na yatapotea waliyokuwa wakiyazua.”***

Maana yake: Kimeondoka na kunyauka walichokuwa wanakiabudu kwa kumzulia tu Allah تعالى, basi hawatampata wa kuwanusuru na adhabu wala msaidizi wala muokozi

### **Wale Miongoni mwa Waharibifu Waliyowaharibu Wengine Watapata Adhabu Kubwa**

Kisha Akasema:

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَاهُمْ عَذَابًا

***“Waliokufuru na wakawazuwia wengine kuingia katika Dini ya Allah Tukawaongezea adhabu.”***

Maana yake: Adhabu juu ya ukafiri wao na adhabu juu ya kuwazuwia kwao watu kuifuata Dini ya haki. Kama ilivyokuja katika Kauli Yake تعالى:

وَهُمْ يَنْهَوْنَ عَنْهُ وَيَنْعَوْنَ عَنْهُ<sup>ط</sup>

***“Nao wanawakataza wengine kwenye Dini hiyo nao wanakuwa mbali na Dini hiyo.”***

Maana: Wanawakataza watu kuifuata na wanakuwa mbali wao na Dini hiyo,

وَإِنْ يُهْلِكُونَ إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ

***“Nao hawaangamizi ila nafsi zao tu, wala wao hawatambui.”***

Pia na hakuna wanachokiangamiza isipokuwa nafsi zao. Na wenyewe hawajui. Na hii ni dalili ya tofauti ya makafiri katika adhabu yao kama wanavyo tofautiana waumini katika vyeo vyao peponi na daraja zao. Kama Alivyosema,

قَالَ لِكُلِّ ضَعْفٌ وَلَيْكِن لَّا تَعْلَمُونَ

**“Atasema: Itakuwa kwenu nyote marudufu, lakini nyinyi hamjui tu...”**

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِّنْ أَنْفُسِهِمْ<sup>ط</sup> وَجَعَلْنَا بِلِكِّ شَهِيدًا عَلَىٰ هَتُولَاءِ<sup>ع</sup>  
وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ بَيِّنَاتًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً<sup>ط</sup> وَنُذْرًا لِّلْمُسْلِمِينَ ﴿٨٩﴾

**89. Na (waonye) siku Tutakapo wainua mashahidi katika kila umma wakiwashuhudia kwa yanayotokana na wao, na Tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hao. Na Tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.**

**Kila Nabii Atatoa Ushahidi kwa Umma Wake Siku ya Kufufuliwa**

Allah ﷻ Anasema Akimueleza mja Wake na Mtume Wake Muhammad ﷺ

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِّنْ أَنْفُسِهِمْ<sup>ط</sup> وَجَعَلْنَا بِلِكِّ شَهِيدًا عَلَىٰ هَتُولَاءِ<sup>ع</sup>

**“Na (waonye) siku Tutakapowainua mashahidi katika kila umma wakiwashuhudia kwa yanayotokana na wao, na Tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hao.”**

Maana yake: Umma wako. Yaani: Kumbuka siku hiyo na misukosuko yake. Na Alichokupa Allah ndani ya siku hiyo nacho ni heshima kubwa na cheo cha juu. Na aya hii inafanana na Aya ambayo aliyoishia Abdullahi Ibn Mas’ud wakati alipomsomea Mtume ﷺ mwanzo wa Surati Nisaa, alipofika kwenye Kauli Yake:

فَكَيْفَ إِذَا جَعَلْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا وَجَعَلْنَا بِكَ عَلَىٰ هَتُولَاءِ<sup>ع</sup> شَهِيدًا ﴿٩٠﴾

**“Itakuwaje Tunapouleta kila umma shahidi wake na Tukakuleta kuwa shahidi juu ya hawa.” (4:41).**

Mtume ﷺ akamuambia, ﴿حَسْبُكَ﴾

**“Basi inakutosha.”** Akasema Ibn Mas’ud رضي الله عنه, ‘nikageuka nikayakuta macho yake yanatoa machozi.’<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:99.

## Qur'an ni Ufafanuzi wa Kila Kitu

وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تَبَيِّنًا لِّكُلِّ شَيْءٍ

**"Na Tumekuteremshia kitabu chenye ufafanuzi wa kila kitu."**

Ibn Mas'uud رضي الله عنه amesema: Tumefafanuliwa kila elimu katika Qur'an.<sup>1</sup> Bila shaka Qur'an imekusanya kila elimu ya manufaa kama vile habari ya waliopita na elimu itakayokuja na kila halali na haramu na wanachokihitaji watu katika dunia yao na dini yao, maisha yao na marejeo yao.

وَهُدًى

**"...na ni uwongofu,"**

وَرَحْمَةً وَنُصْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ

**"...na rehema, na bishara kwa Waislamu."** Na amesema Al-Auzai:

وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تَبَيِّنًا لِّكُلِّ شَيْءٍ

**"Na Tumekuteremshia kitabu chenye kubainisha kila kitu."**

Maana: Kwa Sunna.<sup>2</sup> Ndiyo sababu maneno yafuatayo,

وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ

**"Na Tumekuteremshia kitabu..."** Yanafuatia mara tu baada ya maneno hayo.

وَجَعَلْنَا بَلَكَ شَهِيدًا عَلَىٰ هَتُولَاءِ

**"Na Tukakuleta ukiwa shahidi juu ya hawa."**

Ni kuwa madhumuni – na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi - bila shaka Aliyekulazimisha kukitangaza kitabu Alichokuteremshia Atakuuliza Siku ya Kiama.

فَلَنَسْأَلَنَّ الَّذِينَ أُرْسِلَ إِلَيْهِمْ وَلَنَسْأَلَنَّ الْمُرْسَلِينَ ﴿٦﴾

**"... bila shaka Tutawauliza ambao Tumewapelekea na Tutawauliza Mitume..." (7:6)**

Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:269.

<sup>2</sup> Ad-Dur Al-Manthur 5:158.

فَوَرَبِّكَ لَنَسَعَلَنَّاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٦﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

**“...Naapa kwa Mola wako Tutawauliza wote. Wote waliyokuwa wanayafanya” (15:92 - 93)**

يَوْمَ يَجْمَعُ اللَّهُ الرُّسُلَ فَيَقُولُ مَاذَا أُجِبْتُمْ قَالُوا لَا عِلْمَ لَنَا إِنَّا كُنَّا نَعْلَمُ الْغُيُوبَ ﴿١٥﴾

**“Siku Allah Atawakusanya Mitume na Atasema: Mmejibiwa nini watasema hatuna tunachokijua bila shaka Wewe Ndiye Mjuzi wa ghaibu.” (5:109).**

إِنَّ الَّذِي فَرَضَ عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لَرَأْدُكَ إِلَىٰ مَعَادٍ ﴿١٦﴾

**“Hakika Aliyekulazimisha kuifuata Qur’ani hapana shaka Atakurudisha pahala pa marejeo.” (28:85)**

Hii ni moja ya kauli nyingi nayo ni mtazamo mzuri.

\* إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَايَ ذِي الْقُرْبَىٰ وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ  
وَالْبَغْيِ يَعِظُكُمْ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿١٦﴾

**90. “Hakika Mwenyezi Mungu Anaamrisha Kufanya uadilifu, na hisani, na Kuwapa jamaa; na Anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka...”**

### Amri ya Kufanya Uadilifu na Kufanya Hisani

Allah تعالى Anaeleza kuwa Anawaamuru waja Wake uadilifu na Anatoa wito wa Kufanya hisani. Kama ilivyo katika Kauli Yake تعالى:

وَإِنْ عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ ۗ وَإِنَّ صَبْرًا لَّهُوَ خَيْرٌ لِلصَّابِرِينَ ﴿١٦﴾

**“Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanaosubiri.” (16:126)**

Na Kauli Yake:

وَجَزَاءُ سَيِّئَةٍ سَيِّئَةٌ مِّثْلُهَا ۗ فَمَنْ عَفَا وَأَصْلَحَ فَأَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ﴿١٦﴾

**“Na malipo ya ovu ni ovu kama hilo na mwenye kusamehe na akarekebisha basi malipo yake yako kwa Allah.” (42:40)**

وَالْجُرُوحَ قِصَاصٌ ۚ فَمَن تَصَدَّقَ بِهِ ۖ فَهُوَ كَفَّارَةٌ لَّهُ ۚ

**“Na majeraha yana kisasi na ataelitoa sadaka jeraha basi hilo ni kafara kwake.” (5:45)**

Na kuna Aya nyingi zinazohimiza suala la uadilifu katika Uislamu, kadhalika na kuhimiza haki na tabia ya wema.

**Amri ya Kudumisha Mahusiano ya Kindugu na Kukatazwa Madhambi, Uovu na Uasi**

وَإِيتَايَ ذِي الْقُرْبَىٰ

**“...Na kumpa ndugu...”**Maana: Anaamuru Kuunga undugu. Kama Alivyosema:

وَأَتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تَبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾

**“Na mpe ndugu haki yake na masikini na msafiri na usifanye israfu.” (17:26)**

Na Kauli Yake:

وَيَنْهَىٰ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ وَالْبَغْيِ

**“Na Anakataza machafu na maovu na dhulma.”**

Fawahishi ni yaliyoharamishwa na *Munkarati* ni yale yaliyoonekana kwa mfanyaji wake. Kwa sababu hii Amesema mahala pengine

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّي الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ

**“Sema hakika si vingine alichokiharamisha Bwana Wangu ni mambo machafu yaliyodhihiri na siri.”**

Ama *baghiy* ni uadui dhidi ya watu. Na imekuja katika Hadithi:

«مَا مِنْ ذَنْبٍ أَجْدَرَ أَنْ يُعَجَّلَ اللَّهُ عُقُوبَتَهُ فِي الدُّنْيَا مَعَ مَا يَدَّخِرُ لِصَاحِبِهِ فِي الْآخِرَةِ مِنْ الْبَغْيِ وَقَطِيعَةِ الرَّجْمِ»

**“Hakuna dhambi yenye haki ya kuharakisha Adhabu ya Allah hapa duniani pamoja na anayowekewa akhera kuliko husuda na kukata undugu.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Abu Dawud 5:208.

يَعِظُكُمْ

“Anawaonya.”

Maana yake: Anawaamuru kwa kile Anachowaamuru miongoni mwa heri na Anawakataza kile Anachowakataza cha shari.

لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ

“...ili mkumbuke...”

Shaabi amepokea kutoka kwa Shatir Ibn Shakli kuwa amemsikia Ibn Mas’uud رضي الله عنهما akisema: “Hakika aya iliyokusanya zaidi katika *Surat Nnahl* ni:

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ

“... *hakika Allah Anaamuru uadilifu na kufanya hisani...*”

Ameinukuu kauli hiyo bin Jariri رحمه الله تعالى.

### Tukio la Ushuhuda la Uthman Ibn Madhuun رضي الله عنه

Sababu za kuteremka aya hii, Imamu Ahmad amepokea Hadithi *Hasan* kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa, Mtume ﷺ alipokuwa amekaa katika uwanja wa nyumba, alipita Uthman Ibn Madhuun رضي الله عنه, akatabasamu. Mtume ﷺ akamuambia,

«أَلَا تَجْلِسُ؟»

“Unaonaje ukikaa?”

Uthman رضي الله عنه akajibu, ‘Sawa nitakaa.’ Alikaa mbele ya Mtume ﷺ na akawa anazungumza naye. Mara Mtume ﷺ akawa anaangalia mbinguni kwa muda kisha kuliani mwake ardhini. Mtume ﷺ akageukia ule upande aliokaa Uthman akainamisha kichwa chake, kama vile anakifahamu anachoelezwa na Ibn Madhuun. Naye alikuwa akimuangalia Mtume ﷺ kisha akaangalia tena mbinguni kama alivyoangalia mara ya kwanza, akamuelekea Uthman رضي الله عنه kama mara ile ya mwanzo. Kisha Uthman رضي الله عنه akamuambia Mtume ﷺ, “Ewe Muhammad nilipokaa nawe haukuwa unafanya kama ulivyofanya leo.” Akamuuliza,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:280.



«وَمَا رَأَيْتَنِي فَعَلْتُ؟»

*“Umeniona nafanya nini?”*

Uthman akasema: “Nimekuona umekodolea macho mbinguni kisha ukayaweka ulipoyaweka kuliani kwako, ukanigeukia na ukaniacha na ukawa unatikisa, ukainamiza kichwa kama vile unafahamu kitu unachoelezwa.” Mtume ﷺ akamuuliza Uthman رضي الله عنه،

«وَفَطِنْتُ لِدَلِكْ؟»

*“Je uliliona hilo?”*

Uthman رضي الله عنه akajibu, ‘Ndio’ Mtume ﷺ akasema:

«أَتَانِي رَسُولُ اللَّهِ أَيُّهَا وَأَنْتَ جَالِسٌ»

*“Kanijia Mjumbe wa Allah ulipokuwa umekaa hapa.”*

Akasema: “Mjumbe wa Allah?” Akasema:

«نَعَمْ»،

*“Ndiyo.”* Akamuuliza, “amekuambia nini?” Akasema،

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ

*“Hakika Allah Anaamuru uadilifu na kufanya hisani”.*

Uthman رضي الله عنه akasema “Hapo ikanikaa imani na kumpenda “Muhammad ﷺ.” Isnadi yake ni nzuri imeungana.<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ahmad 1:318. Hadithi hii ina udhaifu katika usimulizi wake, uliomfanya Al-Albani kuipa daraja la dhaifu katika *Dhaif Al-Adab Al-Mufrad*, pia Al-Arna’ut katika nukuu zake katika *Musnad*. Udhaifu wa kwanza ni mpokezi wake mmoja, Shahr bin Hawshab, ambaye alichukulika na maulamaa wengi kuwa ni dhaifu. Udhaifu wa pili umetajwa na Ahmad Shakir ambaye katika isnadi yake aliipa daraja la *Sahih*, lakini alionesha kuwa ni mojawapo katika riwaya *Mursal* ya Ibn ‘Abbas kwa kuwa hakumuona Uthman bin Madhuun.

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْقُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٩١﴾ وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِي نَقَضَتْ غَزَلَهَا مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ أَنْكَنَّا تَخَذُوا مِنَ الْأَيْمَانِ كَمَا دَخَلُوا مِنْ بَيْنِكُمْ أَنْ تُكُونُوا مِنْ أُمَّةٍ مِنْ أُمَّةٍ إِنَّمَا يَبْتَلُواكُمُ اللَّهُ بِهِمْ ۗ وَلِيُبَيِّنَ لَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٩٢﴾ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ وَلَتُسْأَلُنَّ عَمَّا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾ وَلَا تَتَّخِذُوا أَيْمَانَكُمْ دَخَلًا بَيْنَكُمْ فَتَرِلَّ قَدَمٌ بَعْدَ ثُبُوتِهَا وَتَذُوقُوا أَلْسُوَّةَ بِمَا صَدَدْتُمْ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَلَكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٩٤﴾ وَلَا تَشْتَرُوا بِعَهْدِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ إِنَّمَا عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩٥﴾ مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ ۗ وَلَنَجْزِيَنَّهُ الَّذِينَ صَبَرُوا أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾ مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً ۗ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾

وَأَوْفُوا بِعَهْدِ اللَّهِ إِذَا عَاهَدْتُمْ وَلَا تَنْقُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا وَقَدْ جَعَلْتُمُ اللَّهَ عَلَيْكُمْ كَفِيلًا ۗ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ ﴿٩١﴾ وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِي نَقَضَتْ غَزَلَهَا مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ أَنْكَنَّا تَخَذُوا مِنَ الْأَيْمَانِ كَمَا دَخَلُوا مِنْ بَيْنِكُمْ أَنْ تُكُونُوا مِنْ أُمَّةٍ مِنْ أُمَّةٍ إِنَّمَا يَبْتَلُواكُمُ اللَّهُ بِهِمْ ۗ وَلِيُبَيِّنَ لَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٩٢﴾ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ ۗ وَلَتُسْأَلُنَّ عَمَّا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾ وَلَا تَتَّخِذُوا أَيْمَانَكُمْ دَخَلًا بَيْنَكُمْ فَتَرِلَّ قَدَمٌ بَعْدَ ثُبُوتِهَا وَتَذُوقُوا أَلْسُوَّةَ بِمَا صَدَدْتُمْ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَلَكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٩٤﴾ وَلَا تَشْتَرُوا بِعَهْدِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ إِنَّمَا عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩٥﴾ مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ ۗ وَلَنَجْزِيَنَّهُ الَّذِينَ صَبَرُوا أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٦﴾ مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً ۗ وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾

91. "Na timizeni ahadi mnapozitoa kwa jina la Allah mnapohidi wala msivunje hizo ahadi baada ya kuzithibitisha hali mumekwishamfanya Allah kuwa shahidi wenu. Hakika Allah Anayajua yote mnyoyafanya."

92. "Wala msiwe kama mwanamke anayeuzongoa uzi wake baada ya kuisha

usokota ukawa mgumu. Mnavifanya viapo vyenu kuwa ni njia ya kudanganyana baina yenu kwa kuwa ati taifa moja lina nguvu zaidi kuliko jengine? Hakika Mwenyezi Mungu Anakujaribuni kwa njia hiyo. Na bila ya shaka Atakubainishieni Siku ya Kiyama mliyokuwa mkikhitalifiana."

## Amri ya Kutekeleza Ahadi

Hili ni miongoni mwa Anayoyaamuru Allah تعالى, nalo ni kutekeleza ahadi na mikataba na kuvilinda viapo vilivyo sisitizwa.

وَلَا تَنْقُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا

**“Na wala msizivunje ahadi zenu baada ya kuzithibitisha.”**

Na hakuna mgongano kati ya hili na Kauli Yake تعالى:

وَلَا تَجْعَلُوا اللَّهَ عُرْضَةً لِأَيْمَانِكُمْ

**“Wala msifanye jina la Mwenyezi Mungu katika viapo vyenu kuwa ni kisingizio.” (2:224)**

ذَلِكَ كَفْرَةٌ أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ<sup>ع</sup> وَأَحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ<sup>ع</sup>

**“Hilo ni kafara la viapo vyenu mnapoapa na vitunzeni viapo vyenu.” (5:89)**

Maana yake: Msiviache bila ya kafara. Na kati ya kauli yake Mtume ﷺ iliyothibiti kutoka kwake katika sahihi mbili kuwa rehema na amani iwe juu yake. Amesema:

«إِنِّي وَاللَّهِ إِن شَاءَ اللَّهُ لَا أَخْلِفُ عَلَى يَمِينٍ فَأَرَى غَيْرَهَا خَيْرًا مِنْهَا إِلَّا أَتَيْتُ الَّذِي هُوَ خَيْرٌ وَتَحَلَّلْتُهَا - وَفِي رِوَايَةٍ - وَكَفَّرْتُ عَنْ يَمِينِي»

*‘Hakika mimi Wallahi inshallah siapi kiapo, halafu nikaona kinyume na ndio bora zaidi isipokuwa nitalifanya hilo bora na kisha kuihalalisha na katika mapokezi mengine nitalipa kafara la yamini, yangu.’<sup>1</sup>*

Hakuna mgongano kati ya hizi zote si kati ya aya iliyotajwa hapa, nayo ni Kauli Yake:

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 11:525, Muslim 3:1269.

وَلَا تَنْقُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا

**"Na wala msizivunje ahadi zenu baada ya kuzithibitisha."**

Kwa sababu madhumuni ya viapo hivi ni vile vinavyokuwa katika mikataba si viapo vile vinavyokuja himiza au kuzuia. Kwa sababu hii Mujahid akasema katika Kauli Yake:

وَلَا تَنْقُضُوا الْأَيْمَانَ بَعْدَ تَوْكِيدِهَا

**"Na wala msizivunje ahadi zenu baada ya kuzithibitisha."**

Maana yake: Kiapo cha kabla ya Uislamu.<sup>1</sup> Inasaidiwa maana hii na alichokipokea Imam Ahmad kutoka kwa Jubair Ibni Mut-im رضي الله عنه amesema: Mtume wa Allah ﷺ amesema:

«لَا جُنْفَ فِي الْإِسْلَامِ، وَأَيُّمَا جُنْفٍ كَانَ فِي الْجَاهِلِيَّةِ فَإِنَّهُ لَا يَزِيدُهُ الْإِسْلَامُ إِلَّا شِدَّةً»

*"Hakuna ushirika katika Waislamu. Na viapo vya ushirika vilikuwa kabla ya Uislamu kwa sababu haumuongezei Muislamu isipokuwa matatizo".<sup>2</sup>*

Hii pia imeandikwa na Muslim.<sup>3</sup> Na maana yake Uislamu hauhitaji ushirika ambao wakiufanya kabla ya Uislamu, kwani kushikilia Uislamu kunatosha yote ya kabla yake.

Ama yaliyokuja katika Sahihi mbili kutoka kwa Anas رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ aliingia katika ushirika kati ya Muhajirina na Answari katika zama zetu.<sup>4</sup> Maana yake yeye amewafanya wawe ndugu kwa hiyo wakawa wanarithiana kwa undugu huo mpaka ulipofutwa na Allah تعالى. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا تَفْعَلُونَ

**"Hakika Allah Anaelewa mnachofanya."**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:282.

<sup>2</sup> Ahmad 4:83.

<sup>3</sup> Muslim 4:1961.

<sup>4</sup> Fat'hul Al-Bari 4:562, Muslim 3:1960.

Ni tishio na kemeo kwa mwenye kuvunja kiapo, ahadi baada ya kuthibitisha,

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ نَقَضَتْ غَزْلَهَا مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ أَنْكَبَتْ

**“Na wala msiwe kama yule mwanamke aliyezikuta nyuzi zake vipande vipande baada ya kuwa nyuzi ndefu zenye nguvu.”**

Abdallah Ibn Kathiri na As-Suddi wamesema: Huyu ni mwanamke alikuwa Makkah kila aliposokota uzi anaufumua baada ya kuwa imara.<sup>1</sup> Na amesema Mujahid, Qatadah na Ibn Zaid: Huu ni mfano wa mwenye kuvunja ahadi yake baada ya kuithibitisha.<sup>2</sup> Na kauli hii ina nguvu zaidi na iko wazi mno ni sawa iwe Makkah ndiko alikuwa mwanamke anayefumua nyuzi zake au hapana. Kisha Allah تعالی Anasema,

تَّخَذُونَ أَيْمَانَكُمْ دَخَلًا بَيْنَكُمْ

**“Mnavifanya viapo vyenu kuwa ni njia ya kudanganyana baina yenu.”**

Maana yake: Kwa lengo la kuhadaiana na kufanyiana hila.

أَنْ تَكُونَ أُمَّةً هِيَ أَرْبَى مِنْ أُمَّةٍ

**“...Ili umma uwe bora kuliko mwingine...”**

Maana: Mnawaapia baadhi ya watu wanapokuwa wengi zaidi yenu ili wapate kuwaamini, na kama mtapata mwanja wa kwenda kinyume nao na kuwageuka basi mnafanya hivyo. Allah تعالی Amekataza hilo ili azindue kuwa maadam hiyana hairuhusiwi katika hali hiyo ya udhaifu wa mtu basi hairuhusiwi zaidi mtu anapokuwa na nguvu na cheo bila kujali uwezo bila ya kujali chochote.

Mujahid amesema walikuwa wanawaapisha washirika wao na hapo wanawakuta wenzao ni wengi kuliko wao na wana nguvu zaidi. Na hapo wanavunja ushirika wao na wanashirikiana na ambao ni wengi zaidi na wana nguvu. Wakakatazwa hilo, Qatadah, Adh-Dhahak na Ibn Zaid wamesema kama hivyo na Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:285.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:285.

إِنَّمَا يَبْتَلُواكُمُ اللَّهُ بِمِ

**“Hakika si vingine bali Allah Anawapeni mtihani kwa hilo.”**

Ibn Jubair amesema, anakusudia uwingi.<sup>1</sup> Ameipokea Ibn Abi Hatim. Amesema Ibn Jarir رحمه الله تعالى: kwa kuwaamuru kutimiza ahadi.

وَلِيَّبِّينَ لَكُمْ يَوْمَ الْقِيَمَةِ مَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٩٦﴾

**“Na hakika Atawaelezea Siku ya Kiama kile mlichokuwa mnahitilafiana.”**

Na Atamlipa kila mtendaji kwa alichokitenda ikiwa kheri au shari.<sup>2</sup>

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَٰكِن يُضِلُّ مَن يَشَاءُ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ ۗ وَلَسْتَ عَلَىٰ  
عَمَّا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾ وَلَا تَتَّخِذُوا أَيْمَانَكُمْ دَخَلًا بَيْنَكُمْ فَتَرِلَّ أَدْمُكُمْ بَعْدَ ثُبُوتِهَا  
وَتَذُوقُوا أَلْسِنَةَ السُّوءِ بِمَا صَدَدْتُمْ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَلِكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٩٨﴾ وَلَا تَشْتَرُوا بِعَهْدِ  
اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ إِنَّمَا عِنْدَ اللَّهِ هُوَ خَيْرٌ لِّكُمْ إِن كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٩٩﴾ مَا عِنْدَكُمْ  
يَنْفَدُ ۗ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ ۗ وَلَنَجْزِيَنَّهُ الَّذِينَ صَبَرُوا أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا  
يَعْمَلُونَ ﴿١٠٠﴾

**93. Na Mwenyezi Mungu Angelitaka, kwa yakini Angelikufanyeni umma mmoja. Lakini Anamuachia kupotea Anayemtaka, na Anamuongoa Amtakaye. Na hakika mtaulizwa kwa yale mliyokuwa mkiyafanya.**

**94. Wala msifanye viapo vyenu ni njia ya kudanganyana baina yenu. Usije mguu ukateleza badala ya kuthibiti, na mkaonja maovu kwa sababu ya kule kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu, na mkapata adhabu kubwa.**

<sup>1</sup> Ad-Dur Al-Manthur 5:163.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:287.

**95. Wala msinunue ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa thamani ndogo. Hakika kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ndicho bora kwenu, ikiwa mnajua.**

**96. Mliyonyavyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyobakia. Na kwa yakini Sisi Tutawapa waliosubiri ujira wao kwa bora ya waliyokuwa wakiyatenda.**

Allah تعالیٰ Kama Angalitaka Watu Wote Angewafanya Umma Mmoja

Allah تعالیٰ Anasema:

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَجَعَلَكُمْ

**“Na Mwenyezi Mungu Angelitaka, kwa yakini Angelikufanyeni...”**

أُمَّةً وَاحِدَةً

**“...umma mmoja.”** Sawa na Kauli Yake:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا

**“Angeli taka Mola wako Mlezi wangeli amini wote waliomo katika ardhi.” (10:99)**

Maana yake: Angeliwakalifisheni na isingelikuwapo khitilafu, chuki, wala ugomvi.

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٨﴾ إِلَّا مَنْ رَحِمَ رَبُّكَ ۗ وَلِذَلِكَ خَلَقَهُمْ

**“Lau kama Mola wako Angalitaka watu Angaliwafanya umma moja. Na wataendelea kuhitilafiana. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu; na kwa (Rehema) hiyo Mwenyezi Mungu Amewaumba.” (11:118-119)**

Isipokuwa aliyerehemewa na Mola wako na kwa hilo Amewaumba na ndivyo Alivyosema hapa:

وَلَيْكِن يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

**“Lakini anamuachia kupotea Anayemtaka, na Anamuongoa Amtakaye.”**

Kisha Atawauliza Siku ya Kiama kuhusu matendo yenu yote na Atawalipa kwa dogo mlilolifanya.”

### **Katazo la Kuapa kwa Lengo la Hadaa**

Kisha Allah تعالی Anawahadharisha waja Wake kula yamini za hadaa na njama ili zisije kuteleza nyayo baada ya kusimama. Huo ni mfano wa aliyekuwa katika usawa. Kisha akauacha, na akateleza kutoka katika usawa kwa sababu ya viapo vilivyovunjwa kwa lengo la kuzuia Dini ya Allah تعالی. Kwa sababu kafiri anapomuona muumini amemuahidi na asitekeleze anakuwa hana imani naye tena katika Dini. Hivyo kwa sababu yake amezuilika kusilimu. Kwa sababu hii Akasema:

وَتَذُقُوا أَلْسُوَءَ بِمَا صَدَدْتُمْ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَلَكُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

***“Na mtaonja ubaya kwa mlichoziwa katika Dini ya Allah na mtapata adhabu kubwa.”***

### **Msivunje Yamini kwa Sababu ya Manufaa ya Dunia**

Kisha Allah تعالی Akasema:

وَلَا تَشْتَرُوا بِعَهْدِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا

***“Na wala msibadilishe ahadi ya Allah kwa thamani chache.”***

Maana yake: Msibadilishe viapo kwa Allah تعالی kwa kupata starehe ya dunia na pambo lake. Kwani hilo ni chache sana hata kama mwanadamu angalipewa dunia yote, bado kilichokuwa kwa Allah تعالی ni bora kwake kuliko hicho. Maana: Malipo ya Allah تعالی ni bora kwa mwenye kuyataraji na akayaamini na akayatafuta na akailinda ahadi yake kwa kutaraji kiahidiwa chake. Na kwa sababu hii Akasema:

إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾ مَا عِنْدَكُمْ يَنْفَدُ

***“...ikiwa mnajua. Mlivyo navyo vitakwisha...”***

Maana yake: Kinaisha na kinamalizika kwa kuwa kina muda mchache uliojulikana mwisho wake. Na kilicho kwa Allah تعالی ni cha kudumu.



وَمَا عِنْدَ اللَّهِ بَاقٍ<sup>ط</sup>

**“...na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyobakia.”**

Maana yake: Malipo Yake peponi ni ya kudumu hayakatiki na hayana mwisho kwa hiyo hayo ni ya kudumu hayabadiliki na hayaondoki:

وَلَنَجْزِيَنَّهُ الَّذِينَ صَبَرُوا أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**“Na Wallahi Tutawalipa wale ambao wamesubiri malipo yao kwa malipo mazuri zaidi ya walichokuwa wamekifanya.”**

Ni kiapo kutoka kwa Allah تعالى kilichosisitizwa kwa herufi ya “Laam” ya kiapo. Kuwa Yeye Atawalipa wenye kusubiri kwa mazuri mno ya matendo yao. Maana: atafuta maovu yake.

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهٗ حَيٰوةً طَيِّبَةً<sup>ط</sup> وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾

**“Wafanyaji mema, wanaume au wanawake hali ya kuwa ni Waislamu Tutawahuisha maisha mema, na Tutawapa ujira wao akhera mkubwa kabisa kwa sababu ya yale mema waliyokuwa wakiyafanya.” (16:97)**

### Matendo Mema na Malipo Yake

Hii ni ahadi ya Allah تعالى kwa aliyefanya mema. Nayo ni matendo yaliyofuata kitabu cha Allah تعالى na Sunna ya Mtume wake ﷺ, awe mwanamume au mwanamke, katika wanadamu. Na moyo wake unamuamini Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na kwamba amali hii iliyoamrisha ni sheria kutoka kwa Allah تعالى. Basi Allah تعالى Atampa maisha mazuri duniani, na Atamlipa malipo mazuri zaidi ya aliyoyafanya huko akhera. Maisha mazuri hujumuisha aina zote za raha, katika maisha ya dunia na akhera. Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na kikundi cha masahaba رضي الله عنهم kuwa wao wameifasiri kwa maana ya riziki ya halali na nzuri. Na imepokewa kutoka kwa Ali Ibn Abi Twalib رضي الله عنه kuwa ameifasiri kwa maana ya kutosheka; na vivyo hivyo amesema Ibni Abbas رضي الله عنهما na Ikrima na Wahbi Ibn Abi Twalha kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما: Hayo ni maisha ya furaha.

Ama Hassan, Mujahid, na Qatadah wamesema kuwa maisha hayawi mazuri kwa yeyote isipokuwa peponi. Na amesema Adh-Dhahhak pia: Hayo ni matendo ya kutii na kukunjuka. Na amesema Adh-Dhahhak: Hiyo ni riziki halali duniani na ibada. Na kauli sahihi ni 'maisha mazuri' kwani yanakusanya yote haya. Kama ilivyokuja katika Hadithi ambayo ameipokea Imam Ahmad kutoka kwa Abdulahi Ibn 'Amri kuwa Mtume ﷺ amesema,

«قَدْ أَفْلَحَ مَنْ أَسْلَمَ، وَرُزِقَ كِفَافًا، وَقَتَّعَهُ اللَّهُ بِمَا آتَاهُ»

*"Amefaulu anayejisalimisha kwa Allah na akapewa riziki ya kumtosha na Allah Akamtosheleza kwa Alichompa."*<sup>1</sup>

Pia iliandikwa na Muslim.<sup>2</sup>




---

<sup>1</sup> Ahmad 4:268.

<sup>2</sup> Muslim 2:730.

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ  
 ٩٨ إِنَّهُ لَيْسَ لَهُ سُلْطَانٌ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَلَىٰ  
 رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ٩٩ إِنَّمَا سُلْطَانُهُ عَلَى الَّذِينَ  
 يَتَوَلَّوْنَهُ وَالَّذِينَ هُمْ بِهِ مُشْرِكُونَ ١٠٠ وَإِذَا بَدَلْنَا  
 ءَايَةً مَّكَانَ ءَايَةٍ ۗ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُنزِلُ قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ  
 مُفْتَرٍ ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ١٠١ قُلْ نَزَّلَهُ رُوحُ الْقُدُسِ  
 مِنْ رَبِّكَ بِالْحَقِّ لِيُثَبِّتَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهُدًى وَبُشْرَىٰ  
 لِلْمُسْلِمِينَ ١٠٢ وَلَقَدْ نَعَلِمَ أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ  
 بَشَرٌ ۗ لِسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِيٌّ ۖ وَهَذَا  
 لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُبِينٌ ١٠٣ إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ  
 بِعَايَتِ اللَّهِ لَا يَهْدِيهِمُ اللَّهُ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ١٠٤ إِنَّمَا  
 يَفْتَرِي الْكَذِبَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ ۗ وَأُولَٰئِكَ  
 هُمُ الْكَافِرُونَ ١٠٥

فَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْتَعِذْ بِاللَّهِ مِنَ  
 الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ٩٨ إِنَّهُ لَيْسَ  
 لَهُ سُلْطَانٌ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ٩٩  
 إِنَّمَا سُلْطَانُهُ عَلَى الَّذِينَ  
 يَتَوَلَّوْنَهُ وَالَّذِينَ هُمْ بِهِ  
 مُشْرِكُونَ ١٠٠

**98. Na ukisoma Qur'ani muombe Mwenyezi Mungu Akulinde na Shetani maluuni.**

**99. Hakika yeye hana madaraka juu ya walio-amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi.**

**100. Hakika madaraka yake ni juu ya wanaomfanya rafiki yao, na wale wanaofanya ushirika naye.**

### Amri ya Kuanza Kujilinda na Shetani Kabla ya Kusoma Qur'an.

Hii ni amri ya Allah تعالیٰ kwa waja Wake kupitia Nabii wake ﷺ wanapotaka kusoma Qur'an wajilinde kwa Allah تعالیٰ, Awakinge na shetani aliyotolewa katika rehema. Na tumekwisha zitaja hadithi zilizokuja katika kujilinda kwa urefu mwanzo wa tafsiri, na sifa njema ni za Allah تعالیٰ.

Na maana iliyo katika kujikinga wakati wa kuanza kusoma ni asimvurugie kisomo chake na kumzuia kutafakari na kuzingatia. Na kwa sababu hii Jamhuri wanasema *audhu* inakuwa kabla ya kusoma.

إِنَّهُ لَيْسَ لَهُ سُلْطَانٌ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٩٨﴾

**“Hakika yeye hana madaraka juu ya walioamini na wakamtegemea Mola wao Mlezi.” (16:99)**

Ath-Thauri رحمه الله تعالى amesema, ‘hana juu yao nguvu ya kuwaingiza katika dhambi wasioiletea toba.’<sup>1</sup> Na wengine wamesema: Maana yake hana hoja dhidi yao. Na wamesema wengine: sawa na Kauli Yake:

إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ ﴿٩٩﴾

**“Isipokuwa waja wako waumini.” (15:40)**

إِنَّمَا سُلْطَانُهُ عَلَى الَّذِينَ يَتَوَلَّوْنَهُ

**“Hakika si vingine nguvu zake ziko juu ya wanaompenda.”**

Mujahid amesema: Wanaomtii.<sup>2</sup> Na wengine wamesema wamemfanya mpenzi badala ya Allah تعالى.

وَالَّذِينَ هُمْ بِهِ مُشْرِكُونَ

**“Na ambao wao wanamshirikisha.”**

Maana: Wamemshirikisha katika ibada ya Allah تعالى.

وَإِذَا بَدَلْنَا آيَةً مَّكَانَ آيَةٍ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُنزِلُ قَالُوا إِنَّمَا أَنْتَ مُفْتَرٍ ۚ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠١﴾ قُلْ نَزَّلَهُ رُوحُ الْقُدُسِ مِنْ رَبِّكَ بِالْحَقِّ لِيُثَبِّتَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ ﴿١٠٢﴾

**101. Na Tunapoibadili Aya kwa Aya nyingine na hali ya kuwa Allah Anajua Anayoyateremsha wanasema: Wewe ni mzushi tu! Bali wengi katika wao hawajui lolote, wanajisemea wanayoyasikia kwa wakubwa wao tu.**

**102. Sema: Ameiteremsha hii Roho Mtakatifu kutoka kwa Mola wako Mlezi kwa haki, ili Awathibitisha wale walioamini, na kuwa ni uwongofu, na ni bishara kwa Waislamu.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:294.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:294.

## Tuhuma za Washirikina Kuwa Mtume ni Mzushi kwa Sababu ya Kufutwa Baadhi ya Aya, na Majibu Yao

Allah تعالى Anaelezea udhaifu wa akili za washirikina na uchache wa ukweli wao na uhakika wao na kwamba suala la kuamini kwao wao halipo. Na Allah Amewaandikia maisha mabaya, na hiyo ni kwa sababu wanapoona kuletwa hukumu mpya iliyoondosha hukumu ya zamani wanamuambia Mtume ﷺ,

إِنَّمَا أَنْتَ مُفْتَرٍ

'**Wewe ni mzushi.**' Maana yake: Mwongo, bali huyo ni Mola تعالى Anafanya Atakavyo na Anahukumu Atakalo. Mujahid amesema,

بَدَلْنَا آيَةَ مَكَانٍ آيَةٍ

**"Tunapoibadili Aya kwa Aya nyingine."**

Maana yake: Tumeiondoa na Tukaiweka nyingine.<sup>1</sup> Na Qatadah amesema: Hiyo sawa na Kauli Yake تعالى,

مَا نَنْسَخْ مِنْ آيَةٍ أَوْ نُنسِهَا

**"Aya yoyote Tunayoifuta au Tunayoisahaulisha." (2:106)<sup>2</sup>**

Allah تعالى Akawajibu:

قُلْ نَزَّلَهُ رُوحُ الْقُدُسِ

**"Wambie ameiteremsha roho mtakatifu."** Maana yake: Jibrili عليه السلام

مِنْ رَبِّكَ بِالْحَقِّ

**"Kutokana na Mola wako Mlezi kwa haki,"**

Maana yake: Kwa ukweli na uadilifu,

لِيُثَبِّتَ الَّذِينَ آمَنُوا

**"Ili Awathibitisha wale walioamini,"**

Ili wakubali kilichoteremshwa; na ili zimnyenyekee nyoyo zao

<sup>1</sup> At-Tabari 17:297.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:297.

وَهْدَىٰ وَدُشِّرَ لِلْمُسْلِمِينَ

**“...na kuwa ni uwongofu, na ni bishara kwa Waislamu.”**

Maana yake: Na amekifanya ni muongozo na bishara njema kwa waliosilimu ambao wameamini kwa Allah تعالى na Mitume wake.

وَلَقَدْ نَعَلْنَا أَنَّهُمْ يَقُولُونَ إِنَّمَا يُعَلِّمُهُ بَشَرٌ لِّسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِي

وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ ﴿١٠٣﴾

**103. Na Sisi hakika Tunajua kwamba wanasema: Yuko mtu anayemfundisha. Lugha ya huyo wanayemuelekeza ni ya kigeni, na hii ni lugha ya Kiarabu m-bayana.**

**Washirikina Wainasibisha Qur'an kuwa ni Mafundisho ya Mwanadamu na Kujibiwa Kwao.**

Allah تعالى Anawaelezea washirikina uongo waliokuwa wanauzusha kuwa Mtume Muhammad ﷺ anafundishwa na kusomeshwa na mwanadamu. Wakati huo wakimuashiria mtu asiyekuwa Mwarabu ambae alikuwa ni mtumwa wa baadhi ya matumbo ya Makureishi na mfanyabiashara katika eneo la Swafa. Mtume ﷺ alipendelea kwenda kwa huyo bwana na kukaa naye kwa muda huku akizungumza naye. Huyu hakuwa Mwarabu na alikuwa hajui lugha ya Kiarabu. Au wanasema kuwa alikuwa anajua kidogo kiasi cha kukitumia katika kujibu katika mambo ya lazima tu. Allah تعالى Akasema Akiwajibu uzushi wao huo kuwa,

لِّسَانُ الَّذِي يُلْحِدُونَ إِلَيْهِ أَعْجَمِي وَهَذَا لِسَانٌ عَرَبِيٌّ مُّبِينٌ

**“Lugha ya yule wanayemuelekeza kuwa anamfundisha Mtume ni ya kigeni na hii lugha hii inayotumika katika Qur'an ni lugha ya Kiarabu.”**

Maana yake: Qur'an. Basi vipi atajifunza aliyekuja na Qur'an hii pamoja na ufasaha wake na balagha yake na maana yake kamili, iliyokusanya maana iliyokamilika mno, na kukusanya maana ya kila kitabu kilichoteremka kwa Nabii aliyetumwa, atajifunzaje kwa asiyekuwa Mwarabu?

Haya hawezi kuyasema aliye na japo mguso mdogo wa akili. Na Ibn Jarir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa amesema: Mtume ﷺ alikuwa anamuendea mhunzi fulani pale Makkah, jina lake Bal-aam, na alikuwa hajui lugha ya Kiarabu, na washirikina walikuwa wanamuona Mtume ﷺ anaingia kwake na anatoka kwake, kwa hiyo basi wakasema: Si vingine bali Bal-aam anamfundisha.

Allah تعالى Akaiteremsha aya hii,

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ لَا يَحْسِبُهُمُ اللَّهُ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٠٤﴾ إِنَّمَا يَفْتَرِي  
الْكَذِبَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿١٠٥﴾

**104. Hakika wale wasioziamini aya za Allah, Allah Hawaongozi njia ya kheri, kwani wenyewe hawataki basi watapata adhabu iumizayo.**

**105. Wanaozua uongo (wakipita wakitangaza kama hivyo kusema Mtume anafundishwa Qur'an na huyo Mrumi) ni wasioamini aya za Allah, na hao ndio waongo.**

Allah تعالى Anaeleza kuwa Hatamuongoza aliyeupuuza utajo Wake, na Akajifanya hana habari ya Alichomteremshia Mtume Wake ﷺ, na wala hana nia ya kuamini kilichokuja kutoka kwa Allah تعالى. Basi jinsi hii ya watu Allah تعالى Hawaongozi kwenye kuziamini aya Zake na Alichowatuma nacho Mitume Wake hapa duniani, na akhera watapata adhabu iumizayo mno.

Kisha Allah تعالى Akaeleza kuwa Mtume wake ﷺ si mzushi na wala si muongo, kwa sababu wanaobuni uongo kwa Allah تعالى na kwa Mtume ﷺ ni watu wabaya wasioziamini aya za Allah تعالى.

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ

**“Hakika wale wasioziamini aya za Allah.”**

Miongoni mwa ambao Allah تعالى Anawaeleza ni makafiri na wapotoshaji wanaojulikana na watu kwa uongo. Ama Mtume Muhammad ﷺ alikuwa ni mkweli kuliko watu wote, na mwema wao mno na mkamilifu wao mno, kwa elimu na utendaji, imani na itikadi.

Mtume ﷺ anajulikana kwa ukweli kati ya watu wake, hakuna aliye na shaka naye katika hilo. Haitwi kati yao, isipokuwa mkweli muaminifu. Kwa sababu hii Hiraqli, mfalme wa Warumi, alipomuuliza Abi Sufiani kuhusu sifa zake Mtume ﷺ katika aliyomuuliza yalikuwa ni: 'Je mlikuwa mnamtuhumu uwongo kabla hajasema aliyoyasema?' Akasema, 'Hapana.' Hiraqli akasema, 'haiwezekani aache kuwaongopea watu akaamua kumuongopee Allah ﷻ.'





مَن كَفَرَ بِاللَّهِ مِن بَعْدِ إِيْمَانِهِ إِلَّا مَن أَكْرَهَ وَقَلْبُهُ  
 مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيْمَانِ وَلَكِن مِّن شَرَحٍ بِالْكَفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ  
 غَضَبٌ مِّنَ اللَّهِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٠٦﴾ ذَلِكَ  
 بِأَنَّهُمْ اسْتَحْبَبُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا  
 يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿١٠٧﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ طَبَعَ  
 اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَسَمِعِهِمْ وَأَبْصَرِهِمْ ۗ وَأُولَئِكَ هُمُ  
 الْغَافِلُونَ ﴿١٠٨﴾ لَا جَرَمَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمُ  
 الْخَاسِرُونَ ﴿١٠٩﴾ ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ هَاجَرُوا  
 مِن بَعْدِ مَا فُتِنُوا ثُمَّ جَاهَدُوا وَصَبَرُوا إِنَّ رَبَّكَ مِن  
 بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٠﴾ \* يَوْمَ تَأْتِي كُلُّ نَفْسٍ  
 تُجَادِلُ عَن نَّفْسِهَا وَتُوَفَّىٰ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهُمْ لَا  
 يُظْلَمُونَ ﴿١١١﴾

مَن كَفَرَ بِاللَّهِ مِن بَعْدِ إِيْمَانِهِ إِلَّا  
 مَن أَكْرَهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيْمَانِ  
 وَلَكِن مِّن شَرَحٍ بِالْكَفْرِ صَدْرًا  
 فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِّنَ اللَّهِ وَلَهُمْ  
 عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٠٦﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ  
 اسْتَحْبَبُوا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا عَلَى الْآخِرَةِ  
 وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ  
 الْكَافِرِينَ ﴿١٠٧﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ  
 طَبَعَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَسَمِعِهِمْ  
 وَأَبْصَرِهِمْ ۗ وَأُولَئِكَ هُمُ  
 الْغَافِلُونَ ﴿١٠٨﴾ لَا جَرَمَ لَهُمْ  
 فِي الْآخِرَةِ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٠٩﴾

**106.** Anayemkataa Mwenyezi Mungu baada ya kuamini kwake - isipokuwa aliyelazimishwa na hali ya kuwa moyo wake umetua juu ya Imani, lakini aliyekifungulia kifua chake kukataa - basi hao ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ipo juu yao, na wao watapata adhabu kubwa.

**107.** Hayo ni kwa sababu wameyapenda zaidi maisha ya duniani kuliko ya Akhera, na kwa sababu Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu makafiri.

**108.** Hao ndio Mwenyezi Mungu Ameziziba nyoyo zao na masikio yao na macho yao. Na hao ndio walioghafilika.

**109.** Hapana shaka ya kwamba hao ndio wenye kukhasiri Akhera.

**Ghadhabu za Allah تعالی Juu ya Aliyeritadi Isipokuwa Aliyelazimishwa Ukafiri**

Allah تعالی Akamuelezea aliyemkufuru baada ya kumuamini na kumuelewa na akakunjua kifua chake na akatulia na imani. Allah تعالی Amewakasirikia kwa sababu imani wanaijua kisha wanaiacha. Na kwamba wana adhabu kubwa akhera. Kwa sababu wao wameyapenda maisha ya dunia kuliko ya akhera, wakafanya waliyoyafanya ya kuacha Dini kwa ajili ya dunia.

Na Allah تعالی Hakuzipa uongofu nyoyo zao na kuwathibitisha katika Dini ya haki. Akazifunga nyoyo zao, kwa hiyo, wao hawafahamu chochote kwa nyoyo hizo kitachowafaa. Na Akayafunga masikio yao na macho yao hawafaidiki navyo na wala havikuwatosheleza chochote. Kwa hiyo wao hawana habari na litalowatokea,

لَا جَرَمَ

**“Hapana shaka...”**

Maana yake: Ni lazima kwa wenye sifa hii.

أَنَّهُمْ فِي الْآخِرَةِ هُمُ الْخَاسِرُونَ

**“...ya kwamba hao ndio wenye kukhasiri Akhera.”**

Maana yake: Waliokhasiri nafsi zao na familia zao Siku ya Kiama.

Ama Kauli Yake:

إِلَّا مَنْ أَكْرَهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ

**“Isipokuwa mwenye kulazimishwa ukafiri hali moyo wake umetulia juu ya imani.”**

Hiyo ni kumtoa aliyekufuru kwa ulimi tu, na akaafikiana na washirikina kwa neno lake akiwa amelazimishwa kwa njia ya kipigo au maudhi yaliyompata. Na moyo wake unakataa anachokisema, na umetulizana juu ya Imani ya Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ.

### Sababu ya Kuteremka kwa Aya

Awfi amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa aya hii imeteremka kwa sababu ya Ammar Ibn Yasir رضي الله عنهما alipoadhibiwa na washirikina mpaka akamkufuru Mtume ﷺ. Ammar رضي الله عنه akalalamikia hali hiyo kwa Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akamuuliza:

«كَيْفَ تَجِدُ قَلْبَكَ؟»

*"Vipi unaukuta moyo wako?"*

Akasema: 'Umetulia kwa imani.' Mtume ﷺ akasema:

«إِنْ عَادُوا فَعُدُّ»

*"Wakirudia, nawe rudia."*

Na amepokea Baihaqi kwa upana zaidi na yaliyo humo ni: 'Yeye alimtukana Mtume ﷺ na aliitaja vema miungu yao. Akaenda kulalamika hayo kwa Mtume ﷺ, akasema, 'Ewe Mtume wa Allah! Sikuachiwa mpaka nilipokutukana na nikaitaja kwa kheri miungu yao.' Akamuuliza:

«كَيْفَ تَجِدُ قَلْبَكَ؟»

*'Unauona vipi moyo wako?'*

Akasema, 'Umetulia kwa imani.'" Akasema:

«إِنْ عَادُوا فَعُدُّ»

*"Wakirudia, nawe rudia."*

Na katika hilo Allah تعالى Akateremsha,

إِلَّا مَنْ أَكْرَهَ وَقَلْبُهُ مُطْمَئِنٌّ بِالْإِيمَانِ

***"...isipokuwa aliyelazimishwa ukafiri hali ya kuwa moyo wake umetulia juu ya imani..."***

Kwa sababu hii wanawazuoni wameafikiana kuwa, aliyelazimishwa ukafiri anaruhusiwa kuwa nao kwa ajili ya kuibakisha roho yake. Na anaruhusiwa kukataa, kama alivyo kuwa anakataa Bilal رضي الله عنه huku wakimfanyia matendo mabaya, mpaka walikuwa wanamuwekea jiwe kubwa juu ya kifua chake, katika

kipindi cha joto kali. Na wanamlazimisha amshirikishe Allah تعالى, naye akawa anawakatalia, huku akisema, 'ahad ahad' mmoja, mmoja.

Kadhalika Bilal رضي الله عنه anahadithia kwa kusema, 'Wallahi lau kama ningalilielewa tamko linalowakera zaidi ya hili ningalilisema.' Pia Habib Ibn Zaid Al-Answari رضي الله عنه alipomuambia Musailima Al Kadh-dhab: 'Unakiri kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah?' Akasema: 'Ndiyo.' Akasema, 'Unakiri kuwa mimi ni Mtume wa Allah?' Akasema: 'Sisikii.' Akaendelea kumkata kipande kipande na kumuadhibu naye habadiliki.<sup>1</sup>

Lililo bora kwa Muislam asubiri na kubakia na Dini yake hata kama itafikia hatua ya kuuawa. Kama alivyosema Al-Hafidh Ibn Asakir katika kumuelezea Abdillahi Ibn Hudhafa Ssahmi رضي الله عنه mmoja wa Masahaba kuwa alitekwa na Warumi wakamleta kwa mfalme, akamuambia: 'Ingia ukristo nami nitakushirikisha katika ufalme wangu na nitakuozesha binti yangu.' Akamjibu: 'Kama ungali nipa vyote unavyovimiliki, na vyote wanavyovimiliki Waarabu ili niache Dini ya Muhammad ﷺ, kufumba na kufumbua jicho, sitafanya hivyo.' Akasema: 'Kama ni hivyo nitakuua.' Akamjibu: 'Uko huru kufanya utakavyo.' Amesema: 'Akaamuru asulubiwe na wampige mawe, wakampiga mawe huku wakimtaka aingie Ukristo naye anakataa, akaamuru ateremshwe, kisha kuletwa chungu, na katika mapokezi mengine, aliamuru liletwe sufuria la shaba, likatiwa moto akawaleta mateka Waislamu akawatia jikoni huku akiwaona, na walipotiwa tu wakabaki mifupa akatakiwa aingie Ukristo akakataa, akaamuru atiwe mle, akabebwa ili atiwe ndani ya sufuria. Abdullah رضي الله عنه akalia. Mfalme akatumaini kuwa Abdullah رضي الله عنه atakubali ukristo. Akamuita. Abdullah رضي الله عنه akasema, 'Nililia kwa sababu nina roho moja tu inayotiwa katika sufuria hii leo kwa ajili ya Allah تعالى. Nilipenda ningekuwa na roho kwa idadi ya nywele nilizo nazo mwilini, zipewe adhabu hii kwa ajili ya Allah تعالى.' Katika baadhi ya riwaya alimfunga na kumnyima chakula na maji kwa siku kadhaa, kisha akapelekewa pombe na nyama ya nguruwe akavikataa kisha akamuita akamuuliza nini kilichokuzuia kula? Akasema, 'Ingawa ni halali kwangu lakini siko tayari kukufurahisha.' Mfalme akamuambia: 'Basi busu kichwa changu nikuachie.' Akamuuliza, 'Je utawaachia na mateka wengine Waislamu wote?' Akasema, 'ndiyo' Akabusu kichwa chake na akamuachia pamoja na mateka wote Waislamu alionao, Aliporejea Umar

<sup>1</sup> Asad Al-Ghabah 1049.

رضي الله عنه alisema, 'ni haki kwa kila Muislamu kubusu kichwa cha Abdullah Ibn Hudhafa nami ninaanza.' Akainuka akakibusu.<sup>1</sup>

ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلذَّيِّبِ هَاجِرُوا مِنْ بَعْدِ مَا فُتِنُوا ثُمَّ جَاهِدُوا وَصَبِرُوا إِنَّ رَبَّكَ  
 مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٠٦﴾ \* يَوْمَ تَأْتِي كُلُّ نَفْسٍ تُجَادِلُ عَنْ نَفْسِهَا وَتُوَفَّى كُلُّ  
 نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ وَهَمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٠٧﴾

**110. Kisha hakika Mola wako Mlezi, kwa wale waliohama makwao baada ya kuteswa, kisha wakapigania Dini na wakasubiri, bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.**

**111. Siku ambayo kila nafsi itakuja jitetea, na kila nafsi italipwa sawa sawa na a'mali ilizozifanya, nao hawatadhumiwa.**

### Atasamehewa Mwenye Kulazimishwa Kama Atafanya Mema Baada ya Kulazimishwa

Hawa ni watu waliodhalilishwa Makkah. Wamedhalilishwa katika kaumu zao wakaafikiana nao katika fitina, kisha wakajikomboa kwa kuhama, wakaiacha nchi yao, watoto wao, na mali zao ili kutaka radhi za Allah تعالی na msamaha Wake. Wakajiunga katika safu ya Waislamu na wakapigana jihadi pamoja na waumini dhidi ya makafiri na wakavumilia. Akawaeleza kuwa baada ya hayo (tendo la kukubali wakati wa fitina), Atawasamehe na Atawarehemu siku ya kurejea kwao.

\* يَوْمَ تَأْتِي كُلُّ نَفْسٍ تُجَادِلُ عَنْ نَفْسِهَا

**"...Siku itakuja kila nafsi kujitetea."**

Maana yake: Kutoa hoja, hakuna atayeitetea si baba, si mtoto, si ndugu wala mke.

وَتُوَفَّى كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ

**"..na kila nafsi italipwa sawa sawa na a'mali ilizozifanya."**

<sup>1</sup> Al-Hafidh (Ibn Hajar) ameeleza habari hiyo kwa kifupi katika *Al-Isabah* (4641), na ameinasibisha na Al-Bayhaqi.

Hayatapunguzwa malipo ya kheri na hawataongezewa malipo ya shari.

وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

*"...nao hawatadhulumiwa."*

Maana yake: Malipo mema hayatapungua wala malipo kwa ajili ya uovu hayatazidishwa. Hawatadhulumiwa hata kidogo.

\* \* \*

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ ءَامِنَةً مُطْمَئِنَّةً يَأْتِيهَا  
 رِزْقُهَا رَغَدًا مِّنْ كُلِّ مَكَانٍ فَكَفَرَتْ بِأَنْعَمِ اللَّهِ فَأَذَاقَهَا  
 اللَّهُ لِبَاسَ الْجُوعِ وَالْخَوْفِ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ ﴿١١٢﴾  
 وَلَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِّنْهُمْ فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُمُ الْعَذَابُ وَهُمْ  
 ظَالِمُونَ ﴿١١٣﴾ فَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَلًا طَيِّبًا  
 وَاشْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١١٤﴾ إِنَّمَا  
 حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالْدَّمَ وَلَحْمَ الْخَيْزِرِ وَمَا أَهْلٌ لِّغَيْرِ  
 اللَّهِ بِهِ ۗ فَمَنِ اضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿١١٥﴾ وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِفُ أَلْسِنَتِكُمُ الْكَذِبَ  
 هَذَا حَلَلٌ وَهَذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ ۗ إِنَّ  
 الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١١٦﴾ مَتَّعْ  
 قَلِيلٌ وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١١٧﴾ وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا مَا  
 فَصَّصْنَا عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ ۗ وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا  
 أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١١٨﴾ ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ عَمِلُوا  
 السُّوءَ بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا إِنَّ رَبَّكَ  
 مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٩﴾

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا قَرْيَةً كَانَتْ  
 ءَامِنَةً مُطْمَئِنَّةً يَأْتِيهَا  
 رِزْقُهَا رَغَدًا مِّنْ كُلِّ مَكَانٍ فَكَفَرَتْ  
 بِأَنْعَمِ اللَّهِ فَأَذَاقَهَا اللَّهُ لِبَاسَ  
 الْجُوعِ وَالْخَوْفِ بِمَا كَانُوا  
 يَصْنَعُونَ ﴿١١٢﴾  
 وَلَقَدْ جَاءَهُمْ رَسُولٌ مِّنْهُمْ  
 فَكَذَّبُوهُ فَأَخَذَهُمُ  
 الْعَذَابُ وَهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١١٣﴾

112. Na Mwenyezi Mungu  
 Amepiga mfano wa mji  
 uliokuwa na amani na  
 utulivu, riziki yake ikiufikia  
 kwa nafasi kutoka kila  
 mahali. Lakini ukazikufuru  
 neema za Mwenyezi  
 Mungu; kwa hivyo  
 Mwenyezi Mungu Akau-  
 vika vazi la njaa na khofu  
 kwa sababu ya yale waliyo-  
 kuwa wakiyafanya.

113. Na alikwishawajia  
 Mjumbe miongoni mwao

wenyewe. Lakini wakamkanusha; basi iliwafika adhabu hali ya kuwa  
 wamedhulumu.

## Huu ni Mfano wa Mji wa Makkah

Mfano huu umekusudiwa watu wa Makkah. Makkah ulikuwa mji wenye amani na utulivu na watu wa Miji jirani na mji huo wanaporwa na maadui, na mwenye kuingia Makka anakuwa yuko katika amani haogopi.

Kama Alivyosema تعالى:

وَقَالُوا إِن نَّتَّبِعِ الْهُدَىٰ مَعَكَ تَتَخَطَّفَ مِنَّا أَرْضُنَا أَوْلَمْ نُنَمِكَنَّ لَهُمْ حَرَمًا ءَامِنًا مُّجَبَّىٰ إِلَيْهِ  
ثُمَّ رَتُّ كُلِّ شَيْءٍ رِّزْقًا مِن لَدُنَّا

**“Na wakasema: Tukiufuata uwongofu huu pamoja nawe tutanyakuliwa kutoka nchi yetu. Je! Kwani Sisi hatukuwaweka imara katika pahala patakatifu, penye amani, ambapo huletewa matunda ya kila aina kuwa ni riziki itokayo Kwetu?” (28:57)**

Na hivi hivi Amesema hapa:

يَأْتِيهَا رِزْقُهَا رَغَدًا

**“..Ina ujia riziki yake kwa nafasi..”**

Maana yake: Kwa urahisi na kwa wingi.

مِن كُلِّ مَكَانٍ فَكَفَرَتْ بِأَنْعَمِ اللَّهِ

**“...kutoka kila mahala ukazikufuru neema za Allah...”**

Umezikufuru neema za Allah تعالى katika mji huo na kubwa ya neema hizo ni kupelekwa Muhammad ﷺ kwao kama Alivyosema تعالى:

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَّلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ۗ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا  
وَبِئْسَ الْقَرَارُ

**“Hebu hukuwaona wale waliobadilisha neema ya Mwenyezi Mungu kwa kufuru, na wakawafikisha watu wao kwenye nyumba ya maangamizo? Nayo ni Jahannamu! Maovu yaliyoje makaazi hayo!” (14:28-29)**

Hivyo, Allah تعالى Akawabadilishia hali mbili za mwanzo kwa zingine akasema,



فَأَذَقَهَا اللَّهُ لِبَاسَ الْجُوعِ وَالْخَوْفِ

**“...Akauonjesha Allah vazi la njaa na hofu...”**

Maana yake: Akauvisha na Akauonjesha njaa baada kuwa wakiletewa matunda ya kila aina, na unajiwa na riziki yake kwa urahisi kutoka kila mahala. Na hayo ni pale walipomshupalia Mtume ﷺ na wakakataa isipokuwa wawe kinyume naye. Akawaombea ukame kama wa Nabii Yusuf عليه السلام. Ukawapata ukame uliowaondolea kila kitu chao, wakala manyoya ya Ngamia, wakiyachanganya na damu yake wakimchinja. Na Kauli Yake,

وَالْخَوْفِ

**“...na hofu...”**

Hayo ni kwa sababu wamebadilisha amani yao kuwa hofu ya kumuogopa Mtume ﷺ na masahaba wake walipohamia Madina kutokana na nguvu zake, vikosi vyake na jeshi lake. Na akakifanya kila walicho nacho ni kuteketea na takataka, mpaka alipomfungulia Allah تعالى Mtume wake ﷺ, kwa sababu ya tendo lao, husuda yao, na kumpinga kwao, Mtume ﷺ ambaye aliyempeleka kwao Allah تعالى, akiwa miongoni mwao na ambaye alikuwa ni neema kwao. Kama Alivyosema,

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema mkubwa Waumini vile Alivyowaletea Mtume Aliye miongoni mwao wenyewe.”**

فَاتَّقُوا اللَّهَ يَا أُولِي الْأَلْبَابِ الَّذِينَ ءَامَنُوا قَدْ أَنزَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ الذِّكْرَ ۖ رُسُلًا

**“Basi mcheni Mwenyezi Mungu, enyi wenye akili, mlioamini! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuteremshieni Ukumbusho, Mtume...” (65:10-11)**

كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِّنكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ ءَايَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ  
وَالْحِكْمَةَ

**“Kama Tulivyowaletea Mtume miongoni mwenu. Anawasomea aya Zetu na Anawatakasa na Anawafundisha kitabu na hekima.”**Mpaka,

## وَلَا تَكْفُرُونَ ﴿١١٧﴾

“... wala msinikufuru.” (2:152)

Na kama ilivyowajia kinyume makafiri hali yao, wakawa na hofu baada ya amani, wakawa na njaa baada ya shibe. Basi Allah تعالى Akawabadilishia waumini baada ya hofu yao - amani. Na Akawapa riziki baada ya umasikini, na Akawafanya viongozi wa watu na mabwana wao. Na haya tuliyoyasema kuwa mfano huu wamepigiwa watu wa Makkah, ameyasema Al-Awfi kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما<sup>1</sup> na hiyo ndio kauli ya Mujahid, Qatadah, na Abdir-Rahmani Ibn Zaidi . Ibn Aslam ameipokea kutoka kwa Malik kutoka kwa Zuhairi, Allah تعالى Awarehemu.<sup>2</sup>

فَكُلُوا مِمَّا رَزَقَكُمُ اللَّهُ حَلَلًا طَيِّبًا وَاشْكُرُوا بِنِعْمَتِ اللَّهِ إِنَّ كُنتُمْ لِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١١٤﴾  
 إِنَّمَا حَرَّمَ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةَ وَالْدَّمَ وَلَحْمَ الْخَيْزِرِ وَمَا أَهْلٌ لِّغَيْرِ اللَّهِ بِهِ ط  
 فَمَنْ أَضْطَرَّ غَيْرِ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَلَيْسَ اللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٥﴾ وَلَا تَقُولُوا لِمَا  
 نَصِفُ أَلْسِنَتُكُمُ الْكَذِبَ هَذَا حَلَلٌ وَهَذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ إِنَّ  
 الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١١٦﴾ مَتَّعَ قَلِيلٌ وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١١٧﴾

**114. Basi kuleni katika vile Alivyokupeni Mwenyezi Mungu, vilivyo halali na vizuri. Na shukuruni neema za Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye.**

**115. Amekuharimishieni nyamafu tu, na damu, na nyama ya nguruwe, na mnyama aliyechinjwa kwa ajili isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu. Lakini anayelazimishwa bila ya kuasi, wala kuruka mipaka, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.**

**116. Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali, na hichi haramu - mkimzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa.”**

**117. Ni starehe ndogo, nao watapata adhabu chungu.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:309.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:310.

## Baadhi ya Mazuri Waliyoharamishiwa Mayahudi

Allah تعالى Anasema Akiwaamuru waja Wake waumini kula riziki Yake ya halali nzuri na kumshukuru kwa hayo. Kwa sababu Yeye ndiye Mwenye Kuneemesha na Ambaye Anastahiki ibada Peke Yake na wala hana mshirika. Kisha Allah تعالى Akavitaja Alivyoviharamisha juu yao katika vilivyo na madhara kwao katika Dini yao na dunia yao, kama vile mzoga, damu na nyama ya nguruwe,

وَمَا أَهْلٌ لِّغَيْرِ اللَّهِ بِهِ<sup>ط</sup>

**“...na mnyama aliyechinjwa kwa ajili isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu.”**

Kwa kutajwa jina lisilo la Allah.

فَمِنْ أَضْطَرُّ

**“...Lakini anayelazimishwa...”** Si kwa kuvuka mipaka ya uadui.

فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

**“...basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.”**

Maelezo ya aya kama hii yameshatangulia katika *Suratil Baqarah* hakuhitajiki kuyarejesha, kuhimidiwa ni kwa Allah تعالى.

Kisha Allah تعالى Akakataza kupita njia ya washirikina ambao wamehalalisha na wameharamisha kwa kusema wao tu. Na wakafanya istilahi yao ya majina kwa maoni yao kama vile *Al-Bahira*, *As-Saiba*, *Al-Waswila*, *Al-Haami* na mengineyo katika yaliyokuwa sharia yao wakati wa Ujahilia wao. Allah تعالى Akasema:

وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِفُ أَلْسِنَتُكُمُ الْكَذِبَ هَذَا حَلَلٌ وَهَذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ<sup>ع</sup>

**“Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali, na hichi haramu - mkimzulia uwongo Mwenyezi Mungu.”**

Anaingia hapa kila mwenye kufanya bidaa isiyokuwa na dalili ya kisharia, au amehalalisha kitu katika Alivyoviharamisha Allah تعالى au ameharamisha katika vile Alivyovihalalisha Allah تعالى kwa maoni yake tu.

## لِمَا تَصِفُ

"...*kwa kuropokwa...*" Na haramu yake na kilicho katika kauli yake kwa kinachoeleza. Maana: Msiseme uwongo kwa kusema ndimi zenu tu, kisha Akakemea hayo. Akasema,

إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ

**"Hakika wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa..."**

Maana yake: Duniani wala Akhera. Ama duniani ni starehe chache tu na ama akhera wana adhabu yenye kuumiza mno. Kama Alivyosema,

نُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٣١﴾

**"Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu." (31:24) na,**

إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾ مَتَّعَ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٣٢﴾

**"...Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.**

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَمْنَا مَا قَصَصْنَا عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٣٣﴾ ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ عَمِلُوا السُّوءَ بِجَهْلَةٍ ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٤﴾

**118. Na Mayahudi Tuliwaharamishia yale Tuliyokuhadithia zamani,<sup>1</sup> na sisi hatukuwadhulumu, bali walikuwa wakijidhulumu wenyewe".**

**119. Kisha hakika Mola wako Mlezi kwa waliotenda uovu kwa ujinga, kisha wakatubia baada ya hayo na wakatenda mema; bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.**

<sup>1</sup> Angalia Al-An'am 6:146.

## Mayahudi Kuharamisha Vilivyo Vizuri

Allah تعالى Alipoelezea kuwa Alichotuharamishia ni mzoga, damu, nyama ya nguruwe na kilichochinjwa kwa kutajwa jina lisilokuwa la Allah تعالى. Na hakika si vingine na ameruhusu hayo kwa dharura tu na kufanya hivyo ni kuwapa nafasi umma huu ambao Allah تعالى Anaupendelea kheri na wala Haupendelei shari. Allah تعالى Akavitaja Alivyoviharamisha kwa Mayahudi katika sheria yao kabla hajaifuta, na magumu waliyonayo miongoni mwa, ufinyu, minyororo, na mashaka,

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا مَا قَصَصْنَا عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ

**“Na Mayahudi Tuliwaharamishia yale Tuliyo kuhadithia zamani.”**

Maana yake: Katika Suratil Al-An'aam.

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا كُلَّ ذِي ظُفْرٍ مِّنَ الْأَبْقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا إِلَّا مَا حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا

**“Na wale waliofuata dini ya Kiyahudi Tumewaharimishia kila mwenye kucha. Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi Tumewaharimishia shahamu yao, isipokuwa ile iliyobeba migongo yao...”** mpaka,

لَصَلِفُونَ

**“...ndio wasema kweli.”** (6:146) Na kwa sababu hii hapa Akasema,

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ

**“...na sisi Hatukuwadhulumu,..”** Katika kile Tulichowadhikisha nacho.

وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ

**“...bali walikuwa wakijidhulumu wenyewe.”**

Wakastahiki adhabu hiyo. Sawa na Kauli Yake:

فَيُظْلَمُونَ مِنَ الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ طَيِّبَاتٍ أُحِلَّتْ لَهُمْ وَبِصَدِّهِمْ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ كَثِيرًا

**“Basi kwa dhulma yao Mayahudi Tuliwaharimishia vitu vizuri walivyohalalishiwa. Na kwa sababu ya kuwazuilia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu.”** (4:160)

Kisha Akaeleza takrima na neema kwa walioasi katika waumini kuwa atayetubu miongoni mwao kwa Allah تعالى, basi, Allah تعالى Atapokea toba hiyo. Akasema:

ثُمَّ إِنَّ رَبَّكَ لِلَّذِينَ عَمِلُوا السُّوءَ بِجَهْلَةٍ

**“Kisha hakika ya Mola wako kwa waliotenda uovu kwa ujinga,...”**

Baadhi ya Salafu wamesema kila aliyemuasi Allah تعالى ni mjinga. Kisha wakatubu.

ثُمَّ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا

**“...kisha wakatubia baada ya hayo na wakatenda mema;”**

Maana yake: Wakayaacha waliyo kuwa wanayafanya ya maasi na wakafanya amali njema.

إِنَّ رَبَّكَ مِنْ بَعْدِهَا

**“...bila ya shaka Mola wako Mlezi baada ya hayo...”**

Maana yake: Baada ya tendo hilo na utelezi huo,

لَعَفُورٌ رَحِيمٌ

**“...ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.”**

\* \* \*

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ  
 حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾  
 شَاكِرًا لِأَنْعَمِهِ ۚ اجْتَبَاهُ وَهَدَاهُ إِلَى  
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾ ۚ وَآتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً ۗ وَإِنَّهُ فِي  
 الْآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١٢٢﴾ ۗ ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ  
 أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَمَا  
 كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٣﴾  
 جَعَلْنَا السَّبْتُ عَلَى الَّذِينَ آخْتَلَفُوا فِيهِ ۗ وَإِنَّ رَبَّكَ  
 لَيَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ  
 ﴿١٢٤﴾ ۗ أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۗ  
 وَجَدِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ  
 عَنْ سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾ ۗ وَإِنْ عَاقَبْتُمْ  
 فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ ۗ وَلَئِنْ صَبَرْتُمْ لَهُوَ خَيْرٌ  
 لِلصَّابِرِينَ ﴿١٢٦﴾ ۗ وَأَصْبِرْ وَمَا صَبْرُكَ إِلَّا بِاللَّهِ ۗ وَلَا تَحْزَنْ  
 عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُ فِي ضَلَالٍ مِمَّا يَمْكُرُونَ ﴿١٢٧﴾ ۗ إِنَّ اللَّهَ  
 مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ  
 حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾  
 شَاكِرًا لِأَنْعَمِهِ ۚ اجْتَبَاهُ وَهَدَاهُ إِلَى  
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٢١﴾ ۚ وَآتَيْنَاهُ فِي  
 الدُّنْيَا حَسَنَةً ۗ وَإِنَّهُ فِي الْآخِرَةِ لَمِنَ  
 الصَّالِحِينَ ﴿١٢٢﴾ ۗ ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ  
 أَنِ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَمَا  
 كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٣﴾

120. Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

121. Mwenye kuzishukuru neema Zake, Mwenyezi Mungu. Yeye Kamteua, na Akamuongoa kwenye njia Iliyonyooka.

122. Na Tukampa wema duniani, na hakika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.

123. Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

**Rafiki wa Allah تعالى (Khalil)**

Allah تعالى Anamsifu mja Wake na Mtume Wake na mpenzi Wake Ibrahim عليه السلام, Imamu wa waadilifu na baba wa Mitume na Anamtakasa na washirikina, na Mayahudi na Manasara. Akasema:

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا

***“Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu.”***

Maana yake: Ni Imamu anayefuatwa. Na *Qanit*; ni mnyenyekevu mtiifu. *Hanifa*: aliyeepuka kwa makusudi akauacha ushirikina, akaelekea kwenye Tauhidi. Kwa sababu hii Akasema,

وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

***“...wala hakuwa miongoni mwa washirikina.”***

Mujahid ameeleza kuwa yeye (Ibrahim عليه السلام) mwenyewe alikuwa umma. Kauli Yake:

شَاكِرًا لِأَنْعُمِهِ

***“Mwenye kuzishukuru neema Zake...”***

Maana yake: Alishukuru neema alizoneemeshwa na Allah تعالى. Ni sawa na Kauli nyingine,

وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى

***“Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi?” (53:37)***

Maana yake: Alifanya kila aliloamrisha na Allah تعالى.

أَحْتَبَهُ

***“Yeye Kamteua...”***

Sawa na Kauli Yake:

وَلَقَدْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُشْدَهُ مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا بِمِمْ عَلِيمِينَ

***“Hakika Tulikwisha mpa Ibrahim uongofu wake zamani na Tulikuwa Tunamjua.” (21:51)***



Kisha Akasema,

وَهَدَنَاهُ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

**“...na Akamuongoa kwenye njia Iliyonyooka.”**

Nayo ni kumuabudu Allah تعالى Peke Yake hana mshirika juu ya sheria ridhiwa.

وَأَتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً

**“Na Tukampa wema duniani,...”**

Maana yake: Tumempa kheri ya dunia kwa yote ayatakayo muumini kwa Allah تعالى katika kukamilisha maisha yake mazuri,

وَأَنَّهُ فِي الآخِرَةِ لَمِنَ الصَّالِحِينَ

**“...na hakika yake, akhera atakuwa miongoni mwa watu wema.”**

Kuhusu Aya ifuatayo,

وَأَتَيْنَاهُ فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً

**“Na Tukampa wema duniani,...”**

Mujahid alisema, inamaanisha ulimi usemao kweli. Na Kauli Yake:

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَن اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا

**“Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu.”**

Maana yake: Na miongoni mwa Ukamilifu Wake na Utukufu Wake, na usahihi wa Tauhidi Yake, na Njia Yake, ni kwamba Sisi Tumekufunulia Ewe mwisho wa Mitume na Mtukufu wa Manabii.

أَن اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

**“...kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.”**

Sawa na Kauli Yake katika Suratil An-am,

قُلْ إِنِّي هَدَيْتَنِي رَبِّيَ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قَبِيماً مِثْلَ دِينِ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفاً وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾

**“Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi Ameniongoa kwenye njia iliyo nyooka, Dini iliyo sawa kabisa, ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliye kuwa mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.”**

Kisha Allah تعالی Akasema, Akiwakemea Mayahudi.

إِنَّمَا جُعِلَ السَّبْتُ عَلَى الَّذِينَ أَحْتَلَفُوا فِيهِ وَإِنَّ رَبَّكَ لَيَحْكُمُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٢١﴾

**124. Hakika siku ya Sabato (Jumaamosi) waliwekewa wale waliokhitalifiana kwa ajili yake. Na hakika Mola wako Mlezi bila ya shaka Atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitalifiana.”**

### Jumamosi Iliwekwa kwa Mayahudi

Bila shaka Allah تعالی Ameweka katika kila dini, siku moja, katika wiki watu wanakusanyika humo kwa ibada. Kwa hiyo Allah تعالی Akauwekea umma huu siku ya Ijumaa. Kwa sababu hiyo ni siku ya sita ambayo Allah تعالی Amekamilisha ndani ya siku hiyo Kuumba, na viumbe vikakusanyika humo na ikakamilika neema kwa waja Wake. Na inasemwa kuwa Allah تعالی Ameiweka siku hiyo kwa Bani Israil, kwa ulimi wa Musa عليه السلام wakaipotoa, na wakaiteua Jumamosi. Kwa sababu siku hiyo Allah تعالی Hakuumba kitu katika viumbe ambao umbile lao limekamilika Ijumaa. Akawalazimisha nayo Allah تعالی siku hiyo ndani ya Taurati, na Akawaamuru kushikamana nayo wasiache, pamoja na kuwataka kumfuata Muhammad ﷺ atapokuja. Na wakachukua ahadi juu ya hayo na kwa sababu hii Akasema:

إِنَّمَا جُعِلَ السَّبْتُ عَلَى الَّذِينَ أَحْتَلَفُوا فِيهِ

**“Hakika siku ya Sabato (Jumaamosi) waliwekewa wale walio khitalifiana kwa ajili yake.”**

Mujahid amesema wakaifuata na wakaiacha Ijumaa,<sup>1</sup> kisha wakaendelea kuwa nayo mpaka alipotumwa Issa Ibn Mariam عليه السلام. Inasemekana kuwa yeye ndiye aliyewahamishia Jumapili na inasemwa hakuiacha Issa عليه السلام sheria ya Taurati isipokuwa iliyofutwa miongoni mwa baadhi ya hukumu. Na kwamba aliendelea na Jumamosi mpaka aliporufaishwa, na kwamba manaswara baada ya Issa عليه السلام wakati wa Qustwantin ndio waliobadili kwenda Jumapili ili kutofautiana na Mayahudi. Na katika Sala wakaelekea mashariki ya Swakhrh. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

Na imethibiti katika Sahihi mbili kutoka kwa Abu Huraira رضي الله عنه kuwa yeye amemsikia Mtume Muhammad ﷺ akisema,

«نَحْنُ الْأَخْرُونَ السَّابِقُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، بَيَدِ أُنْهَمُ أَوْثَرِ الْكِتَابِ مِنْ قَبْلِنَا، ثُمَّ هَذَا يَوْمُهُمُ الَّذِي فَرَضَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ فَأَخْتَلَفُوا فِيهِ، فَهَدَانَا اللَّهُ لَهُ، فَالْتَأَسُّ لَنَا فِيهِ نَبِيٌّ: الْيَهُودُ عَدَا وَالنَّصَارَى بَعْدَ عَدِي»

*"Sisi ndio wa mwisho na mwanzo Siku ya Kiama, isipokuwa wao wamepewa kitabu kabla yetu, kisha hii ni siku yao ambayo Allah Amewalazimisha, nayo wakahitilafiana humo. Allah Akatuongoza sisi kwenye siku hiyo, kwa hiyo watu wanatufuata sisi katika siku hiyo na Mayahudi ni kesho, na manaswara ni kesho kutwa."*<sup>2</sup>

Na hili ni tamko la Bukhari. Na kutoka kwa Abu Huraira na Hudhaifa عنهما رضي الله عنهما wamesema Mtume ﷺ amesema kuwa,

«أَصْلَ اللَّهِ عَنِ الْجُمُعَةِ مَنْ كَانَ قَبْلَنَا، فَكَانَ لِلْيَهُودِ يَوْمَ السَّبْتِ، وَكَانَ لِلنَّصَارَى يَوْمَ الْأَحَدِ، فَجَاءَ اللَّهُ بِنَا فَهَدَانَا اللَّهُ لِيَوْمِ الْجُمُعَةِ، فَجَعَلَ الْجُمُعَةَ وَالسَّبْتَ وَالْأَحَدَ، وَكَذَلِكَ هُمْ تَبِعُ لَنَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ نَحْنُ الْأَخْرُونَ مِنْ أَهْلِ الدُّنْيَا، وَالْأَوْلُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَالْمَقْضِيُّ بَيْنَهُمْ قَبْلَ الْخَلَائِقِ»

*"Allah Amewapoteza waliokuwa kabla yenu, Mayahudi kwao ikawa Jumamosi na kwa Manaswara Jumapili. Allah Akatuleta sisi*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:320.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 11:526, Muslim 2:586.

Akatuongoza kwa siku ya Ijumaa, Akazifanya Ijumaa, Jumamosi na Jumapili. Na hivyo hivyo wao wanatufuata sisi Siku ya Kiama, na wenye kupata hukumu kati yao kabla ya viumbe.”<sup>1</sup>

أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ وَجَدِلْ لَهُم بِآيَاتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ رَبَّكَ  
هُوَ أَعْلَمُ بِمَنْ ضَلَّ عَنْ سَبِيلِهِ ۗ وَهُوَ أَعْلَمُ بِالْمُهْتَدِينَ ﴿١٢٥﴾

**125. Waite waelekee kwenye njia ya Mola Wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Anayemjua zaidi aliyepotea njia Yake, na Yeye Ndiye Anayewajua zaidi walioongoka.**

### Amri ya Kulingania kwa Hekima na Mawaidha Mazuri

Allah تعالیٰ Anasema Akimuamuru Mtume Wake Muhammad ﷺ awaite viumbe kwa Allah تعالیٰ kwa hekima. Ibn Jarir رحمه الله تعالیٰ amesema na hicho ndicho Alichomteremshia katika kitabu na Sunna.

وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۗ

**“...na mawaidha mema,...”**

Maana yake: Pamoja na makemeo yaliomo na matukio kwa watu yaliyoelezwa katika Qur’an.<sup>2</sup> Amewakumbusha hayo ili wajihadhari na adhabu ya Allah تعالیٰ. Na Kauli Yake:

وَجَدِلْ لَهُم بِآيَاتِي هِيَ أَحْسَنُ ۗ

**“...na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora.”**

Maana yake: Kwa yule anayehitaji mjadala miongoni mwao. Na mjadala uwe kwa sura nzuri kwa upole, ulaini na maelezo mazuri. Kama ilivyo katika Kauli Yake تعالیٰ:

وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ ۗ

**“Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa, isipo kuwa wale walio dhulumu miongoni mwao...” (29:46)**

<sup>1</sup> Muslim 2:586.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:321.

Kwa hiyo Allah تعالى Akamuamuru kuwa mpole kama Alivyomuamuru Musa عليه السلام na Haruna عليه السلام Alipowatuma kwenda kwa Fir-aun katika Kauli Yake:

﴿١٢٠﴾ فَقُولَا لَهُ قَوْلًا لَّيِّنًا لِّعَلَّهُ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَخْشَىٰ

**“Muambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa.” (20:44).**

﴿١٢١﴾ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِ

**“Hakika Mola Wako Mlezi Ndiye Anayemjua zaidi aliyeipotea njia yake...”**

Maana yake: Anamjua muovu miongoni mwao na mwema na Ameshayaandika na yamekwisha. Kwa hiyo waite kwa Allah تعالى na wala usiwajutie waliopotea miongoni mwao, na si juu yako hilo halipo mikononi mwako, wewe ni muhadharishaji tu na hesabu iko juu Yetu.

﴿١٢٢﴾ إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

**“Kwa hakika wewe humuongoi umpendaye,”**

﴿١٢٣﴾ لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

**“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa amtakaye.”**

﴿١٢٤﴾ وَإِنْ عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ ۗ وَلَئِن صَبَرْتُمْ لَهُوَ خَيْرٌ لِلصَّابِرِينَ

﴿١٢٥﴾ وَأَصْبِرْ وَمَا صَبْرُكَ إِلَّا بِاللَّهِ ۗ وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ وَلَا تَكُ فِي ضَيْقٍ مِّمَّا يَمْكُرُونَ

﴿١٢٦﴾ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ

**126. Na mkilipiza basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa. Na ikiwa mtasubiri, basi hakika hivyo ni bora zaidi kwa wanao subiri.”**

**127. Na subiri. Na kusubiri kwako kusiwe ila kwa sababu ya Mwenyezi Mungu tu. Wala usiwahuzunikie; wala usiwe katika dhiki kwa hila wanazozifanya.”**

**128. Hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema.<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Angalia Tafsiri ya Surat At-Tawbah 9:120.

## Amri ya Kufanya Usawa Katika Kisasi

Allah تعالی Anaamuru uadilifu katika kisasi, na usawa katika kutekeleza haki. Kama alivyopokea Abdur-Raz-zaq kutoka kwa Ibn Siri رحمه الله تعالی, yeye amesema katika Kauli Yake تعالی،

فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُمْ بِهِ

**“...basi lipizeni sawa na vile mlivyoadhibiwa.”**

Endapo mtu amewachukulia kitu basi nanyi chukuweni sawa na hicho.<sup>1</sup> Na hivyo hivyo amesema: Mujahid, Ibrahim, na Al-Hassan Al Basri na wengineo.<sup>2</sup> Na Ibn Jarir رحمه الله تعالی ameiteua na Ibn Zaid amesema, ‘Walikuwa wameamrisha kuwasamehe washirikina, wakashilimu watu wengi wenye nguvu, wakasema: ‘Ewe Mtume ﷺ kama Allah تعالی Angalituruhusu kupigana tungaliwashinda mbwa hawa.’ Ikateremka aya hii.” Kisha ikafutwa hiyo kwa amri ya jihadi.<sup>3</sup>

وَأَصْبِرْ وَمَا صَبْرُكَ إِلَّا بِاللَّهِ

**“Na subiri. Na kusubiri kwako kusiwe ila kwa sababu ya Mwenyezi Mungu tu.”**

Ni sitizito la amri ya kusubiri. Na taarifa ya kwamba hayo hayafikii ila kwa kutaka Allah تعالی na Msaada Wake, Uwezo Wake na Nguvu Zake. Kisha Akasema,

وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ

**“Na wala usiwahuzunike.”** Maana yake: Wanaokupinga kwani Allah تعالی Ameshapitisha kuwa hayo yatokee.

وَلَا تَلُكُ فِي ضَيْقٍ

**“...wala usiwe katika dhiki...”** Maana yake: Huzuni na unyonge

مِمَّا يَمْكُرُونَ

**“...kwa hila wanazozifanya.”** Katika yale wanayojisumbua katika kukufanyia uadui, na kukuletea madhara. Hakika Allah تعالی Anakutosha na ni Muokozi wako, Msaidizi wako, Mwenye Kukupa ushindi na Atakulipizia wao. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Abdur-Razzaq 2:361.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:524, 525.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:324.

إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾

**"Hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema." (16:128)**

Yu pamoja na wao kwa Msaada Wake, Nusra Yake, Muongozo Wake, na huu ni upamoja maalum. Kama ilivyo katika Kauli Yake:

إِذْ يُوحِي رُؤْيَاكَ إِلَى الْمَلَكَةِ إِنِّي مَعَكُمْ فَتَبَيَّنُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا

**"Hakika si vingine Mola wako Anapeleka wahyi kwa malaika kuwa Mimi Niko pamoja nanyi wapeni subira walioamini." (8:12)**

Na Kauli Yake kwa Musa عليه السلام na Haruna عليه السلام,

لَا تَخَافَا إِنِّي مَعَكُمْ أَسْمَعُ وَأَرَى ﴿٢٤﴾

**"...msiogope Mimi Niko pamoja nanyi Nasikia na Naona..." (20:46)**

Na kauli ya Mtume ﷺ kwa Swiddiq na wote wamo pangoni.

«لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا»

*"...usihuzunike Hakika Allah Yuko pamoja na sisi."*<sup>1</sup>

Ama pamoja ya ujumla ni kwa kusikia, kuona na kuelewa ilimu kama ilivyo katika Kauli Yake:

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٥٧﴾

**"Na Yeye Yu pamoja nanyi popote mlipo na Allah mnayoyafanya Anayaona." (57:4)**

Na kama ilivyo katika Kauli Yake:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَانِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَا يَكُونُ مِنْ نَجْوَى ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا آدْنَى مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْثَرُ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا

**"Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu Anajua vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi? Hauwi mning'ono wa watu**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 7:11.

**watatu ila Yeye huwa ni wanne wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye Yu pamoja nao popote pale walipo.”**

Na kama Alivyosema تعالى:

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا

**“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo.”(10:61)**

Na maana ya:

الَّذِينَ اتَّقَوْا

**“...Na ambao wamemcha...”**

Wameyaacha ya haramu

وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ

**“...na ambao wanafanya wema...”**

Maana yake: Wameyafanya ya utiifu, kwa hiyo Allah تعالى Anawahifadhi hawa na Kuwalea, Anawanusuru, Anawasaidia na Kuwapa ushindi dhidi ya maadui zao na wapinzani wao.

Huu ni mwisho wa Tafsiri ya *Surat Annahl*. Mwenyezi Mungu Ndiye wa Kushukuriwa na Kuombwa na Rehma na Amani zimfikie Mtume wetu Muhammad ﷺ pamoja na Ali zake na sahaba wake رضي الله عنهم.

\* \* \*